JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA

# HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2025

Juni 2026
Dodoma

# HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2025

# YALIYOMO

**ORODHA YA MAJEDWALI** ..... **viii**
**KIREFU/TAFSIRI YA MANENO** ..... **xiii**
**SURA YA 1** ..... **1**
**HALI YA UCHUMI WA TAIFA** ..... **1**
Ukuaji wa Uchumi ..... 1
Pato la Taifa kwa Mtu ..... 3
Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi ..... 4
Mfumuko wa Bei ..... 7
Ukuzaji Rasilimali ..... 9
**SURA YA 2** ..... **34**
**FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA** ..... **34**
Utekelezaji wa Sera ya Fedha ..... 34
Ujazi wa Fedha ..... 34
Mikopo kwa Sekta Binafsi ..... 35
Amana katika Benki za Biashara ..... 36
Mwenendo wa Viwango vya Riba ..... 36
Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania ..... 37
**MAENDELEO KATIKA SEKTA YA FEDHA** ..... **37**
Huduma za Benki ..... 37
Mwenendo wa Viashiria vya Sekta ya Benki ..... 38
Maboresho katika Sekta ya Benki ..... 38
Huduma Ndogo za Fedha ..... 38
Masoko ya Mitaji na Dhamana ..... 39
Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ..... 40
Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ..... 41
Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ..... 42
Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ..... 42
Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa ..... 44
Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania ..... 44
Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ..... 46
Benki ya Biashara Tanzania ..... 47
Soko la Bidhaa Tanzania ..... 48
**SURA YA 3** ..... **54**
**FEDHA ZA SERIKALI** ..... **54**
Utangulizi ..... 54
Mwenendo wa Makusanyo ..... 55
Mwenendo wa Matumizi ..... 57
Deni la Serikali ..... 58
Uhimilivu wa Deni ..... 60
Uwezo wa Nchi Kukopa na Kulipa Madeni katika Masoko ya Kimataifa ..... 61
**SURA YA 4** ..... **66**
**SEKTA YA NJE** ..... **66**
Bidhaa Zilizouzwa Nje ..... 66

Bidhaa Asilia ... 66
Bidhaa Zisizo Asilia ... 67
Mapato ya Huduma ... 70
Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje ya Nchi ... 70
Malipo ya Huduma ... 71
Mwenendo wa Biashara Baina ya Tanzania na Nchi Mbalimbali ... 71
Mizania ya Malipo na Nchi za Nje ... 76
Akiba ya Fedha za Kigeni ... 77
**SURA YA 5 ... 87**
**HALI YA UCHUMI WA DUNIA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA ... 87**
**HALI YA UCHUMI WA DUNIA ... 87**
Ukuaji wa Uchumi ... 87
Mwenendo wa Bei ... 89
Mwenendo wa Biashara Duniani ... 90
**USHIRIKIANO WA KIMATAIFA ... 91**
Ushirikiano wa Uchumi Kimataifa ... 91
Ushirikiano wa Kiuchumi Barani Afrika ... 93
Ushirikiano wa Kiuchumi Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ... 94
Ushirikiano wa Kiuchumi katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ... 94
Ushirikiano wa Kiuchumi katika Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu ... 95
**SURA YA 6 ... 96**
**RASILIMALI WATU ... 96**
Idadi ya Watu ... 96
Mgawanyiko wa Watu Kimkoa ... 96
Mgawanyo wa Watu kwa Umri Tanzania Bara ... 98
Nguvu Kazi na Ajira ... 99
**SURA YA 7 ... 106**
**KILIMO NA USHIRIKA ... 106**
**UZALISHAJI WA MAZAO YA KILIMO ... 106**
Mazao ya Chakula ... 106
Miundombinu ya Hifadhi ya Chakula ... 106
Mazao ya Asilia ya Biashara ... 107
Mazao ya Bustani ... 107
Mazao ya Mbegu za Mafuta ... 108
Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo ... 108
Upatikanaji wa Mikopo ya Kilimo ... 109
Mwenendo wa Bei na Masoko ya Mazao ... 110
Huduma za Ugani ... 111
Utafiti katika Uzalishaji wa Mazao ... 111
Mafunzo ya Kilimo ... 112
Umwagiliaji ... 112
**MIFUGO ... 112**
Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake ... 112
Biashara ya Mifugo na Mazao ya Mifugo ... 114
Uzalishaji wa Chanjo za Mifugo ... 116
Uzalishaji wa Malisho na Utengenezaji wa Vyakula vya Mifugo ... 116

Mafunzo ya Mifugo ..... 117
Utafiti wa Mifugo ..... 117
Huduma za Ugani katika Mifugo ..... 117
**UVUVI ..... 118**
Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi ..... 118
Ukuzaji Viumbe Maji ..... 118
Uvunaji wa Samaki ..... 120
Udhibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi ..... 120
Uuzaji na Uagizaji wa Mazao ya Uvuvi Nje ya Nchi ..... 121
Uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi ..... 121
Mafunzo ya Uvuvi ..... 122
**MAENDELEO YA USHIRIKA ..... 123**
**MIZANIA YA CHAKULA NCHINI ..... 123**
Dhana ya Mizania ya Chakula ..... 123
Upatikanaji wa Nishati ya Chakula ..... 123
Kiwango cha Utoshelevu wa Chakula ..... 124
Kiwango cha Utegemezi wa Uagizaji wa Chakula Kutoka Nje ya Nchi ..... 125
**SURA YA 8 ..... 134**
**MISITU, WANYAMAPORI NA UTALII ..... 134**
Misitu na Nyuki ..... 134
Upandaji wa Miti ..... 134
Wanyamapori ..... 135
Utalii ..... 137
Uwindaji wa Kitalii na Utalii wa Picha ..... 139
Malikale ..... 139
Makumbusho ya Taifa ..... 140
**SURA YA 9 ..... 146**
**MADINI ..... 146**
Leseni za Shughuli za Madini ..... 146
Vibali vya Uuzaji wa Madini ..... 146
Dhahabu ..... 146
Almasi ..... 147
Vito vya Thamani ..... 147
Tanzanite ..... 147
Makaa ya Mawe ..... 147
Madini ya Jasi ..... 148
Madini ya Ujenzi ..... 148
Madini Mengine ..... 148
Masoko ya Madini ..... 148
**SURA YA 10 ..... 152**
**VIWANDA NA BIASHARA ..... 152**
Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani ..... 152
Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ..... 152
Usajili wa Biashara na Viwanda ..... 154
Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa ..... 154
Udhibiti Ubora wa Viwango na Vipimo ..... 155

Usawa wa Ushindani na Udhibiti wa Bidhaa Bandia ........ 157
Shirika la Taifa la Maendeleo ........ 158
Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala ........ 158
**SURA YA 11 ........ 165**
**UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI ........ 165**
**UJENZI ........ 165**
Mtandao wa Barabara Nchini ........ 165
Vivuko na Magari ........ 167
Mfuko wa Barabara ........ 167
Nyumba na Majengo ya Serikali ........ 168
Usajili wa Makandarasi ........ 168
Usajili wa Wahandisi ........ 168
Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ........ 169
Baraza la Taifa la Ujenzi ........ 170
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi ........ 170
**MAENDELEO YA ARDHI ........ 170**
Usajili wa Hatimiliki, Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na Nyaraka za Kisheria ........ 170
Uthamini wa Mali na Upimaji wa Viwanja na Mashamba ........ 171
Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji ........ 172
Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi ........ 175
Urasimishaji wa Makazi Yasiyopangwa ........ 175
Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Biashara ........ 176
**SURA YA 12 ........ 177**
**UCHUKUZI NA UHIFADHI MIZIGO ........ 177**
Usafiri wa Barabara ........ 177
Usafiri wa Reli ........ 178
Usafiri wa Anga ........ 180
Usafiri na Usafirishaji kwa Njia ya Maji ........ 182
Muda wa Meli Kukaa Bandarini ........ 184
Shehena za Nchi Jirani ........ 185
Huduma za Uchukuzi katika Maziwa Makuu ........ 185
Kampuni ya Meli ya China na Tanzania ........ 186
Huduma za Hali ya Hewa ........ 186
**SURA YA 13 ........ 188**
**MAWASILIANO, HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO ........ 188**
**MAWASILIANO ........ 188**
Huduma za Posta ........ 188
Huduma za Simu ........ 189
Huduma za Intaneti ........ 190
Utoaji wa Leseni za Mawasiliano ........ 190
Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ........ 191
Huduma za Mawasiliano ........ 191
**HABARI ........ 192**
**MAENDELEO YA UTAMADUNI ........ 193**
**MAENDELEO YA SANAA ........ 194**
**MAENDELEO YA MICHEZO ........ 197**

**SURA YA 14** .......... **200**
**NISHATI** .......... **200**
Upatikanaji wa Umeme Nchini .......... 200
Gesi Asilia .......... 202
Uagizaji Mafuta .......... 203
Mafuta Yaliyoingizwa Nchini Kwenda Nchi Jirani .......... 204
Mwenendo wa Bei za Mafuta .......... 205
Gesi Inayotokana na Petroli .......... 207
**SURA YA 15** .......... **212**
**MAJI** .......... **212**
Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji .......... 212
Ubora wa Maji .......... 212
Huduma ya Maji Vijijini .......... 213
Huduma ya Maji Mijini .......... 213
Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa .......... 214
Uondoaji wa Majitaka .......... 215
**SURA YA 16** .......... **220**
**ELIMU, MAFUNZO NA TEKNOLOJIA** .......... **220**
Elimu ya Awali .......... 220
Elimu ya Msingi .......... 220
Elimu ya Sekondari .......... 221
Elimu katika Vyuo vya Ualimu .......... 222
Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu .......... 223
Elimu ya Ufundi na Mafunzo .......... 223
Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi .......... 223
Sayansi, Teknolojia na Ubunifu .......... 224
Elimu ya Juu .......... 224
Udhibiti wa Mionzi .......... 225
**SURA YA 17** .......... **229**
**AFYA NA MAENDELEO YA JAMII** .......... **229**
**AFYA** .......... **229**
Vituo vya Kutolea Huduma za Afya .......... 229
Hali ya Utoaji Huduma .......... 229
Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba .......... 230
Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto .......... 230
Huduma za Matibabu ya Kibingwa .......... 231
Udhibiti wa Malaria .......... 232
Udhibiti wa Kifua Kikuu .......... 232
Lishe .......... 233
Mafunzo katika Kada za Afya .......... 233
**MAENDELEO YA JAMII** .......... **234**
Huduma ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto .......... 234
Huduma za Ustawi na Maendeleo ya Watoto .......... 234
Ukatili wa Kijinsia .......... 235
Huduma za Ustawi kwa Wazee na Wasiojiweza .......... 236
Mafunzo ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii .......... 236

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ..... 237
**SURA YA 18 ..... 241**
**MASUALA MTAMBUKA ..... 241**
Mazingira ..... 241
Usalama wa Raia ..... 242
Utambuzi na Usajili wa Watu ..... 244
Usajili wa Jumuiya ..... 244
Usajili, Ufilisi na Udhamini ..... 244
Maendeleo ya Sheria na Mahakama ..... 245
Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu ..... 246
Mapambano dhidi ya Rushwa ..... 246
Jitihada za Kupunguza Umaskini ..... 247
**SURA YA 19 ..... 250**
**UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI ..... 250**
Usajili wa Miradi ya Uwekezaji ..... 250
Mgawanyo wa Miradi Iliyosajiliwa Kisekta ..... 250
Mgawanyo wa Miradi Iliyosajiliwa Kimkoa ..... 251
Uwekezaji wa Sekta Binafsi Ndani ya Nchi ..... 251
Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kutoka Nje ..... 252
Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje ..... 252
Mazingira ya Biashara na Uwekezaji ..... 255
Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ..... 255
Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati ..... 257
Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ..... 257
**SURA YA 20 ..... 260**
**MABORESHO YA TAKWIMU ZA PATO LA TAIFA ..... 260**
Utangulizi ..... 260
Historia ya Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa ..... 260
Dhana na Umuhimu wa Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa ..... 261
Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa kwa Kutumia Mwaka wa Kizio 2019 ..... 262
Muhtasari wa Matokeo ya Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa ..... 263
Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa katika Nchi Nyingine ..... 273
Hitimisho ..... 273

## ORODHA YA MAJEDWALI

**Ukurasa**


Jedwali A: TAKWIMU MUHIMU KATIKA UCHUMI - TANZANIA BARA...................xviii

Jedwali B: MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI JUMLA NA BAJETI............xix

Jedwali Na. 1: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, 2019 - 2025 ....................................................11

Jedwali Na. 2: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA, 2019 - 2025.....................................................................................................12

Jedwali Na. 3: MCHANGO KATIKA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, 2019 - 2025...........................13

Jedwali Na. 4: MCHANGO KATIKA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA, 2019 - 2025.................................................................................14

Jedwali Na. 5: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA AINA YA MATUMIZI, 2019 - 2025 .........................................................................15

Jedwali Na. 6: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2019 KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, 2019 - 2025 .....................................................16

Jedwali Na. 7: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2019 KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI -SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA, 2019 - 2025.....................................................................................................17

Jedwali Na. 8: UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2019 KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, 2019 - 2025..........................................18

Jedwali Na. 9: UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2019 KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI -SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA, 2019 - 2025.................................................................................19

Jedwali Na. 10: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2019 KWA AINA YA MATUMIZI, 2019 - 2025 ...................................................................20

Jedwali Na. 11: UKUZAJI RASILIMALI KWA KWA BEI ZA MIAKA HUSIKA KWA AINA YA RASILIMALI, 2019 - 2025.............................................................21

Jedwali Na. 12: UKUZAJI RASILIMALI KWA BEI ZA MWAKA 2019 KWA AINA YA RASILIMALI, 2019 - 2025 ..... 22
Jedwali Na. 13: MCHANGO KATIKA UKUZAJI RASILIMALI KWA BEI ZA MIAKA HUSIKA KWA AINA YA RASILIMALI, 2019 - 2025 ..... 23
Jedwali Na. 14: UKUZAJI RASILIMALI KWA BEI ZA MIAKA HUSIKA KWA AINA YA SEKTA, 2016 - 2025 ..... 24
Jedwali Na. 15: FAHIRISI ZA BEI ZA REJAREJA ZA BIDHAA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR-ES-SALAAM (Jan - Des. 2020 =100) ..... 25
Jedwali Na. 16: FAHIRISI ZA BEI ZA REJA REJA ZA BIDHAA ZITUMIKAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR ES SALAAM (Jan - Des. 2020 = 100) ..... 26
Jedwali Na. 17: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA KATI - DAR-ES-SALAAM (Jan - Des. 2020 =100) ..... 27
Jedwali Na. 18: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA KATI DAR ES SALAAM (Jan - Des. 2020 =100) ..... 28
Jedwali Na. 19:FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA JUU DAR ES SALAAM (Jan - Des. 2020 =100) ..... 29
Jedwali Na. 20: FAHIRISI YA GHARAMA YA MAISHA YA WENYE KIPATO CHA JUU DAR-ES-SALAAM (Jan - Des. 2020 =100) ..... 30
Jedwali Na. 21: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA (Jan - Des. 2020 =100) ..... 31
Jedwali Na. 22: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI TANZANIA BARA (Jan - Des. 2020 =100) ..... 32
Jedwali Na. 23: FAHIRISI ZA BEI MBALIMBALI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI-TANZANIA BARA ( Jan - Des. 2020 =100) ..... 33
Jedwali Na. 24: MWENENDO WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA ..... 49
Jedwali Na. 25: VIWANGO VYA UKUAJI WA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA 50
Jedwali Na. 26: MWENENDO WA VIWANGO VYA UBADILISHAJI KATI YA SHILINGI NA DOLA YA MAREKANI, MWAKA 2019 - 2025 ..... 51

Jedwali Na. 27: MWENENDO WA AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA, MWAKA 2019 - 2025 ........ 52
Jedwali Na. 28: VIWANGO VYA WASTANI WA RIBA, MWAKA 2019 - 2025 ........ 53
Jedwali Na. 29: MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI ........ 62
Jedwali Na. 30: MGAWANYO WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA HUDUMA ZA SERIKALI ........ 64
Jedwali Na. 31: THAMANI YA BIASHARA YA BIDHAA BAINA YA TANZANIA NA NCHI NYINGINE, MWAKA 2020 - 2025 ........ 78
Jedwali Na. 32: KIASI NA THAMANI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NJE YA NCHI, MWAKA 2020 - 2025 ........ 79
Jedwali Na. 33: KIASI NA THAMANI YA BIDHAA ZA ASILIA NA ZISIZO ZA ASILIA ZILIZOUZWA NJE YA NCHI, MWAKA 2020 - 2025 ........ 80
Jedwali Na. 34: WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE YA NCHI, MWAKA 2020 - 2025 ........ 83
Jedwali Na. 35: WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NJE YA NCHI, MWAKA 2017 - 2025 ........ 84
Jedwali Na. 36: MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE MWAKA 2020 - 2025 ........ 85
Jedwali Na. 37: IDADI YA WATU NCHINI TANZANIA KIMKOA, MWAKA 2018 - 2025 ........ 104
Jedwali Na. 38: UZALISHAJI WA MIWA NA SUKARI NCHINI, MWAKA 2009/10 - 2024/25 ........ 127
Jedwali Na. 39: PAMBA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI, MWAKA 2009/10 - 2024/25 ........ 128
Jedwali Na. 40: ENEO LILILOPANDWA CHAI NA MAJANI MABICHI YALIYOPATIKANA, MWAKA 2009/10 - 2024/25 ........ 129
Jedwali Na. 41: ENEO LILILOPANDWA MKONGE NA KATANI ILIYOPATIKANA, MWAKA 2009/10 - 2024/25 ........ 130
Jedwali Na. 42: UZALISHAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI, MWAKA 2010 - 2025 ........ 131
Jedwali Na. 43: MWENENDO WA UUZAJI WA SAMAKI NJE YA NCHI, MWAKA 2011 - 2025 ........ 132
Jedwali Na. 44: MAUZO YA SANGARA NJE YA NCHI, MWAKA 2010 - 2025 ........ 133

Jedwali Na. 45: WATALII WALIOTEMBELEA HIFADHI ZA TAIFA, MWAKA 2010 - 2025 .......... 142
Jedwali Na. 46: MAUZO YA BIDHAA ZA MISITU NJE YA NCHI MWAKA 2025 .......... 143
Jedwali Na. 47: MWENENDO WA BIASHARA YA UTALII, MWAKA 2019 - 2025 .......... 144
Jedwali Na. 48: WATALII WALIOTEMBELEA MAMLAKA YA HIFADHI YA NGORONGORO, MWAKA 2010 - 2025 .......... 145
Jedwali Na. 49: UCHIMBAJI WA MADINI: KIASI KILICHOPATIKANA,MWAKA 2020 - 2025 .......... 150
Jedwali Na. 50: KIASI NA THAMANI YA MADINI YALIYOPATA KIBALI CHA KUUZWA NJE YA NCHI, MWAKA 2022 - 2025 .......... 151
Jedwali Na. 51: MATUMIZI YA SARUJI NCHINI (Tani), MWAKA 2010 - 2025 .......... 159
Jedwali Na. 52: UZALISHAJI WA BAADHI YA BIDHAA VIWANDANI, MWAKA 2016 - 2025 .......... 160
Jedwali Na. 53: VIWANDA: IDADI YA WATU WALIOAJIRIWA, MWAKA 2023 - 2025 .......... 161
Jedwali Na. 54: VIWANDA: GHARAMA ZA KAZI, MWAKA 2023 - 2025 .......... 162
Jedwali Na. 55: VIWANDA: MUHTASARI WA MATOKEO, MWAKA 2023 - 2025 .......... 163
Jedwali Na. 56: VIWANDA: MUHTASARI WA MATOKEO KIMKOA, MWAKA 2023 - 2025 .......... 164
Jedwali Na. 57: SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA (ATCL)+, MWAKA 2018 - 2025 .......... 187
Jedwali Na. 58: HUDUMA ZA POSTA, MWAKA 2018 - 2025 .......... 198
Jedwali Na. 59: IDADI YA KADI ZA SIMU ZA MEZANI NA VIGANJANI, MWAKA 2019 - 2025 .......... 199
Jedwali Na. 60: UWEZO WA MITAMBO YA KUFUA UMEME NA UPATIKANAJI WA UMEME NCHINI MWAKA 2025 .......... 208
Jedwali Na. 61: MAUZO YA UMEME KWA WATUMIAJI MBALIMBALI (Saa za Megawati 000"), MWAKA 2013 - 2025 .......... 210
Jedwali Na. 62: MAUZO YA UMEME KWA MIKOA (Saa za Megawati 000"), MWAKA 2019 - 2025 .......... 211
Jedwali Na. 63: UZALISHAJI WA MAJI NA MAPATO YATOKANAYONA MAJI MIJINI, MWAKA 2024 - 2025 .......... 216

Jedwali Na. 64: KIWANGO CHA UPATIKANAJI WA MAJI KATIKA MIJI MIKUU YA MIKOA MWAKA 2025 ....................219
Jedwali Na. 65: SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO, MWAKA 2010 - 2025 ....................226
Jedwali Na. 66: SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO, MWAKA 2010 - 2025 ....................227
Jedwali Na. 67: IDADI YA WAGONJWA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA, MWAKA 2010 - 2025 ....................238
Jedwali Na. 68: IDADI YA VITANDA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA NCHINI, MWAKA 2024 - 2025....................239
Jedwali Na. 69: KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA: MIRADI YA UWEKEZAJI ILIYOSAJILIWA, MWAKA 2024 - 2025 ....................258

## KIREFU/TAFSIRI YA MANENO

| | |
|---|---|
| AfCFTA | African Continental Free Trade Area (Eneo Huru la Biashara Afrika) |
| ASA | Agricultural Seed Agency (Wakala wa Mbegu za Kilimo) |
| ATCL | Air Tanzania Company Limited (Kampuni ya Ndege Tanzania) |
| BAKITA | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| BASA | Bilateral Air Services Agreement (Mikataba ya Usafiri wa Anga Baina ya Tanzania na Nchi Nyingine ) |
| BASATA | Baraza la Sanaa la Taifa |
| BMT | Baraza la Michezo la Taifa |
| BRELA | Business Registrations and Licensing Agency (Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni) |
| CAMARTEC | Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology (Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini) |
| CBE | College of Business Education (Chuo cha Elimu ya Biashara) |
| CMSA | Capital Market and Securities Authority (Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ) |
| COASCO | Co-operative Audit and Supervision Corporation (Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika) |
| COSOTA | Chama cha Hakimiliki Tanzania |
| DSE | Dar es Salaam Stock Exchange (Soko la Hisa la Dar es Salaam) |
| EAC | The East African Community (Jumuiya ya Afrika Mashariki) |
| FCC | The Fair Competition Commission (Tume ya Ushindani) |
| FCT | Fair Competition Tribunal (Baraza la Ushindani) |
| IMF | International Monetary Fund (Shirika la Fedha la Kimataifa) |
| LATRA | Land Transport Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini) |
| LPG | Liquified Petroleum Gas (Gesi inayotokana na Petroli) |
| M1 | Narrow Money Supply (Ujazi wa fedha kwa Tafsiri Finyu) |
| M2 | Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana) |
| M3 | Extended Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana Zaidi) |
| MKUMBI | Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara |

| | |
|---|---|
| MPRU | Marine Parks and Reserves Tanzania (Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu) |
| NDC | The National Development Corporation (Shirika la Maendeleo la Taifa) |
| NEDF | National Entrepreneurship Development Fund (Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali) |
| NFRA | National Food Reserve Agency (Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula) |
| NGOs | Non Government Organisations (Mashirika Yasiyo ya Kiserikali) |
| NHC | National Housing Corporation (Shirika la Nyumba la Taifa) |
| NHIF | National Health Insurance Fund (Mfuko wa Taifa Wa Bima ya Afya) |
| NIMR | The National Institute for Medical Research (Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu) |
| NSSF | National Social Security Fund (Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii) |
| OECD | Organisation for Economic Co-operation and Development (Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo) |
| OPV | Oral Polio Vaccine |
| PPP | Public Private Partnership (Ubia kati ya sekta ya Umma na Sekta Binafsi) |
| PSSSF | Public Service Social Security Fund (Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma) |
| RITA | Registration Insolvency and Trusteeship Agency (Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini) |
| SADC | The Southern African Development Community (Jumuiya ya maendeleo Kusini mwa Afrika) |
| SIDO | Small Industries Development Organization (Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo) |
| SGR | Standard Gauge Railway (Reli ya Kati ya Kiwango cha Kimataifa) |
| TADB | Tanzania Agricultural Development Bank (Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania) |
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TALIRI | Tanzania Livestock Research Institute (Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania) |
| TANESCO | Tanzania Electricity Supply Company (Shirika la Ugamvi wa Umeme |

| | |
|---|---|
| | Tanzania) |
| TANROADS | Tanzania National Roads Agency (Wakala wa Barabara Tanzania) |
| TanTrade | Tanzania Trade Development Authority (Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania) |
| TARI | Tanzania Agricultural Research Institute (Taaasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania) |
| TARURA | Tanzania Rural and Urban Roads Agency (Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini) |
| TASAC | Tanzania Shipping Agency Corporation (Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania) |
| TASAF | Tanzania Social Action Fund (Mfuko wa Maendeleo ya Jamii) |
| TAWA | Tanzania Wildlife Management Authority (Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania) |
| TAZARA | Tanzania Zambia Railway Authority (Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia) |
| TBA | Tanzania Building Agency (Wakala wa Majengo Tanzania) |
| TBC | Tanzania Broadcasting Corporation (Shirika la Utangazaji Tanzania) |
| TBS | Tanzania Bureau of Standards (Shirika la Viwango Tanzania) |
| TCAA | Tanzania Civil Aviation Authority (Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania) |
| TCB | Tanzania Commercial Bank (Benki ya Biashara Tanzania) |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TEMDO | Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organisation (Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania) |
| TEMESA | Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency (Wakala wa Ufundi na Umeme) |
| TIC | Tanzania Investment Centre (Kituo cha Uwekezaji Tanzania) |
| TIRA | Tanzania Insurance Regulatory Authority (Mamlaka ya Usimamazi wa Bima Tanzania) |
| TIRDO | Tanzania Industrial Research and Development Organization (Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania) |
| TMA | Tanzania Meteorological Authority (Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania) |

| | |
|---|---|
| TMX | Tanzania Merchantile Exchange (Soko la Bidhaa Tanzania) |
| TPA | Tanzania Ports Authority (Mamlaka ya Bandari Tanzania) |
| TRA | Tanzania Revenue Authority (Mamlaka ya Mapato Tanzania) |
| TRC | Tanzania Railway Corporation (Shirika la Reli Tanzania) |
| UCSAF | The Universal Communications Service Access Fund (Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote) |
| VETA | Vocational Education and Training Authority (Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi) |
| VVU | Virusi vya Ukimwi |
| WCF | Workers Compensation Fund (Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi) |
| WEO | World Economic Outlook |
| WMA | Weight and Measurement Agency (Wakala wa Vipimo) |
| WTO | The World Trade Organization (Shirika la Biashara Duniani) |

## MATUKIO YA KIUCHUMI KATIKA MWAKA 2025

| Na. | TAREHE | MWEZI | TUKIO |
|---|---|---|---|
| 1 | 27- 28 | Januari | Kufanyika kwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi kuhusu masuala ya Nishati Afrika - Misheni 300 uliolenga kuwa na nishati endelevu na ya uhakika kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya nchi za Afrika. |
| 2 | 01 | Februari | Uzinduzi wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 Toleo la Mwaka 2023 yenye mtaala uliboreshwa kwa lengo la kuwawezesha wahitimu kujiajiri au kuajirika. |
| 3 | 26 | Machi | Kufanyika kwa hafla ya utiaji saini Mkataba wa mradi wa ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu Dodoma wenye uwezo wa kubeba mashabiki 32,500 kwa ajili ya maandalizi ya kombe la Mataifa ya Afrika - AFCON ambapo Tanzania ni mwandaaji mweza wa mashindano hayo. |
| 4 | 19 | Juni | Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan azindua Daraja la JPM maarufu kama Kigongo-Busisi ambalo ni refu zaidi Afrika Mashariki na Kati lenye urefu wa kilomita 3.0 na linaunganisha Wilaya za Misungwi na Sengerema mkoani Mwanza. |
| 5 | 31 | Julai | Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan azindua rasmi Bandari Kavu ya Kwala na huduma ya usafiri wa treni ya mizigo kupitia reli ya kisasa - SGR kati ya Dar es Salaam na Dodoma kwa lengo la kupunguza msongamano bandarini na barabarani, gharama za usafirishaji na kuongeza fursa za biashara na ajira kwa watanzania. |
| 6 | 30 | Septemba | Kufikia ukomo kwa Mkataba wa biashara kati ya Marekani na nchi za Afrika za Kusini mwa Jangwa la Sahara, ujulikanao kama AGOA (African Growth and Opportunity Act), uliokuwa mahususi kwa ajili ya kuwezesha nchi za Afrika kuuza bidhaa katika masoko ya Marekani bila kulipa kodi. |
| 7 | 29 | Oktoba | Kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani. |

## Jedwali A: TAKWIMU MUHIMU KATIKA UCHUMI - TANZANIA BARA


| Maelezo | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watu Tanzania Bara (Milioni) | 54.3 | 55.9 | 57.7 | 59.9 | 62.4 | 64.2 | 66.1 | 3.0 |
| Pato la Taifa kwa Bei za miaka inayohusika (Sh. Milioni) | 139,135,212 | 149,836,983 | 161,991,897 | 179,409,952 | 193,359,937 | 211,974,663 | 234,104,003 | 10.4 |
| Pato la Taifa kwa Bei za mwaka 2019 (Sh. Milioni) | 139,135,212 | 144,176,142 | 151,203,623 | 158,084,440 | 166,366,353 | 175,727,157 | 186,102,786 | 5.9 |
| Wastani Pato kwa Mtu (Shs.) | 2,563,988 | 2,677,284 | 2,806,299 | 2,997,593 | 3,096,626 | 3,299,637 | 3,544,124 | 7.4 |
| Mfumuko wa Bei (Asilimia) | 3.4 | 3.3 | 3.7 | 4.3 | 3.8 | 3.1 | 3.3 | 6.5 |
| Urari wa Biashara ya Bidhaa (US$ milioni) | -3,237.60 | -1,460.00 | -3,247.70 | -6,984.90 | -6,032.30 | -5,074.0 | -4,524.8 | -10.8 |
| Saruji Iliyotumika (Tani ) | 6,104,108 | 5,887,775 | 6,863,004 | 7,532,173 | 7,950,515 | 7,705,918 | 9,324,518 | 21.0 |
| Umeme Uliouzwa (GWH)* | 6,642.60 | 6,674.30 | 7,313.20 | 7,729.60 | 8,232.00 | 9,114.7 | 9,713.0 | 6.6 |
| Utalii (Mapato US$ milioni) | 2,604 | 715 | 1,248 | 2,527.8 | 3,373.8 | 3,903.0 | 4,410.6 | 13.0 |
| Elimu: Wanafunzi katika Shule za Msingi ('000) * | 10,605 | 10,925 | 11,196.80 | 11,420.97 | 11,425.48 | 11,391.19 | 11,428.4 | 0.3 |
| Elimu: Wanafunzi katika Shule za Sekondari ('000) * | 2,338 | 2,473 | 2,671.90 | 2,823.60 | 3,077.36 | 3,314.19 | 3,425.8 | 3.4 |
| Hospitali: Idadi ya Vitanda | 80,164 | 84,162 | 86,131 | 104,687 | 125,500 | 145,374 | 156,932 | 8.0 |
| **Thamani ya Mauzo Nje ya Mazao Muhimu ya Biashara (Dola za Marekani Milioni)** | | | | | | | | |
| **Bidhaa Asilia** | | | | | | | | |
| Kahawa | 152.2 | 145 | 155.2 | 161.2 | 227.9 | 292.9 | 361.3 | 28.5 |
| Pamba | 91.8 | 87.5 | 81.3 | 103.4 | 101.9 | 69.3 | 99.1 | -32.0 |
| Katani | 19.3 | 17.6 | 20.2 | 24.3 | 20.4 | 23.4 | 34.5 | 14.7 |
| Chai | 45.7 | 32.4 | 32.9 | 30 | 31.1 | 19.4 | 14.5 | -37.6 |
| Tumbaku | 146.5 | 148.7 | 127.5 | 178.5 | 340.4 | 509.5 | 561.1 | 49.7 |
| Korosho | 353.1 | 359.6 | 159 | 226.9 | 206.4 | 541.7 | 398.8 | 162.5 |
| Karafuu | 9.1 | 17.1 | 51.8 | 42.1 | 25.1 | 17.1 | 22.5 | -31.9 |
| **Bidhaa zisizo Asilia** | | | | | | | | |
| Madini | 2,326.70 | 3369.1 | 3,116.40 | 3,395.30 | 3,551.40 | 4,119.9 | 5,401.9 | 16.0 |
| Bidhaa za Viwanda | 851.8 | 908.6 | 1,200.00 | 1,419.20 | 1,363.30 | 1,341.3 | 1,595.8 | -1.6 |
| Samaki na Mazao ya Samaki | 168 | 139.6 | 164.3 | 168.2 | 164.0 | 180.6 | 161.2 | 10.1 |
| Mazao ya Mboga na Maua | 202.4 | 274.1 | 378.6 | 289.6 | 417.2 | 507.1 | 443.6 | 21.5 |
| Bidhaa zilizouzwa tena (Re-export) | 242.8 | 87.7 | 90.2 | 131.2 | 135.2 | 240.8 | 130.9 | 78.1 |
| Bidhaa nyinginezo | 394.3 | 474.2 | 813.5 | 654.9 | 690.5 | 839.1 | 731.2 | 21.5 |
| **Ujazi wa Fedha** | | | | | | | | |
| Ujazi wa Fedha - M3 (Sh. bilioni) | 28,313.10 | 29,920.60 | 34,558.00 | 38,580.00 | 44,002.60 | 48,905.30 | 61,524.29 | 25.8 |
| Karadha (Sh. bilioni) | 28,103.30 | 26,139.60 | 30,030.50 | 37,557.30 | 43,455.91 | 47,499.00 | 57,178.59 | 20.4 |
| **Fedha za Serikali** | **2019/20** | **2020/21** | **2021/22** | **2022/23** | **2023/24** | **2024/25** | **2025/26 (Matarajio)** | **Badiliko (Asilimia)** |
| Mapato ya Ndani ya Serikali (Sh. milioni) | 21,051,755 | 20,594,735 | 24,395,567 | 26,277,887 | 29,829,895 | 34,845,867 | 41,027,366 | 17.7 |
| Matumizi ya Kawaida ya Serikali (Sh. milioni) | -14,201,148 | -14,883,723 | -15,817,056 | -20,475,132 | -21,931,209 | -26,674,397 | -31,420,652 | 17.8 |
| Matumizi ya Maendeleo ya Serikali (Sh. milioni) | -9,926,993 | -11,701,584 | -15,080,341 | -15,682,330 | -14,636,421 | -15,402,723 | -17,353,600 | 12.7 |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha

## Jedwali B: MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI JUMLA NA BAJETI

| Mwaka wa Kalenda | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PATO LA TAIFA** | | | | | | | | |
| Ukuaji halisi wa Pato la Taifa Bei za Mwaka 2019 (Mp) | 6.6% | 6.4% | 3.6% | 4.9% | 4.6% | 5.2% | 5.6% | 5.9% |
| Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika (Mp) | 11.3% | 8.4% | 7.7% | 8.1% | 10.8% | 7.8% | 9.6% | 10.4% |
| Uwiano wa Uwekezaji na Pato la Taifa (Investment/GDP) | 31.8% | 35.7% | 34.2% | 37.4% | 40.7% | 38.3% | 38.9% | 36.5% |
| Uwiano wa Akiba kwa Pato la Taifa (Savings/GDP) | 31.9% | 34.8% | 33.4% | 34.3% | 34.7% | 35.9% | 38.2% | 38.6% |
| **MWENENDO WA BEI NA VIWANGO VYA RIBA** | | | | | | | | |
| Kasi ya Upandaji wa Bei (mwisho wa kipindi) | 3.3% | 3.8% | 3.2% | 4.2% | 4.8% | 3.0% | 3.1% | 3.6% |
| Kasi ya Upandaji wa Bei (wastani wa mwaka) | 3.5% | 3.4% | 3.3% | 3.7% | 4.3% | 3.8% | 3.1% | 3.3% |
| GDP deflator Inflation (MP) | 4.4% | 1.9% | 3.9% | 3.1% | 5.9% | 2.4% | 3.8% | 4.3% |
| Riba za Mikopo (mwaka mmoja) | 18.25% | 16.69% | 15.73% | 16.43% | 16.79% | 16.53% | 15.82% | 15.69% |
| Riba za Amana za muda maalum (miezi 12) | 8.78% | 8.80% | 8.28% | 8.32% | 8.53% | 9.17% | 9.17% | 9.58% |
| Tofauti ya riba za amana na za mikopo (mwaka) | 9.47% | 7.89% | 7.45% | 8.11% | 8.26% | 7.36% | 6.65% | 6.11% |
| Thamani ya Tshs/USD (wastani wa mwaka) | 2,275.4 | 2,299.8 | 2,305.6 | 2,309.2 | 2,314.5 | 2,395.7 | 2,610.5 | 2,549.8 |
| **UJAZI WA FEDHA** | | | | | | | | |
| Kiwango cha ukuaji wa M3 | 4.5% | 9.6% | 5.7% | 15.5% | 11.6% | 14.1% | 11.1% | 25.8% |
| Kiwango cha ukuaji wa M2 | 3.8% | 11.8% | 8.2% | 17.6% | 12.1% | 11.9% | 9.3% | 29.6% |
| Mikopo Chechefu | 10.7% | 9.8% | 9.8% | 8.5% | 5.8% | 4.3% | 3.3% | 2.8% |
| Kiwango cha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi | 4.9% | 11.1% | 3.1% | 10.0% | 22.5% | 17.1% | 12.4% | 23.6% |
| **UWIANO WA MIZANIA YA MALIPO YA NJE NA PATO LA TAIFA** | | | | | | | | |
| Bidhaa zilizouzwa nje | 7.9% | 9.0% | 9.6% | 9.5% | 9.1% | 9.5% | 11.4% | 11.3% |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 14.8% | 15.8% | 12.9% | 13.7% | 15.0% | 16.9% | 19.5% | 18.2% |
| Bidhaa zilizonunuliwa kutoka nje | 14.7% | 13.9% | 11.9% | 13.9% | 18.2% | 16.8% | 17.4% | 15.4% |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 17.9% | 16.7% | 13.8% | 16.1% | 21.2% | 19.4% | 20.2% | 18.7% |
| Urari wa malipo ya kawaida | -4.0% | -2.2% | -2.2% | -3.4% | -7.1% | -3.7% | -2.9% | -2.2% |
| Akiba ya fedha za kigeni (miezi ya Uagizaji) | 4.6 | 5.9 | 5.3 | 6.2 | 4.7 | 4.5 | 4.4 | 4.9 |
| **UWIANO WA BAJETI YA SERIKALI NA PATO LA TAIFA** | | | | | | | | |
| **Mwaka wa fedha** | **2017/18** | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** | **2021/22** | **2022/23** | **2023/24** | **2024/25** |
| Mapato ya ndani | 14.7% | 13.9% | 14.6% | 13.2% | 14.1% | 13.9% | 14.6% | 15.5% |
| Mapato ya kodi | 12.4% | 11.5% | 12.1% | 11.1% | 11.7% | 11.5% | 12.2% | 12.8% |
| Matumizi (Bila rollover) | 16.8% | 16.6% | 16.7% | 17.1% | 18.2% | 18.5% | 18.0% | 18.9% |
| Matumizi ya kawaida | 10.2% | 10.3% | 9.8% | 9.5% | 9.4% | 11.0% | 10.8% | 12.0% |
| Matumizi ya maendeleo | 6.6% | 6.3% | 6.9% | 7.5% | 8.8% | 7.5% | 7.2% | 6.9% |
| Misaada | 0.8% | 0.3% | 0.6% | 0.5% | 0.4% | 0.3% | 0.3% | 0.4% |
| Nakisi (kabla ya misaada) | -2.7% | -3.5% | -2.5% | -4.3% | -3.9% | -4.4% | -3.4% | -3.4% |
| Nakisi (baada ya misaada) | -1.9% | -3.2% | -1.9% | -3.9% | -3.5% | -4.1% | -3.1% | -3.1% |
| Mikopo ya nje | 1.4% | 0.9% | 1.6% | 1.7% | 1.8% | 1.7% | 2.0% | 1.3% |
| Mikopo ya ndani (kutoka benki) | -0.3% | 1.8% | -0.3% | 1.2% | 1.1% | 0.8% | -0.1% | 0.0% |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha




Sehemu ya Kwanza

# Maendeleo ya Uchumi Jumla

## SURA YA 1


## HALI YA UCHUMI WA TAIFA

**Ukuaji wa Uchumi**

1. Mwaka 2025, Serikali kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilikamilisha maboresho ya takwimu za Pato la Taifa kwa kutumia mwaka 2019 kama mwaka wa kizio kutoka mwaka wa kizio wa 2015. Kufuatia maboresho hayo, mabadiliko kadhaa yalijitokeza ikiwemo mfumo na ukubwa wa Pato la Taifa; viwango vya ukuaji, mchango wa shughuli za kiuchumi katika Pato la Taifa; na uwiano wa viashiria mbalimbali vya kiuchumi kwa Pato la Taifa. Maelezo ya kina kuhusu maboresho hayo yako katika Sura ya 20. Kutokana na maboresho hayo, kuanzia toleo hili takwimu zitakazotumika zitakuwa za mwaka wa kizio wa 2019.


2. Kwa mujibu wa takwimu mpya za mwaka wa kizio wa 2019, uchumi wa Taifa uliendelea kuimarika ambapo Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 5.6 mwaka 2024 (**Kielelezo Na. 1.1**). Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi, kuimarika kwa miundombinu ya usafiri na usafirishaji, kuimarika kwa shughuli za kilimo, kuongezeka kwa uzalishaji wa madini na shughuli za ujenzi wa umma na binafsi pamoja na utekelezaji wa miradi ya kimkakati, hususan katika sekta za nishati, usafirishaji na huduma za jamii.

**Kielelezo Na. 1.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi, Mwaka 2017 - 2025**




3. Shughuli za fedha na bima ziliongoza kwa ukuaji wa asilimia 15.7 kutokana na kuongezeka kwa amana za wateja katika benki za biashara na mikopo kwa sekta binafsi. Hii ilifuatiwa na shughuli za uzalishaji na usambazaji umeme na gesi (asilimia 11.8) kufuatia kuongezeka kwa uzalishaji kupitia Bwawa la kuzalisha umeme wa maji la Julius Nyerere; na uchimbaji madini na mawe (asilimia 9.4) kutokana na kuongezeka kwa mauzo na bei ya dhahabu katika soko la dunia. Sekta nyingine zilizofuatia kwa kuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji ilikuwa habari na mawasiliano (asilimia 8.8), sanaa na burudani (asilimia 8.5) na usafirishaji na uhifadhi mizigo (asilimia 8.0) kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 1.2.** Ukuaji huo unaakisi kuongezeka kwa uwekezaji, matumizi ya teknolojia pamoja na mahitaji ya huduma hizo.

**Kielelezo Na. 1.2: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi (Asilimia), Mwaka 2024 - 2025**





4. Mwaka 2025, shughuli za kilimo zilikuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa zikichangia asilimia 24.3 ya Pato Ghafi la Taifa ikifuatiwa na shughuli za ujenzi (asilimia 11.9), uchimbaji madini na mawe (asilimia 10.3) na biashara na matengenezo (asilimia 8.6) kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 1.3a.** Shughuli hizo kwa ujumla zilichangia asilimia 55.1 ya Pato Ghafi la Taifa na hivyo kuashiria kuwa ziliendelea kuwa mhimili wa uchumi. Aidha, shughuli za kilimo, fedha na bima, usafirishaji na uhifadhi mizigo, uchimbaji madini na mawe pamoja na ujenzi zilikuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa Pato la Taifa (**Kielelezo Na. 1.3b**).

**Kielelezo Na. 1.3a: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa, Mwaka 2025 (Asilimia)**





**Kielelezo Na. 1.3b: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Ukuaji wa Pato la Taifa, Mwaka 2025**




**Pato la Taifa kwa Mtu**

5. Miongoni mwa matokeo ya maboresho ya takwimu za Pato la Taifa ni kuongezeka kwa Pato la Wastani la kila mtu. Pato la Taifa kwa bei za miaka husika lilifikia shilingi milioni 234,104,003.29 mwaka 2025, sawa na dola za Marekani milioni 91,812.69. Aidha, idadi ya watu Tanzania bara ilifikia 66,054,123 mwaka 2025 ikilinganishwa na watu 64,241,822 mwaka 2024. Kutokana na mwenendo huo, wastani wa Pato la Taifa kwa mtu uliongezeka kwa asilimia 7.4 na kufikia shilingi 3,544,124 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi 3,299,637 mwaka 2024 (**Kielelezo Na. 1.4**). Kiasi hicho ni sawa na takribani dola za Marekani 1,390 kwa mtu mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,264 kwa mtu mwaka 2024.

**Kielelezo Na. 1.4: Pato la Taifa kwa Mtu (Shilingi 000'), Mwaka 2018 - 2025**




**Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi**

**Kilimo**

6. Mwaka 2025, shughuli za kilimo zinazojumuisha kilimo mazao, mifugo, misitu, uvuvi na huduma za kilimo zilikua kwa asilimia 5.5 ikilinganishwa na asilimia 5.1 mwaka 2024. Ukuaji huo ulitokana na uwepo wa hali nzuri ya hewa, matumizi ya pembejeo bora za kilimo, teknolojia na huduma za ugani pamoja na utoaji wa ruzuku ya mbolea uliochangia kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao. Sababu nyingine ni pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za mifugo pamoja na kuimarika kwa usimamizi wa uvunaji wa mazao ya uvuvi na uvunaji endelevu wa bidhaa za misitu. Shughuli ndogo za misitu ziliongoza kwa ukuaji wa asilimia 7.4, ikifuatiwa na huduma katika shughuli za kilimo (asilimia 6.4), uvuvi (asilimia 6.3), mifugo (asilimia 5.3) na kilimo cha mazao (asilimia 5.0).

7. Mwaka 2025, shughuli za kilimo sehemu inayouzika zilikua kwa asilimia 5.5 na sehemu isiyouzika asilimia 5.4 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.3 kwa sehemu inayouzika na asilimia 4.7 sehemu isiyouzika mwaka 2024. Aidha, mchango wa sekta ya kilimo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 24.3 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 24.9 mwaka 2024. Hii inatokana na jitihada za Serikali katika kuimarisha shughuli nyingine za kiuchumi ili kupunguza utegemezi kwa shughuli chache za kiuchumi.

**Viwanda na Ujenzi**

8. Mwaka 2025, shughuli za uchimbaji madini na mawe zilikua kwa asilimia 9.4 ikilinganishwa na asilimia 8.1 mwaka 2024. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa

uzalishaji wa madini, hususan dhahabu, almasi, tanzanite na jasi kufuatia kuimarika kwa bei na kuongezeka kwa mahitaji ndani na nje ya nchi pamoja na kuimarika kwa ununuzi wa dhahabu unaofanywa na Benki Kuu ya Tanzania. Aidha, mchango wa shughuli za uchimbaji madini na mawe katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 10.3 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 7.8 mwaka 2024.

9. Mwaka 2025, shughuli za uzalishaji viwandani zilikua kwa asilimia 5.2 mwaka 2025 ikilinganishwa na akuaji wa asilimia 4.9 mwaka 2024. Ukuaji huo ulitokana na Serikali kuendelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara pamoja na kuhamasisha uzalishaji wa ndani na uongezaji thamani. Aidha, mchango wa shughuli za uzalishaji viwandani katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 5.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2024.

10. Mwaka 2025, shughuli za uzalishaji na usambazaji umeme na gesi zilikua kwa asilimia 11.8 ikilinganishwa na asilimia 7.8 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme wa maji kufuatia kukamilika kwa bwawa la kuzalisha umeme wa maji la Julius Nyerere na matumizi ya nishati mbadala ikiwemo umeme wa jua. Hata hivyo, mchango wa shughuli za uzalishaji na usambazaji umeme na gesi katika Pato la Taifa ulipungua hadi asilimia 0.3 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 0.4 mwaka 2024.

11. Mwaka 2025, shughuli za usambazaji wa majisafi na udhibiti wa majitaka zilikua kwa asilimia 3.0 ikilinganishwa na asilimia 4.8 mwaka 2024. Katika kipindi hicho, mchango wa shughuli hizo katika Pato la Taifa uliendelea kuwa asilimia 0.4 kama ilivyokuwa mwaka 2024. Aidha, shughuli za usambazaji wa majisafi na udhibiti wa majitaka sehemu inayouzika ilikua kwa asilimia 1.9 na sehemu isiyouzika ilikua kwa asilimia 6.8 mwaka 2025 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.8 kwa sehemu inayouzika na isiyouzika mwaka 2024.

12. Mwaka 2025, shughuli za ujenzi zilikua kwa asilimia 4.0 ikilinganishwa na asilimia 3.0 mwaka 2024. Ongezeko la ukuaji lilitokana na kuendelea kwa utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya kiuchumi na majengo ya kijamii pamoja na kuongezeka kwa ujenzi wa sekta binafsi. Hii imejidhihirisha katika kuongezeka kwa matumizi ya bidhaa za saruji na chuma ambazo ni muhimu katika shughuli za ujenzi. Katika kipindi hicho, matumizi ya saruji yaliongezeka kwa asilimia 21.0 na kufikia tani 9,324,518 ikilinganishwa na tani 7,705,918 mwaka 2024. Hata hivyo, mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa ulipungua hadi asilimia 11.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 12.5 mwaka 2024. Aidha, shughuli za ujenzi sehemu isiyouzika zilikua kwa asilimia 6.3 na sehemu inayouzika ilikua kwa asilimia 3.8 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 7.4 sehemu isiyouzika na asilimia 2.8 sehemu inayouzika mwaka 2024, mtawalia.

**Huduma**

13. Mwaka 2025, shughuli za biashara na matengenezo zilikua kwa asilimia 5.1 ikilinganishwa na asilimia 4.9 mwaka 2024. Ukuaji huo ulichangiwa na kuendelea kuimarishwa kwa mazingira ya uwekezaji na biashara pamoja na upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Katika kipindi hicho, mchango wa shughuli za biashara na matengenezo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.6 kama ilivyokuwa mwaka 2024. Aidha, shughuli za usafirishaji na uhifadhi mizigo zilikua kwa asilimia 8.0 ikilinganishwa na asilimia 7.2 mwaka 2024. Ukuaji huo ulichangiwa na ongezeko la mizigo na idadi ya abiria waliosafirishwa kupitia huduma za usafiri wa barabarani na treni ya mwendo kasi. Shughuli za usafirishaji na uhifadhi wa mizigo zilichangia asilimia 8.3 katika pato la Taifa mwaka 2025 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 8.1 mwaka 2024.

14. Mwaka 2025, shughuli za huduma za malazi na chakula zilikuwa na ukuaji wa asilimia 3.6 ikilinganishwa na asilimia 4.1 mwaka 2024. Aidha, michango shughuli hizo katika Pato la Taifa ulipungua kwa nukta za asilimia 0.2 hadi asilimia 1.8 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 2.0 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na ongezeko dogo la watalii ambapo mwaka 2025 watalii walioingia nchini walifikia 2,294,495 ikiwa ni ongezeko la asilimia 7.1 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 18.5 mwaka 2024. Kwa upande mwingine, shughuli za upangishaji majengo zilikuwa na ukuaji wa asilimia 4.2 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 4.0 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na ongezeko la mahitaji ya majengo kwa ajili ya makazi na biashara. Shughuli za upangishaji majengo sehemu inayouzika zilikua kwa asilimia 4.3 na sehemu isiyouzika ilikua kwa asilimia 2.6 mwaka 2025.

15. Mwaka 2025, shughuli za habari na mawasiliano zilikuwa na ukuaji wa asilimia 8.8 ikilinganishwa na asilimia 11.2 mwaka 2024. Pamoja na kupungua kwa kiwango cha ukuaji, shughuli hii ilikuwa miongoni mwa shughuli tano zenye kiwango kikubwa cha ukuaji. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na kuendelea kutengamaa kwa sekta baada ya uwekezaji mkubwa uliofanyika. Aidha, mchango wa shughuli za habari na mawasiliano katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.6 ikilinganishwa na asilimia 1.7 mwaka 2024. Kwa upande mwingine, shughuli za huduma za fedha na bima ndizo zilikuwa na ukuaji mkubwa ikilinganishwa na shughuli nyingine, zikikua kwa asilimia 15.7 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 12.7 mwaka 2024. Aidha, michango wa shughuli za fedha na bima katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 4.3 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 3.9 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa amana za wateja katika benki za biashara, mikopo kwa sekta binafsi pamoja na kupungua kwa mikopo chechefu.

16. Mwaka 2025, ukuaji wa shughuli zinazohusiana na elimu ulikuwa asilimia 5.2 na shughuli za afya na huduma za jamii asilimia 6.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.5

na asilimia 7.3 mwaka 2024, mtawalia. Aidha, ukuaji wa shughuli za kitaaluma, sayansi na ufundi ulikuwa asilimia 5.6 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2024.

17. Mwaka 2025, shughuli za utawala wa umma na ulinzi zilikua kwa asilimia 5.8 ikiakisiwa na ongezeko la matumizi ya Serikali katika uendeshaji na utoaji wa huduma ikiwemo ulipaji wa mishahara na malimbikizo ya madai ya wafanyakazi na wazabuni pamoja na utekelezaji wa kazi za ulinzi na usalama. Aidha, huduma zinazohusiana na utawala zilikua kwa wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 2.1 mwaka 2024.

18. Mwaka 2025, shughuli za sanaa na burudani ziliendelea kuimarika ambapo ukuaji ulifikia asilimia 8.5 ikilinganishwa na asilimia 4.8 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za sanaa ya maonesho, uendeshaji wa makumbusho, michezo na burudani. Katika kipindi hicho, mchango wa shughuli za sanaa na burudani katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.3 kama ilivyokuwa mwaka 2024.

19. Mwaka 2025, ukuaji wa shughuli za kaya katika kuajiri ulikuwa asilimia 2.8 ikilinganishwa na asilimia 2.9 mwaka 2024. Katika kipindi hicho, mchango wa shughuli hizi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 0.2 kama ilivyokuwa mwaka 2024. Aidha, huduma nyingine za kijamii ambazo zinajumuisha shughuli za mashirika ya uanachama, ukarabati wa vifaa vya kieletroniki na bidhaa za kibinafsi za nyumbani na huduma za binafsi zilikua kwa asilimia 5.4 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2024. Shughuli hizo zilichangia asilimia 1.2 katika Pato la Taifa kama ilivyokuwa mwaka 2024.

**Mfumuko wa Bei**

20. Mwaka 2025, mfumuko wa bei ulikuwa wa wastani wa asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa bei za vyakula. Pamoja na ongezeko hilo, kiwango hicho kilikuwa ndani ya lengo la nchi la muda wa kati la asilimia 3.0 hadi 5.0 na kilikidhi vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (asilimia isiyozidi 8.0) pamoja na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (asilimia 3.0 hadi 7.0), kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1.1**.


**Jedwali Na. 1.1: Fahirisi za Kitaifa za Bei ya Mtumiaji na Mfumuko wa Bei (Kizio 2020 = 100), Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | | Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | Fahirisi Bidhaa Zote |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uzito | | 28.2 | 1.9 | 10.8 | 15.1 | 7.9 | 2.5 | 14.1 | 5.4 | 1.6 | 2.0 | 6.6 | 2.1 | 2.1 | 100.0 |
| 2021 | Fahirisi za Bei | 104.3 | 102.2 | 104.6 | 104.1 | 103.2 | 102.7 | 103.3 | 101.8 | 102.7 | 101.1 | 104.9 | 100.3 | 102.8 | 103.7 |
| 2022 | | 111.9 | 103.5 | 107.1 | 107.8 | 106.8 | 104.2 | 109.6 | 102.8 | 104.3 | 101.7 | 107.3 | 100.4 | 105.2 | 108.2 |
| 2023 | | 119.5 | 105.9 | 110.4 | 109.5 | 110.2 | 105.9 | 112.7 | 104.5 | 106.6 | 105.1 | 111.9 | 100.5 | 108.2 | 112.3 |
| 2024 | | 122.0 | 109.0 | 112.6 | 115.2 | 113.3 | 107.9 | 117.4 | 106.0 | 109.7 | 108.4 | 115.7 | 101.7 | 115.4 | 115.7 |
| 2025 | | 129.9 | 112.7 | 114.8 | 118.1 | 116.1 | 109.4 | 120.0 | 106.3 | 111.0 | 112.1 | 117.2 | 102.3 | 118.1 | 119.6 |
| 2021 | Mfumuko wa Bei | 4.3 | 2.2 | 4.6 | 4.1 | 3.2 | 2.7 | 3.3 | 1.8 | 2.7 | 1.1 | 4.9 | 0.3 | 2.8 | 3.7 |
| 2022 | | 7.3 | 1.2 | 2.5 | 3.6 | 3.5 | 1.4 | 6.1 | 0.9 | 1.5 | 0.6 | 2.3 | 0.1 | 2.3 | 4.3 |
| 2023 | | 6.8 | 2.4 | 3.0 | 1.6 | 3.2 | 1.7 | 2.8 | 1.7 | 2.2 | 3.4 | 4.3 | 0.1 | 2.9 | 3.8 |
| 2024 | | 2.1 | 3.0 | 2.0 | 5.2 | 2.8 | 1.9 | 4.2 | 1.4 | 2.9 | 3.1 | 3.4 | 1.3 | 6.6 | 3.1 |
| 2025 | | 6.4 | 3.4 | 1.9 | 2.5 | 2.5 | 1.4 | 2.2 | 0.3 | 1.2 | 3.4 | 1.3 | 0.6 | 2.3 | 3.3 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

21. Mwaka 2025, mfumuko wa bei wa msingi (core inflation) ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 2.2 ikilinganishwa na asilimia 3.4 mwaka 2024. Aidha, mfumuko wa bei katika kundi la nishati, mafuta na huduma za maji ulipungua na kufikia asilimia 4.3 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 9.3 mwaka 2024. Hii ilitokana na kupungua kwa bei za mafuta katika soko la dunia. Kwa upande wa chakula na vinywaji baridi, mfumuko wa bei uliongezeka hadi wastani wa asilimia 6.4 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 2.1 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa bei za mazao ya chakula, hususan ulezi, mahindi na mchele (**Kielelezo Na. 1.5**).

**Kielelezo Na. 1.5: Mfumuko wa Bei kwa Baadhi ya Makundi, Mwaka 2016 - 2025**




| | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfumuko wa bei | 5.2 | 5.3 | 3.5 | 3.4 | 3.3 | 3.7 | 4.3 | 3.8 | 3.1 | 3.3 |
| Chakula | 7.6 | 9.6 | 3.7 | 4.3 | 5.0 | 4.3 | 7.3 | 6.8 | 2.1 | 6.4 |
| Nishati | 6.3 | 10.5 | 17.2 | 9.0 | 5.0 | 3.1 | 9.1 | 2.3 | 9.3 | 4.3 |
| Msingi | 2.6 | 2.0 | 1.9 | 3.0 | 2.3 | 4.1 | 3.0 | 2.3 | 3.4 | 2.2 |

22. Mwaka 2025, mfumuko wa bei kwa wakazi wa Dar es Salaam ulipungua kwa matabaka yote ya kipato (**Jedwali Na. 1.2**). Kwa tabaka la kipato cha chini, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 4.6 ikilinganishwa na asilimia 5.8 mwaka 2024; tabaka la kati ulikuwa wastani wa asilimia 4.5 ikilinganishwa na asilimia 7.9; na tabaka la juu ulikuwa wastani wa asilimia 3.9 ikilinganishwa na asilimia 6.2. Hii ilichangiwa na kupungua kwa bei za bidhaa na huduma zinazotumika kwa wingi katika matabaka yote ikiwemo usafiri, nishati na burudani.

**Jedwali Na. 1.2: Mfumuko wa Bei za Bidhaa na Huduma kwa Wakazi wa Dar es Salaam kwa Kipato (Msingi 2020 = 100), Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | Fahirisi Bidhaa Zote |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **WAKAZI WENYE KIPATO CHA CHINI** | | | | | | | | | | | | | | |
| **2021** | 0.6 | 7.3 | 3.1 | 2.9 | 3.9 | 1.9 | -7.4 | 1.4 | 3.8 | 10.3 | 5.5 | 0.0 | 0.7 | 2.4 |
| **2022** | 7.5 | 0.5 | 3.7 | 3.9 | 6.3 | 2.9 | -2.1 | 1.8 | 13.3 | 2.3 | 3.0 | 0.0 | 3.5 | 4.7 |
| **2023** | 9.8 | 0.7 | 2.4 | 3.4 | 5.3 | 9.1 | -8.4 | 1.0 | 13.8 | 4.4 | 1.9 | 0.0 | 3.5 | 5.2 |
| **2024** | 4.4 | 3.2 | 3.8 | 11.5 | 3.9 | 8.6 | 21.0 | 0.6 | 16.2 | 3.9 | 2.3 | 0.1 | 9.4 | 5.8 |
| **2025** | 9.0 | 1.0 | 5.3 | 2.5 | 3.6 | 0.7 | 4.5 | 0.0 | 4.7 | 1.8 | 0.4 | 0.0 | 2.4 | 4.6 |
| **WAKAZI WENYE KIPATO CHA KATI** | | | | | | | | | | | | | | |
| **2021** | 1.2 | 4.2 | 0.7 | -1.1 | 4.1 | 4.0 | 2.7 | 1.3 | 0.5 | 5.4 | 10.1 | 0.4 | 0.7 | 2.4 |
| **2022** | 9.5 | 0.5 | 2.6 | 5.0 | 4.5 | 1.8 | 7.3 | 0.2 | 16.5 | 1.2 | 3.7 | 0.1 | 3.4 | 5.8 |
| **2023** | 9.9 | 4.0 | 3.0 | 2.5 | 3.8 | 3.5 | 1.2 | 0.0 | 6.4 | 2.8 | 2.9 | -0.1 | 3.5 | 4.9 |
| **2024** | 5.6 | 9.6 | 5.6 | 14.3 | 5.2 | 5.1 | 17.9 | 1.6 | 5.3 | 3.6 | 4.3 | 0.1 | 8.9 | 7.9 |
| **2025** | 8.6 | 1.4 | 4.7 | -0.5 | 4.8 | 1.3 | 4.2 | 0.5 | 1.7 | 10.0 | 0.9 | 0.0 | 2.6 | 4.5 |
| **WAKAZI WENYE KIPATO CHA JUU** | | | | | | | | | | | | | | |
| **2021** | 3.9 | 11.2 | 3.4 | 0.1 | 8.2 | 3.3 | 1.8 | 1.3 | -1.3 | 3.0 | 7.0 | 0.2 | 1.5 | 3.0 |
| **2022** | 4.8 | 2.3 | 3.1 | 3.4 | 2.5 | 2.0 | 5.9 | 1.1 | 2.3 | 0.8 | 4.0 | 0.0 | 2.3 | 3.8 |
| **2023** | 4.0 | 1.8 | 2.9 | 2.4 | 2.0 | 4.9 | 0.8 | 0.6 | 3.7 | 1.2 | 4.2 | -0.1 | 7.4 | 2.5 |
| **2024** | 5.1 | 5.4 | 5.5 | 8.5 | 3.8 | 4.9 | 5.8 | 4.7 | 9.2 | 6.0 | 5.2 | 0.4 | 26.4 | 6.2 |
| **2025** | 8.4 | 0.0 | 4.0 | 1.1 | 4.9 | 1.0 | 3.5 | 1.0 | 3.5 | 11.3 | 1.0 | 0.0 | 5.7 | 3.9 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Ukuzaji Rasilimali

23. Mwaka 2025, ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka 2019 uliongezeka kwa asilimia 2.2 na kufikia shilingi bilioni 71,354.7 kutoka shilingi bilioni 69,840.1 mwaka 2024. Kwa upande wa bei za mwaka husika, ukuzaji rasilimali ulifikia shilingi bilioni 85,516.8 mwaka 2025 kutoka shilingi bilioni 82,547.34 mwaka 2024. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 75,460.6 zilikuwa rasilimali za kudumu na shilingi bilioni 10,056.2 zilikuwa ongezeko la limbikizo. Aidha, uwiano wa ukuzaji rasilimali (kwa bei za mwaka husika) kwa Pato la Taifa ulikuwa asilimia 36.5 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 38.9 mwaka 2024. Hii

ilitokana na ongezeko kubwa la Pato la Taifa ikilinganishwa na kasi ya ukuzaji wa rasilimali kulikochangiwa na kupungua kwa malimbikizo ya rasilimali. (**Jedwali Na. 1.3**).


24. Mwaka 2025, majengo yaliendelea kuwa na mchango mkubwa wa asilimia 75.3 ya rasilimali zote ikifuatiwa na malimbikizo ya rasilimali (asilimia 11.8). Kwa upande wa mgawanyo wa sekta, ukuzaji rasilimali uliendelea kutawaliwa na sekta binafsi iliyokuwa na jumla ya shilingi bilioni 52,547.2, sawa na asilimia 69.6 ya rasilimali zote za kudumu (**Kielelezo Na. 1.6**). Hii inaonesha umuhimu wa sekta binafsi katika uwekezaji na ukuaji wa uchumi.

**Jedwali Na. 1.3: Ukuzaji Rasilimali (Shilingi Milioni), Mwaka 2024 - 2025**

| Aina ya Rasilimali/ Mwaka | Bei za mwaka 2019 | | Bei za miaka husika | | Mchango (Asilimia) | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2024** | **2025** | **2024** | **2025** | **2024** | **2025** |
| 1. Majengo | 47,296,176 | 49,197,305 | 61,341,767 | 64,425,392 | 74.3 | 75.3 |
| 2. Vifaa vya Usafiri | 4,659,950 | 4,747,255 | 3,397,840 | 3,488,733 | 4.1 | 4.1 |
| 3. Mitambo na Vifaa | 4,650,023 | 4,936,945 | 2,788,876 | 2,959,040 | 3.4 | 3.5 |
| 4. Mitambo na Vifaa vingine | 1,679,322 | 1,736,824 | 870,286 | 934,014 | 1.1 | 1.1 |
| 5. Rasilimali za Mazao ya Mifugo | 503,968 | 534,227 | 1,122,549 | 1,188,968 | 1.4 | 1.4 |
| 6. Haki ya Umiliki,Utafiti na Maendeleo na Huduma za Kitaalamu | 1,586,635 | 1,645,411 | 2,251,361 | 2,464,430 | 2.7 | 2.9 |
| **A. Rasilimali za kudumu (1+2+3+4+5+6)** | **60,376,075** | **62,797,966** | **71,772,679** | **75,460,577** | **86.9** | **88.2** |
| 7. Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 286,091 | 315,302 | 467,139 | 696,253 | 0.6 | 0.8 |
| 8. Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | 9,177,922 | 8,241,446 | 10,307,521 | 9,359,980 | 12.5 | 10.9 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali (A+7+8)** | **69,840,089** | **71,354,714** | **82,547,339** | **85,516,810** | **100** | **100** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kielelezo Na. 1.6: Ukuzaji Rasilimali za Kudumu kwa Sekta**



**Jedwali Na. 1: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, 2019 - 2025**

**Shilingi Milioni**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **34,531,749** | **37,721,484** | **40,397,852** | **44,642,340** | **48,551,924** | **52,873,630** | **56,826,257** |
| Kilimo cha Mazao | 18,476,138 | 19,792,431 | 20,480,487 | 22,724,998 | 25,022,645 | 27,096,205 | 29,769,595 |
| Mifugo | 9,445,788 | 10,921,487 | 12,026,380 | 12,950,839 | 14,021,127 | 15,134,993 | 15,689,296 |
| Misitu | 3,980,090 | 4,169,893 | 4,516,476 | 5,119,862 | 5,390,362 | 5,794,642 | 6,172,890 |
| Uvuvi | 2,587,867 | 2,791,990 | 3,325,857 | 3,796,017 | 4,061,799 | 4,786,931 | 5,128,759 |
| Huduma katika Shughuli za Kilimo | 41,866 | 45,683 | 48,652 | 50,625 | 55,991 | 60,858 | 65,718 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **37,621,647** | **42,629,018** | **46,687,864** | **51,547,613** | **54,298,706** | **59,254,634** | **67,456,948** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 7,382,971 | 10,570,922 | 11,494,048 | 12,038,251 | 13,084,076 | 16,569,193 | 24,119,805 |
| Viwanda | 10,123,642 | 10,954,377 | 12,393,952 | 13,409,855 | 13,908,275 | 14,425,003 | 13,823,046 |
| Umeme | 541,731 | 664,722 | 702,850 | 604,956 | 814,896 | 886,953 | 748,355 |
| Maji safi na Maji taka | 680,656 | 740,704 | 790,881 | 819,721 | 833,779 | 880,823 | 906,219 |
| Ujenzi | 18,892,648 | 19,698,292 | 21,306,134 | 24,674,829 | 25,657,679 | 26,492,662 | 27,859,523 |
| **Huduma** | **56,214,390** | **59,691,402** | **63,952,495** | **70,148,119** | **76,579,598** | **83,316,965** | **91,440,476** |
| Biashara na Matengenezo | 12,261,827 | 12,860,758 | 14,064,171 | 15,277,282 | 16,667,538 | 18,297,797 | 20,067,582 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 10,569,576 | 11,910,559 | 12,594,395 | 13,897,704 | 15,590,668 | 17,108,754 | 19,504,758 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 3,608,481 | 2,990,521 | 3,331,277 | 3,819,120 | 4,166,734 | 4,313,521 | 4,212,320 |
| Habari na Mawasiliano | 2,166,463 | 2,552,983 | 2,518,782 | 2,789,752 | 3,158,075 | 3,497,661 | 3,736,321 |
| Fedha na Bima | 5,075,182 | 5,656,024 | 5,763,932 | 7,018,583 | 7,434,680 | 8,357,599 | 10,024,522 |
| Upangishaji Majengo | 3,962,175 | 4,063,954 | 4,299,643 | 4,580,397 | 4,868,356 | 5,176,790 | 5,470,017 |
| Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 576,175 | 554,741 | 609,828 | 648,734 | 692,100 | 737,008 | 787,699 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 3,233,509 | 3,097,953 | 3,197,175 | 3,439,214 | 3,721,675 | 3,746,762 | 3,901,247 |
| Utawala na Ulinzi | 6,186,903 | 7,168,904 | 8,312,656 | 8,684,963 | 9,062,157 | 9,828,955 | 10,621,074 |
| Elimu | 3,599,275 | 3,749,111 | 3,826,798 | 4,114,142 | 4,651,031 | 5,027,391 | 5,359,507 |
| Afya na Huduma za Jamii | 2,409,985 | 2,433,387 | 2,680,963 | 2,949,801 | 3,252,894 | 3,650,046 | 3,854,222 |
| Sanaa na Burudani | 498,036 | 485,548 | 524,180 | 557,093 | 631,424 | 657,902 | 708,911 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 1,751,021 | 1,836,990 | 1,879,355 | 2,002,055 | 2,288,467 | 2,502,698 | 2,761,461 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 315,780 | 329,970 | 349,341 | 369,277 | 393,799 | 414,081 | 430,835 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **128,367,786** | **140,041,904** | **151,038,211** | **166,338,072** | **179,430,228** | **195,445,228** | **215,723,682** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 10,767,426 | 9,795,079 | 10,953,686 | 13,071,880 | 13,929,709 | 16,529,435 | 18,380,321 |
| **Pato la Taifa kwa bei za soko za miaka husika** | **139,135,212** | **149,836,983** | **161,991,897** | **179,409,952** | **193,359,937** | **211,974,663** | **234,104,003** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 2: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA, 2019 - 2025**

**Shilingi Milioni**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A: SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | | |
| **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **22,107,758** | **24,098,787** | **25,817,812** | **28,653,677** | **31,101,605** | **34,131,301** | **36,695,558** |
| Kilimo cha Mazao | 11,699,893 | 12,520,219 | 12,899,546 | 14,392,616 | 15,800,995 | 17,230,572 | 19,051,486 |
| Mifugo | 5,549,821 | 6,416,860 | 7,066,033 | 7,609,194 | 8,238,036 | 8,892,482 | 9,091,204 |
| Misitu | 2,566,590 | 2,688,997 | 2,912,473 | 3,301,431 | 3,475,734 | 3,736,194 | 3,999,169 |
| Uvuvi | 2,249,587 | 2,427,027 | 2,891,109 | 3,299,810 | 3,530,850 | 4,211,194 | 4,487,981 |
| Huduma katika Shughuli za Kilimo | 41,866 | 45,683 | 48,652 | 50,625 | 55,991 | 60,858 | 65,718 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **36,585,710** | **41,582,963** | **45,589,922** | **50,351,636** | **53,092,447** | **57,758,270** | **65,851,323** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 7,382,971 | 10,570,922 | 11,494,048 | 12,038,251 | 13,084,076 | 16,569,193 | 24,119,805 |
| Viwanda | 10,123,642 | 10,954,377 | 12,393,952 | 13,409,855 | 13,908,275 | 14,425,003 | 13,823,046 |
| Umeme | 541,731 | 664,722 | 702,850 | 604,956 | 814,896 | 886,953 | 748,355 |
| Maji safi na Maji taka | 528,283 | 577,155 | 617,270 | 639,779 | 650,752 | 684,284 | 707,814 |
| Ujenzi | 18,009,083 | 18,815,787 | 20,381,803 | 23,658,794 | 24,634,448 | 25,192,837 | 26,452,303 |
| **Huduma** | **56,056,822** | **59,529,786** | **63,781,507** | **69,965,965** | **76,385,993** | **83,111,094** | **91,222,645** |
| Biashara na Matengenezo | 12,261,827 | 12,860,758 | 14,064,171 | 15,277,282 | 16,667,538 | 18,297,797 | 20,067,582 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 10,569,576 | 11,910,559 | 12,594,395 | 13,897,704 | 15,590,668 | 17,108,754 | 19,504,758 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 3,608,481 | 2,990,521 | 3,331,277 | 3,819,120 | 4,166,734 | 4,313,521 | 4,212,320 |
| Habari na Mawasiliano | 2,166,463 | 2,552,983 | 2,518,782 | 2,789,752 | 3,158,075 | 3,497,661 | 3,736,321 |
| Fedha na Bima | 5,075,182 | 5,656,024 | 5,763,932 | 7,018,583 | 7,434,680 | 8,357,599 | 10,024,522 |
| Upangishaji Majengo | 3,804,607 | 3,902,339 | 4,128,655 | 4,398,244 | 4,674,752 | 4,970,919 | 5,252,185 |
| Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 576,175 | 554,741 | 609,828 | 648,734 | 692,100 | 737,008 | 787,699 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 3,233,509 | 3,097,953 | 3,197,175 | 3,439,214 | 3,721,675 | 3,746,762 | 3,901,247 |
| Utawala na Ulinzi | 6,186,903 | 7,168,904 | 8,312,656 | 8,684,963 | 9,062,157 | 9,828,955 | 10,621,074 |
| Elimu | 3,599,275 | 3,749,111 | 3,826,798 | 4,114,142 | 4,651,031 | 5,027,391 | 5,359,507 |
| Afya na Huduma za Jamii | 2,409,985 | 2,433,387 | 2,680,963 | 2,949,801 | 3,252,894 | 3,650,046 | 3,854,222 |
| Sanaa na Burudani | 498,036 | 485,548 | 524,180 | 557,093 | 631,424 | 657,902 | 708,911 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 1,751,021 | 1,836,990 | 1,879,355 | 2,002,055 | 2,288,467 | 2,502,698 | 2,761,461 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 315,780 | 329,970 | 349,341 | 369,277 | 393,799 | 414,081 | 430,835 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **114,750,289** | **125,211,536** | **135,189,242** | **148,971,278** | **160,580,046** | **175,000,665** | **193,769,526** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 10,767,426 | 9,795,079 | 10,953,686 | 13,071,880 | 13,929,709 | 16,529,435 | 18,380,321 |
| **Jumla ya Pato la Taifa - Sehemu inayouzika** | **125,517,716** | **135,006,615** | **146,142,927** | **162,043,158** | **174,509,755** | **191,530,100** | **212,149,847** |
| **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | | |
| **Jumla ya Pato la Taifa - sehemu isiyouzika** | **13,617,496** | **14,830,368** | **15,848,970** | **17,366,794** | **18,850,182** | **20,444,563** | **21,954,156** |
| Kilimo, Misitu na Uvuvi | **12,423,991** | **13,622,698** | **14,580,040** | **15,988,664** | **17,450,319** | **18,742,329** | **20,130,699** |
| Mazao | 6,776,244 | 7,272,212 | 7,580,942 | 8,332,382 | 9,221,650 | 9,865,633 | 10,718,108 |
| Mifugo | 3,895,967 | 4,504,628 | 4,960,347 | 5,341,645 | 5,783,091 | 6,242,511 | 6,598,092 |
| Misitu | 1,413,499 | 1,480,895 | 1,604,003 | 1,818,430 | 1,914,629 | 2,058,448 | 2,173,721 |
| Uvuvi | 338,280 | 364,962 | 434,748 | 496,207 | 530,949 | 575,737 | 640,778 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **1,035,938** | **1,046,055** | **1,097,942** | **1,195,977** | **1,206,258** | **1,496,364** | **1,605,625** |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 152,373 | 163,549 | 173,611 | 179,942 | 183,028 | 196,538 | 198,405 |
| Ujenzi | 883,564 | 882,506 | 924,331 | 1,016,035 | 1,023,231 | 1,299,826 | 1,407,220 |
| **Huduma** | **157,568** | **161,615** | **170,988** | **182,153** | **193,605** | **205,871** | **217,832** |
| Upangishaji Majengo | 157,568 | 161,615 | 170,988 | 182,153 | 193,605 | 205,871 | 217,832 |
| **Pato la Taifa (A+B) kwa bei za soko za miaka husika** | **139,135,212** | **149,836,983** | **161,991,897** | **179,409,952** | **193,359,937** | **211,974,663** | **234,104,003** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 3: MCHANGO KATIKA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, 2019 - 2025**

**Asilimia**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **24.8** | **25.2** | **24.9** | **24.9** | **25.1** | **24.9** | **24.3** |
| Kilimo cha Mazao | **13.3** | **13.2** | **12.6** | **12.7** | **12.9** | **12.8** | **12.7** |
| Mifugo | *6.8* | *7.3* | *7.4* | *7.2* | *7.3* | *7.1* | *6.7* |
| Misitu | *2.9* | *2.8* | *2.8* | *2.9* | *2.8* | *2.7* | *2.6* |
| Uvuvi | *1.9* | *1.9* | *2.1* | *2.1* | *2.1* | *2.3* | *2.2* |
| Huduma katika Shughuli za Kilimo | 0.03 | 0.03 | 0.03 | 0.03 | 0.03 | 0.03 | 0.03 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **27.0** | **28.5** | **28.8** | **28.7** | **28.1** | **28.0** | **28.8** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | *5.3* | *7.1* | *7.1* | *6.7* | *6.8* | *7.8* | *10.3* |
| Viwanda | *7.3* | *7.3* | *7.7* | *7.5* | *7.2* | *6.8* | *5.9* |
| Umeme | *0.4* | *0.4* | *0.4* | *0.3* | *0.4* | *0.4* | *0.3* |
| Maji safi na Maji taka | *0.5* | *0.5* | *0.5* | *0.5* | *0.4* | *0.4* | *0.4* |
| Ujenzi | *13.6* | *13.1* | *13.2* | *13.8* | *13.3* | *12.5* | *11.9* |
| **Huduma** | **40.4** | **39.8** | **39.5** | **39.1** | **39.6** | **39.3** | **39.1** |
| Biashara na Matengenezo | 8.8 | 8.6 | 8.7 | 8.5 | 8.6 | 8.6 | 8.6 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 7.6 | 7.9 | 7.8 | 7.7 | 8.1 | 8.1 | 8.3 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 2.6 | 2.0 | 2.1 | 2.1 | 2.2 | 2.0 | 1.8 |
| Habari na Mawasiliano | 1.6 | 1.7 | 1.6 | 1.6 | 1.6 | 1.7 | 1.6 |
| Fedha na Bima | 3.6 | 3.8 | 3.6 | 3.9 | 3.8 | 3.9 | 4.3 |
| Upangishaji Majengo | 2.8 | 2.7 | 2.7 | 2.6 | 2.5 | 2.4 | 2.3 |
| Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 0.4 | 0.4 | 0.4 | 0.4 | 0.4 | 0.3 | 0.3 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 2.3 | 2.1 | 2.0 | 1.9 | 1.9 | 1.8 | 1.7 |
| Utawala na Ulinzi | 4.4 | 4.8 | 5.1 | 4.8 | 4.7 | 4.6 | 4.5 |
| Elimu | 2.6 | 2.5 | 2.4 | 2.3 | 2.4 | 2.4 | 2.3 |
| Afya na Huduma za Jamii | 1.7 | 1.6 | 1.7 | 1.6 | 1.7 | 1.7 | 1.6 |
| Sanaa na Burudani | 0.4 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 1.3 | 1.2 | 1.2 | 1.1 | 1.2 | 1.2 | 1.2 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | 92.3 | 93.5 | 93.2 | 92.7 | 92.8 | 92.2 | 92.1 |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 7.7 | 6.5 | 6.8 | 7.3 | 7.2 | 7.8 | 7.9 |
| **Pato la Taifa kwa bei za soko za miaka husika** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 4: MCHANGO KATIKA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA, 2019 - 2025**

Asilimia

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A: SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | | |
| **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **15.9** | **16.1** | **16.1** | **16.0** | **16.2** | **16.0** | **15.7** |
| Kilimo cha Mazao | 8.4 | 8.4 | 8.0 | 8.0 | 8.2 | 8.1 | 8.1 |
| Mifugo | 4.0 | 4.3 | 4.4 | 4.2 | 4.3 | 4.2 | 3.9 |
| Misitu | 1.8 | 1.8 | 1.8 | 1.8 | 1.8 | 1.8 | 1.7 |
| Uvuvi | 1.6 | 1.6 | 1.8 | 1.8 | 1.8 | 2.0 | 1.9 |
| Huduma katika Shughuli za Kilimo | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **26.3** | **27.6** | **27.8** | **27.7** | **27.2** | **27.3** | **28.1** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 5.3 | 7.1 | 7.1 | 6.7 | 6.8 | 7.8 | 10.3 |
| Viwanda | 7.3 | 7.3 | 7.7 | 7.5 | 7.2 | 6.8 | 5.9 |
| Umeme | 0.4 | 0.4 | 0.4 | 0.3 | 0.4 | 0.4 | 0.3 |
| Maji safi na Maji taka | 0.4 | 0.4 | 0.4 | 0.4 | 0.3 | 0.3 | 0.3 |
| Ujenzi | 12.9 | 12.6 | 12.6 | 13.2 | 12.7 | 11.9 | 11.3 |
| **Huduma** | **40.3** | **39.8** | **39.5** | **39.2** | **39.6** | **39.2** | **39.0** |
| Biashara na Matengenezo | 8.8 | 8.6 | 8.7 | 8.5 | 8.6 | 8.6 | 8.6 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 7.6 | 7.9 | 7.8 | 7.7 | 8.1 | 8.1 | 8.3 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 2.6 | 2.0 | 2.1 | 2.1 | 2.2 | 2.0 | 1.8 |
| Habari na Mawasiliano | 1.6 | 1.7 | 1.6 | 1.6 | 1.6 | 1.7 | 1.6 |
| Fedha na Bima | 3.6 | 3.8 | 3.6 | 3.9 | 3.8 | 3.9 | 4.3 |
| Upangishaji Majengo | 2.7 | 2.6 | 2.5 | 2.5 | 2.4 | 2.3 | 2.2 |
| Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 0.4 | 0.4 | 0.4 | 0.4 | 0.4 | 0.3 | 0.3 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 2.3 | 2.1 | 2.0 | 1.9 | 1.9 | 1.8 | 1.7 |
| Utawala na Ulinzi | 4.4 | 4.8 | 5.1 | 4.8 | 4.7 | 4.6 | 4.5 |
| Elimu | 2.6 | 2.5 | 2.4 | 2.3 | 2.4 | 2.4 | 2.3 |
| Afya na Huduma za Jamii | 1.7 | 1.6 | 1.7 | 1.6 | 1.7 | 1.7 | 1.6 |
| Sanaa na Burudani | 0.4 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 1.3 | 1.2 | 1.2 | 1.1 | 1.2 | 1.2 | 1.2 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **82.5** | **83.6** | **83.5** | **83.0** | **83.0** | **82.6** | **82.8** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 7.7 | 6.5 | 6.8 | 7.3 | 7.2 | 7.8 | 7.9 |
| **Jumla ya Pato la Taifa - Sehemu inayouzika** | **90.2** | **90.1** | **90.2** | **90.3** | **90.3** | **90.4** | **90.6** |
| **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | | |
| **Jumla ya Pato la Taifa - sehemu isiyouzika** | **9.8** | **9.9** | **9.8** | **9.7** | **9.7** | **9.6** | **9.4** |
| **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **8.9** | **9.1** | **9.0** | **8.9** | **9.0** | **8.8** | **8.6** |
| Mazao | 4.9 | 4.9 | 4.7 | 4.6 | 4.8 | 4.7 | 4.6 |
| Mifugo | 2.8 | 3.0 | 3.1 | 3.0 | 3.0 | 2.9 | 2.8 |
| Misitu | 1.0 | 1.0 | 1.0 | 1.0 | 1.0 | 1.0 | 0.9 |
| Uvuvi | 0.2 | 0.2 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **0.7** | **0.7** | **0.7** | **0.7** | **0.6** | **0.7** | 0.7 |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 |
| Ujenzi | 0.6 | 0.6 | 0.6 | 0.6 | 0.5 | 0.6 | 0.6 |
| **Huduma** | **0.1** | **0.1** | **0.1** | **0.1** | **0.1** | **0.1** | 0.1 |
| Upangishaji Majengo | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 |
| **Pato la Taifa (A+B) kwa bei za soko za miaka husika** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 5: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MIAKA HUSIKA KWA AINA YA MATUMIZI, 2019 - 2025**

**Shilingi Milioni**

| Aina ya Matumizi/ Mwaka | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Pato la Taifa kwa Bei za Soko za miaka husika** | **139,135,212** | **149,836,983** | **161,991,897** | **179,409,952** | **193,359,937** | **211,974,663** | **234,104,003** |
| **Matumizi ya Mwisho** | **90,712,163** | **99,814,363** | **106,379,060** | **117,121,984** | **123,850,014** | **130,959,689** | **143,634,501** |
| Serikali | 13,229,874 | 14,375,812 | 16,016,838 | 17,176,892 | 19,307,876 | 20,698,739 | 22,507,102 |
| Binafsi | 77,255,732 | 85,210,757 | 90,119,200 | 99,673,983 | 104,242,441 | 109,934,705 | 120,773,317 |
| Taasisi binafsi zinazotoa huduma za kijamii | 226,558 | 227,795 | 243,022 | 271,109 | 299,697 | 326,246 | 354,083 |
| **Ukuzaji rasilimali** | **49,647,162** | **51,198,890** | **60,519,526** | **72,959,675** | **73,960,311** | **82,547,339** | **85,516,810** |
| Rasilimali za kudumu | 49,173,777 | 50,705,986 | 55,502,878 | 65,483,965 | 68,498,024 | 71,772,679 | 75,460,577 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani | 228,991 | 329,584 | 351,571 | 351,216 | 360,207 | 467,139 | 696,253 |
| Ongezeko la limbikizo | 244,394 | 163,319 | 4,665,077 | 7,124,494 | 5,102,080 | 10,307,521 | 9,359,980 |
| **Mauzo nje** | **22,032,684** | **19,281,759** | **22,253,899** | **26,922,316** | **32,748,026** | **41,366,816** | **42,668,470** |
| Bidhaa | 12,527,577 | 14,426,384 | 15,310,360 | 16,289,242 | 18,303,327 | 24,170,178 | 26,425,831 |
| Huduma | 9,505,107 | 4,855,374 | 6,943,539 | 10,633,074 | 14,444,698 | 17,196,638 | 16,242,639 |
| **Uagizaji** | **23,256,797** | **20,706,904** | **26,044,289** | **37,974,224** | **37,553,124** | **42,822,923** | **43,820,758** |
| Bidhaa | 19,357,732 | 17,880,107 | 22,594,405 | 32,667,734 | 32,421,872 | 36,879,734 | 36,148,887 |
| Huduma | 3,899,065 | 2,826,797 | 3,449,884 | 5,306,490 | 5,131,252 | 5,943,189 | 7,671,871 |
| Makosa na Mapungufu | 0 | 248,875 | -1,116,298 | 380,201 | 354,711 | -76,258 | 6,104,980 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 6: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2019 KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, 2019 - 2025**

**Shilingi Milioni**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ***Kilimo, Misitu na Uvuvi*** | ***34,531,749*** | ***36,340,713*** | ***37,680,402*** | ***39,287,406*** | ***40,979,899*** | ***43,053,540*** | ***45,409,415*** |
| Kilimo cha Mazao | 18,476,138 | 19,446,203 | 20,222,964 | 20,928,339 | 21,836,776 | 22,830,176 | 23,968,866 |
| Mifugo | 9,445,788 | 9,924,822 | 10,399,541 | 10,939,964 | 11,479,950 | 12,070,569 | 12,713,252 |
| Misitu | 3,980,090 | 4,185,238 | 4,409,638 | 4,625,931 | 4,898,479 | 5,224,073 | 5,612,976 |
| Uvuvi | 2,587,867 | 2,739,878 | 2,602,263 | 2,745,794 | 2,714,035 | 2,875,753 | 3,057,937 |
| Huduma katika Shughuli za Kilimo | 41,866 | 44,571 | 45,996 | 47,378 | 50,658 | 52,970 | 56,383 |
| ***Viwanda na Ujenzi*** | ***37,621,647*** | ***39,675,040*** | ***42,103,557*** | ***43,234,185*** | ***44,536,523*** | ***46,623,739*** | ***49,221,787*** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 7,382,971 | 8,303,988 | 8,972,374 | 9,001,092 | 9,223,233 | 9,973,551 | 10,910,248 |
| Viwanda | 10,123,642 | 10,519,002 | 11,005,801 | 11,478,078 | 12,012,150 | 12,599,729 | 13,256,459 |
| Umeme | 541,731 | 529,545 | 581,900 | 650,083 | 716,424 | 772,551 | 863,762 |
| Maji safi na Maji taka | 680,656 | 720,252 | 766,803 | 808,787 | 829,470 | 869,435 | 895,267 |
| Ujenzi | 18,892,648 | 19,602,253 | 20,776,680 | 21,296,144 | 21,755,245 | 22,408,473 | 23,296,052 |
| ***Huduma*** | ***56,214,390*** | ***57,466,923*** | ***59,866,728*** | ***63,453,981*** | ***67,907,435*** | ***72,432,472*** | ***77,449,446*** |
| Biashara na Matengenezo | 12,261,827 | 12,499,128 | 12,875,078 | 13,405,537 | 14,034,177 | 14,719,248 | 15,466,116 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 10,569,576 | 11,145,449 | 11,720,296 | 12,481,717 | 13,361,363 | 14,326,187 | 15,465,819 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 3,608,481 | 3,075,277 | 3,218,187 | 3,589,877 | 3,851,083 | 4,008,624 | 4,152,926 |
| Habari na Mawasiliano | 2,166,463 | 2,363,032 | 2,583,448 | 2,723,413 | 3,013,605 | 3,352,552 | 3,646,045 |
| Fedha na Bima | 5,075,182 | 5,162,356 | 5,376,970 | 5,884,415 | 6,804,183 | 7,665,511 | 8,866,777 |
| Upangishaji Majengo | 3,962,175 | 4,011,739 | 4,134,299 | 4,310,884 | 4,477,109 | 4,654,222 | 4,851,593 |
| Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 576,175 | 547,570 | 586,386 | 611,787 | 638,468 | 665,399 | 702,873 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 3,233,509 | 3,073,790 | 3,122,616 | 3,326,910 | 3,555,437 | 3,631,014 | 3,787,921 |
| Utawala na Ulinzi | 6,186,903 | 6,828,945 | 7,006,483 | 7,166,967 | 7,302,052 | 7,815,545 | 8,268,194 |
| Elimu | 3,599,275 | 3,716,432 | 3,825,006 | 4,156,416 | 4,610,398 | 4,954,314 | 5,213,280 |
| Afya na Huduma za Jamii | 2,409,985 | 2,414,177 | 2,607,492 | 2,814,803 | 3,014,001 | 3,233,665 | 3,428,584 |
| Sanaa na Burudani | 498,036 | 472,569 | 513,755 | 539,561 | 606,230 | 635,095 | 688,980 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 1,751,021 | 1,830,782 | 1,960,804 | 2,093,406 | 2,275,966 | 2,397,260 | 2,525,955 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 315,780 | 325,678 | 335,910 | 348,287 | 363,363 | 373,836 | 384,382 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **128,367,786** | **133,482,676** | **139,650,687** | **145,975,572** | **153,423,856** | **162,109,751** | **172,080,648** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 10,767,426 | 10,693,465 | 11,552,937 | 12,108,868 | 12,942,497 | 13,617,406 | 14,022,137 |
| **Pato la Taifa kwa bei za soko za mwaka 2019** | **139,135,212** | **144,176,142** | **151,203,623** | **158,084,440** | **166,366,353** | **175,727,157** | **186,102,786** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 7: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2019 KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI -SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA, 2019 - 2025**

**Shilingi Milioni**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A: SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | | |
| **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **22,107,758** | **23,270,648** | **24,067,929** | **25,097,628** | **26,141,464** | **27,524,644** | **29,045,247** |
| Kilimo cha Mazao | 11,699,893 | 12,314,181 | 12,806,060 | 13,252,734 | 13,827,987 | 14,511,656 | 15,183,318 |
| Mifugo | 5,549,821 | 5,831,275 | 6,110,193 | 6,427,716 | 6,744,982 | 7,091,996 | 7,476,372 |
| Misitu | 2,566,590 | 2,698,893 | 2,843,578 | 2,982,931 | 3,158,565 | 3,368,310 | 3,674,554 |
| Uvuvi | 2,249,587 | 2,381,728 | 2,262,102 | 2,386,869 | 2,359,272 | 2,499,712 | 2,654,619 |
| Huduma katika Shughuli za Kilimo | 41,866 | 44,571 | 45,996 | 47,378 | 50,658 | 52,970 | 56,383 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **36,585,710** | **38,570,683** | **40,929,771** | **42,047,051** | **43,263,734** | **45,260,921** | **47,772,381** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 7,382,971 | 8,303,988 | 8,972,374 | 9,001,092 | 9,223,233 | 9,973,551 | 10,910,248 |
| Viwanda | 10,123,642 | 10,519,002 | 11,005,801 | 11,478,078 | 12,012,150 | 12,599,729 | 13,256,459 |
| Umeme | 541,731 | 529,545 | 581,900 | 650,083 | 716,424 | 772,551 | 863,762 |
| Majisafi na Majitaka | 528,283 | 561,219 | 598,478 | 631,245 | 647,389 | 678,580 | 691,399 |
| Ujenzi | 18,009,083 | 18,656,929 | 19,771,219 | 20,286,552 | 20,664,539 | 21,236,510 | 22,050,513 |
| **Huduma** | **56,056,822** | **57,307,385** | **59,702,315** | **63,282,545** | **67,729,389** | **72,247,383** | **77,259,608** |
| Biashara na Matengenezo | 12,261,827 | 12,499,128 | 12,875,078 | 13,405,537 | 14,034,177 | 14,719,248 | 15,466,116 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 10,569,576 | 11,145,449 | 11,720,296 | 12,481,717 | 13,361,363 | 14,326,187 | 15,465,819 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 3,608,481 | 3,075,277 | 3,218,187 | 3,589,877 | 3,851,083 | 4,008,624 | 4,152,926 |
| Habari na Mawasiliano | 2,166,463 | 2,363,032 | 2,583,448 | 2,723,413 | 3,013,605 | 3,352,552 | 3,646,045 |
| Fedha na Bima | 5,075,182 | 5,162,356 | 5,376,970 | 5,884,415 | 6,804,183 | 7,665,511 | 8,866,777 |
| Upangishaji Majengo | 3,804,607 | 3,852,200 | 3,969,886 | 4,139,448 | 4,299,063 | 4,469,133 | 4,661,755 |
| Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 576,175 | 547,570 | 586,386 | 611,787 | 638,468 | 665,399 | 702,873 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 3,233,509 | 3,073,790 | 3,122,616 | 3,326,910 | 3,555,437 | 3,631,014 | 3,787,921 |
| Utawala na Ulinzi | 6,186,903 | 6,828,945 | 7,006,483 | 7,166,967 | 7,302,052 | 7,815,545 | 8,268,194 |
| Elimu | 3,599,275 | 3,716,432 | 3,825,006 | 4,156,416 | 4,610,398 | 4,954,314 | 5,213,280 |
| Afya na Huduma za Jamii | 2,409,985 | 2,414,177 | 2,607,492 | 2,814,803 | 3,014,001 | 3,233,665 | 3,428,584 |
| Sanaa na Burudani | 498,036 | 472,569 | 513,755 | 539,561 | 606,230 | 635,095 | 688,980 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 1,751,021 | 1,830,782 | 1,960,804 | 2,093,406 | 2,275,966 | 2,397,260 | 2,525,955 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 315,780 | 325,678 | 335,910 | 348,287 | 363,363 | 373,836 | 384,382 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **114,750,289** | **119,148,715** | **124,700,015** | **130,427,225** | **137,134,587** | **145,032,948** | **154,077,236** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 10,767,426 | 10,693,465 | 11,552,937 | 12,108,868 | 12,942,497 | 13,617,406 | 14,022,137 |
| **Jumla ya Pato la Taifa - Sehemu inayouzika** | **125,517,716** | **129,842,181** | **136,252,951** | **142,536,093** | **150,077,084** | **158,650,355** | **168,099,373** |
| **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | | |
| **Jumla ya Pato la Taifa - sehemu isiyouzika** | **13,617,496** | **14,333,961** | **14,950,672** | **15,548,347** | **16,289,269** | **17,076,803** | **18,003,413** |
| Kilimo, Misitu na Uvuvi | 12,423,991 | 13,070,065 | 13,612,473 | 14,189,778 | 14,838,435 | 15,528,896 | 16,364,168 |
| Mazao | 6,776,244 | 7,132,022 | 7,416,904 | 7,675,605 | 8,008,790 | 8,318,519 | 8,785,548 |
| Mifugo | 3,895,967 | 4,093,548 | 4,289,348 | 4,512,248 | 4,734,969 | 4,978,572 | 5,236,880 |
| Misitu | 1,413,499 | 1,486,345 | 1,566,060 | 1,643,000 | 1,739,914 | 1,855,763 | 1,938,422 |
| Uvuvi | 338,280 | 358,150 | 340,160 | 358,924 | 354,763 | 376,041 | 403,318 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **1,035,938** | **1,104,357** | **1,173,787** | **1,187,134** | **1,272,788** | **1,362,818** | **1,449,406** |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 152,373 | 159,033 | 168,325 | 177,541 | 182,082 | 190,855 | 203,867 |
| Ujenzi | 883,564 | 945,324 | 1,005,461 | 1,009,593 | 1,090,707 | 1,171,963 | 1,245,539 |
| **Huduma** | **157,568** | **159,539** | **164,413** | **171,435** | **178,046** | **185,089** | **189,839** |
| Upangishaji Majengo | 157,568 | 159,539 | 164,413 | 171,435 | 178,046 | 185,089 | 189,839 |
| **Pato la Taifa (A+B) kwa bei za soko za mwaka 2019** | **139,135,212** | **144,176,142** | **151,203,623** | **158,084,440** | **166,366,353** | **175,727,157** | **186,102,786** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 8: UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2019 KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, 2019 - 2025**

**Asilimia**

| **SHUGHULI YA KIUCHUMI** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **5.9** | **5.2** | **3.7** | **4.3** | **4.3** | **5.1** | **5.5** |
| Kilimo cha Mazao | 4.6 | 5.3 | 4.0 | 3.5 | 4.3 | 4.5 | 5.0 |
| Mifugo | 5.6 | 5.1 | 4.8 | 5.2 | 4.9 | 5.1 | 5.3 |
| Misitu | 6.9 | 5.2 | 5.4 | 4.9 | 5.9 | 6.6 | 7.4 |
| Uvuvi | 16.0 | 5.9 | -5.0 | 5.5 | -1.2 | 6.0 | 6.3 |
| Huduma katika Shughuli za Kilimo | 4.1 | 6.5 | 3.2 | 3.0 | 6.9 | 4.6 | 6.4 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **11.8** | **5.5** | **6.1** | **2.7** | **3.0** | **4.7** | **5.6** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 19.0 | 12.5 | 8.0 | 0.3 | 2.5 | 8.1 | 9.4 |
| Viwanda | 5.7 | 3.9 | 4.6 | 4.3 | 4.7 | 4.9 | 5.2 |
| Umeme | 9.8 | -2.2 | 9.9 | 11.7 | 10.2 | 7.8 | 11.8 |
| Maji safi na Maji taka | 6.9 | 5.8 | 6.5 | 5.5 | 2.6 | 4.8 | 3.0 |
| Ujenzi | 13.0 | 3.8 | 6.0 | 2.5 | 2.2 | 3.0 | 4.0 |
| **Huduma** | **4.0** | **2.2** | **4.2** | **6.0** | **7.0** | **6.7** | **6.9** |
| Biashara na Matengenezo | 5.4 | 1.9 | 3.0 | 4.1 | 4.7 | 4.9 | 5.1 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 4.9 | 5.4 | 5.2 | 6.5 | 7.0 | 7.2 | 8.0 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 4.7 | -14.8 | 4.6 | 11.5 | 7.3 | 4.1 | 3.6 |
| Habari na Mawasiliano | 4.2 | 9.1 | 9.3 | 5.4 | 10.7 | 11.2 | 8.8 |
| Fedha na Bima | 5.7 | 1.7 | 4.2 | 9.4 | 15.6 | 12.7 | 15.7 |
| Upangishaji Majengo | 2.0 | 1.3 | 3.1 | 4.3 | 3.9 | 4.0 | 4.2 |
| Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 7.1 | -5.0 | 7.1 | 4.3 | 4.4 | 4.2 | 5.6 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 0.6 | -4.9 | 1.6 | 6.5 | 6.9 | 2.1 | 4.3 |
| Utawala na Ulinzi | -2.1 | 10.4 | 2.6 | 2.3 | 1.9 | 7.0 | 5.8 |
| Elimu | 4.7 | 3.3 | 2.9 | 8.7 | 10.9 | 7.5 | 5.2 |
| Afya na Huduma za Jamii | 8.8 | 0.2 | 8.0 | 8.0 | 7.1 | 7.3 | 6.0 |
| Sanaa na Burudani | 3.0 | -5.1 | 8.7 | 5.0 | 12.4 | 4.8 | 8.5 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 7.3 | 4.6 | 7.1 | 6.8 | 8.7 | 5.3 | 5.4 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.7 | 4.3 | 2.9 | 2.8 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **6.7** | **4.0** | **4.6** | **4.5** | **5.1** | **5.7** | **6.2** |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 3.1 | -0.7 | 8.0 | 4.8 | 6.9 | 5.2 | 3.0 |
| **Pato la Taifa kwa bei za soko za mwaka 2019** | **6.4** | **3.6** | **4.9** | **4.6** | **5.2** | **5.6** | **5.9** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 9: UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2019 KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI -SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA, 2019 - 2025**

**Asilimia**

| SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A: SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | | |
| **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **6.2** | **5.3** | **3.4** | **4.3** | **4.2** | **5.3** | **5.5** |
| Kilimo cha Mazao | 4.6 | 5.3 | 4.0 | 3.5 | 4.3 | 4.9 | 4.6 |
| Mifugo | 5.6 | 5.1 | 4.8 | 5.2 | 4.9 | 5.1 | 5.4 |
| Misitu | 6.9 | 5.2 | 5.4 | 4.9 | 5.9 | 6.6 | 9.1 |
| Uvuvi | 16.0 | 5.9 | - 5.0 | 5.5 | - 1.2 | 6.0 | 6.2 |
| Huduma katika Shughuli za Kilimo | 4.1 | 6.5 | 3.2 | 3.0 | 6.9 | 4.6 | 6.4 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **12.4** | **5.0** | **6.2** | **2.7** | **3.2** | **4.5** | **5.7** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 19.0 | 12.5 | 8.0 | 0.3 | 2.5 | 8.1 | 9.4 |
| Viwanda | 5.7 | 3.9 | 4.6 | 4.3 | 4.7 | 4.9 | 5.2 |
| Umeme | 9.8 | - 2.2 | 9.9 | 11.7 | 10.2 | 7.8 | 11.8 |
| Maji safi na Maji taka | 7.2 | 6.2 | 6.6 | 5.5 | 2.6 | 4.8 | 1.9 |
| Ujenzi | 14.1 | 3.6 | 6.0 | 2.6 | 1.9 | 2.8 | 3.8 |
| **Huduma** | **4.0** | **2.2** | **4.2** | **6.0** | **7.0** | **6.7** | **6.9** |
| Biashara na Matengenezo | 5.4 | 1.9 | 3.0 | 4.1 | 4.7 | 4.9 | 5.1 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 4.9 | 5.4 | 5.2 | 6.5 | 7.0 | 7.2 | 8.0 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 4.7 | - 14.8 | 4.6 | 11.5 | 7.3 | 4.1 | 3.6 |
| Habari na Mawasiliano | 4.2 | 9.1 | 9.3 | 5.4 | 10.7 | 11.2 | 8.8 |
| Fedha na Bima | 5.7 | 1.7 | 4.2 | 9.4 | 15.6 | 12.7 | 15.7 |
| Upangishaji Majengo | 2.0 | 1.3 | 3.1 | 4.3 | 3.9 | 4.0 | 4.3 |
| Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 7.1 | - 5.0 | 7.1 | 4.3 | 4.4 | 4.2 | 5.6 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 0.6 | - 4.9 | 1.6 | 6.5 | 6.9 | 2.1 | 4.3 |
| Utawala na Ulinzi | - 2.1 | 10.4 | 2.6 | 2.3 | 1.9 | 7.0 | 5.8 |
| Elimu | 4.7 | 3.3 | 2.9 | 8.7 | 10.9 | 7.5 | 5.2 |
| Afya na Huduma za Jamii | 8.8 | 0.2 | 8.0 | 8.0 | 7.1 | 7.3 | 6.0 |
| Sanaa na Burudani | 3.0 | - 5.1 | 8.7 | 5.0 | 12.4 | 4.8 | 8.5 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 7.3 | 4.6 | 7.1 | 6.8 | 8.7 | 5.3 | 5.4 |
| Shughuli za Kaya katika kuajiri | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.7 | 4.3 | 2.9 | 2.8 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | 7.0 | 3.7 | 4.7 | 4.6 | 5.2 | 5.7 | 6.3 |
| Ongeza kodi katika bidhaa | 3.1 | - 0.7 | 8.0 | 4.8 | 6.9 | 5.2 | 3.0 |
| **Jumla ya Pato la Taifa - Sehemu inayouzika** | **6.6** | **3.3** | **5.0** | **4.6** | **5.4** | **5.7** | **6.0** |
| **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | | |
| **Jumla ya Pato la Taifa - sehemu isiyouzika** | **4.6** | **6.3** | **4.1** | **4.0** | **4.0** | **5.1** | **5.1** |
| Kilimo, Misitu na Uvuvi | 5.4 | 5.2 | 4.1 | 4.2 | 4.6 | 4.7 | 5.4 |
| Mazao | 4.6 | 5.3 | 4.0 | 3.5 | 4.3 | 3.9 | 5.6 |
| Mifugo | 5.6 | 5.1 | 4.8 | 5.2 | 4.9 | 5.1 | 5.2 |
| Misitu | 6.9 | 5.2 | 5.4 | 4.9 | 5.9 | 6.7 | 4.5 |
| Uvuvi | 16.0 | 5.9 | - 5.0 | 5.5 | - 1.2 | 6.0 | 7.3 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **- 4.8** | **6.6** | **6.3** | **1.1** | **7.2** | **7.1** | **6.4** |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 5.8 | 4.4 | 5.8 | 5.5 | 2.6 | 4.8 | 6.8 |
| Ujenzi | - 6.4 | 7.0 | 6.4 | 0.4 | 8.0 | 7.4 | 6.3 |
| **Huduma** | **2.0** | **1.3** | **3.1** | **4.3** | **3.9** | **4.0** | **2.6** |
| Upangishaji Majengo | 2.0 | 1.3 | 3.1 | 4.3 | 3.9 | 4.0 | 2.6 |
| **Pato la Taifa (A+B) kwa bei za soko za mwaka 2019** | **6.4** | **3.6** | **4.9** | **4.6** | **5.2** | **5.6** | **5.9** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 10: PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO ZA MWAKA 2019 KWA AINA YA MATUMIZI, 2019 - 2025**

**Shilingi Milioni**

| Aina ya Matumizi | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Pato la Taifa kwa Bei za Soko za Mwaka 2019** | **139,135,212** | **144,176,142** | **151,203,623** | **158,084,440** | **166,366,353** | **175,727,157** | **186,102,786** |
| **Matumizi ya Mwisho (Final consumption)** | **90,712,163** | **96,750,701** | **99,579,705** | **103,579,798** | **106,421,263** | **109,249,889** | **117,166,145** |
| Serikali | 13,229,874 | 14,032,705 | 14,710,079 | 15,566,711 | 17,315,324 | 18,517,479 | 19,886,287 |
| Binafsi | 77,255,732 | 82,491,298 | 84,629,147 | 87,746,971 | 88,814,133 | 90,416,087 | 96,930,430 |
| Taasisi binafsi Zinazotoa huduma za kijamii | 226,558 | 226,698 | 240,480 | 266,116 | 291,805 | 316,323 | 349,429 |
| **Ukuzaji rasilimali** | **49,647,162** | **51,112,308** | **59,113,200** | **64,244,724** | **63,089,268** | **69,840,089** | **71,354,714** |
| Rasilimali za kudumu | 49,173,777 | 50,686,822 | 54,256,837 | 56,675,649 | 58,087,991 | 60,376,075 | 62,797,966 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 228,991 | 270,935 | 288,939 | 268,521 | 259,987 | 286,091 | 315,302 |
| Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | 244,394 | 154,551 | 4,567,423 | 7,300,555 | 4,741,289 | 9,177,922 | 8,241,446 |
| **Mauzo nje*** | **22,032,684** | **17,830,346** | **20,867,940** | **25,909,359** | **26,917,236** | **34,886,226** | **32,509,226** |
| Bidhaa-fob | 12,527,577 | 12,894,069 | 13,646,701 | 13,440,511 | 14,478,496 | 17,723,031 | 16,328,550 |
| Huduma | 9,505,107 | 4,936,277 | 7,221,239 | 12,468,847 | 12,438,740 | 17,163,195 | 16,180,676 |
| **Uagizaji toka nje*** | **23,256,797** | **23,096,991** | **27,553,380** | **33,142,088** | **32,422,696** | **37,642,157** | **37,305,692** |
| Bidhaa-fob | 19,357,732 | 20,394,808 | 24,264,772 | 28,287,485 | 27,777,168 | 32,208,682 | 30,578,868 |
| Huduma | 3,899,065 | 2,702,182 | 3,288,608 | 4,854,603 | 4,645,528 | 5,433,475 | 6,726,825 |
| Makosa na Mapungufu | 0 | 1,579,777 | -803,842 | -2,507,352 | 2,361,283 | -606,889 | 2,378,394 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 11: UKUZAJI RASILIMALI KWA KWA BEI ZA MIAKA HUSIKA KWA AINA YA RASILIMALI, 2019 - 2025**

**Shilingi Milioni**

| **Aina ya Rasilimali/ Mwaka** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 43,396,945 | 45,044,981 | 48,882,121 | 57,297,698 | 59,515,118 | 61,341,767 | 64,425,392 |
| Vifaa vya Usafiri | 1,602,767 | 1,160,044 | 1,614,662 | 2,257,399 | 2,553,496 | 3,397,840 | 3,488,733 |
| Mitambo na Vifaa | 1,761,955 | 1,607,099 | 1,870,536 | 2,369,156 | 2,480,041 | 2,788,876 | 2,959,040 |
| Mitambo na Vifaa vingine | 486,032 | 524,239 | 544,987 | 695,993 | 753,692 | 870,286 | 934,014 |
| Rasilimali za Mazao ya Mifugo | 684,094 | 778,692 | 843,622 | 978,342 | 1,072,330 | 1,122,549 | 1,188,968 |
| Haki ya Umiliki,Utafiti na Maendeleo na Huduma za Kitaalamu | 1,241,985 | 1,590,931 | 1,746,950 | 1,885,377 | 2,123,347 | 2,251,361 | 2,464,430 |
| Rasilimali za kudumu | **49,173,777** | **50,705,986** | **55,502,878** | **65,483,965** | **68,498,024** | **71,772,679** | **75,460,577** |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 228,991 | 329,584 | 351,571 | 351,216 | 360,207 | 467,139 | 696,253 |
| Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | 244,394 | 163,319 | 4,665,077 | 7,124,494 | 5,102,080 | 10,307,521 | 9,359,980 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **49,647,162** | **51,198,890** | **60,519,526** | **72,959,675** | **73,960,311** | **82,547,339** | **85,516,810** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 12: UKUZAJI RASILIMALI KWA BEI ZA MWAKA 2019 KWA AINA YA RASILIMALI, 2019 - 2025**

**Shilingi Milioni**

| **Aina ya Rasilimali/ Mwaka** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 43,396,945 | 41,880,557 | 44,830,322 | 46,875,301 | 46,901,780 | 47,296,176 | 49,197,305 |
| Vifaa vya Usafiri | 1,602,767 | 1,929,769 | 1,975,941 | 2,119,080 | 2,802,076 | 4,659,950 | 4,747,255 |
| Mitambo na Vifaa | 1,761,955 | 3,403,755 | 3,733,238 | 3,803,242 | 4,714,601 | 4,650,023 | 4,936,945 |
| Mitambo na Vifaa vingine | 486,032 | 1,655,555 | 1,774,853 | 1,884,035 | 1,630,210 | 1,679,322 | 1,736,824 |
| Rasilimali za Mazao ya Mifugo | 684,094 | 471,158 | 505,240 | 524,942 | 499,788 | 503,968 | 534,227 |
| Haki ya Umiliki,Utafiti na Maendeleo na Huduma za Kitaalamu | 1,241,985 | 1,346,029 | 1,437,243 | 1,469,049 | 1,539,535 | 1,586,635 | 1,645,411 |
| **Rasilimali za kudumu** | **49,173,777** | **50,686,822** | **54,256,837** | **56,675,649** | **58,087,991** | **60,376,075** | **62,797,966** |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 228,991 | 270,935 | 288,939 | 268,521 | 259,987 | 286,091 | 315,302 |
| Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | 244,394 | 154,551 | 4,567,423 | 7,300,555 | 4,741,289 | 9,177,922 | 8,241,446 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **49,647,162** | **51,112,308** | **59,113,200** | **64,244,724** | **63,089,268** | **69,840,089** | **71,354,714** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 13: MCHANGO KATIKA UKUZAJI RASILIMALI KWA BEI ZA MIAKA HUSIKA KWA AINA YA RASILIMALI, 2019 - 2025**

**Asilimia**

| Aina ya Rasilimali | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 87.4 | 88.0 | 80.8 | 78.5 | 80.5 | 74.3 | 75.3 |
| Vifaa vya Usafiri | 3.2 | 2.3 | 2.7 | 3.1 | 3.5 | 4.1 | 4.1 |
| Mitambo na Vifaa | 3.5 | 3.1 | 3.1 | 3.2 | 3.4 | 3.4 | 3.5 |
| Mitambo na Vifaa vingine | 1.0 | 1.0 | 0.9 | 1.0 | 1.0 | 1.1 | 1.1 |
| Rasilimali za Mazao ya Mifugo | 1.4 | 1.5 | 1.4 | 1.3 | 1.4 | 1.4 | 1.4 |
| Haki ya Umiliki,Utafiti na Maendeleo na Huduma za Kitaalamu | 2.5 | 3.1 | 2.9 | 2.6 | 2.9 | 2.7 | 2.9 |
| Rasilimali za kudumu | **99.0** | **99.0** | **91.7** | **89.8** | **92.6** | **86.9** | **88.2** |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 0.5 | 0.6 | 0.6 | 0.5 | 0.5 | 0.6 | 0.8 |
| Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | 0.5 | 0.3 | 7.7 | 9.8 | 6.9 | 12.5 | 10.9 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 14: UKUZAJI RASILIMALI KWA BEI ZA MIAKA HUSIKA KWA AINA YA SEKTA, 2016 - 2025**

**Shilingi Milioni**

| Sekta | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A. Rasilimali za kudumu | 49,173,777 | 50,705,986 | 55,502,878 | 65,483,965 | 68,498,024 | 71,772,679 | 75,460,577 |
| Serikali: | 12,391,783 | 13,132,850 | 13,986,716 | 16,060,425 | 16,439,526 | 17,600,311 | 18,804,988 |
| Mashirika ya Umma: | 1,032,648 | 1,216,944 | 1,358,470 | 1,674,126 | 1,780,949 | 1,887,044 | 1,963,597 |
| Taasisi: | 1,180,170 | 1,318,356 | 1,444,599 | 1,677,345 | 1,849,447 | 2,041,273 | 2,144,791 |
| Sekta binafsi | 34,569,176 | 35,037,837 | 38,713,092 | 46,072,069 | 48,428,103 | 50,244,050 | 52,547,201 |
| B: Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 228,991 | 329,584 | 351,571 | 351,216 | 360,207 | 467,139 | 696,253 |
| C. Ongezeko la Limbikizo | 244,394 | 163,319 | 4,665,077 | 7,124,494 | 5,102,080 | 10,307,521 | 9,359,980 |
| **Jumla la Ukuzaji Rasilimali (A+B+C)** | **49,647,162** | **51,198,890** | **60,519,526** | **72,959,675** | **73,960,311** | **82,547,339** | **85,516,810** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 15: FAHIRISI ZA BEI ZA REJAREJA ZA BIDHAA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR-ES-SALAAM (Jan - Des. 2020 =100)**

| MWAKA | BIDHAA ZOTE | | ***VYAKULA NA VINYWAJI BARIDI | |
|---|---|---|---|---|
| | FAHIRISI | BADILIKO (ASILIMIA) | FAHIRISI | BADILIKO (ASILIMIA) |
| 2016 | 90.9 | | 87.52 | |
| 2017 | 92.6 | 1.9 | 90.53 | 3.4 |
| 2018 | 94.4 | 2.0 | 94.59 | 4.5 |
| 2019 | 98.0 | 3.8 | 98.93 | 4.6 |
| **2020 | 100.00 | 2.1 | 100.00 | 1.1 |
| 2021 | 102.37 | 2.4 | 100.58 | 0.6 |
| 2022 | 107.16 | 4.7 | 108.16 | 7.5 |
| 2023 | 112.77 | 5.2 | 118.78 | 9.8 |
| 2024 | 119.30 | 5.8 | 123.98 | 4.4 |
| 2025 | 124.76 | 4.6 | 135.18 | 9.0 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

***Jina limebadilika kutoka Kundi la chakula Desemba 2020 na kusomeka vyakula na vinywaji baridi

**Jedwali Na. 16: FAHIRISI ZA BEI ZA REJA REJA ZA BIDHAA ZITUMIKAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR ES SALAAM (Jan - Des. 2020 = 100)**

| Mwaka | Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2016 | 87.52 | 96.37 | 90.95 | 81.16 | 92.80 | 94.57 | 109.22 | 98.54 | 95.16 | 91.47 | 96.60 | 91.76 | 95.45 | 90.94 |
| 2017 | 90.53 | 99.20 | 92.14 | 81.89 | 95.71 | 96.03 | 109.11 | 98.91 | 96.76 | 95.02 | 97.12 | 94.10 | 96.08 | 92.63 |
| 2018 | 94.59 | 99.20 | 95.03 | 86.58 | 97.53 | 96.10 | 95.51 | 98.82 | 97.84 | 100.22 | 97.23 | 96.17 | 97.49 | 94.44 |
| 2019 | 98.93 | 99.98 | 98.79 | 91.42 | 99.42 | 99.13 | 100.23 | 99.79 | 100.13 | 100.12 | 99.36 | 100.00 | 99.66 | 97.99 |
| 2020 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 |
| 2021 | 100.58 | 107.27 | 103.06 | 102.93 | 103.91 | 101.93 | 92.55 | 101.39 | 103.83 | 110.34 | 105.46 | 100.00 | 100.71 | 102.37 |
| 2022 | 108.16 | 107.86 | 106.86 | 106.97 | 110.42 | 104.89 | 90.61 | 103.25 | 117.66 | 112.84 | 108.58 | 100.00 | 104.23 | 107.16 |
| 2023 | 118.78 | 108.60 | 109.45 | 110.63 | 116.24 | 114.46 | 82.97 | 104.32 | 133.86 | 117.78 | 110.68 | 99.97 | 107.88 | 112.77 |
| 2024 | 123.98 | 112.13 | 113.60 | 123.32 | 120.74 | 124.33 | 100.38 | 104.97 | 155.60 | 122.42 | 113.21 | 100.04 | 117.99 | 119.30 |
| 2025 | 135.18 | 113.30 | 119.60 | 126.34 | 125.05 | 125.17 | 104.89 | 104.95 | 162.88 | 124.61 | 113.67 | 100.04 | 120.81 | 124.76 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

**Jedwali Na. 17: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA KATI - DAR-ES-SALAAM (Jan - Des. 2020 =100)**

| Mwaka | Miezi/ Robo-Mwaka | | | | | Badiliko Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo ya Kwanza | Robo ya Pili | Robo ya Tatu | Robo ya Nne | Wastani | |
| 2016 | 87.19 | 89.15 | 88.69 | 88.67 | 88.43 | |
| 2017 | 89.26 | 91.18 | 91.12 | 91.43 | 90.75 | 2.6 |
| 2018 | 90.35 | 92.69 | 92.89 | 93.83 | 92.44 | 1.9 |
| 2019 | 95.62 | 96.95 | 96.51 | 97.36 | 96.61 | 4.5 |
| **2020 | 99.69 | 99.96 | 100.42 | 99.92 | 100.00 | 3.5 |
| 2021 | 101.71 | 102.57 | 101.87 | 103.45 | 102.40 | 2.4 |
| 2022 | 105.12 | 108.89 | 109.48 | 110.01 | 108.38 | 5.8 |
| 2023 | 112.37 | 113.39 | 113.78 | 115.33 | 113.72 | 4.9 |
| 2024 | 120.76 | 124.14 | 123.00 | 122.80 | 122.68 | 7.9 |
| 2025 | 126.15 | 129.01 | 128.22 | 129.58 | 128.24 | 4.5 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

**Jedwali Na. 18: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA KATI DAR ES SALAAM (Jan - Des. 2020 =100)**

| | ***Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2019 Robo ya kwanza | 93.66 | 99.85 | 98.02 | 90.52 | 99.33 | 98.34 | 100.45 | 99.40 | 99.92 | 100.03 | 99.34 | 100.00 | 99.95 | 95.62 |
| Robo ya pili | 96.72 | 99.85 | 98.57 | 90.39 | 99.55 | 99.59 | 101.06 | 99.87 | 100.12 | 100.03 | 99.47 | 100.00 | 100.03 | 96.95 |
| Robo ya tatu | 95.12 | 99.85 | 99.20 | 91.58 | 99.39 | 99.60 | 101.06 | 99.15 | 101.01 | 100.03 | 99.45 | 100.00 | 99.44 | 96.51 |
| Robo ya nne | 97.19 | 99.85 | 99.17 | 92.21 | 99.71 | 99.69 | 100.61 | 99.30 | 99.70 | 100.03 | 99.04 | 100.00 | 99.67 | 97.36 |
| **2020 Robo ya kwanza | 101.46 | 99.85 | 99.85 | 96.53 | 99.93 | 99.71 | 100.93 | 99.54 | 99.97 | 100.00 | 99.05 | 100.00 | 99.25 | 99.87 |
| Robo ya pili | 99.72 | 99.85 | 99.96 | 101.49 | 99.99 | 100.04 | 99.31 | 100.15 | 99.99 | 100.00 | 99.05 | 100.00 | 99.88 | 99.99 |
| Robo ya tatu | 99.38 | 99.85 | 99.95 | 102.39 | 100.04 | 100.12 | 99.53 | 100.15 | 100.02 | 100.00 | 100.95 | 100.00 | 100.30 | 100.26 |
| Robo ya nne | 99.44 | 100.44 | 100.24 | 99.59 | 100.03 | 100.12 | 100.23 | 100.15 | 100.02 | 100.00 | 100.95 | 100.00 | 100.57 | 99.89 |
| 2021 Robo ya kwanza | 100.68 | 104.06 | 100.68 | 99.92 | 102.79 | 103.70 | 100.91 | 101.36 | 100.06 | 104.76 | 107.20 | 100.00 | 100.21 | 101.71 |
| Robo ya pili | 102.03 | 104.31 | 99.99 | 97.98 | 104.06 | 103.97 | 102.50 | 101.24 | 100.64 | 105.60 | 110.88 | 100.57 | 100.75 | 102.57 |
| Robo ya tatu | 99.63 | 103.90 | 100.16 | 97.71 | 104.07 | 103.97 | 103.47 | 101.25 | 100.57 | 105.53 | 110.88 | 100.57 | 100.69 | 101.87 |
| Robo ya nne | 102.36 | 104.56 | 101.79 | 99.97 | 105.36 | 104.32 | 103.99 | 101.54 | 100.55 | 105.54 | 111.53 | 100.57 | 100.99 | 103.45 |
| 2022 Robo ya kwanza | 104.28 | 104.70 | 102.85 | 103.83 | 107.30 | 104.48 | 104.25 | 101.62 | 115.16 | 105.54 | 112.88 | 100.57 | 102.20 | 105.12 |
| Robo ya pili | 111.70 | 104.70 | 102.92 | 105.35 | 107.68 | 105.19 | 111.04 | 101.59 | 116.25 | 106.11 | 114.50 | 100.55 | 104.65 | 108.89 |
| Robo ya tatu | 112.07 | 104.98 | 103.70 | 102.76 | 108.73 | 106.41 | 116.39 | 101.55 | 118.18 | 107.27 | 114.05 | 100.50 | 104.76 | 109.48 |
| Robo ya nne | 115.03 | 104.70 | 103.78 | 103.51 | 111.09 | 107.18 | 109.37 | 101.56 | 118.64 | 107.38 | 115.53 | 100.46 | 104.89 | 110.01 |
| 2023 Robo ya kwanza | 121.13 | 104.70 | 104.57 | 103.76 | 111.53 | 107.83 | 109.30 | 101.54 | 120.57 | 109.58 | 116.90 | 100.49 | 105.45 | 112.37 |
| Robo ya pili | 123.48 | 104.70 | 104.99 | 105.94 | 111.20 | 107.82 | 108.40 | 101.42 | 123.91 | 109.58 | 117.24 | 100.45 | 105.68 | 113.39 |
| Robo ya tatu | 120.59 | 112.05 | 106.94 | 106.05 | 113.29 | 111.18 | 113.17 | 101.55 | 126.12 | 109.58 | 117.83 | 100.41 | 110.01 | 113.78 |
| Robo ya nne | 121.68 | 114.61 | 109.24 | 109.89 | 115.50 | 111.20 | 115.27 | 101.69 | 127.72 | 109.58 | 118.07 | 100.52 | 110.03 | 115.33 |
| 2024 Robo ya kwanza | 127.91 | 117.08 | 111.54 | 115.23 | 117.49 | 114.84 | 127.60 | 103.23 | 129.17 | 111.59 | 122.17 | 100.58 | 115.08 | 120.76 |
| Robo ya pili | 131.42 | 119.97 | 112.36 | 123.99 | 118.04 | 115.23 | 133.69 | 103.17 | 130.84 | 113.37 | 122.45 | 100.60 | 117.31 | 124.14 |
| Robo ya tatu | 127.13 | 120.31 | 112.72 | 124.73 | 118.97 | 115.30 | 133.48 | 103.18 | 132.08 | 114.66 | 122.75 | 100.60 | 117.82 | 123.00 |
| Robo ya nne | 127.69 | 120.64 | 113.16 | 122.70 | 120.41 | 115.18 | 131.27 | 103.32 | 132.48 | 114.63 | 122.66 | 100.60 | 119.16 | 122.80 |
| 2025 Robo ya kwanza | 135.63 | 121.28 | 117.09 | 121.14 | 122.63 | 115.70 | 132.77 | 103.41 | 133.52 | 125.05 | 122.73 | 100.60 | 120.19 | 126.15 |
| Robo ya pili | 141.36 | 121.28 | 117.42 | 123.95 | 124.31 | 116.71 | 135.16 | 103.83 | 133.93 | 125.16 | 124.04 | 100.60 | 120.48 | 129.01 |
| Robo ya tatu | 139.66 | 121.19 | 117.41 | 120.69 | 124.88 | 116.53 | 136.70 | 103.70 | 133.16 | 124.74 | 123.96 | 100.60 | 120.63 | 128.22 |
| Robo ya nne | 141.83 | 120.78 | 118.79 | 118.44 | 125.79 | 117.42 | 143.51 | 103.92 | 132.74 | 124.52 | 123.51 | 100.56 | 120.12 | 129.58 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

***Jina limebadilika kutoka Kundi la CHAKULA; Toka Des 2020 linasomeka VYAKULA NA VINYWAJI BARIDI

**Jedwali Na. 19:FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA JUU DAR ES SALAAM (Jan - Des. 2020 =100)**

| | ***Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2019 Robo ya kwanza | 90.9 | 99.8 | 97.9 | 89.1 | 99.3 | 98.4 | 101.5 | 99.4 | 99.8 | 100.0 | 99.6 | 100.0 | 100.8 | 96.4 |
| Robo ya pili | 93.6 | 99.8 | 98.5 | 94.5 | 99.6 | 99.8 | 102.3 | 99.9 | 100.4 | 100.0 | 99.7 | 100.0 | 100.8 | 98.1 |
| Robo ya tatu | 92.9 | 99.8 | 99.0 | 95.3 | 99.5 | 99.7 | 102.0 | 99.1 | 101.0 | 100.0 | 98.9 | 100.0 | 100.4 | 97.9 |
| Robo ya nne | 94.3 | 99.8 | 99.2 | 95.9 | 99.7 | 99.7 | 101.6 | 99.3 | 99.2 | 100.0 | 99.3 | 100.0 | 99.0 | 98.2 |
| **2020 Robo ya kwanza | 99.6 | 99.8 | 99.9 | 97.9 | 99.9 | 99.7 | 101.8 | 99.5 | 100.0 | 100.0 | 99.4 | 100.0 | 98.7 | 100.0 |
| Robo ya pili | 99.1 | 99.8 | 100.0 | 100.8 | 100.0 | 100.1 | 99.4 | 100.2 | 100.0 | 100.0 | 99.4 | 100.0 | 100.2 | 99.7 |
| Robo ya tatu | 100.0 | 99.8 | 100.0 | 101.4 | 100.1 | 100.1 | 99.4 | 100.2 | 100.0 | 100.0 | 100.6 | 100.0 | 100.5 | 100.1 |
| Robo ya nne | 101.3 | 100.7 | 100.2 | 99.8 | 100.1 | 100.1 | 99.5 | 100.2 | 100.0 | 100.0 | 100.6 | 100.0 | 100.6 | 100.3 |
| 2021 Robo ya kwanza | 102.8 | 104.6 | 102.6 | 100.3 | 107.1 | 102.9 | 100.6 | 101.3 | 98.6 | 102.4 | 105.4 | 100.0 | 100.7 | 102.2 |
| Robo ya pili | 104.7 | 113.5 | 103.1 | 99.7 | 108.1 | 103.3 | 101.7 | 101.0 | 98.6 | 103.6 | 107.4 | 100.2 | 101.6 | 103.1 |
| Robo ya tatu | 102.7 | 113.2 | 103.1 | 99.6 | 108.1 | 103.3 | 102.3 | 101.0 | 98.6 | 103.0 | 107.3 | 100.2 | 101.5 | 102.8 |
| Robo ya nne | 105.5 | 113.7 | 104.8 | 101.0 | 109.3 | 103.7 | 102.7 | 102.0 | 99.0 | 103.0 | 108.1 | 100.2 | 102.1 | 104.0 |
| 2022 Robo ya kwanza | 108.0 | 113.9 | 106.0 | 103.0 | 110.2 | 103.9 | 103.1 | 102.4 | 99.7 | 103.0 | 109.7 | 100.2 | 102.7 | 105.3 |
| Robo ya pili | 111.2 | 113.9 | 106.1 | 103.9 | 110.4 | 104.3 | 108.4 | 102.4 | 99.7 | 103.5 | 111.7 | 100.2 | 103.3 | 107.4 |
| Robo ya tatu | 107.9 | 113.9 | 107.0 | 103.0 | 110.7 | 105.6 | 113.1 | 102.3 | 101.9 | 104.3 | 111.3 | 100.1 | 103.6 | 107.8 |
| Robo ya nne | 108.5 | 113.5 | 107.6 | 104.1 | 112.0 | 107.7 | 106.9 | 102.5 | 102.5 | 104.4 | 112.5 | 100.0 | 105.7 | 107.1 |
| 2023 Robo ya kwanza | 112.9 | 113.6 | 108.2 | 104.6 | 112.3 | 109.2 | 107.2 | 102.8 | 102.5 | 105.0 | 115.1 | 100.1 | 106.2 | 108.5 |
| Robo ya pili | 114.0 | 113.6 | 108.4 | 105.4 | 112.1 | 109.3 | 106.6 | 102.8 | 102.3 | 105.0 | 115.7 | 100.0 | 107.4 | 108.8 |
| Robo ya tatu | 112.4 | 117.0 | 110.1 | 105.7 | 113.3 | 111.9 | 110.4 | 103.5 | 105.6 | 105.0 | 116.4 | 100.0 | 115.5 | 110.0 |
| Robo ya nne | 114.0 | 118.9 | 112.5 | 108.3 | 114.4 | 111.9 | 110.8 | 103.0 | 108.2 | 105.0 | 116.8 | 100.2 | 117.0 | 111.3 |
| 2024 Robo ya kwanza | 118.5 | 121.4 | 114.9 | 112.9 | 116.0 | 115.5 | 113.9 | 106.7 | 111.1 | 108.6 | 121.3 | 100.3 | 137.3 | 115.1 |
| Robo ya pili | 121.3 | 122.7 | 115.9 | 116.5 | 117.0 | 116.1 | 115.5 | 108.0 | 113.5 | 111.3 | 122.0 | 100.4 | 141.5 | 117.1 |
| Robo ya tatu | 117.5 | 122.5 | 116.6 | 115.2 | 117.6 | 116.1 | 115.6 | 108.1 | 115.4 | 112.7 | 122.3 | 100.4 | 142.0 | 116.5 |
| Robo ya nne | 119.3 | 121.7 | 116.1 | 115.5 | 118.8 | 116.0 | 115.3 | 108.6 | 117.2 | 112.8 | 122.3 | 100.4 | 143.1 | 116.9 |
| 2025 Robo ya kwanza | 124.8 | 122.3 | 120.1 | 116.1 | 120.9 | 116.4 | 116.4 | 108.8 | 118.3 | 124.1 | 122.6 | 100.4 | 148.6 | 119.2 |
| Robo ya pili | 129.8 | 122.3 | 120.4 | 117.4 | 122.8 | 117.4 | 118.1 | 109.0 | 118.9 | 124.3 | 123.7 | 100.4 | 149.2 | 121.1 |
| Robo ya tatu | 129.4 | 121.7 | 120.1 | 116.3 | 123.9 | 117.4 | 119.2 | 108.9 | 118.6 | 123.8 | 123.4 | 100.4 | 149.4 | 121.1 |
| Robo ya nne | 132.6 | 122.1 | 121.3 | 115.4 | 125.0 | 117.2 | 122.6 | 109.2 | 117.5 | 123.6 | 123.4 | 100.3 | 148.6 | 122.4 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

***Jina limebadilika kutoka Kundi la CHAKULA; Toka Des 2020 linasomeka vyakula na vinywaji baridi

**Jedwali Na. 20: FAHIRISI YA GHARAMA YA MAISHA YA WENYE KIPATO CHA JUU DAR-ES-SALAAM (Jan - Des. 2020 =100)**

| Mwaka | Miezi/ Robo-Mwaka | | | | Wastani | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo ya Kwanza | Robo ya Pili | Robo ya Tatu | Robo ya Nne | | |
| 2016 | 85.46 | 86.73 | 86.65 | 86.98 | 86.45 | |
| 2017 | 87.99 | 89.47 | 90.83 | 92.16 | 90.11 | 4.2 |
| 2018 | 92.65 | 94.11 | 94.87 | 95.59 | 94.31 | 4.7 |
| 2019 | 96.37 | 98.13 | 97.92 | 98.21 | 97.66 | 3.6 |
| **2020 | 99.96 | 99.70 | 100.08 | 100.26 | 100.00 | 2.4 |
| 2021 | 102.17 | 103.08 | 102.81 | 104.03 | 103.02 | 3.0 |
| 2022 | 105.30 | 107.39 | 107.81 | 107.14 | 106.91 | 3.8 |
| 2023 | 108.47 | 108.78 | 110.02 | 111.25 | 109.63 | 2.5 |
| 2024 | 115.15 | 117.11 | 116.45 | 116.90 | 116.40 | 6.2 |
| 2025 | 119.23 | 121.06 | 121.07 | 122.43 | 120.95 | 3.9 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

**Jedwali Na. 21: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA (Jan - Des. 2020 =100)**

| Mwaka | *** Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **2020 Robo ya kwanza | 98.80 | 99.48 | 99.52 | 98.10 | 99.44 | 99.41 | 101.06 | 99.12 | 100.52 | 99.87 | 99.51 | 99.97 | 99.61 | 99.16 |
| Robo ya pili | 101.16 | 99.92 | 100.06 | 100.58 | 100.05 | 99.85 | 101.33 | 99.98 | 100.57 | 100.04 | 99.67 | 99.97 | 100.20 | 100.72 |
| Robo ya tatu | 100.11 | 100.28 | 100.08 | 100.57 | 100.26 | 100.31 | 98.69 | 100.22 | 100.07 | 100.04 | 100.35 | 100.03 | 100.24 | 100.04 |
| Robo ya nne | 99.92 | 100.33 | 100.34 | 100.76 | 100.25 | 100.43 | 98.93 | 100.68 | 98.85 | 100.05 | 100.47 | 100.03 | 99.95 | 100.08 |
| 2021 Robo ya kwanza | 102.31 | 101.37 | 103.65 | 103.09 | 102.60 | 102.04 | 101.86 | 101.25 | 102.49 | 100.92 | 103.50 | 100.20 | 102.25 | 102.46 |
| Robo ya pili | 106.03 | 102.28 | 104.50 | 104.18 | 102.98 | 102.51 | 103.09 | 101.82 | 102.87 | 101.24 | 105.13 | 100.28 | 102.62 | 104.16 |
| Robo ya tatu | 104.33 | 102.49 | 104.76 | 104.50 | 103.33 | 103.06 | 103.88 | 102.03 | 102.96 | 101.17 | 105.31 | 100.31 | 103.03 | 103.94 |
| Robo ya nne | 104.34 | 102.79 | 105.30 | 104.69 | 103.88 | 103.35 | 104.51 | 102.26 | 102.56 | 101.16 | 105.59 | 100.34 | 103.26 | 104.20 |
| 2022 Robo ya kwanza | 108.75 | 103.23 | 106.51 | 106.56 | 105.60 | 103.55 | 105.61 | 102.42 | 103.98 | 101.41 | 106.54 | 100.44 | 104.59 | 106.29 |
| Robo ya pili | 112.39 | 103.49 | 106.83 | 108.63 | 106.31 | 103.92 | 109.96 | 102.46 | 104.01 | 101.60 | 107.19 | 100.49 | 105.16 | 108.41 |
| Robo ya tatu | 112.17 | 103.46 | 107.30 | 108.26 | 107.17 | 104.39 | 112.42 | 102.69 | 104.45 | 101.87 | 107.27 | 100.54 | 105.31 | 108.80 |
| Robo ya nne | 114.18 | 103.65 | 107.86 | 107.88 | 107.96 | 104.88 | 110.52 | 103.50 | 104.68 | 101.90 | 108.28 | 100.14 | 105.75 | 109.30 |
| 2023 Robo ya kwanza | 119.35 | 103.76 | 109.16 | 108.19 | 108.67 | 105.39 | 111.89 | 104.06 | 105.28 | 104.65 | 109.62 | 100.28 | 106.46 | 111.40 |
| Robo ya pili | 121.89 | 104.86 | 110.25 | 109.44 | 109.33 | 105.56 | 111.84 | 104.33 | 105.94 | 105.10 | 111.90 | 100.09 | 107.22 | 112.69 |
| Robo ya tatu | 118.66 | 107.31 | 110.81 | 109.66 | 111.01 | 106.34 | 113.18 | 104.73 | 107.02 | 105.32 | 112.85 | 100.74 | 109.44 | 112.42 |
| Robo ya nne | 118.16 | 107.66 | 111.26 | 110.72 | 111.77 | 106.38 | 113.95 | 104.88 | 108.07 | 105.48 | 113.21 | 100.74 | 109.85 | 112.73 |
| 2024 Robo ya kwanza | 121.24 | 108.11 | 112.06 | 113.48 | 112.43 | 107.49 | 115.83 | 105.74 | 109.08 | 107.52 | 114.62 | 101.41 | 114.11 | 114.75 |
| Robo ya pili | 123.46 | 108.56 | 112.45 | 115.68 | 113.01 | 107.68 | 117.54 | 106.16 | 109.49 | 108.42 | 115.45 | 101.72 | 115.40 | 116.18 |
| Robo ya tatu | 121.18 | 109.52 | 112.87 | 116.21 | 113.68 | 108.14 | 118.16 | 106.03 | 109.93 | 108.79 | 116.25 | 101.86 | 115.72 | 115.90 |
| Robo ya nne | 122.24 | 109.92 | 113.03 | 115.29 | 114.11 | 108.35 | 118.12 | 106.12 | 110.33 | 108.80 | 116.30 | 101.94 | 116.44 | 116.15 |
| 2025 Robo ya kwanza | 127.61 | 111.95 | 114.25 | 116.91 | 114.89 | 108.94 | 118.81 | 106.07 | 110.92 | 112.09 | 116.60 | 102.12 | 117.80 | 118.37 |
| Robo ya pili | 130.92 | 112.27 | 114.70 | 119.09 | 115.50 | 109.47 | 119.65 | 106.21 | 111.14 | 112.16 | 117.22 | 102.44 | 118.08 | 119.94 |
| Robo ya tatu | 130.22 | 113.00 | 114.92 | 118.45 | 116.54 | 109.59 | 120.02 | 106.29 | 111.09 | 112.05 | 117.34 | 102.36 | 118.27 | 119.83 |
| Robo ya nne | 130.67 | 113.77 | 115.30 | 117.95 | 117.58 | 109.71 | 121.55 | 106.54 | 110.96 | 112.01 | 117.45 | 102.31 | 118.19 | 120.25 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

***Jina limebadilika kutoka Kundi la CHAKULA; Toka Des 2020 linasomeka VYAKULA NA VINYWAJI BARIDI

**Jedwali Na. 22: FAHIRISI ZA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI TANZANIA BARA (Jan - Des. 2020 =100)**

| Mwaka | Robo ya Mwaka | | | | | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo ya Kwanza | Robo ya Pili | Robo ya Tatu | Robo ya Nne | Wastani wa Fahirisi | |
| **2020 | 99.16 | 100.72 | 100.04 | 100.08 | 100.00 | |
| 2021 | 102.46 | 104.16 | 103.94 | 104.20 | 103.69 | 3.7 |
| 2022 | 106.29 | 108.41 | 108.80 | 109.30 | 108.20 | 4.3 |
| 2023 | 111.40 | 112.69 | 112.42 | 112.73 | 112.31 | 3.8 |
| 2024 | 114.75 | 116.18 | 115.90 | 116.15 | 115.75 | 3.1 |
| 2025 | 118.37 | 119.94 | 119.83 | 120.25 | 119.60 | 3.3 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

**Jedwali Na. 23: FAHIRISI ZA BEI MBALIMBALI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI-TANZANIA BARA ( Jan - Des. 2020 =100)**

| Mwaka | FAHIRISI | | | WAKAZI MIJINI TANZ. BARA | BADILIKO (Asilimia) | | | WAKAZI MIJINI TANZ. BARA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | KIPATO CHA | | | | KIPTO CHA | | | |
| | CHINI | KATI | JUU | | CHINI | KATI | JUU | |
| **2020 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | | | | |
| 2021 | 102.37 | 102.40 | 103.02 | 103.69 | 2.4 | 2.4 | 3.0 | 3.7 |
| 2022 | 107.16 | 108.38 | 106.91 | 108.20 | 4.7 | 5.8 | 3.8 | 4.3 |
| 2023 | 112.77 | 113.72 | 109.63 | 112.31 | 5.2 | 4.9 | 2.5 | 3.8 |
| 2024 | 119.30 | 122.68 | 116.40 | 115.75 | 5.8 | 7.9 | 6.2 | 3.1 |
| 2025 | 124.76 | 128.24 | 120.95 | 119.60 | 4.6 | 4.5 | 3.9 | 3.3 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
**Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika (Jan - Dec. 2020 = 100)

## SURA YA 2

## FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA


### Utekelezaji wa Sera ya Fedha

25. Mwaka 2025, riba ya Benki Kuu ilikuwa asilimia 6.0 katika robo mbili za kwanza na ilipunguzwa hadi asilimia 5.75 kwa robo ya tatu na kubaki katika kiwango hicho katika robo ya nne ikilinganishwa asilimia 5.5 katika robo ya kwanza na asilimia 6.0 katika robo tatu zilizobaki mwaka 2024. Aidha, riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha baina ya benki za biashara ilikuwa wastani wa asilimia 7.25 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.67 mwaka 2024. Kiwango hiki kilibaki ndani ya wigo wa asilimia +/-2 ya riba ya Benki Kuu. Hii iliakisi uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi kinachoendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi.

### Ujazi wa Fedha

26. Mwaka 2025, kasi ya ukuaji wa ujazi wa fedha iliendelea kuwa ya kuridhisha sambamba na mwelekeo wa sera ya fedha na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi nchini. Katika kipindi kilichoishia Desemba 2025, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 25.8 na kufikia shilingi bilioni 61,524.3 kutoka shilingi bilioni 48,905.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Hii ilichangiwa zaidi na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi. Aidha, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa asilimia 29.6 na kufikia shilingi bilioni 48,143.2 katika kipindi kilichoishia Desemba 2025, ikilinganishwa na shilingi bilioni 37,139.7 kipindi kama hicho mwaka 2024. Vilevile, ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu (M1) ulikua kwa asilimia 31.8 na kufikia shilingi bilioni 30,199.0 katika kipindi kilichoishia Desemba 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 22,905.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (**Kielelezo Na. 2.1**).

**Kielelezo Na. 2.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Ujazi wa Fedha, Mwaka 2021 - 2025**



**Mikopo kwa Sekta Binafsi**


27. Mwaka 2025, mikopo iliyotolewa na benki za biashara kwa sekta binafsi iliongezeka kwa wastani wa asilimia 23.6 na kufikia shilingi bilioni 44,603.1 kutoka shilingi bilioni 36,097.4 mwaka 2024. Ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi lilichangiwa na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi, kuboreshwa kwa mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji pamoja na utekelezaji thabiti wa sera za fedha na bajeti. Katika kipindi hicho, mikopo katika shughuli za uchimbaji madini na mawe iliongoza kwa ukuaji wa asilimia 91.1 ikifuatiwa na shughuli za biashara (asilimia 49.7), shughuli za uchukuzi na mawasiliano (asilimia 29.4) na shughuli za kilimo (asilimia 28.9). Aidha, mikopo iliyoelekezwa katika shughuli binafsi (ambayo hutumika kugharamia biashara ndogo na za kati) iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo iliyotolewa kwa sekta binafsi, ikichangia asilimia 37.0 ya mikopo yote iliyotolewa, ikifuatiwa na mikopo kwa shughuli za biashara (asilimia 15.9) na shughuli za kilimo (asilimia 13.6). **Jedwali Na. 2.1 na Kielelezo Na. 2.2** vinaonesha mwenendo wa mikopo kwa sekta binafsi.

**Jedwali Na. 2.1: Mikopo Iliyotolewa na Benki za Biashara katika Shughuli za Kiuchumi, Mwaka 2021 - 2025**

| Shughuli | Kipindi kilichoishia Desemba (Shilingi Bilioni) | | | | | Ukuaji (Asilimia) | | Mchango (Asilimia) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 | 2024 | 2025 |
| Uchimbaji madini na mawe | 474.0 | 575.9 | 785.4 | 500.3 | 955.9 | -36.3 | 91.1 | 1.4 | 2.1 |
| Biashara | 3,657.3 | 4,556.4 | 4,473.4 | 4,723.9 | 7,072.7 | 5.6 | 49.7 | 13.1 | 15.9 |
| Uchukuzi na mawasiliano | 1,053.9 | 1,207.0 | 1,420.3 | 1,607.9 | 2,080.1 | 13.2 | 29.4 | 4.5 | 4.7 |
| Kilimo | 1,592.5 | 2,327.4 | 3,340.8 | 4,712.1 | 6,073.1 | 41 | 28.9 | 13.1 | 13.6 |
| Ujenzi | 998.4 | 1,200.6 | 1,483.1 | 1,655.1 | 2,079.4 | 11.6 | 25.6 | 4.6 | 4.7 |
| Shughuli binafsi | 8,047.7 | 10,365.7 | 12,238.0 | 14,032.9 | 16,512.2 | 14.7 | 17.7 | 38.9 | 37.0 |
| Umeme | 143.9 | 130.3 | 291.3 | 268.5 | 281.5 | -7.8 | 4.8 | 0.7 | 0.6 |
| Mahoteli na migahawa | 542.7 | 511.3 | 534.0 | 548.4 | 562.1 | 2.7 | 2.5 | 1.5 | 1.3 |
| Uzalishaji viwandani | 2,111.1 | 2,709.5 | 3,132.0 | 3,643.1 | 3,345.4 | 16.3 | -8.2 | 10.1 | 7.5 |
| Shughuli nyinginezo | 3,722.5 | 3,788.3 | 4,403.8 | 4,405.1 | 5,640.6 | 0 | 28 | 12.2 | 12.6 |
| **Jumla** | **22,344.1** | **27,372.5** | **32,102.0** | **36,097.4** | **44,603.1** | **12.4** | **23.6** | **100.0** | **100.0** |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo Na. 2.2: Mchango wa Mikopo Iliyotolewa na Benki za Biashara katika baadhi ya Shughuli za Kiuchumi (Asilimia)**




**Amana katika Benki za Biashara**

28. Mwaka 2025, amana katika benki za biashara zilifikia shilingi bilioni 54,376.9 kutoka shilingi bilioni 41,465.7 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 31.1. Hii ilichangiwa na kuendelea kuongezeka kwa mawakala wa benki na matumizi ya mifumo ya kidijitali katika kutoa huduma za fedha. Aidha, amana za sekta binafsi ziliongezeka kwa asilimia 32.4 na kufikia shilingi bilioni 53,032.0 mwaka 2025 kutoka shilingi bilioni 40,025.8 mwaka 2024. Kwa upande mwingine, uwiano wa amana za fedha za kigeni kwa amana zote ulipungua na kufikia asilimia 26.4 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 27.4 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kuimarika kwa thamani ya shilingi na utekelezaji wa katazo la matumizi ya fedha za kigeni katika miamala ya ndani ya nchi.

**Mwenendo wa Viwango vya Riba**

29. Mwaka 2025, viwango vya riba katika masoko ya fedha vilipungua kutokana na uwepo wa kiwango cha ukwasi kinachoendana na mahitaji ya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Katika kipindi hicho, wastani wa riba ya jumla katika soko la fedha baina ya benki ulipungua na kufikia asilimia 7.26 ikilinganishwa na asilimia 7.50 mwaka 2024. Aidha, riba ya jumla ya dhamana za Serikali za muda mfupi ilipungua na kufikia asilimia 8.38 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 10.67 mwaka 2024.


30. Mwaka 2025, wastani wa riba za jumla za mikopo ulipungua hadi asilimia 15.26 ikilinganishwa na asilimia 15.47 mwaka 2024. Aidha, viwango vya riba za mikopo ya mwaka mmoja vilipungua na kufikia wastani wa asilimia 15.69 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 15.82 mwaka 2024. Vilevile, wastani wa riba za amana za muda

maalum uliongezeka hadi asilimia 8.40 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 7.85 mwaka 2024. Wastani wa riba za amana za mwaka mmoja uliongezeka na kufikia asilimia 9.58 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 9.17 mwaka 2024. Tofauti ya viwango vya riba za amana za mwaka mmoja na riba za mikopo za mwaka mmoja ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 6.11 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 6.65 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuendelea kutekeleza hatua za kisera zinazolenga kupunguza viwango vya riba za mikopo nchini.

**Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania**

31. Mwaka 2025, thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani iliendelea kuwa imara kutokana na: kuimarika kwa mazingira ya kiuchumi duniani yaliyosababisha kushuka kwa viwango vya riba katika nchi zilizoendelea na kuimarika kwa bei za bidhaa ikiwemo mafuta ghafi; na kuongezeka kwa ukwasi wa fedha za kigeni nchini kulikotokana na shughuli za utalii, mauzo ya dhahabu na bidhaa za kilimo. Katika kipindi hicho, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,549.8 ikilinganishwa na shilingi 2,610.5 kwa dola moja ya Marekani mwaka 2024, sawa na ongezeko la thamani ya shilingi dhidi ya dola kwa asilimia 2.3 (**Kielelezo Na. 2.3**).

**Kielelezo Na. 2.3: Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji Kati ya Shilingi na Dola ya Marekani**




**MAENDELEO KATIKA SEKTA YA FEDHA**

**Huduma za Benki**

32. Hadi Desemba 2025, idadi ya benki nchini iliendelea kubaki 42 kama ilivyokuwa mwaka 2024. Aidha, matawi ya benki yaliongezeka na kufikia 1,049 mwaka 2025 kutoka matawi 1,027 mwaka 2024. Katika kipindi hicho, benki 30 ziliendelea kutoa huduma za benki kwa njia ya uwakala kama ilivyokuwa mwaka 2024. Aidha, idadi ya mawakala wa

benki iliongezeka kwa asilimia 29.1 na kufikia mawakala 187,692 mwaka 2025 kutoka mawakala 145,430 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilichangiwa na hatua ya Benki Kuu ya Tanzania kuendelea kulegeza masharti ya kufanya biashara ya uwakala.

**Mwenendo wa Viashiria vya Sekta ya Benki**

33. Mwaka 2025, uwiano wa mtaji halisi na mtaji mkuu kwa rasilimali hatarishi ulikuwa asilimia 19.3 na asilimia 20.2 ikilinganishwa na asilimia 19.4 na asilimia 20.0, mtawalia mwaka 2024. Aidha, uwiano wa ukwasi dhidi ya amana za muda mfupi katika benki ulipungua hadi asilimia 27.2 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 28.6 mwaka 2024.

34. Mwaka 2025, kiwango cha mikopo chechefu kilipungua na kufikia wastani wa asilimia 2.8 ikilinganishwa na asilimia 3.3 mwaka 2024. Hii ilitokana na hatua mbalimbali zilizoendelea kuchukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania, ikiwemo: kuendelea kuzielekeza benki kutumia taarifa za wakopaji kutoka kwa kampuni za kuchakata na kutunza kumbukumbu za mikopo; na kuzitaka benki na taasisi za fedha kuimarisha taratibu za utoaji na ufuatiliaji wa mikopo. Aidha, idadi ya taasisi zilizotumia kanzidata ya wakopaji iliongezeka na kufikia 295 mwaka 2025 ikilinganishwa na taasisi 188 mwaka 2024. Vilevile, idadi ya wakopaji waliosajiliwa kwenye kanzidata ya wakopaji iliongezeka kwa asilimia 35.8 na kufikia 15,224,451 mwaka 2025 ikilinganishwa na wakopaji 11,209,343 mwaka 2024.

**Maboresho katika Sekta ya Benki**

35. Mwaka 2025, Benki Kuu iliendelea kutoa kanuni na miongozo mbalimbali ya kusimamia benki na taasisi za fedha ili kuhakikisha sekta hii inaendelea kuwa thabiti, imara na himilivu. Katika kipindi hicho, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa kanuni ya usimamizi kwa benki zisizo na riba (islamic banking). Aidha, Benki Kuu ilitoa miongozo mitatu ambayo ni: Mwongozo kwa Wakopeshaji wa Kidijitali; Mwongozo ya Kudhibiti Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Sekta ya fedha; na Mwongozo wa Uwasilishwaji wa Taarifa za Vihatarishi na Fursa za Uendelevu wa Benki na Taasisi za Fedha.

**Huduma Ndogo za Fedha**

36. Hadi Desemba 2025, leseni za watoa huduma ndogo za fedha daraja la pili zilizotolewa ziliongezeka kwa asilimia 25.4 na kufikia leseni 2,938 kutoka leseni 2,342 Desemba 2024. Katika kipindi hicho, leseni za watoa huduma za fedha daraja la tatu ziliongezeka kwa asilimia 5.4 na kufikia leseni 1,016 kutoka leseni 964 Desemba 2024. Aidha, watoa huduma ndogo za fedha daraja la nne waliosajiliwa walifikia 74,534 Desemba 2025 kutoka watoa huduma ndogo daraja la nne 58,926 kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 26.5. Ongezeko la leseni na usajili wa watoa huduma ndogo za fedha lilitokana na kuongezeka kwa uelewa wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018 na Kanuni

zake za Mwaka 2019 pamoja na utayari wa watoa huduma ndogo za fedha kuomba leseni na kujisajili.

**Masoko ya Mitaji na Dhamana**

37. Mwaka 2025, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana - CMSA ilitoa na kuhuisha leseni 251 ikilinganishwa na leseni 231 zilizotolewa na kuhuishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 8.7. Leseni zilizotolewa zilikuwa katika makundi yafuatayo: Soko la Hisa leseni moja; Soko la Bidhaa (1); Hifadhi Kuu ya Dhamana (1); kampuni za utendaji katika Soko la Hisa (22); watendaji katika Soko la Bidhaa (5); watendaji katika Soko la Hatifungani (8); Washauri Wateule (4); Washauri wa Uwekezaji (27); Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (28); mameneja wa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (26); Watunza Dhamana (10); na wawakilishi wa taasisi zinazotoa huduma katika masoko ya mitaji (118). Hadi Desemba 2025, mtaji wa soko la hisa kwa kampuni za ndani uliongezeka kwa asilimia 27.3 na kufikia shilingi trilioni 15.58 ikilinganishwa na shilingi trilioni 12.24 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, mtaji wa jumla wa soko la hisa uliongezeka kwa asilimia 34.3 na kufikia shilingi trilioni 23.99 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi trilioni 17.87 mwaka 2024. Kuongezeka kwa mtaji kulitokana na kuimarika kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa, ikiwemo CRDB Bank Plc, NMB Bank Plc, DSE Plc, National Investment Company Limited (NICO), Swissport Tanzania Plc, Twiga Cement Plc na Afriprise.

38. Mwaka 2025, fahirisi ya Soko la Hisa la Dar es Salaam - DSE kwa hisa za kampuni za ndani iliongezeka kwa asilimia 24.7 na kufikia alama 5,759.41 ikilinganishwa na alama 4,618.78 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa DSE zinazotoa huduma katika sekta za viwanda na fedha. Ongezeko la fahirisi liliashiria ufanisi wa soko. Kwa upande mwingine, fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni zote za ndani na nje iliongezeka kwa asilimia 29.1 na kufikia alama 2,761.93 mwaka 2025 ikilinganishwa na alama 2,139.73 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni za ndani na nje ya nchi zilizoorodheshwa DSE.

39. Mwaka 2025, mauzo ya hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam yalikuwa shilingi bilioni 659.63 ikilinganishwa na shilingi bilioni 228.64 mwaka 2024. Ongezeko la mauzo lilitokana na elimu iliyotolewa na matumizi ya mfumo wa kidigitali (DSE Hisa Kiganjani). Aidha, mauzo ya hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka kwa asilimia 84.5 na kufikia shilingi trilioni 6.2 ikilinganishwa na shilingi trilioni 3.36 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kufuatia elimu inayoendelea kutolewa kuhusu umuhimu wa kuwekeza katika hatifungani. Vilevile, mauzo ya hatifungani za kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la

DSE yaliongezeka kwa asilimia 79.7 na kufikia shilingi bilioni 11.5 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6.4 mwaka 2024.

40. Hadi Desemba 2025, thamani ya uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja iliongezeka kwa asilimia 63.5 na kufikia shilingi trilioni 4.40 ikilinganishwa na shilingi trilioni 2.69 katika kipindi kilichoishia Desemba 2024 (**Jedwali Na. 2.2**). Ongezeko hilo lilitokana na mwitikio wa wawekezaji uliochangiwa na elimu iliyotolewa pamoja na matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma kwa wawekezaji.

**Jedwali Na. 2.2: Thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja, Mwaka 2024 - 2025**

| Meneja wa Mifuko | Jina la Mfuko | 31 Desemba 2024 | | 31 Desemba 2025 | | Ongezeko la Thamani ya Mfuko (Asilimia) | Ongezeko la Bei ya Kipande (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Thamani ya Mfuko (Shilingi) | Bei ya Kipande (Shilingi | Thamani ya Mfuko (Shilingi) | Bei ya Kipande (Shilingi) | | |
| UTT AMIS Plc | Mfuko wa Umoja | 371,502,175,945.9 | 1,101.10 | 423,247,456,732.1 | 1,267.60 | 13.9 | 15.1 |
| | Mfuko wa Wekeza Maisha | 19,141,116,469.0 | 970.9 | 30,165,154,017.1 | 1,121.30 | 57.6 | 15.5 |
| | Mfuko wa Watoto | 24,012,875,156.0 | 715.8 | 40,568,673,717.1 | 829.7 | 68.9 | 15.9 |
| | Mfuko wa Jikimu | 32,326,675,609.9 | 184 | 47,753,135,309.9 | 199.6 | 47.7 | 8.5 |
| | Mfuko wa Ukwasi | 1,359,669,789,869.2 | 434 | 2,307,807,292,757.4 | 489.6 | 69.7 | 12.8 |
| | Mfuko wa Hatifungani | 768,247,503,090.0 | 119.6 | 1,104,811,359,034.2 | 122.5 | 43.8 | 2.4 |
| Watumishi Housing Investments | Mfuko wa Faida | 33,491,896,212.6 | 123.2 | 51,360,152,055.8 | 139.2 | 53.4 | 13 |
| Zan Securities Limited | Mfuko wa Timiza | 14,455,172,884.5 | 106.4 | 27,157,407,547.0 | 122.4 | 87.9 | 15 |
| Sanlam Investments | Mfuko wa Sanlam Money Market | 4,187,410,197.0 | 1 | 96,916,895,764.0 | 1 | 2,214.5 | 0 |
| Orbit Securities Limited | Mfuko wa Inuka money market | 10,557,081,716.0 | 120.98 | 33,882,447,121.0 | 121 | 220.9 | 0 |
| | Mfuko wa Inuka Dozen | - | - | 7,050,640,257.0 | 100.45 | - | - |
| iTrust Finance Limited | Mfuko wa iCash | 13,079,699,510.1 | 100.8 | 35,158,177,888.9 | 112.8 | 168.8 | 11.9 |
| | Mfuko wa iGrowth | 18,031,630,301.1 | 100.45 | 97,122,955,898.2 | 145.8 | 438.6 | 45.1 |
| | Mfuko wa iSave | 4,131,979,890.3 | 100.47 | 10,595,541,755.1 | 113.9 | 156.4 | 13.4 |
| | Mfuko wa iIncome | 11,656,771,316.1 | 100.92 | 16,305,514,019.6 | 114.3 | 39.9 | 13.3 |
| | Mfuki wa Imaan | 5,389,155,139.1 | 108.82 | 14,826,612,682.7 | 139 | 175.1 | 27.7 |
| | Mfuko wa iDollar | - | - | 32,327,003,542.0 | 102.2 | - | - |
| Global Alpha Capital Limited | Halal Fund | - | - | 1,303,921,859.0 | - | - | - |
| Vertex International Securities | Vertex Bond Fund | - | - | 5,896,683,809.0 | - | - | - |
| | Vertex ETF | - | - | 14,499,163,434.0 | - | - | - |
| **Thamani ya Jumla** | | **2,689,880,933,306.8** | | **4,398,756,189,201.1** | | **63.5** | |

**Chanzo:** Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja na Watumishi Housing Investments

## Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma

41. Mwaka 2024/25, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma - PSSSF ulisajili wanachama wapya 42,271 ikilinganishwa na wanachama 42,811 waliosajiliwa mwaka 2023/24. Aidha, wanachama wachangiaji wa Mfuko walifikia 807,010 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na wanachama 767,234 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ajira mpya za watumishi wa Serikali hususan katika sekta ya elimu na afya. Katika kipindi hicho, idadi ya wastaafu walionufaika na Mfuko iliongezeka kwa asilimia 22.2 na kufikia wastaafu 44,451 kutoka wastaafu 36,371 mwaka 2023/24. Kwa upande mwingine, Mfuko ulikusanya shilingi bilioni 2,084.10 kutokana na michango ya wanachama ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,842.45 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 13.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ajira na kupanda kwa madaraja ya watumishi. Aidha, PSSSF ililipa mafao yenye thamani ya shilingi bilioni 1,484.73 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na mafao ya shilingi bilioni 1,484.78 mwaka 2023/24. Hii ilitokana na kupungua kwa thamani ya madai yaliyowasilishwa.

42. Mwaka 2024/25, thamani ya uwekezaji wa Mfuko ilifikia shilingi trilioni 9.15 kutoka shilingi trilioni 8.44 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 8.4. Hii ilitokana na uwekezaji mpya katika amana za muda maalum na hatifungani za Serikali. Aidha, mapato yatokanayo na uwekezaji yaliongezeka kwa asilimia 78.3 na kufikia shilingi bilioni 977.69 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na shilingi bilioni 548.28 mwaka 2023/24. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mapato ya riba kutoka katika uwekezaji. Vilevile, thamani ya rasilimali halisi za Mfuko iliongezeka kwa asilimia 7.9 na kufikia shilingi bilioni 9,966.36 mwaka 2024/25 kutoka shilingi bilioni 9,239.28 mwaka 2023/24. Ongezeko hilo lilichangiwa na kupungua kwa gharama za uendeshaji.

**Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii**

43. Mwaka 2024/25, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii - NSSF ulisajili wanachama wapya 363,925 ikilinganishwa na wanachama wapya 291,266 waliosajiliwa mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 25.0. Katika kipindi hicho, wanachama wachangiaji wa NSSF walifikia 1,616,026 kutoka wanachama 1,358,882 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 18.9. Ongezeko hilo lilichangiwa na maboresho ya mifumo ya ukaguzi na matumizi ya TEHAMA yaliyowezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za wajiri na wanachama wa mfuko kwa wakati. Aidha, NSSF ilikuwa na wastaafu 35,143 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na wastaafu 31,914 waliokuwepo mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 10.1.

44. Mwaka 2024/25, mafao yaliyolipwa kwa wanachama yaliongezeka kwa asilimia 8.7 na kufikia shillingi bilioni 961.78 ikilinganishwa na shilingi bilioni 884.82 zilizolipwa mwaka 2023/24. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa maombi ya fao la ukosefu wa ajira pamoja na idadi ya wastaafu. Katika kipindi hicho, mapato halisi yatokanayo na uwekezaji wa NSSF yaliongezeka kwa asilimia 25.5 na kufikia shilingi bilioni 543.99 ikilinganishwa na shilingi bilioni 433.47 zilizokusanywa mwaka 2023/24. Aidha, thamani ya vitega uchumi vya NSSF iliongezeka kwa asilimia 8.8 na kufikia shilingi bilioni 8,090.86 mwaka 2024/25 kutoka shilingi bilioni 7,434.27 mwaka 2023/24. Ongezeko la mapato ya uwekezaji na thamani ya vitega uchumi lilichangiwa na uwekezaji uliofanywa katika hatifungani za Serikali, amana za muda maalumu pamoja na gawio la hisa na mapato ya kodi za upangishaji.

45. Mwaka 2024/25, NSSF ilikusanya michango ya shilingi bilioni 2,462.86 kutoka kwa wanachama ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,969.61 zilizokusanywa mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 25.0. Hii ilichangiwa na ukuaji wa sekta binafsi, maboresho ya mifumo ya ukaguzi na matumizi ya TEHAMA katika usajili na uchangiaji. Aidha, thamani ya Mfuko iliongezeka kwa asilimia 18.4 na kufikia shilingi bilioni 9,840.73 mwaka 2024/25 kutoka shilingi bilioni 8,308.18 mwaka 2023/24. Ongezeko hilo lilitokana na kukua kwa thamani ya uwekezaji na kuongezeka kwa michango ya wanachama.

**Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi**

46. Mwaka 2024/25, waajiri waliosajiliwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi - WCF waliongezeka kwa asilimia 12.4 na kufikia 39,322 kutoka waajiri 34,996 mwaka 2023/24. Aidha, idadi ya waajiri wanaochangia ilipungua kwa asilimia 16.7 na kufikia waajiri 24,362 mwaka 2024/25 kutoka waajiri 29,238 mwaka 2023/24. Vilevile, idadi ya wafanyakazi wanaochangiwa ilipungua kwa asilimia 10.3 na kufikia wafanyakazi 1,629,960 mwaka 2024/25 kutoka wafanyakazi 1,817,054 mwaka 2023/24. Kupungua kwa waajiri wanaochangia na wafanyakazi wanaochangiwa kulitokana na kufungwa kwa baadhi ya biashara za waajiri. Kwa upande mwingine, michango kutoka kwa waajiri iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 104.48 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na shilingi bilioni 91.68 mwaka 2023/24. Ongezeko hilo lilitokana na matumizi ya mifumo ya TEHAMA, utoaji wa elimu kwa wadau na uboreshaji wa mazingira ya kazi.

47. Mwaka 2024/25, mapato ya uwekezaji wa WCF yaliongezeka kwa asilimia 12.9 na kufikia shilingi bilioni 99.18 ikilinganishwa na shilingi bilioni 87.88 mwaka 2023/24. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika hatifungani za Serikali. Aidha, mapato yaliyotokana na shughuli nyingine za kiuchumi yalikuwa shilingi milioni 231.96 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na shilingi milioni 138.48 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 67.5.

48. Mwaka 2024/25, WCF ililipa madai ya shilingi bilioni 51.43 kama gharama ya fidia kwa wafanyakazi walioumia au kufariki wakiwa kazini ikilinganishwa na shilingi bilioni 26.78 zilizolipwa mwaka 2023/24, sawa ongezeko la asilimia 92.0. Hii ilitokana na kuhuishwa kwa kiwango cha malipo ya pensheni kwa wanufaika, ongezeko la madai pamoja na maboresho ya mifumo ya utoaji wa huduma. Aidha, thamani halisi ya rasilimali za WCF iliongezeka kwa asilimia 12.8 na kufikia shilingi bilioni 770.27 mwaka 2024/25 kutoka shilingi bilioni 683.13 mwaka 2023/24. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato ya uwekezaji na michango pamoja na usimamizi mathubuti wa matumizi.

**Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya**

49. Mwaka 2024/25, idadi ya wanachama wachangiaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya - NHIF iliongezeka kwa asilimia 17.2 na kufikia wanachama 1,402,459 kutoka wanachama 1,196,205 mwaka 2023/24. Hii ilitokana na utekelezaji wa mikakati ya uhamasishaji, matumizi ya TEHAMA katika kusajili wanachama pamoja na kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi na isiyo rasmi. Aidha, idadi ya wanufaika ilifikia 5,339,210 mwaka 2024/25 kutoka wanufaika 5,028,735 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 6.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya wanachama wachangiaji pamoja na wanufaika kwa kila mwanachama (**Jedwali Na. 2.3**).

**Jedwali Na. 2.3: Wanachama Wachangiaji na Wanufaika wa Mfuko, Mwaka 2020/21 - 2024/25**

| Mwaka | Idadi ya Wanachama | Idadi ya Wanufaika | Ongezeko la Wanachama (Asilimia) | Ongezeko la Wanufaika (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| 2020/21 | 1,212,519 | 4,550,207 | 14.9 | 3.3 |
| 2021/22 | 1,353,535 | 4,821,233 | 11.6 | 6.0 |
| 2022/23 | 1,246,046 | 4,987,292 | -7.9 | 3.4 |
| 2023/24 | 1,196,205 | 5,028,735 | -4.0 | 0.8 |
| 2024/25 | 1,402,459 | 5,339,210 | 17.2 | 6.2 |

**Chanzo:** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

50. Mwaka 2024/25, thamani ya madai yaliyowasilishwa na watoa huduma ilikuwa shilingi bilioni 587.96 ikilinganishwa na madai ya shilingi bilioni 667.83, sawa na upungufu wa asilimia 12.0. Kati ya madai yaliyowasilishwa, madai ya shilingi bilioni 529.11 yalilipwa, sawa na asilimia 90.0 ikilinganishwa na shilingi bilioni 605.60 zilizolipwa mwaka 2023/24. Kutolipwa kwa baadhi ya madai yaliyowasilishwa kulitokana na: baadhi ya watoa huduma kutozingatia miongozo ya matibabu; matumizi yasiyo sahihi au ya ziada ya dawa na vipimo; upungufu au kutokamilika kwa nyaraka za madai; na vitendo vya udanganyifu.

51. Mwaka 2024/25, rasilimali halisi za NHIF ziliongezeka kwa asilimia 22.3 na kufikia shilingi trilioni 1.06 kutoka shilingi bilioni 866.48 mwaka 2023/24. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa akiba kutokana na matumizi ya TEHAMA, kuimarika kwa ukusanyaji wa michango, kudhibiti matumizi, uwekezaji wa kimkakati na kupungua kwa madeni. Kuongezeka kwa rasilimali halisi kuliiwezesha NHIF kupunguza muda wa kulipa madai toka wastani wa siku 60 mwaka 2023/24 hadi siku 50 mwaka 2024/25. Katika kipindi hicho, NHIF ilikusanya mapato ya shilingi bilioni 837.42 kutokana na michango ya wanachama, uwekezaji na vitega uchumi vingine ikilinganishwa na shilingi bilioni 758.1 zilizokusanywa mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 10.5 (**Jedwali Na. 2.4**). Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa michango ya wanachama, mapato ya uwekezaji na mapato kutoka vyanzo vingine.

**Jedwali Na. 2.4: Mapato ya Mfuko (Shilingi Milioni) Mwaka 2020/21- 2024/25**

| Vyanzo vya Mapato | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | Ongezeko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Michango | 489,479.6 | 552,580.2 | 633,627.1 | 700,106.8 | 773,418.07 | 10.5 |
| Uwekezaji | 77,110.9 | 69,447.0 | 59,259.4 | 51,002.0 | 56,295.82 | 10.4 |
| Vyanzo vingine | 3,161.6 | 2,468.6 | 4,230.2 | 7,010.5 | 7,705.9 | 9.9 |
| **Jumla** | **569,752.1** | **624,495.8** | **697,116.7** | **758,119.3** | **837,419.79** | 10.5 |

**Chanzo:** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

52. Mwaka 2024/25, vituo vya kutolea huduma za afya vilivyosajiliwa na NHIF vilifikia 10,139 kutoka vituo 10,003 mwaka 2023/24 (**Jedwali Na. 2.5)**. Kati ya hivyo, vituo 8,263, sawa na asilimia 81.5 vilikuwa vinamilikiwa na Serikali; vituo 1,176 vya binafsi (asilimia 11.6); na vituo 700 taasisi za kidini (asilimia 6.9). Ongezeko la vituo lilitokana na kuendelea kuboreshwa kwa upatikanaji wa huduma za afya kwa wote.

**Jedwali Na. 2.5: Vituo Vilivyosajiliwa na Mfuko, Mwaka 2020/21 - 2024/25**

| Ngazi ya Kituo | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Zahanati | 6,252 | 6,582 | 6,619 | 7,229 | 7,849 | 8.6 |
| Vituo vya Afya | 832 | 912 | 939 | 1,096 | 1,296 | 18.2 |
| Hospitali | 381 | 417 | 434 | 461 | 519 | 12.6 |
| Maduka ya Dawa | 560 | 685 | 635 | 648 | 149 | -77.0 |
| ADDO | 179 | 207 | 195 | 199 | 2 | -99.0 |
| Polikliniki | 265 | 360 | 349 | 357 | 311 | -12.9 |
| Vituo vya Uchunguzi | 13 | 14 | 13 | 12 | 12 | 0 |
| Vituo vya Uokozi | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 0 |
| **Jumla** | **8,483** | **9,178** | **9,185** | **10,003** | **10,139** | **1.4** |

**Chanzo:** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

**Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa**

53. Mwaka 2024/25, wanachama 221,334 walijiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa - iCHF ikilinganishwa na wanachama 510,040 waliojiunga mwaka 2023/24, sawa na upungufu wa asilimia 56.6. Hii ilitokana na wananchi kusubiri kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote na uhiari wa kujiunga na Mfuko. Katika kipindi hicho, vituo 7,817 vilitoa huduma kwa wanachama wa iCHF ikilinganishwa na vituo 7,334 mwaka 2023/24. Kati ya hivyo, vituo vya umma vilikuwa 7,795, vituo vya mashirika ya dini 20 na vituo binafsi viwili (2). Aidha, vituo vya Serikali vilijumuisha zahanati 6,528, vituo vya afya 1,048, hospitali za halmashauri 184, hospitali za wilaya 6 na hospitali za rufaa za mikoa 29.

54. Mwaka 2024/25, shilingi milioni 3,310.2 zilikusanywa kutokana na michango ya wanachama ikilinganishwa na shilingi milioni 3,587.7 zilizokusanywa mwaka 2023/24, sawa na upungufu wa asilimia 7.7. Hii ilitokana na kupungua kwa idadi ya wanachama waliojiunga na iCHF. Katika kipindi hicho, shilingi milioni 2,160.8 zililipwa kwa watoa huduma ikilinganishwa na shilingi milioni 2,224.4 zilizolipwa mwaka 2023/24.

**Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania**

55. Mwaka 2025, watoa huduma za bima waliosajiliwa na Mamlaka ya Usimamazi wa Shughuli za Bima Tanzania - TIRA waliongezeka kwa asilimia 28.7 na kufikia 2,444 ikilinganishwa na watoa huduma 1,899 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kuimarika kwa usimamizi wa watoa huduma na kuongezeka kwa matumizi ya mifumo ya kidijitali. Aidha,

idadi ya kampuni za bima ziliongezeka na kufikia 37 mwaka 2025 kutoka kampuni 36 mwaka 2024. Vilevile, kampuni za bima mtawanyo ziliendelea kuwa nne (4) na konsotia (consortium) mbili (2) mwaka 2025.

56. Mwaka 2025, mauzo ya bima yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 1,630.0 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,516.3 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 7.5. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za bima na matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma. Aidha, mauzo ya bima za kawaida yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 1,020.0 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 957.3 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 6.5. Vilevile, mauzo ya bima za maisha yaliongezeka kwa asilimia 6.8 na kufikia shilingi bilioni 330.0 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 309.0 mwaka 2024. Katika kipindi hicho, mauzo ya bima ya afya yaliongezeka kwa asilimia 9.3 na kufikia shilingi bilioni 205.0 ikilinganishwa na shilingi bilioni 187.5 mwaka 2024. Kwa upande mwingine, bima ya vyombo vya moto iliendelea kuongoza katika soko la bima kwa kuchangia asilimia 24.7 ya thamani ya mauzo ya bima yote ikifuatiwa na bima za maisha za vikundi asilimia 17.4, bima ya moto asilimia 13.4, bima ya afya asilimia 12.6 na bima ya uhandisi asilimia 5.1, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2.6**.

**Jedwali Na. 2.6: Ada za Bima Zilizoandikishwa (Shilingi Bilioni), Mwaka 2024 - 2025**

| Aina ya Bima | 2024 | Mchango (Asilimia) | 2025 | Mchango (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Bima ya vyombo vya Moto | 380.0 | 25.1 | 402.0 | 24.7 |
| Bima ya Moto | 202.9 | 13.4 | 218.0 | 13.4 |
| Bima ya usafiri wa anga | 59.5 | 3.9 | 65.0 | 4.0 |
| Bima ya Uhandisi | 76.0 | 5.0 | 83.0 | 5.1 |
| Bima ya usafiri wa Baharini | 37.1 | 2.4 | 38.0 | 2.3 |
| Bima zingine | 27.6 | 1.8 | 28.0 | 1.7 |
| Bima ya Ajali | 19.2 | 1.3 | 22.0 | 1.4 |
| Bima ya Dhima | 35.1 | 2.3 | 36.0 | 2.2 |
| Bima ya Wizi | 31.4 | 2.1 | 33.0 | 2.0 |
| Bima ya Dhamana | 39.6 | 2.6 | 41.0 | 2.5 |
| Bima ya Nishati | 4.5 | 0.3 | 5.0 | 0.3 |
| Bima ya Usafirishaji | 6.3 | 0.4 | 7.0 | 0.4 |
| Bima ya Kilimo | 7.8 | 0.5 | 9.0 | 0.6 |
| Bima za Safari | 30.3 | 2.0 | 33.0 | 2.0 |
| **Jumla ya Bima za Kawaida** | **957.3** | **63.1** | **1,020.0** | **62.6** |
| Bima za maisha za Binafsi | 45.1 | 3.0 | 47.0 | 2.9 |
| Bima za maisha za Vikundi | 263.9 | 17.4 | 283.0 | 17.4 |
| **Jumla ya Bima za Maisha** | **309.0** | **20.4** | **330.0** | **20.3** |
| Bima za Afya | 187.5 | 12.4 | 205.0 | 12.6 |
| Takaful | 4.6 | 0.3 | 6.0 | 0.4 |
| Bima mtawanyo | 58.0 | 3.8 | 69.0 | 4.2 |
| **Jumla** | **1,516.4** | **100.0** | **1,630.0** | **100.0** |

**Chanzo**: Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania

57. Mwaka 2025, thamani ya mali za kampuni za bima iliongezeka kwa asilimia 12.6 na kufikia shilingi bilioni 2,633.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,339.9 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za uandikishaji bima na uwekezaji wa kampuni za bima. Aidha, madeni ya kampuni za bima yaliongezeka kwa asilimia 13.9 na kufikia shilingi bilioni 1,699.8 mwaka 2025 ikilinganishwa na madeni ya shilingi bilioni 1,492.6 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na malipo ya madai. Vilevile, thamani halisi ya kampuni za bima iliongezeka kwa asilimia 10.2 na kufikia shilingi bilioni 933.8 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 847.3 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuimarika kwa mitaji ya kampuni na uthabiti wa sekta ya bima.

58. Mwaka 2025, mali za uwekezaji katika sekta ya bima ziliongezeka kwa asilimia 8.9 na kufikia shilingi bilioni 1,567.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,440.1 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarika kwa mapato ya ada za bima na usimamizi wa fedha pamoja na mikakati ya uwekezaji inayolenga vitega uchumi salama na vyenye ukwasi. Aidha, uwekezaji katika hatifungani za Serikali uliongezeka kwa asilimia 9.3 na kufikia shilingi bilioni 470.0 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 430.0 mwaka 2024. Vilevile, uwekezaji katika majengo na ardhi uliongezeka kwa asilimia 7.0 na kufikia shilingi bilioni 175.0 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 163.5 mwaka 2024. Kwa upande mwingine, hisa za kampuni zilizoorodheshwa zilifikia shilingi bilioni 135.0 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 128.0 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 5.5.

59. Mwaka 2025, idadi ya wakata bima na wanufaika iliongezeka na kufikia milioni 26.3 ikilinganishwa na wakata bima na wanufaika milioni 25.9 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa bima pamoja na matumizi ya mifumo ya kidijitali katika utoaji wa huduma za bima. Aidha, madai yaliyopokelewa yaliongezeka kwa asilimia 9.7 na kufikia shilingi bilioni 798.2 mwaka 2025 kutoka shilingi bilioni 727.6 mwaka 2024. Kati ya hayo, madai yaliyolipwa yalifikia shilingi bilioni 577.6 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 545.4 zilizolipwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 5.9. Ongezeko la ulipaji wa madai lilitokana na kuendelea kuimarika kwa mifumo ya usimamizi wa madai, matumizi ya TEHAMA pamoja na maboresho katika taratibu za tathmini na ulipaji wa madai.

**Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania**

60. Mwaka 2025, mtaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania - TADB uliongezeka kwa asilimia 6.3 na kufikia shilingi bilioni 539.42 kutoka shilingi bilioni 507.33 mwaka 2024. Hii ilitokana na juhudi za Serikali kuendelea kukuza mtaji wa TADB ili kuwafikia wakulima, wavuvi na wafugaji. Aidha, rasilimali za benki ziliongezeka kwa asilimia 41.3 na kufikia shilingi bilioni 1,296.52 mwaka 2025 kutoka shilingi bilioni 917.41 mwaka 2024. Vilevile, thamani ya mikopo iliyotolewa na TADB iliongezeka kwa asilimia 50.1 na

kufikia shilingi bilioni 429.74 mwaka 2025 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 286.38 iliyotolewa mwaka 2024. Kwa upande mwingine, TADB kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo ilitoa dhamana kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 213.4 mwaka 2025 ikilinganishwa na dhamana kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 130.79 iliyotolewa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 63.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uhitaji wa mikopo katika sekta ya kilimo inayotolewa na benki washirika.

61. Mwaka 2025, TADB ilipata faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 35.40 ikilinganishwa na shilingi bilioni 24.68 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 43.4. Hii ilitokana na ongezeko la utoaji wa mikopo, kuboreshwa kwa ufuatiliaji na urejeshwaji wa mikopo pamoja na kupungua kwa gharama za uendeshaji. Katika kipindi hicho, kiwango cha mikopo chechefu kilipungua na kufikia asilimia 2.6 ikilinganishwa na asilimia 2.8 mwaka 2024. Aidha, kiwango cha mikopo chechefu kipo chini ya ukomo wa asilimia 5.0 uliowekwa na Benki Kuu ya Tanzania.

**Benki ya Biashara Tanzania**

62. Mwaka 2025, amana za Benki ya Biashara Tanzania - TCB ziliongezeka kwa asilimia 27.5 na kufikia shilingi bilioni 1,662.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,303.4 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilitokana na maboresho yaliyofanyika katika huduma za fedha na uanzishwaji wa huduma mpya, ikiwemo hatifungani ya TCB Stawi, huduma za benki kwa watanzania walio nje ya nchi, kadi za Visa na kadi ya malipo ya tiketi za SGR. Aidha, idadi ya wateja iliongezeka kwa asilimia 12.9 na kufikia 1,031,730 mwaka 2025 ikilinganishwa na wateja 914,159 mwaka 2024.

63. Hadi Desemba 2025, mikopo yenye thamani shilingi bilioni 1,472.2 iliyotolewa ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,137.0 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 29.5. Hii ilichangiwa na maboresho katika utaratibu wa utoaji na urejeshwaji wa mikopo. Katika kipindi hicho, kiwango cha mikopo chechefu kiliongezeka na kufikia asilimia 3.5 ikilinganishwa na asilimia 3.4 mwaka 2024. Pamoja na kuongezeka kidogo, kiwango hicho kiliendelea kuwa chini ya uwiano wa ukomo wa asilimia 5.0 uliowekwa na Benki Kuu ya Tanzania.

64. Mwaka 2025, uwekezaji wa TCB katika hatifungani za Serikali uliongezeka kwa asilimia 56.9 na kufikia shilingi bilioni 328.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 209.2 mwaka 2024. Aidha, TCB ilipata faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 47.6. mwaka 2025 ikilinganishwa na faida ya shilingi bilioni 31.9 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 49.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mikopo na huduma zilizotolewa. Kwa upande mwingine, thamani ya rasilimali za benki iliongezeka kwa asilimia 30.8 na kufikia shilingi

bilioni 2,272.8 mwaka 2025 kutoka shilingi bilioni 1,738.0 mwaka 2024. Ongezeko la rasilimali za benki lilichangiwa na ukuaji wa mikopo.

**Soko la Bidhaa Tanzania**

65. Mwaka 2025, mauzo ya mazao na madini ya vito kupitia Soko la Bidhaa Tanzania - TMX yaliongezeka na kufikia tani 1,126,107.2 zenye thamani ya shilingi bilioni 2,944.78 ikilinganishwa na mauzo ya tani 716,186.5 za mazao na madini ya vito zenye thamani ya shilingi bilioni 2,624.58 zilizouzwa mwaka 2024 (**Jedwali Na 2.7**). Hii ilitokana na kuongezeka kwa bidhaa zilizouzwa, idadi ya wanunuzi pamoja na bei ya baadhi ya bidhaa. Aidha, mapato ya ushuru wa halmashauri kutokana na mauzo yaliongezeka kwa asilimia 11.4 na kufikia shilingi bilioni 60.00 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 53.87 zilizokusanywa mwaka 2024.

**Jedwali Na. 2.7: Bidhaa Zilizouzwa Kupitia TMX, Mwaka 2024 - 2025**

| Bidhaa | 2024 | | 2025 | |
|---|---|---|---|---|
| | Kiasi (Kg) | Thamani (Shilingi) | Kiasi (Kg) | Thamani (Shilingi) |
| Korosho | 402,956,008 | 1,451,347,767,933 | 435,237,488 | 1,291,415,502,447 |
| Kakao | 9,096,727 | 195,574,954,107 | 15,049,170 | 241,256,304,804 |
| Chai | 629,642 | 1,139,974,294 | 329,460 | 938,471,560 |
| Choroko | 104,557 | 126,378,786 | 23,966,009 | 40,211,926,992 |
| Madini ya vito | 176.259 | 1,219,949,020 | 101 | 1,597,978,867 |
| Ufuta | 145,886,611 | 535,678,706,743 | 220,753,600 | 617,452,642,479 |
| Mbaazi | 100,082,095 | 198,473,280,306 | 270,739,556 | 286,435,430,773 |
| Dengu | 21,508,219 | 42,258,331,595 | 131,424,481 | 160,876,822,670 |
| Soya | 1,204,201 | 1,812,095,039 | 1,195,739 | 1,729,468,821.70 |
| Kahawa | 34,718,288 | 196,945,963,470 | 27,411,620 | 151,432,724,282 |
| **Jumla** | **716,186,524** | **2,624,577,401,293** | **1,126,107,224** | **2,793,347,273,696** |

**Chanzo:** Soko la Bidhaa Tanzania

**Jedwali Na. 24: MWENENDO WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA**

| | Kipindi Kilichoishia Desemba (Shilingi Bilioni) | | | | | | | Badiliko 2024 - 2025 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Kiasi | Asilimia |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)** | **13,325.1** | **14,321.7** | **17,625.5** | **18,948.2** | **20,601.6** | **22,905.5** | **30,199.0** | **7,293.5** | **31.8** |
| Amana za Akiba na za muda maalum | 7,955.1 | 8,711.0 | 9,462.8 | 11,430.7 | 13,400.1 | 14,234.2 | 17,944.2 | 3,710.0 | 26.1 |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)** | **21,280.3** | **23,032.6** | **27,088.8** | **30,378.9** | **34,001.7** | **37,139.7** | **48,143.2** | **11,003.5** | **29.6** |
| Amana za fedha za kigeni | 7,032.9 | 6,887.9 | 7,469.7 | 8,201.1 | 10,000.8 | 11,765.3 | 13,381.1 | 1,615.8 | 13.7 |
| **Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)** | **28,313.1** | **29,920.6** | **34,558.0** | **38,580.0** | **44,002.6** | **48,905.0** | **61,524.3** | **12,619.3** | **25.8** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za kigeni (Net foreign assets)** | **12,034.5** | **10,722.5** | **13,966.0** | **9,437.5** | **11,302.4** | **13,558.2** | **15,283.5** | **1,725.2** | **12.7** |
| Rasilimali halisi katika fedha za kigeni Benki Kuu | 12,063.1 | 10,308.8 | 13,219.1 | 10,732.8 | 12,079.3 | 11,863.4 | 13,707.3 | 1,843.9 | 15.5 |
| Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye mabenki | -28.5 | 413.8 | 746.8 | -1,295.3 | -776.9 | 1,694.8 | 1,576.1 | -118.7 | -7.0 |
| **Rasilimali halisi katika fedha za ndani (Net domestic assets)** | **16,278.6** | **19,198.0** | **20,592.1** | **29,142.5** | **32,700.2** | **35,346.8** | **46,240.8** | **10,894.0** | **30.8** |
| **Madai rasmi ya ndani** | **23,589.3** | **26,139.6** | **30,030.5** | **37,557.3** | **43,411.5** | **47,559.0** | **57,178.6** | **9,619.6** | **20.2** |
| Madai halisi kwa serikali kuu | 3,893.9 | 5,831.3 | 7,686.4 | 10,184.8 | 11,353.9 | 11,461.6 | 12,575.5 | 1,113.9 | 9.7 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 19,695.4 | 20,308.3 | 22,344.1 | 27,372.5 | 32,057.6 | 36,097.4 | 44,603.1 | 8,505.6 | 23.6 |
| Amana za Serikali zilizopo Benki Kuu na Benki za Biashara | 4,514.1 | 6,767.7 | 7,089.0 | 8,076.2 | 11,445.2 | 12,316.9 | 11,965.6 | -351.2 | -2.9 |
| Mikopo kwa serikali kuu | 8,408.0 | 12,599.1 | 14,775.4 | 18,261.0 | 22,799.1 | 23,778.5 | 24,785.8 | 1,007.3 | 4.2 |
| Rasilimali nyinginezo (Other Items Net) | -7,310.7 | -6,941.6 | -9,438.4 | -8,414.8 | -10,711.3 | -12,212.2 | -10,919.3 | 1,292.9 | -10.6 |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 25: VIWANGO VYA UKUAJI WA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA**

| | Kipindi kilichoishia Desemba (Asilimia) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)** | **13.7** | **7.5** | **23.1** | **7.5** | **8.7** | **11.2** | **31.8** |
| Amana za Akiba na za muda maalum | 8.7 | 9.5 | 8.6 | 20.8 | 17.2 | 6.2 | 26.1 |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)** | **11.8** | **8.2** | **17.6** | **12.1** | **11.9** | **9.2** | **29.6** |
| Amana za fedha za kigeni | 3.7 | -2.1 | 8.4 | 9.8 | 21.9 | 17.6 | 13.7 |
| **Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)** | **9.6** | **5.7** | **15.5** | **11.6** | **14.1** | **11.1** | **25.8** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za kigeni (Net foreign assets)** | **13.2** | **-10.9** | **30.2** | **-32.4** | **19.8** | **20.0** | **12.7** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za ndani (Net domestic assets)** | **7.1** | **17.9** | **7.3** | **41.5** | **12.2** | **8.1** | **30.8** |
| Madai rasmi ya ndani | 6.2 | 10.8 | 14.9 | 25.1 | 15.6 | 9.6 | 20.2 |
| Madai halisi kwa serikali kuu | -13.1 | 49.8 | 31.8 | 32.5 | 11.5 | 0.9 | 9.7 |
| Mikopo kwa sekta Binafsi | 11.1 | 3.1 | 10.0 | 22.5 | 17.1 | 12.6 | 23.6 |
| Rasilimali nyinginezo (Other Items Net) | 4.2 | -5.0 | 36.0 | -10.8 | 27.3 | 14.0 | -10.6 |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 26: MWENENDO WA VIWANGO VYA UBADILISHAJI KATI YA SHILINGI NA DOLA YA MAREKANI, MWAKA 2019 - 2025**

| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Shiling/Dola (Mwisho wa mwaka) | 2,300.0 | 2,309.8 | 2,307.4 | 2,320.2 | 2,516.0 | 2,420.8 | 2,452.8 |
| Badiliko la thamani ya shilingi (Asilimia) | 0.4 | 0.4 | -0.1 | 0.6 | 8.4 | -3.8 | 1.3 |
| Shilingi/Dola (Wastani wa mwaka) | 2,299.8 | 2,305.6 | 2,309.2 | 2,314.5 | 2,395.7 | 2,610.5 | 2,549.8 |
| Badiliko la wastani wa thamani ya shilingi (Asilimia) | 1.1 | 0.25 | 0.2 | 0.2 | 3.5 | 9.0 | (2.3) |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 27: MWENENDO WA AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA, MWAKA 2019 - 2025**

| | Kipindi kilichoishia Desemba (Shilingi Bilioni) | | | | | | | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** | **2025** |
| Amana za Sekta Binafsi | | | | | | | | |
| Amana za Hundi (Zinazohamishika) | 7,866.5 | 8,121.4 | 9,894.0 | 11,909.1 | 12,976.1 | 14,695.1 | 21,706.7 | 47.7 |
| Amana za Akiba na za Muda Maalum | 7,750.4 | 8,519.4 | 9,350.8 | 11,240.7 | 13,037.2 | 13,999.0 | 17,944.2 | 28.2 |
| Amana za fedha za kigeni | 6,160.6 | 6,427.1 | 7,146.0 | 7,575.1 | 9,331.7 | 11,358.6 | 13,381.1 | 17.8 |
| **Jumla** | **21,777.5** | **23,067.9** | **26,390.7** | **30,724.9** | **35,345.0** | **40,052.8** | **53,032.0** | **32.4** |
| Amana za Serikali | 981.3 | 652.9 | 422.5 | 704.4 | 1,156.0 | 1,413.0 | 1,344.9 | -4.8 |
| **Jumla ya Amana zote** | **22,758.9** | **23,720.7** | **26,813.2** | **31,429.4** | **36,501.1** | **41,465.7** | **54,376.9** | **31.1** |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 28: VIWANGO VYA WASTANI WA RIBA, MWAKA 2019 - 2025**

| Aina ya Riba | Wastani (Asilimia) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
| Riba ya Benki kuu (Discount rate) | 7.00 | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 8.38 | 8.38 |
| Riba katika soko la fedha kati ya benki za biashara kwa ujumla | 5.13 | 4.50 | 4.44 | 4.53 | 5.37 | 7.50 | 7.26 |
| Riba za dhamana za serikali kwa ujumla | 7.71 | 4.42 | 4.78 | 4.64 | 7.32 | 10.67 | 8.38 |
| Siku 35 | 3.47 | 2.37 | 2.60 | 2.25 | 4.20 | 5.99 | 6.26 |
| Siku 91 | 4.17 | 2.88 | 2.74 | 2.80 | 5.36 | 6.94 | 7.11 |
| Siku 182 | 5.07 | 3.32 | 3.20 | 3.47 | 6.37 | 8.00 | 7.50 |
| Siku 364 | 8.04 | 4.68 | 4.85 | 4.79 | 7.69 | 10.72 | 8.42 |
| **Riba za Hatifungani** | | | | | | | |
| Miaka miwili | 11.45 | 8.14 | 7.67 | 6.56 | 9.75 | 11.64 | 11.64 |
| Miaka mitano | 12.56 | 11.24 | 9.19 | 9.04 | 9.89 | 10.67 | 12.45 |
| Miaka saba | 13.09 | 11.48 | 10.09 | 9.58 | 9.71 | 9.71 | 9.71 |
| Miaka kumi | 15.04 | 12.51 | 11.59 | 10.63 | 11.35 | 12.63 | 13.63 |
| Miaka kumi na tano | 15.52 | 14.05 | 13.59 | 11.7 | 11.95 | 14.73 | 14.21 |
| Miaka ishirini | 17.35 | 15.79 | 15.27 | 12.22 | 12.96 | 15.30 | 14.39 |
| Miaka ishirini na tano | | | 16.06 | 12.76 | 13.46 | 15.55 | 14.62 |
| **Riba za Amana** | | | | | | | |
| Amana za akiba | 2.44 | 2.34 | 1.95 | 1.69 | 1.86 | 2.80 | 2.89 |
| Amana za muda maalum kwa ujumla | 7.25 | 6.7 | 6.85 | 7.11 | 7.07 | 7.85 | 8.40 |
| Amana za Mwaka mmoja | 8.8 | 8.28 | 8.32 | 8.53 | 8.65 | 9.17 | 9.58 |
| **Riba za Mikopo** | | | | | | | |
| Mikopo kwa ujumla | 16.97 | 16.66 | 16.59 | 16.18 | 15.75 | 15.47 | 15.26 |
| Mikopo ya muda mfupi hadi mwaka mmoja | 16.69 | 15.73 | 16.43 | 16.79 | 16.53 | 15.82 | 15.69 |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

## SURA YA 3

## FEDHA ZA SERIKALI

**Utangulizi**

66. Katika bajeti ya mwaka 2025/26 maeneo mahsusi yaliyopewa kipaumbele ni pamoja na kuendelea: kutekeleza na kukamilisha miradi ya kielelezo na ya kimkakati; kuimarisha sekta za uzalishaji zenye matokeo chanya katika kukuza uchumi; kuimarisha rasilimali watu hususan katika sekta za huduma za jamii; na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini ili kuvutia ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. Aidha, sera za bajeti za mwaka 2025/26 zililenga kuongeza makusanyo ya mapato kwa kuendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo: kuimarisha na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini; kupanua wigo wa kodi; na kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato. Kwa upande wa matumizi, sera zililenga kuendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria mbalimbali, ikiwemo Sheria ya Bajeti, Sura 439, Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410.

67. Shabaha za uchumi jumla katika bajeti ya mwaka 2025/26 zilikuwa: kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa na kufikia asilimia 6.0 mwaka 2025 kutoka ukuaji halisi wa asilimia 5.5 mwaka 2024; kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja wa wastani wa asilimia 3.0 - 5.0 katika muda wa kati; mapato ya ndani kufikia asilimia 16.7 ya Pato la Taifa mwaka 2025/26 ikilinganishwa na makadirio ya asilimia 15.8 mwaka 2024/25; mapato ya kodi kufikia asilimia 13.3 ya Pato la Taifa mwaka 2025/26 kutoka makadirio ya asilimia 12.8 mwaka 2024/25; kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

68. Tathmini ya awali iliyofanyika inaonesha mwenendo wa kuridhisha kwa baadhi ya malengo na shabaha hizo na tathmini kamili itafanyika baada ya mwaka wa fedha kukamilika ili kubainisha hali ya ufikiaji wa malengo hayo. Shabaha zilizoainishwa zilizingatia misingi mbalimbali ikiwemo: kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji na biashara; kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, vita, magonjwa ya mlipuko na mafuriko; uchumi imara wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa; kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini; na uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

69. Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2025/26 ilikuwa shilingi bilioni 56,490.3. Katika bajeti hiyo, mapato ya ndani yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 40,466.1 na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo

shilingi bilioni 1,069.9. Aidha, mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 14,954.3 ilikadiriwa kugharamia nakisi ya bajeti ambapo shilingi bilioni 6,278.2 ni mikopo ya ndani na shilingi bilioni 8,676.1 ni mikopo kutoka nje ya nchi.

70. Kwa upande wa matumizi, Serikali iliidhinishiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania shilingi bilioni 56,490.3, ambapo shilingi bilioni 9,172.0 zilitengwa kwa ajili ya stahiki za watumishi na michango ya pensheni (Serikali Kuu); shilingi bilioni 5,576.1 kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa na huduma; malipo ya riba za mikopo shilingi bilioni 6,493.7; na ruzuku (subsidies & transfers) kwa taasisi za Serikali, mashirika ya umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi trilioni 22,052.9. Aidha, Serikali ilitenga shilingi trilioni 7,715.3 kugharamia malipo ya mtaji kwa deni la ndani na nje.

**Mwenendo wa Makusanyo**

**Mapato**


71. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, mapato (ikijumuisha misaada) yalifikia shilingi bilioni 31,482.6, sawa na asilimia 103.2 ya lengo la kipindi hicho na ukuaji wa asilimia 18.0 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2024/25. Katika kipindi hicho, mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 25,405.4, sawa na ufanisi wa asilimia 106.7 na ukuaji wa asilimia 19.7 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2024/25 (**Jedwali Na. 3.1**). Ongezeko hilo lilitokana na kuimarishwa kwa ufuatiliaji na usimamizi pamoja na kuongezeka kwa uhiari wa kulipa kodi kufuatia kuimarisha mahusiano na walipakodi. Katika kipindi hicho, shilingi bilioni 712.1 zilipokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, sawa na asilimia 99.1 ya lengo la kipindi hicho. Kupungua kwa misaada ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2024/25 kulitokana na mabadiliko ya sera za nchi wahisani kutokana na mdororo wa shughuli za kiuchumi pamoja na mabadiliko ya uongozi wa kisiasa na mifumo ya uzalishaji wa bidhaa na huduma. Mwenendo wa Mapato (ikijumuisha misaada) na mchanganuo wa makusanyo ya mapato kwa mwezi Julai 2025 hadi Machi 2026 ni kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 3.1 na Kielelezo Na. 3.2**.

**Jedwali Na. 3.1: Mwenendo wa Mapato Ikijumuisha Misaada (Shilingi Bilioni)**


| | Julai - Machi | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2024/25 | 2025/26 | | Ufanisi | Ukuaji |
| | Halisi | Makadirio | Halisi | (Asilimia) | (Asilimia) |
| **Mapato** | **26,669.4** | **30,494.9** | **31,482.6** | **103.2** | **18.0** |
| **Mapato ya Ndani** | **25,669.8** | **29,776.2** | **30,770.5** | **103.3** | **19.9** |
| **Mapato Yanayokusanywa na TRA** | **22,291.7** | **25,320.7** | **26,555.0** | **104.9** | **19.1** |
| Kodi | 21,223.3 | 23,799.8 | 25,405.4 | 106.7 | 19.7 |
| Yasiyo ya Kodi | 1,068.4 | 1,520.9 | 1,149.6 | 75.6 | 7.6 |
| **Mapato Yasiyo ya Kodi** | **3,378.1** | **4,455.6** | **4,215.5** | **94.6** | **24.8** |
| Wizara na Idara Zinazojitegemea | 1,678.9 | 2,195.0 | 2,212.3 | 100.8 | 31.8 |
| Ofisi ya Msajili wa Hazina | 658.3 | 983.9 | 780.0 | 79.3 | 18.5 |
| Halmashauri | 1,040.9 | 1,276.7 | 1,223.2 | 95.8 | 17.5 |
| **Misaada** | **999.6** | **718.7** | **712.1** | **99.1** | **(28.8)** |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

**Kielelezo Na. 3.1: Mwenendo wa Mapato Ikijumuisha Misaada (Shilingi Bilioni), Julai 2025 - Machi 2026**





**Kielelezo Na. 3.2: Mchanganuo wa Mapato (Shilingi Bilioni), Julai 2025 - Machi 2026**




**Mikopo Nafuu**

72. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, mikopo nafuu iliyopokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 4,474.0, sawa na asilimia 119.0 ya makadirio ya kipindi hicho ya shilingi bilioni 3,673.0 (**Kielelezo Na. 3.3**). Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 1,143.6 zilikuwa ni za mikopo nafuu ya kibajeti, shilingi bilioni 3,268.4 mikopo ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 61.9 mikopo kwa ajili ya mifuko ya kisekta (basket fund).

**Kielelezo Na. 3.3: Mwenendo wa Mikopo Nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (Shilingi Bilioni), Julai 2025 - Machi 2026**




**Mikopo Yenye Masharti ya Kibiashara ya Ndani na Nje**


73. Mwaka 2025/26, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 8,168.7 kutoka vyanzo vya ndani na nje vyenye masharti ya kibiashara. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Serikali ilikopa kiasi cha shilingi bilioni 4,312.6 kutoka vyanzo vya ndani, sawa na asilimia 77.8 ya lengo la mwaka 2025/26 la kukopa shilingi bilioni 5,539.7. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 2,132.7 zilitumika kwa ajili ya kulipia hati fungani na dhamana za Serikali zilizoiva na shilingi bilioni 2,180.0 kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwa upande wa vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibiashara, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 2,629.01 kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo mwaka 2025/26. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Serikali ilikopo shilingi bilioni 1,590.34 kutoka vyanzo hivyo, sawa na asilimia 60.5 ya kiasi kilichopangwa kukopwa mwaka 2025/2026. Aidha, katika kipindi hicho, Serikali imetumia jumla ya shilingi bilioni 2,174.1 kwa ajili ya kugharamia ulipaji wa mikopo ya nje iliyoiva.

**Mwenendo wa Matumizi**

74. Mwaka 2025/26, utekelezaji wa bajeti ulizingatia maeneo ya vipaumbele ikiwemo ugharamiaji wa mishahara, deni la Serikali, shughuli za uchaguzi mkuu, mahitaji ya sekta ya hifadhi ya jamii na ujenzi wa miundombinu ya nishati, usafiri na usafirishaji ili kuchochea ukuaji wa uchumi na kuimarisha ustawi wa jamii. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, matumizi ya Serikali bila kujumuisha malipo ya mtaji wa deni yalikuwa shilingi bilioni 37,459.7 sawa na asilimia 103.3 ya lengo. Kati ya kiasi hicho: mishahara na stahiki za watumishi ilikuwa shilingi bilioni 6,389.8; malipo ya riba shilingi bilioni 4,541.3;

gharama za bidhaa na huduma shilingi bilioni 6,395.3; uwekezaji katika mali zisizo za kifedha 2,745.4; na shilingi bilioni 17,387.8 kwa ajili ya ruzuku, michango na gharama nyingine. Mwenendo wa matumizi katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 3.4.**

**Kielelezo Na: 3.4: Mwenendo wa Matumizi (Shilingi Bilioni), Julai 2025 - Machi 2026**




**Deni la Serikali**

75. Hadi Machi 2026, deni la Serikali lilifikia shilingi bilioni 114,342.1 kutoka shilingi bilioni 104,931.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2025, sawa na ongezeko la asilimia 8.97. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 38,447.9 na deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 75,894.2. Ongezeko la deni lilitokana na Serikali kuendelea kupokea mikopo mipya na ya zamani kutoka vyanzo vya ndani na nje kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli ya kisasa, viwanja vya ndege, na miradi ya umeme, elimu na afya.

**Deni la Nje**

76. Hadi Machi 2026, deni la Serikali la nje lilifikia shilingi bilioni 75,894.23 ikilinganishwa na shilingi bilioni 70,675.71 katika kipindi kama hicho mwaka 2025, sawa na ongezeko la asilimia 7.4. Aidha, mashirika ya fedha ya kimataifa yaliendelea kuongoza kwa kuchangia asilimia 68.9 ya deni lote la nje hadi Machi 2026 ikilinganishwa na asilimia 67.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Benki za biashara zilichangia asilimia 25.6 na Washirika wa Maendeleo walichangia asilimia 5.4 ya deni lote la nje (**Jedwali Na. 3.2**).

**Jedwali Na. 3.2: Deni la Nje kwa Wakopeshaji (Shilingi Bilioni), Mwaka 2024 - 2026**


| Taasisi | Machi 2024 | Mchango (asilimia) | Machi 2025 | Mchango (asilimia) | Machi 2026 | Mchango (asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mashirika ya Fedha | 41,044.13 | 67.3 | 47,889.52 | 67.8 | 52,327.27 | 68.9 |
| Washirika wa Maendeleo | 3,543.74 | 5.8 | 3,779.37 | 5.3 | 4,102.99 | 5.4 |
| Benki za kibiashara | 16,366.60 | 26.9 | 19,006.82 | 26.9 | 19,463.98 | 25.6 |
| **Jumla** | **60,954.47** | **100.0** | **70,675.71** | **100.0** | **75,894.23** | **100.0** |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

**Deni la Ndani**

77. Hadi Machi 2026, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 38,447.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 34,255.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2025, sawa na ongezeko la asilimia 12.2. Katika kipindi hicho, mikopo ya hatifungani iliendelea kuwa sehemu kubwa ya deni la ndani ikichangia asilimia 68.8 ya deni lote la ndani. Aidha, dhamana za Serikali za muda mfupi zilikuwa asilimia 4.1, hati fungani maalum asilimia 13.4 na madeni mengine asilimia 13.7 (**Kielelezo Na. 3.5**).

**Kielelezo Na. 3.5: Mwenendo wa Deni la Ndani (Shilingi Bilioni), Mwaka 2021 - 2026**




78. Hadi Machi 2026, benki za biashara ziliendelea kuongoza kwa kuhodhi asilimia 28.4 ya deni la ndani ikilinganishwa na asilimia 29.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2025 ikifuatiwa na mifuko ya hifadhi ya jamii iliyohodhi asilimia 27.2. Aidha, mchango wa watu binafsi katika dhamana za Serikali uliongezeka na kufikia asilimia 13.6 Machi 2026 kutoka asilimia 8.9. Hii ilichangiwa na kuendelea kutoloewa kwa elimu ya fedha na uhamasishaji kwa umma (**Jedwali Na. 3.3**).

**Jedwali Na. 3.3: Deni la Ndani kwa Wakopeshaji (Shilingi Bilioni), Mwaka 2024 - 2026**

| Taasisi | Machi 2024 | Mchango (Asilimia) | Machi 2025 | Mchango (Asilimia) | Machi 2026 | Mchango (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Benki za Biashara | 10,170.0 | 33.1 | 9,948.4 | 29.0 | 10,925.8 | 28.4 |
| Mifuko ya Jamii | 8,211.8 | 26.7 | 9,091.5 | 26.5 | 10,463.9 | 27.2 |
| Benki Kuu | 6,513.4 | 21.2 | 7,439.7 | 21.7 | 7,724.0 | 20.1 |
| Watu binafsi | 2,733.6 | 8.9 | 3,918.9 | 11.4 | 5,148.0 | 13.4 |
| Kampuni za Bima | 1,844.8 | 6.0 | 1,845.5 | 5.4 | 1,997.1 | 5.2 |
| Taasisi za Fedha | 686.4 | 2.2 | 1,178.5 | 3.4 | 1,318.1 | 3.4 |
| Mashirika Madogo | 593.8 | 1.9 | 700.6 | 2.0 | 738.6 | 1.9 |
| Taasisi za Kigeni | - | - | 132.3 | 0.4 | 132.3 | 0.3 |
| **Jumla** | **30,753.8** | **100.0** | **34,255.4** | **100.0** | **38,447.9** | **100.0** |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha

**Uhimilivu wa Deni**

79. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Novemba 2025 ililenga kubaini uwezo wa Serikali kuhimili deni katika kipindi cha muda mfupi, kati na mrefu, pamoja na kuwa na ukopaji endelevu bila kuathiri ukuaji wa uchumi. Tathmini hiyo hufanyika kwa kuzingatia vigezo vya uhimilivu, ikiwemo uwiano wa deni halisi kwa Pato la Taifa; uwiano wa deni halisi kwa malipo ya nje; na uwiano wa malipo ya deni kwa mapato ya ndani na mapato yatokanayo na mauzo ya nje.

80. Kwa mujibu wa tathmini hiyo, deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda wa kati na mrefu na viashiria vya deni vilionesha kuwa mwaka 2025/26: thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 24.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 123.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180; ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato yatokanayo na mauzo ya nje ni asilimia 12.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 15; na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani ni asilimia 15.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 18. Kwa upande wa viashiria vya deni la nje na ndani, thamani ya sasa ya deni kwa Pato la Taifa ni asilimia 39.6 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55 (**Jedwali Na. 3.4**).

**Jedwali Na. 3.4: Mwenendo wa Viashiria vya Deni la Serikali**

| **Viashiria vya Deni la Nje** | **2025/26** | **2026/27** | **2027/28** | **2028/29** | **2029/30** | **2030/31** | **2035/36** | **Ukomo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Deni (PV)/pato la Taifa | 24.4 | 23.6 | 22.4 | 21.1 | 20 | 19.5 | 18 | 40 |
| Deni (PV)/uuzaji wa bidhaa nje | 123.1 | 123.8 | 119.3 | 114.3 | 110.4 | 108.2 | 103 | 180 |
| Ulipaji wa deni la nje/Uuzaji wa bidhaa | 12.8 | 12.2 | 13.7 | 13.3 | 13.1 | 12 | 10.2 | 15 |
| Ulipaji wa deni /Mapato ya ndani | 15.4 | 13.8 | 15.1 | 14.3 | 13.9 | 12.9 | 10.6 | 18 |
| **Viashiria vya Deni la Nje na Ndani** | **2025/26** | **2026/27** | **2027/28** | **2028/29** | **2029/30** | **2030/31** | **2035/36** | **Ukomo** |
| Deni (PV)/ Pato la Taifa | 39.6 | 38.6 | 36.9 | 35.9 | 34.8 | 34.6 | 34.7 | 55 |
| Deni (PV)/ Mapato ya ndani | 233.4 | 225.6 | 214.8 | 208.2 | 202.8 | 205.6 | 205.8 | - |
| Ulipaji wa deni/ Mapato ya ndani | 45.2 | 32.9 | 34.1 | 30.8 | 31.4 | 32.9 | 31.2 | - |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha

**Uwezo wa Nchi Kukopa na Kulipa Madeni katika Masoko ya Kimataifa**

81. Februari 2026, kampuni ya *Moody's Investors Services* ilifanya mapitio ya uchumi wa Tanzania ili kubaini uwezo wa nchi kukopesheka. Katika mapitio hayo, Tanzania iliendelea kubaki katika daraja la B1 ikiwa ni mtazamo thabiti (Stable Outlook) kama ilivyokuwa Machi 2025. Kwa upande mwingine, Kampuni ya Fitch Ratings ilifanya mapitio kama hayo Machi 2026 na kuipa Tanzania alama ya B+ ikiwa na mtazamo thabiti (Stable Outlook) kama ilivyokuwa mwaka 2025. Hii inatokana na kuendelea kuwepo kwa misingi imara ya uchumi, ikiwemo ukuaji Pato la Taifa, uthabiti wa mfumuko wa bei, na deni la Serikali himilivu. Aidha, matokeo haya yanaimarisha imani ya wawekezaji wa ndani na nje kuhusu uthabiti wa uchumi na uwezo wa Serikali kusimamia deni na hivyo kuwezesha kupunguza gharama za kukopa katika masoko ya kimataifa na kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.


**Jedwali Na. 29: MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI**

**Shilingi Milioni**

| | 2022/23 Halisi | 2023/24 Halisi | 2024/25 Halisi | 2025/26 Bajeti | 2025/26 Halisi Hadi Machi | 2025/26 Matarajio Hadi Juni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| A. MAPATO YA NDANI (yakijumuisha Halmashauri) | **26,277,887.1** | **29,829,894.6** | **34,845,867.4** | **40,466,131.4** | **30,770,524.3** | **41,027,365.7** |
| MAPATO YA NDANI | 25,256,847.8 | 28,683,341.7 | 33,408,589.5 | 38,785,624.7 | 29,547,275.7 | 39,396,367.6 |
| 1. Mapato yatokanayo na Kodi | 21,411,398.9 | 24,760,798.4 | 28,777,081.1 | 32,175,999.8 | 25,405,443.5 | 33,873,924.7 |
| Ushuru wa Forodha na Excise Duty | 4,583,909.9 | 5,351,281.6 | 6,074,692.4 | 6,718,161.7 | 5,263,966.1 | 7,018,621.5 |
| Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) | 7,066,881.5 | 7,594,384.7 | 9,329,061.5 | 10,339,078.6 | 7,645,919.5 | 10,194,559.3 |
| Bidhaa toka nje | 3,639,577.6 | 3,748,862.6 | 4,652,263.7 | 4,973,448.9 | 3,926,746.4 | 5,235,661.9 |
| Bidhaa za ndani | 3,427,304.0 | 3,845,522.2 | 4,676,797.8 | 5,365,629.7 | 3,719,173.1 | 4,958,897.4 |
| Kodi ya Mapato | 7,760,301.5 | 9,159,412.6 | 10,557,007.1 | 11,367,876.5 | 9,741,362.2 | 12,988,482.9 |
| Kodi nyingine | 3,073,133.2 | 3,718,162.4 | 4,342,799.2 | 4,887,699.8 | 3,647,878.7 | 4,863,838.3 |
| Marejesho (Refunds Accounts) | (1,072,827.2) | (1,062,443.0) | (1,526,479.0) | (1,136,816.9) | (893,683.0) | (1,191,577.3) |
| 2. Mapato yasiyotokana na Kodi | 3,845,448.9 | 3,922,543.3 | 4,631,508.3 | 6,609,624.9 | 4,141,832.2 | 5,522,442.9 |
| 3. Mapato ya Halmashauri | 1,021,039.3 | 1,146,552.9 | 1,437,277.9 | 1,680,506.8 | 1,223,248.5 | 1,630,998.1 |
| B. JUMLA YA MATUMIZI | **34,445,838.0** | **36,567,630.8** | **42,077,119.1** | **48,774,989.1** | **35,629,761.8** | **48,774,251.4** |
| 1. Matumizi ya Kawaida | 20,475,131.8 | 21,931,209.5 | 26,674,396.5 | 31,281,255.8 | 23,028,488.7 | 31,420,651.5 |
| 2. Matumizi ya Maendeleo | 13,970,706.2 | 14,636,421.3 | 15,402,722.6 | 17,493,733.4 | 12,601,273.1 | 17,353,599.8 |
| Fedha za ndani | 12,259,082.3 | 11,182,316.4 | 12,715,893.8 | 12,117,828.4 | 9,925,069.1 | 12,712,761.6 |
| Fedha za nje | 1,711,623.9 | 3,454,104.9 | 2,686,828.7 | 5,375,904.9 | 2,676,204.0 | 4,640,838.2 |
| C. NAKISI/SALIO (A-B) | **(8,167,950.9)** | **(6,737,736.2)** | **(7,231,251.7)** | **(8,308,857.7)** | **(4,859,237.5)** | **(7,746,885.7)** |
| D. KUZIBA NAKISI | **8,167,950.9** | **6,737,736.2** | **7,231,251.7** | **8,308,858.7** | **4,859,237.5** | **7,746,885.7** |
| 1. Fedha kutoka nje | 3,681,040.7 | 4,671,036.5 | 4,287,844.8 | 6,094,746.9 | 2,992,889.0 | 4,840,254.0 |
| Misaada | 506,327.7 | 634,687.6 | 880,051.5 | 925,088.1 | 712,072.9 | 919,430.5 |
| Basket support | 90,052.5 | 40,312.1 | 73,278.2 | 80,624.2 | 68,887.9 | 77,483.6 |
| Mikopo ya uagizaji bidhaa/OGL | 1,851,237.4 | 2,013,708.2 | 2,335,248.4 | 2,510,536.7 | 1,143,646.0 | 2,040,872.3 |
| Mikopo ya miradi | 1,115,243.7 | 2,892,901.4 | 1,786,465.9 | 4,339,192.6 | 1,895,243.3 | 3,188,889.0 |
| Mikopo ya masharti ya kibiashara | 3,011,725.4 | 2,101,240.6 | 2,410,773.6 | 2,629,011.8 | 1,347,180.8 | 2,630,688.2 |
| Kulipia madeni ya nje (Amortization Foreign) | (2,893,546.0) | (3,011,813.4) | (3,197,972.8) | (4,389,706.5) | (2,174,141.8) | (4,017,109.6) |
| 2. Fedha za Ndani | 4,597,523.4 | 2,175,319.3 | 3,402,273.0 | 2,214,111.8 | 2,179,973.8 | 2,906,631.7 |
| Mikopo isiyo ya mabenki | 2,171,460.3 | 2,445,972.9 | 3,693,659.5 | 486,526.0 | 1,109,508.0 | 1,479,343.9 |
| Mikopo ya mabenki | 2,426,063.1 | (270,653.6) | (291,386.5) | 1,727,585.9 | 1,070,465.9 | 1,427,287.8 |
| Mikopo ya ndani (Rollover) | 3,513,913.7 | 3,257,143.9 | 4,087,193.3 | 3,325,556.5 | 2,132,650.8 | 3,122,373.0 |
| Marekebisho (Adjustment to Cash) | (97,656.8) | (99,896.3) | (458,866.1) | - | (313,625.3) | - |
| Kulipia madeni ya ndani (amortization) | (3,513,913.7) | (3,257,143.9) | (4,087,193.3) | (3,325,556.5) | (2,132,650.8) | (3,122,373.0) |
| Expenditure float | (12,956.4) | (8,723.3) | - | | - | - |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha

**Kielelezo Na. 3.6: MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI (Shilingi Milioni)**



## Jedwali Na. 30: MGAWANYO WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA HUDUMA ZA SERIKALI

Shilingi Milioni

| Fungu | Maelezo | Halisi 2024/25 | | | Bajeti iliyoidhinishwa 2025/26 | | | Makadirio 2026/27 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla |
| **701** | **Huduma za Kawaida** | **15,333,186** | **2,096,016** | **17,429,202** | **18,009,703** | **2,753,466** | **20,763,169** | **19,097,497** | **2,891,977** | **21,989,474** |
| 70111 | Utawala na Shughuli za Bunge (CS) | 5,092,187 | 1,539,110 | 6,631,297 | 5,803,531 | 2,142,103 | 7,945,634 | 6,293,175 | 1,961,364 | 8,254,539 |
| 70112 | Fedha na Masuala ya Kodi (CS) | 4,594,646 | 514,458 | 5,109,104 | 5,328,348 | 490,827 | 5,819,175 | 4,909,450 | 807,953 | 5,717,403 |
| 70113 | Mambo ya Nje (CS) | 376,384 | 18,384 | 394,768 | 290,225 | 45,540 | 335,765 | 307,859 | 46,365 | 354,224 |
| 70121 | Misaada ya Kiuchumi kutoka Nje (CS) | 2,349 | 0 | 2,349 | 3,210 | 0 | 3,210 | 3,847 | 0 | 3,847 |
| 70122 | Misaada ya Kiuchumi kupitia Mashirika ya Kimataifa(CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70131 | Huduma za Umma (CS) | 16,812 | 3,025 | 19,836 | 19,108 | 1,823 | 20,931 | 20,775 | 1,679 | 22,453 |
| 70132 | Huduma za Mipango na Takwimu (CS) | 48,773 | 20,920 | 69,693 | 51,927 | 71,996 | 123,922 | 51,894 | 70,156 | 122,050 |
| 70133 | Huduma nyingine za Kawaida (CS) | 4,630 | 120 | 4,750 | 6,665 | 1,177 | 7,842 | 7,394 | 4,461 | 11,855 |
| 70140 | Utafiti wa Msingi (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70150 | Utafiti na Maendeleo Huduma za Umma (CS) | 2,158 | 0 | 2,158 | 2,601 | 0 | 2,601 | 2,703 | 0 | 2,703 |
| 70160 | Huduma za Umma zisizotajwa hapo Juu (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70170 | Deni la Taifa (CS) | 5,195,246 | 0 | 5,195,246 | 6,504,088 | 0 | 6,504,088 | 7,500,401 | 0 | 7,500,401 |
| 70180 | Uhamishaji Fedha Ndani ya Serikali (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **702** | **Ulinzi** | **3,582,492** | **1,352,481** | **4,934,973** | **3,307,262** | **315,298** | **3,622,560** | **3,832,096** | **422,534** | **4,254,630** |
| 70210 | Huduma za Ulinzi wa Kijeshi (CS) | 3,581,756 | 158,406 | 3,740,162 | 3,306,225 | 116,043 | 3,422,269 | 3,830,559 | 157,280 | 3,987,839 |
| 70220 | Huduma za Ulinzi wa Kiraia (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70230 | Misaada ya Nje ya Ulinzi (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70240 | Utafiti na Maendeleo ya Ulinzi (CS) | 737 | 1,194,075 | 1,194,811 | 1,037 | 199,254 | 200,291 | 1,537 | 265,253 | 266,791 |
| 70250 | Huduma za Ulinzi zisizotajwa hapo Juu (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **703** | **Usalama wa Raia** | **1,672,894** | **696,118** | **2,369,012** | **1,967,405** | **377,385** | **2,344,790** | **2,368,050** | **464,185** | **2,832,236** |
| 70310 | Huduma za Ulinzi wa Kijeshi (CS) | 947,925 | 603,621 | 1,551,546 | 1,054,660 | 203,355 | 1,258,015 | 1,239,779 | 202,655 | 1,442,434 |
| 70320 | Huduma za Ulinzi wa Kiraia (CS) | 53,231 | 9,203 | 62,434 | 62,714 | 15,139 | 77,853 | 79,075 | 25,214 | 104,289 |
| 70330 | Mahakama (CS) | 243,256 | 68,344 | 311,600 | 369,938 | 70,804 | 440,743 | 473,333 | 116,319 | 589,652 |
| 70340 | Magereza (CS) | 286,030 | 6,123 | 292,153 | 310,043 | 6,357 | 316,400 | 371,651 | 13,289 | 384,940 |
| 70350 | Huduma za utafiti na Maendeleo Usalama wa Raia (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70360 | Huduma Usalama wa Raia zisizotajwa hapo juu (CS) | 142,451 | 8,827 | 151,279 | 170,049 | 81,729 | 251,778 | 204,212 | 106,708 | 310,921 |
| **704** | **Shughuli za Kiuchumi** | **1,310,859** | **6,514,603** | **7,825,462** | **1,360,920** | **8,916,392** | **10,277,312** | **1,511,768** | **10,353,210** | **11,864,978** |
| 70411 | Shughuli za Kiuchumi na Biashara (CS) | 120,276 | 65,766 | 186,042 | 176,687 | 92,138 | 268,826 | 221,540 | 111,786 | 333,325 |
| 70412 | Masuala ya Kazi (CS) | 19,156 | 12,415 | 31,571 | 23,690 | 9,892 | 33,582 | 25,639 | 11,542 | 37,181 |
| 70421 | Kilimo (CS) | 276,407 | 596,036 | 872,443 | 361,780 | 1,168,960 | 1,530,740 | 409,705 | 1,092,807 | 1,502,512 |
| 70422 | Misitu (CS) | 50,986 | 1,024 | 52,010 | 63,532 | 34,442 | 97,973 | 75,234 | 14,518 | 89,752 |
| 70423 | Uvuvi na Uwindaji (CS) | 13,016 | 15,388 | 28,404 | 21,663 | 76,753 | 98,416 | 22,035 | 74,145 | 96,180 |
| 70431 | Makaa ya Mawe na Nishati nyingine (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70432 | Petroli na Gesi Asilia (CS) | 8,980 | 1,000 | 9,980 | 8,149 | 169,332 | 177,481 | 10,640 | 175,000 | 185,640 |
| 70433 | Nishati ya Nyukilia (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70434 | Nishati nyingine (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70435 | Umeme (CS) | 2,713 | 1,648,265 | 1,650,978 | 56,147 | 1,714,181 | 1,770,329 | 32,901 | 2,284,365 | 2,317,265 |
| 70436 | Nishati isiyo ya umeme (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70441 | Uchimbaji Madini yasiyo Nishati (CS) | 76,114 | 195,171 | 271,284 | 91,076 | 124,605 | 215,681 | 94,200 | 71,508 | 165,708 |
| 70442 | Uzalishaji Viwandani (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70443 | Ujenzi (CS) | 22,310 | 34,604 | 56,914 | 27,157 | 54,475 | 81,632 | 31,884 | 54,475 | 86,360 |
| 70451 | Usafiri wa Barabara (CS) | 215,561 | 3,749,676 | 3,965,237 | 237,491 | 4,905,228 | 5,142,719 | 255,996 | 6,020,973 | 6,276,969 |
| 70452 | Usafiri wa Majini (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70453 | Usafiri wa Reli (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70454 | Usafiri wa Anga (CS) | 49 | 55,341 | 55,390 | 278 | 218,870 | 219,147 | 263 | 119,885 | 120,148 |
| 70455 | Usafirishaji kwa njia ya Bomba na njia nyingine za usafiri (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70460 | Mawasiliano (CS) | 53,560 | 43,677 | 97,236 | 98,744 | 266,758 | 365,502 | 129,706 | 227,191 | 356,897 |
| 70471 | Huduma za Biashara na Utunzaji Mizigo (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |

**Jedwali Na. 30 linaendelea**

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 70472 | Hoteli na Migahawa (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70473 | Utalii (CS) | 442,737 | 82,954 | 525,692 | 141,588 | 28,758 | 170,346 | 147,396 | 40,228 | 187,624 |
| 70474 | Miradi ya Maendeleo (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70481 | Utafiti katika shughuli za Kiuchumi, Biashara na Kazi (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70482 | Utafiti na Maendeleo ya Kilimo, Misitu, Uvuvi na Uwindaji (CS) | 8,994 | 13,286 | 22,280 | 52,938 | 52,000 | 104,938 | 54,630 | 54,787 | 109,417 |
| 70483 | Utafiti na Maendeleo ya Mafuta na Nishati (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70484 | Utafiti na Maendeleo ya Uchimbaji Madini, Uzalishaji Viwandani na Ujenzi (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70485 | Utafiti na Maendeleo ya Usafiri (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70486 | Utafiti na Maendeleo ya Mawasiliano (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70487 | Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Vingine (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70490 | Shughuli nyingine za Kiuchumi zisizotajwa hapo juu (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **705** | **Hifadhi ya Mazingira** | **59,223** | **3,073** | **62,296** | **74,099** | **44,725** | **118,825** | **83,004** | **73,440** | **156,444** |
| 70510 | Hifadhi ya Taka (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70520 | Hifadhi ya Maji Taka (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70530 | Kupunguza Uharibifu wa Mazingira (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70540 | Hifadhi ya Viumbehai na Mazingira (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70550 | Utafiti na Maendeleo ya Hifadhi ya Mazingira (CS) | 838 | 0 | 838 | 1,145 | 0 | 1,145 | 1,046 | 0 | 1,046 |
| 70560 | Huduma nyingine za Hifadhi ya Mazingira zisizotajwa hapo juu (CS) | 58,385 | 3,073 | 61,458 | 72,954 | 44,725 | 117,680 | 81,957 | 73,440 | 155,397 |
| **706** | **Nyumba na Huduma za Jamii** | **178,174** | **517,422** | **695,597** | **224,654** | **1,020,170** | **1,244,823** | **274,504** | **1,206,393** | **1,480,897** |
| 70610 | Maendeleo ya Nyumba (CS) | 31,170 | 3,222 | 34,392 | 34,806 | 75,049 | 109,855 | 48,485 | 89,740 | 138,226 |
| 70620 | Maendeleo ya Jamii (CS) | 85,929 | 46,583 | 132,512 | 115,094 | 112,093 | 227,187 | 136,551 | 69,957 | 206,508 |
| 70630 | Usambazaji Maji (CS) | 61,075 | 467,617 | 528,692 | 74,754 | 833,027 | 907,782 | 89,468 | 1,046,696 | 1,136,164 |
| 70640 | Taa za Barabarani (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70650 | Utafiti wa Nyumba na Maendeleo ya Jamii (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70660 | Nyumba na Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **707** | **Afya** | **803,632** | **852,821** | **1,656,454** | **903,984** | **1,168,281** | **2,072,265** | **1,069,530** | **1,118,376** | **2,187,906** |
| 70711 | Madawa (IS) | 180 | 493,705 | 493,885 | 1,382 | 371,000 | 372,382 | 1,591 | 459,989 | 461,580 |
| 70712 | Bidhaa nyingine za madawa (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70713 | Huduma za Tiba na Vifaa vya Tiba (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70721 | Huduma za Tiba za Jumla (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70722 | Huduma Maalumu za Tibas (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70723 | Huduma za Meno (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70724 | Huduma za Wakunga Wasaidizi (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70731 | Huduma za Hospitali (IS) | 23,798 | 7,758 | 31,556 | 22,645 | 16,992 | 39,637 | 47,502 | 3,969 | 51,471 |
| 70732 | Huduma Maalumu za Hospitali (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70733 | Huduma za Vifaa vya Kujifungulia (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70734 | Huduma za Wakunga na Wakunga wa Jadi (IS) | 181 | 0 | 181 | 930 | 0 | 930 | 972 | 0 | 972 |
| 70740 | Huduma za Afya kwa Umma (IS) | 750,752 | 288,624 | 1,039,375 | 826,773 | 546,503 | 1,373,275 | 966,775 | 488,224 | 1,454,999 |
| 70750 | Utafiti na Maendeleo ya Huduma za Afya (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70760 | Huduma za Afya zisizotajwa hapo juu (CS) | 28,722 | 62,735 | 91,457 | 52,255 | 233,786 | 286,041 | 52,689 | 166,194 | 218,882 |
| **708** | **Burudani, Utamaduni na Dini** | **26,981** | **295,583** | **322,564** | **34,771** | **426,821** | **461,592** | **36,323** | **426,768** | **463,091** |
| 70810 | Huduma za Burudani na Michezo (IS) | 1,621 | 30 | 1,651 | 2,971 | 130 | 3,101 | 4,550 | 278 | 4,828 |
| 70820 | Huduma za Utamaduni (IS) | 25,360 | 295,553 | 320,914 | 31,710 | 426,691 | 458,401 | 31,681 | 426,491 | 458,172 |
| 70830 | Huduma za Utangazaji na Uchapishaji (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70840 | Dini na Huduma nyingine za Kijamii (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70850 | Utafiti na Maendeleo katika Burudani, Utamaduni na Dini (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70860 | Huduma nyingine za Burudani, Utamaduni na Dini zisizotajwa hapo juu (CS) | 0 | 0 | 0 | 89 | 0 | 89 | 91 | 0 | 91 |
| **709** | **Elimu** | **3,686,534** | **1,762,247** | **5,448,781** | **3,896,463** | **3,507,600** | **7,404,063** | **4,132,095** | **2,589,087** | **6,721,182** |
| 70911 | Elimu ya Awali (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70912 | Elimu ya Msingi (IS) | 1,986,157 | 496,515 | 2,482,672 | 2,059,578 | 952,294 | 3,011,872 | 2,263,674 | 546,246 | 2,809,920 |
| 70921 | Elimu ya Sekondari (Kidato cha I - IV) (IS) | 1,121,165 | 425,223 | 1,546,388 | 1,163,690 | 663,569 | 1,827,258 | 1,224,736 | 525,551 | 1,750,287 |
| 70922 | Elimu ya Sekondari (Kidato cha V - VI) (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70930 | Elimu baada ya Sekondari isiyo ya Chuo Kikuu (IS) | 409,880 | 777,643 | 1,187,523 | 465,053 | 1,684,200 | 2,149,253 | 476,845 | 1,372,833 | 1,849,678 |
| 70941 | Daraja la Awali Elimu ya Chuo Kikuu (IS) | 26,434 | 10,390 | 36,825 | 44,954 | 40,483 | 85,437 | 13,134 | 5,700 | 18,834 |
| 70942 | Daraja linalofuata Elimu ya Chuo Kikuu (IS) | 16,804 | 2,200 | 19,004 | 20,962 | 1,200 | 22,162 | 15,179 | 14,200 | 29,379 |
| 70950 | Elimu isiyopambanuliwa (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70960 | Huduma za Ziada kwa Elimu (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70970 | Utafiti na Maendeleo ya Elimu (CS) | 56,894 | 11,455 | 68,349 | 65,096 | 25,523 | 90,619 | 67,018 | 23,506 | 90,525 |
| 70980 | Huduma za Elimu zisizotajwa hapo juu (CS) | 69,200 | 38,821 | 108,022 | 77,132 | 140,332 | 217,463 | 71,508 | 101,051 | 172,559 |
| **710** | **Kinga ya Jamii** | **16,279** | **73,599** | **89,878** | **19,735** | **126,190** | **145,925** | **19,292** | **115,154** | **134,446** |
| 71011 | Ugonjwa (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71012 | Ulemavu (IS) | 1,984 | 1,256 | 3,240 | 1,726 | 1,000 | 2,726 | 602 | 0 | 602 |
| 71020 | Wazee (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71030 | Waathirika (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71040 | Familia na Watoto (IS) | 2,286 | 1,809 | 4,096 | 2,995 | 4,420 | 7,415 | 2,675 | 2,981 | 5,656 |
| 71050 | Ukosefu wa Ajira (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71060 | Nyumba (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71070 | Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71080 | Utafiti na Maendeleo ya Kinga ya Jamii (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71090 | Huduma za Kinga ya Jamii zisizotajwa hapo juu (CS) | 12,009 | 70,534 | 82,543 | 15,014 | 120,770 | 135,784 | 16,015 | 112,173 | 128,188 |
| **7** | **Jumla** | **26,670,254** | **14,163,964** | **40,834,219** | **29,798,996** | **18,656,328** | **48,455,324** | **32,424,158** | **19,661,125** | **52,085,283** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## SURA YA 4

## SEKTA YA NJE

**Bidhaa Zilizouzwa Nje**

82. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 12.5 na kufikia dola za Marekani milioni 10,262.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 9,121.6 mwaka 2024 (**Jedwali Na. 4.1**). Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa asilia, hususan kahawa, tumbaku na katani pamoja na bidhaa zisizo asilia, ikiwemo dhahabu, bidhaa za viwandani na mazao ya mbogamboga na maua. Aidha, thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia ilichangia asilimia 82.5 ya mauzo yote nje ya nchi ikifuatiwa na bidhaa asilia asilimia 14.5 na bidhaa zisizorekodiwa asilimia 3.0.

**Bidhaa Asilia**

83. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya bidhaa asilia nje ya nchi iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 1,491.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,473.3 Hii ilitokana na kupanda kwa thamani ya mauzo ya mazao ya tumbaku, katani na kahawa kufuatia kuongezeka kwa mahitaji nje na uzalishaji wa ndani.

**Kahawa**

84. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya kahawa nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 23.4 na kufikia dola za Marekani milioni 361.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 292.9 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa bei ya kahawa na kufikia wastani wa dola za Marekani 5,103.6 kwa tani mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani 3,564.3 kwa tani mwaka 2024. Hata hivyo, kiasi cha kahawa kilichouzwa nje ya nchi kilipungua kwa asilimia 13.9 na kufikia tani 70,800 mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 82,200 mwaka 2024.

**Korosho**

85. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya korosho nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 26.4 na kufikia dola za Marekani milioni 398.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 541.7 mwaka 2024. Hii ilitokana na kupungua kwa wastani wa bei ya korosho hadi dola za Marekani 1,176.9 kwa tani mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,264.7 kwa tani mwaka 2024. Aidha, kiasi cha korosho kilichouzwa nje ya nchi kilipungua kwa asilimia 20.9 na kufikia tani 338,878.6 mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 428,295.7 mwaka 2024. Pamoja na kupungua kwa thamani ya mauzo, korosho iliendelea kuwa miongoni mwa bidhaa asilia zilizoongoza kwa mchango katika mauzo ya nje.

**Pamba**

86. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya pamba nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 43.0 na kufikia dola za Marekani milioni 99.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 69.3

mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa wastani wa bei na kiasi cha pamba kilichouzwa nje ya nchi. Katika kipindi hicho, tani 66,291.1 za pamba ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 52,600.2 zilizouzwa mwaka 2024. Aidha, wastani wa bei ya pamba katika soko la dunia uliongezeka kwa asilimia 13.4 na kufikia dola za Marekani 1,495.2 kwa tani mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,318.0 kwa tani mwaka 2024.

**Katani**

87. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya katani nje ilikuwa dola za Marekani milioni 34.53 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 23.36 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 47.8. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa wastani wa bei na kiasi cha katani kilichouzwa nje ya nchi. Katika kipindi hicho, tani 24,064.3 za katani ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 21,195.8 zilizouzwa mwaka 2024. Aidha, wastani wa bei ya katani uliongezeka kwa asilimia 30.2 na kufikia dola za Marekani 1,434.89 kwa tani mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,102.32 kwa tani mwaka 2024.

**Chai**

88. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya chai nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 14.46 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 19.44 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 25.6. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha chai kilichouzwa nje kilichofikia tani 10,848.6 mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 15,742.7 mwaka 2024. Hata hivyo, wastani wa bei ya chai uliongezeka kwa asilimia 7.9 na kufikia dola za Marekani 1,332.74 kwa tani mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,234.94 kwa tani mwaka 2024.

**Tumbaku**

89. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya tumbaku nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 10.1 na kufikia dola za Marekani milioni 561.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 509.5 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa wastani wa bei na kiasi cha tumbaku kilichouzwa nje ya nchi. Katika kipindi hicho, tani 119,204.2 za tumbaku ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 108,497.8 zilizouzwa mwaka 2024. Aidha, bei ya tumbaku iliongezeka na kufikia wastani wa dola za Marekani 4,707.2 kwa tani mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani 4,695.9 kwa tani mwaka 2024.

**Bidhaa Zisizo Asilia**

90. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 8,464.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 7,228.8 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 17.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya madini na bidhaa za viwandani.

**Madini**

91. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 5,401.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 4,119.9 mwaka 2024, sawa na

ongezeko la asilimia 31.1. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu sambamba na kuongezeka kwa wastani wa bei ya dhahabu katika soko la dunia. Katika kipindi hicho, thamani ya mauzo ya dhahabu iliongezeka kwa asilimia 39.0 na kufikia dola za Marekani milioni 4,753.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,419.6 mwaka 2024. Aidha, thamani ya mauzo ya dhahabu ilichangia asilimia 88.0 ya mauzo ya madini yote mwaka 2025.

**Bidhaa za Viwandani**

92. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 19.0 na kufikia dola za Marekani milioni 1,595.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,341.3 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za viwandani katika nchi jirani. Katika kipindi hicho, mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi yalichangia asilimia 18.8 ya mauzo yote ya bidhaa zisizo asilia.

**Samaki na Mazao ya Samaki**

93. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya samaki na mazao ya samaki nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 161.2 ikilinganishwa na mauzo ya dola za Marekani milioni 180.6 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 10.7. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha samaki na mazao ya samaki kilichouzwa hadi tani 23,300 mwaka 2025 kutoka tani 29,000 mwaka 2024.

**Mbogamboga na Maua**

94. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya mbogamboga na maua nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 443.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 507.0 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 12.5. Hii ilitokana na kupungua kwa wastani wa bei ya mbogamboga na maua katika soko la kimataifa. Hata hivyo, kiasi cha mbogamboga na maua kilichouzwa kiliongezeka na kufikia tani 757,700 mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 730,400 mwaka 2024.

**Bidhaa Nyinginezo Zilizouzwa Nje**

95. Mwaka 2025, thamani ya bidhaa nyinginezo zilizouzwa nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 731.2 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 839.1 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 12.9. Hii ilitokana na kupungua kwa mauzo ya mbegu za mafuta, kakao na nafaka.

**Jedwali Na. 4.1: Bidhaa Zilizouzwa Nje (Dola za Marekani Milioni), Mwaka 2021 - 2025**

| Bidhaa | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa Asilia** | | | | | | |
| **Kahawa** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 155.2 | 161.2 | 227.9 | 292.9 | 361.3 | 23.4 |
| Kiasi ('000 tani) | 68.0 | 55.2 | 84.4 | 82.2 | 70.8 | -13.8 |
| Bei (US$ kwa tani) | 2,284.4 | 2,919.6 | 2,700.8 | 3,564.3 | 5,103.6 | 43.2 |
| **Pamba** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 81.3 | 103.4 | 101.9 | 69.3 | 99.1 | 43.0 |
| Kiasi ('000 tani) | 48.8 | 48.9 | 69.6 | 52.6 | 66.3 | 26.0 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,665.0 | 2,113.2 | 1,463.4 | 1,318.0 | 1,495.2 | 13.4 |
| **Katani** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 20.2 | 24.3 | 20.4 | 23.4 | 34.5 | 47.8 |
| Kiasi ('000 tani) | 12.6 | 14.9 | 12.5 | 21.2 | 24.1 | 13.5 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,600.0 | 1,629.1 | 1,628.9 | 1,102.3 | 1,434.9 | 30.2 |
| **Chai** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 32.9 | 30.0 | 31.1 | 19.4 | 14.5 | -25.6 |
| Kiasi ('000 tani) | 24.2 | 21.1 | 22.2 | 15.7 | 10.8 | -31.1 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,356.5 | 1,420.3 | 1,403.6 | 1,234.9 | 1,332.7 | 7.9 |
| **Tumbaku** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 127.5 | 178.5 | 340.4 | 509.5 | 561.1 | 10.1 |
| Kiasi ('000 tani) | 37.7 | 49.3 | 82.0 | 108.5 | 119.2 | 9.9 |
| Bei (US$ kwa tani) | 3,381.5 | 3,624.1 | 4,150.8 | 4,695.9 | 4,707.2 | 0.2 |
| **Korosho** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 159.0 | 226.9 | 206.4 | 541.7 | 398.8 | -26.4 |
| Kiasi ('000 tani) | 154.4 | 234.0 | 219.6 | 428.3 | 338.9 | -20.9 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,030.3 | 970.0 | 939.9 | 1,264.7 | 1,176.9 | -6.9 |
| **Karafuu** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 51.8 | 42.1 | 25.1 | 17.1 | 22.5 | 31.7 |
| Kiasi ('000 tani) | 7.0 | 5.9 | 4.7 | 2.8 | 3.3 | 17.2 |
| Bei (US$ kwa tani) | 7,347.6 | 7,104.0 | 5,356.9 | 6,011.1 | 6,757.5 | 12.4 |
| **Jumla (Bidhaa Asilia)** | **627.9** | **766.5** | **953.3** | **1,473.3** | **1,491.9** | **1.3** |
| **Bidhaa Zisizo Asilia (US$ millioni)** | | | | | | |
| **Madini** | **3,116.4** | **3,395.3** | **3,551.4** | **4,119.9** | **5,401.9** | **31.1** |
| Dhahabu | 2,737.1 | 2,835.1 | 3,058.9 | 3,419.6 | 4,753.9 | 39.0 |
| Almasi | 8.5 | 62.7 | 23.6 | 53.2 | 44.7 | -15.9 |
| Madini mengine | 370.8 | 497.4 | 469.0 | 647.1 | 603.2 | -6.8 |
| **Bidhaa za Viwandani** | **1,200.0** | **1,419.2** | **1,363.3** | **1,341.3** | **1,595.8** | **19.0** |
| Nyuzi za Pamba | 3.6 | 1.9 | 0.5 | 1.2 | 1.1 | -8.4 |
| Kahawa iliyozalishwa | 16.3 | 21.8 | 4.5 | 11.1 | 12.0 | 8.4 |
| Tumbaku iliyozalishwa | 32.0 | 34.5 | 37.9 | 14.7 | 38.7 | 163.3 |
| Mazao ya Katani | 33.6 | 35.4 | 31.4 | 22.9 | 27.3 | 19.2 |
| Bidhaa nyingine za Viwandani | 1,114.5 | 1,325.6 | 1,289.0 | 1,291.5 | 1,516.7 | 17.4 |
| **Samaki na Mazao ya Samaki** | **164.3** | **168.2** | **164.0** | **180.6** | **161.2** | **-10.7** |
| **Mazao ya Mboga na Maua** | **378.6** | **289.6** | **417.2** | **507.0** | **443.6** | **-12.5** |
| **Bidhaa zilizouzwa tena (re-exports)** | **90.2** | **131.2** | **135.2** | **240.8** | **130.9** | **-45.6** |
| **Bidhaa nyinginezo** | **813.5** | **654.9** | **690.5** | **839.2** | **731.2** | **-12.9** |
| **Jumla (Bidhaa zisizo Asilia)** | **5,763.0** | **6,058.4** | **6,321.6** | **7,228.8** | **8,464.5** | **17.1** |
| Bidhaa zisizo rekodiwa | 365.4 | 399.0 | 421.6 | 419.6 | 306.6 | -26.9 |
| **Jumla Kuu (Bidhaa Zote)** | **6,756.2** | **7,223.8** | **7,696.6** | **9,121.6** | **10,262.9** | **12.5** |

**Chanzo**: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

**Mapato ya Huduma**

96. Mwaka 2025, mapato yatokanayo na biashara ya huduma nje ya nchi yalikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 7,477.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 6,846.8 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 9.2. Hii ilitokana na kuendelea kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma za utalii na usafirishaji. Aidha, mapato yatokanayo na huduma za safari za utalii yaliongezeka kwa asilimia 13.0 na kufikia dola za Marekani milioni 4,410.6 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,903.1 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuimarika kwa shughuli za kitalii nchini. Katika kipindi hicho, watalii walioingia nchini walikuwa 2,294,495 ikilinganishwa na watalii 2,141,895 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 7.1. Vilevile, mapato yatokanayo na huduma ya usafirishaji yalikuwa dola za Marekani milioni 2,647.6 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,353.4 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 12.5.

**Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje ya Nchi**

97. Mwaka 2025, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 14,787.7 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 14,195.6 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 4.2 (**Jedwali Na. 4.2**). Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za kukuza mitaji pamoja na bidhaa za matumizi ya kawaida. Katika kipindi hicho, sehemu kubwa ya bidhaa zilizoagizwa nchini zilikuwa bidhaa za kukuza mitaji hususan vifaa vya usafirishaji na mitambo zilizochangia asilimia 45.6 ikifuatiwa na bidhaa za matumizi ya kati zikijumuisha mafuta ya petroli na malighafi za viwanda asilimia 27.3 na bidhaa za matumizi ya kawaida asilimia 27.0.

**Bidhaa za Kukuza Mitaji**

98. Mwaka 2025, thamani ya bidhaa za kukuza mitaji zilizoingizwa nchini ilikuwa dola za Marekani milioni 6,745.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 6,034.3 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 11.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa vyombo vya usafirishaji, mitambo na vifaa vya ujenzi na majengo.

**Bidhaa za Kati**

99. Mwaka 2025, thamani ya bidhaa za kati zilizoingizwa nchini ilipungua kwa asilimia 7.9 na kufikia dola za Marekani milioni 4,044.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 4,392.7 mwaka 2024. Hii ilitokana na kupungua kwa gharama ya uagizaji wa bidhaa za petroli kufuatia kushuka kwa bei katika soko la dunia. Katika kipindi hicho, thamani ya bidhaa za petroli zilizoagizwa ilipungua kwa asilimia 21.9 na kufikia dola za Marekani milioni 2,216.0 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,837.2 mwaka 2024. Aidha, thamani ya uagizaji wa mafuta ilichangia asilimia 15.0 ya bidhaa zote zilizoagizwa kutoka nje ya nchi mwaka 2025.

**Bidhaa za Matumizi ya Kawaida**

100. Mwaka 2025, thamani ya bidhaa za matumizi ya kawaida zilizoagizwa kutoka nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 3,995.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,766.5 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 6.1. Hii ilitokana na ongezeko la thamani ya bidhaa nyingine zisizo za chakula zilizoagizwa kutoka nje, ikiwemo bidhaa za kifamasia (dawa). Katika kipindi hicho, uagizaji wa bidhaa nyingine uliongezeka kwa asilimia 13.6 na kufikia dola za Marekani milioni 3,189.2 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,808.2 mwaka 2024.

**Jedwali Na. 4.2: Thamani ya Bidhaa Zilizoagizwa kutoka Nje ya Nchi (Dola za Marekani Milioni), Mwaka 2021 - 2025**

| Bidhaa | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa za Kukuza Mitaji** | **3,836.0** | **5,167.5** | **5,592.9** | **6,034.3** | **6,745.8** | **11.8** |
| Vifaa vya Usafirishaji | 970.4 | 1,420.4 | 1,571.4 | 1,892.0 | 2,159.9 | 14.2 |
| Majengo na Ujenzi | 1,159.0 | 1,455.1 | 1,486.4 | 1,670.0 | 1,908.2 | 14.3 |
| Mitambo | 1,706.6 | 2,291.9 | 2,535.2 | 2,472.4 | 2,677.7 | 8.3 |
| **Bidhaa za Kati** | **3,250.5** | **5,102.1** | **4,466.3** | **4,392.7** | **4,044.4** | **-7.9** |
| Uagizaji Mafuta | 2,084.4 | 3,532.6 | 2,967.0 | 2,837.2 | 2,216.0 | -21.9 |
| Mbolea | 189.4 | 500.9 | 414.0 | 345.4 | 434.7 | 25.9 |
| Malighafi za Viwanda | 976.7 | 1,068.6 | 1,085.2 | 1,210.1 | 1,393.7 | 15.2 |
| **Bidhaa za Matumizi ya Kawaida** | **2,914.7** | **3,936.9** | **3,667.5** | **3,766.5** | **3,995.4** | **6.1** |
| Bidhaa za Vyakula | 500.9 | 735.5 | 885.5 | 958.3 | 806.1 | -15.9 |
| Bidhaa Nyingine | 2,413.8 | 3,201.4 | 2,782.0 | 2,808.2 | 3,189.2 | 13.6 |
| **Jumla (FOB)** | **10,003.4** | **14,208.7** | **13,728.9** | **14,195.6** | **14,787.7** | **4.2** |
| **Jumla (CIF)** | **10,849.9** | **15,654.5** | **15,117.5** | **15,593.0** | **16,234.4** | **4.1** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

**Malipo ya Huduma**


101. Mwaka 2025, malipo ya huduma nje ya nchi yalikuwa dola za Marekani milioni 3,241.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,795.0 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 16.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa gharama za huduma za usafirishaji wa bidhaa zilizoagizwa na malipo ya huduma nyingine nje ya nchi.

**Mwenendo wa Biashara Baina ya Tanzania na Nchi Mbalimbali**

102. Mwaka 2025, mahusiano ya kibiashara kati ya Tanzania na nchi mbalimbali duniani ikiwemo jumuiya za kikanda na kimataifa yaliendelea kuimarika. Katika kipindi hicho, bidhaa za Tanzania ziliuzwa zaidi katika nchi ya Afrika Kusini iliyochangia asilimia 29.2 ya mauzo yote, ikifuatiwa na Umoja wa Falme za Kiarabu (asilimia 13.3) na India (asilimia 9.4), kama inavyooneka katika **Kielelezo Na. 4.1**. Aidha, mazao ya nafaka (mahindi na mchele) yaliuzwa zaidi nchi jirani, hususan Kenya na Uganda. Vilevile, bidhaa za tumbaku,

kahawa, korosho, mbogamboga na mbegu za mafuta ziliuzwa katika nchi za Ubelgiji, India, Umoja wa Falme za Kiarabu, China na Uswisi. Kwa upande mwingine, dhahabu iliuzwa katika nchi za Afrika Kusini, Umoja wa Falme za Kiarabu, Uswisi na India ambapo asilimia 52.2 ya dhahabu yote iliuzwa Afrika Kusini.

**Kielelezo Na. 4.1: Mchanganuo wa Masoko ya Bidhaa za Tanzania Nje ya Nchi kwa Nchi zenye Mchango wa Zaidi ya Asilimia 2, Mwaka 2025**




103. Mwaka 2025, thamani ya bidhaa zilizouzwa katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC ilikuwa dola za Marekani milioni 1,226.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,163.8 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 5.4. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za mchele, mahindi, chuma na mbolea kwenda nchi za Burundi, Rwanda na Kenya.

104. Mwaka 2025, thamani ya bidhaa zilizouzwa katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC ilikuwa dola za Marekani milioni 3,525.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,968.3 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 18.8. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu kwenda nchi ya Afrika ya Kusini.

105. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda katika soko la Jumuiya ya Ulaya na Uswisi ilikuwa dola za Marekani milioni 1,376.2 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 962.7 mwaka 2024, sawa na ongezeko kwa asilimia 43.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa kwenda Italia, Uswisi na Ubelgiji, hususan dhahabu, tumbaku na kahawa.

106. Mwaka 2025, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda nchi za Bara la Asia ilikuwa dola za Marekani milioni 3,787.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,638.3 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 4.1. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa kwenda Umoja wa Falme za Kiarabu na Singapuri, hususan dhahabu na makinikia (**Jedwali Na. 4.3**).


**Jedwali Na. 4.3: Mauzo ya Bidhaa Kwenda Nchi Mbalimbali (Dola za Marekani Milioni), Mwaka 2021 - 2025**

| JUMUIYA/ NCHI | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI | 874.0 | 936.4 | 1,100.4 | 962.7 | 1,376.2 | 43.0 |
| NCHI NYINGINE ZA ULAYA | 32.3 | 26.6 | 25.9 | 26.9 | 64.1 | * |
| **JUMLA- BARA LA ULAYA** | **906.3** | **963.0** | **1,126.3** | **989.6** | **1,440.3** | **45.5** |
| **AFRIKA** | | | | | | |
| **JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)** | | | | | | |
| Afrika ya Kusini | 916.7 | 929.6 | 1123.5 | 2292.7 | 2,908.2 | 26.8 |
| Zambia | 68.6 | 80.0 | 98.6 | 162.6 | 156.8 | -3.6 |
| Swaziland | 0.1 | 0.3 | 0.4 | 0.1 | 0.0 | -97.6 |
| Zimbabwe | 14.8 | 15.5 | 38.9 | 34.6 | 34.0 | -1.9 |
| Msumbiji | 15.5 | 35.2 | 17.7 | 37.0 | 31.3 | -15.6 |
| Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 207.2 | 280.5 | 312.8 | 313.3 | 276.8 | -11.7 |
| Nchi nyingine za SADC | 80.4 | 100.7 | 135.7 | 127.9 | 118.3 | -7.5 |
| **JUMLA-SADC** | **1,303.4** | **1,441.8** | **1,727.5** | **2,968.3** | **3,525.4** | **18.8** |
| **JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)** | | | | | | |
| Burundi | 163.3 | 212.8 | 172.3 | 61.5 | 134.0 | * |
| Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 207.2 | 280.5 | 312.8 | 313.3 | 276.8 | -11.7 |
| Kenya | 397.2 | 381.7 | 176.5 | 320.9 | 393.9 | 22.8 |
| Rwanda | 277.8 | 262.5 | 188.2 | 163.8 | 251.5 | 53.5 |
| Uganda | 314.0 | 264.2 | 311.7 | 291.0 | 164.3 | -43.6 |
| Sudani ya Kusini | 8.9 | 13.1 | 19.2 | 10.1 | 5.2 | -47.8 |
| Somalia | 0.6 | 1.1 | 1.0 | 3.2 | 1.2 | -63.8 |
| **JUMLA-EAC** | **1,369.0** | **1,415.9** | **1,181.8** | **1,163.8** | **1,226.8** | **5.4** |
| Nchi nyingine za Afrika | 49.0 | 66.5 | 70.1 | 127.3 | 98.8 | -22.4 |
| **JUMLA-AFRIKA** | **2,514.2** | **2,643.7** | **2,666.6** | **3,946.1** | **4,574.2** | **15.9** |
| **BARA LA AMERIKA** | | | | | | |
| Marekani | 39.1 | 74.6 | 97.8 | 101.5 | 127.0 | 25.1 |
| Canada | 3.7 | 6.1 | 4.1 | 13.8 | 5.3 | -61.6 |
| Nchi nyingine za bara la Amerika | 1.8 | 2.7 | 4.4 | 6.0 | 12.3 | * |
| **JUMLA - BARA LA AMERIKA** | **44.5** | **83.4** | **106.4** | **121.2** | **144.6** | **19.2** |
| **BARA LA ASIA** | | | | | | |
| China | 273.1 | 293.7 | 427.9 | 443.0 | 439.8 | -0.7 |
| India | 1,008.7 | 1,178.6 | 1,554.0 | 1,637.0 | 937.8 | -42.7 |
| Japani | 67.5 | 89.0 | 67.9 | 99.8 | 110.6 | 10.8 |
| Umoja wa falme za kiarabu | 1,051.8 | 763.0 | 686.4 | 625.2 | 1,323.5 | * |
| Honkong | 61.3 | 177.0 | 45.9 | 42.5 | 39.3 | -7.5 |
| Singapuri | 139.2 | 183.0 | 142.0 | 15.9 | 328.4 | * |
| Nchi nyingine za Asia | 319.6 | 445.2 | 446.3 | 775.0 | 607.8 | -21.6 |
| **JUMLA-ASIA** | **2,921.2** | **3,129.4** | **3,370.5** | **3,638.3** | **3,787.1** | **4.1** |
| Nchi nyinginezo | 4.7 | 5.2 | 5.2 | 6.8 | 10.2 | 51.4 |
| **JUMLA KUU** | **6,390.9** | **6,824.8** | **7,274.9** | **8,702.0** | **9,956.4** | **14.4** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
* Badiliko linazidi asilimia 100

107. Mwaka 2025, Tanzania iliagiza zaidi bidhaa kutoka nchi za China (asilimia 35.5), India (asilimia 12.7), Umoja wa Falme za Kiarabu (asilimia 10.2), Japani (asilimia 4.3), Afrika Kusini (asilimia 3.3) na Kenya (asilimia 2.7), kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 4.2**. Aidha, bidhaa zilizoagizwa kwa kiasi kikubwa zilijumuisha mitambo, malighafi za viwandani, mafuta pamoja na vifaa vya usafirishaji.

**Kielelezo Na. 4.2: Mchanganuo wa Uagizaji wa Bidhaa Nchini kwa Nchi zenye Mchango wa Zaidi ya Asilimia 2, Mwaka 2025**




108. Mwaka 2025, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za EAC ilikuwa dola za Marekani milioni 582.2 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 526.8 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 10.5. Aidha, bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za SADC zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 846.1 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 781.5 zilizoagizwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 8.3 (**Jedwali Na. 4.4**). Kwa upande mwingine, urari wa biashara ya bidhaa baina ya Tanzania na nchi za EAC ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 644.6 mwaka 2025 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 637.0 mwaka 2024. Vilevile, urari wa biashara ya bidhaa baina ya Tanzania na nchi za SADC ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 2,679.3 mwaka 2025 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 2,186.8 mwaka 2024.

109. Mwaka 2025, thamani ya uagizaji wa bidhaa kutoka nchi za Bara la Asia ilikuwa dola za Marekani milioni 12,214.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 11,237.4 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 8.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za mitaji na malighafi za viwandani. Kwa upande mwingine, thamani ya uagizaji

wa bidhaa kutoka Jumuiya ya Ulaya na Uswisi ilikuwa dola za Marekani milioni 1,364.5 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,508.7 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 9.6. Hii ilitokana na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa za mafuta (petroleum gases) kutoka Uswisi.

**Jedwali Na. 4.4: Uagizaji wa Bidhaa Kutoka Nchi Mbalimbali Duniani (Dola za Marekani Milioni), Mwaka 2021 - 2025**

| JUMUIYA/ NCHI | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI | 1,001.9 | 1,659.1 | 1,275.5 | 1,508.7 | 1,364.5 | -9.6 |
| NCHI NYINGINE ZA ULAYA | 368.3 | 326.3 | 623.9 | 496.6 | 507.6 | 2.2 |
| **JUMLA - BARA LA ULAYA** | **1,370.2** | **1,985.4** | **1,899.4** | **2,005.3** | **1,872.1** | **-6.6** |
| **AFRIKA** | | | | | | |
| **JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)** | | | | | | |
| Afrika ya Kusini | 432.1 | 548.9 | 555.5 | 526.5 | 527.7 | 0.2 |
| Zambia | 70.5 | 91.0 | 113.1 | 149.9 | 187.7 | 25.2 |
| Swaziland | 39.6 | 43.7 | 37.8 | 42.9 | 38.3 | -10.8 |
| Zimbabwe | 9.9 | 8.1 | 9.8 | 13.0 | 8.2 | -36.9 |
| Msumbiji | 4.6 | 22.6 | 3.4 | 3.7 | 2.1 | -44.6 |
| Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 2.6 | 3.1 | 2.9 | 6.8 | 27.6 | 308.9 |
| Nchi nyingine za SADC | 57.4 | 61.8 | 63.7 | 38.6 | 54.5 | 41.0 |
| **JUMLA-SADC** | **616.6** | **779.2** | **786.1** | **781.5** | **846.1** | **8.3** |
| **JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)** | | | | | | |
| Burundi | 0.6 | 2.6 | 3.1 | 1.0 | 1.8 | 76.1 |
| Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 2.6 | 3.1 | 2.9 | 6.8 | 27.6 | 308.9 |
| Kenya | 413.0 | 426.6 | 408.9 | 399.9 | 438.2 | 9.6 |
| Rwanda | 2.2 | 3.1 | 1.4 | 3.2 | 3.6 | 11.7 |
| Uganda | 109.6 | 142.6 | 107.3 | 115.8 | 110.9 | -4.2 |
| Sudani ya Kusini | 0.1 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 0.1 | 8.9 |
| Somalia | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.0 | 120.1 |
| **JUMLA-EAC** | **528.0** | **578.0** | **523.6** | **526.8** | **582.2** | **10.5** |
| Nchi nyingine za Afrika | 70.1 | 251.4 | 204.3 | 111.0 | 109.8 | -1.1 |
| **JUMLA-AFRIKA** | **1,212.2** | **1,605.6** | **1,511.2** | **1,412.6** | **1,510.5** | **6.9** |
| **BARA LA AMERIKA** | | | | | | |
| Marekani | 260.4 | 335.1 | 378.3 | 455.1 | 343.1 | -24.6 |
| Canada | 45.4 | 56.9 | 81.8 | 69.7 | 67.5 | -3.2 |
| Nchi nyingine za bara la Amerika | 79.2 | 176.1 | 113.9 | 332.3 | 73.1 | -78.0 |
| **JUMLA - BARA LA AMERIKA** | **385.0** | **568.2** | **574.0** | **857.1** | **483.8** | **-43.6** |
| **BARA LA ASIA** | | | | | | |
| China | 2,700.0 | 3,946.3 | 4,158.7 | 4,752.8 | 5,767.3 | 21.3 |
| India | 1,209.1 | 1,960.6 | 1,949.0 | 2,125.5 | 2,056.6 | -3.2 |
| Japani | 465.5 | 521.6 | 649.5 | 571.3 | 692.6 | 21.2 |
| Umoja wa Falme za Kiarabu | 1,378.6 | 2,492.3 | 1,417.9 | 1,661.4 | 1,662.4 | 0.1 |
| Honkong | 53.1 | 83.9 | 77.7 | 68.2 | 77.8 | 14.0 |
| Singapuri | 82.2 | 107.9 | 156.5 | 58.5 | 60.8 | 4.0 |
| Nchi nyingine za Asia | 1,901.9 | 2,203.3 | 2,578.1 | 1,999.7 | 1,897.3 | -5.1 |
| **JUMLA-ASIA** | **7,790.4** | **11,315.9** | **10,987.4** | **11,237.4** | **12,214.8** | **8.7** |
| Nchi nyinginezo | 92.0 | 179.4 | 145.5 | 80.7 | 153.2 | 89.8 |
| **JUMLA KUU (CIF)** | **10,849.9** | **15,654.5** | **15,117.5** | **15,593.0** | **16,234.4** | **4.1** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
*Badiliko linazidi asilimia 100

**Mizania ya Malipo na Nchi za Nje**

**Urari wa Malipo Yote**

110. Mwaka 2025, urari wa malipo yote ya nje ya nchi ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 968.9 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 70.1 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma.

**Urari wa Biashara ya Bidhaa**

111. Mwaka 2025, urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 4,524.8 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 5,074.0 mwaka 2024, sawa na upungufu wa nakisi kwa asilimia 11.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kasi ya mauzo ya bidhaa nje, hususan dhahabu, tumbaku, kahawa na bidhaa za viwandani, ikilinganishwa na kasi ya ongezeko la uagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi.

**Urari wa Biashara ya Huduma**

112. Mwaka 2025, urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 4,235.7 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 4,051.7 mwaka 2024, sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 4.5. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii na huduma za usafirishaji.

**Urari wa Biashara ya Bidhaa na Huduma**

113. Mwaka 2025, urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 289.1 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,022.3 mwaka 2024, sawa na upungufu wa nakisi kwa asilimia 71.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ziada ya urari wa biashara ya huduma pamoja na kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa.

**Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi**

114. Mwaka 2025, urari wa mapato ya vitega uchumi unaojumuisha malipo yatokanayo na ajira kwa wafanyakazi, mapato ya uwekezaji na malipo ya riba ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,050.1 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,887.4 mwaka 2024, sawa na ongezeko la nakisi kwa asilimia 8.6. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa malipo ya riba ya mikopo na gawio.

**Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida**

115. Mwaka 2025, urari wa uhamisho mali wa kawaida unaojumuisha uhamisho wa fedha unaofanywa na sekta binafsi, misaada na unafuu wa kulipa deni ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 289.9 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 529.9 mwaka 2024, sawa na upungufu wa ziada kwa asilimia 45.3.

**Urari wa Malipo ya Kawaida**

116. Mwaka 2025, urari wa malipo ya kawaida unaojumuisha biashara ya bidhaa, huduma, mapato ya vitega uchumi na uhamisho mali wa kawaida ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,049.4 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,379.8 mwaka 2024, sawa na upungufu wa nakisi kwa asilimia 13.9. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa nje, mapato ya huduma pamoja na kupungua kwa gharama za uagizaji wa bidhaa kutoka nje, hususan bidhaa za petroli.

**Urari wa Uhamisho wa Mitaji**

117. Mwaka 2025, urari wa uhamisho wa mitaji unaojumuisha misaada ya vitega uchumi na misamaha ya madeni ya nje kutoka kwa mashirika ya fedha ya kimataifa na nchi wahisani ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 348.9 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 318.7 mwaka 2024, sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 9.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Urari wa Uwekezaji**

118. Mwaka 2025, urari wa malipo katika uwekezaji unaojumuisha uwekezaji wa moja kwa moja na mikopo ya fedha kutoka nje ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 3,070.1 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 2,174 mwaka 2024, sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 41.2. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa uwekezaji wa moja kwa moja katika hisa na miradi ya maendeleo.

**Akiba ya Fedha za Kigeni**

119. Hadi Desemba 2025, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 6,329 kutoka dola za Marekani milioni 5,546.9 kipindi kama hicho mwaka 2024. Kiasi hicho kilitosheleza malipo ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.9. Kiwango hicho ni zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.0 na Jumuiya ya Afrika Mashariki isiyopungua miezi 4.5.

**Jedwali Na. 31: THAMANI YA BIASHARA YA BIDHAA BAINA YA TANZANIA NA NCHI NYINGINE, MWAKA 2020 - 2025**

**Shilingi Milioni**

| Aina ya Bidhaa | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Zilizouzwa Nje | 14,620,151 | 15,523,687 | 16,639,962 | 18,388,713 | 23,775,150 | 25,892,845 |
| Bidhaa Halisi | 13,706,747 | 14,476,957 | 15,418,594 | 17,059,277 | 22,053,264 | 24,790,476 |
| Zilizouzwa Tena | 201,233 | 207,226 | 302,281 | 321,494 | 626,859 | 332,398 |
| Zilizoagizwa | 19,428,048 | 24,928,264 | 36,061,025 | 36,108,449 | 40,545,861 | 41,068,891 |
| Urari | -4,807,897 | -9,404,577 | -19,421,063 | -17,719,736 | -16,770,711 | -15,176,046 |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 32: KIASI NA THAMANI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NJE YA NCHI, MWAKA 2020 - 2025**

| Kiasi (000'Tani) | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** | **Badiliko (Asilimia)** |
| Kahawa | 64.0 | 68.0 | 55.2 | 84.4 | 82.2 | 70.8 | -13.8 |
| Pamba | 72.6 | 48.8 | 48.9 | 69.6 | 52.6 | 66.3 | 26.0 |
| Katani | 11.2 | 12.6 | 14.9 | 12.5 | 21.2 | 24.1 | 13.5 |
| Chai | 24.1 | 24.2 | 21.1 | 22.2 | 15.7 | 10.8 | -31.1 |
| Tumbaku | 42.6 | 37.7 | 49.3 | 82.0 | 108.5 | 119.2 | 9.9 |
| Korosho | 320.9 | 154.4 | 234.0 | 219.6 | 428.3 | 338.9 | -20.9 |
| Karafuu | 3.6 | 7.0 | 5.9 | 4.7 | 2.8 | 3.3 | 17.2 |
| Almasi (Carat) | 154,331.1 | 58,163.4 | 313,143.7 | 201,923.0 | 383,698.4 | 487,638.5 | 27.1 |
| Dhahabu( gms) | 66,871,114.9 | 59,392,496.2 | 64,091,782.5 | 79,706,632.9 | 57,591,069.6 | 61,186,629.9 | 6.2 |
| 1 Carat = 200 milligrams | | | | | | | |
| **Thamani (Shilingi Milioni)** | | | | | | | |
| **Bidhaa** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** | **Badiliko (Asilimia)** |
| Kahawa | 333,113 | 356,557 | 371,288 | 545,332 | 762,929 | 901,461 | 18.2 |
| Pamba | 200,797 | 186,844 | 238,317 | 247,138 | 181,135 | 246,306 | 36.0 |
| Katani | 40,270 | 46,358 | 56,062 | 48,335 | 61,037 | 87,597 | 43.5 |
| Chai | 74,356 | 75,550 | 69,124 | 73,612 | 50,323 | 37,024 | -26.4 |
| Tumbaku | 341,133 | 292,867 | 411,542 | 828,228 | 1,334,712 | 1,388,276 | 4.0 |
| Korosho | 824,866 | 365,040 | 523,031 | 509,196 | 1,398,470 | 974,927 | -30.3 |
| Karafuu | 39,110.1 | 119,004.8 | 97,083.7 | 61,214.8 | 43,669.5 | 55,036.2 | 26.0 |
| Almasi (Carat) | 46,312 | 19,546 | 144,514 | 57,347 | 139,489 | 112,293 | -19.5 |
| Dhahabu( gms) | 6,786,265 | 6,289,142 | 6,530,001 | 7,301,344 | 8,896,276 | 12,013,444 | 35.0 |


**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 33: KIASI NA THAMANI YA BIDHAA ZA ASILIA NA ZISIZO ZA ASILIA ZILIZOUZWA NJE YA NCHI, MWAKA 2020 - 2025**


| | Kiasi (000" Tani) | | | | | | Badiliko (Asilimia) | Thamani (Dola za Marekani Milioni) | | | | | | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** | **2023/24** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** | **2023/24** |
| **Bidhaa Asilia** | | | | | | | | | | | | | | |
| Kahawa | 64 | 68 | 55.2 | 84.4 | 82.2 | 70.8 | -2.6 | 145.2 | 155.2 | 161.2 | 227.9 | 292.9 | 361.3 | 23.4 |
| Pamba | 72.6 | 48.8 | 48.9 | 69.6 | 52.6 | 66.3 | -24.4 | 87.5 | 81.3 | 103.4 | 101.9 | 69.3 | 99.1 | 43.0 |
| Katani | 11.2 | 12.6 | 14.9 | 12.5 | 21.2 | 24.1 | 69.6 | 17.6 | 20.2 | 24.3 | 20.4 | 23.4 | 34.5 | 47.6 |
| Chai | 24.1 | 24.2 | 21.1 | 22.2 | 15.7 | 10.8 | -29.1 | 32.4 | 32.9 | 30 | 31.1 | 19.4 | 14.5 | -25.5 |
| Tumbaku | 42.6 | 37.7 | 49.3 | 82 | 108.5 | 119.2 | 32.3 | 148.7 | 127.5 | 178.5 | 340.5 | 509.5 | 561.1 | 10.1 |
| Korosho | 320.9 | 154.4 | 234 | 219.6 | 428.3 | 338.9 | 95 | 359.6 | 159 | 226.9 | 206.4 | 541.7 | 398.8 | -26.4 |
| Karafuu | 3.6 | 7 | 5.9 | 4.7 | 2.8 | 3.3 | -39.6 | 17.1 | 51.8 | 42.1 | 25.1 | 17.1 | 22.5 | 31.5 |
| **Jumla** | | | | | | | | **808.1** | **627.9** | **766.5** | **953.3** | **1,473.3** | **1,491.9** | **1.3** |
| **Bidhaa zisizo asilia** | | | | | | | | | | | | | | |
| Madini | | | | | | | | 3,375.0 | 3,116.4 | 3,395.3 | 3,551.4 | 4,119.9 | 5,401.9 | 31.1 |
| Bidhaa za Viwanda | | | | | | | | 902.7 | 1,200.0 | 1,419.2 | 1,363.3 | 1,341.3 | 1,595.8 | 19.0 |
| Samaki na Mazao ya Samaki | | | | | | | | 139.6 | 164.3 | 168.2 | 164.0 | 180.6 | 161.2 | -10.7 |
| Mazao ya Mboga na Maua | | | | | | | | 274.1 | 378.6 | 289.6 | 417.2 | 507.0 | 443.6 | -12.5 |
| Bidhaa zilizouzwa tena | | | | | | | | 87.7 | 90.2 | 131.2 | 135.2 | 240.8 | 130.9 | -45.6 |
| Bidhaa nyinginezo | | | | | | | | 474.2 | 813.5 | 654.9 | 690.5 | 839.2 | 731.2 | -12.9 |
| **Jumla** | | | | | | | | **5,253.3** | **5,763.0** | **6,058.4** | **6,321.6** | **7,228.8** | **8,464.5** | **17.1** |
| Bidhaa Zisizorekodiwa | | | | | | | | 310.4 | 365.4 | 399 | 421.6 | 419.6 | 306.6 | -0.5 |
| **Jumla Kuu** | | | | | | | | **6,371.7** | **6,756.2** | **7,223.8** | **7,696.6** | **9,121.6** | **10,262.9** | **18.5** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo Na. 4.3: THAMANI YA BIDHAA ZILIZOUZWA NJE YA NCHI MWAKA 2020 - 2025**



**Kielelezo Na. 4.4: MCHANGO WA BIDHAA KATIKA MAUZO NJE YA NCHI MWAKA 2025 (Asilimia)**



**Jedwali Na. 34: WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE YA NCHI, MWAKA 2020 - 2025**

| Bidhaa | (Shilingi/Tani*) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
| Kahawa | 5,205,124 | 5,248,924 | 6,723,911 | 6,433,589 | 9,257,809 | 12,950,686 | 39.9 |
| Pamba | 2,767,587 | 3,825,827 | 4,866,797 | 3,486,004 | 3,423,213 | 3,794,097 | 10.8 |
| Katani | 3,593,150 | 3,676,368 | 3,751,967 | 3,880,245 | 2,863,138 | 3,641,161 | 27.2 |
| Chai | 3,086,856 | 3,116,943 | 3,271,126 | 3,343,553 | 3,207,588 | 3,381,916 | 5.4 |
| Tumbaku | 8,016,254 | 7,769,878 | 8,346,508 | 9,887,596 | 12,196,880 | 11,944,810 | -2.1 |
| Korosho | 2,570,875 | 2,367,306 | 2,233,860 | 2,238,988 | 3,284,987 | 2,986,404 | -9.1 |
| Karafuu | 10,943,125 | 16,883,010 | 16,360,839 | 12,760,591 | 15,613,008 | 17,147,572 | 9.8 |
| Almasi (Shilingi/ carat) | 300,079 | 336,053 | 461,493 | 284,003 | 363,537 | 230,280 | -36.7 |
| Dhahabu (Shilingi/gramu) | 101,483 | 105,891 | 101,885 | 91,603 | 154,473 | 196,341 | 27 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania
*Isipokuwa kwa almasi na dhahabu

**Jedwali Na. 35: WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NJE YA NCHI, MWAKA 2017 - 2025**

**USD/Tani***

| **Bidhaa** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | 3,019.2 | 2,633.0 | 1,996.5 | 2,268.9 | 2,284.4 | 2,919.6 | 2,700.8 | 3,564.3 | 5,103.6 | 43.2 |
| Pamba | 1,450.3 | 1,461.1 | 1,162.2 | 1,206.4 | 1,665.0 | 2,113.2 | 1,463.4 | 1,318.0 | 1,495.2 | 13.4 |
| Katani | 1,686.7 | 1,535.6 | 1,581.7 | 1,566.2 | 1,600.0 | 1,629.1 | 1,628.9 | 1,102.3 | 1,434.9 | 30.2 |
| Chai | 1,783.6 | 1,727.4 | 1,444.2 | 1,345.5 | 1,356.5 | 1,420.3 | 1,403.6 | 1,234.9 | 1,332.7 | 7.9 |
| Tumbaku | 4,055.6 | 3,648.6 | 3,440.9 | 3,494.2 | 3,381.5 | 3,624.1 | 4,150.8 | 4,695.9 | 4,707.2 | 0.2 |
| Korosho | 1,607.5 | 1,580.6 | 1,194.6 | 1,120.6 | 1,030.3 | 970.0 | 939.9 | 1,264.7 | 1,176.9 | -6.9 |
| Karafuu | 7,865.1 | 4,384.6 | 5,047.8 | 4,770.0 | 7,347.6 | 7,104.0 | 5,356.9 | 6,011.1 | 6,757.5 | 12.4 |
| Almasi (kwa carat) | 227.5 | 200.1 | 137.8 | 131.0 | 179.6 | 204.7 | 116.7 | 143.9 | 193.6 | 34.5 |
| Dhahabu (kwa gramu) | 28.1 | 25.1 | 27.3 | 44.0 | 46.0 | 44.2 | 38.4 | 60.7 | 63.5 | 4.6 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania

*Isipokuwa kwa almasi na dhahabu


## Jedwali Na. 36: MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE MWAKA 2020 - 2025

**Dola za Marekani Milioni**

| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025p |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Urari wa Biashara** | **-1,460.0** | **-3,247.1** | **-6,984.9** | **-6,032.3** | **-5,074.0** | **-4,524.8** |
| Zilizouzwa nje (fob) | 6,371.7 | 6,756.2 | 7,223.8 | 7,696.6 | 9,121.6 | 10,262.9 |
| Zilizonunuliwa toka nje (fob)* | 7,831.7 | 10,003.4 | 14,208.7 | 13,728.9 | 14,195.6 | 14,787.7 |
| **Urari wa Huduma** | **864.7** | **1,510.7** | **2,296.6** | **3,835.9** | **4,051.7** | **4,235.7** |
| Mapato | 2,183.8 | 3,117.7 | 4,762.0 | 6,231.7 | 6,846.8 | 7,477.5 |
| Malipo | 1,319.0 | 1,607.0 | 2,465.4 | 2,395.9 | 2,795.0 | 3,241.8 |
| **Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi** | **-1,264.5** | **-1,191.6** | **-1,393.2** | **-1,496.6** | **-1,887.4** | **-2,050.1** |
| Yaliyoingia | 111.2 | 102.5 | 183.9 | 301.2 | 311.7 | 306.2 |
| Yaliyotoka | 1,375.7 | 1,294.2 | 1,577.1 | 1,797.7 | 2,199.2 | 2,356.3 |
| **Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida** | **401.2** | **553.7** | **599.3** | **732.5** | **529.9** | **289.9** |
| Iliyoingia | 453.9 | 640.1 | 716.5 | 1,280.9 | 1,177.4 | 899.1 |
| Serikalini | 141.2 | 104.7 | 76.4 | 131.0 | 139.2 | 19.7 |
| Sekta nyingine | 312.7 | 535.4 | 640.2 | 1,150.0 | 1,038.3 | 879.4 |
| Iliyotoka | 52.7 | 86.4 | 117.2 | 548.4 | 647.5 | 609.2 |
| **Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali** | **-1,458.5** | **-2,374.3** | **-5,482.2** | **-2,960.6** | **-2,379.8** | **-2,049.4** |
| **Urari wa Uhamisho wa Mitaji** | **344.3** | **412.1** | **274.0** | **298.2** | **318.7** | **355.1** |
| Iliyoingia | 344.3 | 412.1 | 274.0 | 298.2 | 318.7 | 355.1 |
| Iliyotoka | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| **Urari katika uwekezaji** | **682.7** | **4,037.7** | **3,637.5** | **3,530.1** | **1,874.8** | **2,330.1** |
| Uwekezaji katika miradi | 943.8 | 1,190.5 | 1,437.6 | 1,648.9 | 1,656.0 | 1,850.4 |
| Uwekezaji katika hisa | -3.6 | -7.9 | 24.6 | 13.9 | -26.1 | -52.4 |
| Uwekezaji aina nyingine | -257.5 | 2,855.1 | 2,175.3 | 1,867.2 | 244.9 | 532.1 |
| Makosa na Masahihisho | -333.3 | -223.4 | 582.3 | -890.2 | 256.4 | 312.9 |
| **Urari wa Malipo yote** | **-764.9** | **1,852.1** | **-988.4** | **-22.5** | **70.1** | **968.9** |

**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo Na. 4.5: MWENENDO WA MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE (Dola za Marekani Milioni), MWAKA 2019 - 2025**



# SURA YA 5

# HALI YA UCHUMI WA DUNIA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

## HALI YA UCHUMI WA DUNIA

### Ukuaji wa Uchumi

120. Mwaka 2025, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.4 kama ilivyokuwa mwaka 2024 (**Jedwali Na. 5.1**). Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji kulikotokana na uwekezaji katika teknolojia ikiwemo matumizi ya akili unde pamoja na hatua zilizochukuliwa na nchi mbalimbali katika kukabiliana na mabadiliko ya sera za biashara.

121. Mwaka 2025, kasi ya ukuaji wa Pato la nchi zilizoendelea iliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 1.9 ikilinganishwa na asilimia 1.8 mwaka 2024. Kuongezeka kwa ukuaji kulichangiwa na kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi katika nchi hizo kufuatia kupungua kwa athari za majanga yanayokabili uchumi wa dunia. Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2024. Vilevile, ukuaji wa Pato la nchi za Asia zinazoibukia na zinazoendelea kiuchumi ikijumuisha China na India ulikuwa wastani wa asilimia 5.5 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 5.4 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo nje pamoja na sera madhubuti za fedha zilizosababisha kuimarika kwa thamani ya sarafu katika baadhi ya nchi hizo ikilinganishwa na dola ya Marekani.

122. Mwaka 2025, ukuaji wa uchumi kwa Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.5 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilichangiwa na maboresho ya sera za kiuchumi, kupungua kwa bei za bidhaa, hususan mafuta pamoja na kuongezeka kwa mauzo nje kwa baadhi ya nchi.

**Jedwali Na. 5.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia, Mwaka 2021 - 2025**

| Kundi/Mwaka | Ukuaji Halisi (Asilimia) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
| Dunia | 6.7 | 3.8 | 3.3 | 3.4 | 3.4 |
| Nchi Zilizoendelea | 6.1 | 3.1 | 1.7 | 1.8 | 1.9 |
| Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea | 7.0 | 4.3 | 4.4 | 4.5 | 4.4 |
| Nchi za Asia Zinazoibukia na Zinazoendelea | 7.8 | 4.7 | 5.6 | 5.4 | 5.5 |
| Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara | 3.9 | 4.4 | 3.8 | 4.2 | 4.5 |

**Chanzo:** Shirika la Fedha la Kimataifa, *World Economic Outlook* (WEO), Aprili 2026

123. Mwaka 2025, nchi iliyoongoza kwa ukuaji wa Pato la Taifa kwa upande wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC ilikuwa Zimbabwe iliyokuwa na ukuaji wa asilimia 7.5 ikifuatiwa na Tanzania asilimia 5.9 na DRC asilimia 5.7 ikilinganishwa na

ukuaji wa asilimia 1.7, asilimia 5.6 na asilimia 6.1 mtawalia mwaka 2024. Aidha, kwa upande wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC, Sudani Kusini iliongoza kwa kuwa na ukuaji wa asilimia 46.1 ikifuatiwa na Rwanda (asimilia 7.0), Uganda (asilimia 6.7) na Tanzania (asilimia 5.9) ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia -26.1, asilimia 7.2, asilimia 6.0 na asilimia 5.6 mtawalia mwaka 2024 (**Jedwali Na. 5.2**). Ongezeko la ukuaji katika nchi hizo lilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo nje, uwekezaji katika miundombinu ya kiuchumi pamoja na jitihada za kutatua migogoro ya kisiasa katika nchi ya Sudan Kusini kulikosababisha kuimarika kwa uchumi. Aidha, kiwango kikubwa cha ukuaji wa uchumi wa Sudani Kusini kilitokana na msingi wa uchumi wa taifa hilo ambao ulitoka kwenye hali ya mdororo (contraction) wa ukuaji hasi wa asilimia 26.1 mwaka 2024.

**Jedwali Na. 5.2: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi za SADC na EAC, Mwaka 2021 - 2025**

| Nchi/Mwaka | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Ukuaji wa Nchi za SADC** | | | | | |
| Angola | 2.1 | 4.2 | 1.3 | 5.0 | 3.1 |
| Botswana | 11.9 | 5.5 | 3.2 | -3.0 | -0.9 |
| Comoros | 2.0 | 2.6 | 3.0 | 3.3 | 3.8 |
| Tanzania* | 4.9 | 4.6 | 5.2 | 5.6 | 5.9 |
| DRC | 6.4 | 9.3 | 8.5 | 6.1 | 5.7 |
| Eswatini | 4.2 | 0.4 | 3.5 | 3.0 | 3.6 |
| Lesotho | 4.6 | 1.6 | 2.5 | 4.9 | 1.4 |
| Madagascar | 4.7 | 4.1 | 4.2 | 4.3 | 2.8 |
| Malawi | 4.6 | 0.9 | 1.9 | 1.7 | 2.1 |
| Mauritius | 3.4 | 8.7 | 5.0 | 4.9 | 3.1 |
| Msumbiji | 2.4 | 4.4 | 5.5 | 2.1 | -0.5 |
| Namibia | 3.6 | 5.4 | 4.4 | 3.7 | 2.4 |
| Seychelles | 0.6 | 9.9 | 5.2 | 3.4 | 5.1 |
| Afrika Kusini | 4.9 | 2.1 | 0.8 | 0.5 | 1.1 |
| Zambia | 6.2 | 5.2 | 5.4 | 3.8 | 3.8 |
| Zimbabwe | 8.5 | 6.1 | 5.3 | 1.7 | 7.5 |
| **Ukuaji wa Nchi za EAC** | | | | | |
| Burundi | 3.1 | 1.8 | 2.7 | 4.1 | 3.9 |
| Kenya | 7.6 | 4.9 | 5.7 | 4.7 | 4.9 |
| Rwanda | 8.4 | 9.8 | 8.6 | 7.2 | 7.0 |
| Somalia | 3.5 | 2.7 | 4.2 | 4.1 | 3.0 |
| Sudan Kusini | 5.3 | -5.2 | 3.0 | -26.1 | 46.1 |
| Tanzania* | 4.9 | 4.6 | 5.2 | 5.6 | 5.9 |
| Uganda | 5.5 | 6.2 | 5.0 | 6.0 | 6.7 |
| DRC | 6.4 | 9.3 | 8.5 | 6.1 | 5.7 |

**Chanzo:** Shirika la Fedha la Kimataifa, *World Economic Outlook* (WEO), Aprili 2026
*Takwimu za NBS zimetumika badala ya takwimu za IMF kwa kuwa zilitolewa kabla NBS haijatoa takwimu rasmi za mwaka mpya wa kizio wa 2019

**Mwenendo wa Bei**

124. Mwaka 2025, mfumuko wa bei wa dunia ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 4.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.8 mwaka 2024. Kupungua kwa kasi ya mfumuko wa bei kulitokana na nchi mbalimbali kuendelea kutekeleza sera za fedha zilizolenga kupunguza ongezeko la ukwasi pamoja na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia ikiwemo bidhaa za mafuta.

125. Mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea ulifikia wastani wa asilimia 2.7 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.9 mwaka 2024. Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi za Ulaya zinazoibukia na zinazoendelea ulikuwa wastani wa asilimia 13.5 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 17.2 mwaka 2024. Vilevile, mfumuko wa bei kwa nchi za Asia zinazoibukia na zinazoendelea ulikuwa wastani wa asilimia 1.1 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.9 mwaka 2024.

126. Mwaka 2025, mfumuko wa bei kwa Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 12.5 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 20.7 mwaka 2024. Katika kipindi hicho, nchi wanachama wa SADC iliyokuwa na wastani mkubwa wa mfumuko wa bei ilikuwa Zimbabwe ikiwa na wastani wa asilimia 81.4 ikifuatia na Malawi (asilimia 28.4) na Angola (asilimia 20.2) ikilinganishwa na wastani wa asilimia 736.1, asilimia 32.2 na asilimia 28.2 mtawalia, mwaka 2024. Pamoja na kuwa na viwango vikubwa vya mfumuko wa bei mwaka 2025, kasi ya kupanda kwa wastani wa bei ilipungua ikilinganishwa na mwaka 2024. Kwa upande wa Nchi Wanachama wa EAC, nchi za Sudani ya Kusini na Burundi zilikuwa na wastani wa juu wa mfumuko wa bei wa asilimia 97.6 na asilimia 34.2 mtawalia mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 99.8 na 20.2 mwaka 2024 (**Jedwali Na. 5.3**).

**Jedwali Na. 5.3: Mfumuko wa Bei Nchi za SADC na EAC, Mwaka 2021 - 2025**

| Nchi | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mfumuko wa Bei wa Nchi za SADC (Asilimia)** | | | | | |
| Angola | 25.8 | 21.4 | 13.6 | 28.2 | 20.2 |
| Botswana | 6.7 | 12.2 | 5.1 | 2.8 | 2.8 |
| Comoros | 0.0 | 12.4 | 8.5 | 5 | 3.2 |
| Tanzania | 3.7 | 4.4 | 3.8 | 3.1 | 3.3 |
| DRC | 9.0 | 9.3 | 19.9 | 17.7 | 7.4 |
| Eswatini | 3.7 | 4.8 | 4.9 | 4.0 | 3.1 |
| Lesotho | 6.5 | 8.2 | 6.5 | 5.2 | 4.4 |
| Madagascar | 5.8 | 8.2 | 9.9 | 7.6 | 8.0 |
| Malawi | 9.3 | 20.8 | 28.8 | 32.2 | 28.4 |
| Mauritius | 4.0 | 10.8 | 7.0 | 3.6 | 3.7 |
| Msumbiji | 6.6 | 10.4 | 7.0 | 3.2 | 4.4 |
| Namibia | 3.6 | 6.1 | 5.9 | 4.2 | 3.5 |
| Seychelles | 9.8 | 2.6 | -1.0 | 0.3 | 0.3 |
| Afrika Kusini | 4.6 | 6.9 | 5.9 | 4.4 | 3.2 |
| Zambia | 22.0 | 11.0 | 10.9 | 15.0 | 13.9 |
| Zimbabwe | 98.5 | 193.4 | 667.4 | 736.1 | 81.4 |
| **Mfumuko wa Bei wa Nchi za EAC (Asilimia)** | | | | | |
| Tanzania | 3.7 | 4.4 | 3.8 | 3.1 | 3.3 |
| Uganda | 2.2 | 7.2 | 5.4 | 3.3 | 3.6 |
| Kenya | 6.1 | 7.6 | 7.7 | 4.5 | 4.1 |
| Rwanda | 0.8 | 13.9 | 14.0 | 4.8 | 7.0 |
| Burundi | 8.4 | 18.9 | 27.1 | 20.2 | 34.2 |
| Sudani ya Kusini | 30.2 | -3.2 | 39.7 | 99.8 | 97.6 |
| Somalia | 4.6 | 6.8 | 6.2 | 5.5 | 3.7 |
| DRC | 9.0 | 9.3 | 19.9 | 17.7 | 7.4 |

**Chanzo**: Shirika la Fedha la Kimataifa, *World Economic Outlook* (WEO), Aprili 2026

**Mwenendo wa Biashara Duniani**

127. Mwaka 2025, biashara ya bidhaa duniani ilikua kwa asilimia 4.6 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.7 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa matumizi ya akili unde katika uzalishaji na biashara ya bidhaa iliyopunguza athari hasi za sera za biashara zisizotabirika pamoja na ongezeko la ushuru. Vilevile, biashara ya huduma ilikua kwa asilimia 5.3 mwaka 2025 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.8 mwaka 2024. Hii ilitokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa huduma za usafiri na utalii kufuatia kurejea katika mwenendo wa kawaida wa shughuli hizo kabla ya UVIKO - 19.

128. Mwaka 2025, uuzaji wa bidhaa nje ya Bara la Ulaya ulikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 0.5 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 1.9 mwaka 2024. Aidha, uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya Bara la Ulaya ulikuwa na ukuaji wa asilimia 2.1 mwaka 2025 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 2.0 mwaka 2024. Kwa upande mwingine, uuzaji

wa bidhaa nje ya Bara la Asia ulikua kwa asilimia 9.5 mwaka 2025 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.3 mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kuendelea kuongezeka kwa uuzaji wa bidhaa kutoka nchi ya China kwenda nchi nyingine za Asia, Ulaya na nchi zinazoibukia kulikopunguza athari hasi za kupungua kwa uuzaji wa bidhaa nchini Marekani. Katika kipindi hicho, uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya Bara la Asia ulikua kwa asilimia 6.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.8 mwaka 2024.

129. Mwaka 2025, uuzaji wa bidhaa nje ya Bara la Afrika ulikuwa na ukuaji wa asilimia 10.3 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 2.0 mwaka 2024. Ongezeko la uuzaji wa bidhaa nje ya Bara la Afrika lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya kakao, kahawa, chai, dhahabu, mbolea na malighafi za chuma. Kwa upande mwingine, uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya Bara la Afrika ulikua kwa asilimia 8.7 mwaka 2025 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.5 mwaka 2024 (**Jedwali Na. 5.4**). Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa meli/boti, magari, mafuta ya mimea na wanyama na mitambo.

**Jedwali Na. 5.4: Mwenendo wa Biashara ya Bidhaa Duniani, Mwaka 2022 - 2025**

| **Kundi/Mwaka** | **Ukuaji Halisi (Asilimia)** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
| Dunia | 2.3 | -0.9 | 2.7 | 4.6 |
| **Uuzaji wa bidhaa nje** | | | | |
| Bara la Ulaya | 2.2 | -2.9 | -1.9 | -0.5 |
| Bara la Asia | 0.4 | 0.2 | 8.3 | 9.5 |
| Afrika | -2.4 | 5.8 | -2.0 | 10.3 |
| **Uagizaji wa bidhaa kutoka nje** | | | | |
| Bara la Ulaya | 4.5 | -4.9 | -2.0 | 2.1 |
| Bara la Asia | -0.8 | -0.7 | 4.8 | 6.0 |
| Bara la Afrika | 6.2 | 2.8 | 1.5 | 8.7 |

**Chanzo:** Shirika la Biashara Duniani (WTO), Machi 2026

## USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

### Ushirikiano wa Uchumi Kimataifa

130. Mwaka 2025, Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uhalifu wa Kimtandao (Hanoi Convention) ulitiwa saini jijini Hanoi, Vietnam. Aidha, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitia saini Mkataba huo kuunga mkono juhudi za kimataifa za kupambana na uhalifu wa kimtandao. Hatua hii inaashiria dhamira ya Tanzania katika kuimarisha usalama wa kidijitali, kulinda mifumo ya Serikali na sekta binafsi, na kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa katika kukabiliana na uhalifu wa kimtandao unaoathiri biashara na huduma za kijamii.

131. Mwaka 2025, Tanzania ilishiriki kwenye Mkutano Mkuu wa 43 wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni - UNESCO uliofanyika Samarkand,

Uzbekistan. Katika Mkutano huo, Kiswahili kilipitishwa rasmi kuwa lugha ya Mkutano Mkuu wa UNESCO kuanzia mwaka 2027, hatua ambayo inathibitisha Kiswahili kuwa nyenzo ya kidiplomasia katika nyanja za kimataifa. Aidha, Tanzania ilichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Kimataifa la Usimamizi wa Maeneo ya Hifadhi Hai za UNESCO kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2025 hadi 2029.

132. Mwaka 2025, Tanzania ilishiriki kwenye Kikao cha 25 cha Nchi Wanachama wa Mkataba wa kulinda na kuhifadhi urithi wa utamaduni na asili wa Mwaka 1972, kilichofanyika kwenye Makao Makuu ya UNESCO. Katika kikao hicho, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilichaguliwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Urithi wa Dunia (World Heritage Committee) kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia mwaka 2025 hadi 2029.

133. Mwaka 2025, Tanzania ilishiriki katika Mkutano Mkuu wa Shirika la Utalii Duniani la Umoja wa Mataifa uliofanyika Riyadh, Saudi Arabia. Katika Mkutano huo, Chama cha Waendeshaji Utalii Tanzania - TATO kilipokea Tuzo ya Umoja wa Mataifa ya Utalii pamoja na kutambuliwa kuwa miongoni mwa wanachama washirika 11 pekee duniani kwa kazi bora katika mfumo wa kimataifa wa utalii. Kwa upande mwingine, Tanzania ilichaguliwa kuwa Eneo Bora la Safari Duniani 2025 kwenye hafla ya *World Travel Awards Grand Finals* zilizofanyika nchini Bahrain, Desemba 2025. Katika hafla hiyo, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ilitangazwa kuwa hifadhi bora zaidi duniani mwaka 2025. Aidha, kupitia hafla ya Tuzo za Utalii za Afrika na Bahari ya Hindi iliyofanyika jijini Dar es Salaam, Tanzania ilitambuliwa kama sehemu bora ya utalii barani Afrika.

134. Mwaka 2025, Tanzania ilishiriki katika Mkutano Mkuu wa 69 wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomu uliofanyika Vienna, Austria. Katika Mkutano huo, Tanzania ilipata fursa ya kutoa tamko na kuainisha dhamira yake ya kutumia nyuklia katika kuzalisha nishati, kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na utayari wa nchi katika kutekeleza sera ya Shirika la Kimataifa la Nguvu ya Atomu kuhusu matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia kwa maendeleo endelevu.

135. Mwaka 2025, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 28 wa Umoja wa Posta Duniani - UPU uliofanyika Dubai. Katika Mkutano huo, Tanzania ilishinda nafasi ya mjumbe wa Baraza la Utawala na Baraza la Uendeshaji wa Huduma za Posta. Aidha, Tanzania ilichaguliwa kuwa mjumbe wa Bodi ya Mfuko wa Ubora wa Huduma kuanzia mwaka 2025 hadi 2028.

136. Mwaka 2025, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa Maendeleo ya Mawasiliano Duniani uliofanyika mjini Baku, Azerbaijan. Katika Mkutano huo, Tanzania ilishinda nafasi ya Makamu Spika wa Kikundi cha Utafiti cha Shirika la Umoja wa Mataifa la

Mawasiliano Duniani linaloshughulikia Maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano (ITU-D) kuanzia mwaka 2026 hadi 2029.

**Ushirikiano wa Kiuchumi Barani Afrika**

137. Mwaka, 2025 Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Afrika kuhusu Nishati (Mission 300 *Africa Energy Summit*) uliofanyika jijini Dar es Salaam. Mkutano huo ulijadili fursa, changamoto na mustakabali wa maendeleo ya nishati endelevu barani Afrika. Katika mkutano huo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alieleza dhamira ya Tanzania katika kukuza matumizi ya nishati safi na endelevu kwa ajili ya kaya, viwanda na sekta za uzalishaji. Miongoni mwa mafanikio ya Mkutano huo ni kuandaliwa kwa Mipango ya Kitaifa ya Nishati (*National Energy Compacts*) ili kuwezesha upatikanaji wa umeme, kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi na ya umma, na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa kwa ajili ya maendeleo endelevu ya nishati. Aidha, Mkutano wa 38 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika mwezi Februari 2025 uliridhia na kupitisha Azimio la Dar es Salaam kwa kutambua mchango wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuchagiza ajenda ya nishati, hususan nishati safi ya kupikia barani Afrika. Azimio la Dar es Salaam linalenga kuwezesha upatikanaji wa umeme kwa watu milioni 300 barani Afrika ifikapo mwaka 2030 pamoja na kuboresha miundombinu ya umeme, kukuza nishati mbadala na kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi.

138. Mwaka 2025, Tanzania ilishiriki Mkutano wa 17 wa Baraza la Mawaziri wa Eneo Huru la Biashara Afrika - AfCFTA uliofanyika nchini Misri. Katika Mkutano huo kanuni za utambuzi wa uasili wa bidhaa katika nguo, mavazi na uundaji wa magari zilihitimishwa. Kanuni hizo zinalenga kulinda malighafi za ndani huku zikiruhusu uagizaji wa malighafi adimu Afrika. Kupitia Kanuni hizo zaidi ya kampuni 50 za Tanzania zilizokidhi vigezo zilisajiliwa kufanya biashara ndani ya Soko Huru la Biashara Afrika.

139. Mwaka 2025, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji ya Umoja wa Afrika (Continental Africa Water Investment Programme - AU-AIP) uliofanyika jijini Cape Town, Afrika ya Kusini. Katika Mkutano huo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitunukiwa Tuzo ya *Presidential Global Water Changemakers* kwa uongozi wake katika usimamizi wa rasilimali maji, ikiwa ni juhudi za Serikali katika kumtua mwanamke ndoo kichwani.

140. Mwaka 2025, Tanzania iliendelea kushiriki katika majadiliano ya Umoja wa Afrika, ikiwemo kushiriki katika Mkutano wa 38 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia. Katika Mkutano huo, Tanzania iliteuliwa kuwa

mjumbe wa Kamati ya Uongozi ya Umoja wa Afrika na kuwa Makamu Mwenyekiti wa Tatu kutoka Kanda ya Mashariki.

**Ushirikiano wa Kiuchumi Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki**

141. Mwaka 2025, Tanzania ilishiriki Mkutano wa 17 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Nishati, Petroli na Madini la EAC uliofanyika jijini Arusha. Katika Mkutano huo, nchi za Tanzania, Rwanda na Uganda zilisaini Hati ya Makubaliano ya Uendelezaji wa Mradi wa Kufua Umeme wa Nsongezi utakaozalisha megawati 39 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera. Kwa upande mwingine, Tanzania ilishiriki katika Kongamano na Maonesho ya 11 ya Petroli ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika jijini Dar es Salaam. Tanzania ilitumia Kongamano hilo kutangaza duru ya tano ya kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia na kuhamasisha miradi ya kikanda, hususan katika miundombinu ya usafirishaji wa bidhaa za petroli na gesi.

142. Mwaka 2025, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 25 wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Afya wa EAC. Katika Mkutano huo, Tanzania ilithibitishwa kuwa mwenyeji wa vituo viwili (2) vipya vya Kikanda vya Umahiri wa Elimu ya Juu ya Matibabu, Huduma za Afya na Utafiti, ikiwemo Kituo cha Umahiri wa Sayansi ya Afya ya Kinywa na Meno kinachosimamiwa na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, na Kituo cha Umahiri wa Sayansi ya Upandikizaji Uloto na Magonjwa ya Damu kinachosimamiwa na Hospitali ya Benjamin Mkapa.

143. Mwaka 2025, Tanzania ilishiriki kwenye Maonesho ya 25 ya Wajasiriamali Wadogo na wa Kati wa EAC yaliyofanyika Nairobi, Kenya, yaliyoshirikisha wajasiriamali 271 kutoka Tanzania. Bidhaa zilizouzwa zilijumuisha nguo, bidhaa za kilimo kama viungo vya chakula, ungalishe, unga wa nafaka, mvinyo, asali, ngozi, tibalishe, korosho, bidhaa za ufundi, sanaa za uchoraji, mwani, samaki na dagaa. Aidha, Tanzania ilitangazwa mshindi wa jumla katika Maonesho hayo.

144. Mwaka 2025, EAC iliandaa na kupitisha Kanuni za Usimamizi wa Himaya Moja ya Forodha ili kurahisisha biashara miongoni mwa nchi wanachama kwa kuhakikisha taratibu za forodha zimekamilika kabla ya mzigo kufika mipakani. Aidha, viwango 96 vya ubora viliwianishwa na kutambulika kama viwango vya ubora vya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuondoa vikwazo vya biashara vya kiufundi.Viwango hivyo vilijumuisha viwango vya mazao ya kilimo pamoja na vilainishi vya magari na mitambo.

**Ushirikiano wa Kiuchumi katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika**

145. Mwaka 2025, Tanzania ilishiriki Mkutano wa Kwanza wa Pamoja wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa EAC na SADC uliofanyika jijini Dar es Salaam kujadili hali ya ulinzi na usalama Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Katika Mkutano huo, Wakuu wa Nchi na Serikali walisisitiza umuhimu wa kusitisha mapigano na kutumia njia

za kidiplomasia kutatua mgogoro huo, ikiwemo usuluhishi kupitia EAC na Umoja wa Afrika.

146. Mwaka 2025, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 45 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC uliofanyika Antananarivo, Madagascar. Katika Mkutano huo, Tanzania ilisisitiza utekelezaji wa maazimio ya Mkutano wa Nishati wa Afrika wa Mission 300 kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na washirika wengine wa maendeleo.

**Ushirikiano wa Kiuchumi katika Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu**

147. Mwaka 2025, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa Mawaziri wa Afya kuhusu uzalishaji wa dawa barani Afrika uliofanyika Algiers, Algeria. Katika mkutano huo, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba ilisaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano na Wakala wa Dawa wa Algeria katika uzalishaji na usambazaji wa dawa. Aidha, Bohari ya Dawa ilianzisha ushirikiano na kampuni tano (5) za dawa hatua itakayoimarisha uzalishaji na upatikanaji wa dawa nchini.

# SURA YA 6

# RASILIMALI WATU

**Idadi ya Watu**

148. Mwaka 2025, idadi ya watu Tanzania ilikadiriwa kuwa 68,153,004 ikilinganishwa na watu 66,278,276 mwaka 2024. Kati ya hao, Tanzania Bara ilikuwa na watu 66,054,123, sawa na asilimia 96.9 ya watu wote na Tanzania Zanzibar watu 2,098,881 (asilimia 3.1). Aidha, wanawake walikadiriwa kuwa 34,732,602, sawa na asilimia 51.0 ya watu wote na wanaume walikuwa 33,420,402 (asilimia 49.0). Makadirio ya mwaka 2025 ni maoteo ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

**Mgawanyiko wa Watu Kimkoa**

149. Mwaka 2025, Mkoa wa Dar es Salaam ulikadiriwa kuwa na watu 5,874,418 ambayo ni idadi kubwa zaidi, sawa na asilimia 8.9 ya watu wote Tanzania Bara, ikifuatiwa na mkoa wa Mwanza uliokuwa na watu 4,116,854 (asilimia 6.2). Idadi kubwa ya watu katika mkoa wa Dar es Salaam ilitokana na upatikanaji wa fursa mbalimbali za kiuchumi na huduma muhimu za kijamii zilizowavutia watu kuhamia kutoka mikoa mingine. Kwa upande mwingine, Mkoa wa Njombe ulikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu wapatao 956,702, sawa na asilimia 1.4 ya watu wote Tanzania Bara. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na idadi kubwa zaidi ya watu wapatao 989,928, sawa na asilimia 47.2 ya watu wote Tanzania Zanzibar. Aidha, Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu wapatao 214,888, sawa na asilimia 10.2 ya watu wote Tanzania Zanzibar.

150. Mwaka 2025, msongamano wa watu Tanzania ulikuwa wastani wa watu 77 kwa kila kilometa ya mraba ikilinganishwa na wastani wa watu 75 kwa kila kilometa ya mraba mwaka 2024. Kwa upande wa Tanzania Bara, msongamano wa watu ulikuwa wastani wa watu 75 kwa kila kilometa ya mraba ikilinganishwa na wastani wa watu 73 kwa kila kilometa ya mraba mwaka 2024. Aidha, Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na msongamano mkubwa zaidi, ukiwa na wastani wa watu 4,217 kwa kila kilometa ya mraba, ikifuatiwa na Mkoa wa Mwanza uliokuwa na wastani wa watu 435 kwa kila kilometa ya mraba. Kwa upande mwingine, Mkoa wa Lindi uliendelea kuwa na msongamano mdogo zaidi wa wastani wa watu 19 kwa kila kilometa ya mraba. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, msongamano wa watu ulikuwa wastani wa watu 853 kwa kila kilometa ya mraba mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa watu 828 kwa kila kilometa ya mraba mwaka 2024. Vilevile, Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na msongamano mkubwa wa wastani wa watu 4,304 kwa kila kilometa ya mraba, ukifuatiwa na Mkoa wa Kusini Pemba uliokuwa na wastani wa watu 914 kwa kila kilometa ya mraba. Kwa upande mwingine, Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na msongamano mdogo zaidi wa wastani wa watu 252 kwa kila kilometa ya mraba.

151. Mwaka 2025, wastani wa idadi ya watu kwa kaya kwa Tanzania ulikuwa watu 4.3 kama ilivyokuwa mwaka 2024 ambao ni sawa na wastani wa Tanzania Bara. Aidha, Mkoa wa Simiyu uliongoza kwa kuwa na wastani wa watu 6.7 kwa kaya na Mkoa wa Mtwara ulikuwa na wastani mdogo zaidi wa watu 3.3 kwa kaya. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, wastani wa idadi ya watu kwa kaya ulikuwa 5.0 mwaka 2025 kama ilivyokuwa mwaka 2024. Mkoa wa Kusini Pemba uliongoza kwa kuwa na wastani mkubwa wa idadi ya watu kwa kaya wa 5.7 na Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na wastani mdogo zaidi wa watu 4.2 kwa kaya kama ilivyokuwa mwaka 2024. **Jedwali Na. 6.1** linaonesha mgawanyo wa idadi ya watu kimkoa Mwaka 2025.

**Jedwali 6.1: Mgawanyo wa Idadi ya Watu Kimkoa Mwaka 2025**

| Mkoa | Idadi ya Watu | | | Uwiano Kijinsia | Msongamano wa Watu | Idadi ya Kaya | Wastani wa Idadi ya Watu kwa Kaya |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jumla | Wanaume | Wanawake | | | | |
| **Tanzania** | **68,153,004** | **33,420,402** | **34,732,602** | **96.2** | **77** | **15,749,151** | **4.3** |
| **Tanzania Bara** | **66,054,123** | **32,395,734** | **33,658,389** | **96.2** | **75** | **15,327,103** | **4.3** |
| Dodoma | 3,389,537 | 1,670,943 | 1,718,594 | 97.2 | 82 | 832,461 | 4.1 |
| Arusha | 2,593,834 | 1,252,501 | 1,341,333 | 93.4 | 69 | 677,210 | 3.8 |
| Kilimanjaro | 2,018,855 | 989,747 | 1,029,108 | 96.2 | 152 | 539,808 | 3.7 |
| Tanga | 2,861,741 | 1,406,476 | 1,455,265 | 96.6 | 107 | 695,320 | 4.1 |
| Morogoro | 3,488,328 | 1,731,277 | 1,757,051 | 98.5 | 49 | 905,482 | 3.9 |
| Pwani | 2,195,974 | 1,089,647 | 1,106,327 | 98.5 | 67 | 588,774 | 3.7 |
| Dar es Salaam | 5,874,418 | 2,851,589 | 3,022,829 | 94.3 | 4,217 | 1,691,344 | 3.5 |
| Lindi | 1,286,839 | 629,640 | 657,199 | 95.8 | 19 | 374,225 | 3.4 |
| Mtwara | 1,772,766 | 847,796 | 924,970 | 91.7 | 106 | 534,660 | 3.3 |
| Ruvuma | 2,030,461 | 996,472 | 1,033,989 | 96.4 | 32 | 512,694 | 4.0 |
| Iringa | 1,285,523 | 624,015 | 661,508 | 94.3 | 36 | 346,932 | 3.7 |
| Mbeya | 2,556,431 | 1,238,113 | 1,318,318 | 93.9 | 68 | 687,279 | 3.7 |
| Singida | 2,231,481 | 1,113,653 | 1,117,828 | 99.6 | 45 | 439,899 | 5.1 |
| Tabora | 3,775,329 | 1,862,562 | 1,912,767 | 97.4 | 50 | 666,376 | 5.7 |
| Rukwa | 1,742,773 | 849,009 | 893,764 | 95 | 76 | 373,352 | 4.7 |
| Kigoma | 2,757,544 | 1,341,079 | 1,416,465 | 94.7 | 74 | 534,675 | 5.2 |
| Shinyanga | 2,483,928 | 1,229,696 | 1,254,232 | 98 | 131 | 469,205 | 5.3 |
| Kagera | 3,322,078 | 1,632,719 | 1,689,359 | 96.6 | 131 | 780,607 | 4.3 |
| Mwanza | 4,116,854 | 2,020,882 | 2,095,972 | 96.4 | 435 | 836,341 | 4.9 |
| Mara | 2,647,733 | 1,285,134 | 1,362,599 | 94.3 | 122 | 525,617 | 5.0 |
| Manyara | 2,098,332 | 1,063,437 | 1,034,895 | 102.8 | 47 | 447,349 | 4.7 |
| Njombe | 956,702 | 455,416 | 501,286 | 90.8 | 45 | 264,994 | 3.6 |
| Katavi | 1,297,568 | 644,439 | 653,129 | 98.7 | 28 | 243,070 | 5.3 |
| Simiyu | 2,425,871 | 1,186,880 | 1,238,991 | 95.8 | 96 | 360,354 | 6.7 |
| Geita | 3,357,323 | 1,663,275 | 1,694,048 | 98.2 | 167 | 633,603 | 5.3 |
| Songwe | 1,485,900 | 719,337 | 766,563 | 93.8 | 66 | 365,472 | 4.1 |
| **Tanzania Zanzibar** | **2,098,881** | **1,024,668** | **1,074,213** | **95.4** | **853** | **422,048** | **5.0** |
| Kaskazini Unguja | 283,792 | 140,108 | 143,684 | 97.5 | 604 | 60,456 | 4.7 |
| Kusini Unguja | 214,888 | 108,136 | 106,752 | 101.3 | 252 | 51,574 | 4.2 |
| Mjini Magharibi | 989,928 | 478,184 | 511,744 | 93.4 | 4,304 | 201,804 | 4.9 |
| Kaskazini Pemba | 306,849 | 149,913 | 156,936 | 95.5 | 535 | 54,780 | 5.6 |
| Kusini Pemba | 303,424 | 148,327 | 155,097 | 95.6 | 914 | 53,434 | 5.7 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Mgawanyo wa Watu kwa Umri Tanzania Bara**


152. Mwaka 2025, watoto wenye umri chini ya miaka mitano walikuwa 11,073,544, sawa na asilimia 16.8 ya watu wote Tanzania Bara. Idadi ya watu wenye umri wa miaka 5 hadi 14 ilikuwa 17,735,920, sawa na asilimia 26.9. Aidha, idadi ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 34 ilikuwa 22,389,784, sawa na asilimia 33.9. Idadi ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 ambayo ndiyo nguvukazi ilikuwa 34,835,408, sawa na asilimia 52.7. Vilevile, idadi ya watu wenye umri wa miaka 65 na zaidi ilikuwa 2,409,251, sawa na asilimia 3.6. Idadi ya watu wenye umri tegemezi ambao ni umri chini ya miaka 15 na umri wa miaka 65 na zaidi ilikuwa 31,218,715, sawa na asilimia 47.3 ya watu wote Tanzania Bara (**Jedwali Na. 6.2**).

**Jedwali Na. 6.2: Idadi ya Watu Tanzania Bara kwa Umri na Jinsi Mwaka 2025**


| Umri | Jinsia | | Jumla | Uwiano (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| | Wanawake | Wanaume | | |
| 0 - 4 | 5,485,013 | 5,588,531 | 11,073,544 | 16.8 |
| 5 - 14 | 8,790,439 | 8,945,481 | 17,735,920 | 26.9 |
| 15 - 34 | 11,625,179 | 10,764,605 | 22,389,784 | 33.9 |
| 35 - 64 | 6,424,355 | 6,021,269 | 12,445,624 | 18.8 |
| 65+ | 1,333,403 | 1,075,848 | 2,409,251 | 3.6 |
| **Jumla** | **33,658,389** | **32,395,734** | **66,054,123** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kielelezo Na. 6.1: Idadi ya Watu Tanzania Bara kwa Umri Mwaka 2025**



**Kielelezo Na. 6.2: Idadi ya Watu Tanzania Bara kwa Umri na Jinsi Mwaka 2025**




## Nguvu Kazi na Ajira

153. Mwaka 2025, vijana 11,043 walipata mafunzo ya ujuzi unaohitajika katika soko la ajira kupitia Programu ya Taifa ya Ukuzaji Ujuzi kwa Vijana ikilinganishwa na vijana 10,699 waliopatiwa mafunzo mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 3.2. Mafunzo hayo yalilenga kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana. Kati ya waliopata mafunzo, vijana 8,000 walipata mafunzo ya uanagenzi, vijana 2,086 mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi, na vijana 957 mafunzo ya kukuza ujuzi katika ufanyaji biashara au kujihusisha katika sekta ndogo ya madini.

154. Mwaka 2025, Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania - TaESA ilisajili watafutakazi 16,031 kupitia Mfumo wa Kidijitali wa Huduma za Ajira ikilinganishwa na watafutakazi 18,916 waliosajiliwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 15.3. Kati ya hao, wanawake walikuwa 8,841 (asilimia 55.1) na wanaume 7,190. Aidha, watafutakazi 8,364 (wanaume 4,489 na wanawake 3,875) walipata mafunzo ya kushindania fursa za ajira ndani na nje ya nchi pamoja na kukuza maadili ya kazi mwaka 2025 ikilinganishwa na watafutakazi 11,542 waliopata mafunzo mwaka 2024.

155. Mwaka 2025, wahitimu 2,546 (wanaume 1,322 na wanawake 1,224) wa ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo waliunganishwa na waajiri kwa ajili ya kufanya mafunzo ya uzoefu wa kazi ikilinganishwa na wahitimu 3,085 mwaka 2024. Aidha, vijana 787

(wanaume 420 na wanawake 367) waliunganishwa na fursa za ajira nchini mwaka 2025 ikilinganishwa na vijana 1,253 waliounganishwa na fursa za ajira mwaka 2024. Vilevile, watanzania 5,454 (wanaume 1,377 na wanawake 4,077) waliunganishwa na fursa za ajira nje ya nchi mwaka 2025 ikilinganishwa na watanzania 3,591 waliofaidika na fursa hizo mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 51.9.

156. Kwa mujibu wa Utafiti wa Ajira na Mapato katika sekta rasmi wa mwaka 2023/24, ajira katika sekta rasmi zilikuwa 3,990,457 ikilinganishwa na ajira 3,635,755 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 9.8. Kati ya hizo, ajira 1,173,608 zilikuwa za sekta ya umma, sawa na asilimia 29.4 ya ajira zote na ajira 2,816,850 zilikuwa za sekta binafsi (asilimia 70.6). Aidha, matokeo ya Utafiti huo yalibainisha kuwa ajira za masharti ya muda mrefu zilikuwa 3,495,715 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na ajira 3,313,909 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 5.5. Kwa upande mwingine, ajira za muda mfupi ziliongezeka kwa asilimia 53.7 na kufikia ajira 494,742 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na ajira 321,846 mwaka 2022/23 (**Jedwali Na. 6.3**).

**Jedwali Na: 6.3 Mchanganuo wa Idadi ya Ajira Rasmi, Mwaka 2022/23 - 2023/24**

| Aina za Ajira | 2022/23 | | | Mchango | 2023/24 | | | Mchango |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Umma | Binafsi | Jumla | | Umma | Binafsi | Jumla | |
| Ajira za Masharti ya Muda Mrefu | 1,082,917 | 2,230,992 | 3,313,909 | 91.1 | 1,132,340 | 2,363,376 | 3,495,715 | 87.6 |
| Ajira za Muda Mfupi | 12,810 | 309,036 | 321,846 | 8.9 | 41,268 | 453,474 | 494,742 | 12.4 |
| **Jumla*** | **1,095,726** | **2,540,029** | **3,635,755** | **100.0** | **1,173,608** | **2,816,850** | **3,990,457** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
* Ujumuishaji wa namba unaweza usifikie kikamilifu kutokana na makadirio

157. Matokeo ya Utafiti wa Ajira na Mapato katika sekta rasmi wa mwaka 2023/24 yalibainisha kuwa wanawake walioajiriwa katika ajira za masharti ya muda mrefu walikuwa asilimia 40.5 ya ajira zote na wanaume asilimia 59.5. Aidha, asilimia 61.3 ya vijana wenye umri wa miaka 15 - 35 waliajiriwa kwa masharti ya muda mrefu mwaka 2023/24 ikilinganishwa na asilimia 67.1 walioajiriwa mwaka 2022/23. Vilevile, kiwango cha ajira za masharti ya muda mrefu kwa wenye umri wa miaka 36 na zaidi kilikuwa asilimia 38.7 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na asilimia 32.9 mwaka 2022/23. Kwa upande mwingine, mchango wa sekta binafsi katika ajira za masharti ya muda mrefu ulikuwa asilimia 67.6 na sekta ya umma ulikuwa asilimia 32.4 mwaka 2023/24. Sekta binafsi ilichangia asilimia 91.7 katika ajira za muda mfupi na sekta ya umma asilimia 8.3.

158. Kwa mujibu wa matokeo ya Utafiti huo, idadi ya waajiriwa wenye ulemavu katika ajira za masharti ya muda mrefu ilikuwa 19,371, sawa na asilimia 0.6. Kati ya hao, wanawake walikuwa 7,176 (asilimia 37.0) na wanaume 12,194 (asilimia 63.0). Aidha, sekta ya umma ilikuwa na waajiriwa wengi wenye ulemavu (asilimia 67.4) ikilinganishwa na sekta binafsi (asilimia 32.6).

159. Mchanganuo wa ajira kimkoa unaonesha kuwa Mkoa wa Dar es Salaam ulichangia idadi kubwa ya ajira 1,371,641 sawa na asilimia 34.4 ya waajiriwa wote mwaka 2023/24 ikilinganishwa na ajira 1,232,637 mwaka 2022/23 **(Jedwali Na. 6.4)**. Aidha, kiwango kidogo cha ajira kilikuwa katika mikoa ya Katavi (23,768) na Songwe (32,181) Kwa upande mwingine, shughuli za uzalishaji viwandani zilikuwa na mchango mkubwa wa asilimia 18.0 kwenye ajira, ikifuatiwa na shughuli za elimu asilimia 15.7 na utawala asilimia 11.9 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 6.5.**

**Jedwali Na. 6.4: Mchanganuo wa Idadi ya Ajira Kimkoa Mwaka 2023/24**

| **Mkoa** | **Binafsi** | **Umma** | **Jumla** | **Mchango (Asilimia)** |
|---|---:|---:|---:|---:|
| Dodoma | 67,655 | 63,689 | 131,344 | 3.3 |
| Arusha | 194,989 | 32,674 | 227,663 | 5.7 |
| Kilimanjaro | 135,799 | 57,438 | 193,237 | 4.8 |
| Tanga | 126,801 | 62,515 | 189,316 | 4.7 |
| Morogoro | 203,427 | 95,809 | 299,236 | 7.5 |
| Pwani | 51,222 | 50,783 | 102,004 | 2.6 |
| Dar es Salaam | 1,269,213 | 102,428 | 1,371,640 | 34.4 |
| Lindi | 13,769 | 42,326 | 56,095 | 1.4 |
| Mtwara | 35,669 | 24,232 | 59,901 | 1.5 |
| Ruvuma | 42,037 | 27,863 | 69,900 | 1.8 |
| Iringa | 66,511 | 33,485 | 99,996 | 2.5 |
| Mbeya | 126,606 | 57,785 | 184,391 | 4.6 |
| Singida | 32,456 | 36,287 | 68,743 | 1.7 |
| Tabora | 25,032 | 33,313 | 58,345 | 1.5 |
| Rukwa | 24,859 | 22,731 | 47,590 | 1.2 |
| Kigoma | 37,942 | 35,763 | 73,705 | 1.8 |
| Shinyanga | 44,459 | 81,505 | 125,964 | 3.2 |
| Kagera | 39,966 | 50,929 | 90,896 | 2.3 |
| Mwanza | 121,029 | 57,017 | 178,046 | 4.5 |
| Mara | 45,961 | 47,845 | 93,806 | 2.4 |
| Manyara | 32,385 | 32,716 | 65,101 | 1.6 |
| Njombe | 16,923 | 32,026 | 48,949 | 1.2 |
| Katavi | 8,067 | 15,701 | 23,767 | 0.6 |
| Simiyu | 19,529 | 22,891 | 42,420 | 1.1 |
| Geita | 22,357 | 33,866 | 56,223 | 1.4 |
| Songwe | 12,190 | 19,991 | 32,181 | 0.8 |
| **Jumla*** | **2,816,850** | **1,173,608** | **3,990,457** | **100.0** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Ujumuishaji wa namba unaweza usifikie kikamilifu kutokana na makadirio

**Jedwali Na. 6.5: Mchanganuo wa Idadi ya Ajira kwa Shughuli za Kiuchumi Mwaka 2023/24**

| Shughuli | Ajira za Masharti ya Muda Mrefu | Ajira za Muda Mfupi | Jumla | Mchango (Asilimia) |
|---|---:|---:|---:|---:|
| Kilimo, Misitu na uvuvi | 122,380 | 65,823 | 188,202 | 4.7 |
| Uchimbaji madini na mawe | 75,003 | 3,817 | 78,819 | 2.0 |
| Uzalishaji wa viwandani | 583,707 | 135,137 | 718,843 | 18.0 |
| Umeme, gesi, mvuke na kubadilisha hali (joto/baridi) | 24,599 | 1,253 | 25,852 | 0.6 |
| Usambazaji majisafi na udhibiti wa majitaka | 21,969 | 3,100 | 25,068 | 0.6 |
| Ujenzi | 56,793 | 58,852 | 115,646 | 2.9 |
| Biashara na matengenezo | 267,993 | 57,384 | 325,377 | 8.2 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 120,874 | 13,644 | 134,518 | 3.4 |
| Malazi na huduma za chakula | 296,013 | 41,042 | 337,054 | 8.4 |
| Habari na Mawasiliano | 37,511 | 10,378 | 47,889 | 1.2 |
| Fedha na Bima | 91,634 | 470 | 92,104 | 2.3 |
| Upangishaji majengo | 8,546 | 211 | 8,757 | 0.2 |
| Shughuli za Kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 52,313 | 4,723 | 57,035 | 1.4 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | 255,628 | 11,924 | 267,552 | 6.7 |
| Utawala na Ulinzi | 468,304 | 5,440 | 473,744 | 11.9 |
| Elimu | 609,765 | 14,951 | 624,716 | 15.7 |
| Afya na Huduma za Jamii | 254,545 | 13,636 | 268,181 | 6.7 |
| Sanaa na Burudani | 22,064 | 2,627 | 24,691 | 0.6 |
| Huduma nyingine | 126,076 | 50,331 | 176,407 | 4.4 |
| **Jumla** | **3,495,715** | **494,742** | **3,990,457** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

160. Kwa upande wa ajira mpya, matokeo ya Utafiti yanaonesha kuwa ajira mpya zilikuwa 360,852 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na ajira mpya 129,055 mwaka 2022/23. Kati ya hizo, ajira kwa wanawake zilikuwa 175,743 na wanaume 185,109. Aidha, sekta binafsi ilitoa ajira mpya 266,721, sawa na asilimia 73.9 na sekta ya umma ajira mpya 94,131. Kwa upande mwingine, kada ya watoa huduma na wauza maduka ilikuwa na ajira nyingi zaidi (96,658), ikifuatiwa na kada ya ajira za msingi 77,249. Kada iliyokuwa na ajira chache zaidi (8,061) ni wanasheria, watawala na mameneja.

161. Kwa mujibu wa Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa Mwaka 2025, kiwango cha ushiriki wa nguvu kazi Tanzania Bara kiliongezeka na kufikia asilimia 76.1 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 73.4 mwaka 2024. Kiwango cha ushiriki wa nguvu kazi kwa wanaume kilikuwa asilimia 82.6 na wanawake asilimia 70.1. Katika kipindi

hicho, uwiano wa ajira kwa idadi ya watu Tanzania Bara uliongezeka na kufikia asilimia 71.6 ikilinganishwa na asilimia 69.0 mwaka 2024 (**Jedwali Na. 6.6**). Aidha, kiwango cha ukosefu wa ajira kilipungua na kufikia asilimia 5.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 6.1 mwaka 2024 ikiashiria kuimarika kwa upatikanaji wa ajira. Kwa upande wa mgawanyo wa ajira kwa shughuli za kiuchumi, matokeo ya Utafiti yanaonesha kuwa shughuli za kilimo ziliongoza kwa kutoa ajira 15,310,182 sawa na asilimia 55.1 ya ajira zote, ikifuatiwa na biashara na matengenezo ajira 4,274,076 (asilimia 15.4) na uzalishaji viwandani ajira 1,496,251 (asilimia 5.4) Mgawanyo wa ajira kwa shughuli za kiuchumi ni kama inavyoonekana katika **Jedwali 6.7**.

**Jedwali Na. 6.6: Mchanganuo wa Ajira kwa Idadi ya Watu Tanzania Bara, Mwaka 2024 - 2025**

| Umri | 2024 | | | 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanawake | Wanaume | Jumla | Wanawake | Wanaume | Jumla |
| Idadi ya Watu (Umri wa miaka 15+) | 18,932,825 | 17,207,530 | 36,140,354 | 20,114,430 | 18,645,776 | 38,760,206 |
| Ushiriki katika nguvu kazi (Wenye ajira na wanaotafuta ajira) | 12,821,078 | 13,718,590 | 26,539,668 | 14,103,050 | 15,405,744 | 29,508,794 |
| Wenye Ajira (Umri wa miaka 15+) | 11,884,295 | 13,046,629 | 24,930,924 | 13,084,185 | 14,681,200 | 27,765,385 |
| **Kiwango cha ushiriki wa nguvu kazi (Asilimia)** | **67.7** | **79.7** | **73.4** | **70.1** | **82.6** | **76.1** |
| **Uwiano wa ajira kwa idadi ya watu (Asilimia)** | **62.8** | **75.8** | **69.0** | **65.0** | **78.7** | **71.6** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 6.7: Mchanganuo wa Ajira kwa Shughuli za Kiuchumi Tanzania Bara Mwaka 2025**

| Shughuli | Wanawake | Wanaume | Jumla | Mchango wa Shughuli katika Ajira (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Kilimo, misitu na uvuvi | 7,610,557 | 7,699,625 | 15,310,182 | 55.1 |
| Uchimbaji wa madini na mawe | 48,828 | 283,701 | 332,529 | 1.2 |
| Uzalishaji Viwandani | 463,913 | 1,032,337 | 1,496,251 | 5.4 |
| Umeme, Gesi, usambazaji wa mifumo ya upozaji | 1,590 | 50,723 | 52,313 | 0.2 |
| Usambazaji na usimamizi wa majisafi na majitaka | 4,286 | 22,855 | 27,142 | 0.1 |
| Ujenzi | 25,546 | 803,199 | 828,745 | 3.0 |
| Biashara na matengenezo | 2,358,821 | 1,915,255 | 4,274,076 | 15.4 |
| Uchukuzi na uhifadhi mizigo | 31,789 | 1,186,060 | 1,217,849 | 4.4 |
| Malazi na huduma ya chakula | 1,051,935 | 215,632 | 1,267,566 | 4.6 |
| Habari na mawasilisno | 13,848 | 34,118 | 47,966 | 0.2 |
| Huduma ya fedha na bima | 94,098 | 41,060 | 135,158 | 0.5 |
| Upangishaji, ununuzi na uuzaji majengo | 7,761 | 8,468 | 16,229 | 0.1 |
| Shughuli za kitaaluma, kisayansi na ufundi | 20,429 | 41,362 | 61,791 | 0.2 |
| Huduma za masuala ya kiutawala | 431,862 | 416,899 | 848,762 | 3.1 |
| Utawala, ulinzi na huduma za hifadhi ya jamii; | 32,637 | 103,177 | 135,813 | 0.5 |
| Elimu | 221,970 | 287,460 | 509,430 | 1.8 |
| Afya na huduma za kijamii | 103,355 | 87,350 | 190,705 | 0.7 |
| Sanaa na burudani | 16,508 | 37,654 | 54,161 | 0.2 |
| Huduma nyingine | 381,418 | 323,828 | 705,246 | 2.5 |
| Shughuli za kaya, huduma na uzalishaji katika kaya | 162,166 | 90,005 | 252,171 | 0.9 |
| Shughuli nyingine katika taasisi na mamlaka za kigeni | 868 | 431 | 1,299 | 0.0 |
| **Jumla** | **13,084,185** | **14,681,200** | **27,765,385** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Jedwali Na. 37: IDADI YA WATU NCHINI TANZANIA KIMKOA, MWAKA 2018 - 2025**

| Mkoa | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | 2,492,989 | 2,568,514 | 2,647,410 | 2,729,668 | 3,085,625 | 3,211,342 | 3,300,186 | 3,389,537 |
| Arusha | 1,999,907 | 2,051,852 | 2,104,074 | 2,156,511 | 2,356,255 | 2,453,164 | 2,524,141 | 2,593,834 |
| Kilimanjaro | 1,864,329 | 1,906,978 | 1,951,252 | 1,996,952 | 1,861,934 | 1,934,278 | 1,976,588 | 2,018,855 |
| Tanga | 2,337,053 | 2,391,791 | 2,449,235 | 2,509,439 | 2,615,597 | 2,720,044 | 2,790,841 | 2,861,741 |
| Morogoro | 2,596,287 | 2,662,468 | 2,730,058 | 2,799,260 | 3,197,104 | 3,322,152 | 3,405,761 | 3,488,328 |
| Pwani | 1,265,504 | 1,295,267 | 1,325,852 | 1,357,271 | 2,024,947 | 2,092,960 | 2,144,928 | 2,195,974 |
| Dar es Salaam | 5,147,070 | 5,275,315 | 5,401,814 | 5,526,638 | 5,383,728 | 5,600,194 | 5,739,734 | 5,874,418 |
| Lindi | 983,738 | 1,004,439 | 1,025,800 | 1,047,783 | 1,194,028 | 1,237,901 | 1,262,641 | 1,286,839 |
| Mtwara | 1,424,083 | 1,451,078 | 1,478,874 | 1,507,426 | 1,634,947 | 1,702,874 | 1,738,231 | 1,772,766 |
| Ruvuma | 1,579,811 | 1,616,991 | 1,655,443 | 1,695,057 | 1,848,794 | 1,933,611 | 1,982,240 | 2,030,461 |
| Iringa | 1,095,172 | 1,122,131 | 1,149,481 | 1,177,327 | 1,192,728 | 1,234,438 | 1,260,104 | 1,285,523 |
| Mbeya | 2,070,412 | 2,136,614 | 2,204,543 | 2,274,236 | 2,343,754 | 2,434,636 | 2,495,901 | 2,556,431 |
| Singida | 1,612,854 | 1,658,086 | 1,705,182 | 1,754,370 | 2,008,058 | 2,102,316 | 2,166,130 | 2,231,481 |
| Tabora | 2,870,522 | 2,974,427 | 3,081,263 | 3,191,194 | 3,391,679 | 3,542,880 | 3,657,677 | 3,775,329 |
| Rukwa | 1,195,550 | 1,231,959 | 1,270,049 | 1,310,007 | 1,540,519 | 1,619,636 | 1,680,335 | 1,742,773 |
| Kigoma | 2,616,200 | 2,706,831 | 2,800,919 | 2,898,568 | 2,470,967 | 2,584,236 | 2,669,703 | 2,757,544 |
| Shinyanga | 1,874,709 | 1,933,768 | 1,993,589 | 2,054,229 | 2,241,299 | 2,337,809 | 2,410,306 | 2,483,928 |
| Kagera | 3,022,037 | 3,127,908 | 3,238,347 | 3,353,241 | 2,989,299 | 3,131,795 | 3,226,032 | 3,322,078 |
| Mwanza | 3,532,378 | 3,676,300 | 3,826,573 | 3,983,793 | 3,699,872 | 3,869,312 | 3,992,565 | 4,116,854 |
| Mara | 2,209,143 | 2,298,317 | 2,391,845 | 2,490,155 | 2,372,015 | 2,485,120 | 2,565,172 | 2,647,733 |
| Manyara | 1,750,864 | 1,810,929 | 1,873,105 | 1,937,450 | 1,892,502 | 1,973,968 | 2,035,641 | 2,098,332 |
| Njombe | 803,299 | 820,355 | 837,557 | 854,932 | 889,946 | 922,044 | 939,503 | 956,702 |
| Katavi | 738,237 | 771,287 | 805,887 | 842,200 | 1,152,958 | 1,209,848 | 1,253,158 | 1,297,568 |
| Simiyu | 2,094,798 | 2,196,449 | 2,304,228 | 2,418,495 | 2,140,497 | 2,254,092 | 2,338,396 | 2,425,871 |
| Geita | 2,239,949 | 2,335,134 | 2,434,800 | 2,539,114 | 2,977,608 | 3,127,548 | 3,241,053 | 3,357,323 |
| Songwe | 1,202,419 | 1,239,970 | 1,278,850 | 1,319,064 | 1,344,687 | 1,403,938 | 1,444,855 | 1,485,900 |
| **Tanzania Bara** | **52,619,314** | **54,265,158** | **55,966,030** | **57,724,380** | **59,851,347** | **62,442,136** | **64,241,822** | **66,054,123** |
| Kaskazini Unguja | 222,066 | 227,317 | 232,480 | 237,505 | 257290 | 267,219 | 275,531 | 283,792 |
| Kusini Unguja | 133,767 | 136,235 | 138,589 | 140,821 | 195873 | 204,063 | 209,534 | 214,888 |
| Mjini Magharibi | 700,791 | 717,468 | 733,914 | 750,033 | 893169 | 933,760 | 962,135 | 989,928 |
| Kaskazini Pemba | 271,594 | 282,716 | 294,267 | 306,173 | 272091 | 284,963 | 295,724 | 306,849 |
| Kusini Pemba | 251,631 | 261,853 | 272,348 | 283,076 | 271350 | 283,901 | 293,530 | 303,424 |
| **Zanzibar** | **1,579,849** | **1,625,589** | **1,671,598** | **1,717,608** | **1,889,773** | **1,973,906** | **2,036,454** | **2,098,881** |
| **Tanzania** | **54,199,163** | **55,890,747** | **57,637,628** | **59,441,988** | **61,741,120** | **64,416,042** | **66,278,276** | **68,153,004** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu




Sehemu ya Pili

# Maendeleo Katika Sekta Mbalimbali

## SURA YA 7

## KILIMO NA USHIRIKA

### UZALISHAJI WA MAZAO YA KILIMO

**Mazao ya Chakula**

162. Mwaka 2025, tani 23,783,128 za mazao makuu ya chakula zilizalishwa ikilinganishwa na tani 22,803,316 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 4.3 (**Jedwali Na. 7.1**). Hii ilitokana na kuimarishwa kwa huduma za ugani; matumizi ya teknolojia; upatikanaji wa pembejeo bora za kilimo na vitendea kazi; kuimarika kwa usimamizi wa mazao kabla na baada ya kuvuna; na uwepo wa mvua za kutosha katika maeneo mengi ya uzalishaji. Kati ya kiasi kilichozalishwa, tani 14,924,582 zilikuwa za mazao ya nafaka na tani 8,858,546 mazao yasiyo ya nafaka. Aidha, mahitaji ya mazao makuu ya chakula yalikuwa tani 18,279,054 mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 17,753,989 mwaka 2024. Kwa kuzingatia mahitaji na uzalishaji wa mazao makuu ya chakula, nchi ilikuwa na ziada ya mazao ya chakula tani 5,504,074 ikilinganishwa na tani 5,049,327 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 9.0. Hii ilifanya nchi kuwa na kiwango cha utoshelevu wa chakula kitokanacho na mazao makuu ya chakula cha asilimia 130.1 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 128.4 mwaka 2024.

**Jedwali Na. 7.1: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Chakula (Tani '000'), Mwaka 2021 - 2025**

| Zao | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mazao ya Nafaka** | | | | | | |
| Mahindi | 7,039 | 6,417 | 8,011 | 10,084 | 10,925 | 8.3 |
| Mchele | 2,687 | 1,708 | 2,332 | 3,046 | 2,640 | -13.3 |
| Ngano | 70 | 62 | 87 | 119 | 116 | -2.5 |
| Mtama/Uwele/ Ulezi | 1,077 | 1,046 | 1,019 | 1,339 | 1,244 | -7.1 |
| **Mazao yasiyo Nafaka** | | | | | | |
| Muhogo | 2,486 | 2,411 | 2,575 | 2,317 | 2649 | 14.3 |
| Maharage/ Mikunde | 2,235 | 2,499 | 2,803 | 2,495 | 2,523 | 1.1 |
| Ndizi | 1,442 | 1,290 | 1,224 | 1,152 | 1,414 | 22.7 |
| Viazi (Vitamu na Mviringo) | 1,626 | 1,715 | 2,351 | 2,252 | 2,273 | 0.9 |
| **Jumla** | **18,662** | **17,148** | **20,402** | **22,804** | **23,784** | **4.3** |

**Chanzo:** Wizara ya Kilimo

**Miundombinu ya Hifadhi ya Chakula**

163. Mwaka 2025, Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula - NFRA iliongeza uwezo wa kuhifadhi chakula na kufikia tani 776,000 ikilinganishwa na tani 360,000 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilitokana na kukamilika kwa ujenzi wa maghala na

vihenge vya kisasa. Aidha, akiba ya uhifadhi wa chakula ilipungua kutoka tani 683,928 mwaka 2024 na kufikia tani 555,857.5 mwaka 2025. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uuzaji wa mazao ya chakula ili kulinda ubora wa nafaka na kuimarisha bei katika soko.

**Mazao ya Asilia ya Biashara**

164. Mwaka 2025, uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ulikuwa tani 1,687,105 ikilinganishwa na tani 1,487,364 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 13.4 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 7.2**. Hii ilitokana na wakulima kuendelea kufuata kanuni bora za kilimo cha mazao ya biashara; matumizi ya mbolea kupitia mpango wa ruzuku; kilimo cha umwagiliaji; kuimarika kwa huduma za ugani; utafiti; na matumizi ya mbegu bora.

**Jedwali Na. 7.2: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Asilia ya Biashara (Tani), Mwaka 2021 - 2025**

| Zao | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Pamba | 122,836 | 144,792 | 174,486 | 282,510 | 221,853 | -21.5 |
| Kahawa | 73,027 | 66,837 | 62,917 | 77,417 | 110,369 | 42.6 |
| Chai | 27,510 | 24,825 | 26,451 | 22,337 | 22,484 | 0.7 |
| Pareto | 2,412 | 2,694 | 3,815 | 2,866 | 8,583 | 199.5 |
| Tumbaku | 58,508 | 70,699 | 122,858 | 117,464 | 185,776 | 58.2 |
| Korosho | 210,786 | 240,158 | 310,787 | 528,262 | 617,684 | 16.9 |
| Mkonge | 36,170 | 44,151 | 56,773 | 61,216 | 66,973 | 9.4 |
| Sukari | 367,718 | 379,280 | 460,049 | 395,293 | 453,383 | 14.7 |
| **Jumla** | **898,967** | **973,436** | **1,218,136** | **1,487,364** | **1,687,105** | **13.4** |

**Chanzo**: Wizara ya Kilimo

**Mazao ya Bustani**

165. Mwaka 2025, uzalishaji wa mazao ya bustani unaojumuisha maua, matunda, viungo na mbogamboga ulikuwa tani 9,782,338 ikilinganishwa na tani 7,513,502 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 30.2 (**Jedwali Na. 7.3**). Hii ilitokana na kuimarika kwa huduma za ugani, kilimo cha umwagiliaji, utafiti, matumizi ya mbegu bora, ongezeko la matumizi ya mbolea kupitia mpango wa ruzuku, na uwepo wa masoko ya uhakika ya mazao ya bustani.

**Jedwali Na. 7.3: Uzalishaji wa Mazao ya Bustani (Tani), Mwaka 2021 - 2025**

| Zao | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Matunda | 5,199,312 | 5,407,284 | 6,530,302 | 6,212,065 | 8,051,187 | 29.6 |
| Mboga | 2,011,684 | 2,212,852 | 1,777,878 | 1,232,526 | 1,634,591 | 32.6 |
| Maua | 1,338 | 1,351 | 577 | 534 | 1,102 | 106.4 |
| Viungo | 92,389 | 101,628 | 129,517 | 68,377 | 95,458 | 39.6 |
| **Jumla** | **7,304,723** | **7,723,115** | **8,438,274** | **7,513,502** | **9,782,338** | **30.2** |

**Chanzo**: Wizara ya Kilimo

**Mazao ya Mbegu za Mafuta**

166. Mwaka 2025, uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta ulikuwa tani 2,283,072 ikilinganishwa na tani 2,230,135 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 2.4 **(Jedwali Na. 7.4**). Hii ilichangiwa na upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa mpango wa ruzuku, kuimarika kwa huduma za ugani na hali nzuri ya hewa.

**Jedwali Na. 7.4: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Mbegu za Mafuta (Tani), Mwaka 2021 - 2025**

| Zao | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Alizeti | 478,900 | 425,653 | 1,132,298 | 1,217,026 | 1,222,210 | 0.4 |
| Karanga | 895,219 | 936,799 | 586,216 | 620,603 | 609,340 | -1.8 |
| Ufuta | 236,162 | 79,170 | 266,994 | 240,010 | 257,041 | 7.1 |
| Chikichi | 58,791 | 60,790 | 62,125 | 51,834 | 74,303 | 43.3 |
| Soya | 44,106 | 5,152 | 13,584 | 48,532 | 35,025 | -27.8 |
| Nazi | 192,239 | 201,539 | 95,465 | 52,131 | 85,153 | 63.3 |
| **Jumla** | **1,905,417** | **1,709,103** | **2,156,683** | **2,230,135** | **2,283,072** | **2.4** |

**Chanzo**: Wizara ya Kilimo

**Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo**

167. Mwaka 2025, upatikanaji wa mbegu bora ulikuwa tani 72,031 ikilinganishwa na tani 72,032 mwaka 2024. Kati ya mbegu zilizopatikana, tani 54,236 zilizalishwa nchini ikilinganishwa na tani 56,114 zilizozalishwa nchini mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 3.3. Upungufu huo ulisababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa. Kati ya mbegu zilizozalishwa nchini, tani 50,883 zilizalishwa na sekta binafsi na tani 3,353 zilizalishwa na Wakala wa Mbegu za Kilimo - ASA. Aidha, tani 17,795 za mbegu ziliingizwa kutoka nje ya nchi mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 15,917 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 11.8. Hii ilitokana na kupungua kwa uzalishaji wa ndani na kuongezeka kwa mahitaji ya mbegu nchini.

168. Mwaka 2024/25, upatikanaji wa mbolea ulikuwa tani 1,323,798 ikilinganishwa na tani 1,213,780 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 9.1. Katika kipindi hicho, tani 152,336 za mbolea zilizalishwa nchini ikilinganishwa na tani 158,628 zilizozalishwa mwaka 2023/24, sawa na upungufu wa asilimia 4.0. Hii ilitokana na upungufu wa mitaji katika baadhi ya viwanda vikubwa vya uzalishaji wa mbolea vilivyokuwa vikifanya upanuzi wa viwanda ili kuongeza uzalishaji. Aidha, tani 911,059 za mbolea ziliagizwa kutoka nje ya nchi mwaka 2024/25 ikilinganishwa na tani 728,758 zilizoagizwa mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 25.0. Vilevile, matumizi ya mbolea nchini yaliongezeka kwa asilimia 15.6 na kufikia tani 972,074 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na tani 840,714 mwaka 2023/24 (**Jedwali Na. 7.5**). Ongezeko la matumizi ya mbolea lilitokana na kuboreshwa kwa huduma za ugani kwa wakulima kuhusu matumizi sahihi ya mbolea pamoja na kuimarishwa kwa mifumo ya kidijitali ya kutolea mbolea ya ruzuku.

**Jedwali Na. 7.5: Upatikanaji wa Mbolea Nchini (Tani), Mwaka 2020/21 - 2024/25**

| **Mwaka** | **2020/21** | **2021/22** | **2022/23** | **2023/24** | **2024/25** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Makadirio ya Mahitaji | 718,051 | 698,260 | 667,730 | 848,884 | 1,000,000 | 17.8 |
| **Upatikanaji** | | | | | | |
| Bakaa | 219,206 | 117,900 | 126,964 | 326,344 | 260,403 | -20.2 |
| Uzalishaji Ndani ya Nchi | 42,695 | 62,724 | 84,696 | 158,678 | 152,336 | -4.0 |
| Kiasi kilichoingizwa Ndani ya Nchi | 504,122 | 407,994 | 824,085 | 728,758 | 911,059 | 25.0 |
| **Jumla ya Upatikanaji** | **766,023** | **588,618** | **1,035,745** | **1,213,780** | **1,323,798** | **9.1** |
| Kiasi kilichouzwa Nje ya Nchi | 171,254 | 98,055 | 128,774 | 112,612 | 118,048 | 4.8 |
| Matumizi ya Ndani ya Nchi | 476,870 | 363,599 | 580,628 | 840,714 | 972,074 | 15.6 |

**Chanzo**: Wizara ya Kilimo

169. Mwaka 2024/25, wastani wa bei ya mbolea ya kukuzia - UREA katika soko la dunia ulikuwa dola za Marekani 392 kwa tani ikilinganishwa na dola za Marekani 391 kwa tani mwaka 2023/24. Aidha, wastani wa bei ya mbolea ya kupandia - DAP katika soko la dunia ulikuwa dola za Marekani 599 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na dola za Marekani 590 kwa tani mwaka 2023/24.

**Upatikanaji wa Mikopo ya Kilimo**

170. Mwaka 2025, mikopo 24 yenye thamani ya shilingi milioni 5,425.5 ilitolewa na Mfuko wa Pembejeo za Kilimo - AGITF ikilinganishwa na mikopo 19 yenye thamani ya shilingi milioni 208.36 iliyotolewa mwaka 2024. Ongezeko la mikopo lilitokana na AGITF kwa kushirikiana na taasisi za kifedha kutoa mikopo na kudhamini wakulima wanaohitaji mikopo. Kati ya mikopo iliyotolewa, mikopo kwa ajili ya uendeshaji wa shamba ilikuwa shilingi milioni 215.11, miundombinu ya umwagiliaji (shilingi milioni 101.19), Benki ya Ushirika kwa matumizi ya mikopo ya kilimo (shilingi milioni 5,000), mashine za kuongeza

thamani (shilingi milioni 93.45) na matrekta madogo (powertiller) (shilingi milioni 15.75). Aidha, shilingi bilioni 1.95 zilirejeshwa, sawa na asilimia 39 ya lengo la marejesho ya shilingi bilioni 4.95 mwaka 2025.

**Mwenendo wa Bei na Masoko ya Mazao**

171. Mwaka 2025, wastani wa bei ya jumla ya mahindi uliongezeka kwa asilimia 9.0 na kufikia shilingi 75,000 kwa gunia la kilogramu 100 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 68,800 kwa gunia la kilogramu 100 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mahindi katika nchi jirani. Aidha, bei ya mchele iliongezeka kwa asilimia 2.5 na kufikia wastani wa shilingi 225,000 kwa gunia la kilogramu 100 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 219,600 kwa gunia la kilogramu 100 mwaka 2024. Hii ilitokana na kupungua kwa uzalishaji wa mchele kwa asilimia 13.3. Kwa upande mwingine, bei ya maharage ilishuka kwa asilimia 6.2 na kufikia wastani wa shilingi 245,000 kwa gunia la kilogramu 100 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 261,150 kwa gunia la kilogramu 100 mwaka 2024 (**Jedwali Na. 7.6**). Hii ilichangiwa na kuwepo kwa hali nzuri ya hewa katika maeneo ya uzalishaji iliyopelekea kuongezeka kwa uzalishaji wa maharage.

**Jedwali Na. 7.6: Wastani wa Bei za Jumla za Mazao Makuu ya Chakula (Shilingi/Gunia la Kilogramu 100), Mwaka 2021 - 2025**

| Zao | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 47,800 | 83,200 | 105,200 | 68,800 | 75,000 | 9.0 |
| Mchele | 142,800 | 216,800 | 275,440 | 219,600 | 225,000 | 2.5 |
| Mtama | 99,200 | 123,600 | 139,910 | 140,500 | 147,816 | 5.2 |
| Ulezi | 151,800 | 169,500 | 141,000 | 180,400 | 227,250 | 26.0 |
| Ngano | 124,900 | 182,100 | 191,930 | 194,900 | 198,866 | 2.0 |
| Maharage | 176,100 | 215,100 | 276,930 | 261,150 | 245,000 | -6.2 |
| Viazi mviringo | 68,000 | 82,000 | 97,710 | 99,300 | 95,747 | -3.6 |

**Chanzo**: Wizara ya Kilimo

172. Mwaka 2025, wastani wa bei ya jumla ya kahawa aina ya arabika katika soko la ndani ulikuwa shilingi 11,000 kwa kilogramu ikilinganishwa na shilingi 7,500 kwa kilogramu mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 46.7. Aidha, wastani wa bei ya jumla ya mkonge uliongezeka kwa asilimia 11.2 na kufikia shilingi 3,966,800 kwa tani mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 3,566,000 kwa tani mwaka 2024. Kupanda kwa bei ya mkonge na kahawa (arabika) kulitokana na kuongezeka kwa mahitaji katika soko la kimataifa, ubora wa mazao, na maboresho katika mifumo ya masoko na minada. Kwa upande mwingine, wastani wa bei ya jumla ya korosho daraja la kwanza ulipungua kwa asilimia 21.4 kutoka shilingi 3,188 kwa kilogramu mwaka 2024 hadi shilingi 2,505 kwa kilogramu mwaka 2025. Vilevile, wastani wa bei ya jumla ya korosho daraja la pili

ulipungua kwa asilimia 8.8 kutoka shilingi 2,076 kwa kilogramu mwaka 2024 na kufikia shilingi 1,893 kwa kilogramu mwaka 2025. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa bei ya korosho kwenye soko la dunia kulikosababishwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa korosho katika nchi nyingine (**Jedwali Na. 7.7**).

**Jedwali Na. 7.7: Wastani wa Bei za Jumla za Mazao ya Asili ya Biashara (Shilingi/Kilogramu), Mwaka 2021 - 2025**

| Zao | Aina/Daraja | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | Arabika | 6,500 | 8,428 | 5,978 | 7,500 | 11,000 | 46.7 |
| | Robusta | 1,400 | 2,646 | 2,965 | 5,060 | 5,000 | -1.2 |
| Pamba | Pamba mbegu | 1,400 | 1,800 | 1,150 | 1,350 | 1,150 | -14.8 |
| Korosho | Daraja la kwanza | 2,150 | 1,860 | 1,720 | 3,188 | 2,505 | -21.4 |
| | Daraja la pili | 1,595 | 1,331 | 1,200 | 2,076 | 1,893 | -8.8 |
| Tumbaku* | Mvuke (VFC) | 1.79 | 1.79 | 2.34 | 2.3 | 2.6 | 13.0 |
| | Moshi (DFC) | 1.51 | 1.51 | 1.69 | 1.91 | 1.9 | - 0.5 |
| Chai* | Majani mabichi | 314 | 366 | 366 | 366 | 366 | 0.0 |
| | Majani makavu | 1.62 | 1.55 | 1.24 | 1.46 | 1.7 | 16.4 |
| Mkonge (‘000’) | Singa | 3,500 | 3,626 | 3,483 | 3,566 | 3,967 | 11.2 |
| Pareto | Maua makavu | 3,200 | 3,200 | 3,500 | 3,700 | 4,000 | 8.1 |

**Chanzo**: Wizara ya Kilimo
* Dola za Marekani/Kilogramu

**Huduma za Ugani**

173. Mwaka 2025, wakulima 677,842 walisajiliwa katika mfumo wa ruzuku ya pembejeo za kilimo ikilinganishwa na wakulima 530,384 waliosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 27.8. Aidha, maswali na hoja 6,020 za wadau wa kilimo kuhusu uzalishaji wa mazao, ubora wa mbegu, ruzuku ya pembejeo za kilimo (mbolea), vibali vya usafirishaji mazao na masoko ya mazao ya kilimo ziliulizwa kupitia kituo cha huduma kwa wateja mwaka 2025 ikilinganishwa na maswali na hoja 5,879 zilizoulizwa mwaka 2024. Vilevile, magari 44 yalinunuliwa na kusambazwa kwa maafisa ugani kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma kwa wakulima nchini. Kati ya hayo, magari 15 yalipelekwa katika ngazi ya mikoa, magari 14 ngazi ya halmashauri na magari 15 katika Vituo vya Uhaulishaji wa Teknolojia za Kilimo - MATI.

**Utafiti katika Uzalishaji wa Mazao**

174. Mwaka 2025, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo - TARI iligundua aina mpya 30 za mbegu bora za mazao mbalimbali ikilinganishwa na aina 16 za mbegu bora za mazao zilizogunduliwa mwaka 2024. Aina mpya za mbegu zilizogunduliwa zilikuwa za pilipili kichaa (5), pilipili mwendokasi (habanero - 3), pilipili hoho (5), nyanya (6), mtama (5),

ngogwe (3) na choroko (3). Aidha, sifa za mbegu zilizogunduliwa ni pamoja na kutoa mavuno mengi na kustahimili ukame, magonjwa na wadudu.

175. Mwaka 2025, TARI ilizalisha tani 565.4 za mbegu bora za mazao ya nafaka, jamii ya mikunde na mafuta ikilinganishwa na tani 846.6 za mbegu zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 33.2. Hii ilitokana na mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha mvua nyingi zilizoathiri uzalishaji wa mbegu. Kati ya mbegu zilizozalishwa, tani 9.4 zilikuwa mbegu mama, tani 51 mbegu za awali, tani 264.9 mbegu za msingi na tani 240.1 mbegu zilizothibitishwa. Aidha, miche 14,199,661 ilizalishwa mwaka 2025 ikilinganishwa na miche 10,766,506 iliyozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 31.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya miche ya miti ya matunda, ikiwemo parachichi na mazao mbegu.

**Mafunzo ya Kilimo**

176. Mwaka 2025, wanafunzi 2,312 walidahiliwa katika vyuo 10 vya mafunzo ya kilimo ngazi ya astashahada na stashahada ikilinganishwa na wanafunzi 2,580 waliodahiliwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 10.4. Hii ilitokana na kuendelea na utekelezaji wa mabadiliko ya utoaji wa mafunzo kwa kujielekeza katika uhaulishaji wa teknolojia za kilimo kwa wakulima. Aidha, wakulima 13,237 walipatiwa mafunzo kuhusu teknolojia na mbinu bora za kilimo kupitia vyuo na vituo vya mafunzo ya kilimo mwaka 2025 ikilinganishwa na wakulima 10,892 waliopatiwa mafunzo mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 21.5.

**Umwagiliaji**

177. Mwaka 2025, eneo la kilimo linalomwagiliwa nchini liliongezeka kwa asilimia 35.2 na kufikia hekta 983,466.1 kutoka hekta 727,280.6 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilichangiwa na kukamilika kwa uchimbaji wa visima 268, ujenzi wa skimu tisa (9) na ukarabati wa skimu tisa (9) za umwagiliaji. Katika kipindi hicho, idadi ya vyama vya umwagiliaji vilivyosajiliwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iliongezeka kwa asilimia 35.1 na kufikia vyama 1,021, kutoka vyama 756 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilitokana na uhamasishaji na utoaji mafunzo kwa wakulima kuhusu umuhimu wa kujiunga na kusajili vyama vya umwagiliaji.

**MIFUGO**

**Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake**

178. Mwaka 2025, idadi ya ng’ombe nchini ilikadiriwa kuwa 40,569,621 ikilinganishwa na ng’ombe 39,241,375 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 3.4. Aidha, idadi ya mbuzi ilikadiriwa kuwa 29,598,648 mwaka 2025 ikilinganishwa na mbuzi 28,592,597 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 3.5 (**Jedwali Na. 7.8**). Ongezeko la mifugo

lilichangiwa na kuboreshwa kwa mbari za mifugo, kupima na kutenga maeneo ya maji na malisho pamoja na kuendelea kutoa elimu ya ufugaji wenye tija.

**Jedwali Na. 7.8: Idadi ya Mifugo, Mwaka 2021 - 2025**

| Aina ya Mifugo | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ng'ombe | 35,256,637 | 36,584,883 | 37,913,129 | 39,241,375 | 40,569,621 | 3.4 |
| Mbuzi | 25,574,446 | 26,580,497 | 27,586,547 | 28,592,597 | 29,598,648 | 3.5 |
| Kondoo | 8,802,462 | 9,087,935 | 9,373,407 | 9,658,880 | 9,944,352 | 3.0 |
| Nguruwe | 3,439,362 | 3,670,229 | 3,901,096 | 4,131,962 | 4,362,829 | 5.6 |
| Kuku | 92,799,956 | 97,940,332 | 103,080,708 | 108,221,085 | 113,361,461 | 4.7 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

179. Mwaka 2025, tani 1,100,489.9 za nyama zilizalishwa ikilinganishwa na tani 1,054,114.0 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 4.4. Aidha, mayai milioni 7,878.3 yalizalishwa mwaka 2025 ikilinganishwa na mayai milioni 7,105.9 yaliyozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 10.9. Vilevile, uzalishaji wa maziwa uliongezeka kwa asilimia 5.2 na kufikia lita milioni 4,218.5 mwaka 2025 ikilinganishwa na lita milioni 4,009.9 zilizozalishwa mwaka 2024 (**Jedwali Na. 7.9**). Ongezeko la uzalishaji wa mazao ya mifugo lilitokana na utoaji wa elimu ya ufugaji bora wa kibiashara, kuongezeka kwa upatikanaji wa mbegu bora za ng'ombe wa maziwa na nyama pamoja na ulaji wa mazao ya mifugo.

180. Mwaka 2025, lita milioni 101.5 za maziwa zilisindikwa ikilinganishwa na lita milioni 81.9 zilizosindikwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 23.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uwezo wa usindikaji halisi wa viwanda pamoja na uwekezaji katika teknolojia ya kuongeza thamani ya maziwa. Katika kipindi hicho, vituo vya kukusanyia maziwa viliongezeka kwa asilimia 2.2 na kufikia vituo 275 ikilinganishwa na vituo 269 mwaka 2024. Aidha, lita milioni 97.8 za maziwa zilikusanywa katika vituo hivyo mwaka 2025 ikilinganishwa na lita milioni 95.6 zilizokusanywa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 2.3.

**Jedwali Na. 7.9: Uzalishaji wa Mazao ya Mifugo, Mwaka 2021 - 2025**

| Aina ya zao | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Uzalishaji wa Nyama (Tani)** | | | | | | |
| Ng'ombe | 526,350.95 | 544,983.80 | 612,808.50 | 666,227.02 | 689,811.46 | 3.5 |
| Mbuzi/Kondoo | 107,791.38 | 113,781.80 | 162,693.35 | 181,661.89 | 192,552.76 | 6.0 |
| Nguruwe | 44,420.33 | 47,583.10 | 55,912.42 | 58,775.14 | 61,784.42 | 5.1 |
| Kuku | 91,403.99 | 96,915.60 | 132,442.28 | 147,450.0 | 156,341.21 | 6.0 |
| **Jumla** | **769,966.65** | **803,264.30** | **963,856.55** | **1,054,114.03** | **1,100,489.85** | **4.4** |
| **Uzalishaji wa Maziwa ('000' Lita)** | | | | | | |
| Ng'ombe wa Asili | 2,345,650.13 | 2,400,000 | 2,637,863 | 2,605,008,454 | 2,826,414,580 | 8.5 |
| Ng'ombe wa Maziwa | 1,102,421.52 | 1,200,000 | 1,299,246 | 1,404,976,867 | 1,392,114,644 | -0.9 |
| Maziwa ya Mbuzi | - | - | 34,694 | 0 | 0 | - |
| **Jumla** | **3,448,071.65** | **3,600,000** | **3,971,803** | **4,009,985.3** | **4,218,529.2** | **5.2** |
| **Uzalishaji wa Mayai ('000')** | | | | | | |
| Mayai | 4,979,772 | 5,500,000 | 6,409,224 | 7,105,908 | 7,878,320 | 10.9 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

181. Mwaka 2025, tani 57,208 za vipande vya ngozi zilizalishwa ikilinganishwa na tani 55,410 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 3.2 (**Jedwali Na. 7.10**). Ongezeko hilo lilitokana na elimu iliyotolewa kwa wafugaji kuhusu ufugaji wa kisasa na wa kibiashara pamoja na uvunaji wa mifugo. Kati ya hizo, ngozi za ng'ombe zilikuwa tani 22,748 na ngozi za mbuzi na kondoo zilikuwa tani 34,460.

**Jedwali Na. 7.10: Uzalishaji wa Ngozi (Tani), Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Ngozi za Ng'ombe | Ngozi za Mbuzi na Kondoo | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2021 | 20,340 | 30,773 | 51,113 |
| 2022 | 21,180 | 32,076 | 53,256 |
| 2023 | 21,168 | 32,340 | 53,508 |
| 2024 | 22,080 | 33,330 | 55,410 |
| 2025 | 22,748 | 34,460 | 57,208 |

**Chanzo**: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Biashara ya Mifugo na Mazao ya Mifugo**

182. Mwaka 2025, ng'ombe 3,411,000, mbuzi 2,664,000 na kondoo 666,000 wenye thamani ya shilingi bilioni 3,700 waliuzwa katika minada nchini ikilinganishwa na ng'ombe 1,809,310 mbuzi 1,861,005 na kondoo 465,251 wenye thamani ya shilingi bilioni 1,680.07 waliouzwa mwaka 2024 (**Jedwali Na. 7.11**). Mauzo ya mifugo yaliongezeka kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi na uboreshaji wa miundombinu ya machinjio na minada.

**Jedwali Na. 7.11: Biashara ya Mifugo na Mazao ya Mifugo katika Minada Nchini, Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Ng'ombe | Kondoo | Mbuzi | Punda | Thamani (Shilingi Bilioni) |
|---|---|---|---|---|---|
| 2021 | 1,843,904 | 360,745 | 2,081,233 | 191,656 | 1,531.0 |
| 2022 | 2,194,937 | 201,610 | 1,879,623 | * | 1,741.0 |
| 2023 | 2,957,724 | 273,982 | 2,554,266 | * | 3,478.0 |
| 2024 | 1,809,310 | 465,251 | 1,861,005 | * | 1,680.1 |
| 2025 | 3,411,000 | 666,000 | 2,664,000 | * | 3,700.0 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi
*Haikuuzwa

183. Mwaka 2025, idadi ya mifugo hai iliyouzwa nje ya nchi ilikuwa ng'ombe 34,863, mbuzi na kondoo 81,059 wenye thamani ya shilingi bilioni 47.1 ikilinganishwa na ng'ombe 48,080, mbuzi na kondoo 210,643 wenye thamani ya shilingi bilioni 70.7 waliouzwa nje ya nchi mwaka 2024, sawa na upungufu wa thamani wa asilimia 33.4 (**Jedwali Na. 7.12**). Kupungua kwa idadi na thamani ya mifugo hai iliyouzwa nje ya nchi kulitokana na uboreshaji wa miundombinu ya machinjio inayotumika kuchinja mifugo kwa ajili ya soko la nje. Kuboreshwa kwa miundombinu hususan machinjio kuliwezesha kuchinja mifugo na kuuza nyama nje ya nchi badala ya kuuza mifugo hai nje ya nchi.

**Jedwali Na. 7.12: Biashara ya Mifugo Nje ya Nchi, Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Ng'ombe | Kondoo na Mbuzi | Thamani (Shilingi Bilioni) |
|---|---|---|---|
| 2021 | 24,014 | 106,099 | 46.6 |
| 2022 | 23,356 | 39,952 | 62.4 |
| 2023 | 20,536 | 37,157 | 44.4 |
| 2024 | 48,080 | 210,643 | 70.7 |
| 2025 | 34,683 | 81,059 | 47.1 |

**Chanzo**: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

184. Mwaka 2025, tani 15,693.0 za nyama zenye thamani ya shilingi bilioni 140.97 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 13,745.4 zenye thamani ya shilingi bilioni 126.7 zilizouzwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la thamani kwa asilimia 11.3. Kati ya hizo, nyama ya ng'ombe ilikuwa tani 828.57, nyama ya mbuzi tani 10,892.3, nyama ya kondoo tani 3,744.3, nyama ya kuku tani 159.4, nyama ya nguruwe tani 50.7 na nyama nyingine tani 17.7. Ongezeko la mauzo ya nyama nje ya nchi lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama nje ya nchi.

185. Mwaka 2025, tani 7,243 za vipande vya ngozi zenye thamani ya shilingi bilioni 9.12 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 6,689 zenye thamani ya shilingi bilioni 8.06 zilizouzwa nje mwaka 2024, sawa na ongezeko la thamani kwa asilimia 13.2 (**Jedwali**

**Na. 7.13**). Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya ngozi ghafi nje ya nchi, kufutwa kwa tozo ya kibali cha kusafirisha ngozi nje na kuongezeka kwa ubora wa mifugo.

**Jedwali Na. 7.13: Uuzaji wa Ngozi Nje ya Nchi (Tani), Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Ngozi za Ng'ombe (Tani) | Ngozi za Mbuzi na Kondoo (Tani) | Jumla (Tani) |
|---|---|---|---|
| 2021 | 7,251 | 120 | 7,371 |
| 2022 | 6,691 | 781 | 7,472 |
| 2023 | 4,511 | 422 | 4,933 |
| 2024 | 5,970 | 719 | 6,689 |
| 2025 | 6,782 | 461 | 7,243 |

**Chanzo**: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Uzalishaji wa Chanjo za Mifugo**

186. Mwaka 2025, Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania ilizalisha na kusambaza dozi 82,836,009 za chanjo katika halmashauri zote nchini ikilinganishwa na dozi 76,221,600 zilizozalishwa na kusambazwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 8.7. Hii ilitokana na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kuzalisha chanjo pamoja na utoaji wa elimu kwa wafugaji kuhusu umuhimu wa kuchanja mifugo. Kati ya chanjo zilizozalishwa na kusambazwa, dozi 75,154,550 zilikuwa dhidi ya ugonjwa wa mdondo, dozi 487,000 kimeta, dozi 151,450 chambavu, dozi 6,288,905 mapafu ya ng'ombe, dozi 6,800 kutupa mimba, dozi 380,504 mapafu ya mbuzi na dozi 366,800 ugonjwa wa kimeta na chambavu.

**Uzalishaji wa Malisho na Utengenezaji wa Vyakula vya Mifugo**

187. Mwaka 2025, mashamba ya Serikali yalizalisha mbegu bora za malisho zenye uzito wa kilogramu 45,492 ikilinganishwa na kilogramu 36,964 zilizozalishwa mwaka 2024. Aidha, mashamba ya Serikali yalizalisha hei marobota 169,172 mwaka 2025 ikilinganishwa na marobota 135,991 yaliyozalishwa mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mashamba ya uzalishaji wa malisho pamoja na kuendelea kuwekeza katika zana na vifaa vya shamba. Katika kipindi hicho, mashamba binafsi yalizalisha hei marobota 172,253.3 ikilinganishwa na marobota 142,332 yaliyozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 21.0. Hii ilitokana na wadau kuendelea kuwekeza katika uzalishaji wa malisho.

188. Mwaka 2025, viwanda vya kuzalisha vyakula vya mifugo vilifikia 279 kutoka viwanda 250 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 11.6. Hii ilitokana na kuendelea kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji wa sekta binafsi kulikowezesha usajili wa viwanda vipya katika mikoa ya Arusha (viwanda vinne 4), Dar es Salaam (viwanda 11), Pwani (6), Morogoro (2), Njombe (2), Tanga (1), Manyara (1), Rukwa (1) na Kigoma (1). Hata hivyo, uzalishaji wa vyakula vya mifugo katika viwanda vya sekta binafsi ulipungua kwa asilimia 61.7 na kufikia tani 720,000 mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 1,880,000

zilizozalishwa mwaka 2024. Upungufu huo ulitokana na uhaba wa malighafi za vyakula vya mifugo.

**Mafunzo ya Mifugo**

189. Mwaka 2025, Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo ulidahili wanafunzi 4,991 katika ngazi ya astashahada na stashahada ikilinganishwa na wanafunzi 4,936 waliodahiliwa mwaka 2024. Ongezeko la udahili lilitokana na Serikali kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi, kuhuishwa kwa mitaala ya mafunzo, kuboreshwa kwa mazingira ya kufundishia na kujifunzia pamoja na kuongezeka kwa wakufunzi.

**Utafiti wa Mifugo**

190. Mwaka 2025, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania - TALIRI ilifanya tafiti 51 ikilinganishwa na tafiti 57 zilizofanyika mwaka 2024. Tafiti hizo zilihusu uboreshaji wa mbari za mifugo, uendelezaji wa malisho na uzalishaji wa mbegu bora za malisho. Tafiti hizo ziliwezesha uzalishaji na usambazaji wa ng'ombe chotara 450 wa nyama na maziwa na mbuzi chotara 407 katika wilaya za Bahi, Mpwapwa, Mkuranga, Morogoro na Muheza pamoja na Jiji la Tanga na Jiji la Mbeya. Aidha, kondoo 65 walizalishwa kupitia tafiti zilizofanyika na kusambazwa katika wilaya za Siha na Longido mwaka 2025 ikilinganishwa na kondoo 56 waliozalishwa mwaka 2024.

191. Mwaka 2025, TALIRI ilizalisha na kusambaza kilogramu 8,569 za mbegu bora za malisho (punje na vipando) ikilinganishwa na kilogramu 5,589 za mbegu zilizozalishwa na kusambazwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 53.3. Hii ilitokana na kuendelea na uboreshaji wa mitambo, ununuzi wa vifaa shamba na upanuzi wa mashamba. Mbegu hizo zilisambazwa katika mikoa ya Dodoma, Rukwa, Mbeya, Tabora, Pwani, Kilimanjaro, Kigoma, Shinyanga, Tanga, Simiyu, Mara, Mwanza, Morogoro, Manyara na Arusha.

**Huduma za Ugani katika Mifugo**

192. Mwaka 2025, Serikali ilitoa mafunzo rejea kwa maafisa ugani 523 ikilinganishwa na maafisa ugani 1,058 mwaka 2024. Katika kipindi hicho, maafisa ugani 3,764 na wafugaji 196,543 walisajiliwa katika mfumo wa M-Kilimo na wa Utambuzi mtawalia ikilinganishwa na maafisa ugani 3,517 na wafugaji 2,879 waliosajiliwa mwaka 2024. Ongezeko la usajili wa wafugaji lilitokana na kuanza kutumika kwa mfumo wa Utambuzi. Aidha, pikipiki 700 zilitolewa kwa maafisa ugani mwaka 2025 ili kuboresha utoaji wa huduma ikilinganishwa na pikipiki 252 zilizotolewa mwaka 2024. Vilevile, vishikwambi 4,500, masanduku ya ubaridi 3,270, mabomba na sindano 3,270, mabuti 2,180 na makoti 2,180 yalinunuliwa na kusambazwa kwa maafisa ugani.

## UVUVI

### Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi

193. Mwaka 2025, Serikali kupitia ulinzi na usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi iliwezesha kukamatwa kwa vifaa na zana mbalimbali zinazotumika katika uvuvi haramu kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 7.14**. Aidha, samaki wachanga kilogramu 70,562, kaa wachanga kilogramu 10,342 na jongoo bahari kilogramu 550 walikamatwa na kuteketezwa kwa idhini ya mahakama. Vilevile, watuhumiwa 1,031 wa uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira walikamatwa na kulipa faini ya shilingi milion 1,900 mwaka 2025 ikilinganishwa na watuhumiwa 990 waliokamatwa na kulipa faini ya shilingi milioni 372.5 mwaka 2024.

**Jedwali Na. 7.14: Vifaa na Zana Zilizokamatwa katika Uvuvi Haramu, Mwaka 2022 - 2025**

| Na. | Zana Zilizokamatwa | Mwaka | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
| 1 | Nyavu za Makila | 2,988 | 176 | 460 | 875 |
| 2 | Kokoro | 2,268 | 416 | 386 | 485 |
| 3 | Nyavu za timba | 11,264 | 3,842 | 2,138 | 5,760 |
| 4 | Nyavu za dagaa | 443 | 10 | 12 | 89 |
| 5 | Vyandarua | 42 | 0 | 42 | 20 |
| 6 | Pikipiki | 0 | 4 | 0 | 0 |
| 7 | Magari | 0 | 1 | 0 | 0 |
| 8 | Kamba za kokoro (mita) | 290,133 | 362,509 | 307,350 | 618,320 |
| 9 | Nyavu za gonga | 1 | 0 | 0 | 0 |
| 10 | Boti | 60 | 17 | 30 | 88 |
| 11 | Mitumbwi | 380 | 432 | 301 | 631 |
| 12 | Injini za boti | 70 | 80 | 66 | 21 |
| 13 | Kasia | 2 | 2 | 53 | 0 |
| 14 | Kipe | 1 | 0 | 0 | 0 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

### Ukuzaji Viumbe Maji

194. Mwaka 2025, wakuzaji viumbe maji walikuwa 49,084 ikilinganishwa na wakuzaji viumbe maji 35,986 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 36.4. Hii ilitokana na kuendelea kutolewa kwa elimu ya ugani kuhusu ukuzaji viumbe maji, mikopo ya vizimba pamoja na pembejeo za kilimo cha mwani. Aidha, mabwawa ya kufugia samaki yalikuwa 34,642 mwaka 2025 ikilinganishwa na mabwawa 34,417 mwaka 2024. Vilevile, vizimba vya kuzalishia samaki katika maziwa viliongezeka kwa asilimia 34.7 na kufikia vizimba 1,636 mwaka 2025 ikilinganishwa na vizimba 1,215 mwaka 2024. Kati ya hivyo, vizimba 1,620 viko katika Ziwa Victoria na vizimba 16 katika Ziwa Tanganyika.

195. Mwaka 2025, vifaranga 140,018,196 vya samaki vilizalishwa ikilinganishwa na vifaranga 66,684,806 vilivyozalishwa mwaka 2024 (**Jedwali Na. 7.15**). Kati ya hivyo, vituo vya sekta binafsi vilizalisha vifaranga 127,540,428 na vituo vya umma vilizalisha vifaranga 12,477,768. Ongezeko la uzalishaji lilitokana na matumizi ya mbinu bora za ukuzaji viumbe maji na uboreshwaji wa mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara, ikiwemo kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na ushuru wa forodha katika uingizaji wa pembejeo na vifaa mbalimbali vya ukuzaji viumbe maji. Aidha, tani 17,928.5 za chakula cha samaki zilitumika mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 7,911.4 zilizotumika mwaka 2024. Ongezeko la matumizi ya chakula cha samaki lilitokana na uwekezaji katika vizimba na mabwawa. Kati ya kiasi cha chakula cha samaki kilichotumika, tani 7,336.0 zilizalishwa nchini na tani 10,592.5 ziliingizwa kutoka nje ya nchi. Vilevile, wananchi 14,940 walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora za ufugaji samaki na udhibiti wa magonjwa mwaka 2025 ikilinganishwa na wananchi 11,723 mwaka 2024.

**Jedwali Na. 7.15: Maendeleo katika Ukuzaji Viumbe Maji, Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Idadi ya Wakuzaji Viumbe Maji | Idadi ya Mabwawa ya Samaki | Idadi ya Vizimba | Idadi ya Vifaranga |
|---|---:|---:|---:|---:|
| 2021 | 30,064 | 30,032 | 473 | 27,120,320 |
| 2022 | 31,998 | 31,407 | 780 | 29,295,638 |
| 2023 | 34,057 | 32,878 | 993 | 35,967,180 |
| 2024 | 35,986 | 34,417 | 1,215 | 66,684,806 |
| 2025 | 49,084 | 34,642 | 1,636 | 140,018,196 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

196. Mwaka 2025, tani 43,590.5 za samaki (sato na kambale) zenye thamani ya shilingi bilioni 305 zilizalishwa ikilinganishwa na tani 34,828.5 zenye thamani ya shilingi bilioni 261 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la uzalishaji la asilimia 25.2. Hii ilitokana na upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu, matumizi ya mbinu bora za ukuzaji viumbe maji na uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara. Aidha, uzalishaji wa mwani ulikuwa tani 9,497.7 zenye thamani ya shilingi bilioni 9.97 mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 8,637.8 zenye thamani ya shilingi bilioni 9.10 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la uzalishaji la asilimia 10.0 (**Jedwali Na. 7.16**). Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mwani katika masoko ya nje ya nchi, ikiwemo China, Korea, Vietnam na Ulaya.

**Jedwali Na. 7.16: Mwenendo wa Ukuzaji Viumbe Maji, Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Samaki (Sato na Kambale) (Tani) | Samaki Maji Chumvi Mwatiko (Tani) | Mwani (Tani) | Kambamiti (Tani) | Kambakoche (Tani) | Kaa (Kg) | Majongoo Bahari (Kg) | Lulu (Vipande) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2021 | 20,258.0 | - | 2,438.0 | 97.0 | - | 410.0 | 115.0 | 360.0 |
| 2022 | 25,286.5 | 6.0 | 3,514.8 | 74.9 | 30.0 | 1,144.0 | 370.0 | 164.0 |
| 2023 | 29,106.6 | - | 4,379.1 | - | 30.0 | 600.0 | 860.0 | 550.0 |
| 2024 | 34,828.5 | - | 8,637.8 | 5.2 | 30.0 | 2,500.0 | 1,500.0 | 250.0 |
| 2025 | 43,590.5 | - | 9,497.7 | 1.2 | - | 2,840.0 | 35,630.0 | 360.0 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Uvunaji wa Samaki**

197. Mwaka 2025, tani 519,650.5 za samaki zenye thamani ya shilingi bilioni 5,375.78 zilivunwa ikilinganishwa na tani 522,788.3 zenye thamani ya shilingi bilioni 4,352.73 zilizovunwa mwaka 2024 (**Jedwali Na. 7.17**). Upungufu wa uvunaji wa samaki ulitokana na kupungua kwa uvunaji wa samaki katika maji baridi kulikochangiwa na ukosefu wa vyombo vya kisasa vya uvuvi na mabadiliko ya tabianchi. Kati ya kiasi kilichovunwa, tani 452,697.1 zilivunwa katika maji baridi na tani 66,953.4 katika maji chumvi.

**Jedwali Na. 7.17: Uvunaji wa Samaki (Tani), Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Maji baridi | Maji chumvi | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2021 | 414,104.8 | 62,914.0 | 477,018.8 |
| 2022 | 404,639.1 | 66,873.4 | 471,512.5 |
| 2023 | 415,879.6 | 64,097.0 | 479,977.6 |
| 2024 | 458,799.6 | 63,988.8 | 522,788.3 |
| 2025 | 452,697.1 | 66,953.4 | 519,650.5 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Udhibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi**

198. Mwaka 2025, kaguzi 8,452 zilifanyika ili kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi ikilinganishwa na kaguzi 7,652 zilizofanyika mwaka 2024. Kaguzi hizo zilifanyika katika viwanda 64 vikubwa na vya kati vya kuchakata mazao ya uvuvi, mialo 143, masoko sita (6), maghala 555 na vyombo sita (6) vya kusafirisha mazao ya uvuvi. Aidha, vibali 46,026 vilitolewa kwa wafanyabiashara wa mialoni kwa ajili ya kuuza tani 44,810.6 za mazao ya uvuvi katika masoko ya ndani mwaka 2025 ikilinganishwa na vibali 18,232 vilivyotolewa kwa uuzaji wa tani 24,372.7 mwaka 2024. Ongezeko la vibali lilitokana na kuendelea kwa utaratibu wa utoaji wa kibali kwa kila mfanyabiashara badala ya kibali kimoja kutumika na mfanyabiashara zaidi ya mmoja. Vilevile, vyeti vya afya 9,644 vilitolewa kwa wafanyabiashara kwa ajili ya uuzaji wa tani 31,034.1 za mazao ya uvuvi nje ya nchi mwaka 2025 ikilinganishwa na vyeti 8,711 vilivyotolewa kwa uuzaji wa tani 39,792.0 mwaka 2024.

199. Mwaka 2025, Maabara ya Taifa ya Uvuvi ilifanya uchunguzi wa vimelea na kemikali katika sampuli 3,325 za samaki, mazao ya uvuvi, maji na vyakula ikilinganishwa na sampuli 2,938 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 13.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uchakataji wa samaki na mazao ya uvuvi kwa wafanyabiashara wadogo na viwandani wanaojihusisha na usafirishaji wa samaki na mazao ya uvuvi katika soko la ndani na nje ya nchi. Kati ya sampuli zilizofanyiwa uchunguzi, sampuli 3,315, sawa na asilimia 99.7 zilikidhi viwango vya ubora vinavyokubalika kimataifa mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 98.7 ya sampuli zilizokidhi viwango mwaka 2024.

**Uuzaji na Uagizaji wa Mazao ya Uvuvi Nje ya Nchi**

200. Mwaka 2025, samaki hai wa mapambo 259,876 na tani 45,053.4 za mazao ya uvuvi zenye thamani ya shilingi bilioni 648.91 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na samaki hai wa mapambo 173,377 na tani 59,746.4 za mazao ya uvuvi zenye thamani ya shilingi bilioni 677.55 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2024. Kupungua kwa mauzo ya mazao ya uvuvi nje ya nchi kulitokana na kupungua kwa uzalishaji na uchakataji wa samaki. Katika kipindi hicho, mapato ya mrabaha yaliyotokana na mauzo ya mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo nje ya nchi yalikuwa shilingi bilioni 16.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 19.9 mwaka 2024. Aidha, mauzo ya mazao ya uvuvi yalijumuisha tani 395.6 za mabondo zenye thamani ya shilingi bilioni 125.36 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 424.5 za mabondo zenye thamani ya shilingi bilioni 176.84 mwaka 2024. Kupungua kwa mauzo ya mabondo nje ya nchi kulitokana na kupungua kwa uzalishaji wa sangara. Mauzo ya mabondo yaliwezesha upatikanaji wa mapato ya shilingi bilioni 3.52 kama mrabaha mwaka 2025 ikilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 3.74 mwaka 2024.

201. Mwaka 2025, tani 5,455.0 za samaki zenye thamani ya shilingi milioni 9,183.1 ziliingizwa nchini ikilinganishwa na tani 6.5 zenye thamani ya shilingi milioni 99.91 mwaka 2024. Kuongezeka kwa uingizaji wa samaki kulitokana na kuongezeka kwa ulaji wa samaki wa mtu kwa mwaka kutoka kilo 7.9 hadi kilo 10.2 hivyo kupelekea kuongezeka kwa mahitaji ya samaki nchini sambamba na kupunguzwa kwa tozo za uagizaji wa samaki. Mathalani, mahitaji halisi ya samaki nchini yalikuwa tani 1,253,344.7 mwaka 2025 ambapo uzalishaji wa ndani baada ya kuondoa mauzo nje ya nchi ni tani 518,187.5 (tani 474,597 za samaki kutoka maji ya asili na tani 43,590.5 kutokana na ukuzaji viumbe maji), hivyo nchi ilikuwa na nakisi ya tani 735,157.2 za samaki kwa mwaka 2025. Aidha, mapato ya mrabaha yaliyotokana na uagizaji wa samaki yalikuwa shilingi milioni 7,200 mwaka 2025 ikilinganishwa na mapato ya shilingi milioni 26.63 mwaka 2024.

**Uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi**

202. Mwaka 2025, Serikali iliendelea na jitihada za kuboresha sekta ya uvuvi kwa kujenga Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko. Hadi Desemba 2025, ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko ulifika asilimia 90 ambapo kazi zilizofanyika zilikuwa: kuongeza kina

cha maji (dredging) ili kuwezesha meli kutia nanga (kugoa); kuchimba na kuondoa udongo usiofaa katika eneo la ujenzi; kujaza na kushindiria udongo maalumu wa mchanga mita za ujazo 112,583 katika eneo la ujenzi; kukamilisha ujenzi wa gati la mita 315; na kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya majitaka, majisafi na mafuta. Aidha, ujenzi wa jengo la kupokelea samaki, soko la samaki, barabara na jengo la utawala upo hatua za ukamilishaji. Vilevile, ujenzi wa meli ya uvuvi wa Bahari Kuu kutoka nchini Japan ulikuwa umefikia hatua za mwisho. Aidha mchakato wa ununuzi wa meli mpya mbili za uvuvi wa bahari kuu ulikuwa katika hatua za kutangazwa.

203. Mwaka 2025, masoko ya samaki yalifikia 21 kutoka masoko saba (7) mwaka 2024. Aidha, mialo ya samaki ilifikia 143 mwaka 2025 kutoka mialo 130 iliyokuwepo mwaka 2024. Vilevile, maghala ya kuhifadhia mazao ya uvuvi yaliongezeka na kufikia 555 mwaka 2025 kutoka maghala 98 mwaka 2024. Ongezeko la maghala lilitokana na urasimishaji wa maghala. Kwa upande mwingine, vyombo vya kusafirisha mazao ya uvuvi viliongezeka kwa asilimia 2.0 na kufikia vyombo 2,694 (magari 2,156 na vyombo vya uvuvi 538) mwaka 2025 ikilinganishwa na vyombo 2,641 vya kusafirisha mazao ya uvuvi mwaka 2024.

204. Hadi Desemba 2025, viwanda vikubwa vya samaki vilifikia 64 na viwanda vidogo 38 ikilinganishwa na viwanda vikubwa 25 na viwanda vidogo 32 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko la viwanda lilitokana na kuendelea kwa uwekezaji katika sekta ya uvuvi. Aidha, viwanda vya kati vya kutengeneza nyavu vilifikia sita (6), viwanda vya kutengeneza boti vitatu (3), na viwanda 18 vya kuchakata mabondo mwaka 2025 kama ilivyokuwa mwaka 2024.

205. Mwaka 2025, wageni 49,856 walitembelea maeneo ya hifadhi za bahari ikilinganishwa na wageni 49,108 waliotembelea mwaka 2024. Aidha, mapato ya shilingi milioni 2,521.6 yalikusanywa kutokana na wageni waliotembelea maeneo ya hifadhi za bahari mwaka 2025 ikilinganishwa na mapato ya shilingi milioni 2,727.5 yaliyokusanywa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 7.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika utalii wa kiikolojia uliofanywa na Serikali kupitia Kitengo cha Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu - MPRU.

**Mafunzo ya Uvuvi**

206. Mwaka 2025, Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi ulidahili wanafunzi 1,092 ikilinganishwa na wanafunzi 1,116 waliodahiliwa mwaka 2024. Katika kipindi hicho, wavuvi na wakuzaji viumbe maji 11,364 walipatiwa mafunzo kuhusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi, upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa na ukuzaji viumbe maji ikilinganishwa na wavuvi na wakuzaji viumbe maji 10,892 waliopatiwa mafunzo mwaka 2024.

## MAENDELEO YA USHIRIKA

207. Mwaka 2025, vyama vya ushirika vilifikia 7,143 kutoka vyama 7,820 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 8.7. Kupungua kwa vyama kulitokana na uhakiki na uhuishaji wa taarifa za vyama uliowezesha kuondoa vyama visivyokuwa hai au vilivyokuwa vinajirudia kwenye kumbukumbu. Kati ya hivyo, vyama vya masoko ya mazao vilikuwa 4,330, vyama vya akiba na mikopo 1,367, vyama vya aina nyingine 1,369 na vyama vikuu vilikuwa 77. Katika kipindi hicho, wanachama wa vyama vya ushirika walifikia 2,827,894 kutoka wanachama 8,405,413 mwaka 2024. Kupungua kwa wanachama kulitokana na uhakiki na uhuishaji wa taarifa za vyama uliowezesha kuondoa vyama visivyokuwa hai au vilivyokuwa vinajirudia kwenye kumbukumbu. Aidha, viwanda vya kuchakata mazao vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika vilifikia 336 mwaka 2025 kutoka viwanda 329 mwaka 2024.

208. Mwaka 2025, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika - COASCO lilikagua hesabu za vyama vya ushirika 4,884 ikilinganishwa na vyama 4,760 vilivyokaguliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 2.6. Kati ya hivyo, vyama 916 sawa na asilimia 18.8 vilipata hati inayoridhisha kwa kufuata kanuni na taratibu zote zinazohitajika, vyama 3,300 (asilimia 67.6) vilipata hati yenye mashaka, vyama 585 (asilimia 12.0) vilipata hati mbaya kwa kutozingatia kanuni na taratibu na vyama 83 (asilimia 1.6) vilipata hati isiyo na maoni. Aidha, COASCO ilitoa mafunzo kwa viongozi wa bodi 1,357 na watendaji 1,656 wa vyama vya ushirika kuhusu uzingatiaji wa miongozo mbalimbali ya ushirika, haki na wajibu kwa mwanachama, uongozi bora pamoja na uandishi wa vitabu vya hesabu.

## MIZANIA YA CHAKULA NCHINI

### Dhana ya Mizania ya Chakula

209. Mizania ya Chakula - FBS ni mfumo wenye takwimu jumuishi zinazotoa taswira pana ya ugavi na matumizi ya chakula nchini katika kipindi maalum. Aidha, FBS hutoa viashiria muhimu vya upatikanaji wa chakula, ikiwemo wastani wa nishati lishe (kilokalori), protini na mafuta kwa kila mtu. Vilevile, FBS hutoa viashiria vya usalama wa chakula kama vile Kiwango cha Utoshelevu wa Chakula - SSR na Kiwango cha Utegemezi wa Uagizaji wa Chakula kutoka Nje ya Nchi - IDR.

### Upatikanaji wa Nishati ya Chakula

210. Mwaka 2025, wastani wa kiwango cha upatikanaji wa nishati ya chakula - DES kwa mtu kwa siku ulikuwa kilokalori 2,593 ikilinganishwa na kilokalori 2,645 kwa mtu kwa siku mwaka 2024. Aidha, mazao ya asili ya mimea yaliendelea kuwa chanzo kikuu cha nishati ya chakula ambayo yalichangia asilimia 90.1 ya kiwango chote cha upatikanaji wa nishati ya chakula. Kwa upande mwingine, mazao asili ya wanyama yalichangia asilimia 9.9 ya kiwango chote cha upatikanaji wa nishati ya chakula. Licha ya mazao asili ya wanyama

kuwa na mchango mdogo katika DES, wastani wa kiwango cha upatikanaji wa nishati hiyo uliendelea kuimarika kutokana na mabadiliko ya taratibu katika mifumo ya ulaji na kufika kilokalori 256 kwa mtu kwa siku mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa kilokalori 246 kwa kila mtu kwa siku mwaka 2024 (**Jedwali Na. 7.18**).


**Jedwali Na. 7.18: Mwenendo wa Wastani wa Upatikanaji wa Nishati Lishe (Kilokalori) kwa Mtu kwa Siku, Mwaka 2018 - 2025**

| **Mwaka** | **2018** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mazao Asili ya Mimea | 2,269 | 2,298 | 2,263 | 2,304 | 2,349 | 2,416 | 2,399 | 2,337 |
| Mazao Asili ya Wanyama | 203 | 208 | 210 | 222 | 219 | 239 | 246 | 256 |
| **Jumla** | **2,472** | **2,506** | **2,472** | **2,526** | **2,567** | **2,655** | **2,645** | **2,593** |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

211. Kwa kuzingatia makundi makuu ya vyakula, bidhaa na mazao ya nafaka (isipokuwa bia) yaliongoza kwa mchango katika upatikanaji wa nishati lishe yakichangia asilimia 51.1 mwaka 2025 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 50.6 mwaka 2024. Hii ilifuatiwa na mazao ya mizizi na mazao jamii ya kunde yaliyochangia asilimia 13.7 na asilimia 7.2 mtawalia mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 12.2 na asilimia 6.7 mwaka 2024. Aidha, mchango wa bidhaa za wanyama kama maziwa na nyama ulikuwa asilimia 4.2 na asilimia 3.4 mtawalia mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 4.1 na asilimia 3.4 mwaka 2024 (**Kielelezo Na. 7.1**).

**Kielelezo Na. 7.1: Mgawanyo wa Upatikanaji wa Nishati Lishe kwa Makundi Makuu ya Vyakula (Asilimia), Mwaka 2024 - 2025**





## Kiwango cha Utoshelevu wa Chakula

212. Kiwango cha Utoshelevu wa Chakula - SSR hupima kiwango ambacho uzalishaji wa ndani unakidhi mahitaji ya chakula ya nchi. Kwa muktadha wa FBS, ukokotoaji wa SSR huzingatia upatikanaji wa chakula unaojumuisha uzalishaji wa ndani, mauzo ya chakula nje

ya nchi, uagizaji wa chakula kutoka nje na mabadiliko katika akiba ya chakula (stock change). Aidha, ukokotoaji huo unajumuisha makundi ya chakula yanayotokana na mazao ya kilimo (mimea), wanyama na samaki. Kiwango cha asilimia 100 cha SSR kinaonesha kuwa uzalishaji wa ndani unakidhi mahitaji, na SSR chini ya asilimia 100 inaonesha utegemezi wa uagizaji kutoka nje. Vilevile, kiwango cha SSR zaidi ya asilimia 100 kinaashiria kuwepo kwa ziada katika uzalishaji wa ndani. Mwaka 2025, kiwango cha Utoshelevu wa Chakula kiliendelea kuwa asilimia 112 kama ilivyokuwa mwaka 2024 (**Kielelezo Na. 7.2**).


**Kielelezo Na. 7.2: Kiwango cha Utoshelevu wa Chakula, Mwaka 2018 - 2025**




**Kiwango cha Utegemezi wa Uagizaji wa Chakula Kutoka Nje ya Nchi**

213. Kiwango cha Utegemezi wa Uagizaji wa Chakula Kutoka Nje ya Nchi - IDR hupima sehemu ya upatikanaji wa chakula inayotokana na uagizaji kutoka nje ya nchi. Mwaka 2025, Kiwango cha IDR kilipungua na kufikia asilimia 9 ikilinganishwa na asilimia 11 mwaka 2024 (**Kielelezo Na. 7.3)**. Kiwango hiki kinaashiria kupungua kwa utegemezi na kuimarika kwa uzalishaji wa chakula nchini.

**Kielelezo Na. 7.3: Kiwango cha Utegemezi wa Uagizaji wa Chakula kutoka Nje ya Nchi, Mwaka 2018 - 2025**



**Jedwali Na. 38: UZALISHAJI WA MIWA NA SUKARI NCHINI, MWAKA 2009/10 - 2024/25**

| Msimu[1] | Miwa | | | | Sukari | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wakulima | | Jumla (000 Tani) | Bei[2] (Shs/Tani) | Iliyozalishwa (Tani) | iliyotumika[3] (Tani) | Kilo kwa mtu[4] |
| | Umma (000 Tani) | Binafsi (000 Tani) | | | | | |
| 2009/10 | 1,972 | 598 | 2,570 | 42,046 | 263,461 | 398,070 | 13.7 |
| 2010/11 | 2,357 | 661 | 3,018 | 43,865 | 304,135 | 410,259 | 12.0 |
| 2011/12 | 2,036 | 680 | 2,716 | 48,833 | 262,879 | 439,307 | 12.0 |
| 2012/13 | 2,242 | 711 | 2,953 | 52,167 | 296,698 | 468,000 | 12.0 |
| 2013/14 | 2,198 | 602 | 2,800 | 50,500 | 294,300 | 434,782 | 12.0 |
| 2014/15 | 2,466 | 697 | 3,163 | 51,333 | 304,007 | 511,680 | 12.0 |
| 2015/16 | 2,270 | 569 | 2,839 | 59,707 | 293,075 | 525,784 | 12.0 |
| 2016/17 | 2,504 | 557 | 3,061 | 72,667 | 324,930 | 456,000 | 12.8 |
| 2017/18 | 2,550 | 626 | 3,175 | 72,667 | 303,752 | 515,004 | 13.5 |
| 2018/19 | 2,792 | 797 | 3,589 | 72,667 | 359,219 | 524,772 | 13.5 |
| 2019/20 | 2,659 | 728 | 3,387 | 77,333 | 311,358 | 372,787 | 12.8 |
| 2020/21 | 2,985 | 1,092 | 4,014 | 79,000 | 367,718 | - | 12.0 |
| 2021/22 | 2,697 | 1,060 | 3,757 | 77,500 | 379,281 | 379,281 | 12.0 |
| 2022/23r | 3,396 | 1,046 | 4,442 | 78,375 | 460,049 | 460,049 | 12.0 |
| 2023/24 | 3,377 | 865 | 4,242 | 75,000 | 395,293 | 783,487 | 12.0 |
| 2024/25 | 1,196 | 3,737 | 4,933 | 110,000 | 453,383 | 829,896 | 12.0 |
| **Badiliko 2024/25 - 2023/24 (Asilimia)** | **-64.6** | **332.0** | **16.3** | **46.7** | **14.7** | **5.9** | **0.0** |

**Chanzo:** Bodi ya Sukari Tanzania

1 Msimu ni Kati ya Julai na Juni

2 Bei ya Mimea ni ile iliyo na asilimia 10 za Sucrose

3 Ni pamoja na Sukari iliyopelekwa Zanzibar

4 Ni kwa Tanzania bara

**Jedwali Na. 39: PAMBA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI, MWAKA 2009/10 - 2024/25**

| Msimu [1] | Pamba yenye Mbegu | | Pamba iliyoondolewa Mbegu | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Uzalishaji (Tani) | Bei ya wastani (Shs/kg) | Kiasi (Tani) | Mauzo nchini | |
| | | | | Kiasi (Tani)[2] | Bei ya wastani (Shs/tani) |
| 2009/10 | 267,644 | 480 | 54,851 | .. | .. |
| 2010/11 | 163,518 | 900 | 54,809 | .. | .. |
| 2011/12 | 225,938 | 1,000 | 75,731 | .. | .. |
| 2012/13 | 351,156 | 660 | 117,702 | .. | .. |
| 2013/14 | 245,815 | 700 | 82,394 | .. | .. |
| 2014/15 | 202,312 | 750 | 67,812 | | |
| 2015/16 | 149,765 | 800 | 50,199 | 525,784 | |
| 2016/17 | 132,934 | 1,000 | 42,203 | - | - |
| 2017/18 | 222,790 | 1,100 | 80,575 | 39,244 | 3,667 |
| 2018/19 | 348,901 | 1,200 | 129,408 | 51,942 | 3,123 |
| 2019/20 | 348,958 | 1,200 | 128,660 | 25,162 | 3,781 |
| 2020/21 | 122,836 | 900 | 46,923 | 9,479 | 2,924 |
| 2021/22 | 144,792 | 1,800 | 67,178 | 14,779 | 2,761 |
| 2022/23r | 174,486 | 1,150 | 108,633 | 11,950 | 1,952 |
| 2023/24 | 282,510 | 1,400 | 108,766 | 13,052 | 2,557 |
| 2024/25 | 221,853 | 1,150 | 84,061 | 20,175 | 1,600 |
| **Badiliko (Asilimia) 2024/25 - 2023/24** | **-21.5** | **-17.9** | **-22.7** | **54.6** | **-37.4** |

**Chanzo:** Bodi ya Mauzo ya Pamba
[1]Msimu ni kati ya Juni na Mei
Takwimu hazikupatikana

**Jedwali Na. 40: ENEO LILILOPANDWA CHAI NA MAJANI MABICHI YALIYOPATIKANA, MWAKA 2009/10 - 2024/25**

| Msimu [1] | Eneo lililopandwa (Hekta) | | | Majani Mabichi yaliyopatikana (Tani) | | | | | | Bei kwa Mkulima (Shs/Kilo) | Mauzo Nchini[2] (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Kiumilikaji: mashamba | | | Kikanda: mashamba | | | | |
| | Makubwa | Madogo | Jumla | Makubwa | Madogo | Jumla | Kaskazini | Kusini | Jumla | | |
| 2009/10 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 106,021 | 44,716 | 150,737 | 33,309 | 117,428 | 150,737 | 124 | 5,084 |
| 2010/11 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 95,511 | 47,616 | 143,127 | 112,368 | 30,759 | 143,127 | 152 | 6,065 |
| 2011/12 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 88,582 | 52,359 | 140,941 | 27,009 | 113,932 | 140,941 | 200 | 4,839 |
| 2012/13 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 113,628 | 54,872 | 168,500 | 30,997 | 137,503 | 168,500 | 206 | 5,498 |
| 2013/14 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 101,489 | 47,001 | 148,490 | 27,935 | 120,555 | 148,490 | 225 | 5,672 |
| 2014/15 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 100,018 | 52,467 | 152,485 | 23,283 | 129,202 | 152,485 | 176 | 6,302 |
| 2015/16 | 11,272 | 11,449 | 22,721 | 96,759 | 44,605 | 141,364 | 25,413 | 115,915 | 141,328 | 230 | 10,257 |
| 2016/17 | 11,272 | 11,449 | 22,722 | 78,929 | 41,495 | 120,424 | 20,592 | 99,832 | 120,424 | 285 | 4,648 |
| 2017/18 | 11,322 | 11,705 | 23,028 | 97,428 | 55,620 | 153,048 | 31,599 | 121,449 | 153,048 | 299 | 5,434 |
| 2018/19 | 11,322 | 11,705 | 23,027 | 104,203 | 61,081 | 165,284 | 36,506 | 128,778 | 165,284 | 312 | 3,926 |
| 2019/20 | 12,445 | 11,030 | 23,475 | 76,028 | 53,188 | 129,216 | 22,930 | 106,286 | 129,216 | 312 | 27,128 |
| 2020/21 | 12,445 | 11,361 | 23,806 | 72,138 | 51,655 | 123,793 | 25,178 | 98,614 | 123,792 | 312 | 28,875 |
| 2021/22 | 12,445 | 11,361 | 23,806 | 73,030 | 54,203 | 127,233 | 25,872 | 101,361 | 127,233 | 314 | 4,312 |
| 2022/23r | 12,445 | 11,361 | 23,806 | 58,729 | 45,209 | 103,938 | 16,735 | 87,203 | 103,938 | 366 | 3,414 |
| 2023/24 | 11,272 | 11,500 | 22,772 | 55,526 | 44,991 | 100,517 | 15,260 | 85,257 | 100,517 | 366 | 2,672 |
| 2024/25 | 11,501 | 11,221 | 22,722 | 58,235 | 42,944 | 101,179 | 21,510 | 79,668 | 101,178 | 366 | 2,923 |
| **Badiliko 2024/25 - 2023/24 (Asilimia)** | **2.0** | **-2.4** | **-0.2** | **4.9** | **-4.5** | **0.7** | **41.0** | **-6.6** | **0.7** | **0.0** | **9.4** |

**Chanzo:** Bodi ya Chai Tanzania

1Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Chai iliyotengenezwa

**Jedwali Na. 41: ENEO LILILOPANDWA MKONGE NA KATANI ILIYOPATIKANA, MWAKA 2009/10 - 2024/25**

| Msimu[1] | Eneo (Hekta) | | | Katani iliyopatikana | | Mauzo Nchini+ | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uliokomaa | Usiokomaa | Jumla | Kiasi (Tani) | Bei kwa Mkulima (Shs/Tani) | Kiasi (Tani) | Thamani (Shilingi Milioni) |
| 2009/10 | 30,556 | 11,849 | 42,405 | 24,092 | 1,200,000 | 12,761 | 10,375 |
| 2010/11 | 31,117 | 12,169 | 43,286 | 25,090 | 1,300,000 | 11,617 | 13,154 |
| 2011/12 | 32,601 | 14,302 | 46,903 | 36,600 | 1,500,000 | 11,511 | 14,390 |
| 2012/13 | 33,649 | 11,994 | 45,643 | 34,874 | 1,600,000 | 11,466 | 16,823 |
| 2013/14 | 35,266 | 11,044 | 46,310 | 37,805 | 1,724,864 | 9,160 | - |
| 2014/15 | 35,946 | 12,494 | 48,440 | 38,872 | 2,071,446 | 8,972 | 17,513 |
| 2015/16 | 34,723 | 13,231 | 47,954 | 41,795 | 2,700,000 | 9,075 | 20,342 |
| 2016/17 | 41,661 | 12,850 | 54,511 | 36,533 | 2,700,000 | 9,559 | 21,541 |
| 2017/18 | 40,635 | 14,389 | 55,024 | 43,280 | 3,000,000 | 12,111 | 30,803 |
| 2018/19 | 43,406 | 18,031 | 61,437 | 33,271 | 3,300,000 | 14,646 | 43,907 |
| 2019/20 | 41,757 | 17,044 | 58,801 | 35,341 | 3,500,000 | 12,646 | 38,323 |
| 2020/21 | 41,685 | 16,898 | 58,583 | 39,343 | 3,500,000 | 13,440 | 39,545 |
| 2021/22 | 45,505 | 21,687 | 67,192 | 48,359 | 3,626,139 | 12,428 | 45,065 |
| 2022/23r | 47,774 | 24,575 | 72,349 | 56,773 | 3,482,613 | 14,289 | 49,710 |
| 2023/24 | 73,687 | 25,689 | 99,376 | 61,216 | 3,566,226 | 15,120 | 53,921 |
| 2024/25 | 47,849 | 18,343 | 66,193 | 66,973 | 3,966,792 | 11,600 | 46,014 |
| **Badiliko (Asilimia) 2024/25 - 2023/24** | **-35.1** | **-28.6** | **-33.4** | **9.4** | **11.2** | **-23.3** | **-14.7** |

**Chanzo:** Bodi ya Katani

Katani aina ya Line fibre, Tow na Flume Tow

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

### Jedwali Na. 42: UZALISHAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI, MWAKA 2010 - 2025

| Mwaka | Maji Baridi | | | | Maji Chumvi | | | | Jumla Kuu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi ya Wavuvi | Idadi ya Vyombo | Uzito (Tani) | Thamani "000" (Shilingi) | Idadi ya Wavuvi | Idadi ya Vyombo | Uzito (Tani) | Thamani "000" (Shilingi) | Idadi ya Wavuvi | Idadi ya Vyombo | Uzito (Tani) | Thamani "000" (Shilling) |
| 2010 | 141,206 | 47,635 | 294,474.00 | 684,844,020.0 | 36,321 | 7,664 | 52,683.40 | 89,639,934.0 | 177,527 | 55,299 | 347,157.40 | 774,483,954.0 |
| 2011 | 141,206 | 47,635 | 290,473.60 | 1,031,883,680.9 | 36,321 | 7,664 | 50,592.40 | 166,954,953.0 | 177,527 | 55,299 | 341,066.00 | 1,198,838,633.9 |
| 2012 | 146,420 | 49,321 | 314,944.00 | 1,129,349,924.7 | 36,321 | 7,664 | 50,079.40 | 177,781,799.0 | 182,741 | 56,985 | 365,023.40 | 1,307,131,723.7 |
| 2013 | 147,020 | 49,721 | 315,008.00 | 1,248,903,393.0 | 36,321 | 7,664 | 52,846.00 | 195,529,127.0 | 183,341 | 57,385 | 367,854.00 | 1,444,432,520.0 |
| 2014 | 147,479 | 49,627 | 314,061.54 | 1,287,248,813.0 | 36,321 | 7,664 | 51,912.40 | 207,649,600.0 | 183,800 | 57,291 | 365,973.94 | 1,503,574,790.0 |
| 2015 | 147,479 | 49,627 | 309,922.00 | 1,270,856,679.9 | 36,321 | 7,664 | 52,723.00 | 210,892,897.1 | 183,800 | 57,291 | 362,645.00 | 1,481,749,577.0 |
| 2016 | 149,018 | 49,688 | 308,771.59 | 1,274,485,403.6 | 54,511 | 9,650 | 53,823.30 | 211,891,899.2 | 203,529 | 59,338 | 362,594.89 | 1,486,377,302.7 |
| 2017 | 149,018 | 49,688 | 309,922.08 | 1,270,856,679.8 | 54,511 | 9,650 | 52,723.22 | 210,892,897.1 | 203,529 | 59,338 | 362,645.30 | 1,481,749,577.0 |
| 2018 | 149,018 | 49,688 | 323,120.77 | 1,495,678,680.0 | 53,035 | 9,242 | 53,231.94 | 248,262,840.0 | 202,053 | 58,930 | 376,352.71 | 1,743,941,520.0 |
| 2019 | 149,018 | 49,688 | 365,104.02 | 1,715,988,902.7 | 53,035 | 9,242 | 105,205.21 | 494,464,497.7 | 202,053 | 58,930 | 470,309.23 | 2,210,453,400.4 |
| 2020 | 149,504 | 50,116 | 409,828.31 | 2,049,141,547.2 | 53,035 | 9,242 | 63,763.93 | 318,819,664.2 | 202,539 | 59,358 | 473,592.24 | 2,367,961,211.4 |
| 2021 | 141,769 | 48,749 | 414,104.81 | 2,418,489,585.3 | 53,035 | 9,242 | 62,914.03 | 357,308,946.0 | 194,804 | 57,991 | 477,018.84 | 2,775,798,531.3 |
| 2022 | 144,728 | 49,206 | 404,639.12 | 2,711,082,104.0 | 53,035 | 9,242 | 66,873.42 | 448,051,914.0 | 197,763 | 58,448 | 471,512.54 | 3,159,134,018.0 |
| 2023 | 144,728 | 49,206 | 415,879.60 | 2,911,157,221.9 | 53,035 | 9,242 | 64,097.01 | 448,679,086.3 | 197,763 | 58,448 | 479,976.62 | 3,359,836,308.2 |
| 2024 | 148,626 | 50,024 | 458,799.57 | 3,850,702,150.5 | 53,035 | 9,242 | 63,988.76 | 502,033,490.1 | 201,661 | 59,266 | 522,788.33 | 4,352,735,640.5 |
| 2025 | 148,626 | 50,024 | 452,707.07 | 4,683,254,639.2 | 53,035 | 9,242 | 66,943.43 | 692,529,783.4 | 201,661 | 59,266 | 519,650.50 | 5,375,784,422.5 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Jedwali Na. 43: MWENENDO WA UUZAJI WA SAMAKI NJE YA NCHI, MWAKA 2011 - 2025**

| Mwaka | Uzito (Tani) | Samaki wa Mapambo | Thamani (dola za Marekani) | Thamani (Shilingi) | Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|---|
| 2011 | 37,996 | 61,215 | 152,973,357 | 233,714,590,011 | 6,153,278,023 |
| 2012 | 41,394 | 45,550 | 163,299,366 | 254,901,017,111 | 6,819,926,007 |
| 2013 | 38,574 | 44,260 | 147,659,779 | 234,884,628,956 | 6,117,769,194 |
| 2014 | 43,354 | 42,100 | 188,101,262 | 314,489,903,877 | 7,490,632,355 |
| 2015 | 41,060 | 87,630 | 259,286,762 | 547,228,222,096 | 13,097,411,199 |
| 2016 | 39,692 | 65,841 | 257,257,101 | 526,985,019,569 | 14,302,761,907 |
| 2017 | 36,063 | 101,110 | 182,450,278 | 406,568,122,272 | 10,446,850,539 |
| 2018 | 44,940 | 63,978 | 239,680,015 | 546,993,779,393 | 13,520,367,822 |
| 2019 | 45,775 | 136,915 | 158,657,946 | 376,763,802,643 | 25,567,600,873 |
| 2020 | 40,478 | 128,316 | 169,111,837 | 386,369,197,733 | 21,678,640,820 |
| 2021 | 42,302 | 181,268 | 176,083,787 | 414,232,629,494 | 18,436,276,859 |
| 2022 | 37,236 | 208,744 | 199,810,554 | 457,047,515,491 | 16,557,211,745 |
| 2023 | 42,371 | 166,024 | 213,383,805 | 509,909,916,965 | 16,214,093,692 |
| 2024 | 59,746 | 173,377 | 259,603,653 | 677,552,034,741 | 19,921,220,485 |
| 2025 | 45,053 | 259,876 | 252,977,424 | 648,916,826,907 | 16,280,548,787 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Jedwali Na. 44: MAUZO YA SANGARA NJE YA NCHI, MWAKA 2010 - 2025**

| Mwaka | Kiasi (Tani) | Thamani (USD) | Thamani (Shilingi) | Ushuru (Shilingi) |
|---|---:|---:|---:|---:|
| 2010 | 27,229 | 139,666,995 | 194,012,069,314 | 4,509,670,994 |
| 2011 | 25,426 | 127,601,694 | 197,899,741,508 | 4,299,987,312 |
| 2012 | 28,951 | 141,189,162 | 220,149,518,646 | 4,967,311,025 |
| 2013 | 33,733 | 124,551,585 | 197,578,220,799 | 5,085,642,906 |
| 2014 | 24,473 | 665,856,773 | 1,131,575,531,076 | 4,569,314,170 |
| 2015 | 23,001 | 250,279,107 | 528,534,413,019 | 11,251,591,352 |
| 2016 | 26,045 | 177,338,054 | 345,417,803,263 | 6,964,514,349 |
| 2017 | 26,680 | 168,554,019 | 376,572,501,425 | 7,057,407,121 |
| 2018 | 32,167 | 179,522,959 | 409,654,290,065 | 9,689,153,198 |
| 2019 | 32,609 | 176,894,903 | 400,195,293,574 | 17,622,314,163 |
| 2020 | 24,173 | 132,369,802 | 302,303,225,916 | 13,627,647,551 |
| 2021 | 21,846 | 143,135,053 | 337,103,408,189 | 9,704,591,513 |
| 2022 | 21,647 | 162,165,160 | 375,439,047,154 | 8,917,297,123 |
| 2023 | 20,192 | 132,207,272 | 316,336,648,585 | 7,783,579,857 |
| 2024 | 24,433 | 174,810,125 | 455,716,058,504 | 9,647,995,399 |
| 2025 | 15,684 | 74,751,531 | 191,746,463,435 | 7,998,196,508 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

## SURA YA 8

## MISITU, WANYAMAPORI NA UTALII

**Misitu na Nyuki**

214. Mwaka 2025, tani 34,987 za asali na tani 1,922.4 za nta zilizalishwa ikilinganishwa na tani 33,861 za asali na tani 1,918 za nta zilizozalishwa mwaka 2024. Kati ya kiasi kilichozalishwa, tani 1,596.8 za asali zenye thamani ya shilingi milioni 19,161.3 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 951.6 zenye thamani ya shilingi milioni 11,419.5 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2024, sawa na ongezeko la thamani la asilimia 67.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa asali nchini pamoja na kupatikana kwa masoko mapya nje ya nchi. Kwa upande mwingine, tani 366.3 za nta zenye thamani ya shilingi milioni 2,930 ziliuzwa nje ya nchi mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 458.1 za nta zenye thamani ya shilingi milioni 6,675.4 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2024, sawa na upungufu wa thamani wa asilimia 56.1. Hii ilitokana na kupungua kwa bei ya nta katika soko la dunia. Aidha, asali na nta ziliuzwa katika nchi za Denmark, Marekani, Ubelgiji, India, Oman, Uingereza, Sweden, Italia na Ujerumani. **Jedwali Na. 8.1** linaonesha mauzo ya asali na nta nje ya nchi.

**Jedwali Na. 8.1: Mauzo ya Asali na Nta Nje ya Nchi, Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Asali | | Nta | |
|---|---|---|---|---|
| | Kiasi (Tani) | Thamani (Shilingi) | Kiasi (Tani) | Thamani (Shilingi) |
| 2021 | 1,988.0 | 19,878,220,000 | 393 | 6,489,999,500 |
| 2022 | 1,562.9 | 15,629,295,500 | 793.5 | 11,903,470,950 |
| 2023 | 1,199.8 | 11,998,150,000 | 479.2 | 4,792,300,000 |
| 2024 | 951.6 | 11,419,488,000 | 458.1 | 6,675,405,000 |
| 2025 | 1,596.8 | 19,161,288,000 | 366.3 | 2,930,360,000 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

215. Mwaka 2025, thamani ya bidhaa nyingine za misitu zilizouzwa nje ya nchi ilikuwa shilingi bilioni 196.98 ikilinganishwa na bidhaa za misitu zenye thamani ya shilingi bilioni 427.2 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 53.9. Upungufu huo ulitokana na utekelezaji wa Kanuni za Utaratibu wa Usafirishaji wa Venia kwenda Nje ya Nchi za Mwaka 2024 iliyolenga kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa rasilimali za misitu.

**Upandaji wa Miti**

216. Mwaka 2025, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS iliotesha miche ya miti 35,039,365 ikilinganishwa na miche 34,126,916 iliyooteshwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 2.7 (**Jedwali Na. 8.2**). Miche hiyo ilipandwa katika maeneo

yaliyovunwa yenye hekta 6,723, hekta 2,180 za maeneo yaliyorudishiwa miti, na hekta 1,970 za maeneo ambayo miti haikuota vizuri ikilinganishwa na maeneo yaliyovunwa yenye hekta 4,930, maeneo yaliyorudishiwa miti (hekta 2,296) na maeneo ambayo miti haikuota vizuri (hekta 2,308) mwaka 2024.

**Jedwali Na. 8.2: Uendelezaji wa Mashamba ya Miti, Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Idadi ya Miche Iliyooteshwa | Eneo la Mashamba Mapya | Maeneo Yaliyorudishiwa Miti | Eneo Lililopandwa Miche baada ya Miti Kuvunwa | Eneo Lililorudishiwa Miche katika Maeneo Yasiyoota Vizuri | Eneo la Mashamba ya Miti Lililosafishwa | Eneo la Mashamba ya Miti Lililopogolewa | Eneo la Mashamba ya Miti ambalo Miti Ilipunguziwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Hekta | | | | | | |
| 2021 | 31,295,703 | 30,000 | 4,498 | 3,328 | 2,076 | 41,527 | 10,860 | 4,685 |
| 2022 | 30,705,653 | 0 | 5,538 | 3,219 | 3,496 | 38,357 | 9,869 | 3,197 |
| 2023 | 33,068,643 | 0 | 2,071.10 | 4,508.20 | 2,384.30 | 27,681.30 | 7,155.50 | 2,690.60 |
| 2024 | 34,126,916 | 0 | 2,296 | 4,930 | 2,308 | 30,205 | 12,654 | 2,816 |
| 2025 | 35,039,365 | 28,000 | 2,180 | 6,723 | 1,970 | 34,678 | 11,383 | 3,315 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

217. Mwaka 2025, miche ya miti 15,496,105 ilipandwa katika maeneo mbalimbali, ikiwemo misitu ya asili, vyanzo vya maji, makazi na maeneo yaliyoharibiwa kutokana na shughuli za binadamu ikilinganishwa na miche ya miti 14,820,189 iliyopandwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 4.6. Hii ilitokana na kuendelea kutekelezwa kwa mpango wa upandaji miti pamoja na kampeni za uhamasishaji kuhusu umuhimu wa kupanda miti. Aidha, mipango 24 ya usimamizi wa hifadhi za misitu iliandaliwa, mipaka ya hifadhi ya misitu yenye urefu wa kilometa 1,503 ilisafishwa na vigingi 773 na mabango 178 yaliwekwa mwaka 2025 ikilinganishwa na mipango 30 iliyoandaliwa, mipaka yenye urefu wa kilometa 2,194 iliyosafishwa, na vigingi 769 na mabango 177 yaliyowekwa mwaka 2024.

218. Mwaka 2025, TFS ilikamata na kutaifisha magunia 48,394 ya mkaa, nguzo 4,004, mbao zenye mita za ujazo 2,275, kuni zenye mita za ujazo 264, na magogo yenye mita za ujazo 286. Aidha, pikipiki 2,753, baiskeli 5,467, magari 275, majahazi 5 na pikipiki 85 za miguu mitatu za kubebea mizigo zilikamatwa kwa kuhusika katika uvunaji haramu wa rasilimali za misitu kinyume cha Sheria ya Misitu Na. 14 ya Mwaka 2002 na wamiliki wa vyombo hivyo kutozwa faini.

**Wanyamapori**

219. Mwaka 2025, doria 378,083 zilifanyika kudhibiti ujangili na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa ikilinganishwa na doria 279,956 zilizofanyika mwaka 2024. Kati ya doria hizo, Shirika la Hifadhi za Taifa lilifanya doria 54,319, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro doria 4,064, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori doria 319,680 na Kikosi cha Taifa cha Kupambana na Ujangili doria 20. Kupitia doria hizo nyara mbalimbali zilikamatwa kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 8.3**. Aidha, doria hizo

ziliwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 8,398 wa makosa ya ujangili wa wanyamapori na misitu ikilinganishwa na watuhumiwa 6,295 waliokamatwa mwaka 2024. Kuongezeka kwa watuhumiwa na idadi ya nyara zilizokamatwa kunaakisi jitihada zilizofanywa na Serikali katika kuimarisha ulinzi na kudhibiti ujangili na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa kuongeza idadi ya doria zilizofanyika.

**Jedwali Na. 8.3: Nyara Zilizokamatwa katika Doria, Mwaka 2021 - 2025**

| Aina za Nyara | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Meno ya tembo | 90 | 222 | 208 | 105 | 281 |
| Vipande vya meno ya tembo | 74 | 544 | 390 | 93 | 427 |
| Nyamapori (kilogramu) | 1,518 | 1,023 | 1,986 | 411 | 2,815 |
| Nyama kavu (vipande) | 0 | 170 | 299 | 346 | 274 |
| Kobe hai | 849 | 406 | 63 | 10 | 396 |
| Ngozi (vipande) | 0 | 4 | 9 | 5 | 52 |
| Magamba ya kakakuona | 37 | 436 | 123 | 734 | 0 |
| Chatu | 0 | 1 | 3 | 2 | 2 |
| Silaha | 444 | 315 | 408 | 127 | 301 |
| Risasi | 1,577 | 1,427 | 2,807 | 424 | 1,489 |
| Mitego | 2,314 | 19,263 | 17,211 | 2,367 | 16,371 |
| Magari | 11 | 7 | 34 | 4 | 13 |
| Pikipiki | 19 | 21 | 81 | 217 | 397 |
| Mifugo | 0 | 30,030 | 40,752 | 62,568 | 143,501 |
| Meno ya kiboko | 24 | 0 | 6 | 4 | 4 |
| Pembe za Faru | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kucha za simba | 130 | 0 | 11 | 8 | 0 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

220. Mwaka 2025, mapato yatokanayo na sekta ndogo ya wanyamapori yalikuwa shilingi bilioni 899.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 819.9 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 9.7 (**Jedwali Na. 8.4**). Ongezeko hilo lilitokana na utekelezaji wa mikataba ya uwekezaji mahiri kwenye maeneo ya wanyamapori; utangazaji wa vivutio vya utalii; uboreshaji wa huduma kwa watalii katika maeneo yaliyohifadhiwa; na kuimarika kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato.

**Jedwali Na. 8.4: Mapato ya Sekta Ndogo ya Wanyamapori, Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Shirika la Hifadhi za Taifa | Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro | Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 2021 | 127,028,556,252.0 | 63,852,180,870.0 | 60,651,257,787.0 | 251,531,994,909.0 |
| 2022 | 293,079,503,086.0 | 144,354,627,647.0 | 63,030,304,315.3 | 500,464,435,048.3 |
| 2023 | 379,790,063,492.1 | 195,748,756,367.0 | 58,730,532,598.2 | 634,269,352,457.3 |
| 2024 | 480,223,465,704.4 | 254,396,987,140.3 | 85,228,986,090.1 | 819,849,438,934.8 |
| 2025 | 528,645,214,275.9 | 280,380,289,482.5 | 90,612,396,211.2 | 899,637,899,969.5 |
| **Ukuaji (Asilimia)** | **10.1** | **10.2** | **6.3** | **9.7** |
| **Mchango (Asilimia)** | **58.8** | **31.2** | **10.1** | **100.0** |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

## Utalii

221. Mwaka 2025, watalii 2,294,495 waliingia nchini ikilinganishwa na watalii 2,141,895 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 7.1 (**Jedwali Na. 8.5**). Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kutangaza utalii kupitia programu maalum, balozi za Tanzania katika nchi mbalimbali, matamasha, mikutano na matukio mbalimbali, pamoja na utalii wa faru weusi na weupe. Kati ya hao, watalii 1,173,172 walitembelea Hifadhi za Taifa na watalii 1,121,323 walitembelea vivutio vingine vya utalii nchini ikiwemo utalii wa masomo, matibabu, biashara na kutembelea ndugu. Aidha, mapato yatokanayo na watalii wa kimataifa yalikuwa dola za Marekani milioni 4,410.6 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,903.0 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 13.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii na wastani wa matumizi ya mtalii kwa siku.

222. Mwaka 2025, watalii wa ndani walikuwa 3,641,066 ikilinganishwa na watalii 3,218,352 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 13.1. Kati ya hao, watalii 374,648 walitembelea Hifadhi za Taifa mwaka 2025 ikilinganishwa na watalii 968,766 mwaka 2024. Aidha, watalii wa ndani na nje waliotembelea vivutio vya utalii walikuwa 5,935,561 mwaka 2025 ikilinganishwa na watalii 5,360,247 wa ndani na nje mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 10.7. Idadi hii pia ni zaidi ya lengo la nchi la kufikisha watalii milioni 5 ifikapo mwaka 2025.

223. Mwaka 2025, watalii 868,819 walitembelea Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ikilinganishwa na watalii 1,012,673 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 14.2. Kati ya hao, watalii 707,075 walitoka nje ya nchi na watalii 161,744 walikuwa wa ndani.

**Jedwali Na. 8.5: Idadi ya Watalii Walioingia Nchini, Mwaka 2021 - 2025**

| Mwezi | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Ukuaji (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 79,116 | 94,441 | 146,877 | 180,422 | 195,946 | 8.6 |
| Februari | 79,730 | 101,042 | 144,019 | 184,092 | 190,313 | 3.4 |
| Machi | 72,285 | 93,889 | 118,186 | 155,810 | 140,597 | -9.8 |
| Aprili | 43,966 | 79,405 | 96,852 | 116,280 | 130,340 | 12.1 |
| Mei | 42,173 | 89,271 | 106,497 | 129,492 | 137,365 | 6.1 |
| Juni | 57,689 | 117,349 | 146,892 | 179,264 | 202,226 | 12.8 |
| Julai | 81,307 | 166,736 | 185,929 | 218,065 | 274,130 | 25.7 |
| Agosti | 87,397 | 158,049 | 186,030 | 211,056 | 246,187 | 16.6 |
| Septemba | 80,733 | 134,231 | 168,708 | 186,160 | 214,420 | 15.2 |
| Oktoba | 92,345 | 141,517 | 171,573 | 189,557 | 201,166 | 6.1 |
| Novemba | 92,939 | 123,351 | 154,012 | 174,042 | 165,133 | -5.1 |
| Desemba | 113,012 | 155,639 | 182,630 | 217,655 | 196,672 | -9.6 |
| **Jumla** | **922,692** | **1,454,920** | **1,808,205** | **2,141,895** | **2,294,495** | **7.1** |

**Chanzo:** Idara ya Uhamiaji na Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali Na. 8.6: Mwenendo wa Utalii katika Hifadhi za Taifa, Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Idadi ya Watalii | | Jumla | Mapato (Shilingi milioni) |
|---|---|---|---|---|
| | Nje | Ndani | | |
| 2021 | 317,654 | 518,480 | 836,134 | 127,028.6 |
| 2022 | 697,264 | 787,742 | 1,485,006 | 293,079.5 |
| 2023 | 888,506 | 902,176 | 1,790,682 | 379,790.1 |
| 2024 | 1,041,473 | 968,766 | 2,010,239 | 480,223.4 |
| 2025 | 1,173,172 | 374,648 | 1,547,820 | 528,645.2 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

224. Mwaka 2025, jumla ya watalii 377,116 walitembelea Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia na mashamba ya miti ikilinganishwa na watalii 298,893 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 26.2. Kati ya hao, watalii wa ndani walikuwa 322,579 na watalii wa nje walikuwa 54,537. Katika kipindi hicho, mapato yaliyotokana na watalii waliotembelea Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia yalikuwa shilingi milioni 3,608.02 ikilinganishwa na mapato ya shilingi milioni 2,123.05 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 69.9. (**Jedwali Na. 8.7**). Hii ilitokana na utangazaji wa vivutio vya utalii, doria zilizofanyika katika misitu ili kuzuia ukataji wa miti na kuboreshwa kwa miundombinu katika maeneo ya hifadhi za misitu.

**Jedwali Na. 8.7: Mwenendo wa Watalii Waliotembelea Vivutio vilivyopo katika Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia na Mashamba ya Miti Mwaka 2025**

| Mwezi | Idadi ya Watali | | | Mapato | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ndani | Nje | Jumla | Ndani | Nje | Jumla |
| Januari | 21,732 | 3,807 | 25,539 | 116,309,379 | 112,817,914 | 229,127,293 |
| Februari | 23,780 | 4,875 | 28,655 | 133,067,765 | 138,381,595 | 271,449,360 |
| Machi | 12,665 | 2,156 | 14,821 | 59,921,675 | 60,419,402 | 120,341,077 |
| Aprili | 11,713 | 1,264 | 12,977 | 56,506,950 | 36,974,100 | 93,481,050 |
| Mei | 17,154 | 2,208 | 19,362 | 91,370,275 | 78,030,825 | 169,401,100 |
| Juni | 44,354 | 6,955 | 51,309 | 259,394,000 | 291,543,000 | 550,937,000 |
| Julai | 43,250 | 10,544 | 53,794 | 293,376,500 | 418,854,500 | 712,231,000 |
| Agosti | 44,041 | 7,832 | 51,873 | 211,220,340 | 252,884,160 | 464,104,500 |
| Septemba | 35,922 | 6,096 | 42,018 | 164,280,000 | 199,741,000 | 364,021,000 |
| Oktoba | 26,288 | 4,292 | 30,580 | 123,959,500 | 134,137,000 | 258,096,500 |
| Novemba | 12,890 | 1,411 | 14,301 | 61,501,000 | 46,366,500 | 107,867,500 |
| Desemba | 28,790 | 3,097 | 31,887 | 172,199,500 | 94,759,520 | 266,959,020 |
| **Jumla** | **322,579** | **54,537** | **377,116** | **1,743,106,884** | **1,864,909,516** | **3,608,016,400** |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Uwindaji wa Kitalii na Utalii wa Picha**

225. Mwaka 2025, watalii 279,091 wa nje walitembelea maeneo ya uwindaji ikilinganishwa na watalii 232,424 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 20.1. Kati ya hao, watalii wa uwindaji walikuwa 598, watazamaji 529 na watalii wa picha 277,964. Ongezeko la watalii katika maeneo ya uwindaji lilitokana na kuendelea kushamiri kwa utalii wa picha pamoja na kuongezeka kwa maeneo ya vivutio vya utalii wa picha. Aidha, mapato yaliyotokana na uwindaji wa kitalii, watazamaji na utalii wa picha yalikuwa shilingi milioni 90,612.4 ikilinganishwa na shilingi milioni 85,229.0 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 6.3 (**Jedwali Na. 8.8**).

**Jedwali Na. 8.8: Idadi ya Wawindaji wa Kitalii na Mapato, Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Idadi ya Watalii | | | | Mapato (Shilingi Milioni) |
|---|---|---|---|---|---|
| | Wawindaji | Watazamaji | Watalii wa Picha | Jumla | |
| 2021 | 548 | 101,382 | 66,648 | 168,578 | 35,726.0 |
| 2022 | 687 | 503 | 139,967 | 141,157 | 63,030.3 |
| 2023 | 599 | 498 | 190,378 | 191,475 | 58,730.5 |
| 2024 | 671 | 718 | 231,035 | 232,424 | 85,229.0 |
| 2025 | 598 | 529 | 277,964 | 279,091 | 90,612.4 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Malikale**

226. Mwaka 2025, wageni 151,367 walitembelea vivutio vya malikale ikilinganishwa na wageni 260,398 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 41.9. Upungufu huo

ulitokana na mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha watalii kubadilisha misimu ya utalii. Aidha, mapato yaliyotokana na wageni waliotembelea vivutio vya malikale yalikuwa shilingi milioni 2,420.6 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi milioni 3,302.5 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 26.7. **Jedwali Na. 8.9** linaonesha idadi ya wageni waliotembelea vivutio vya malikale na mapato yaliyokusanywa.

**Jedwali Na. 8.9: Wageni Waliotembelea Vivutio vya Malikale na Mapato, Mwaka 2023 - 2025**

| Kituo | 2023 | | 2024 | | 2025 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wageni | Mapato | Wageni | Mapato | Wageni | Mapato |
| Magomeni | 688 | 1,069,522 | 4,912 | 282,234,640 | 1,204 | 2,218,400 |
| Kaole | 39,481 | 75,895,283 | 53,355 | 101,392,300 | 36,214 | 150,497,325 |
| Isimila | 3,890 | 3,845,142 | 26,416 | 102,418,740 | 8,846 | 36,800,400 |
| Mji Mkongwe Bagamoyo | 21,940 | 37,489,242 | 25,470 | 81,719,596.65 | 16,745 | 100,114,500 |
| Kalenga | 4,494 | 6,527,284 | 29,836 | 52,084,000 | 11,784 | 19,386,000 |
| Kilwa | 6,902 | 12,649,553 | 6,525 | 87,138,540 | 4,317 | 144,818,920 |
| Olduvai | 24,290 | 2,010,926,123.49 | 28,152 | 2,430,203,754.24 | 31,714 | 1,817,378,510 |
| Mbozi | 3,953 | 6,686,300 | 2,649 | 4,358,000 | 2,491 | 9,903,880 |
| Amboni | 15,522 | 25,368,567 | 22,192 | 36,810,000 | 13,102 | 27,695,000 |
| Tongoni | 657 | 1,003,257 | 717 | 1,410,500 | 1,990 | 4,824,000 |
| Ujiji | 4,531 | 10,437,353 | 21,668 | 30,632,000 | 4,678 | 16,255,360 |
| Kwihara | 1,013 | 1,343,103 | 987 | 3,108,135 | 1,402 | 3,488,300 |
| Kolo | 6,900 | 21,677,337 | 8,195 | 36,266,944.33 | 6,470 | 57,120,875 |
| CaravanSerai | 5,738 | 9,702,250 | 25,136 | 45,980,000 | 7,103 | 15,499,760 |
| Kunduchi | 4031 | 4,981,032 | 3,982 | 5,593,000 | 2,256 | 7,915,849 |
| Laetoli | 78 | 0 | 164 | 0 | 69 | 3,257,850 |
| Ngorongoro Lengai Jiopaki | 0 | 0 | 0 | 0 | 861 | 2,746,250 |
| Engaruka | 26 | 407,100 | 42 | 1,171,740 | 121 | 719,800 |
| **Jumla** | **144,134** | **2,230,008,448** | **260,398** | **3,302,521,890** | **151,367** | **2,420,640,979** |

**Chanzo**: Wizara ya Maliasili na Utalii

### Makumbusho ya Taifa

227. Mwaka 2025, wageni 282,567 walitembelea Makumbusho ya Taifa ikilinganishwa na wageni 475,175 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 40.5. Hii ilitokana na kutofanyika kwa baadhi ya programu za kimakumbusho pamoja na kupungua kwa idadi ya wadau waliohudhuria programu za kimakumbusho zilizofanyika. Kati ya waliotembelea makumbusho ya Taifa, wageni wa ndani walikuwa 21,994 na wageni wa nje 260,573. Aidha, mapato yaliyotokana na viingilio vya wageni katika vituo vya Makumbusho ya Taifa yalikuwa shilingi milioni 938.5 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi milioni 1,004.9 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 6.6. **Jedwali Na. 8.10** linaonesha idadi ya watalii na mapato katika vivutio vya makumbusho ya Taifa.

**Jedwali Na. 8.10: Idadi ya Watalii na Mapato katika Makumbusho ya Taifa, Mwaka 2024 - 2025**

| Kituo | 2024 | | | | 2025 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi ya Watalii | | | Mapato | Idadi ya Watalii | | | Mapato |
| | Nje | Ndani | Jumla | | Nje | Ndani | Jumla | |
| Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni | 11,338 | 182,557 | 193,895 | 373,356,036 | 110,125 | 10,495 | 120,620 | 447,496,525.83 |
| Kijiji cha Makumbusho | 6,464 | 188,152 | 194,616 | 452,512,960 | 44,696 | 5,747 | 50,443 | 244,199,665.25 |
| Makumbusho ya Azimio la Arusha | 495 | 17,786 | 18,281 | 32,507,267 | 11,910 | 622 | 12,532 | 30,433,865 |
| Makumbusho ya Elimu Viumbe | 4,039 | 37,090 | 41,129 | 110,913,381 | 19,262 | 4,947 | 24,209 | 158,805,070 |
| Makumbusho ya Mwl.Nyerere | 68 | 12,192 | 12,260 | 18,411,461 | 59,880 | 79 | 59,959 | 27,346,154 |
| Makumbusho ya Vita ya Majimaji | 107 | 12,071 | 12,178 | 14,137,239 | 11,664 | 95 | 11,759 | 25,669,512 |
| Makumbusho ya Dkt.Rashid Kawawa | 4 | 834 | 838 | 872,500 | 130 | 0 | 130 | 280,500 |
| Mji wa Kihistoria Mikindani | 120 | 1,858 | 1,978 | 2,149,884 | 2,906 | 9 | 2,915 | 4,290,970 |
| **Jumla** | **22,635** | **452,540** | **475,175** | **1,004,860,728** | **260,573** | **21,994** | **282,567** | **938,522,262** |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Jedwali Na. 45: WATALII WALIOTEMBELEA HIFADHI ZA TAIFA, MWAKA 2010 - 2025**

| Mwaka | Idadi ya Watalii | | | Mapato (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|
| | Nje | Ndani | Jumla | |
| 2010 | 540,440 | 333,294 | 873,734 | 113,856,861,145 |
| 2011 | 586,869 | 360,928 | 947,797 | 119,549,704,203 |
| 2012 | 537,675 | 364,217 | 901,892 | 137,545,109,618 |
| 2013 | 530,142 | 427,208 | 957,350 | 150,861,426,031 |
| 2014 | 535,140 | 417,220 | 952,360 | 152,977,487,000 |
| 2015 | 432,124 | 526,110 | 958,234 | 149,957,485,000 |
| 2016 | 439,119 | 518,457 | 957,576 | 175,089,696,000 |
| 2017 | 386,529 | 595,811 | 982,340 | 207,587,218,000 |
| 2018 | 726,003 | 442,543 | 1,168,546 | 214,486,751,736 |
| 2019 | 763,276 | 494,676 | 1,257,952 | 292,539,502,030 |
| 2020 | 218,310 | 288,867 | 507,177 | 85,614,710,442 |
| 2021 | 317,654 | 518,480 | 836,134 | 127,028,556,252 |
| 2022 | 697,264 | 787,742 | 1,485,006 | 293,079,503,086 |
| 2023 | 888,506 | 902,176 | 1,790,682 | 379,790,063,492 |
| 2024 | 1,041,473 | 968,766 | 2,010,239 | 480,223,465,704 |
| 2025 | 1,173,172 | 374,648 | 1,547,820 | 528,645,214,276 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Jedwali Na. 46: MAUZO YA BIDHAA ZA MISITU NJE YA NCHI MWAKA 2025**

| Na. | Bidhaa | Kiasi | Thamani (Dola za Marekani ) | Thamani (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Arrowroot powder | 9,650 | 9,513.55 | 23,284,071.14 |
| 2 | Baobab | 208,023 | 82,333.77 | 201,508,938.06 |
| 3 | Baobab Oil | 200 | 1,339.00 | 3,277,154.30 |
| 4 | Baobab powder | 263 | 1,452.50 | 3,554,941.46 |
| 5 | Barks | 101 | 165 | 403,831.56 |
| 6 | Bee Hives | 14 | 100 | 244,746.40 |
| 7 | Briquettes | 2,005,867 | 709,575.00 | 1,736,659,267.80 |
| 8 | Broom Sticks | 872,007 | 187,533.60 | 458,981,734.79 |
| 9 | Carvings | 11,072 | 678,887.24 | 1,661,552,079.96 |
| 10 | Chairs & Stools | 245 | 705 | 1,725,462.12 |
| 11 | Clarinets | 82 | 806,017.48 | 1,972,698,765.67 |
| 12 | Clarinets Sets | 13 | 436,624.19 | 1,068,621,986.55 |
| 13 | Construction Poles | 7,068 | 33,988.08 | 83,184,602.23 |
| 14 | Door Shutters | 185 | 323 | 790,530.87 |
| 15 | Firewood | 60 | 3,150.00 | 7,709,511.60 |
| 16 | Furniture | 1,975 | 3,068.00 | 7,508,819.55 |
| 17 | Gum Arabic | 123,704 | 99,303.64 | 243,042,083.97 |
| 18 | Logs | 255 | 97,043.03 | 237,509,322.38 |
| 19 | Marine board | 31,215 | 7,690,954.00 | 18,823,333,040.66 |
| 20 | MDF Laminated Board | 38,377 | 11,138,839.00 | 27,261,907,454.30 |
| 21 | MDF Plain Board | 553 | 99,939.00 | 244,597,104.70 |
| 22 | Medicinal Plants (Leaves, Flowers, Roots) | 13,197 | 28,466.40 | 69,670,489.21 |
| 23 | Ornamental Plants | 34,042 | 110,802.50 | 271,185,129.86 |
| 24 | Other wooden small items | 5,846 | 613,574.08 | 1,501,700,472.13 |
| 25 | Pallet | 75 | 1,770.00 | 4,332,011.28 |
| 26 | Palm Fruit | 342,000 | 63,139.91 | 154,532,656.69 |
| 27 | Plywood | 24,627 | 6,674,759.40 | 16,336,233,340.16 |
| 28 | Reject Timber | 116 | 14,000.00 | 34,264,496.00 |
| 29 | Resin | 6,978,123 | 4,782,628.21 | 11,705,310,369.36 |
| 30 | sandalwood oil | 6 | 2,098,135.00 | 5,135,109,879.64 |
| 31 | Sandalwood spent dust | 20,001 | 14,001.00 | 34,266,943.46 |
| 32 | Saw Dust | 138 | 2,200.00 | 5,384,420.80 |
| 33 | Sawn Timber | 254,335 | 25,342,036.55 | 62,023,722,142.81 |
| 34 | Slabs | 62 | 4,000.00 | 9,789,856.00 |
| 35 | sleepers | 13,211 | 4,960,862.70 | 12,141,532,867.19 |
| 36 | Tamarind | 147,100 | 42,020.00 | 102,842,437.28 |
| 37 | Transmission Poles | 1,701 | 721,345.00 | 1,765,465,919.08 |
| 38 | Tree Seedlings | 24 | 185 | 452,780.84 |
| 39 | Tree Seeds | 4 | 200 | 489,492.80 |
| 40 | Veneer | 150,052 | 11,054,406.27 | 27,055,261,387.20 |
| 41 | Wattle extract | 852,053 | 1,656,269.00 | 4,053,658,751.82 |
| 42 | Wattle Extract Powder | 1 | 1.71 | 4,185.16 |
| 43 | Wattle Extract Solid | 24,000 | 34,967.00 | 85,580,473.69 |
| 44 | Wild Fruits | 43,200 | 3,393.60 | 8,305,713.83 |
| 45 | Withies | 98,400 | 87,200.00 | 213,418,860.80 |
| 46 | Withies (kg) | 10,000 | 7,000.00 | 17,132,248.00 |
| 47 | Wood chips | 7,413 | 3,499.00 | 8,563,676.54 |
| 48 | Wood oil | 200 | 200 | 489,492.80 |
| 49 | Wood planks | 1,332 | 42,163.67 | 103,194,064.43 |
| 50 | Wooden Office/Dinning Table | 5,835 | 4,466.00 | 10,930,374.22 |
| 51 | Wooden small items | 549 | 1,282.00 | 3,137,648.85 |
| 52 | Woven products | 2,114 | 33,325.99 | 81,564,160.79 |
| **Jumla** | | | | **196,979,622,192.78** |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Jedwali Na. 47: MWENENDO WA BIASHARA YA UTALII, MWAKA 2019 - 2025**

| Maelezo | Kipimo | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya Watalii | Idadi | 1,527,230 | 620,867 | 922,692 | 1,454,920 | 1,808,205 | 2,141,895 | 2,294,495 |
| Watalii wa Hotelini | Idadi | 1,353,279 | 563,779 | 848,936 | 1,365,861 | 1,710,333 | 1,990,697 | 2,088,115 |
| Mapato | Dola za Marekani Milioni | 2,604 | 715 | 1,248 | 2,528 | 3,374 | 3,903 | 4,410.6 |
| Wastani wa siku za kukaa watalii hotelini | Siku | 13 | 10 | 10 | 9 | 10 | 10 | 9 |
| Wastani wa matumizi ya fedha kwa mtalii kwa siku (Dola za Marekani | *Package Tour* | 379 | 312 | 364 | 377 | 419 | 416 | 479 |
| | *Non Package Tour* | 216 | 115 | 141 | 166 | 178 | 172 | 203 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Jedwali Na. 48: WATALII WALIOTEMBELEA MAMLAKA YA HIFADHI YA NGORONGORO, MWAKA 2010 - 2025**

| Mwaka | Wageni kutoka Nje | Watanzania | Jumla |
|---|---:|---:|---:|
| 2010 | 281,513 | 242,133 | 523,646 |
| 2011 | 281,513 | 307,086 | 588,599 |
| 2012 | 310,537 | 254,730 | 565,267 |
| 2013 | 350,970 | 296,763 | 647,733 |
| 2014 | 332,469 | 278,221 | 610,690 |
| 2015 | 289,061 | 278,922 | 567,983 |
| 2016 | 284,794 | 265,845 | 550,639 |
| 2017 | 391,030 | 249,428 | 640,458 |
| 2018 | 410,574 | 268,880 | 679,454 |
| 2019 | 445,283 | 279,255 | 724,538 |
| 2020 | 122,228 | 125,953 | 248,181 |
| 2021 | 160,877 | 165,235 | 326,112 |
| 2022 | 388,853 | 256,422 | 645,275 |
| 2023 | 515,961 | 327, 512 | 843,473 |
| 2024 | 728,111 | 476,700 | 1,204,811 |
| 2025 | 707,075 | 161,744 | 868,819 |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

## SURA YA 9

## MADINI

**Leseni za Shughuli za Madini**

228. Mwaka 2025, Serikali ilitoa leseni 14,958 za shughuli za madini ikilinganishwa na leseni 12,009 zilizotolewa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 24.6. Hii ilitokana na kuboreshwa kwa mfumo wa utoaji leseni wa *Trimble landfolio* na kutolewa kwa mafunzo kwa watumiaji wa Mfumo huo pamoja na kuongezeka kwa vitendea kazi. Kati ya leseni zilizotolewa, leseni 548 zilikuwa za utafutaji wa madini, leseni moja (1) ya uchimbaji mkubwa, leseni 41 za uchimbaji wa kati, leseni 12,135 za uchimbaji mdogo, leseni 44 za uchenjuaji madini, leseni mbili (2) za uyeyushaji madini, leseni kubwa 848 za biashara ya madini (Dealers) na leseni 1,339 za biashara ndogo ya madini (Brokers).

**Vibali vya Uuzaji wa Madini**

229. Mwaka 2025, vibali 11,922 vya kuuza madini nje ya nchi vyenye thamani ya dola za Marekani milioni 4,991.13 vilitolewa ikilinganishwa na vibali 12,073 vilivyokuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 4,176.18 vilivyotolewa mwaka 2024. Kupungua kwa idadi ya vibali kulichangiwa na kupungua kwa uzalishaji wa makaa ya mawe pamoja na kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu kwenda Benki Kuu ya Tanzania.

**Dhahabu**

230. Mwaka 2025, uzalishaji wa dhahabu ulikuwa kilogramu 68,225.38 ikilinganishwa na kilogramu 61,680.81 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 10.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa bei ya madini ya dhahabu katika soko la dunia. Aidha, wastani wa bei ya dhahabu katika soko la dunia uliongezeka kwa asilimia 43.9 na kufikia dola za Marekani 3,431.0 kwa wakia mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani 2,384.8 kwa wakia mwaka 2024.

231. Mwaka 2025, kilogramu 48,563 za dhahabu zilipata vibali vya kuuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na kilogramu 59,471 zilizopata vibali mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 18.3. Hii ilitokana na wachimbaji kutekeleza takwa la Sheria ya Madini Sura, 123 Kifungu cha 59 kinachowaelekeza wachimbaji na wafanyabiashara kuiuzia Benki Kuu ya Tanzania - BOT angalau asilimia 20 ya dhahabu inayozalishwa kwa lengo la kuongeza akiba ya fedha za kigeni. Katika kipindi hicho, kilogramu 15,075.37 za dhahabu zenye thamani ya shilingi milioni 4,529.47 zilinunuliwa na Benki Kuu ya Tanzania kutoka kwa wachimbaji na wafanyabiashara wa dhahabu ikilinganishwa na kilogramu 1,957.17 zenye thamani ya shilingi milioni 445.27 zilizonunuliwa mwaka 2024. Aidha, thamani ya dhahabu iliyopata vibali vya kuuzwa nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 24.0 na kufikia dola za Marekani milioni 4,253.47 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,431.08 mwaka 2024.

**Almasi**

232. Mwaka 2025, uzalishaji wa madini ya almasi ulikuwa karati 407,840.00 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 63.55 ikilinganishwa na karati 373,252.76 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 59.24 zilizozalishwa mwaka 2024. Uzalishaji wa almasi uliongezeka kwa asilimia 9.3 kutokana na kuendelea kuimarika kwa shughuli za uzalishaji katika mgodi wa Williamson Diamond Limited. Katika kipindi hicho, karati 374,000 za almasi zenye thamani ya dola za Marekani milioni 52.9 zilipata vibali vya kusafirishwa nje ya nchi ikilinganishwa na karati 373,170 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 59.2 mwaka 2024. Aidha, wastani wa bei ya almasi ghafi ilikuwa dola za Marekani 163.17 kwa karati mwaka 2025 ikilinganishwa dola za Marekani 177.86 kwa karati mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 8.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya almasi zinazotengenezwa maabara (lab grown diamond) katika soko la kimataifa ambayo ina bei nafuu ikilinganishwa na almasi ghafi.

**Vito vya Thamani**

233. Mwaka 2025, kilogramu 29,447,271 za madini ya vito ghafi (isipokuwa tanzanite na almasi) zilizalishwa ikilinganishwa na kilogramu 46,299,069 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 36.4. Hii ilitokana na kushuka kwa bei za madini hayo katika masoko ya kimataifa.

**Tanzanite**

234. Mwaka 2025, kilogramu 144,308.48 za madini ya Tanzanite ghafi na magonga zilizalishwa ikilinganishwa na kilogramu 83,014.66 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 73.8. Hii ilitokana na uzalishaji kufanyika katika miamba yenye ubora pamoja na kurejeshwa kwa shughuli za minada iliyokuwa imesitishwa ili kuboresha uendeshaji. Aidha, karati 28,927.34 za madini ya Tanzanite zenye thamani ya dola za Marekani milioni 2.86 zilikatwa na kusanifiwa mwaka 2025 ikilinganishwa na karati 17,469.66 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 2.43 zilizokatwa na kusanifiwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la karati la asilimia 65.6. Kwa upande mwingine, wastani wa bei ya tanzanite ghafi katika soko la dunia uliongezeka kwa asilimia 32.9 na kufikia dola za Marekani 297.16 kwa kilogramu mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani 223.53 mwaka 2024.

**Makaa ya Mawe**

235. Mwaka 2025, tani 3,879,960.85 za makaa ya mawe zilizalishwa ikilinganishwa na tani 3,904,542.69 zilizozalishwa mwaka 2024. Hii ilichangiwa na kupungua kwa uzalishaji wa makaa ya mawe katika mgodi wa *Ruvuma Coal Limited* kulikotokana na kupungua kwa masoko ya madini hayo baada ya kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani katika nchi zinazotumia makaa ya mawe kwa wingi ikiwemo China na India pamoja na matumizi ya nishati mbadala. Aidha, makaa ya mawe yaliyozalishwa yalikuwa na thamani ya shilingi

bilioni 1,197.38 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,035.93 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 14.1.

**Madini ya Jasi**

236. Mwaka 2025, uzalishaji wa madini ya jasi uliongezeka kwa asilimia 11.2 na kufikia tani 913,263.5 ikilinganishwa na tani 821,221.1 zilizozalishwa mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa viwanda vinavyotumia madini ya jasi katika utengenezaji wa bidhaa mbalimbali ikiwemo saruji ndani na nje ya nchi. Aidha, tani 48,354 za madini ya jasi zenye thamani ya dola za Marekani milioni 12.2 zilipata vibali vya kuuzwa nje ya nchi mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 22,575 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 3.9 zilizopata vibali mwaka 2024.

**Madini ya Ujenzi**

237. Mwaka 2025, madini ya ujenzi yaliyozalishwa yalikuwa tani milioni 36.50 yenye thamani ya shilingi bilioni 634.20 ikilinganishwa na tani milioni 33.30 za madini ya ujenzi yenye thamani ya shilingi bilioni 586.48 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la uzalishaji la asilimia 9.6. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi nchini.

**Madini Mengine**

238. Mwaka 2025, kilogramu 1,895.2 za madini ya fedha zilizalishwa ikilinganishwa na kilogramu 3,129.1 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa upungufu wa asilimia 39.4. Hii ilitokana na baadhi ya wachimbaji wa madini ya fedha kuhamia katika uchimbaji wa dhahabu kufuatia kuimarika kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia. Aidha, kilogramu 1,164 za madini ya fedha zenye thamani ya dola za Marekani milioni 1.48 yalipata vibali vya kuuzwa nje ya nchi mwaka 2025 ikilinganishwa na kilogramu 1,067 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 1.14 mwaka 2024, sawa na ongezeko la thamani la asilimia 29.8. Hii ilitokana na kuendelea kuimarika kwa bei ya madini ya fedha katika soko la kimataifa hadi wastani wa dola za Marekani 40.03 kwa wakia mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani 28.27 kwa wakia mwaka 2024.

239. Mwaka 2025, uzalishaji wa madini ya bati ulikuwa tani 380.7 ikilinganishwa na tani 338.0 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 12.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za uchimbaji pamoja na mahitaji ya madini ya bati katika soko la kimataifa. Katika kipindi hicho, vibali 22 vyenye thamani ya dola za Marekani milioni 6.50 kwa ajili ya uuzaji wa madini ya bati nje ya nchi vilitolewa ikilinganishwa na vibali 18 vyenye thamani ya dola za Marekani milioni 6.94 vilivyotolewa mwaka 2024.

**Masoko ya Madini**

240. Mwaka 2025, kulikuwa na masoko 44 na vituo 117 vya ununuzi wa madini ikilinganishwa na masoko 43 na vituo 108 vilivyokuwepo mwaka 2024. Katika kipindi

hicho, maduhuli yaliyokusanywa katika masoko ya madini yaliongezeka kwa asilimia 47.3 na kufikia shilingi bilioni 320.89 ikilinganishwa na shilingi bilioni 217.92 zilizokusanywa mwaka 2024. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 281.34 zilitokana na mrabaha na shilingi bilioni 39.55 zilitokana na ada ya ukaguzi. Kuongezeka kwa makusanyo ya maduhuli kulitokana na kuimarika kwa shughuli za uchimbaji mdogo pamoja na kuendelea kuimarisha usimamizi, ukaguzi na udhibiti wa utoroshaji wa madini kwenye masoko na vituo vya ununuzi wa madini.

241. Mwaka 2025, tani 20.04 za dhahabu zenye thamani ya shilingi trilioni 5.14 ziliuzwa katika masoko ya madini nchini ikilinganishwa na tani 16.49 za dhahabu zenye thamani ya shilingi trilioni 2.99 zilizouzwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la kiasi la asilimia 21.53. Hii ililotokana na kuendelea kuimarika kwa bei ya dhahabu na hivyo kuchochea uzalishaji kwa wachimbaji wadogo pamoja na kuendelea kudhibiti utoroshaji na biashara haramu ya madini nchini. Aidha, karati 50,339.31 za madini ya almasi zenye thamani ya shilingi bilioni 9.22 ziliuzwa katika masoko ya madini mwaka 2025 ikilinganishwa na karati 6,934.16 zenye thamani ya shilingi bilioni 3.20 zilizouzwa mwaka 2024. Ongezeko la mauzo ya madini ya almasi lilitokana na uwepo wa machimbo mapya (rush) ya wachimbaji wadogo wa almasi pamoja na mgodi wa kati wa El Hilal kuanza uzalishaji baada ya kusimama kwa muda mrefu kwa ajili ya matengenezo ya mitambo.

**Jedwali Na. 49: UCHIMBAJI WA MADINI: KIASI KILICHOPATIKANA,MWAKA 2020 - 2025**

| MADINI | Kipimo | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Almasi | Karati | 147,190.95 | 62,545.00 | 442,016.26 | 132,636.40 | 373,252.76 | 407,840.00 |
| Dhahabu | Kg | 55,805.33 | 59,638.00 | 56,942.98 | 54,760.32 | 61,680.81 | 68,225.38 |
| Tanzanite (ghafi) | Kg | 51,542.47 | 177,145.50 | 14,487.48 | 32,870.63 | 28,822.99 | 32,439.47 |
| Tanzanite magonga | Kg | 47,412.00 | 165,968.00 | 75,699.00 | 89,794.00 | 54,191.67 | 111,869.01 |
| Tanzanite (iliyokatwa na kusanifiwa) | Karati | 118,772.95 | 120,175.00 | 57,864.28 | 34,904.33 | 17,469.66 | 28,927.34 |
| Madini mengine ya Vito (ghafi) | Kg | 23,564,524.64 | 7,197,217.00 | 12,752,079.67 | 55,954,779.72 | 46,299,069.32 | 29,447,270.82 |
| Chumvi | Tani | 83,974.32 | 112,995.00 | 181,818.07 | 159,020.49 | 82,953.22 | 90,975.67 |
| *Phosphate* | Tani | 28,376.22 | 24,493.00 | 26,596.79 | 31,745.08 | 29,833.70 | 64,675.75 |
| Mawe ya Chokaa | 000 Tani | 6,788.35 | 8,506.00 | 7,741.00 | 10,128.67 | 9,731.18 | 12,046.75 |
| Bati | Tani | 47 | 211 | 538.17 | 420.81 | 338.01 | 380.68 |
| Jasi | Tani | 443,926.34 | 598,053.00 | 604,407.91 | 549,835.74 | 821,221.08 | 913,263.53 |
| Makaa ya Mawe | Tani | 689,959.96 | 976,319.00 | 2,511,419.40 | 3,256,481.06 | 3,904,542.69 | 3,879,960.85 |
| Pozolana | Tani | 160,077.81 | 216,934.00 | 226,038.26 | 351,988.16 | 287,136.94 | 540,213.71 |
| Kaolin | Tani | 98,453.67 | 100,950.00 | 46,973.44 | 75,246.95 | 86,054.98 | 119,725.92 |
| Madini ya Fedha | Kg | 13,186.58 | 9,324.00 | 13,602.43 | 14,481.35 | 3,129.06 | 1,895.22 |
| Shaba | *Pound* | 3,761,086.16 | 3,352,630.00 | 6,827,930.74 | 5,285,443.13 | 1,654,151.00 | 1,909,631.60 |
| chuma | Tani | 28,431.17 | 78,190.00 | 51,071.14 | 67,626.44 | 66,497.87 | 95,642.45 |
| *Bauxite* | Tani | 25,995.00 | 38,142.00 | 40,920.98 | 61,353.23 | 79,147.89 | 27,663.80 |
| Kinywe | Tani | - | - | - | - | 41,431.27 | 104,798.08 |
| CO2 (ToL) | Kg | - | - | - | - | 17,780,132.68 | 22,069,060.00 |
| Madini ya Ujenzi | 000 Tani | 31,891.75 | 32,304.00 | 37,498.03 | 33,807.05 | 33,302.72 | 36,499.77 |
| Madini mengine ya viwandani | 000 Tani | 2,160.57 | 1,037.00 | 1,458.38 | 1,745.02 | 1,662.69 | 1,131.54 |
| Madini mengine ya metali | 000 Tani | - | - | 93.41 | 63.55 | 33.96 | 25.12 |
| Makinikia ya Shaba | Tani | 33,377.08 | - | 2,013.26 | 5,926.27 | 30,164.91 | 34,744.08 |
| Mbale za shaba (Copper ore) | Tani | 1,204.84 | - | 6,623.58 | 6,307.01 | 17,615.66 | 7,382.40 |

**Chanzo:** Wizara ya Madini

Carat = 0.205 gm

**Jedwali Na. 50: KIASI NA THAMANI YA MADINI YALIYOPATA KIBALI CHA KUUZWA NJE YA NCHI, MWAKA 2022 - 2025**

| Aina ya Madini | Kipimo | Kiasi | | | | Thamani ('000 "USD) | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
| Almasi (Rough) | 000 Karati | 326 | 194 | 373.17 | 374 | 65,903 | 31,474 | 59,243 | 52,908 |
| Dhahabu | 000 Gramu | 62,512 | 62,781 | 59,471 | 48,563 | 2,850,345 | 3,021,627 | 3,431,080 | 4,253,471 |
| Vito - Ghafi | 000 Gramu | 15,017,635 | 98,891,510 | 207,735,738 | 51,751,923 | 19,415 | 28,456 | 21,199 | 20,452 |
| Vito - Vilivyochongwa na kusanifiwa | Karati | 93,351 | 101,153 | 64,493 | 87,819 | 2,480 | 2,622 | 1,916 | 1,160 |
| Chumvi | Tani | 22,225 | 34,350 | 27,298 | 35,954 | 2,375 | 3,509 | 3,237 | 4,611 |
| Phosphate | Tani | 40,710 | 9,934 | 10,953 | 30,481 | 6,944 | 3,646 | 2,997 | 7,348 |
| Bati | Tani | 564 | 440 | 408 | 331 | 12,505 | 7,061 | 6,941 | 6,501 |
| Jasi | Tani | 8,300 | 10,486 | 22,575 | 48,354 | 941 | 1,802 | 3,895 | 12,172 |
| Kinywe | Tani | 7,271 | 13,475 | 38,140 | 92,870 | 2,909 | 5,394 | 22,693 | 47,870 |
| Fedha | 000 Gramu | 802 | 1,214 | 1,067 | 1,164 | 629 | 886 | 1,141 | 1,482 |
| Shaba | 000 Lb | 6,993 | 4,156 | 3 | - | 3,879 | 2,273 | 0.012 | - |
| Makinikia ya shaba | Tani | 26,591 | 25,688 | 35,098 | 38,334 | 189,648 | 179,044 | 245,198 | 339139 |
| Makinikia ya dhahabu | Tani | 2,730 | 2,554 | 3,917 | 3,140 | 8,993 | - | 10,886 | 13635 |
| Bauxite | Tani | 14,790 | 14,430 | 4,520 | - | 758 | 795 | 660 | 0 |
| makaa ya mawe | Tani | 848,434 | 1,601,850 | 995,646 | 2,136,533 | 43,806 | 158,575 | 70,284 | 174138 |
| Madini ujenzi | Tani | 66,667 | 46,544 | 44,119 | 48,894 | 2,410 | 3,105 | 3,604 | 4141.09 |
| Mawe ya chokaa | Tani | 194,980 | 249,396 | 217,072 | 170,375 | 1,806 | 6,344 | 2,281 | 2159 |
| Madini ya metali | Tani | 32,113 | 34,462 | 18,438 | 25,115 | 21,500 | 30,948 | 21,817 | 42123.98 |
| Madini ya Viwandani | Tani | 34,042 | 28,636 | 27,846 | 9,108 | 6,961 | 3,266 | 6,597 | 1955.69 |
| **Jumla** | | | | | | **3,244,207** | **3,490,827** | **3,915,669** | **4,985,267** |

**Chanzo**: Wizara ya Madini

## SURA YA 10

## VIWANDA NA BIASHARA

**Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani**

242. Mwaka 2025, thamani ya bidhaa zilizozalishwa viwandani iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 27,923.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 27,725.7 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kuimarishwa kwa mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Katika kipindi hicho, bidhaa zilizoongoza katika uzalishaji ni pamoja na saruji iliyoongezeka kwa asilimia 21.1, ikifuatiwa na tabaka za mbao (asilimia 19.9), bia (asilimia 16.8), unga wa ngano (asilimia 13.2), bati (asilimia 13.0), rangi (asilimia 13.0) na nguo (asilimia 11.6). Kwa upande mwingine, gharama za uzalishaji bidhaa viwandani ziliongezeka kidogo na kufikia wastani wa shilingi bilioni 12,056.4 mwaka 2025 kutoka wastani wa shilingi bilioni 12,039.2 mwaka 2024. Aidha, idadi ya watu walioajiriwa viwandani iliongezeka kwa asilimia 1.7 na kufikia watu 397,953 mwaka 2025 kutoka watu 391,275 mwaka 2024.

**Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo**

243. Mwaka 2025, Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo - SIDO lilitoa mafunzo mbalimbali kwa wajasiriamali 12,450 ikilinganishwa na wajasiriamali 24,197 waliopata mafunzo mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 48.5. Hii ilitokana na kupungua kwa wafadhili wa mafunzo. Mafunzo yaliyotolewa yalihusu usindikaji wa vyakula, usimamizi wa biashara, mbinu za uzalishaji mali, utunzaji wa vitabu vya hesabu na uongozi wa vikundi/vyama vya wajasiriamali.

244. Mwaka 2025, Vituo vya Uendelezaji Teknolojia vilivyopo chini ya SIDO vilitengeneza na kusambaza mashine 458 ikilinganishwa na mashine 917 mwaka 2024. Katika kipindi hicho, wajasiriamali wapya saba (7) wenye ubunifu wa teknolojia na mawazo ya bidhaa mpya waliatamiwa ili kukuza vipaji vyao kama ilivyokuwa mwaka 2024. Aidha, wajasiriamali 34,498 walipatiwa ushauri wa kiufundi na biashara mwaka 2025 ikilinganishwa na wajasiriamali 32,198 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 7.1. Hii ilitokana na mwitikio wa wananchi kuendelea kuanzisha miradi ya ujasiriamali ili kujiongezea kipato.

245. Mwaka 2025, Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali - NEDF ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 4.1 kwa wajasiriamali 1,214 ikilinganishwa na shilingi bilioni 4.8 zilizotolewa kwa wajasiriamali 1,811 mwaka 2024. Aidha, mikopo iliyotolewa iliwezesha upatikanaji wa fursa za ajira 2,854 mwaka 2025 ikilinganishwa na fursa za ajira 3,727 zilizopatikana mwaka 2024. Vilevile, hali ya marejesho ya mikopo iliendelea kuimarika na kufikia asilimia 93.4 ya mikopo iliyoiva mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 92.3 mwaka 2024.

246. Mwaka 2025, Chuo cha Elimu ya Biashara - CBE kilitoa mafunzo ya kozi 20 za muda mfupi zinazohusu elimu ya biashara katika fani mbalimbali kwa washiriki 1,240 ikilinganishwa na kozi 35 za muda mfupi kwa washiriki 1,511 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 17.9 ya washiriki. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka utoaji wa kozi za muda mfupi katika vyuo vingine. Aidha, CBE iliratibu na kuendesha atamizi za biashara (incubation) kwa kuwaendeleza waatamiwaji 228 waliojisajili.

247. Mwaka 2025, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania - TIRDO lilifanya tafiti sita (6) ikilinganishwa na tafiti tano (5) zilizofanyika mwaka 2024. Tafiti hizo zilijumuisha: utafiti wa mnyororo wa thamani wa madini muhimu (zinc, tantalum na tungsten) katika mikoa ya Kagera, Singida na Dodoma; uibuaji wa fursa za uwekezaji; matumizi ya malighafi bioanuwai kutengeneza mkaa mbadala; matumizi ya vumbi la makaa ya mawe kutengeneza mkaa mbadala; utekelezaji wa mpango wa kwanza wa matumizi bora ya nishati; na usanifu na utengenezaji wa jiko sanifu kwa ajili ya uzalishaji wa mkaa mbadala.

248. Mwaka 2025, TIRDO ilifanya ukaguzi na kutoa ushauri wa kitaalamu katika viwanda nane (8) ikilinganishwa na viwanda 17 mwaka 2024. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa ushindani wa watoa huduma wengine na baadhi ya wateja kuchelewesha au kusitisha utekelezaji wa miradi yao. Aidha, TIRDO ilipima sampuli 344 za maabara mwaka 2025 ikilinganishwa na sampuli 549 zilizopimwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 37.3. Hii ilitokana na kupungua kwa idadi ya wateja waliohitaji kupima sampuli.

249. Mwaka 2025, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - CAMARTEC kiliboresha, kulizalisha na kununua aina 101 za zana za kilimo na teknolojia vijijini ikilinganishwa na aina 83 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 21.7. Katika kipindi hicho, CAMARTEC ilifanya kaguzi na majaribio ya modeli 89 za zana za kilimo zilizozalishwa nje ya nchi ikilinganishwa na kaguzi na majaribio ya modeli 87 mwaka 2024.

250. Mwaka 2025, Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania - TEMDO ilisanifu teknolojia 12 na kutengeneza chasili (prototypes) nane (8) zinazotumika katika shughuli za kiuchumi, ikiwemo uongezaji thamani mazao ya kilimo na utoaji wa huduma za afya. Aidha, TEMDO iliunda na kusimika mitambo ya kusafisha mafuta ya alizeti, kuchakata zao la muhogo pamoja na majokofu nane (8) kwa ajili ya kuhifadhia maiti katika hospitali mbalimbali. Vilevile, TEMDO ilitoa huduma za kihandisi kwa viwanda vitatu (3), hospitali moja (1) na kampuni moja (1) za uchimbaji madini na gesi mwaka 2025 ikilinganishwa na viwanda vitano (5) na kampuni tano (5) za uchimbaji madini mwaka 2024.

**Usajili wa Biashara na Viwanda**

251. Mwaka 2025, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni - BRELA ulisajili kampuni 18,489 ikilinganishwa na kampuni 16,748 zilizosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 10.4. Aidha, majina ya biashara 32,670 yalisajiliwa mwaka 2025 ikilinganishwa na majina ya biashara 30,753 yaliyosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 6.2. Vilevile, leseni 23,653 za biashara daraja "A" zilitolewa mwaka 2025 ikilinganishwa na leseni 20,364 za biashara daraja "A" zilizotolewa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 16.2. Kwa upande mwingine, BRELA ilitoa leseni 496 za viwanda mwaka 2025 ikilinganishwa na leseni 371 za viwanda zilizotolewa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 33.7. Ongezeko la usajili na utoaji wa leseni lilitokana na kuendelea kuboreshwa kwa mazingira ya ufanyaji biashara, ikiwemo matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika utoaji wa leseni pamoja na mafunzo kwa maafisa biashara na elimu kwa umma.

252. Mwaka 2025, BRELA ilisajili alama 3,064 za biashara na huduma ikilinganishwa na alama 3,662 za biashara na huduma zilizosajiliwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 16.3. Upungufu huo ulitokana na usajili kuwa mdogo ikilinganishwa na idadi ya maombi kulikosababishwa na changamoto katika mfumo wa *Industrial Property Automation System - IPAS*. Aidha, BRELA ilifanyia kazi maombi 732 ya kuwekea ulinzi uvumbuzi wa sayansi na teknolojia mwaka 2025 ikilinganishwa na maombi 597 yaliyofanyiwa kazi mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 22.6. Kati ya hayo, maombi 124 yalikuwa ya ndani na maombi 608 yalipitia Shirika la Kanda la Afrika linalosimamia Haki Miliki za Kitaaluma.

**Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa**

253. Mwaka 2025, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania - TanTrade iliratibu Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam. Aidha, kampuni 4,040 zilishiriki katika maonesho hayo mwaka 2025 ikilinganishwa na kampuni 3,954 zilizoshiriki mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 2.2. Ongezeko hilo lilitokana na mwitikio wa wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi kushiriki kwenye maonesho na kuimarika kwa diplomasia ya biashara kati ya Tanzania na mataifa mbalimbali. Kati ya kampuni zilizoshiriki, 3,646 zilikuwa za ndani na 394 kutoka nje ya nchi. Aidha, nchi 22 zilishiriki katika maonesho ya mwaka 2025 ikilinganishwa na nchi 28 mwaka 2024. Upungufu huo ulitokana na ushindani kutoka katika mataifa mengine ya Afrika na hali ya siasa katika baadhi ya mataifa yaliyoshiriki mwaka 2024.

254. Mwaka 2025, mauzo katika Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yalikuwa shilingi bilioni 7.0 ikilinganishwa na mauzo ya shilingi bilioni 3.6 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 94.4. Ongezeko hilo lilitokana na mwitikio wa wadau kutembelea Maonesho hayo kufuatia uhamasishaji na fursa za biashara zilizopo. Aidha, kampuni za ndani zilipata miadi ya kibiashara yenye thamani ya shilingi bilioni 4.8

kwa shughuli za kiuchumi ikiwemo mifugo, usafirishaji, madini, kilimo, uvuvi na ujenzi ikilinganishwa na miadi ya shilingi bilioni 1.93 mwaka 2024. Vilevile, ajira za muda mfupi takribani 22,593 zilipatikana katika maonesho ya mwaka 2025 ikilinganishwa na ajira 21,518 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 5.0.

255. Mwaka 2025, TanTrade iliratibu ushiriki wa kampuni na taasisi 598 za Tanzania katika majukwaa 15 ya kimataifa ya kibiashara yaliyoandaliwa ndani na nje ya nchi ikilinganishwa na taasisi 464 katika majukwaa 14 mwaka 2024, sawa na ongezeko la taasisi la asilimia 28.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mwamko wa kampuni na taasisi kushiriki katika maonesho kwa lengo la kutangaza bidhaa wanazozalisha na huduma wanazotoa pamoja na urahisi wa taratibu za kushiriki katika maonesho hayo kwa kujisajili kielektroniki. Kupitia majukwaa hayo, Tanzania ilipata mauzo ya papo kwa hapo ya shilingi milioni 337.7 pamoja na kusainiwa kwa mikataba nane (8) yenye thamani ya shilingi bilioni 38.0 ya makubaliano katika biashara ya kaboni, sekta ya afya, elimu na nishati.

256. Mwaka 2025, TanTrade iliendelea kukusanya na kusambaza taarifa za biashara kwa wafanyabiashara 224,700 kupitia mifumo ya TanTrade Biashara App na Trade Portal ikilinganishwa na wafanyabiashara 146,888 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 53.0. Hii ilitokana na uhamasishaji wa matumizi ya mifumo hiyo kupitia vipindi vya redio na mitandao ya kijamii. Aidha, kampuni 2,245 zilisajiliwa katika kanzidata ya wafanyabiashara mwaka 2025 ikilinganishwa na kampuni 483 zilizosajiliwa mwaka 2024. Ongezeko la usajili wa kampuni lilitokana na kuboreshwa kwa mifumo ya utoaji huduma pamoja na kuimarika kwa ushirikiano baina ya TanTrade na taasisi wezeshi za biashara.

**Udhibiti Ubora wa Viwango na Vipimo**

257. Mwaka 2025, Shirika la Viwango Tanzania - TBS liliandaa viwango 575 vya ubora ikilinganishwa na viwango 571 vilivyoandaliwa mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa matumizi ya bidhaa zenye ubora uliothibitishwa. Aidha, sampuli 44,809 zilipimwa kwa ajili ya kuhakiki ubora na usalama wa bidhaa mwaka 2025 ikilinganishwa na sampuli 38,724 zilizopimwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 15.7. Hii ilitokana na kuimarishwa kwa ukaguzi na ufuatiliaji katika masoko pamoja na uwekezaji katika vifaa vya kisasa vya maabara. Vilevile, vifaa 11,139 vilifanyiwa uhakiki/ugezi mwaka 2025 ikilinganishwa na vifaa 9,653 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 15.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uhitaji wa huduma ya ugezi kutoka kwa wadau wa ujenzi, vituo vya afya pamoja na maghala ya kuhifadhi mazao.

258. Mwaka 2025, TBS ililitoa leseni 949 za ubora ikilinganishwa na leseni 534 zilizotolewa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 77.7. Hii ilitokana na kuimarishwa kwa udhibiti na usimamizi wa bidhaa katika masoko, kuongezeka kwa uelewa kuhusu umuhimu wa kutumia bidhaa zilizothibitishwa pamoja na kuimarika kwa biashara ndani ya

Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kati ya leseni hizo, leseni 591 zilitolewa kwa wazalishaji wakubwa na wa kati na leseni 358 kwa wajasiriamali wadogo. Aidha, mafunzo ya udhibiti ubora yalitolewa kwa washiriki 2,926 mwaka 2025 ikilinganishwa na washiriki 3,052 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 4.1.

259. Mwaka 2025, TBS ilisajili bidhaa 2,568 za chakula na vipodozi ikilinganishwa na bidhaa 1,748 zilizosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 46.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa udhibiti wa bidhaa za chakula na vipodozi zinazotoka nje ya nchi ili kuzingatia ubora na usalama wa afya kwa watumiaji. Kati ya bidhaa zilizosajiliwa, bidhaa za chakula zilikuwa 1,699 na bidhaa za vipodozi zilikuwa 869. Aidha, TBS ilisajili na kutoa vibali 25,830 vya maeneo ya uzalishaji, uuzaji, na usambazaji wa bidhaa za chakula na vipodozi ikilinganishwa na vibali 9,963 vilivyotolewa mwaka 2024. Kati ya hivyo, vibali 22,503 vilikuwa vya maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vibali 3,327 vya maeneo ya bidhaa za vipodozi. Ongezeko la utoaji wa vibali lilitokana na kuimarishwa kwa udhibiti pamoja na kupungua kwa gharama za usajili wa maeneo hayo.

260. Mwaka 2025, TBS kwa kushirikiana na mawakala wake wa ukaguzi ilikagua magari 56,389 yaliyotumika kabla ya kuingizwa nchini ikilinganishwa na magari 45,697 yaliyokaguliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 23.4. Kati ya hayo, magari 723, sawa na asilimia 1.3 hayakukidhi viwango na hivyo kufanyiwa maboresho ili kukidhi viwango vya kuingizwa nchini. Aidha, TBS ilikagua bidhaa 106,655 baada ya kuwasili nchini mwaka 2025 ikilinganishwa na bidhaa 78,073 zilizokaguliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 36.6. Hii ilitokana na kuimarishwa kwa udhibiti wa bidhaa pindi zinapowasili nchini na kuongezeka kwa wigo wa bidhaa zinazohitajika kukaguliwa kulikochangiwa na matumizi ya Mfumo wa Ukaguzi wa Bidhaa wa Pamoja. Kati ya bidhaa zilizokaguliwa, bidhaa 1,233, sawa na asilimia 1.2 hazikukidhi matakwa ya viwango ambapo wamiliki wa bidhaa husika walielekezwa kuziharibu au kuzirudisha kwenye nchi zilipotoka. Vilevile, bidhaa 37,809 kutoka nje ya nchi zilikaguliwa kupitia mawakala wa TBS kabla ya kuingizwa nchini mwaka 2025 ikilinganishwa na bidhaa 34,589 zilizokaguliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 9.3. Kati ya hizo, bidhaa 168 hazikukidhi matakwa ya viwango vya ubora na hivyo kuzuiwa kuingia nchini.

261. Mwaka 2025, Wakala wa Vipimo - WMA ilihakiki vipimo 1,269,957 ikilinganishwa na vipimo 981,397 vilivyohakikiwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 29.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uelewa wa matumizi ya vipimo sahihi. Aidha, WMA ilifanya kaguzi 5,082 za kushtukiza za vipimo vinavyotumika kwenye biashara, afya, usalama na mazingira mwaka 2025 ikilinganishwa na kaguzi 4,229 zilizofanyika mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 20.2. Hii ilitokana na kuimarishwa kwa usimamizi wa matumizi ya vipimo sahihi kwa lengo la kumlinda mlaji. Kupitia kaguzi hizo, vipimo 67,251 vilikaguliwa ambapo vipimo 64,230, sawa na asilimia 95.5 vilikidhi viwango na vipimo

3,021 havikukidhi. Vilevile, WMA ilipima aina mpya 124 za vipimo kutoka ndani na nje ya nchi mwaka 2025 ikilinganishwa na aina 236 zilizopimwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 52.5. Hii ilichangiwa na kupungua kwa aina mpya za vipimo zilizoingizwa nchini. Kati ya hivyo, aina 92 za vipimo (sawa na asilimia 74.2) ziliidhinishwa na aina 32 hazikuidhinishwa kutokana na kutokidhi vigezo.

262. Mwaka 2025, WMA ilitoa leseni na vibali 552 kwa mafundi wanaojihusisha na uundaji, usimikaji na urekebishaji wa vipimo ikilinganishwa na leseni na vibali 533 vilivyotolewa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 3.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uelewa wa wadau wa vipimo kuhusu umuhimu wa kuwa na vibali na leseni. Aidha, lita milioni 11,001.12 za mafuta ya kupikia, petroli na dizeli katika meli 177 ulihakikiwa ikilinganishwa na lita milioni 9,302.90 kwenye meli 174 uliohakikiwa mwaka 2024. Kati ya hizo, lita milioni 4,477.13 zilikuwa za mafuta kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi na lita milioni 6,523.99 zilikuwa za mafuta yaliyoingizwa nchini kwenda nchi jirani.

**Usawa wa Ushindani na Udhibiti wa Bidhaa Bandia**

263. Mwaka 2025, Tume ya Ushindani - FCC iliidhinisha maombi ya muungano wa kampuni 54 ikilinganishwa na maombi 56 mwaka 2024. Maombi hayo yalitoka katika sekta za kilimo, uzalishaji viwandani, fedha, afya, mawasiliano, madini, biashara na nishati. Aidha, FCC ilisajili mikataba 43 ya walaji iliyoandaliwa na upande mmoja (Standard Form Consumer Contracts) mwaka 2025 ikilinganishwa na mikataba 68 iliyosajiliwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 36.8. Hii ilitokana na mwitikio mdogo wa wadau waliojitokeza kusajili mikataba.

264. Mwaka 2025, FCC ilikagua makasha 6,411 ya kusafirishia mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam na bandari za nchi kavu ikilinganishwa na makasha 6,357 yaliyokaguliwa mwaka 2024. Kati ya hayo, makasha 471 yenye thamani ya shilingi bilioni 8.2 yalibainika kuwa na bidhaa bandia ambazo ziliteketezwa. Bidhaa zilizoteketezwa zilikuwa za matumizi ya nyumbani, vifaa vya ujenzi, shajala, vifaa vya kielektroniki, vipuri vya pikipiki na magari.

265. Mwaka 2025, Baraza la Ushindani - FCT lilipokea kesi za rufaa mpya 18 na kesi za rufaa saba (7) zilikuwa zinaendelea kusikilizwa ikilinganishwa na kesi za rufaa mpya 14 na kesi za rufaa 29 zilizokuwa zinaendelea kusikilizwa mwaka 2024. Kati ya hizo, kesi za rufaa 20 ziliamuliwa mwaka 2025 ikilinganishwa na kesi za rufaa 37 zilizoamuliwa mwaka 2024. Kesi hizo zilitoka kwa wazalishaji, wasambazaji na walaji katika sekta za nishati, maji, mawasiliano na usafirishaji wa anga na nchi kavu.

**Shirika la Taifa la Maendeleo**

266. Mwaka 2025, Shirika la Taifa la Maendeleo - NDC lilizalisha tani 73.1 za mpira kupitia mradi wa mashamba ya Kihuhwi (Muheza) na Kalunga (Kilombero) ikilinganishwa na tani 63.2 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 15.7. Hii ilitokana na uwepo wa hali nzuri ya hewa pamoja na maboresho katika mifumo ya usimamizi wa mashamba. Mpira uliozalishwa uliuzwa nchini kwa ajili ya matumizi ya viwanda mbalimbali. Aidha, NDC ilikusanya shilingi milioni 235 kutokana na mauzo ya mpira mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi milioni 204 zilizokusanywa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 15.2.

267. Mwaka 2025, Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibailojia - TBPL kilizalisha lita 389,847 za dawa za viuadudu kwa ajili ya kuua viluilui vya mbu wanaoeneza malaria ikilinganishwa na lita 269,673 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 44.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji kufuatia kuendelea na utekelezaji wa programu ya kutokomeza malaria katika halmashauri 57 zenye maambukizi makubwa. Aidha, shilingi bilioni 9.5 zilikusanywa kutokana na mauzo ya viuadudu mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 4.2 zilizokusanywa mwaka 2024. Kwa upande mwingine, Kiwanda cha Kuzalisha Mashine na Vipuri - KMTC kilizalisha mashine 12 na vipuri 123 mwaka 2025 ikilinganishwa na mashine 12 na vipuri 37 vilivyozalishwa mwaka 2024. Ongezeko la uzalishaji lilitokana na uboreshwaji na ujenzi wa miundombinu ya kiwanda. Kuongezeka kwa uzalishaji kulienda sambamba na ongezeko la mauzo yaliyofikia shilingi milioni 165.6 mwaka 2025 ikilinganishwa na mauzo ya shilingi milioni 157.2 mwaka 2024.

**Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala**

268. Mwaka 2025, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala - WRRB ilitoa leseni 417 ikilinganishwa na leseni 195 zilizotolewa mwaka 2024. Ongezeko la leseni lilitokana na kuimarishwa kwa miundombinu ya kuhifadhia mazao na usimamizi wa sheria, kanuni na taratibu kuhusu mfumo wa stakabadhi ghalani. Leseni hizo zilitolewa katika mazao ya dengu, kakao, karanga, kahawa, mbaazi, soya, ufuta na korosho. Kati ya hizo, leseni 405 zilitolewa kwa waendesha ghala, leseni saba (7) kwa wakaguzi wa ghala na leseni tano (5) kwa meneja dhamana. Katika kipindi hicho, tani 1,108,403.4 za mazao mbalimbali zilihifadhiwa kwenye ghala hizo ikilinganishwa na tani 696,756.0 zilizohifadhiwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 59.1. Hii ilitokana na uhamasishaji wa matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani.

**Jedwali Na. 51: MATUMIZI YA SARUJI NCHINI (Tani), MWAKA 2010 - 2025**

| Mwaka | Kutoka Nje | Uuzaji Nje | Uzalishaji wa Ndani | Matumizi | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|
| 2010 | 566,828 | 189,321 | 2,312,055 | 2,689,562 | 12.1 |
| 2011 | 768,343 | 217,944 | 2,408,765 | 2,959,164 | 10.0 |
| 2012 | 1,013,986 | 145,793 | 2,557,798 | 3,425,991 | 15.8 |
| 2013 | 1,218,453 | 154,481 | 2,369,819 | 3,433,791 | 0.2 |
| 2014 | 1,428,995 | 142,001 | 2,795,687 | 4,082,681 | 18.9 |
| 2015 | 896,872 | 129,083 | 3,140,160 | 4,404,187 | 7.9 |
| 2016 | 513,307 | 253,506 | 4,047,712 | 4,307,513 | (2.2) |
| 2017 | 188,599 | 226,588 | 4,397,684 | 4,359,695 | 1.2 |
| 2018 | 341,179 | 196,449 | 4,540,309 | 4,685,039 | 7.5 |
| 2019 | 448,579 | 410,607 | 5,290,878 | 5,328,850 | 13.7 |
| 2020 | 716,929 | 493,867 | 5,605,626 | 5,828,688 | 9.4 |
| 2021 | 690,474 | 441,828 | 6,614,359 | 6,863,005 | 17.7 |
| 2022 | 566,826 | 632,726 | 7,598,073 | 7,532,173 | 9.8 |
| 2023 | 809,199 | 531,699 | 7,673,016 | 7,950,515 | 5.6 |
| 2024 | 398,039 | 391,961 | 7,699,840 | 7,705,918 | (3.1) |
| 2025 | 308,711 | 306,510 | 9,322,317 | 9,324,518 | 21.0 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Mapato Tanzania

**Jedwali Na. 52: UZALISHAJI WA BAADHI YA BIDHAA VIWANDANI, MWAKA 2016 - 2025**

| Aina ya Bidhaa | Kipimo | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Biskuti & tambi | Tani | 15,890 | 16,451 | 16,911 | 18,113 | 22,430 | 30,154 | 29,653 | 27,509 | 26,612 | 23,390 | -12.1 |
| Unga wa ngano | Tani | 498,940 | 606,432 | 662,967 | 680,393 | 767,476 | 737,652 | 684,708 | 839,266 | 858,021 | 971,214 | 13.2 |
| Konyagi | 000 Lita | 28,754 | 25,555 | 29,335 | 32,366 | 33,287 | 22,066 | 22,489 | 31,024 | 41,903 | 35,801 | -14.6 |
| Bia | 000 Lita | 383,251 | 396,864 | 412,555 | 391,299 | 385,851 | 380,464 | 456,035 | 498,611 | 646,552 | 755,081 | 16.8 |
| Chibuku | 000 Lita | 26,513 | 22,624 | 20,819 | 20,350 | 21,712 | 22,256 | 24,366 | 23,757 | 23,288 | 22,740 | -2.4 |
| Sigara | Milioni | 8,091 | 7,412 | 7,921 | 8,369 | 7,320 | 7,021 | 12,201 | 11,868 | 9,928 | 10,672 | 7.5 |
| Nguo | 000 $M^2$ | 76,436 | 52,052 | 52,613 | 45,415 | 53,067 | 65,365 | 48,504 | 39,774 | 31,712 | 35,375 | 11.6 |
| Kamba za katani | Tani | 9,216 | 8,188 | 8,148 | 9,287 | 8,187 | 8,583 | 6,171 | 5,093 | 4,846 | 3,136 | -35.3 |
| Nyavu za uvuvi | Tani | 312 | 196 | 228 | 254 | 261 | 273 | 461 | 604 | 411 | 434 | 5.6 |
| Tabaka za mbao | $M^3$ | 34,983 | 37,302 | 37,849 | 42,563 | 34,237 | 29,867 | 25,305 | 17,788 | 22,688 | 27,197 | 19.9 |
| Dawa za pareto | Tani | 126 | 134 | 139 | 145 | 154 | 152 | 173 | 325 | 239 | 244 | 2.1 |
| Rangi | 000 Lita | 35,096 | 40,146 | 47,928 | 58,024 | 48,261 | 62,785 | 64,028 | 75,423 | 77,364 | 87,431 | 13.0 |
| Saruji | 000 Tani | 4,572 | 4,398 | 4,766 | 6,514 | 6,496 | 6,531 | 7,598 | 7,673 | 7,700 | 9,322 | 21.1 |
| Chuma | Tani | 219,765 | 231,591 | 275,267 | 272,531 | 277,785 | 293,797 | 311,781 | 343,575 | 391,100 | 418,708 | 7.1 |
| Bati | Tani | 91,421 | 84,541 | 84,132 | 100,963 | 107,836 | 119,844 | 129,038 | 118,767 | 125,555 | 141,921 | 13.0 |
| Betri | Milioni | 69 | 122 | 115 | 120 | 132 | - | - | - | - | - | - |

**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara ya Viwanda na Biashara
- Hakuna uzalishaji

**Jedwali Na. 53: VIWANDA: IDADI YA WATU WALIOAJIRIWA, MWAKA 2023 - 2025**

| ISIC Rev.4 | Shughuli | Walioajiriwa | | | Wengine | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2023 | 2024 | 2025 | 2023 | 2024 | 2025 | 2023 | 2024 | 2025 |
| 10 | Vyakula | 128,606 | 131,873 | 132,405 | 25,189 | 25,813 | 26,310 | 153,795 | 157,686 | 158,715 |
| 11 | Vinywaji | 37,026 | 38,399 | 40,577 | 7,758 | 7,950 | 7,807 | 44,784 | 46,349 | 48,384 |
| 12 | Tumbaku na Sigara | 7,501 | 7,470 | 7,542 | 2,104 | 2,156 | 2,357 | 9,605 | 9,626 | 9,899 |
| 13,14 | Ufumaji na Ushonaji | 43,938 | 45,670 | 46,100 | 2,455 | 2,516 | 3,813 | 46,393 | 48,186 | 49,913 |
| 15 | Ngozi Bidhaa za Ngozi | 7,116 | 6,696 | 5,825 | 782 | 559 | 855 | 7,898 | 7,255 | 6,680 |
| 16 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 8,474 | 9,838 | 10,579 | 1,555 | 1,602 | 1,972 | 10,029 | 11,440 | 12,551 |
| 17, 18 | Karatasi, Uchapishaji | 10,752 | 9,032 | 7,500 | 468 | 754 | 751 | 11,220 | 9,786 | 8,251 |
| 20, 21 | Utengenezaji Kemikali na Madawa ya Binadamu | 19,982 | 20,661 | 19,627 | 3,317 | 2,538 | 2,132 | 23,299 | 23,199 | 21,759 |
| 22 | Bidhaa za mpira na Plastiki | 11,279 | 11,201 | 12,754 | 1,149 | 1,086 | 1,605 | 12,428 | 12,287 | 14,359 |
| 23 | Bidhaa Nyingine za Madini zisizo za metali | 14,407 | 13,528 | 14,292 | 2,852 | 3,614 | 3,607 | 17,259 | 17,142 | 17,899 |
| 19, 24-33 | Nyinginezo | 35,548 | 45,509 | 46,178 | 2,290 | 2,810 | 3,365 | 37,838 | 48,319 | 49,543 |
| | **Jumla** | **324,629** | **339,877** | **343,379** | **49,919** | **51,398** | **54,574** | **374,548** | **391,275** | **397,953** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
*Takwimu zimekadiriwa kutokana na Utafiti wa Sensa ya Viwanda ya Mwaka 2013 na Utafiti wa Mwaka 2015 na Mwaka 2016 wa Uzalishaji Viwandani
Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

## Jedwali Na. 54: VIWANDA: GHARAMA ZA KAZI, MWAKA 2023 - 2025

| ISIC Rev.4 | Shughuli | Mishahara (Shilingi Milioni) | | | Malipo Mengine (Shilingi Milioni) | | | Jumla ( Shilingi Milioni) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2023*** | **2024*** | **2025*** | **2023*** | **2024*** | **2025*** | **2023*** | **2024*** | **2025*** |
| 10 | Vyakula | 708,073 | 729,315 | 733,967 | 107,197 | 108,269 | 110,512 | 815,270 | 837,584 | 844,479 |
| 11 | Vinywaji | 433,949 | 464,325 | 481,687 | 152,508 | 153,118 | 157,573 | 586,457 | 617,443 | 639,260 |
| 12 | Tumbaku na Sigara | 193,300 | 192,267 | 205,485 | 44,703 | 43,771 | 44,729 | 238,003 | 236,038 | 250,214 |
| 13,14 | Ufumaji na Ushonaji | 215,385 | 239,385 | 251,184 | 94,008 | 98,196 | 99,192 | 309,393 | 337,581 | 350,376 |
| 15 | Ngozi Bidhaa za Ngozi | 12,239 | 11,751 | 10,800 | 1,022 | 973 | 886 | 13,261 | 12,724 | 11,686 |
| 16 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 56,976 | 58,400 | 60,138 | 6,672 | 7,912 | 7,683 | 63,648 | 66,312 | 67,821 |
| 17, 18 | Karatasi, Uchapishaji | 103,534 | 99,022 | 95,299 | 18,983 | 17,902 | 16,506 | 122,517 | 116,924 | 111,805 |
| 20, 21 | Utengenezaji Kemikali na Madawa ya Binadamu | 140,556 | 141,779 | 140,892 | 18,164 | 18,340 | 18,771 | 158,720 | 160,119 | 159,663 |
| 22 | Bidhaa za mpira na Plastiki | 72,230 | 71,247 | 86,588 | 8,782 | 8,579 | 8,751 | 81,012 | 79,826 | 95,339 |
| 23 | Bidhaa Nyingine za Madini zisizo za metali | 190,269 | 189,752 | 195,897 | 47,688 | 46,551 | 45,339 | 237,957 | 236,303 | 241,236 |
| 19, 24-33 | Nyinginezo | 313,884 | 316,615 | 335,387 | 54,015 | 56,371 | 59,460 | 367,899 | 372,986 | 394,847 |
| **Jumla** | | **2,440,395** | **2,513,858** | **2,597,324** | **553,742** | **559,982** | **569,402** | **2,994,137** | **3,073,840** | **3,166,726** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
*Takwimu zimekadiriwa kutokana na Utafiti wa Sensa ya Viwanda ya Mwaka 2013 na Utafiti wa Mwaka 2015 na Mwaka 2016 wa Uzalishaji Viwandani
Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

## Jedwali Na. 55: VIWANDA: MUHTASARI WA MATOKEO, MWAKA 2023 - 2025

| ISIC Rev.4 | Shughuli | Pato (Shilingi Milioni) | | | Gharama (Shilingi Milioni) | | | Thamani iliyoongezeka (Shilingi Milioni) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2023* | 2024* | 2025* | 2023* | 2024* | 2025* | 2023* | 2024* | 2025* |
| 10 | Vyakula | 10,228,274 | 10,793,951 | 10,822,313 | 4,534,228 | 4,754,349 | 4,640,811 | 5,694,046 | 6,039,602 | 6,181,502 |
| 11 | Vinywaji | 4,218,122 | 4,883,542 | 4,953,918 | 1,218,315 | 1,325,629 | 1,354,592 | 2,999,807 | 3,557,913 | 3,599,326 |
| 12 | Tumbaku na Sigara | 1,585,095 | 1,669,632 | 1,679,161 | 383,722 | 581,421 | 572,050 | 1,201,373 | 1,088,211 | 1,107,111 |
| 13,14 | Ufumaji na Ushonaji | 1,237,746 | 1,347,879 | 1,352,589 | 546,555 | 686,180 | 707,177 | 691,191 | 661,699 | 645,412 |
| 15 | Ngozi Bidhaa za Ngozi | 138,920 | 157,123 | 159,774 | 90,965 | 72,211 | 73,375 | 47,955 | 84,912 | 86,399 |
| 16 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 376,057 | 417,660 | 418,419 | 120,325 | 101,906 | 102,988 | 255,732 | 315,754 | 315,431 |
| 17, 18 | Karatasi, Uchapishaji | 679,837 | 717,855 | 719,229 | 406,045 | 404,498 | 411,605 | 273,792 | 313,357 | 307,624 |
| 20, 21 | Utengenezaji Kemikali na Madawa ya Binadamu | 1,489,048 | 1,496,829 | 1,520,911 | 898,770 | 994,008 | 982,642 | 590,278 | 502,821 | 538,269 |
| 22 | Bidhaa za mpira na Plastiki | 1,529,533 | 1,455,808 | 1,465,140 | 953,963 | 988,276 | 955,432 | 575,570 | 467,532 | 509,708 |
| 23 | Bidhaa Nyingine za Madini zisizo za metali | 1,953,064 | 1,779,275 | 1,781,665 | 956,057 | 902,970 | 1,012,120 | 997,007 | 876,305 | 769,545 |
| 19, 24-33 | Nyinginezo | 3,002,764 | 3,006,193 | 3,050,004 | 1,681,774 | 1,227,743 | 1,243,629 | 1,320,990 | 1,778,450 | 1,806,375 |
| **Jumla** | | **26,438,460** | **27,725,747** | **27,923,123** | **11,790,719** | **12,039,191** | **12,056,421** | **14,647,741** | **15,686,556** | **15,866,702** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
*Takwimu zimekadiriwa kutokana na Utafiti wa Sensa ya Viwanda ya Mwaka 2013 na Utafiti wa Mwaka 2015 na Mwaka 2016 wa Uzalishaji Viwandani
Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

## Jedwali Na. 56: VIWANDA: MUHTASARI WA MATOKEO KIMKOA, MWAKA 2023 - 2025

| Jina la Mkoa | Idadi ya Wafanyakazi | | | Idadi ya Waajiriwa | | | Mishahara (Shilingi Milioni) | | | Thamani Iliyoongezeka (Shilingi Milioni) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2023*** | **2024*** | **2025*** | **2023*** | **2024*** | **2025*** | **2023*** | **2024*** | **2025*** | **2023*** | **2024*** | **2025*** |
| Dodoma | 4,053 | 5,851 | 5,959 | 3,512 | 5,060 | 5,112 | 30,537 | 43,440 | 44672 | 183,296 | 272,330 | 276,568 |
| Arusha | 31,789 | 32,262 | 33,413 | 27,552 | 28,281 | 28,572 | 103,684 | 108,870 | 121,485 | 622,345 | 669,528 | 673,309 |
| Kilimanjaro | 23,870 | 24,297 | 24,612 | 20,689 | 20,968 | 21,184 | 131,332 | 131,440 | 135,712 | 788,285 | 823,995 | 832,818 |
| Tanga | 18,019 | 18,851 | 19,917 | 15,618 | 16,516 | 16,686 | 163,657 | 177,039 | 181,917 | 982,310 | 1,088,740 | 1,100,360 |
| Morogoro | 56,466 | 56,833 | 57,547 | 48,939 | 49,811 | 49,824 | 69,432 | 69,785 | 71,076 | 416,735 | 437,465 | 442,489 |
| Pwani | 17,576 | 18,673 | 18,992 | 15,235 | 16,147 | 16,213 | 98,507 | 106,800 | 109,671 | 591,254 | 656,779 | 664,322 |
| Dar es Salaam | 120,853 | 121,564 | 122,619 | 104,744 | 105,110 | 106,093 | 1,401,282 | 1,388,597 | 1,423,718 | 8,410,776 | 8,705,004 | 8,808,973 |
| Lindi | 1,802 | 2,482 | 2,519 | 1,565 | 2,174 | 2,196 | 622 | 884 | 907 | 3,741 | 5,448 | 5,911 |
| Mtwara | 5,225 | 6,044 | 6,145 | 4,529 | 5,228 | 5,282 | 23,238 | 26,490 | 27,870 | 139,472 | 166,058 | 167,965 |
| Ruvuma | 3,372 | 3,464 | 3,523 | 2,923 | 2,996 | 3,027 | 4,684 | 4,911 | 6,094 | 28,129 | 30,217 | 30,571 |
| Iringa | 8,987 | 9,421 | 9,582 | 7,788 | 8,148 | 8,232 | 55,431 | 57,263 | 59,164 | 332,705 | 358,974 | 363,097 |
| Mbeya | 10,763 | 11,356 | 11,550 | 9,327 | 9,953 | 11,056 | 112,773 | 123,104 | 128,191 | 676,882 | 757,044 | 764,735 |
| Singida | 4,164 | 4,898 | 4,912 | 3,610 | 4,292 | 4,136 | 4,056 | 4,762 | 4,920 | 24,339 | 29,847 | 30,197 |
| Tabora | 1,327 | 2,045 | 2,080 | 1,148 | 1,793 | 1,811 | 22,368 | 35,737 | 36,924 | 134,256 | 219,769 | 233,193 |
| Rukwa | 2,774 | 3,063 | 3,215 | 2,403 | 2,649 | 2,676 | 12,922 | 14,065 | 15,532 | 77,548 | 88,167 | 88,387 |
| Kigoma | 3,376 | 4,335 | 4,409 | 2,927 | 3,748 | 3,787 | 2,176 | 2,850 | 3,045 | 13,071 | 17,541 | 17,742 |
| Shinyanga | 4,964 | 5,951 | 6,053 | 4,304 | 5,143 | 5,186 | 22,218 | 26,217 | 27,087 | 133,351 | 164,344 | 157,231 |
| Kagera | 6,469 | 6,859 | 6,976 | 5,607 | 5,925 | 5,986 | 10,344 | 11,182 | 12,553 | 62,091 | 68,770 | 69,560 |
| Mwanza | 19,810 | 20,703 | 21,056 | 17,168 | 17,888 | 17,972 | 129,898 | 133,647 | 135,154 | 779,671 | 837,823 | 847,445 |
| Mara | 6,345 | 6,806 | 6,922 | 5,501 | 5,886 | 5,947 | 11,351 | 12,424 | 12,837 | 68,121 | 76,392 | 77,218 |
| Manyara | 9,230 | 9,561 | 9,724 | 8,000 | 8,267 | 8,352 | 5,404 | 5,514 | 6,897 | 32,440 | 34,573 | 34,970 |
| Njombe | 4,940 | 5,879 | 5,979 | 4,284 | 5,084 | 5,146 | 10,314 | 12,521 | 13,937 | 61,909 | 77,003 | 77,887 |
| Katavi | 2,560 | 3,401 | 3,459 | 2,219 | 2,980 | 3,011 | 2,219 | 2,942 | 3,040 | 13,315 | 18,440 | 18,600 |
| Simiyu | 3,147 | 3,317 | 3,374 | 2,725 | 2,907 | 2,937 | 8,283 | 9,040 | 10,340 | 49,722 | 55,599 | 56,238 |
| Geita | 1,081 | 1,574 | 1,601 | 938 | 1,380 | 1,394 | 409 | 596 | 719 | 2,445 | 3,718 | 3,761 |
| Songwe | 1,586 | 1,785 | 1,815 | 1,374 | 1,543 | 1,561 | 3,254 | 3,738 | 3,862 | 19,532 | 22,988 | 23,155 |
| **Jumla** | **374,548** | **391,275** | **397,953** | **324,629** | **339,877** | **343,379** | **2,440,395** | **2,513,858** | **2,597,324** | **14,647,741** | **15,686,556** | **15,866,702** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu
*Takwimu zimekadiriwa kutokana na Utafiti wa Sensa ya Viwanda ya Mwaka 2013 na Utafiti wa Mwaka 2015 na Mwaka 2016 wa Uzalishaji Viwandani
Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

## SURA YA 11

## UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI

### UJENZI

**Mtandao wa Barabara Nchini**

269. Mwaka 2025, mtandao wa barabara nchini ulifikia kilometa 181,883.59 ikilinganishwa na kilometa 181,864.81 mwaka 2024. Kati ya hizo, kilometa 37,734.41 zinasimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania - TANROADS na kilometa 144,149.18 zinasimamiwa na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini - TARURA.

270. Mwaka 2025, mtandao wa barabara zinazosimamiwa na TANROADS uliongezeka na kufikia kilometa 37,734.41 kutoka kilometa 37,435.04 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilitokana na kukasimishwa, kupandishwa hadhi na kufunguliwa kwa barabara mpya za wilaya. Kati ya mtandao huo, kilometa 12,527.44 ni barabara kuu zinazounganisha mikoa na nchi jirani na kilometa 25,206.97 ni barabara za mikoa zinazounganisha miji mikuu ya mikoa na wilaya.

271. Mwaka 2025, barabara kuu na za mikoa zenye kiwango cha lami na changarawe/udongo zilizofanyiwa tathmini zilikuwa kilometa 34,673.50 ikilinganishwa na kilometa 35,415.75 mwaka 2024. Kati ya barabara zilizofanyiwa tathmini, kilometa 5,782.48 zilikuwa katika hali mbaya, kilometa 18,456.24 zilikuwa katika hali ya wastani na kilometa 10,434.78 zilikuwa katika hali nzuri mwaka 2025 ikilinganishwa na kilometa 5,136.55, kilometa 20,182.79 na kilometa 10,096.41 mtawalia mwaka 2024 (**Jedwali Na. 11.1**). Upungufu wa kilometa zilizofanyiwa tathmini ulitokana na baadhi ya barabara zilizokuwa kwenye mpango wa tathmini (condition survey) kuingia kwenye hatua za ujenzi na ukarabati wa kimkakati (major rehabilitation/upgrading).

272. Mwaka 2025, barabara kuu zenye kiwango cha lami na changarawe/udongo zilizofanyiwa tathmini zilikuwa na urefu wa kilometa 11,654.37 ikilinganishwa na kilometa 11,612.15 mwaka 2024. Kati ya hizo, kilometa 1,982.29 zilikuwa katika hali mbaya, kilometa 3,858.09 katika hali ya wastani na kilometa 5,813.99 katika hali nzuri mwaka 2025 ikilinganishwa na kilometa 1,739.89, kilometa 3,914.34 na kilometa 5,957.92 mtawalia mwaka 2024. Kupungua kwa barabara zenye hali nzuri kulichangiwa na mvua iliyoharibu miundombinu ya Barabara.

273. Mwaka 2025, kilometa 23,019.13 za barabara za mikoa na zinazounganisha mikoa na wilaya zenye kiwango cha lami na changarawe/udongo zilifanyiwa tathmini ikilinganishwa na kilometa 23,803.6 zilizofanyiwa tathmini mwaka 2024. Kati ya barabara zilizofanyiwa tathmini, kilometa 3,800.19 zilikuwa katika hali mbaya, kilometa 14,598.15

katika hali ya wastani na kilometa 4,620.79 katika hali nzuri mwaka 2025 ikilinganishwa na kilometa 3,996.66 kilometa 14,298.15 na kilometa 4,138.29 mtawalia mwaka 2024.

**Jedwali Na. 11.1: Hali ya Mtandao wa Barabara Zilizofanyiwa Tathmini Mwaka 2025**

| Aina ya Barabara | Nzuri | | Wastani | | Mbaya | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Kilometa** | **%** | **Kilometa** | **%** | **Kilometa** | **%** | **Kilometa** |
| Barabara kuu lami | 5,218.40 | 54.5 | 2,612.43 | 27.3 | 1,740.79 | 18.2 | 9,571.62 |
| Barabara kuu changarawe/udongo | 595.59 | 28.6 | 1,245.66 | 59.8 | 241.5 | 11.6 | 2,082.75 |
| **Jumla Ndogo** | **5,813.99** | **49.9** | **3,858.09** | **33.1** | **1,982.29** | **17.0** | **11,654.37** |
| Barabara za mikoa lami | 847.48 | 33.8 | 1,123.95 | 44.9 | 534.19 | 21.3 | 2,505.62 |
| Barabara za mikoa changarawe/udongo | 3,773.31 | 18.4 | 13,474.20 | 65.7 | 3,266.00 | 15.9 | 20,513.51 |
| **Jumla Ndogo** | **4,620.79** | **20.1** | **14,598.15** | **63.4** | **3,800.19** | **16.5** | **23,019.13** |
| **Jumla Kuu** | **10,434.78** | **30.1** | **18,456.24** | **53.2** | **5,782.48** | **16.7** | **34,673.50** |

**Chanzo:** Wizara ya Ujenzi

274. Mwaka 2025, TANROADS ilifanya matengenezo ya barabara kuu za mikoa zenye urefu wa kilometa 2,623.00 ikilinganishwa na kilometa 885.87 zilizofanyiwa matengenezo mwaka 2024. Hii ilitokana na jitihada za Serikali kuendelea na matengenezo ya barabara zenye hali mbaya. Aidha, madaraja 700 yalifanyiwa matengenezo mwaka 2025 ikilinganishwa na madaraja 1,039.16 yaliyofanyiwa matengenezo mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 32.6. Hii ilitokana na kuimarika kwa miundombinu ya barabara na madaraja kufuatia ujenzi na matengenezo ya miundombinu.

275. Mwaka 2025, mtandao wa barabara unaosimamiwa na TARURA ulikuwa kilometa 144,149.18 ikilinganishwa na kilometa 144,429.77 mwaka 2024. Kupungua kwa mtandao huo kulitokana na baadhi ya barabara kuhamishiwa katika mtandao wa barabara unaosimamiwa na TANROADS. Kati ya hizo, kilometa 41,926.14 zilikuwa katika hali nzuri, kilometa 54,753.17 katika hali ya wastani na kilometa 47,469.87 katika hali mbaya. Hadi Desemba 2025 mtandao wa barabara za wilaya zenye kiwango cha lami ulifikia kilometa 3,806.45, changarawe kilometa 46,589.79 na udongo kilometa 93,752.94 ikilinganishwa na kilometa 3,467.30, kilometa 44,372.21 na kilometa 96,590.27 mtawalia, kipindi kama hicho 2024 (**Jedwali Na. 11.2**).

**Jedwali Na. 11.2: Hali ya Mtandao wa Barabara za Vijijini na Mijini Mwaka 2025**

| Aina ya Barabara | Hali ya Barabara (Kilometa) | | | Jumla (Kilometa) | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| | Nzuri | Wastani | Mbaya | | |
| Barabara za lami | 3,185.75 | 483.77 | 136.93 | 3,806.45 | 2.6 |
| Barabara za changarawe | 21,974.37 | 18,972.47 | 5,642.95 | 46,589.79 | 32.3 |
| Barabara za udongo | 16,766.02 | 35,296.93 | 41,689.99 | 93,752.94 | 65.0 |
| **Jumla** | **41,926.14** | **54,753.17** | **47,469.87** | **144,149.18** | **100.0** |
| Asilimia | 29.1 | 38.0 | 32.9 | 100.0 | |

**Chanzo:** Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini

276. Mwaka 2025, TARURA ilijenga na kukarabati barabara za wilaya zenye urefu wa kilometa 23,105.78 ikilinganishwa na kilometa 30,209.86 zilizojengwa na kukarabatiwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 23.5. Hii ilitokana na ukamilishaji wa miradi ya ujenzi na matengenezo ya barabara iliyokuwa inaendelea katika maeneo mbalimbali nchini. Kati ya hizo, barabara zenye urefu wa kilometa 339.15 zilijengwa kwa kiwango cha lami, kilometa 7,408 kwa kiwango cha changarawe na kilometa 15,358.63 zilifanyiwa ukarabati maalum, ukarabati wa kawaida na matengenezo ya maeneo korofi. Aidha, TARURA ilijenga madaraja 138, makalavati 368, mitaro mikubwa ya maji ya mvua yenye mita za mraba 148,230, na kukarabati madaraja 76 mwaka 2025 ikilinganishwa na ujenzi wa madaraja 83, makalavati 485, mitaro ya maji yenye urefu wa kilometa 100,646.46 na madaraja 37 yaliyokarabatiwa mwaka 2024.

**Vivuko na Magari**

277. Mwaka 2025, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania - TEMESA uliendelea kusimamia vivuko 32 kama ilivyokuwa mwaka 2024. Katika kipindi hicho, abiria 27,078,009, magari 522,794 na mizigo tani 474.65 ilivushwa ikilinganishwa na abiria 26,240,229, magari 403,265 na mizigo tani 207.21 iliyovushwa mwaka 2024. Ongezeko la abiria, magari na mizigo iliyovushwa lilitokana na kukua kwa shughuli za kiuchumi na kijamii. Kwa upande mwingine, TEMESA ilitengeneza magari 24,769 mwaka 2025 ikilinganishwa na magari 25,095 yaliyotengenezwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 1.3. Hii ilitokana na baadhi ya taasisi kupunguza idadi ya magari kwa ajili ya matengenezo kufuatia kuanza kutumika kwa mfumo wa malipo kabla ya matengenezo.

**Mfuko wa Barabara**

278. Mwaka 2025, Bodi ya Mfuko wa Barabara ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 1,258.44 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,186.94 zilizokusanywa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 6.0. Hii ilichangiwa na maboresho ya bandari ya Dar es salaam na Tanga yaliyowezesha ongezeko la idadi ya magari yanayoingia nchini kwenda nchi za jirani pamoja na usafirishaji wa mizigo kwenda katika nchi hizo na hivyo kuongeza makusanyo ya ushuru

**Nyumba na Majengo ya Serikali**

279. Mwaka 2025, Wakala wa Majengo Tanzania - TBA uliendelea kusanifu na kusimamia miradi 150 ya ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali ikilinganishwa na miradi 135 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 11.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya majengo ya ofisi na nyumba kwa washitiri. Aidha, TBA ilikarabati nyumba na majengo 159 mwaka 2025 ikilinganishwa na nyumba na majengo 108 yaliyokarabatiwa mwaka 2024. Kwa upande mwingine, TBA ilikusanya shilingi billioni 10.7 kutokana na upangishaji wa majengo ya Serikali kwa ajili ya biashara na makazi mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi billioni 8.8 zilizokusanywa mwaka 2024.

**Usajili wa Makandarasi**

280. Mwaka 2025, Bodi ya Usajili wa Makandarasi - CRB ilisajili makandarasi 1,643 ikilinganishwa na makandarasi 1,812 waliosajiliwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 9.3. Hii ilitokana na kupungua kwa maombi ya usajili wa makandarasi, kufutwa kwa makandarasi wa kudumu walioshindwa kukidhi matakwa ya usajili na kumalizika kwa usajili wa kandarasi za muda. Aidha, Bodi ilisajili miradi 5,277 ya ujenzi mwaka 2025 ikilinganishwa na miradi 4,691 iliyosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 12.5. Hii ilitokana na matumizi ya mfumo wa kidijitali uliorahisisha usajili wa miradi.

281. Mwaka 2025, CRB ilikagua miradi 2,903 ikilinganishwa na miradi 3,581 iliyokaguliwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 18.9. Kati ya hiyo, miradi 1,746 ilikidhi vigezo na miradi 1,157 haikukidhi vigezo. Miradi isiyokidhi vigezo ilitokana na kutekelezwa na wahandisi wasiosajiliwa, miradi kutokusajiliwa, kutokuweka bango la mradi, kutokuzingatia sheria ya usalama wa wafanyakazi na makandarasi kutekeleza miradi isiyoendana na viwango vyao. Aidha, CRB ilipeleka mahakamani mashauri 81 mwaka 2025 ikilinganishwa na mashauri 68 mwaka 2024.

**Usajili wa Wahandisi**

282. Mwaka 2025, Bodi ya Usajili wa Wahandisi - ERB ilisajili wahandisi 3,501 wa fani mbalimbali ikilinganishwa na wahandisi 3,636 waliosajiliwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 3.7. Kati ya hao, wahandisi 3,378, sawa na asilimia 96.5 walikuwa watanzania na wahandisi 123 walitoka nje ya nchi. Aidha, ERB ilisajili mafundi sanifu 407 mwaka 2025 ikilinganishwa na mafundi sanifu 480 waliosajiliwa mwaka 2024.

283. Hadi Desemba 2025, kampuni za ushauri zilizosajiliwa na ERB zilifikia 468 kutoka kampuni 443 zilizosajiliwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, ERB ilisajili wahandisi washauri 61 mwaka 2025 ikilinganishwa na wahandisi washauri 18 waliosajiliwa mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kampuni za ushauri za ndani zilizoshiriki katika shughuli za ujenzi. Kati ya hao, wahandisi washauri 42 walikuwa watanzania na wahandisi washauri 19 walitoka nje ya nchi. Usajili uliofanyika uliwezesha wahandisi washauri

waliosajiliwa kufikia 738 mwaka 2025 kutoka wahandisi washauri 677 mwaka 2024. Hadi Desemba 2025, maabara za vifaa vya ujenzi na uhandisi zilizosajiliwa zilifikia 55 kutoka maabara 53 kipindi kama hicho mwaka 2024.

284. Mwaka 2025, wahandisi 1,789 walipata mafunzo ikilinganishwa na wahandisi 1,722 waliopata mafunzo mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 3.9. Kati ya hao, wahandisi 642 walihitimu na kusajiliwa mwaka 2025 ikilinganishwa na wahandisi 158 waliosajiliwa mwaka 2024. Kwa upande mwingine, ERB ilisajili miradi 1,742 ya ujenzi mwaka 2025 ikilinganishwa na miradi 1,509 iliyosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 15.4. Hii ilichangiwa na matumizi ya mfumo wa kidijitali katika usajili wa miradi. Aidha, ERB ilikagua miradi 694 mwaka 2025 ikilinganishwa na miradi 330 iliyokaguliwa mwaka 2024. Kati ya hiyo, miradi 179 ilibainika kuwa na upungufu ambapo miradi 78 haikusajiliwa na miradi 101 haikuhusisha huduma ya wahandisi washauri wanaohusika na umeme na mitambo.

**Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**

285. Mwaka 2025, Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi - AQRB ilisajili wataalamu 224 ikilinganishwa na wataalamu 174 waliosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 28.7. Hii ilitokana na matumizi ya mfumo wa kidijitali katika usajili wa wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi.

286. Hadi Desemba 2025, wataalamu wa ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi waliosajiliwa walifikia 1,804 kutoka wataalamu 1,616 waliokuwa wamesajiliwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Kati ya hao, watalaamu 1,782 walikuwa watanzania na wataalamu 22 kutoka nje ya nchi. Aidha, wahitimu 289 walishiriki mafunzo kwa vitendo katika fani za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi mwaka 2025 ikilinganishwa na wahitimu 245 walioshiriki mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 18.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa miradi ya ujenzi kulikowezesha upatikanaji wa fursa za mafunzo kwa vitendo.

287. Mwaka 2025, AQRB ilisajili kampuni 43 za ushauri wa ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi ikilinganishwa na kampuni 36 zilizosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 19.4. Hii ilitokana na ongezeko la miradi ya ujenzi na matumizi ya mfumo wa kidijitali katika usajili wa kampuni za ushauri elekezi. Hadi Desemba 2025, kampuni zilizosajiliwa zilifikia 509 kutoka kampuni 475 zilizokuwa zimesajiliwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Kati ya hizo, kampuni 503 zilikuwa za watanzania na kampuni sita (6) kutoka nje ya nchi.

288. Mwaka 2025, AQRB ilisajili miradi 1,819 ya ujenzi wa majengo ikilinganishwa na miradi 1,617 iliyosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 12.5. Hii ilitokana na

ukaguzi wa miradi pamoja na udhibiti wa waendelezaji wa majengo kwa kuzingatia matakwa ya kisheria. Aidha, AQRB ilikagua miradi 5,949 ya ujenzi wa majengo mwaka 2025 ikilinganishwa na miradi 5,153 iliyokaguliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 15.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya wakaguzi nchini. Kati ya miradi hiyo, miradi 4,964 ilikidhi vigezo, sawa na asilimia 83.4 na miradi 985 haikukidhi vigezo kwa mujibu wa Sheria Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, Sura ya 269.

**Baraza la Taifa la Ujenzi**

289. Mwaka 2025, Baraza la Taifa la Ujenzi - NCC lilitoa ushauri wa kiufundi kwa wadau wanne (4) wa sekta ya ujenzi ikilinganishwa na wadau sita (6) waliopewa ushauri wa kiufundi mwaka 2024. Aidha, NCC ilisuluhisha migogoro 371 mwaka 2025 ikilinganishwa na migogoro 277 iliyosuluhishwa mwaka 2024. Kati ya hiyo, migogoro saba (7) ilifungwa baada ya kupata usuluhishi mwaka 2025 ikilinganishwa na migogoro 15 iliyofungwa mwaka 2024. Kwa upande mwingine, NCC iliendesha kozi mbili (2) kwa wadau wa sekta ya ujenzi mwaka 2025 ikilinganishwa na kozi tatu (3) zilizoendeshwa mwaka 2024.

**Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi**

290. Mwaka 2025, Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi - ICoT ilitoa mafunzo ya stashahada kwa wanafunzi 309 ikilinganishwa na wanafunzi 271 waliopatiwa mafunzo mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 14.0. Aidha, ICoT ilitoa mafunzo kwa wanafunzi 445 wa elimu ya ufundi stadi mwaka 2025 ikilinganishwa na wanafunzi 432 waliopata mafunzo mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 3.0.

291. Mwaka 2025, ICoT ilihamasisha matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi kwa wadau 286 ikilinganishwa na wadau 270 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 5.9. Hii ilichangiwa na uhitaji wa teknolojia stahiki ya nguvu kazi nchini. Katika kipindi hicho, ICoT ilitoa mafunzo kwa washiriki 133 wa vikundi vya wanawake na vijana ikilinganishwa na washiriki 24 waliopewa mafunzo mwaka 2024.

## MAENDELEO YA ARDHI

### Usajili wa Hatimiliki, Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na Nyaraka za Kisheria

292. Mwaka 2025, hatimiliki na nyaraka za kisheria zilizosajiliwa zilikuwa 233,031 ikilinganishwa na hatimiliki na nyaraka 224,691 zilizosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 3.7. Hati za hakimiliki za kimila 87,887 zilitolewa kwa wananchi mwaka 2025 ikilinganishwa na hati za hakimiliki 87,110 zilizotolewa mwaka 2024 (**Jedwali Na. 11.3**). Hii ilitokana na kuongezeka kwa viwanja na mashamba yaliyopimwa kufuatia kuendelea kutekelezwa kwa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi; kuimarika kwa kliniki za ardhi; na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa kuwa na hatimiliki na nyaraka za kisheria zilizosajiliwa. Aidha, vyeti 225 vya ardhi za vijiji vilitolewa ikilinganishwa na vyeti 232 vilivyotolewa mwaka 2024.

**Jedwali Na. 11.3: Usajili wa Hatimiliki za Ardhi na Nyaraka za Kisheria, Mwaka 2021 - 2025**

| Hati na Nyaraka Zilizosajiliwa | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| **A: Hati Zilizosajiliwa** | | | | | |
| Hati za kumiliki ardhi zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura ya 334 | 61,527 | 83,195 | 90,408 | 101,262 | 98,515 |
| Hati za Sehemu ya Jengo chini ya Sheria ya Usajili wa Hati za Sehemu ya Jengo (Unit Title Act No.17/2008). | 232 | 380 | 294 | 351 | 918 |
| **Jumla Hatimiliki** | **61,759** | **83,575** | **90,702** | **101,613** | **99,433** |
| B: Miamala na Nyaraka za Kisheria Zilizosajiliwa Miamala iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura ya 334 | 39,252 | 51,413 | 57,395 | 64,624 | 71,976 |
| Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka, Sura ya 117 | 36,354 | 42,112 | 44,655 | 55,954 | 59,051 |
| Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali Zinazohamishika, Sura ya 210 | 4,265 | 5,972 | 7,566 | 2,500 | 2571 |
| **Jumla Nyaraka za Kisheria** | **79,871** | **99,497** | **109,616** | **123,078** | **133,598** |
| **Jumla Kuu: Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria** | **141,630** | **183,072** | **200,318** | **224,691** | **233,031** |

**Chanzo**: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Uthamini wa Mali na Upimaji wa Viwanja na Mashamba**

293. Mwaka 2025, taarifa 52,361 za uthamini wa kawaida na fidia ziliidhinishwa ikilinganishwa na taarifa 60,449 zilizoidhinishwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 13.4. Hii ilitokana na kupungua kwa mahitaji ya fidia katika miradi ya kimkakati na miamala ya ardhi, hususan katika maeneo ya uhamisho wa milki, uhuishaji wa milki, mikopo, na uthamini kwa ajili ya mizania ya kimahesabu.

294. Mwaka 2025, viwanja 272,540 na mashamba 417 yalipimwa katika maeneo mbalimbali nchini ikilinganishwa na viwanja 194,209 na mashamba 7,170 yaliyipimwa mwaka 2024 (**Jedwali Na. 11.4**). Kupungua kwa mashamba yaliyopimwa kulitokana na kukamilika kwa utekelezaji wa mradi katika maeneo ya Msomera (Handeni), Sauni (Kilindi) na Kitwai (Simanjiro).

**Jedwali Na. 11.4: Viwanja na Mashamba Yaliyoidhinishwa, Mwaka 2024 - 2025**

| Na. | Mikoa | 2024 | | 2025 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Viwanja | Mashamba | Viwanja | Mashamba |
| 1 | Arusha | 2,113 | 21 | 4,148 | - |
| 2 | Dar es Salaam | 27,289 | - | 43,230 | - |
| 3 | Dodoma | 29,434 | 162 | 8,528 | - |
| 4 | Geita | 6,105 | - | 12,846 | - |
| 5 | Iringa | 12,114 | 26 | 26,988 | 18 |
| 6 | Kagera | - | - | 5,558 | 94 |
| 7 | Katavi | 4,927 | 13 | 3,688 | 21 |
| 8 | Kigoma | 13,661 | 105 | 5,056 | 60 |
| 9 | Kilimanjaro | 7,688 | 21 | 3,008 | 45 |
| 10 | Lindi | 6,213 | 18 | 8,718 | 7 |
| 11 | Manyara | 5,377 | 53 | 3,098 | 4 |
| 12 | Mara | 5,946 | 10 | 2,606 | 12 |
| 13 | Mbeya | 8,486 | 25 | 24,794 | - |
| 14 | Morogoro | 10,252 | 40 | 8,992 | 40 |
| 15 | Mtwara | 2,200 | 6 | 2,496 | 3 |
| 16 | Mwanza | 14,428 | - | 1,320 | - |
| 17 | Njombe | - | - | 8,272 | - |
| 18 | Pwani | - | - | 44,072 | 34 |
| 19 | Rukwa | - | - | 3,244 | 14 |
| 20 | Ruvuma | 5,615 | 13 | 11,952 | 4 |
| 21 | Shinyanga | 3,445 | - | 4,150 | 10 |
| 22 | Simiyu | 3,301 | 2 | 1,790 | 6 |
| 23 | Singida | 11,328 | 57 | 13,618 | 33 |
| 24 | Songwe | 4,281 | 4 | 8,974 | 12 |
| 25 | Tabora | - | - | 4,752 | - |
| 26 | Tanga | 10,006 | 6,594 | 6,642 | - |
| **Jumla** | | **194,209** | **7,170** | **272,540** | **417** |

**Chanzo**: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

## Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji

295. Mwaka 2025, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 527 iliandaliwa katika wilaya 34 ikilinganishwa na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 562 vilivyoandaliwa katika wilaya 27 mwaka 2024. Hivyo, idadi ya vijiji vilivyoandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi ilifikia 4,801 Desemba 2025 kutoka vijiji 4,274 kipindi kama hicho mwaka 2024 (**Jedwali Na. 11.5**).

**Jedwali Na. 11.5: Vijiji Vilivyoandaliwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Mwaka 2025**

| Na. | Mkoa | Halmashauri ya Wilaya | Vijiji | Idadi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Dodoma | Bahi | Chikopelo, Nondwa, Chidoli, Mkakatika, Mnkhola, Mindola, Chonde, Bankolo, Lamaiti, Maganga, Chiguluka, Ikumbulu, Chali Isanga, Chali Makulu, Ilindi, Nkhome, Mapanga, Chifutuka, Chali Igonndo na Zejele. | 20 |
| | | Mpwapwa | Bumila, Makutupa, Tambi, Mbori, Nana, Nduga, Mwenzele, Muungano, Chinyang'huku, Chamsisili, Chibwegere, Chinoje, Msangambuya, Chaludewa, Mlembule na Nyabu. | 16 |
| 2 | Iringa | Kilolo | Madege, Idete, Isanga, Magome, Mbawi, Idegenda, Ndengisivili, Ilutila, Lulindi, Kising'a, Kidumka, Udekwa, Ifuwa, Ukwega, Wotalisoli, Makungu, Iwiungi, Vitono, Uhambingeto, Ibumu, Kilumbwa, Idasi, Ng'ingula, Nyawegete, Masisiwe na Lyasa. | 26 |
| 3 | Tanga | Kilindi | Mzinga, Michungwani, Kigwama, Kilindi, Kwedigole, Mswaki, Kwadudu, Mafuleta, Balang'a, Tuliani Mswaki, Muungano, Mabalanga, Kileguru, Mzunguwasala, Kimembe, Kwamazuma na Vyadigwa. | 17 |
| | | Lushoto | Lunguza, Tewe, Mng'aro, Mazinde, Kifurio, Kivingo, Kiwanja, Kibandai, Kwemkazu, Kwemshwa, Langoni A, Langoni B, Mkundi Mberu, Mkundi Mtae na Mtii. | 15 |
| | | Korogwe | Kasiga, Kwenangu, Chekelei, Magila, Goha, Magila Gereza, Nanyogie, Mkalamo, Tabora, Kweisewa, Maurui Rutuba, Madumu, Madala, Mpasilasi, Mafuleta na Mbagai. | 16 |
| 4 | Geita | Mbogwe | Nyikonga, Ikunguigazi, Mwigilo, Ibambula, Bugalagala, Isebya, Mgaya, Isungambula, Kasaka, Budoda, Ng'homolwa, Nyanhwiga, Maguta, Nhungwiza, Mpakali, Nanda, Busambilo, Nsango, Nyashimba, Kabanga na Mtakuja. | 21 |
| | | Bukombe | Ikuzi, Nasiluluma, Namalandula, Mjimwema, Kazilamuyaye, Ilyamchele, Shilabela, Kabagole, Kasozi, Nakayenze, Nalusunguti, Nampangwe, Msangila, Namsega, Lulamba na Bulumbaga. | 16 |
| | | Nyang'hwale | Lyulu, Isonda, Mimbili, Igeka, Nyugwa, Kijinga, Nyang'holongo, Nyangalamila na Nundu. | 9 |
| 5 | Mbeya | Mbarali | Azimio Mswiswi, Ipwani, Mhwela, Wimba Mahango, Nyakazombe, Nyakadete, Mapogoro, Iberege na Limseni. | 9 |
| 6 | Pwani | Kibiti | Mkupuka, Machipi, Mlanzi, Nyanjati, Mahege, Hanga, Tomoni, Mangwi, Kivinja B Ruaruke A, Kikale na Mchungu. | 12 |
| 7 | Kilimanjaro | Rombo | Mfuruwashe, Kidondoni, Mamsera Chini, Chala, Ngoyoni, Urauri, Nesae, Kahe, Ture na Mengeni Chini. | 10 |
| 8 | Mwanza | Ukerewe | Namagondo, Busunda, Igongo, Muhande, Busiri, Bwasa, Mkasika, Chankamba, Kaseni, Buguza, Kigara, Buzegwe, Busagami, Mahande, Chamuhunda na Mibungo. | 16 |
| | | Magu | Mwamibanga, Matale, Ng'watelesha, Sagani, Nyashimba, Buhumbi, Shilingwa, Nyashoshi, Nyamahanga, Misambo, Salong'we, Mwamabanza, Mwalinha, Kigangama, Inolelo na Malilika. | 16 |

| Na. | Mkoa | Halmashauri ya Wilaya | Vijiji | Idadi |
|---|---|---|---|---|
| | | Sengerema | Ilekanilo, Mayuya, Busulwangiri, Mami, Lubanda, Nyamahona, Lukumbi, Kalangalala, Sogoso, Butonga, Igulumuki, Kanyerere, Ikoni, Ijinga, Buzilasoga na Nyanzumula. | 16 |
| 9 | Shinyanga | Ushetu | Ilomelo, Ulowa, Ibambala, Mkwangulwa, Itobola, Nonwe, Kidanha, Manungu, Idahin'ha, Lusonzo, Butibu, Mwadui, Iponyanholo, Isanga, Nyankende na Nyarwerwe. | 16 |
| | | Kishapu | Ng’wang’holo, Nyenze, Buchambi, Buganika, Idukilo, Igumangobo, Sanjo, Bulima, Mwadui Lohumbo, Wizunza, Masagala, Ikonongo, Mpumbula, Bupigi, Wela na Mayanji. | 16 |
| 10 | Singida | Manyoni | Itetema, Chidamsulu, Winamila, Mpola, Nkonko, Isseke, Igwamadete, Kasanii, Ilucha, Msemembo, Makuru, Hika, Magasai, Kitalalo, Mvumi na Ilaloo. | 16 |
| | | Ikungi | Kinyamwandyo, Nkuhi, Tumaini, Munkinya, Mkungua Kihendo, Mnane, Nkundi, Matare, Mtunduru, Masweya, Kipunda , Nkhoiree, Chungu, Ihanja, Kintandaa na Msungua. | 16 |
| | | Iramba | Mahola, Ndulungu, Mwanduighembe, Kipuma, Tyegelo, Kidaru, Ndurumo, Nsunsu, Masimba, Mlandala, Ujungu, Mtoa, Msai, Msansao, Kibigiri na Wembere. | 16 |
| 11 | Katavi | Mpimbwe | Mkwajuni, Chamalendi, Ikuba, Kashishi, Ilalangulu, Mirumba, Msadya, Nyambwe, Mbede, Minyoso, Mwamatiga, Luchima, Mamba A, Kilida, Mamba B, Kanindi, Kabunde na Ukingwaminzi. | 18 |
| 12 | Rukwa | Kalambo | Utengule, Kalembe, Mzungwa, Tunyi, Ilonga, Kasusu, Mkombo, Legezamwendo, Mosi, Mtula, Kiundinamema, Kantalemwa, Jengeni, Madibila, Luse na Safu. | 16 |
| 13 | Manyara | Mbulu | Murkuchida, Endamilay, Endalat na Yaeda Chini. | 4 |
| 14 | Kagera | Kyerwa | Masheshe | 1 |
| 15 | Morogoro | Gairo | Lukando, Mamvisi, Kumbulu, Chanjale, Chingholwe, Chagongwe, Mkobwe, Lufikiri, Nongwe, Lukinga, Kinyolisi, Italagwe, Idibo, Ikwamba, Masenge na Ihenje. | 16 |
| 16 | Lindi | Ruangwa | Mmawa, Mpara, Mitope, Mtimbo Ruangwa, Mpumbe, Mchenganyumba, Luchelegwa, Mtawilile, Chinokole, Mabangala, Makanjiro, Mandarawe, Machinyimba, Nangurugai, Liugulu na Ng’imbwa. | 16 |
| | | Mtama | Madangwa, Njonjo, Pangatena, Hingawali, Nachunyu, Mtegu, Kilimani, Sudi, Mmumbu, Navanga. | 10 |
| 17 | Mtwara | Mtwara | Mbuo, Mnyundo, Mwatehi, Changalawe, Ndumbwe, Utende,Nanyani, Lyowa, Mtendachi, Mayaya, Mitambo, Mngoji, Mnuyo, Msimbati, Mtandi, Ruvula, Mnaida,Tangazo, Kilambo, Magomeni, Kihimika, Kitunguli, Mahurunga, Kivava, Libobe, Libobe B, Unguja, Namuhi, Mnyija, Ming’wena, Lipwidi na Mtama. | 32 |
| | | Masasi | Nangomwa, Mwitika, Maparawe, Mkowo, Chikoropola, Mkalivata, Mkachima, Mapili, Rahaleo, Mnavira, Manyuli, Geuza, Liurungu, Utimbe, Sindano na Lichehe. | 16 |

| Na. | Mkoa | Halmashauri ya Wilaya | Vijiji | Idadi |
|---|---|---|---|---|
| | | Tandahimba | Bandari, Mpunda, Ngongo, Mihambwe, Ruvuma, Mkaha, Chikongo, Dinyeke, Naputa Sokoni, Naputa Shuleni ,Chiumo, Kunandundu, Maundo, Namahonga, Pachani na Lipalwe II. | 16 |
| | | Nanyumbu | Mbangala Mbuyuni, Marumba, Makanya, Lukula, Chungu, Lukwika, Chimika, Mpombe, Mchenjeuka na Lumesule. | 10 |
| 18 | Tabora | Igunga | Ngulu, Mwasung'ho, Mwanyalali, Bulenya, Mwabubele, Mwamloli, Mwakwangu, Mwagala, Ibole, Kalangale, Mibuyumiwili, Itunduru, Itale, Mwakipanga, Imalanguzu na Mwamakona. | 16 |
| | | Sikonge | Kabanga, Songambele, Kiloleli, Kanyamsenga, Mtakuja, Kipanga, Lembeli, Mibono Mipya, Mole Mlimani, Mole Kiloleni, Usesula, Majengo, Usunga, Mwanamkata, Urafiki, Kipanga Mlimani, Chabutwa, Kikungu, Mkolye, Isunda, Mpombwe, Ibaya, Kasandalala, Wankolongo na Mitowo. | 25 |
| | | Nzega | Mogwa, Kilino, Kidete, Uduka, Kabanga, Isagenhe, Mbutu, Idubula, Kadoke, Kakulungu, Nkindu, Kishili, Milambo Itobo, Ikindwa, Nawa na Chaming'hwa. | 16 |
| **Jumla** | | | | **527** |

**Chanzo**: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi**

296. Mwaka 2025, migogoro ya ardhi 4,692 ilitatuliwa kwa njia ya kiutawala ikilinganishwa na migogoro 5,464 iliyotatuliwa mwaka 2024. Aidha, migogoro ya mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 121 ilitatuliwa katika halmashauri za wilaya 11 mwaka 2025 ikilinganishwa na migogoro ya vijiji 242 katika halmashauri za wilaya 15 mwaka 2024. Kupungua kwa migogoro kulitokana na kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi pamoja na utoaji wa elimu kuhusu sera, sheria na taratibu za upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi.

297. Mwaka 2025, mashauri 28,975 yalishughulikiwa kisheria katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ikilinganishwa na mashauri 30,545 yaliyoshughilikiwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 5.1. Kati ya hayo, mashauri 18,021 yalitolewa uamuzi mwaka 2025 ikilinganishwa na mashauri 15,949 yaliyoamuliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 13.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mabaraza yaliyotoa huduma na kufikia 117 mwaka 2025 kutoka mabaraza 112 yaliyotoa huduma mwaka 2024.

**Urasimishaji wa Makazi Yasiyopangwa**

298. Mwaka 2025, Serikali iliandaa na kuidhinisha michoro ya urasimishaji makazi 3,634 ikilinganishwa na michoro 2,985 iliyoandaliwa na kuidhinishwa mwaka 2024. Katika kipindi hicho, makazi 355,004 yasiyopangwa yalirasimishwa ikilinganishwa na makazi 297,550 yaliyorasimishwa mwaka 2024. Idadi ya makazi yaliyorasimishwa iliongezeka

kutokana na ushiriki wa wananchi katika utekelezaji wa miradi shirikishi ya urasimishaji makazi.

**Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Biashara**

299. Mwaka 2025, Shirika la Nyumba la Taifa - NHC lilikamilisha ujenzi wa nyumba 1,072 ikilinganishwa na nyumba 147 zilizokamilika mwaka 2024. Ongezeko la nyumba zilizokamilika lilitokana na kukamilika kwa ujenzi wa nyumba zilizokuwa katika hatua mbalimbali za ujenzi. Kati ya nyumba zilizokamilika, nyumba 228 zilikuwa za gharama nafuu na nyumba 844 za bei ya kati na juu. Katika kipindi hicho, Kampuni ya Nyumba kwa Watumishi - WHI ilikamilisha ujenzi wa nyumba 54 za gharama nafuu katika Halmashauri za Iramba (nyumba 9), Mpwapwa (6), Songea Vijijini (12), Lindi Vijijini (6), Chalinze (9) na Manispaa ya Dodoma (12) ikilinganishwa na jumla ya nyumba 30 zilizokamilika mwaka 2024.

## SURA YA 12

## UCHUKUZI NA UHIFADHI MIZIGO

### Usafiri wa Barabara

300. Mwaka 2025, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini - LATRA ilitoa leseni 376,903 za usafirishaji kwa vyombo vya moto vilivyosajiliwa kutoa huduma ya usafirishaji kibiashara ikilinganishwa na leseni 314,221 zilizotolewa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 19.9 (**Jedwali Na. 12.1**). Hii ilichangiwa na kuendelea kukua kwa shughuli za biashara, kuongezeka kwa wawekezaji wapya pamoja na juhudi zinazoendelea kutekelezwa na Serikali kupitia LATRA ikiwemo kutoa elimu kwa umma, kuongeza idadi ya watumishi, kuimarisha na kufanya kaguzi mara kwa mara, na kufungua ofisi katika mikoa yote nchini na katika wilaya za kimkakati ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

**Jedwali Na. 12.1: Leseni za Usafirishaji Zilizotolewa, Mwaka 2021 - 2025**

| Kundi la Leseni | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mabasi ya abiria | 44,517 | 50,452 | 51,455 | 49,744 | 40,050 | -19.5 |
| Magari ya mizigo | 133,428 | 155,456 | 184,310 | 201,388 | 217,392 | 7.9 |
| Bajaji/Pikipiki | 36,984 | 53,817 | 64,579 | 63,089 | 119,461 | 89.4 |
| **Jumla** | **214,929** | **259,725** | **300,344** | **314,221** | **376,903** | **19.9** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini

301. Mwaka 2025, ajali zilizotokana na vyombo vya usafirishaji abiria na mizigo kwa njia ya barabara zilikuwa 829 ikilinganishwa na ajali 940 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 11.8. Kati ya hizo, ajali za barabarani zilizosababishwa na bajaji/pikipiki zilikuwa 322 mwaka 2025 ikilinganishwa na ajali 383 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 15.9. Upungufu wa ajali katika vyombo vya usafirishaji wa abiria na mizigo ulitokana na kuendelea na kaguzi za mara kwa mara barabarani, madereva kuzingatia sheria, matumizi ya mfumo wa kufuatilia mwenendo wa mabasi ya masafa marefu pamoja na elimu iliyotolewa kwa wadau wa vyombo vya usafiri barabarani. **Jedwali Na. 12.2** linaonesha mwenendo wa ajali za barabarani.

**Jedwali Na. 12.2: Mwenendo wa Ajali za Barabarani, Mwaka 2021 - 2025**

| Aina ya Vyombo | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mabasi ya abiria | 365 | 357 | 335 | 303 | 270 | -10.9 |
| Magari ya Mizigo | 224 | 268 | 300 | 254 | 237 | -6.7 |
| Bajaji/Pikipiki | 463 | 780 | 374 | 383 | 322 | -15.9 |
| **Jumla** | **1,052** | **1,405** | **1,009** | **940** | **829** | **-11.8** |

**Chanzo:** Jeshi la Polisi Tanzania

**Usafiri wa Reli**

302. Mwaka 2025, Shirika la Reli Tanzania - TRC lilisafirisha shehena ya mizigo tani 271,481 kwa umbali wa kilometa 208,858,478 kupitia *Meter Gauge Railway* (MGR) ikilinganishwa na tani 247,173 kwa umbali wa kilometa 251,316,724 zilizosafirishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la mizigo iliyosafirishwa la asilimia 9.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa vitendea kazi kufuatia ukarabati na kuanza kutoa huduma kwa mabehewa ya mizigo 369, vichwa vya treni tisa (9), na ununuzi wa mabehewa mapya 50. Kwa upande mwingine TRC ilisafirisha abiria 505,268 wa masafa marefu kwa umbali wa kilometa 376,115,549 kupitia MGR mwaka 2025 ikilinganishwa na abiria 412,730 waliosafirishwa kwa umbali wa kilometa 302,105,666 mwaka 2024, sawa na ongezeko la abiria la asilimia 22.4. Hii ilitokana na kuanza kutoa huduma kwa mabehewa 39 yaliyokarabatiwa. Aidha, TRC ilisafirisha abiria 2,080,029 kwa umbali wa kilometa 69,914,013 katika Jiji la Dar es Salaam mwaka 2025 ikilinganishwa na abiria 3,068,057 waliosafirishwa kwa umbali wa kilometa 86,648,052 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 32.2 Upungufu huo ulitokana na abiria kushindwa kufika kwa urahisi katika vituo ya kupandia na kushukia kutokana na uwepo wa vizuizi vinavyotokana na mwingiliano wa reli ya SGR na MGR **Jedwali Na. 12.3** linaonesha kiasi cha mizigo na idadi ya abiria waliosafirishwa kupitia treni ya MGR.

**Jedwali Na. 12.3: Abiria na Mzigo Iliyosafirishwa na TRC kupitia MGR, Mwaka 2021 - 2025**

| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mizigo (Tani)** | | | | | | |
| Shehena za mizigo | 370,906 | 418,905 | 382,289 | 247,173 | 271,481 | 9.8 |
| Umbali Km | 366,560,583 | 485,141,823 | 360,780,885 | 251,316,724 | 208,858,478 | -16.9 |
| **Abiria (Idadi)** | | | | | | |
| Masafa Marefu | 417,096 | 466,262 | 489,560 | 412,730 | 505,268 | 22.4 |
| Umbali Km | 316,205,354 | 343,076,014 | 370,748,514 | 302,105,666 | 376,115,549 | 24.5 |
| Abiria wa Mjini | 2,876,199 | 2,668,294 | 2,560,891 | 3,068,057 | 2,080,029 | -32.2 |
| Umbali Km | 80,533,572 | 72,712,232 | 71,704,948 | 86,648,052 | 69,914,013 | -19.3 |

**Chanzo:** Shirika la Reli Tanzania

303. Mwaka 2025, TRC kupitia Reli ya Kisasa kwa Kiwango cha Kimataifa - SGR ilisafirisha abiria 3,294,934 ikilinganishwa na abiria 1,422,116 waliosafirishwa mwaka 2024. Ongezeko la abiria lilitokana na kuendelea kuimarika kwa huduma za usafiri wa abiria pamoja na mwitikio wa wananchi kutumia usafiri wa SGR. Kwa upande mwingine, TRC ilianza kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo kupitia SGR kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma Julai 2025 ambapo tani 52,350 za mizigo zilisafirishwa hadi Desemba 2025. (**Jedwali Na. 12.4).**

**Jedwali Na. 12.4: Abiria na Mizigo Iliyosafirishwa kupitia Treni ya SGR, Mwaka 2024 -2025**

| Mwaka/Mwezi | Jan | Feb | Mach | Apr | Mei | Juni | Julai | Agosti | Sept | Okt | Nov | Des | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Abiria** | | | | | | | | | | | | | |
| 2024r | - | - | - | - | - | 46,591 | 126,918 | 264,123 | 210,917 | 221,351 | 258,851 | 293,415 | **1,422,166** |
| 2025 | 255,191 | 233,368 | 263,025 | 277,953 | 275,684 | 298,419 | 294,466 | 299,890 | 290,677 | 272,043 | 234,686 | 299,532 | **3,294,934** |
| **Mizigo (Tani)** | | | | | | | | | | | | | |
| 2025 | - | - | - | - | - | - | 4,500 | 11,100 | 8,700 | 9,375 | 7,575 | 11,100 | **52,350** |

**Chanzo***:* Shirika la Reli Tanzania

304. Mwaka 2025, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia - TAZARA ilisafirisha tani 159,678 za mizigo ikilinganishwa na tani 235,746 zilizosafirishwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 32.3 (**Jedwali Na. 12.5)**. Hii ilitokana na uchakavu wa miundombinu ya usafirishaji, ikiwemo injini na mabehewa.

**Jedwali Na. 12.5: Shehena ya Mzigo Iliyosafirishwa kupitia TAZARA, Mwaka 2021 - 2025**

| Aina ya Mzigo | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kwenda nje ya nchi | 75,140 | 17,863 | 28,064 | 29,249 | 6,219 | -78.7 |
| Kutoka nje ya nchi | 73,843 | 59,155 | 63,936 | 32,946 | 43,669 | 32.5 |
| Ndani ya TAZARA | 50,146 | 88,891 | 73,973 | 26,012 | 10,631 | -59.1 |
| **Jumla Ndogo** | **199,129** | **165,909** | **165,973** | **88,207** | **60,519** | **-31.4** |
| Kampuni binafsi | 192,952 | 22,873 | 135,067 | 147,539 | 99,159 | -32.8 |
| **Jumla Kuu** | **392,081** | **188,782** | **301,040** | **235,746** | **159,678** | **-32.3** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia

305. Mwaka 2025, TAZARA ilisafirisha abiria 1,041,811 ikilinganishwa na abiria 1,950,953 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 46.6. Hii ilitokana na kusimamishwa kwa huduma ya treni ya mjini kutokana na uchakavu wa miundombinu, ikiwemo injini. Kati ya hao, abiria 255,391 walikuwa wa safari ndefu (Dar es Salaam - Mbeya - Zambia), abiria 205,387 wa treni ya Udzungwa na abiria 581,033 wa treni ya jijini Dar es Salaam (**Jedwali Na. 12.6**).

**Jedwali Na. 12.6: Abiria Waliosafirishwa kupitia TAZARA, Mwaka 2021 - 2025**

| Aina ya Abiria | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Njia ndefu | 432,981 | 514,382 | 534,603 | 367,027 | 255,391 | -30.4 |
| Udzungwa | 406,762 | 375,575 | 359,564 | 211,445 | 205,387 | -2.9 |
| Dar es salaam | 1,872,930 | 1,903,631 | 1,815,937 | 1,372,481 | 581,033 | -57.7 |
| **Jumla** | **2,712,673** | **2,793,588** | **2,710,104** | **1,950,953** | **1,041,811** | **-46.6** |


**Chanzo**: Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia

**Usafiri wa Anga**

306. Mwaka 2025, Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania - TCAA ilisajili ndege 30 ikilinganishwa na ndege 21 zilizosajiliwa mwaka 2024. Ongezeko la usajili wa ndege lilitokana na kuendelea kuimarika kwa biashara ya usafiri wa anga nchini pamoja na juhudi za Serikali katika kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege na mitambo ya kuongozea ndege. Katika kipindi hicho, TCAA ilikagua na kutoa vyeti vya ubora kwa ndege 176 ikilinganishwa na ndege 155 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 13.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya ndege mpya pamoja na ndege zilizokuwa zimesitisha huduma kuanza tena shughuli zake. Hadi Desemba 2025, mashirika 28 ya ndege za kimataifa yalitoa huduma kwa utaratibu wa mikataba ya usafiri wa anga baina ya Tanzania na nchi nyingine (Bilateral Air Service Agreement - BASA) ikilinganishwa na mashirika 30 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Upungufu huo ulitokana na kusitishwa kwa huduma za Ewa Air ya Visiwa vya Mayotte na *Saudi Arabian Airlines* kutokana na tathmini zao za kibiashara.

307. Mwaka 2025, abiria 8,111,107 walisafiri kwa njia ya anga ikilinganishwa na abiria 7,404,408 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 9.5. Hii lilichangiwa na kuongezeka kwa miruko ya ndege na njia mpya, kuanza safari mpya kwa baadhi ya mashirika ya ndege, na kuhuisha safari kwa mashirika yalioacha safari. Kati ya hao, abiria 4,344,322 walisafiri ndani ya nchi na abiria 3,766,785 walisafiri nje ya nchi (**Kielelezo Na. 12.1**).


**Kielelezo Na.12.1: Idadi ya Abiria Waliotumia Usafiri wa Anga, Mwaka 2021 - 2025**




| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kimataifa | 1,489,721 | 2,405,076 | 3,019,289 | 3,361,029 | 3,766,785 |
| Ndani ya nchi | 2,338,236 | 3,313,319 | 3,801,252 | 4,043,379 | 4,344,322 |
| Jumla | 3,827,957 | 5,718,395 | 6,820,541 | 7,404,408 | 8,111,107 |

308. Mwaka 2025, safari za ndege zilikuwa 297,151 ikilinganishwa na safari 277,508 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 7.1 (**Kielelezo Na. 12.2**). Aidha, mizigo iliyosafirishwa ilikuwa tani 44,076.0 mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 42,884.5 [1] zilizosafirishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 2.8. Kuongezeka kwa safari za ndege na mizigo iliyosafirishwa kulitokana na kuimarika kwa biashara ya usafiri wa anga pamoja na ongezeko la idadi ya watalii nchini.

**Kielelezo Na. 12.2: Safari za Ndege, Mwaka 2021 - 2025[2]**




| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kimataifa | 27,026 | 39,610 | 45,158 | 46,460 | 52,196 |
| Ndani ya nchi | 130,776 | 204,626 | 218,674 | 231,048 | 244,955 |
| Jumla | 157,802 | 244,236 | 263,832 | 277,508 | 297,151 |

309. Mwaka 2025, Kampuni ya ndege Tanzania - ATCL ilitoa huduma katika vituo 15 vya ndani ikilinganishwa na vituo 13 mwaka 2024. Vituo hivyo ni Arusha, Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Kigoma, Mbeya, Mpanda, Mtwara, Mwanza, Pemba, Songea, Tabora na Zanzibar. Aidha, ATCL ilitoa huduma katika vituo 16 vya nje ya nchi mwaka 2025 ikilinganishwa na vituo 12 mwaka 2024. Vituo vya nje ya nchi ni: Bujumbura (Burundi), Hahaya (Visiwa vya Comoro), Guangzhou (China), Harare na Victoria Falls (Zimbabwe), Lubumbashi na Kinshasa (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo), Ndola na

[1] Takwimu imefanyiwa mapitio

[2] Takwimu zimefanyiwa mapitio.

Lusaka (Zambia), Mumbai (India), Lagos (Nigeria), Johannesburg na Cape Town (Afrika ya Kusini), Dubai (Umoja wa Falme za Kiarabu), Nairobi (Kenya) na Entebbe (Uganda).

310. Mwaka 2025, ATCL ilisafirisha abiria 1,277,522 ikilinganishwa na abiria 1,163,210 waliosafirishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 9.8. Hii ilichangiwa na juhudi za ATCL kupanua mtandao wa safari nje ya nchi kwa kuongeza idadi ya miruko katika vituo. Aidha, ATCL ilisafirisha tani 5,519.9 za mizigo ndani na nje ya nchi mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 9,364.1 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asimilia 41.1. Upungufu huo ulitokana na changamoto katika uendeshaji wa ndege za mizigo, hususan upatikanaji wa marubani.

311. Mwaka 2025, ATCL ilikuwa na viti-kilometa 2,882,631 ikilinganishwa na viti-kilometa 2,328,228 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 23.8. Aidha, viti-kilometa vilivyotumika vilikuwa 1,715,095 mwaka 2025 ikilinganishwa na viti-kilometa 1,491,220 vilivyotumika mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 15.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya safari za ATCL, hususan kufuatia upanuzi wa mtandao wa huduma katika baadhi ya vituo vya nje ya nchi, ikiwemo Lagos, Victoria Falls, Cape Town na Kinshasa, pamoja na kuimarishwa kwa ratiba za safari. Hata hivyo, kiwango cha matumizi ya viti kilipungua kutoka asilimia 64.0 mwaka 2024 hadi asilimia 59.5 mwaka 2025. Hii iliashiria kuwa ongezeko la uwezo wa kubeba abiria lilikuwa kubwa zaidi kuliko ongezeko halisi la mahitaji ya soko katika kipindi husika.

**Usafiri na Usafirishaji kwa Njia ya Maji**

312. Mwaka 2025, Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania - TASAC lilisajili mawakala 1,453 wa ugomboaji wa shehena ikilinganishwa na mawakala 1,188 waliosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 22.3. Katika kipindi hicho, mawakala wa uwakala wa meli waliopewa leseni walifikia 58 ikilinganishwa na mawakala 56 mwaka 2024. Ongezeko la mawakala lilitokana na mapitio ya kanuni ya uwakala wa meli kwa kuanzisha aina nyingine ya leseni ya uwakala wa meli (Local Shipping Agents License).

313. Mwaka 2025, TASAC ilitoa leseni 40 za wakusanyaji na watawanyaji wa mizigo ikilinganishwa na leseni 46 zilizotolewa mwaka 2024. Kupungua kwa leseni zilizotolewa kulitokana kwa baadhi ya watoa huduma kutohuisha leseni zao kwa wakati baada ya kuisha muda wa leseni. Aidha, leseni za upimaji wa uzito wa makasha zilipungua na kufikia 50 mwaka 2025 kutoka leseni 58 mwaka 2024. Kwa upande mwingine, leseni za bandari kavu zilikuwa 126 mwaka 2025 ikilinganishwa na leseni 96 zilizotolewa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 31.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa maombi ya leseni za bandari kavu, kuhuishwa kwa leseni zilizokuwa zimeisha muda wa matumizi pamoja na kuimarishwa kwa utoaji wa elimu na ufuatiliaji wa leseni. **Jedwali Na. 12.7** linaonesha mwenendo wa utoaji leseni kwa watoa huduma za usafirishaji majini.

**Jedwali Na. 12.7: Leseni Zilizotolewa kwa Watoa Huduma, Mwaka 2021 - 2025**

| Aina ya Leseni | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ugomboaji wa shehena | 947 | 1,129 | 1,143 | 1,188 | 1,453 | 22.3 |
| Uwakala wa meli | 24 | 34 | 41 | 56 | 58 | 3.6 |
| Ukusanyaji wa mizigo | 32 | 33 | 54 | 46 | 40 | -13.0 |
| Upimaji wa makasha | 54 | 47 | 48 | 58 | 50 | -13.8 |
| Bandari kavu | 46 | 69 | 77 | 96 | 126 | 31.3 |

**Chanzo:** Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania

314. Mwaka 2025, vyombo vidogo 9,748 vya usafiri majini vyenye urefu usiozidi mita 24 vilikaguliwa na kupewa leseni ikilinganishwa na vyombo 10,675 vilivyokaguliwa na kupewa leseni mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 8.7. Aidha, TASAC ilisajili vyombo vikubwa 100 vya usafiri majini vyenye urefu wa zaidi ya mita 24 mwaka 2025 ikilinganishwa na vyombo 85 vilivyosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 17.6. Hii ilitokana na wamiliki wa vyombo kuhuisha usajili wa vyombo vyao.

315. Mwaka 2025, shehena iliyohudumiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania - TPA ilikuwa tani milioni 37.1 ikilinganishwa na tani milioni 29.1 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 27.7 **(Jedwali Na. 12.8)**. Hii ilitokana na TPA kuendelea kuboresha miundombinu na huduma za uendeshaji bandarini, kuongezeka kwa idadi ya meli zilizohudumiwa, pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya Bandari ya Dar es Salaam kutokana na kuendelea kujitangaza katika nchi jirani zisizopakana na bahari.

**Jedwali Na. 12.8: Shehena Zilizohudumiwa na TPA (Tani '000), Mwaka 2021 - 2025**

| Bandari | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bandari Kuu za Mwambao** | | | | | | |
| Dar es Salaam | 17,025.0 | 19,870.2 | 22,916.2 | 24,509.4 | 31,810.6 | 29.8 |
| Tanga | 844 | 968.6 | 976.1 | 1,260.1 | 1,712.1 | 35.9 |
| Mtwara | 213 | 1,222.0 | 1,671.1 | 2,379.9 | 2,173.8 | (8.7) |
| **Jumla Ndogo** | **18,082.0** | **22,060.8** | **25,563.4** | **28,149.3** | **35,696.5** | **26.8** |
| **Bandari Ndogo na Bandari za Maziwa Makuu** | | | | | | |
| Kilwa, Lindi, Mafia, Bagamoyo na Pwani | 191 | 207.8 | 229.8 | 377.0 | 494.1 | 31.06 |
| Mwanza | 234 | 283.5 | 267.9 | 194.6 | 246.2 | 26.5 |
| Kigoma | 265 | 313.4 | 286.2 | 318.8 | 653.9 | * |
| Kyela | 11 | 13.7 | 11.6 | 10.4 | 7 | (32.7) |
| **Jumla Ndogo** | **701** | **818.4** | **795.5** | **900.8** | **1,401.2** | **55.6** |
| **Jumla Kuu** | **18,783.0** | **22,879.2** | **26,358.9** | **29,050.2** | **37,097.7** | **27.7** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania
* Badiliko ni zaidi ya asimilia 100

316. Mwaka 2025, Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara zilihudumia makasha 1,082,444 ya urefu wa futi 20 ikilinganishwa na makasha 1,075,555 yaliyohudumiwa mwaka 2024. Kati ya hayo, Bandari ya Dar es Salaam ilihudumia makasha 1,044,145 ikilinganishwa na makasha 1,010,430 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 3.3 (**Jedwali Na. 12.9**). Hii ilitokana na kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi pamoja na idadi na ubora wa vifaa vya kuhudumia meli za makasha.

**Jedwali Na. 12.9: Shehena ya Makasha Yenye Urefu wa Futi 20 Yaliyohudumiwa, Mwaka 2021 - 2025**

| Bandari | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Dar es Salaam** | | | | | | |
| *Terminal 1* | 110,732 | 169,771 | 814,695 | 212,268 | 179,701 | -15.3 |
| *Terminal 2* | 606,169 | 715,707 | 163,954 | 798,162 | 864,444 | 8.3 |
| **Jumla ndogo** | **716,901** | **885,478** | **978,649** | **1,010,430** | **1,044,145** | **3.3** |
| Tanga | 5,817 | 7,712 | 7,299 | 8,735 | 7,754 | -11.2 |
| Mtwara | 90 | 0 | 7,951 | 56,390 | 30,545 | -45.8 |
| **Jumla ndogo** | **5,907** | **7,712** | **15,250** | **65,125** | **38,299** | **-41.2** |
| **Jumla Kuu** | **722,808** | **893,190** | **993,899** | **1,075,555** | **1,082,444** | **0.6** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

317. Mwaka 2025, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ilihudumia abiria 3,966,090 ikilinganishwa na abiria 3,907,224 waliohudumiwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 1.5 (**Jedwali Na. 12.10)**. Hii ilitokana na kuendelea kuimarika kwa usimamizi wa huduma za usafiri majini.

**Jedwali Na. 12.10: Abiria Waliohudumiwa, Mwaka 2021 - 2025**

| Bandari | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 2,303,471 | 2,300,228 | 2,302,998 | 2,420,905 | 2,696,139 | 11.4 |
| Tanga | 49,246 | 98,374 | 26,599 | 62,904 | 86,034 | 36.8 |
| Mwanza | 1,461,900 | 1,394,654 | 1,257,947 | 1,211,112 | 975,971 | -19.4 |
| Kigoma | 43,364 | 168,836 | 206,423 | 197,109 | 187,013 | -5.1 |
| Kyela | 17,209 | 37,565 | 70,173 | 15,194 | 20,933 | 37.8 |
| **Jumla** | **3,875,190** | **3,999,657** | **3,864,140** | **3,907,224** | **3,966,090** | **1.5** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

### Muda wa Meli Kukaa Bandarini

318. Mwaka 2025, muda wa meli kukaa bandarini ulikuwa wastani wa siku 9.6 ikilinganishwa na wastani wa siku 12.3 mwaka 2024. Aidha, muda wa meli kukaa bandarini kwa shehena ya makasha ulipungua kutoka wastani wa siku 12.7 mwaka 2024 hadi siku 7.4 mwaka 2025. Vilevile, muda wa meli kukaa bandarini kwa shehena ya kawaida ulipungua kutoka wastani wa siku 13.7 mwaka 2024 hadi siku 5.2 mwaka 2025 (**Jedwali Na. 12.11**).

Kupungua kwa muda wa meli kukaa bandarini kulitokana na kuongezeka kwa vifaa, kuimarika kwa ujuzi na uwezo kulikochangiwa na ushirikishaji wa sekta binafsi katika uendeshaji wa shughuli za bandari.

**Jedwali Na. 12.11: Muda wa Meli Kukaa Bandarini (Siku), Mwaka 2021 - 2025**

| Kitengo/Meli | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Makasha | 3.8 | 10.4 | 9.0 | 12.7 | 7.4 |
| Shehena ya kawaida | 3.7 | 7.4 | 8.0 | 13.7 | 5.2 |
| Mafuta | 6.5 | 14.3 | 14.7 | 10.4 | 16.1 |
| **Wastani** | **4.7** | **10.7** | **10.6** | **12.3** | **9.6** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania

**Shehena za Nchi Jirani**

319. Mwaka 2025, shehena za nchi jirani zilizopita Bandari za Dar es Salaam na Tanga zilikua tani 14,250,087 ikilinganishwa na tani 9,187,061 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 55.1 (**Jedwali Na. 12.12**). Hii ilitokana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kuendelea kutangaza fursa za bandari kupitia ofisi za masoko katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia, Rwanda, na Burundi pamoja na kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya Bandari na ya usafirishaji (barabara na reli).

**Jedwali Na. 12.12: Shehena za Nchi Jirani (Tani), Mwaka 2021 - 2025**

| Nchi | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Zambia | 1,507,746 | 1,975,793 | 2,311,278 | 2,248,505 | 3,535,678 | 57.2 |
| D.R. Congo | 2,357,867 | 3,379,124 | 3,726,938 | 4,180,902 | 7,239,741 | 73.2 |
| Burundi | 507,017 | 520,714 | 385,975 | 349,591 | 494,698 | 41.5 |
| Rwanda | 1,366,290 | 1,483,175 | 1,677,505 | 1,672,431 | 2,156,298 | 28.9 |
| Malawi | 471,385 | 557,826 | 581,981 | 594,281 | 719,838 | 21.1 |
| Uganda | 138,805 | 192,912 | 113,630 | 60,682 | 47,605 | -21.6 |
| Nyinginezo* | 72,488 | 127,546 | 74,131 | 80,669 | 56,229 | -30.3 |
| **Jumla** | **6,421,598** | **8,237,090** | **8,871,438** | **9,187,061** | **14,250,087** | **55.1** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania
*Msumbiji, Sudani, Kenya, Comoro, Angola na Zimbabwe

**Huduma za Uchukuzi katika Maziwa Makuu**

320. Mwaka 2025, Kampuni ya Meli Tanzania - TASHICO ilisafirisha abiria 134,263 ikilinganishwa na abiria 432,309 waliosafirishwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 68.9. Hii ilitokana na ushindani kutoka kwa meli za abiria za mwendokasi pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya usafiri kwa njia ya barabara. Katika kipindi hicho, TASHICO ilisafirisha tani 83,321.9 za mizigo ikilinganishwa na tani 100,845.0 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 17.4. Hii ilitokana na ushindani kutoka njia mbadala za usafirishaji.

**Kampuni ya Meli ya China na Tanzania**

321. Mwaka 2025, Kampuni ya Meli ya China na Tanzania - SINOTASHIP ilisafirisha tani 621,528 za shehena ikilinganishwa na tani 615,375 zilizosafirishwa mwaka 2024. Aidha, makasha 84,500 yalihudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam mwaka 2025 ikilinganishwa na makasha 81,993 yaliyohudumiwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 3.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa biashara ya uwakala na idadi ya meli zinazoleta na kuondosha mizigo katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

**Huduma za Hali ya Hewa**

322. Mwaka 2025, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania - TMA ilihudumia ndege 59,598 ikilinganishwa na ndege 54,357 zilizohudumiwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 9.6. Aidha, jumla ya meli na boti 129,686 zilihudumiwa mwaka 2025 ikilinganishwa na meli na boti 127,143 zilizohudumiwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 2.0. Vilevile, TMA ilitoa huduma mahsusi kwa sekta za kiuchumi na miradi ya kielelezo kwa wateja 1,543 mwaka 2025 ikilinganishwa na wateja 1,642 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 6.0. Katika kipindi hicho, kiwango cha usahihi wa utabiri kilifikia asilimia 88.6 ikilinganishwa na asilimia 88.2 mwaka 2024 (**Jedwali Na. 12.13**). Hii ilitokana na kuimarika kwa uwezo katika utoaji wa huduma za utabiri wa hali ya hewa kulikochangiwa na kuboreshwa kwa mifumo, mitambo na vifaa vya kisasa vya uchunguzi. Kiwango cha usahihi wa utabiri kiliendelea kuwa juu ya kiwango cha asilimia 70 kinachokubalika kimataifa na Shirika la Hali ya Hewa Duniani.

**Jedwali Na. 12.13: Viashiria vya Ufanisi wa Huduma za Hali ya Hewa, Mwaka 2021 - 2025**

| | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya ndege zilizohudumiwa | 35,511 | 45,891 | 48,516 | 54,357 | 59,598 | 9.6 |
| Idadi ya meli na boti zilizohudumiwa | 31,736 | 66,002 | 131,749 | 127,143 | 129,686 | 2.0 |
| Huduma mahsusi kwa sekta za kiuchumi na miradi ya kielelezo | 623 | 674 | 1,420 | 1,642 | 1,543 | 6.0 |
| **Usahihi wa Utabiri** | **88.3** | **88.5** | **86.4** | **88.2** | **88.6** | **0.5** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

**Jedwali Na. 57: SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA (ATCL)+, MWAKA 2018 - 2025**

| Maelezo | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Tani - Kilometa:** | | | | | | | | |
| Zilizokuwepo | 32,095 | 32,927 | 65,968 | 68,806 | 71,872 | 133,124 | 204,221 | 307,992 |
| Zilizotumika | 17,526 | 18,944 | 33,655 | 38,930 | 48,464 | 81,137 | 127,320 | 185,383 |
| Matumizi (%) | 54.6 | 57.5 | 51.0 | 56.6 | 67.4 | 60.9 | 62.3 | 60.2 |
| **Viti - kilometa:** | | | | | | | | |
| Vilivyokuwepo | 231,943 | 321,771 | 557,216 | 552,682 | 690,408 | 1,227,755 | 2,328,228 | 2,882,631 |
| Vilivyotumika | 158,203 | 220,433 | 347,101 | 417,706 | 552,968 | 788,162 | 1,491,220 | 1,715,095 |
| Matumizi (%) | 68.2 | 68.5 | 62.3 | 75.0 | 80.1 | 64.2 | 64.0 | 59.5 |
| Abiria ++ ('000) | 279 | 627 | 434 | 657 | 929 | 1,066 | 1,163 | 1,278 |
| Mizigo ya ziada (Tani) | 55 | 96 | 86 | 75 | 54 | 0 | 0 | 0 |
| Mizigo mingine (Tani) | 220 | 696 | 438 | 526 | 3,030 | 2,992 | 4,054 | 353 |
| Mizigo ya Posta (Tani) | 119 | 295 | 61 | 21 | 72 | 91 | 158 | 0.2 |

**Chanzo:** Shirika la Ndege Tanzania

+ Zinahusu "scheduled traffic" tu

++ Abiria waliolipa nauli kamili

## SURA YA 13

## MAWASILIANO, HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

### MAWASILIANO

**Huduma za Posta**

323. Mwaka 2025, Shirika la Posta Tanzania lilisafirisha barua 604,152 ndani ya nchi ikilinganishwa na barua 789,299 zilizosafirishwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 23.5. Hii ilitokana na kuendelea kukua kwa matumizi ya njia za kidijitali katika mawasiliano ikiwemo barua pepe na simu za mkononi. Katika kipindi hicho, barua 120,747 zilisafirishwa nje ya nchi ikilinganishwa na barua 150,090 zilizosafirishwa nje ya nchi mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 19.6. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya mashirika ya ndege kutosafirisha barua kwenda baadhi ya nchi ikiwemo Marekani kutokana na mabadiliko ya utaratibu uliokuwa unazitaka kampuni za ndege kukusanya kodi na kuziwasilisha wanapofikisha barua, vifurushi na mizigo ambapo awali gharama hizo zililipwa na wapokeaji baada ya barua kufika katika nchi husika. Katika kukabiliana na ushindani wa kibiashara, Shirika limehamia katika mifumo ya kidijitali ili kurahisisha upatikanaji wa huduma ikiwemo mfumo wa "*Posta Kiganjani*" ambao ni Programu tumizi (App) inayomruhusu mteja kupata huduma za posta kupitia simu ya mkononi, ikiwemo ufuatiliaji wa mzigo (tracking) pamoja na Mfumo wa Ufuatiliaji (Track-and-Trace) ambao umeimarisha mifumo ya kielektroniki inayomfanya mteja ajue mzigo ulipo wakati wowote.

324. Mwaka 2025, vifurushi 20,663 vilisafirishwa ndani ya nchi ikilinganishwa na vifurushi 18,542 vilivyosafirishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 11.4. Hii ilitokana na kuboreshwa kwa huduma kwa wateja, kuongezeka kwa vitendea kazi, ikiwemo magari, bajaji na pikipiki pamoja na kampeni mbalimbali za masoko. Aidha, vifurushi 2,516 vilisafirishwa nje ya nchi mwaka 2025 ikilinganishwa na vifurushi 2,340 vilivyosafirishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 7.5. Hii ilitokana na kuboreshwa kwa huduma za Shirika pamoja na kuhamasisha wateja wakubwa kutuma vifurushi nje ya nchi kupitia Shirika la Posta.

325. Mwaka 2025, rejesta 112,249 zilisafirishwa ndani ya nchi ikilinganishwa na rejesta 89,381 zilizosafirishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 25.6. Hii ilitokana na uhamasishaji wa wateja wakubwa wa Shirika wanaotumia huduma ya rejesta, ikiwemo benki na Taasisi za Serikali. Kwa upande mwingine, rejesta 2,309 zilisafirishwa nje ya nchi mwaka 2025 ikilinganishwa na rejesta 2,915 zilizosafirishwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 20.8. Upungufu huo ulitokana na ongezeko la matumizi ya barua pepe na simu za mkononi katika mawasiliano.

326. Mwaka 2025, Shirika lilituma nyaraka na vipeto 529,957 kwa njia ya haraka nchini ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 499,430 vilivyotumwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 6.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa vitendea kazi, ikiwemo magari, bajaji na pikipiki. Aidha, nyaraka na vipeto 15,903 vilitumwa nje ya nchi kwa njia ya haraka mwaka 2025 ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 15,506 vilivyotumwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 2.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya nchi ambazo Shirika linatoa huduma hasa baada ya kuingia ubia na mashirika ya ndege likiwemo Shirika la Ndege la Ethiopia ambalo liliunganisha Tanzania na mataifa takribani 80 duniani kwa usafirishaji wa haraka wa vifurushi. Vilevile, barua na nyaraka 49,936 zilipokelewa na kusambazwa kwa njia ya huduma ya usambazaji wa barua za haraka ndani ya miji mwaka 2025 ikilinganishwa na barua na nyaraka 46,586 zilizopokelewa na kusambazwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 7.2. Hii iilichangiwa na maboresho yaliyofanyika kwenye Mfumo wa usambazaji wa barua na nyaraka ndani ya Miji (pCum Delivery System) na kampeni mbalimbali za matangazo zilizovutia watumiaji wengi zaidi.

327. Mwaka 2025, miamala ya fedha 15,302 ilifanyika kupitia njia ya Western Union ikilinganishwa na miamala 14,161 iliyofanyika mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 8.1. Hii ilitokana na maboresho ya utoaji wa huduma za kifedha kwenye ofisi za Posta. Aidha, miamala 995 ya fedha ilifanyika kupitia njia ya Money Gram mwaka 2025 ikilinganishwa na miamala 964 mwaka 2024.

**Huduma za Simu**

328. Mwaka 2025, kadi za simu za kiganjani zilifikia 106,823,601 kutoka kadi 86,769,161 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 23.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa maeneo yaliyofikiwa na miundombinu ya mawasiliano pamoja na matumizi ya simu za kiganjani katika utoaji wa huduma mbalimbali. Aidha, kadi za simu za mezani ziliongezeka kwa asilimia 42.5 na kufikia 111,600 mwaka 2025 kutoka kadi za simu za mezani 78,299 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya matumizi ya simu za mezani nyumbani na ofisini pamoja na kuimarishwa kwa miundombinu ya mawasiliano.

329. Mwaka 2025, wastani wa gharama za kupiga simu ndani ya mtandao ulikuwa ni shilingi 27.50 kwa dakika kutoka shillingi 26.00 kwa dakika kwa mwaka 2024. Aidha, wastani wa gharama za kupiga simu nje ya mtandao ulikuwa shilingi 28.50 kwa dakika mwaka 2025 kutoka shilingi 28.00 kwa dakika mwaka 2024. Ongezeko dogo la wastani wa gharama za kupiga simu ndani na nje ya mtandao lilitokana na uwepo wa ushindani katika soko la mawasiliano. Katika kipindi hicho, wastani wa bei za kupiga simu kwenye vifurushi ulikuwa shilingi 5.05 kwa dakika ndani ya mtandao na shilingi 6.15 kwa dakika nje ya mtandao ikilinganishwa na shilingi 4.79 kwa dakika ndani ya mtandao na shilingi 6.27 kwa dakika nje ya mtandao mwaka 2024. Aidha, wastani wa gharama za kupiga simu ndani ya Afrika Mashariki ulikuwa shilingi 342.59 kwa dakika mwaka 2025 ikilinganishwa na

shilingi 597.40 kwa dakika mwaka 2024. Kupungua kwa gharama za kupiga simu ndani ya Afrika Mashariki kulitokana na kuongezeka kwa ushindani kwa watoa huduma za mawasiliano za kimataifa. Vilevile, gharama za kupiga simu kwenda mataifa mengine zilikuwa wastani wa shilingi 2,185.45 kwa dakika mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,016.70 kwa dakika mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 8.4. Hii ilitokana na watoa huduma wa kusafirisha huduma ya mawasiliano ya simu za kimataifa (international carriers), kurekebisha viwango vya kusafirisha simu za kimataifa (International Termination Rates) kwa nchi zilizo nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na kupelekea kuongezeka kwa bei za rejareja ili kudumisha faida endelevu za kiuchumi kwa trafiki ya kimataifa.

**Huduma za Intaneti**

330. Mwaka 2025, kadi za simu zinazotumia intaneti zilifikia milioni 58.1 kutoka kadi za simu milioni 48.0 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 21.0 (**Jedwali Na. 13.1)**. Aidha, matumizi ya intaneti nchini yalikuwa Gigabaiti (GB) milioni 2,731 mwaka 2025 ikilinganishwa na Gigabaiti milioni 1,961 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 39.3. Hii ilitokana na kuendelea kukua kwa huduma mbalimbali zinazotolewa kwa njia ya mtandao wa intaneti nchini.

**Jedwali Na. 13.1: Watumiaji wa Intaneti Nchini, Mwaka 2021 - 2025**

| Aina ya Huduma | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| *Fixed wireless* | 1,034,958 | 6,003 | 8,315 | 83,201 | 275,553 | * |
| *Mobile wireless* | 25,176,367 | 31,100,860 | 35,815,632 | 47,859,272 | 57,691,394 | 20.5 |
| *Fixed wired* | 3,647,434 | 65,681 | 61,645 | 85,754 | 139,317 | 62.5 |
| **Jumla** | **29,858,759** | **31,172,544** | **35,885,592** | **48,028,227** | **58,106,264** | **21.0** |

**Chanzo**: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania
* Badiliko zaidi ya asilimia 100

**Utoaji wa Leseni za Mawasiliano**

331. Mwaka 2025, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilitoa leseni 236 za huduma mbalimbali za mawasiliano ikilinganishwa na leseni 316 zilizotolewa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 25.3 (**Jedwali Na. 13.2)**. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya leseni za watoa huduma kuisha muda wake na kuendelea na mchakato wa kuhuisha leseni hizo kufuatia mabadiliko ya masharti ya utoaji wa leseni yaliyotolewa kupitia mwongozo wa utoaji wa leseni wa mwaka 2024.

**Jedwali Na. 13.2: Leseni Zilizotolewa, Mwaka 2021 - 2025**

| Aina ya Leseni | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Huduma za Mawasiliano Daraja B | 0 | 0 | 0 | 0 | 18 |
| Maudhui ya redio | 13 | 15 | 29 | 29 | 14 |
| Maudhui ya luninga | 9 | 9 | 5 | 1 | 4 |
| Ufungaji na utengenezaji wa vifaa vya mawasiliano vya kieletroniki | 50 | 20 | 65 | 84 | 25 |
| Kuingiza nchini vifaa vya mawasiliano vya kieletroniki | 44 | 45 | 42 | 49 | 38 |
| Kusambaza nchini vifaa vya mawasiliano | 16 | 20 | 25 | 8 | 0 |
| Kuuza vifaa vya mawasiliano vya kieletroniki | 201 | 29 | 0 | 0 | 0 |
| Huduma za kusafirisha vifurushi na vipeto | 20 | 22 | 61 | 36 | 30 |
| V-sat | 21 | 69 | 11 | 7 | 0 |
| Maudhui ya mtandaoni | 151 | 0 | 109 | 91 | 103 |
| Maudhui kutokana na matumizi | 21 | 17 | 5 | 11 | 4 |
| **Jumla** | **546** | **246** | **352** | **316** | **236** |

**Chanzo**: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

**Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

332. Hadi Desemba 2025, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ulifikia urefu wa kilometa 15,500 zilizounganishwa katika mikoa yote Tanzania Bara kutoka kilometa 14,795 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 4.8. Hii ilitokana na juhudi za Serikali katika kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na intaneti nchini na nchi jirani ili kuchochea uchumi wa kidijitali. Katika kipindi hicho, mapato yaliyotokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano yalikuwa shilingi bilioni 183.94 ikilinganishwa na shilingi bilioni 51.36 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji wa mapato ulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, hususan katika nchi za Kenya, Burundi, Uganda, Malawi, Rwanda na Zambia.

**Huduma za Mawasiliano**

333. Hadi Desemba 2025, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote - UCSAF kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano ulifikisha huduma za mawasiliano katika kata 2,006 zenye vijiji 5,128 na wakazi 29,595,095 ikilinganishwa na kata 1,705 zilizokuwa na vijiji 4,982 na wakazi 23,582,852 mwaka 2024. Kuongezeka kwa kata, vijiji na wakazi waliofikiwa na huduma za mawasiliano kulitokana na kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Mawasiliano Vijijini. Katika kipindi hicho, UCSAF kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano iliwezesha ukamilishaji wa minara 430 ikilinganishwa na minara 358 mwaka 2024. Kati ya hiyo, Halotel ilikuwa na minara 8, Airtel minara 48, Vodacom minara 92, TTCL minara 123, na Yas minara 159.

**HABARI**

334. Hadi Desemba 2025, kulikuwa na magazeti 369, vituo vya redio 277 na vituo vya runinga 74 vilivyosajiliwa na kupewa leseni ikilinganishwa na magazeti 354, vituo vya redio 250 na vituo vya runinga 67 mwaka 2024. Ongezeko la usajili na utoaji leseni lilichangiwa na kukua kwa hitaji la kupashana habari na kupungua kwa gharama ya leseni kwa baadhi ya huduma kufuatia mabadiliko ya kanuni. Katika kipindi cha mwaka 2025, magazeti na majarida mapya yaliyosajiliwa yalipungua na kufikia 15 ikilinganishwa na magazeti na majarida 26 yaliyosajiliwa mwaka 2024. Aidha, vituo vipya vya redio 27 vilisajiliwa mwaka 2025 ikilinganishwa na vituo vipya 29 vilivyosajiliwa mwaka 2024. Vilevile, vituo vipya saba (7) vya runinga vilisajiliwa mwaka 2025 ikilinganishwa na vituo 15 vilivyosajiliwa mwaka 2024. Kwa upande mwingine, blogu mpya 11 zilisajiliwa mwaka 2025 na kufikisha jumla ya blogu 77 ikilinganishwa na blogu sita (6) zilizosajiliwa mwaka 2024 (**Jedwali Na. 13.3**).

**Jedwali Na. 13.3: Usajili wa Vyombo vya Habari, Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Idadi ya magazeti na Majarida | Idadi ya Vituo vya Redio | Idadi ya Vituo vya Runinga | Idadi ya Blogu |
|---|---:|---:|---:|---:|
| 2021 | 26 | 9 | 10 | 15 |
| 2022 | 46 | 15 | 9 | 6 |
| 2023 | 32 | 18 | 18 | 22 |
| 2024 | 26 | 29 | 15 | 6 |
| 2025 | 15 | 27 | 7 | 11 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

335. Mwaka 2024/25, Shirika la Utangazaji Tanzania - TBC liliendelea kuongeza usikivu wa redio kwa kufunga mitambo ya redio masafa ya FM katika Wilaya mbili (2) ikilinganishwa na Wilaya 14 mwaka 2023/24, hivyo kufikisha usikivu wa TBC katika Wilaya 139

**Huduma za Utangazaji**

336. Mwaka 2025, watumiaji wa huduma za utangazaji (kwa kutumia idadi ya ving'amuzi vilivyolipiwa angalau mara moja ndani ya miezi mitatu) walikuwa 2,136,835 ikilinganishwa na watumiaji 2,148,690 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 0.6. Hii ilitokana na kupanda kwa bei ya vifurushi kwenye visimbuzi. Kati ya hao, watumiaji wa huduma za utangazaji kupitia satelaiti walikuwa 1,579,799, watumiaji wa huduma za utangazaji kupitia mitambo iliyosimikwa ardhini walikuwa 539,756 na watumiaji wa *cable television* walikuwa 17,280 (**Jedwali Na. 13.4**).

**Jedwali Na. 13.4: Watumiaji wa Huduma za Utangazaji Nchini, Mwaka 2021 - 2025**

| Aina ya huduma | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Visimbuzi vinavyotumia mitambo iliyosimikwa Ardhini - DTT | 1,613,465 | 1,667,465 | 1,781,340 | 563,682 | 539,756 | -4.2 |
| Visimbuzi Vinavyotumia Satelaiti - DTH | 1,577,315 | 1,702,056 | 1,880,636 | 1,568,241 | 1,579,799 | 0.7 |
| Cable -Television | 29,403 | 85,802 | 16,223 | 16,767 | 17,280 | 3.1 |
| **Jumla** | **3,220,183** | **3,455,323** | **3,678,199** | **2,148,690** | **2,136,835** | **-0.6** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

## MAENDELEO YA UTAMADUNI

### Maendeleo ya Kiswahili Kitaifa na Kimataifa

337. Mwaka 2025, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) liliandaa na kurusha hewani vipindi 2,457 kuhusu sarufi na fasihi ya kiswahili kupitia redio na runinga ikilinganishwa na vipindi 2,311 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 6.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa matumizi ya lugha ya kiswahili ndani na nje ya nchi. Aidha, miswada ya vitabu vilivyopata ithibati ya lugha vilivyokusudiwa kutumika shuleni ilikuwa 84 mwaka 2025 ikilinganishwa na miswada ya vitabu 62 mwaka 2024. Ongezeko la miswada lilitokana na BAKITA kutangaza huduma za ithibati zinazotolewa kwa mujibu wa sheria pamoja na kuhamasisha vitabu vyote vinavyoandikwa kwa Kiswahili kupatiwa ithibati ya lugha.

338. Mwaka 2025, BAKITA ilisajili wataalamu 56 katika Kanzidata ya Wataalamu wa Lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na wataalamu 78 waliosajiliwa mwaka 2024. Hadi Desemba 2025, watanzania wanaofundisha Kiswahili nje ya nchi waliongezeka na kufikia 537 kutoka watanzania 498 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuendelea na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Ubidhaishaji Kiswahili wa Mwaka 2022 - 2032. Katika kipindi hicho, vituo vya kufundisha kiswahili kwa raia wa kigeni vilivyosajiliwa na BAKITA vilifikia 56 kutoka vituo 51 mwaka 2024.

### Uhariri na Tafsiri ya Nyaraka

339. Mwaka 2025, BAKITA ilitafsiri nyaraka 6,317 ikilinganishwa na nyaraka 6,234 zilizotafsiriwa mwaka 2024. Kuongezeka kwa nyaraka zilizotafsiriwa kulitokana na kuendelea na jitihada za kutangaza huduma za tafsiri kwa wadau mbalimbali. Kati ya nyaraka hizo, nyaraka 634 zilitafsiriwa kutoka lugha ya kiingereza kwenda Kiswahili; nyaraka 108 kutoka lugha ya Kiswahili kwenda kiingereza; nyaraka 578 kutoka lugha ya kifaransa kwenda kiingereza; nyaraka 917 kutoka lugha ya kiarabu kwenda kiingereza; nyaraka 3,054 kutoka lugha ya kichina kwenda kiingereza na Kiswahili; na nyaraka 1,026 zilitafsiriwa kutoka lugha mbalimbali kwenda lugha ya kiingereza na Kiswahili. Vilevile, Baraza liliratibu huduma ya ukalimani katika mikutano 17 ya kitaifa na kimataifa mwaka 2025 ikilinganishwa na mikutano 14 iliyoratibiwa mwaka 2024.

340. Mwaka 2025, Baraza lilihariri miswada 10 ikilinganishwa na miswada mitano (5) iliyohaririwa mwaka 2024. Kuongezeka kwa miswada iliyohaririwa kulitokana na baadhi ya kampuni za uchapishaji kuanza kutumia BAKITA katika uhariri wa miswada baada ya BAKITA kuingia makubaliano na chama cha wachapishaji Tanzania. Kwa upande mwingine, BAKITA ilibaini makosa 87 ya matumizi ya lugha ya kiswahili kupitia vyombo vya habari mwaka 2025 ikilinganishwa na makosa 102 yaliyobainika mwaka 2024. Upungufu huo ulitokana na kuendelea kutolewa kwa elimu kwa waandishi na watangazaji kuhusu matumizi sahihi ya lugha yanayozingatia ufasaha na usanifu (**Jedwali Na. 13.5**).

**Jedwali Na. 13.5: Huduma Zilizotolewa na BAKITA, Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Vipindi vya Redio na Runinga | Huduma za Ithibati | Huduma za Tafsiri | Huduma za Ukalimani | Huduma za Uhariri | Makosa ya Matumizi ya Lugha |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2021 | 1,008 | 203 | 1,148 | 0 | 23 | 1,205 |
| 2022 | 1,064 | 110 | 1,375 | 12 | 20 | 1,005 |
| 2023 | 1,187 | 30 | 1,380 | 11 | 10 | 192 |
| 2024 | 2,311 | 62 | 6,324 | 14 | 5 | 102 |
| 2025 | 2,457 | 84 | 6,317 | 17 | 10 | 87 |

**Chanzo:** Baraza la Kiswahili la Taifa

## MAENDELEO YA SANAA

### Vibali vya Utayarishaji wa Filamu

341. Mwaka 2025, Bodi ya Filamu Tanzania ilitoa vibali 188 vya utayarishaji wa filamu ikilinganishwa na vibali 247 vilivyotolewa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 23.9. Upungufu huo ulitokana na kukua kwa teknolojia inayotumia vifaa vidogo kama simu janja kutumika kurekodi filamu zenye ubora.

### Usajili wa Kazi za Sanaa

342. Mwaka 2025, Ofisi ya Hakimiliki Tanzania - COSOTA ilisajili wabunifu 395 wa kazi za sanaa ikilinganishwa na wabunifu 428 waliosajiliwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 7.7. Hii ilitokana na wabunifu wengi kutambua Sheria ya Hakimiliki ya Mwaka 2022 ambayo inawafanya wabunifu kujisajili kwenye makampuni yao kwa ajili ya kupata mirabaha na hivyo wabunifu wengi kutambua haki zao na kufahamu umuhimu wa kuwa na nyaraka ili kupunguza migogoro. Aidha, COSOTA ilisajili kazi za sanaa 1,579 mwaka 2025 ikilinganishwa na kazi za sanaa 1,409 zilizosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 12.1. Vilevile, COSOTA ilitoa vyeti 923 vya uthibitisho wa umiliki wa hakimiliki mwaka 2025 ikilinganishwa na vyeti 2,074 vilivyotolewa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 55.5. Hii ilitokana na utekelezaji wa Sheria ya Hakimiliki ya Mwaka 2022 (**Jedwali Na. 13.6**).

**Jedwali Na. 13.6: Huduma Zilizotolewa na Ofisi ya Hakimiliki Tanzania, Mwaka 2021 - 2025**

| Huduma | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Usajili wa wabunifu kazi za sanaa | 2,066 | 424 | 518 | 428 | 395 |
| Usajili wa kazi za ubunifu | 3,827 | 3,904 | 2,379 | 1,409 | 1,579 |
| Vyeti vya umiliki | 3,835 | 1,430 | 1,357 | 2,074 | 923 |
| Leseni | 370 | 621 | 360 | 0 | 2 |

**Chanzo:** Ofisi ya Hakimiliki Tanzania

**Usajili wa Wasanii katika Fani za Sanaa**

343. Mwaka 2025, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) liliendelea kurasimisha kazi za sanaa nchini ambapo wasanii binafsi 1,110 walisajiliwa ikilinganishwa na wasanii 992 waliosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 11.9 (**Jedwali Na. 13.7**). Hii ilitokana na kupunguzwa kwa ada ya usajili na kuanzishwa kwa mfumo wa usajili wa BASATA (AMIS) pamoja na kutanua wigo wa usajili kwa kuwatumia maafisa utamaduni katika ngazi za Halmashauri.

**Jedwali Na. 13.7: Wasanii wa Sanaa Waliosajiliwa, Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Ufundi | Maonesho | Muziki | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 2021 | 68 | 197 | 201 | 466 |
| 2022 | 87 | 178 | 207 | 472 |
| 2023 | 225 | 179 | 685 | 1,089 |
| 2024 | 169 | 260 | 563 | 992 |
| 2025 | 189 | 301 | 620 | 1,110 |

**Chanzo:** Baraza la Sanaa la Taifa

**Utoaji wa Tuzo za Kazi za Sanaa**

344. Mwaka 2024/25, tuzo 52 zilitolewa kwa wasanii wa muziki wa kitanzania ikilinganishwa na tuzo 47 zilizotolewa mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 10.6 (**Jedwali Na. 13.8**). Kati ya hizo, tuzo 37 zilikuwa za ndani ya nchi na tuzo 15 zilikuwa za nje ya nchi.

**Jedwali Na. 13.8: Tuzo za Muziki kwa Wasanii wa Kitanzania, Mwaka 2020/21 - 2024/25**

| Mwaka | Idadi ya Tuzo za Ndani | Idadi ya Tuzo za Nje | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2020/21 | 15 | 13 | 28 |
| 2021/22 | 47 | 14 | 61 |
| 2022/23 | 44 | 10 | 54 |
| 2023/24 | 37 | 10 | 47 |
| 2024/25 | 37 | 15 | 52 |

**Chanzo:** Baraza la Sanaa la Taifa

345. Mwaka 2025, tuzo 89 za filamu zilitolewa kwa wadau ikilinganishwa na tuzo 86 zilizotolewa mwaka 2024 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 13.9**. Kati ya hizo, tuzo 66 zilikuwa za ndani ya nchi na tuzo 23 zilikuwa za nje ya nchi.

**Jedwali Na. 13.9: Tuzo za Filamu Zilizotolewa kwa Wasanii, Mwaka 2021 - 2025**

| **Tuzo** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
|---|---|---|---|---|---|
| Tuzo za ndani | 33 | 50 | 41 | 67 | 66 |
| Tuzo za nje | 3 | 13 | 15 | 19 | 23 |
| **Jumla** | **36** | **63** | **56** | **86** | **89** |

**Chanzo:** Bodi ya Filamu Tanzania

**Urasimishaji wa Kazi za Utamaduni na Sanaa**

346. Mwaka 2025, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa uliwezesha urasimishaji wa kazi za utamaduni na sanaa 4,915 ikilinganishwa na kazi 4,533 zilizorasimishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 8.4. Hii ilitokana na kuendelea kuhamasiska kwa wasanii kuhusu umuhimu wa kubadilisha sanaa kuwa biashara.

347. Mwaka 2025, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ulitoa mikopo kwa miradi 229 ya utamaduni na sanaa yenye thamani ya shilingi milioni 3,535.00 ikilinganishwa na miradi 152 yenye thamani ya shilingi milioni 3,128.90 iliyotolewa mwaka 2024, sawa na ongezeko la thamani la asilimia 13.0 (**Jedwali Na. 13.10)**. Hii ilitokana na wasanii kufanya marejesho ya mikopo kwa wakati. Aidha, marejesho ya mikopo yalikuwa asilimia 96.8 ya mikopo iliyoiva mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 95.6 mwaka 2024. Katika kipindi hicho, ajira 971,285 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja zilizalishwa kupitia mikopo iliyotolewa ikilinganishwa na ajira 449,531 zilizozalishwa mwaka 2024.

**Jedwali Na. 13.10: Mikopo Iliyotolewa na Ajira Zilizozalishwa, Mwaka 2022 - 2025**

| **Mwaka** | **Idadi ya Miradi** | **Thamani ya Mikopo (Shilingi)** | **Ajira Zilizozalishwa** |
|---|---|---|---|
| 2022 | 5 | 185,000,000 | 14,732 |
| 2023 | 97 | 2,148,450,000 | 286,985 |
| 2024 | 152 | 3,128,900,000 | 449,531 |
| 2025 | 229 | 3,535,000,000 | 971,285 |

**Chanzo:** Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

348. Mwaka 2025, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa uliwezesha mafunzo ya urasimishaji wa kazi za utamaduni na sanaa kwa wasanii 11,556 ikilinganishwa na wasanii 5,841 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 97.8. Hii ilitokana na mwitikio wa wasanii kupata mafunzo kupitia uhamasishaji katika vyombo vya habari.

**MAENDELEO YA MICHEZO**

349. Mwaka 2025, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) lilisajili vilabu vya michezo 181 ikilinganishwa na vilabu 152 vilivyosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 19.1. Ongezeko hilo lilitokana na kuanzishwa kwa Mfumo wa Usajili wa Vyama vya Michezo Kidigitali pamoja na ushiriki wa maafisa michezo ngazi za halmashauri kama wasajili wasaidizi. Katika kipindi hicho, vyama vya michezo vilivyosajiliwa vilikuwa 43 ikilinganishwa na vyama 45 vilivyosajiliwa mwaka 2024. Aidha, vituo/shule za michezo zilizosajiliwa zilikuwa 43 mwaka 2025 ikilinganishwa na vituo/shule za michezo 49 zilizosajiliwa mwaka 2024. Vilevile, wakuzaji/mawakala waliosajiliwa walikuwa 62 mwaka 2025 ikilinganishwa na wakuzaji/mawakala 66 waliosajiliwa mwaka 2024. Upungufu huo ulitokana na kuanza kutumika kwa masharti mapya ya usajili, hali iliyohitaji muda kwa wadau kuyaelewa na kuyatekeleza kikamilifu.

**Jedwali Na. 13.11: Usajili wa Wadau wa Michezo, Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Vilabu vya Michezo | Vyama vya Michezo | Vituo/shule za Michezo | Wakuzaji/Mawakala wa Michezo | Taasisi za Michezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 2021 | 216 | 15 | 22 | 60 | 9 |
| 2022 | 178 | 15 | 33 | 40 | 10 |
| 2023 | 154 | 34 | 28 | 59 | 0 |
| 2024 | 152 | 45 | 49 | 66 | 0 |
| 2025 | 181 | 43 | 43 | 62 | 0 |

**Chanzo:** Baraza la Michezo la Taifa

## Jedwali Na. 58: HUDUMA ZA POSTA, MWAKA 2018 - 2025

| Maelezo | Kipimo | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ofisi Ndogo Posta | Idadi | 57 | 46 | 40 | 29 | 29 | 29 | 31 | 31 |
| Franchised Post Offices | Idadi | 87 | 79 | 72 | 70 | 70 | 70 | 63 | 63 |
| Ofisi Kubwa | Idadi | 157 | 139 | 132 | 144 | 144 | 144 | 150 | 149 |
| **Jumla** | **Idadi** | **301** | **264** | **244** | **243** | **243** | **243** | **244** | **243** |
| Masanduku Binafsi | 000 | 161 | 145 | 126 | 126 | 126 | 152 | 158 | 194 |
| Masanduku Yaliokodishwa | 000 | 157 | 126 | 125 | 125 | 125 | 119 | 150 | 135 |
| Maombi Yasiotimizwa | 000 | 3 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 8 | 59 |
| Mifuko Pekee Iliyokodishwa | Idadi | 675 | 442 | 291 | 240 | 180 | 60 | 47 | 67 |
| Barua Zilizotumwa bila Vifurushi | Mil. | 9 | 11 | 6 | 4 | 2 | 2 | 1 | 1 |
| Regista na Barua za Amana | 000 | 280 | 186 | 65 | 45 | 50 | 25 | 92 | 115 |
| Vifurushi Nchini | 000 | 63 | 32 | 4 | 6 | 10 | 7 | 19 | 21 |
| Vifurushi Nje | 000 | 4 | 3 | 2 | 2 | 1 | 6 | 2 | 1 |
| Leseni za kuuza stamp | Idadi | 6,027 | 5,570 | 2,803 | 1,726 | 1,374 | 463 | 231 | 231 |
| **Huduma za Haraka, barua na vifurushi** | | | | | | | | | |
| Ndani ya Nchi | Idadi | 655,927 | 511,274 | 466,029 | 627,822 | 481,588 | 354,746 | 499,430 | 546,147 |
| Nje ya Nchi | Idadi | 14,346 | 13,742 | 7,080 | 11,642 | 5150 | 6,254 | 15,506 | 11,641 |
| EMS Money Fax | Idadi | 0 | 0 | 52 | 0 | 0 | 0 | | 0 |
| EMS Fax (Fax message received) | Idadi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | | 0 |
| *Overnight Mail Services* | " | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa | Idadi | 14,553 | 19,598 | 46,093 | 30,339 | 24889 | 26,171 | 16,279 | |
| Vifurushi vya magazeti vilivyosafirishwa | Idadi | 5,346 | 7,800 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Huduma za gari ndogo** | | | | | | | | | |
| Idadi ya Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa | Idadi | 2,919 | 2,518 | 5,651 | 3,293 | 6377 | 5,178 | 427 | 0 |
| Amna za Haraka Zilizotolewa | Idadi | 104 | 109 | 52 | | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Amana za Haraka Zilizolipwa | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Amana za Haraka za Nje ya Nchi** | | | | | | | | | |
| Zilizotumwa | Idadi | 11 | 26 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Zilizopokelewa | Idadi | 37 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Amana za Posta zilizouzwa | Idadi | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Amana za Posta Zilizolipwa | Idadi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Benki ya Akiba (Transaction)** | | | | | | | | - | |
| Uwekaji Amana (Deposit) | Idadi | 108,972 | 91,567 | 56,064 | 94,689 | 96,959 | 70,110 | 56,253 | 17,317 |
| Uchukuaji Amana (Withdrawal) | Idadi | 133,531 | 103,958 | 75,065 | 69,203 | 94,374 | 106,845 | 234,055 | 44,839 |

**Chanzo**: Shirika la Posta Tanzania

**Jedwali Na. 59: IDADI YA KADI ZA SIMU ZA MEZANI NA VIGANJANI, MWAKA 2019 - 2025**

| Kampuni | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A. Simu za Kiganjani** | | | | | | | | |
| Tigo/Yas | 12,572,826 | 13,032,073 | 13,369,276 | 15,940,373 | 19,698,263 | 25,419,851 | 29,810,835 | 17.3 |
| Vodacom | 15,672,390 | 15,621,457 | 15,913,553 | 18,180,904 | 21,272,484 | 26,327,611 | 31,073,644 | 18.0 |
| Airtel | 12,722,224 | 13,823,756 | 14,700,426 | 16,616,488 | 19,146,016 | 20,061,071 | 21,986,955 | 9.6 |
| TTCL Mobile | 981,072 | 963,384 | 1,813,719 | 1,495,577 | 1,644,194 | 1,655,861 | 1,686,826 | 1.9 |
| Hallotel | 4,641,701 | 6,818,228 | 7,200,140 | 8,028,138 | 8,529,919 | 12,371,713 | 16,632,749 | 34.4 |
| **Jumla** | **46,590,213** | **51,292,702** | **52,997,114** | **60,261,480** | **70,290,876** | **85,836,107** | **101,191,009** | **17.9** |
| **B. Simu za Mezani** | | | | | | | | |
| Mobile Network | 47,685,232 | 51,220,233 | 54,044,384 | 60,192,331 | 70,215,144 | 86,769,161 | 106,823,601 | 23.1 |
| Fixed Network | 76,288 | 72,834 | 71,834 | 84,696 | 75,732 | 78,299 | 111,600 | 42.5 |
| **Jumla** | **47,761,520** | **51,293,067** | **54,116,218** | **60,277,027** | **70,290,876** | **86,847,460** | **106,935,201** | **23.1** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

# SURA YA 14

# NISHATI

**Upatikanaji wa Umeme Nchini**

350. Mwaka 2025, uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme ulikuwa megawati 4,093.74 ikilinganishwa na megawati 3,052.46 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 34.1. Hii ilitokana na kukamilika kwa mitambo yote tisa katika Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - JNHPP yenye jumla ya megawati 2,115 ambapo baadhi ya mitambo iliwashwa na kuanza kuzalisha umeme kulingana na mahitaji na kwa mara ya kwanza ilizalisha megawati 362.10 zilizoingizwa katika Gridi ya Taifa.


351. Mwaka 2025, umeme uliozalishwa kutoka vyanzo mbalimbali ulikuwa saa za megawati (MWh) 13,887,330 ikilinganishwa na saa za megawati 11,958,840 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 16.1 (**Jedwali Na. 14.1**). Kati ya kiasi hicho, saa za megawati 13,441,680 zilizalishwa katika Gridi ya Taifa, saa za megawati 160,750 zilizalishwa katika vituo nje ya Gridi ya Taifa na saa za megawati 284,900 zilinunuliwa kutoka nchi jirani. Umeme uliozalishwa katika Gridi ya Taifa ulitokana na mitambo ya nguvu za maji saa za megawati 8,866,740, sawa na asilimia 63.85; gesi asilia saa za megawati 4,371,970 (asilimia 31.48); mafuta saa za megawati 7,400 (asilimia 0.05); tungamotaka saa za megawati 19,360 (asilimia 0.14), umeme jua saa za megawati 13,450 (asilimia 0.10) na umeme ulionunuliwa kutoka Kenya ambao uliingizwa katika grid ya Taifa saa za megawati 162,760 (asilimia 1.2). Aidha, umeme uliozalishwa na vituo vilivyo nje ya Gridi ya Taifa ulikuwa saa za megawati 160,750, sawa na asilimia 1.16 ya umeme uliozalishwa nchini na umeme ulionunuliwa kutoka nchi jirani za Uganda na Zambia ambao haukuingizwa katika grid ulikuwa saa za megawati 284,900 (asilimia 3.22) kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 14.1**. Vilevile, umeme uliozalishwa na mitambo inayomilikiwa na TANESCO ulikuwa saa za megawati 13,183,220 mwaka 2025 ikilinganishwa na saa za megawati 10,776,490 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 22.3. Hadi Desemba 2025, mahitaji ya umeme nchini yalifikia megawati 2,180.50 ambapo megawati 2,069.33 zilikuwa za Gridi ya Taifa na megawati 111.17 zilikuwa nje ya Gridi ya Taifa.

**Jedwali Na. 14.1: Uwezo wa Mitambo na Uzalishaji wa Umeme Kutoka Vyanzo Mbalimbali Mwaka 2025**

| Chanzo | Uwezo wa Mitambo (MW) | Mchango (Asilimia) | Uzalishaji (MWh) | Mchango (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Maji | 2,718.27 | 66.40 | 8,866,720.0 | 63.85 |
| Gesi Asilia | 1,140.72 | 27.86 | 4,371,980.0 | 31.48 |
| Mafuta | 101.05 | 2.47 | 7,400.0 | 0.05 |
| Tungamotaka | 20.50 | 0.50 | 19,360.0 | 0.14 |
| Umeme Jua | 15.00 | 0.37 | 13,460.0 | 0.10 |
| Nje ya Gridi ya Taifa | 98.20 | 2.40 | 160,740.0 | 1.16 |
| Umeme Kutoka Nchi Jirani | - | - | 447,660.0 | 3.22 |
| **Jumla** | **4,093.74** | **100.00** | **13,887,320.0** | **100.00** |

**Chanzo:** Shirika la Umeme Tanzania

**Kielelezo Na. 14.1: Umeme Kutoka Vyanzo Mbalimbali Mwaka 2025**




352. Mwaka 2025, umeme uliouzwa kwa watumiaji mbalimbali ulikuwa saa za megawati (MWh) 9,713,000 ikilinganishwa na saa za megawati (MWh) 9,114,700 zilizouzwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 6.6. Katika kipindi hicho, umeme uliotumika kwa matumizi ya nyumbani ulikuwa saa za megawati (MWh) 4,360,500, wateja wakubwa saa za megawati (MWh) 4,444,400 na Zanzibar saa za megawati (MWh) 908,100. Kwa upande mwingine, umeme uliopotea ulikuwa asilimia 14.48 ya umeme uliozalishwa mwaka 2025 kama ilivyokuwa mwaka 2024. Upotevu huo ulitokana na uchakavu wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme, urefu wa miundombinu ya kusambaza umeme na kuzidiwa kwa transfoma (mashineumba). Hadi Desemba 2025, asilimia 85.5 ya wananchi walifikiwa na huduma ya umeme (accessibility) na asilimia 52.10 waliunganishiwa umeme (connectivity). Aidha, vitongoji 39,003 kati ya vitongoji 64,359 vya Tanzania Bara, sawa na

asilimia 60.6 vilipelekewa huduma ya umeme kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini - REA.

353. Mwaka 2025, miundombinu ya kusafirisha umeme nchini ilifikia urefu wa kilometa 8,500.38 kutoka kilometa 8,025.38 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 5.9. Aidha, miundombinu ya kusambaza umeme ilifikia kilometa 223,389.94 mwaka 2025 kutoka kilometa 197,597.34 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 13.1. Vilevile, wateja waliounganishwa na umeme nchini walifikia 5,831,689 mwaka 2025 kutoka wateja 5,225,193 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 11.6 (**Jedwali Na. 14.2**). Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa urefu wa miundombinu ya kusambaza umeme, kuendelea kutumika kwa mfumo mpya wa maombi ya umeme wa NIKONEKT na usambazaji wa umeme vijijini kupitia REA.

**Jedwali Na. 14.2: Hali ya Upatikanaji wa Umeme Nchini, Mwaka 2024 - 2025**

| | 2024 | 2025 | Ongezeko (Asilimia) |
|---|---:|---:|---:|
| Uwezo wa Mitambo ya Kuzalisha umeme (MW) | 3,052.46 | 4,073.70 | 33.5 |
| Umeme uliozalishwa (MWh) | 11,958,840 | 13,887,330 | 16.1 |
| Umeme uliouzwa (MWh) | 9,114,700 | 9,713,000 | 6.6 |
| Njia za Kusafirisha umeme (Km) | 8,025.38 | 8,500.38 | 5.9 |
| Njia za Kusambaza umeme (Km) | 197,597.34 | 223,389.94 | 13.1 |
| Wateja waliounganishia umeme | 5,225,193 | 5,831,689 | 11.6 |

**Chanzo:** Shirika la Umeme Tanzania

**Gesi Asilia**

354. Mwaka 2025, gesi asilia iliyozalishwa ilikuwa futi za ujazo milioni 61,905.84 ikilinganishwa na futi za ujazo milioni 69,538.30 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 11.0 (**Jedwali Na. 14.3**). Hii ilitokana na kupungua kwa mahitaji ya gesi asilia katika uzalishaji wa umeme baada ya Mradi wa JNHPP kuanza kufanya kazi. Aidha, mapato yaliyotokana na mauzo ya gesi asilia katika vitalu vya Songosongo na Mnazi Bay yalikuwa dola za Marekani milioni 159.2 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 144.10 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 10.5 (**Jedwali Na. 14.4**). Hii ilitokana na kuongezeka kwa wateja wapya hususan viwanda.

**Jedwali Na. 14.3: Uzalishaji wa Gesi Asilia (Futi za Ujazo Milioni), Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Songosongo | Mnazi Bay | Jumla | Badiliko (Asilimia) |
|---|---:|---:|---:|---:|
| 2021 | 35,095.18 | 29,828.96 | 64,924.14 | 13.7 |
| 2022 | 46,116.99 | 32,942.96 | 79,059.95 | 21.8 |
| 2023 | 45,976.38 | 39,196.81 | 85,173.19 | 7.7 |
| 2024 | 33,695.42 | 35,842.88 | 69,538.30 | (18.4) |
| 2025 | 26,249.89 | 35,655.95 | 61,905.84 | (11.0) |

**Chanzo:** Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

**Jedwali Na. 14.4: Mapato ya Mauzo ya Gesi Asilia (Dola za Marekani), Mwaka 2021 - 2025**

| Mwaka | Songosongo | Mnazi Bay | Jumla | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| 2021 | 16,018,066 | 42,886,054 | 58,904,120 | 6.9 |
| 2022 | 26,933,872 | 44,355,811 | 71,269,693 | 21.0 |
| 2023 | 45,264,440 | 79,265,141 | 124,529,581 | 74.7 |
| 2024 | 33,054,000 | 111,041,488 | 144,095,489 | 15.7 |
| 2025 | 48,702,604 | 110,503,969 | 159,206,573 | 10.5 |

**Chanzo:** Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

355. Mwaka 2025, mtandao wa usambazaji wa gesi asilia ulifikia kilometa 249.57 kutoka kilometa 177.82 mwaka 2024. Hadi Desemba 2025, nyumba 2,515, viwanda 59, taasisi 26 na vituo 13 vya kujaza gesi asilia kwenye magari viliunganishwa kwenye miundombinu ya gesi asilia kutoka nyumba 1,514, viwanda 57, taasisi 14 na vituo sita (6) kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, zaidi ya magari 7,000 na pikipiki 8,000 za magurudumu matatu za kusafirisha abiria zilifungiwa mfumo wa gesi asilia mwaka 2025 ikilinganishwa na magari 5,000 na pikipiki 5,000 mwaka 2024.

**Uagizaji Mafuta**

356. Mwaka 2025, mafuta yaliyoingizwa nchini yalikuwa lita za ujazo milioni 4,566.1 ikilinganishwa na lita za ujazo milioni 4,249.2 zilizoingizwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 7.5. Hii ilitokana na kukua kwa shughuli za uchumi, hususan katika sekta za viwanda, ujenzi, biashara na utalii. Kati ya kiasi kilichoingizwa, mafuta ya dizeli yalikuwa lita za ujazo milioni 2,396.9, petroli lita za ujazo milioni 1,932.5, mafuta ya taa lita za ujazo milioni 0.66, mafuta ya ndege lita za ujazo milioni 219.7 na mafuta mazito lita za ujazo milioni 16.3 (**Jedwali Na. 14.5**). Katika kipindi hicho, akiba ya mafuta ilikuwa siku 10 kwa petroli, dizeli siku 15, mafuta ya ndege siku 25 na mafuta ya taa siku 59.

**Jedwali Na. 14.5: Mafuta Yaliyoingizwa Nchini kwa Matumizi ya Ndani (Lita za Ujazo), Mwaka 2025**

| Mwezi | Dizeli | Petroli | Mafuta ya Ndege | Mafuta ya Taa | Mafuta Mazito | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 231,236,313 | 133,672,631 | 19,639,783 | 664,746 | - | 385,213,473 |
| Februari | 177,857,880 | 119,837,052 | 15,953,399 | - | - | 313,648,331 |
| Machi | 177,868,838 | 73,140,904 | 21,145,314 | - | 5,190,941 | 277,345,997 |
| Aprili | 160,474,934 | 131,186,735 | 21,064,528 | - | - | 312,726,197 |
| Mei | 158,793,544 | 161,801,273 | - | - | - | 320,594,817 |
| Juni | 158,484,266 | 126,563,725 | 26,652,264 | - | 8,816,049 | 320,516,304 |
| Julai | 206,319,219 | 169,434,232 | 18,419,530 | - | - | 394,172,981 |
| Agosti | 139,834,354 | 150,160,668 | 15,891,814 | - | - | 305,886,836 |
| Septemba | 198,154,130 | 171,095,126 | 22,492,189 | - | - | 391,741,445 |
| Oktoba | 184,962,480 | 157,598,729 | 26,683,051 | - | - | 369,244,260 |
| Novemba | 260,856,337 | 154,430,000 | 31,795,105 | - | - | 447,081,442 |
| Desemba | 101,590,608 | 203,628,984 | - | - | - | 305,219,592 |
| Yaliyobadilishwa matumizi | 240,501,378 | 179,945,707 | - | - | 2,319,597 | 422,766,682 |
| Jumla 2025 | 2,396,934,281 | 1,932,495,766 | 219,736,977 | 664,746 | 16,326,587 | 4,566,158,357 |
| Jumla 2024 | 2,364,621,322 | 1,632,440,858 | 217,180,244 | 7,188,555 | 27,781,193 | 4,249,212,172 |
| **Badiliko (Asilimia)** | **1.4** | **18.4** | **1.2** | **-90.8** | **-41.2** | **7.5** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

**Mafuta Yaliyoingizwa Nchini Kwenda Nchi Jirani**

357. Mwaka 2025, lita za ujazo milioni 6,684.7 za mafuta ziliingizwa nchini kwenda nchi jirani ikilinganishwa na lita za ujazo milioni 5,304.1 zilizoingizwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 26.0. Hii ilitokana na nchi za jirani kuendelea kutumia bandari za Tanzania kupitisha mafuta, hususan nchi ya Zambia ambayo inatumia bomba la TAZAMA kusafirisha mafuta kutoka Dar es Salaam hadi Ndola. Kati ya kiasi kilichoagizwa, mafuta ya dizeli yalikuwa lita za ujazo milioni 4,792.3, petroli lita za ujazo milioni 1,668.0, mafuta ya ndege lita za ujazo milioni 223.9 na mafuta mazito lita milioni 0.47 (**Jedwali Na. 14.6**).

**Jedwali Na. 14.6: Mafuta Yaliyoingizwa Nchini Kwenda Nchi Jirani Mwaka 2025 (Lita za Ujazo)**

| Mwezi | Dizeli | Petroli | Mafuta ya Ndege | Mafuta ya Taa | Mafuta Mazito | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 440,996,817 | 158,540,841 | 9,634,840 | - | - | 609,172,498 |
| Februari | 489,621,040 | 151,013,638 | 29,957,932 | - | - | 670,592,610 |
| Machi | 339,553,307 | 176,473,049 | 11,047,907 | - | - | 527,074,263 |
| Aprili | 504,001,274 | 94,025,783 | 25,484,606 | - | - | 623,511,663 |
| Mei | 341,191,833 | 109,860,704 | - | - | - | 451,052,537 |
| Juni | 459,807,979 | 149,069,046 | 23,969,236 | - | 466,523 | 633,312,784 |
| Julai | 481,987,418 | 152,094,505 | 21,977,601 | - | - | 656,059,524 |
| Agosti | 349,290,782 | 77,511,642 | 10,643,648 | - | - | 437,446,072 |
| Septemba | 443,072,460 | 169,300,952 | 40,858,334 | - | - | 653,231,746 |
| Oktoba | 405,368,942 | 151,762,961 | 21,639,813 | - | - | 578,771,716 |
| Novemba | 489,241,543 | 267,955,334 | 19,363,307 | - | - | 776,560,184 |
| Desemba | 288,681,333 | 190,365,529 | 9,357,184 | - | - | 488,404,046 |
| Yaliyobadilishwa Matumizi | -240,501,378 | -179,945,707 | - | - | - | -420,447,085 |
| Jumla - 2025 | 4,792,313,350 | 1,668,028,277 | 223,934,408 | - | 466,523 | 6,684,742,558 |
| Jumla - 2024 | 3,642,504,229 | 1,414,788,174 | 241,111,967 | 650,058 | 5,064,827 | 5,304,119,255 |
| **Badiliko (Asilimia)** | **31.6** | **17.9** | **-7.1** | **-100** | **-90.8** | **26** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

**Mwenendo wa Bei za Mafuta**

358. Mwaka 2025, wastani wa bei ya mafuta kwa tani katika soko la dunia ulikuwa dola za Marekani 653.07 kwa mafuta ya petroli, dola za Marekani 638.44 kwa mafuta ya dizeli na dola za Marekani 665.20 kwa mafuta ya taa ikilinganishwa na dola za Marekani 729, dola za Marekani 694 na dola za Marekani 728, mtawalia kwa mwaka 2024. Bei hizo zilipungua kwa asilimia 10.4 kwa mafuta ya petroli, asilimia 8.1 kwa mafuta ya dizeli na asilimia 8.6 kwa mafuta ya taa (**Jedwali Na. 14.7**). Hii ilitokana na: usambazaji mafuta ghafi kuzidi kiwango cha mahitaji kimataifa; kuongezeka kwa uzalishaji wa nchi za OPEC+; na kupungua kwa mahitaji ya mafuta kutokana na mabadiliko katika uchumi wa dunia, hususan kutokana na ongezeko la matumizi ya magari ya umeme na teknolojia za nishati mbadala.

**Jedwali Na. 14.7: Wastani wa Bei za Mafuta Katika Soko la Dunia (Dola za Marekani kwa Tani) Mwaka 2025**

| Mwezi | Dizeli | Petroli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| Januari | 697 | 704 | 722 |
| Februari | 672 | 707 | 710 |
| Machi | 627 | 658 | 654 |
| Aprili | 595 | 624 | 621 |
| Mei | 575 | 619 | 598 |
| Juni | 628 | 660 | 647 |
| Julai | 663 | 645 | 671 |
| Agosti | 627 | 643 | 647 |
| Septemba | 649 | 661 | 671 |
| Oktoba | 651 | 640 | 677 |
| Novemba | 682 | 651 | 720 |
| Desemba | 595 | 624 | 645 |
| **Wastani 2025** | **638** | **653** | **665** |
| **Wastani 2024** | **694** | **728** | **728** |
| **Badiliko (Asilimia)** | **-8.1** | **-10.3** | **-8.7** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

359. Mwaka 2025, wastani wa bei ukomo za mafuta kwa lita katika soko la ndani ulipungua na kufikia shilingi 2,855 kwa mafuta ya petroli, shilingi 2,779 mafuta ya dizeli na shilingi 2,815 mafuta ya taa ikilinganishwa na shilingi 3,130 kwa mafuta ya petroli, shilingi 3,040 mafuta ya dizeli na shilingi 3,041 mafuta ya taa mwaka 2024. Upungufu huo ni sawa na wastani wa asilimia 8.8 kwa mafuta ya petroli, asilimia 8.6 mafuta ya dizeli na asilimia 7.4 mafuta ya taa (**Jedwali Na. 14.8**). Hii ilitokana na kupungua kwa bei za mafuta katika soko la dunia.

**Jedwali Na. 14.8: Wastani wa Bei za Mafuta Katika Soko la Ndani (Shs/Lita) Mwaka 2025**

| Mwezi | Dizeli | Petroli | Mafuta ya Taa |
|---|---:|---:|---:|
| Januari | 2,644 | 2,793 | 2,676 |
| Februari | 2,703 | 2,820 | 2,710 |
| Machi | 2,885 | 2,996 | 3,036 |
| Aprili | 2,936 | 3,037 | 3,053 |
| Mei | 2,868 | 2,947 | 3,053 |
| Juni | 2,826 | 2,885 | 2,877 |
| Julai | 2,767 | 2,877 | 2,629 |
| Agosti | 2,777 | 2,843 | 2,768 |
| Septemba | 2,754 | 2,807 | 2,774 |
| Oktoba | 2,704 | 2,752 | 2,774 |
| Novemba | 2,704 | 2,752 | 2,774 |
| Desemba | 2,779 | 2,749 | 2,653 |
| **Wastani 2025** | **2,779** | **2,855** | **2,815** |
| **Wastani 2024** | **3,040** | **3,130** | **3,041** |
| **Badiliko (Asilimia)** | **-8.6** | **-8.8** | **-7.4** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

**Gesi Inayotokana na Petroli**

360. Mwaka 2025 gesi inayotokana na petroli - LPG iliyoagizwa nchini ilikuwa tani za ujazo 267,877 ikilinganishwa na tani za ujazo 344,374 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 22.2 (**Jedwali Na. 14.9**). Hii ilitokana na nchi ya Kenya iliyokuwa ikiingiza kupitia Tanzania kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kupokelea LPG.

**Jedwali Na. 14.9: LPG Iliyopokelewa Nchini (Tani za Ujazo), Mwaka 2024 - 2025**

| Mwezi/Mwaka | 2024 | 2025 |
|---|:---:|:---:|
| Januari | 28,921 | 17,939 |
| Februari | 33,344 | 24,274 |
| Machi | 29,622 | 16,175 |
| Aprili | 42,961 | 22,443 |
| Mei | 40,634 | 22,393 |
| Juni | 25,397 | 22,190 |
| Julai | 22,894 | 23,340 |
| Agosti | 33,511 | 30,803 |
| Septemba | 24,486 | 21,191 |
| Oktoba | 21,649 | 24,632 |
| Novemba | 26,161 | 22,468 |
| Desemba | 14,793 | 20,030 |
| **Jumla** | **344,373** | **267,878** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

**Jedwali Na. 60: UWEZO WA MITAMBO YA KUFUA UMEME NA UPATIKANAJI WA UMEME NCHINI MWAKA 2025**

| Kituo | Uwezo (MW) | Uzalishaji (Saa za Megawati 000") |
|---|---:|---:|
| **Umeme Kutokana na Maji** | | |
| JNHPP | 2,115.00 | 6,061.17 |
| Kidatu | 204.00 | 991.18 |
| Kihansi | 180.00 | 742.20 |
| Mtera | 80.00 | 415.42 |
| New Pangani Falls | 68.00 | 371.70 |
| Rusumo | 26.67 | 153.80 |
| Hale | 21.00 | - |
| Nyumba ya Mungu | 8.00 | 59.40 |
| Uwemba | 0.84 | 2.03 |
| Mwenga | 4.00 | 15.12 |
| Yovi | 0.95 | 5.98 |
| Matembwe | 0.59 | 0.05 |
| Darakuta | 0.32 | 2.06 |
| Luponde | 0.90 | 16.19 |
| Andoya | 1.00 | 0.81 |
| Tulila | 5.00 | 29.63 |
| Igola | 2.00 | - |
| **Jumla Ndogo Maji** | **2,718.27** | **8,866.74** |
| **Umeme Kutokana na Gesi Asilia** | | |
| Kinyerezi II | 248.22 | 1,484.47 |
| Ubungo Gas Plant II | 129.00 | 866.73 |
| Ubungo Gas Plant I | 102.00 | 423.23 |
| Songas | 189.00 | - |
| Ubungo Gas Plant III | 92.50 | 500.27 |
| Tegeta Gas Plant | 45.00 | 212.88 |
| Kinyerezi I | 335.00 | 779.13 |
| Mtwara I | - | 51.35 |
| Mtwara II (TM 16) | - | 47.96 |
| Somanga | - | 5.95 |
| **Jumla Ndogo Gesi Asilia** | **1,140.72** | **4,371.97** |

**Jedwali Na. 60: Linaendelea**

| | | |
|---|---|---|
| **Umeme Kutokana na Mafuta** | | |
| Zuzu | 7.440 | 0 |
| Nyakato | 63.000 | 7.36 |
| Biharamulo | 2.720 | - |
| Songea | 5.740 | - |
| Liwale | 0.850 | - |
| Tunduru | 1.050 | - |
| Ludewa | 1.270 | - |
| Ngara | 1.250 | - |
| Kasulu | 4.550 | - |
| Kibondo | 2.500 | - |
| Kigoma | 8.750 | 0.04 |
| Inyonga | 1.930 | |
| **Jumla Ndogo Mafuta** | **101.050** | **7.40** |
| **Umeme Kutokana na Tungamotaka** | | |
| TANWAT | 1.50 | 0.50 |
| TPC | 9.00 | 18.80 |
| Kilombero Sugar | 10.00 | - |
| **Jumla Ndogo Tungamotaka** | **20.50** | **19.36** |
| **Umeme Jua** | | |
| Solar Wazi | 5.00 | 5.50 |
| Ushetu | 5.00 | 4.40 |
| Bukombe | 5.00 | 3.60 |
| Jumla Ndogo Umeme Jua | **15.00** | **13.45** |
| **Kupokea kutoka kenya** | | **162.76** |
| **Jumla ya Gridi ya Taifa** | **3,995.54** | **13,441.68** |
| **Umeme Nje ya Gridi ya Taifa (Off-Grid)** | | |
| Bukoba | 2.60 | 0.09 |
| Mafia | 5.20 | 9.29 |
| Mpanda | 7.50 | 31.99 |
| Sumbawanga | 5.00 | 0.28 |
| Inyonga | - | 1.61 |
| Mtwara1 | 30.40 | 54.33 |
| Mtwara 2 | 40.00 | 58.32 |
| Somanga | 7.50 | 4.84 |
| **Jumla Nje ya Gridi ya Taifa** | **98.2** | **160.75** |
| **Umeme Kutoka Nchi Jirani** | | |
| Uganda (Masaka) | | 152.33 |
| Uganda (Kikagati) | | 58.36 |
| Zambia | | 74.21 |
| **Jumla Umeme Kutoka Nchi Jirani** | | **284.9** |
| **Jumla Kuu** | **4,093.74** | **13,887.32** |

**Chanzo:** Wizara ya Nishati

**Jedwali Na. 61: MAUZO YA UMEME KWA WATUMIAJI MBALIMBALI (Saa za Megawati 000"), MWAKA 2013 - 2025**

| Mwaka | Tanzania Bara | | | Zanzibar | Jumla | Umeme Uliozalishwa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wateja wadogo (D1) | Wateja wa Kati (T1) | Wateja Wakubwa (T2, T3 & T8) | T5+T7 | | |
| 2013 | 280.6 | 1,747.0 | 2,560.4 | 218.7 | 4,806.7 | 5,946.2 |
| 2014 | 217.0 | 1,891.0 | 2,595.0 | 348.5 | 5,051.5 | 6,186.8 |
| 2015 | 148.8 | 2,082.7 | 2,721.1 | 344.6 | 5,297.1 | 6,416.9 |
| 2016 | 345.3 | 2,263.4 | 2,887.2 | 375.6 | 5,871.5 | 7,092.2 |
| 2017 | 301.5 | 2,371.0 | 2,893.3 | 390.4 | 5,956.2 | 7,115.3 |
| 2018 | 319.8 | 2,481.9 | 3,075.0 | 414.0 | 6,290.7 | 7,354.8 |
| 2019 | 307.2 | 2,655.9 | 3,198.1 | 481.5 | 6,642.8 | 7,804.9 |
| 2020 | 325.8 | 2,668.6 | 3,205.1 | 474.9 | 6,674.3 | 7,862.9 |
| 2021 | 339.9 | 2,900.0 | 3,527.0 | 546.3 | 7,313.2 | 8,580.8 |
| 2022 | 351.0 | 3,063.1 | 3,730.6 | 584.9 | 7,729.6 | 9,064.9 |
| 2023 | 393.6 | 3,313.2 | 3,864.2 | 661.0 | 8,232.0 | 10,379.6 |
| 2024 | 430.5 | 3,719.6 | 4,187.5 | 777.1 | 9,114.7 | 11,958.9 |
| 2025 | 438.3 | 3,922.2 | 4,444.4 | 908.1 | 9,713.0 | 13,887.3 |

**Chanzo:** Wizara ya Nishati

**Jedwali Na. 62: MAUZO YA UMEME KWA MIKOA (Saa za Megawati 000"), MWAKA 2019 - 2025**

| Mkoa | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | 179.7 | 177.7 | 228.7 | 249.3 | 297.2 | 336.7 | 384.3 |
| Arusha | 406.3 | 385.6 | 395.6 | 413.9 | 452.1 | 496.6 | 370.7 |
| Manyara | 34.8 | 35.2 | 53.5 | 59.0 | 67.3 | 52.5 | 184.1 |
| Kilimanjaro | 185.2 | 183.9 | 195.2 | 206.3 | 218.7 | 260.9 | 188.1 |
| Tanga | 351.3 | 342.2 | 375.5 | 408.7 | 391.5 | 433.1 | 267.5 |
| Morogoro | 268.0 | 266.8 | 298.5 | 307.3 | 329.7 | 327.3 | 143.4 |
| Pwani | 450.7 | 517.9 | 597.9 | 635.7 | 714.8 | 826.7 | 820.5 |
| Dar-es-Salaam | 2,596.5 | 2,534.0 | 2,652.0 | 2,805.9 | 2,932.0 | 3,188.5 | 2,827.9 |
| Lindi | 29.7 | 30.5 | 33.8 | 36.2 | 41.5 | 44.8 | 60.9 |
| Mtwara | 55.9 | 55.9 | 58.6 | 60.9 | 66.5 | 69.0 | 136.1 |
| Ruvuma | 50.3 | 53.7 | 56.9 | 59.4 | 66.5 | 76.5 | 79.0 |
| Iringa | 108.9 | 109.1 | 117.3 | 123.8 | 133.6 | 147.3 | 140.9 |
| Mbeya | 201.6 | 209.9 | 226.9 | 231.5 | 231.8 | 244.3 | 198.5 |
| Singida | 49.5 | 53.1 | 58.1 | 65.1 | 69.5 | 88.7 | 464.3 |
| Tabora | 68.4 | 69.7 | 76.4 | 77.9 | 80.9 | 89.0 | 127.4 |
| Rukwa | 27.3 | 28.6 | 31.1 | 32.5 | 39.0 | 45.1 | 253.8 |
| Kigoma | 40.3 | 41.0 | 47.5 | 52.3 | 59.6 | 69.6 | 91.2 |
| Shinyanga | 354.1 | 352.2 | 421.7 | 411.2 | 395.3 | 440.3 | 518.7 |
| Kagera | 80.3 | 79.2 | 96.8 | 108.1 | 119.2 | 154.9 | 267.2 |
| Mwanza | 295.2 | 300.9 | 325.6 | 344.5 | 348.4 | 371.6 | 306.7 |
| Mara | 163.9 | 188.1 | 195.5 | 215.1 | 241.2 | 246.1 | 202.8 |
| Njombe | 39.1 | 42.0 | 45.7 | 47.8 | 53.0 | 59.7 | 181.0 |
| Katavi | 13.6 | 16.3 | 21.8 | 24.0 | 27.8 | 36.3 | 128.8 |
| Geita | 53.0 | 60.8 | 77.7 | 83.0 | 96.9 | 123.3 | 227.5 |
| Simiyu | 24.2 | 24.8 | 28.6 | 31.0 | 34.3 | 39.8 | 55.8 |
| Songwe | 33.2 | 40.4 | 50.2 | 54.4 | 62.8 | 68.9 | 177.9 |
| **Jumla Tanzania Bara** | **6,161.0** | **6,199.5** | **6,767.1** | **7,144.8** | **7,571.1** | **8,337.6** | **8,805.0** |
| **Zanzibar** | **481.5** | **474.9** | **546.3** | **584.9** | **661.0** | **777.1** | **908.1** |
| **Jumla kuu** | **6,642.5** | **6,674.4** | **7,313.4** | **7,729.7** | **8,232.1** | **9,114.7** | **9,713.1** |

**Chanzo:** Wizara ya Nishati

## SURA YA 15

## MAJI

**Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji**

361. Mwaka 2025, kiwango cha rasilimali za maji kinachofaa kwa matumizi kiliendelea kuwa wastani wa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka kama kilivyokuwa mwaka 2024. Kati ya kiwango hicho, mita za ujazo bilioni 105 zilikuwa juu ya ardhi na mita za ujazo bilioni 21 zilikuwa chini ya ardhi. Aidha, kwa kuzingatia makadirio ya idadi ya watu ya milioni 66.1 kwa Tanzania Bara mwaka 2025, kiasi cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka kilikuwa wastani wa mita za ujazo 1,907.5. Kiwango hicho ni juu ya wastani wa mita za ujazo 1,700 kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa.

362. Mwaka 2025, mahitaji ya maji kwa matumizi mbalimbali yalikadiriwa kuwa mita za ujazo bilioni 70 kwa mwaka ikilinganishwa na mita za ujazo bilioni 68 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 2.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii pamoja na idadi ya watu. Hadi Desemba 2025, vyanzo vya maji vilivyotambuliwa viliongezeka na kufikia 3,401 kutoka vyanzo 3,339 vilivyotambuliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, vyanzo vilivyowekewa mipaka ili visiharibiwe na shughuli za kibinadamu viliongezeka kwa asilimia 15.1 na kufikia 403 mwaka 2025 kutoka vyanzo 350 vilivyowekewa mipaka mwaka 2024. Ongezeko la vyanzo vya maji vilivyotambuliwa na kuwekewa mipaka lilitokana na kuendelea kwa uwekezaji katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji.

363. Mwaka 2025, vituo vya kufuatilia mwenendo wa maji juu na chini ya ardhi vilikuwa 1,258 ikilinganishwa na vituo 1,181 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 6.5. Hii ilitokana na ukarabati wa vituo 68 na ujenzi wa vituo tisa (9). Kati ya vituo hivyo, vituo 361 vilikuwa vya hali ya hewa; vituo 415 vya kufuatilia maji katika mito, maziwa na mabwawa; vituo 95 vya kufuatilia mwenendo wa maji chini ya ardhi; vituo 33 vya kufuatilia mchanga kwenye mito; na vituo 354 vya ubora wa maji.

**Ubora wa Maji**

364. Mwaka 2025, sampuli 9,012 za maji zilikusanywa na kuhakikiwa ubora ikilinganishwa na sampuli 9,187 zilizokusanywa na kuhakikiwa mwaka 2024. Kati ya sampuli hizo: sampuli 6,591 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya majumbani; sampuli 1,747 za ufuatiliaji wa mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji; sampuli 129 za utafiti, sampuli 32 za matumizi ya viwandani; sampuli 70 za umwagiliaji; sampuli 142 za ujenzi; sampuli 262 za viwanda vya samaki; na sampuli 39 za kupima uwezo wa utendaji kazi wa maabara.

365. Mwaka 2025, sampuli 6,591 za matumizi ya majumbani zilifanyiwa uhakiki wa ubora ikilinganishwa na sampuli 8,457 zilizofanyiwa uhakiki wa ubora mwaka 2024. Kati ya hizo, sampuli 4,291 sawa na asilimia 65.1 zilikidhi viwango vya ubora na usalama wa maji vinavyokubalika kimataifa na sampuli 2,300 hazikukidhi viwango. Kutokidhi kwa viwango kulichangiwa na uwepo wa tope, ugumu wa maji, madini ya *nitrate*, *fluoride*, *manganese* na chuma katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, sampuli za maji 674 kwa ajili ya shughuli za viwandani, umwagiliaji, ujenzi, utafiti, upimaji wa uwezo wa utendaji kazi wa maabara pamoja na viwanda vya samaki zilifanyiwa uhakiki wa ubora ikilinganishwa na sampuli 395 mwaka 2024. Kati ya hizo, sampuli 587, sawa na asilimia 87.1 zilikidhi viwango vya ubora vinavyokubalika kwa matumizi na sampuli 87 hazikukidhi viwango.

366. Mwaka 2025, sampuli 402 za majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira zilikusanywa na kuhakikiwa ubora ikilinganishwa na sampuli 281 zilizokusanywa na kuhakikiwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 43.1. Hii ilitokana na kuendelea kwa uwekezaji katika kuimarisha maabara za ubora wa maji nchini. Aidha, matokeo ya uhakiki yalionesha kuwa sampuli 138, sawa na asilimia 34.3 hazikukidhi viwango vya ubora kutokana na kuwepo kwa viwango vya *Chemical Oxygen Demand (COD), Biological Oxygen Demand (BOD)*, *nitrate* na *phosphate* vilivyozidi viwango vinavyohitajika kwa ajili ya maji kurudishwa kwenye mazingira.

**Huduma ya Maji Vijijini**


367. Mwaka 2025, Serikali iliendelea kuboresha miundombinu ya majisafi vijijini kwa kukamilisha vituo 6,820 vya kuchotea maji vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi 4,153,364 ikilinganishwa na vituo 6,832 vya kuchotea maji vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi 4,976,352 mwaka 2024. Kukamilika kwa vituo hivyo kuliongeza idadi ya vituo vinavyotoa huduma kwa asilimia 4.3 na kufikia vituo 165,295 mwaka 2025 kutoka vituo 158,475 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuendelea kwa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji vijijini. Aidha, kaya zilizounganishwa na huduma ya maji ziliongezeka na kufikia 282,127 mwaka 2025 kutoka kaya 276,464 mwaka 2024. Hadi Desemba 2025, wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji vijijini ulifikia asilimia 85.2 ikilinganishwa na asilimia 83.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (**Kielelezo Na. 15.1)**. Hii ilitokana na kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji vijijini na kuimarishwa kwa taasisi za utoaji huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWSOs).

**Huduma ya Maji Mijini**

368. Mwaka 2025, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mijini ilifikia wastani wa asilimia 92.5 ikilinganishwa na asilimia 91.6 mwaka 2024 (**Kielelezo Na. 15.1)**. Hii ilitokana na kukamilika kwa baadhi ya miradi ya maji inayohudumia wakazi wa maeneo ya mijini. Hadi Desemba 2025, miradi 73 ya maji mijini ilikamilika ikilinganishwa na miradi

68 iliyokamika kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, wateja 1,803,330 waliunganishwa na huduma ya majisafi mwaka 2025 ikilinganishwa na wateja 1,734,646 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 4.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uhitaji wa maji safi na salama kwa shughuli mbalimbali za kijamiii na kiuchumi.

**Kielelezo Na. 15.1: Mwenendo wa Upatikanaji wa Huduma ya Maji Mijini na Vijijini, Mwaka 2021 - 2025**




369. Mwaka 2025, uzalishaji wa maji unaojumuisha miji mikuu ya mikoa, mamlaka za maji za miradi ya kitaifa na miji mikuu na midogo ya wilaya ulikuwa mita za ujazo milioni 468.5 ikilinganishwa na uzalishaji wa mita za ujazo milioni 399.9 mwaka 2024. Aidha, mapato yaliyotokana na mauzo ya majisafi na salama yalikuwa shilingi bilioni 451.1 mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 409.4 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 10.2. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya maji kwa shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

**Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa**

370. Mwaka 2025, visima 1,902 vilichimbwa katika maeneo mbalimbali nchini ikilinganishwa na visima 2,034 mwaka 2024. Uchimbaji wa visima ulitokana na uwekezaji wa sekta binafsi na juhudi za Serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi. Kati ya visima hivyo, Bonde la Maji la Ziwa Tanganyika vilichimbwa visima 104, Bonde la Maji la Ziwa Rukwa visima 112, Bonde la Maji la Ziwa Nyasa (15), Bonde la Maji la Pangani (177), Bonde la Kati (420), Bonde la Maji la Rufiji (132), Bonde

la Maji la Ruvuma na Pwani ya Kusini (73), Bonde la Maji la Wami/Ruvu (703) na Bonde la Maji la Ziwa Victoria (166).

371. Mwaka 2025, Serikali iliendelea na ujenzi wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua ili kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji nchini. Katika kipindi hicho, mabwawa saba (7) ya matumizi mbalimbali ikiwemo kuvuna maji ya mvua yalijengwa ikilinganishwa na mabwawa nane (8) yaliyojengwa mwaka 2024. Mabwawa hayo yalijengwa katika maeneo ya Malambo na Soitsambu (Ngorongoro), Gidahababiegi (Hanang); Langai (Simanjiro), Bugarama na Mwamasindike (Maswa) na Mwambazi (Sumbawanga).

**Uondoaji wa Majitaka**

372. Mwaka 2025, mtandao wa majitaka ulifikia urefu wa kilomita 1,532 kutoka kilomita 1,514.6 mwaka 2024. Katika kipindi hicho, wateja waliounganishwa katika mtandao wa majitaka walifikia 130,353 kutoka wateja 118,114 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 10.4. Hii ilitokana na kukamilika kwa mradi wa usafi wa mazingira katika mji wa Musoma. Hadi Desemba 2025, mradi mmoja (1) wa uondoshaji wa majitaka usiotumia mfumo wa mabomba ulikamilika katika mji wa Shinyanga na kufikisha miji 17 inayotumia mfumo huo.

**Jedwali Na. 63: UZALISHAJI WA MAJI NA MAPATO YATOKANAYONA MAJI MIJINI, MWAKA 2024 - 2025**

| **A. MAMLAKA ZA MAJI ZA MIJI MIKUU YA MIKOA (RWSSA)** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **2024** | | **2025** | |
| **Mamlaka ya Maji** | **Uzalishaji (Mita za Ujazo)** | **Mapato (Shilingi)** | **Uzalishaji (Mita za Ujazo)** | **Mapato (Shilingi)** |
| Arusha | 29,910,310 | 24,853,605,909.80 | 30,283,027.00 | 30,327,151,888.80 |
| Babati | 4,046,479 | 5,176,143,778.60 | 6,208,722.00 | 7,751,603,202.70 |
| Bukoba | 3,821,822.55 | 4,948,455,950.59 | 4,348,389.00 | 5,869,346,614.24 |
| Dodoma | 22,074,907 | 26,939,287,694.42 | 24,844,464.24 | 30,609,540,237.75 |
| DAWASA | 128,430,974 | 142,457,866,444.50 | 161,434,183.00 | 138,726,419,053.04 |
| Geita | 1,903,596.50 | 1,779,321,430 | 2,486,611.00 | 2,141,017,512.48 |
| Iringa | 6,842,191 | 9,357,492,342.35 | 7,968,411.00 | 10,830,277,762.12 |
| Kigoma | 4,302,722 | 4,264,177,966.83 | 4,305,201.00 | 4,616,751,789.23 |
| Lindi | 825,297.09 | 1,047,789,152.28 | 893,813.00 | 1,281,351,232.75 |
| Mpanda | 1,690,351.28 | 1,057,504,344.50 | 1,805,658.00 | 1,365,560,557.61 |
| Mbeya | 16,983,394 | 14,877,554,873.70 | 18,838,241.00 | 18,055,936,378.43 |
| Morogoro | 13,204,380 | 13,017,394,443.97 | 16,234,973.08 | 13,892,666,947.63 |
| Moshi | 15,133,589 | 12,077,739,739.30 | 16,116,420.00 | 13,596,659,710.00 |
| Mtwara | 4,571,368 | 4,681,361,139 | 4,538,814.00 | 4,725,801,612.00 |
| Musoma | 7,166,728.75 | 4,820,954,561.95 | 7,877,995.43 | 5,683,178,193.00 |
| Mwanza | 32,506,489 | 28,817,580,006.74 | 39,361,704.00 | 33,007,849,089.73 |
| Njombe | 1,192,753 | 1,235,981,614.30 | 1,291,613.40 | 1,504,390,577.71 |
| Bariadi | 792,598.65 | 573,693,695.80 | 1,001,145.80 | 929,921,783.76 |
| Kahama | 5,296,706 | 9,351,795,738.25 | 6,503,341.00 | 11,581,676,750.52 |
| Singida | 3,860,851 | 4,368,522,065 | 4,014,887.00 | 4,724,615,728.39 |
| Songea | 3,054,507 | 4,148,976,894 | 3,295,603.65 | 4,448,382,378.98 |
| Sumbawanga | 2,080,663 | 2,299,933,211.65 | 2,240,806.50 | 2,576,048,229.45 |
| Tabora | 5,662,197 | 8,742,194,182.47 | 6,448,538.25 | 10,332,563,901.49 |
| Shinyanga | 5,439,369 | 9,334,937,296.92 | 6,610,101.00 | 11,714,239,900.40 |
| Tanga | 12,817,591 | 15,692,481,071.81 | 14,178,351.22 | 17,350,729,819.71 |
| Vwawa-Mlowo | 460,265 | 212,112,523 | 493,337.60 | 330,077,701.00 |
| **Jumla - RWSSA** | **334,072,100** | **356,134,858,072** | **393,624,352.17** | **387,973,758,552.92** |


| **B. MAMLAKA ZA MAJI ZA MIRADI YA KITAIFA (NWP)** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **2024** | | **2025** | |
| **Mamlaka ya Maji** | **Uzalishaji (Mita za Ujazo)** | **Mapato (Shilingi)** | **Uzalishaji (Mita za Ujazo)** | **Mapato (Shilingi)** |
| Wanging'ombe | 594,936 | 516,850,512.65 | 652,837.0 | 559,410,068.21 |
| Kahama Shinyanga | 22,946,316 | 19,215,386,395 | 27,389,205.0 | 22,198,369,863.35 |
| Mugango Kiabakari | 113,416 | 124,152,040.98 | 616,624.0 | 292,940,034.41 |
| Masasi Nachingwea | 2,448,638 | 2,844,822,240 | 2,731,168.0 | 3,101,608,381.31 |
| Makonde | 794,252 | 865,643,748.96 | 872,853.0 | 1,216,576,939.79 |
| Maswa | 1,030,434.60 | 757,912,360 | 806,951.1 | 974,286,330.00 |
| HTM (Handeni Trunk Main) | 2,684,825.20 | 1,185,581,857 | 1,913,312.0 | 1,526,994,600.00 |
| **Jumla - NWP** | **30,612,818** | **25,510,349,155** | **34,982,950.1** | **29,870,186,217.07** |

**Jedwali Na. 63: Linaendelea**

| C. MAMLAKA ZA MAJI ZA MIJI MIKUU NA MIDOGO YA WILAYA (DTWSSA) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mamlaka ya Maji** | **2024** | | **2025** | |
| | **Uzalishaji (Mita za Ujazo)** | **Mapato (Shilingi)** | **Uzalishaji (Mita za Ujazo)** | **Mapato (Shilingi)** |
| Karatu | 1,362,240 | 1,064,503,558 | 1,638,846.26 | 1,429,852,809.09 |
| Kondoa | 517,567 | 463,785,280 | 721,112.00 | 496,685,643.25 |
| Mpwapwa | 753,813 | 523,603,796 | 570,001.30 | 541,431,178.65 |
| Ludewa | 405,485 | 75,037,660 | 514,638.00 | 87,203,468.20 |
| Makete | 366,938 | 200,079,129 | 401,886.00 | 221,310,230.00 |
| Mafinga | 868,160 | 582,908,223 | 808,503.00 | 616,840,327.08 |
| Makambako | 861,974 | 767,776,200 | 659,490.05 | 637,064,873.00 |
| Biharamulo | 531,812 | 337,551,807 | 691,894.00 | 419,332,395.72 |
| Ngara | 653,467 | 353,053,709 | 556,683.00 | 445,417,759.43 |
| Kasulu | 2,605,092.70 | 360,802,781 | 2,212,193.00 | 478,773,733.61 |
| Same-Mwanga | 848,493 | 504,193,937 | 2,958,109.00 | 1,082,924,193.18 |
| Kilwa Masoko | 543,294.68 | 320,429,341 | 500,045.00 | 301,657,590.00 |
| Loliondo | 127,089 | 190,486,645 | 165,114.00 | 246,596,558.00 |
| Kiteto Kibaya | 184,252 | 210,565,786.70 | 260,401.06 | 286,045,455.79 |
| Mbulu | 847,790 | 558,118,048.22 | 510,645.00 | 271,261,487.30 |
| Bunda | 1,109,148 | 1,482,506,024.25 | 1,083,482.17 | 1,449,366,981.94 |
| Orkesumet | 178,095 | 337,823,000 | 178,095.00 | 337,823,000.00 |
| Sengerema | 1,504,470 | 1,271,169,906 | 1,645,930.00 | 1,447,454,195.28 |
| Chunya | 108,257 | 88,844,720 | 122,802.00 | 180,554,000.00 |
| Itumba Isongele | 610,396 | 66,990,185.67 | 605,732.00 | 63,365,852.00 |
| Kyela-Kasumulu | 1,674,713 | 136,372,174.85 | 1,828,171.00 | 147,182,307.40 |
| Mbarali Rujewa | 663,442 | 135,971,594 | 759,612.60 | 140,582,833.76 |
| Rungwe Tukuyu | 3,709,395 | 373,582,485 | 3,995,288.00 | 399,654,972.34 |
| Ifakara | 479,185 | 109,805,527.26 | 450,459.00 | 150,801,628.75 |
| Kilosa | 498,482 | 312,097,280 | 498,482.00 | 312,097,280.00 |
| Mahenge | 13,133 | 121,621,229 | 13,133.00 | 121,621,229.00 |
| Morogoro Mikumi | 234,547 | 265,759,895 | 234,547.00 | 265,759,895.00 |
| Rufiji Utete | 130,315 | 96,016,354.36 | 185,294.00 | 134,667,325.80 |
| Namtumbo | 358,612.56 | 164,978,569 | 399,695.00 | 202,319,179.50 |
| Kahama | 5,296,706 | 9,351,795,738.25 | 6,503,341.00 | 11,581,676,750.52 |
| Kishapu | 201,240 | 283,146,284 | 275,400.00 | 333,119,005.00 |
| Maganzo | 98,670 | 165,793,728 | 202,630.00 | 212,112,180.00 |
| Mwanhuzi | 276,401 | 263,376,171.20 | 293,502.00 | 280,595,633.95 |
| Maswa | 1,030,434.60 | 757,912,360 | 806,951.10 | 974,286,330.00 |
| Manyoni | 616,783 | 561,690,983.90 | 817,593.00 | 734,712,946.15 |
| Korogwe | 480,205 | 433,949,873 | 480,205.00 | 433,949,873.00 |
| Lushoto | 489,596.40 | 294,718,993 | 471,304.86 | 310,858,407.00 |
| Korogwe Mombo | 579,254 | 148,250,389 | 579,254.00 | 148,250,389.00 |
| Songe | 71,369 | 64,872,979 | 108,978.00 | 117,038,111.00 |
| Igunga | 1,391,465 | 1,836,015,647.88 | 1,784,733.00 | 2,474,866,839.64 |
| Nzega | 1,202,285 | 1,737,630,749.60 | 1,495,118.00 | 2,173,572,641.79 |
| Turiani | 749,413.33 | 420,371,639.60 | 913,661.00 | 576,291,815.15 |
| **Jumla - DTWSSA** | **35,233,480** | **27,795,960,382** | **39,902,954.40** | **33,266,979,305.27** |
| **Jumla Kuu (A+B+C)** | **399,918,398** | **409,441,167,609** | **468,510,257** | **451,110,924,075** |

**Chanzo**: Wizara ya Maji

**Kielelezo Na. 15.2: Mchanganuo wa Mapato ya Mamlaka za Maji za Miji Mikuu ya Mikoa Mwaka 2025**



**Jedwali Na. 64: KIWANGO CHA UPATIKANAJI WA MAJI KATIKA MIJI MIKUU YA MIKOA MWAKA 2025**

| Mji | Idadi ya Watu ya Sensa, 2022 | Makadario ya Idadi ya watu | Idadi ya Watu Waliofikiwa na Huduma | Watu Waliofikiwa na Huduma (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Arusha Jiji | 617,631 | 682,282 | 680,952 | 99.8 |
| Dar es Salaam | 5,383,728 | 5,757,282 | 5,448,952 | 94.6 |
| Kibaha Manispaa | 265,360 | 329,664 | 305,934 | 92.8 |
| Dodoma Jiji | 629,020 | 695,286 | 668,332 | 96.1 |
| Geita Mjini | 361,671 | 404,279 | 368,389 | 91.1 |
| Iringa Manispaa | 265,249 | 288,205 | 284,478 | 98.7 |
| Bukoba Manispaa | 144,938 | 161,609 | 157,136 | 97.2 |
| Mpanda Manispaa | 245,764 | 277,739 | 199,348 | 71.8 |
| Kigoma Manispaa | 267,608 | 310,747 | 275,945 | 88.8 |
| Moshi Manispaa | 221,733 | 240,478 | 239,826 | 99.7 |
| Lindi Manispaa | 100,748 | 110,733 | 91,087 | 82.3 |
| Babati Mjini | 129,572 | 136,930 | 134,608 | 98.3 |
| Musoma Manispaa | 164,172 | 184,520 | 183,820 | 99.6 |
| Mbeya Jiji | 541,603 | 592,187 | 542,114 | 91.5 |
| Morogoro Manispaa | 474,409 | 515,638 | 424,472 | 82.3 |
| Mtwara Manispaa | 146,772 | 158,822 | 149,325 | 94.0 |
| Mwanza Jiji | 1,104,521 | 1,230,320 | 1,119,892 | 91.0 |
| Njombe Mjini | 90,353 | 97,154 | 81,459 | 83.8 |
| Sumbawanga Manispaa | 204,785 | 233,058 | 221,021 | 94.8 |
| Songea Manispaa | 286,285 | 307,963 | 296,353 | 96.2 |
| Shinyanga Manispaa | 214,744 | 239,640 | 186,364 | 77.8 |
| Bariadi Mjini | 260,927 | 295,864 | 214,489 | 72.5 |
| Singida Manispaa | 233,161 | 259,813 | 234,730 | 90.3 |
| Vwawa-Mlowo | 133,830 | 146,240 | 82,847 | 56.7 |
| Tabora Manispaa | 308,741 | 346,921 | 331,505 | 95.6 |
| Tanga Jiji | 393,429 | 402,180 | 402,180 | 100 |
| **Jumla** | **13,190,754** | **14,405,554** | **13,325,558** | **92.5** |

**Chanzo:** Wizara ya Maji

# SURA YA 16

## ELIMU, MAFUNZO NA TEKNOLOJIA

**Elimu ya Awali**

373. Mwaka 2025, wanafunzi 1,656,726 (wasichana 816,669 na wavulana 840,057) waliandikishwa katika elimu ya awali ikilinganishwa na wanafunzi 1,676,559 walioandikishwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 1.2. Kati ya walioandikishwa wanafunzi 7,211 (wasichana 3,091 na wavulana 4,120) walikuwa wenye mahitaji maalum mwaka 2025 ikilinganishwa na wanafunzi 7,323 wenye mahitaji maalum mwaka 2024. Katika kipindi hicho, wanafunzi walioandikishwa katika shule za Serikali walikuwa 1,523,955 (wasichana 751,683 na wavulana 772,272) ikilinganishwa na wanafunzi 1,558,549 walioandikishwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 2.2. Aidha, wanafunzi walioandikishwa katika shule zisizo za Serikali walikuwa 132,771 mwaka 2025 ikilinganishwa na wanafunzi 118,010 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 12.5. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa elimu kufuatia maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la Mwaka 2023.

374. Mwaka 2025, idadi ya walimu katika shule za awali za Serikali iliongezeka kwa asilimia 6.7 na kufikia 13,921 (wanawake 9,330 na wanaume 4,591) kutoka walimu 13,042 mwaka 2024. Hii ilitokana na Serikali kuendelea kuajiri walimu ili kukabiliana na upungufu wa walimu. Kati ya hao, walimu wenye sifa za kufundisha elimu ya awali walikuwa 11,342 mwaka 2025 ikilinganishwa na walimu 10,348 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 8.76. Aidha, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi wa elimu ya awali ulifikia 1:109 mwaka 2025 ikilinganishwa na uwiano wa 1:120 mwaka 2024. Uwiano huo ulizidi kiwango cha uwiano wa 1:25 unaokubalika kitaifa.

**Elimu ya Msingi**

375. Mwaka 2025, idadi ya shule za msingi zilifikia 20,889 kutoka shule 20,533 mwaka 2024. Kati ya hizo, shule za Serikali zilikuwa 18,158 ikilinganishwa na shule 18,055 mwaka 2024. Ongezeko la idadi ya shule lilitokana na juhudi za Serikali katika kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na shule ya msingi. Katika kipindi hicho, shule zisizo za Serikali zilifikia 2,731 kutoka shule 2,478 mwaka 2024.

376. Mwaka 2025, idadi ya wanafunzi katika shule za elimu ya msingi ilikuwa 11,428,424 (wasichana 5,846,697 na wavulana 5,581,727) ikilinganishwa na wanafunzi 11,391,185 mwaka 2024. Katika kipindi hicho, wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za elimu ya msingi walikuwa 82,224 (wasichana 35,856 na wavulana 46,368) ikilinganishwa na wanafunzi 78,106 mwaka 2024. Aidha, idadi ya wanafunzi katika shule za msingi za Serikali ilikuwa 10,709,153 (wasichana 5,486,281 na wavulana 5,222,872)

mwaka 2025 ikilinganishwa na wanafunzi 10,739,975 mwaka 2024. Vilevile, idadi ya wanafunzi katika shule zisizo za Serikali ilikuwa 719,271 (wasichana 360,416 na wavulana 358,855) mwaka 2025 ikilinganishwa na wanafunzi 651,210 mwaka 2024. Kwa upande mwingine, wanafunzi waliokatisha masomo kutokana na vifo, utovu wa nidhamu na utoro walikuwa 139,192 (wasichana 60,085 na wavulana 79,107) mwaka 2025 ikilinganishwa na wanafunzi 158,555 mwaka 2024.

377. Mwaka 2025, idadi ya watahiniwa waliofanya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi walikuwa 1,146,164 ikilinganishwa na watahiniwa 1,204,899 mwaka 2024. Kati ya hao, watahiniwa 937,551 (wasichana 508,447 na wavulana 429,104) walifaulu, sawa na asilimia 81.8 ya ufaulu mwaka 2025 ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 80.9 mwaka 2024.

378. Mwaka 2025, idadi ya walimu katika shule za elimu ya msingi za Serikali ilikuwa 195,726 (wanawake 95,543 na wanaume 100,183) ikilinganishwa walimu 194,367 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za Serikali kuendelea kuajiri walimu katika shule za elimu ya msingi. Katika kipindi hicho, idadi ya walimu katika shule za elimu ya msingi zisizo za Serikali ilikuwa 38,798 (wanawake 17,059 na wanaume 21,739) ikilinganishwa walimu 35,473 mwaka 2024. Aidha, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi wa shule za elimu ya msingi ulikuwa 1:49 mwaka 2025 ikilinganishwa na 1:50 mwaka 2024. Uwiano huo uliendelea kuwa juu ya kiwango cha 1:45 kinachokubalika kitaifa.

**Elimu ya Sekondari**

379. Mwaka 2025, idadi ya shule za sekondari iliongezeka kwa asilimia 3.5 na kufikia 6,488 ikilinganishwa na shule 6,269 mwaka 2024. Kati ya hizo, shule 5,092 zilikuwa za Serikali na shule 1,396 zisizo za Serikali. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi katika kuongeza idadi ya madarasa na shule mpya za sekondari ili kukabiliana na idadi kubwa ya wanafunzi waliohitimu darasa la saba na kujiunga na kidato cha kwanza.

380. Mwaka 2025, idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita ilikuwa 3,425,822 ikilinganishwa na wanafunzi 3,314,198 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 3.4. Kati ya hao, wasichana walikuwa 1,839,570 na wavulana 1,586,252. Katika kipindi hicho, wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za sekondari walikuwa 16,409 (wasichana 8,448 na wavulana 7,961) ikilinganishwa na wanafunzi 15,179 mwaka 2024. Aidha, idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari za Serikali ilikuwa 3,090,691 (wasichana 1,663,662 na wavulana 1,427,029) mwaka 2025 ikilinganishwa na wanafunzi 2,999,530 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 3.0.

381. Mwaka 2025, idadi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne ilikuwa 3,176,455 ikilinganishwa na wanafunzi 3,087,870 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 2.9. Kati ya hao, wanafunzi katika shule za Serikali walikuwa 2,879,066 mwaka 2025 ikilinganishwa na wanafunzi 2,811,848 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 2.4. Hii ilitokana na idadi kubwa ya wanafunzi waliohitimu darasa la saba kujiunga na kidato cha kwanza kufuatia utekelezaji wa programu ya elimu msingi bila ada. Kwa upande mwingine, idadi ya wanafunzi waliokatisha masomo kutokana na vifo, utovu wa nidhamu na utoro ilikuwa 100,998 (wasichana 50,059 na wavulana 50,939) mwaka 2025 ikilinganishwa na wanafunzi 148,337 mwaka 2024.

382. Mwaka 2025, watahiniwa waliofanya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne walikuwa 569,883 (wasichana 303,859 na wavulana 266,024), ikilinganishwa na watahiniwa 517,460 waliofanya mtihani mwaka 2024. Kati yao, watahiniwa 526,620 (wasichana 281,694 na wavulana 244,926) walifaulu, sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 92.4 mwaka 2025 kama ilivyokuwa mwaka 2024. Aidha, watahiniwa 79 wa kidato cha nne waliofanya mtihani walifutiwa matokeo kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo udanganyifu na utovu wa nidhamu mwaka 2025, ikilinganishwa na watahiniwa 765 mwaka 2024. Kwa upande mwingine, watahiniwa waliofanya mtihani wa kuhitimu kidato cha sita mwaka 2025 walikuwa 126,135 (wasichana 61,953 na wavulana 64,182), ikilinganishwa na watahiniwa 103,812 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 21.5. Kati yao, watahiniwa 125,779 (wasichana 61,953 na wavulana 63,826) walifaulu, sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 99.7 mwaka 2025, ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 99.9 mwaka 2024. Vilevile, watahiniwa 70 walifutiwa matokeo kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo udanganyifu na utovu wa nidhamu mwaka 2025, ikilinganishwa na watahiniwa 476 waliofutiwa mwaka 2024.

383. Mwaka 2025, idadi ya walimu katika shule za sekondari za Serikali ilifikia 114,408 (wanawake 38,219 na wanaume 76,189) kutoka walimu 106,631 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 7.3. Hii ilitokana na jitihada za Serikali katika kuendelea kuajiri walimu. Aidha, idadi ya walimu katika shule za sekondari zisizo za Serikali iliongezeka kwa asilimia 9.9 na kufikia 24,228 (wanawake 5,796 na wanaume 18,432) mwaka 2025 kutoka walimu 22,055 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuajiriwa kwa walimu wapya kulikochangiwa na ongezeko la shule zisizo za Serikali.

**Elimu katika Vyuo vya Ualimu**

384. Mwaka 2024/25, wanachuo katika vyuo vya ualimu waliodahiliwa walikuwa 25,716 (wanawake 11,715 na wanaume 14,001) ikilinganishwa na wanachuo 20,261 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 21.2 Hii ilitokana na kuendelea kwa maboresho ya mazingira na miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya ualimu. Aidha, wanachuo waliohitimu mafunzo ya ualimu katika ngazi ya stashahada na astashahada

walikuwa 10,675 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na wanachuo 7,918 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 25.8

**Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu**

385. Mwaka 2024/25, taasisi 11,719 za elimu zilikaguliwa ikilinganishwa na taasisi 10,026 zilizokaguliwa mwaka 2023/24. Kuongezeka kwa taasisi zilizokaguliwa kulitokana na kuimarishwa kwa mazingira ya utendaji kazi katika Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule za mikoa na wilaya (**Jedwali Na. 16.1**).

**Jedwali Na. 16.1: Tathmini za Asasi za Elimu, Mwaka 2023/24 - 2024/25**

| Taasisi/ Shule/Vyuo/Vituo | 2023/2024 | 2024/2025 |
|---|---:|---:|
| Shule za Awali na Msingi | 7,837 | 10,050 |
| Shule za Sekondari | 2,137 | 1,640 |
| Vyuo vya Ualimu | 44 | 27 |
| FDCS | 7 | 55 |
| Vituo nje ya mfumo rasmi | | 67 |
| **Jumla** | **10,026** | **11,719** |

**Chanzo:** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**Elimu ya Ufundi na Mafunzo**

386. Mwaka 2024/25, idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ilikuwa 217,204 (wanawake 102,045 na wanaume 115,159) ikilinganishwa na wanafunzi 206,617 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 5.1. katika kipindi hicho. Hii ilitokana na kuongezeka kwa Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo - TET vilivyosajiliwa na kufikia 527 mwaka 2024/2025 kutoka vyuo 490 mwaka 2023/2024. Idadi ya wanafunzi waliomaliza masomo katika vyuo hivyo ilikuwa 129,766 (wanawake 68,492 na wanaume 61,274) mwaka 2024/25 ikilinganishwa na wanafunzi 141,714 mwaka 2023/24, sawa na upungufu wa asilimia 8.4.

**Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi**

387. Mwaka 2024/25, vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi - VET vilidahili wanafunzi 462,224 (wanawake 200,454 na wanaume 261,770) ikilinganishwa na wanafunzi 440,551 kwa mwaka 2023/24. Ongezeko la udahili lilitokana na uanzishwaji wa mafunzo katika vyuo vipya 29 na upanuzi wa vyuo 10. Aidha, wanafunzi 30,785 walihitimu mafunzo ya ufundi stadi kwa kozi za muda mrefu katika vyuo vya VET mwaka 2024/25 ikilinganishwa na wanafunzi 27,676 mwaka 2023/24. Vilevile, vyuo vya elimu ya ufundi stadi - VET viliongezeka kwa asilimia 4.2 na kufikia 953 mwaka 2025 kutoka vyuo 915 mwaka 2024.

388. Mwaka 2024/25, idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi - FDCs ilikuwa 21,104 (wanawake 8,679 na wanaume 12,425) ikilinganishwa na

wanafunzi 17,506 mwaka 2023/24. Katika kipindi hicho, wanafunzi 18,200 walihitimu mafunzo katika vyuo vya FDCs ikilinganishwa na wanafunzi 13,783 waliohitimu mwaka 2023/24. Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi kulitokana na Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia pamoja na kuanzishwa kwa program mpya za masomo.

**Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

389. Mwaka 2024/25, Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha - NM-AIST ilidahili wanafunzi 184 (wanawake 54 na wanaume 130) ikilinganishwa na wanafunzi 148 waliodahiliwa mwaka 2023/24. Aidha, wanafunzi 164 (wanawake 44 na wanaume 120) walihitimu mwaka 2024/25 ikilinganishwa na wanafunzi 92 waliohitimu mwaka 2023/24, sawa na upungufu wa asilimia 8.6. Hii ilitokana na kupungua kwa idadi ya wanafunzi waliofadhiliwa na Mradi wa Vituo vya Umahiri (African Centres of Excellence - ACE II). Kwa upande mwingine, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya - MUST kilidahili wanafunzi 12,815 (wanawake 2,998 na wanaume 9,817) mwaka 2024/25 ikilinganishwa na wanafunzi 12,643 waliodahiliwa mwaka 2023/24. Aidha, wanafunzi 2,876 (wanawake 766 na wanaume 2,110) walihitimu katika chuo cha MUST ikilinganishwa na wanafunzi 2,494 waliohitimu mwaka 2023/24.

390. Mwaka 2024/25, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ilidahili wanafunzi 8,166 (wanawake 2,484 na wanaume 5,682) ikilinganishwa na wanafunzi 8,86 waliodahiliwa mwaka 2023/24. Katika kipindi hicho, wanafunzi 1,403 (wanawake 358 na wanaume 1,045) walihitimu ikilinganishwa na wanafunzi 1,522 waliohitimu mwaka 2023/24. Kwa upande mwingine, Chuo cha Ufundi Arusha kilidahili wanafunzi 5,723 (wanawake 1417 na wanaume 4,308) mwaka 2024/25 ikilinganishwa na wanafunzi 2,877 waliodahiliwa mwaka 2023/24. Aidha, wanafunzi 907 (wanawake 244 na wanaume 663) walihitimu katika Chuo cha Ufundi Arusha mwaka 2024/25 ikilinganishwa na wanafunzi 1,139 waliohitimu mwaka 2023/24.

**Elimu ya Juu**

391. Hadi Desemba 2025, taasisi za elimu ya juu nchini zilikuwa 55 (taasisi za Serikali 21 na binafsi 34) ikilinganishwa na taasisi 54 zilizokuwepo mwaka 2024. Kati ya taasisi hizo, vyuo vikuu vilikuwa 36, vyuo vikuu vishiriki 14 na vituo vya vyuo vikuu vitano (5). Katika kipindi hicho, wanafunzi katika taasisi za elimu ya juu walikuwa 361,257 (wanawake 196,239 na wanaume 165,018) ikilinganishwa na wanafunzi 334,854 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 7.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa wanafunzi wanaohitimu elimu ya sekondari na vyuo vya elimu ya kati, upatikanaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu pamoja na kuongezeka kwa programu zinazotolewa. Aidha, wanafunzi 62,570 (wanawake 30,651 na wanaume 31,919) walihitimu vyuo vikuu mwaka 2024 ikilinganishwa na wanafunzi 56,520 waliohitimu mwaka 2023. Vilevile, idadi ya wanataaluma katika vyuo

vikuu ilikuwa 8,709 (wanawake 2,700 na wanaume 6,009) ikilinganishwa na wanataaluma 8,565 mwaka 2023/24. Kwa upande mwingine, wanafunzi 3,025 (wanawake 1,313 na wanaume 1,712) waliacha masomo mwaka 2023/24 ikilinganishwa na wanafunzi 2,839 walioacha masomo mwaka 2022/23. Ongezeko la wanafunzi waliacha masomo lilitokana na kushindwa masomo, kufutiwa usajili, kuahirisha masomo na kufariki.

392. Mwaka 2024/25, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 787.4 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 786.7 iliyotolewa mwaka 2023/24. Mikopo hiyo iliwanufaisha wanafunzi 246,924 ikilinganishwa na wanafunzi 227,998 walionufaika mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 8.3 Aidha, shilingi bilioni 7.631 zilitolewa kupitia SAMIA Scholarship kwa wanafunzi 1,407 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6.429 zilizotolewa kwa wanafunzi 1,228 mwaka 2023/24.

**Udhibiti wa Mionzi**

393. Mwaka 2024/25, Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania - TAEC ilisajili vyanzo vipya vya mionzi 234 ikilinganishwa na vyanzo 209 vilivyosajiliwa mwaka 2023/2024, sawa na ongezeko la asilimia 12.0. Katika kipindi hicho, TAEC ilitoa leseni 866 ikilinganishwa na leseni 595 zilizotolewa mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 45.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa maombi ya leseni yaliyowasilishwa. Aidha, TAEC ilitoa vyeti 302 kwa wataalamu wapya wa mionzi mwaka 2024/25 ikilinganishwa na vyeti 416 vilivyotolewa mwaka 2023/24. Kwa upande mwingine, shehena 58,016 zinazohusiana na mnyororo wa chakula katika maeneo ya mipakani zilikaguliwa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na shehena 67,996 zilizokaguliwa mwaka 2023/24, sawa na upungufu wa asilimia 14.7. Kaguzi hizo zililenga kuhakikisha usalama wa mionzi na kudhibiti usafirishaji haramu wa vyanzo vya mionzi.

394. Mwaka 2024/25, TAEC ilikagua vituo 728 vya mionzi ikilinganishwa na vituo 932 vilivyokaguliwa mwaka 2023/24, sawa na upungufu wa asilimia 21.9. Katika kipindi hicho, vifaa 90 vilihakikiwa ubora ikilinganishwa na vifaa 60 vilivyohakikiwa mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 50.0. Aidha, wafanyakazi 1,633 kutoka vituo 460 vinavyotumia mionzi walifuatiliwa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na wafanyakazi 1,627 kutoka vituo 506 waliofuatiliwa mwaka 2023/24. Vilevile, TAEC ilipokea na kupima viwango vya mionzi kwenye sampuli 47,913 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na sampuli 41,544 zilizopimwa mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 13.3. Kati ya hizo, sampuli 13,212 zilikuwa za vyakula kutoka nje, sampuli 33,155 za vyakula vilivyosafirishwa nje ya nchi na sampuli 1,476 zilikuwa za mbolea na tumbaku. Matokeo yalionesha kuwa sampuli zote zilizopimwa hazikuwa na uchafuzi wa viasili vya mionzi.

**Jedwali Na. 65: SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO, MWAKA 2010 - 2025**

| Mwaka | I | II | III | IV | V | VI | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2010 | 382,207 | 398,870 | 293,519 | 279,995 | 26,065 | 20,674 | 1,401,330 |
| 2011 | 403,873 | 396,724 | 380,528 | 279,117 | 30,265 | 25,164 | 1,515,671 |
| 2012 | 457,321 | 386,250 | 355,740 | 343,376 | 31,206 | 28,859 | 1,602,752 |
| 2013 | 444,532 | 506,036 | 193,901 | 302,963 | 30,581 | 26,698 | 1,504,711 |
| 2014 | 479,089 | 506,170 | 356,787 | 178,246 | 33,619 | 26,899 | 1,580,810 |
| 2015 | - | - | - | - | - | - | - |
| 2016 | 467,982 | 366,396 | 263,981 | 278,690 | 45,533 | 47,007 | 1,469,589 |
| 2017 | 491,535 | 443,614 | 296,034 | 236,775 | 53,749 | 43,494 | 1,565,201 |
| 2018 | 587,186 | 480,327 | 358,960 | 278,239 | 57,287 | 52,687 | 1,814,686 |
| 2019 | 637,335 | 555,087 | 388,029 | 334,284 | 52,428 | 56,042 | 2,023,205 |
| 2020 | 659,661 | 588,561 | 454,139 | 360,356 | 58,402 | 51,138 | 2,172,257 |
| 2021 | 718,592 | 616,791 | 498,703 | 422,403 | 66,576 | 56,880 | 2,379,945 |
| 2022 | 784,061 | 648,525 | 499,958 | 454,981 | 77,873 | 64,301 | 2,529,699 |
| 2023 | 952,657 | 719,377 | 486,848 | 459,443 | 82,069 | 74,553 | 2,774,947 |
| 2024 | 981,013 | 845,297 | 538,667 | 446,871 | 108,451 | 79,231 | 2,999,530 |
| 2025 | 889,315 | 870,017 | 630,270 | 489,464 | 109,261 | 102,364 | 3,090,691 |
| **Badiliko (Asilimia) 2024 - 2025** | **-9.3** | **2.9** | **17.0** | **9.5** | **0.7** | **29.2** | **3.0** |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia

- Takwimu Hazikupatikana

**Jedwali Na. 66: SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO, MWAKA 2010 - 2025**

| Mwaka | I | II | III | IV | V | VI | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2010 | 56,620 | 57,876 | 50,778 | 46,820 | 12,269 | 13,006 | 237,369 |
| 2011 | 63,282 | 67,205 | 65,859 | 54,521 | 11,083 | 11,926 | 273,876 |
| 2012 | 65,058 | 69,403 | 64,453 | 61,209 | 9,684 | 11,713 | 281,520 |
| 2013 | 70,060 | 77,407 | 67,998 | 65,637 | 8,592 | 9,651 | 299,345 |
| 2014 | 109,784 | 96,732 | 76,574 | 66,898 | 8,865 | 7,686 | 366,539 |
| 2015 | - | - | - | - | - | - | |
| 2016 | 70,844 | 81,499 | 72,970 | 73,231 | 21,091 | 17,731 | 337,366 |
| 2017 | 71,160 | 79,548 | 77,168 | 72,056 | 24,146 | 19,578 | 343,656 |
| 2018 | 64,844 | 71,685 | 74,932 | 74,848 | 24,030 | 23,441 | 333,780 |
| 2019 | 63,629 | 64,488 | 68,064 | 74,121 | 22,050 | 22,900 | 315,252 |
| 2020 | 63,232 | 64,727 | 64,328 | 67,255 | 20,032 | 21,675 | 301,249 |
| 2021 | 61,784 | 64,901 | 64,889 | 63,481 | 17,917 | 19,010 | 291,982 |
| 2022 | 66,052 | 62,741 | 65,172 | 63,625 | 18,989 | 17,310 | 293,889 |
| 2023 | 68,757 | 67,294 | 62,761 | 64,198 | 20,653 | 18,745 | 302,408 |
| 2024 | 75,776 | 70,365 | 67,192 | 62,689 | 18,557 | 20,089 | 314,668 |
| 2025 | 83,188 | 76,853 | 70,688 | 66,660 | 18,840 | 18,902 | 335,131 |
| **Badiliko (Asilimia) 2024 - 2025** | **9.8** | **9.2** | **5.2** | **6.3** | **1.5** | **-5.9** | **6.5** |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

- Takwimu Hazikupatikana

**Jedwali Na. 69: IDADI YA WANAFUNZI NA WALIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA JINSIA, MWAKA 2024 - 2025**

| Elimu ya msingi | 2024 | | | 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Waume | Wake | Jumla | Waume | Wake | Jumla |
| Jumla ya wanafunzi wote walioandikishwa Darasa la I-VII | 5,582,222 | 5,808,963 | 11,391,185 | 5,581,727 | 5,846,697 | 11,428,424 |
| Idadi ya wanafunzi wanaosoma shule za Serikali Darasa la I-VII | 5,257,914 | 5,482,061 | 10,739,975 | 5,222,872 | 5,486,281 | 10,709,153 |
| Idadi ya wanafunzi wanaosoma shule za binafsi Darasa la I-VII | 324,308 | 326,902 | 651,210 | 358,855 | 360,416 | 719,271 |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi | 119,986 | 109,854 | 229,840 | 121,922 | 112,602 | 234,524 |
| Idadi ya walimu katika shule za msingi za Serikali | 99,719 | 94,648 | 194,367 | 100,183 | 95,543 | 195,726 |
| Idadi ya walimu katika shule za msingi za binafsi | 20,267 | 15,206 | 35,473 | 21,739 | 17,059 | 38,798 |
| **Elimu ya Sekondari** | | | | | | |
| Jumla ya wanafunzi wote Kidato I-VI | 1,561,185 | 1,753,013 | 3,314,198 | 1,586,252 | 1,839,570 | 3,425,822 |
| Idadi ya wanafunzi wanaosoma katika shule za Serikali, kidato I-VI | 1,410,645 | 1,588,885 | 2,999,530 | 1,427,029 | 1,663,662 | 3,090,691 |
| Idadi ya wanafunzi wanaosoma katika shule za binafsi, kidato I-VI | 150,540 | 164,128 | 314,668 | 159,223 | 175,908 | 335,131 |
| Idadi ya walimu katika shule za Sekondari za Serikali | 70,994 | 35,637 | 106,631 | 76,189 | 38,219 | 114,408 |
| Idadi ya walimu katika shule za Sekondari za binafsi | 16,870 | 5,185 | 22,055 | 18,432 | 5,796 | 24,228 |
| Jumla ya walimu katika shule za Sekondari | 87,864 | 40,822 | 128,686 | 94,621 | 44,015 | 138,636 |

**Chanzo**: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

- Takwimu Hazikupatikana

## SURA YA 17

## AFYA NA MAENDELEO YA JAMII

### AFYA

### Vituo vya Kutolea Huduma za Afya

395. Mwaka 2025, idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya vilivyokuwa vinafanya kazi iliongezeka kwa asilimia 6.5 na kufikia vituo 13,683 kutoka vituo 12,846 mwaka 2024. Kati ya hivyo, Serikali ilikuwa inamiliki vituo 8,223, sekta binafsi vituo 4,368 na mashirika ya dini vituo 1,092 (**Jedwali Na. 17.1**). Ongezeko la vituo lilitokana na usajili wa vituo vipya, uboreshwaji wa mfumo wa kielektroniki wa kusajili na ukusanyaji taarifa za vituo pamoja na kuendelea kuboreshwa kwa miundombinu ya kutolea huduma za afya kwa kujenga vituo ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.

**Jedwali Na. 17.1: Vituo vya Kutolea Huduma za Afya, Mwaka 2024 - 2025**

| Aina ya Vituo | 2024 | | | | 2025 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Mashirika ya Dini | Binafsi | Jumla | Serikali | Mashirika ya Dini | Binafsi | Jumla |
| Hospitali | 250 | 123 | 89 | 462 | 248 | 122 | 105 | 475 |
| Vituo vya Afya | 958 | 163 | 133 | 1,254 | 1,042 | 164 | 153 | 1,359 |
| Zahanati | 6,394 | 729 | 1,205 | 8,328 | 6,722 | 726 | 1,258 | 8,706 |
| **Jumla ndogo** | **7,602** | **1,015** | **1,427** | **10,044** | **8,012** | **1,012** | **1,516** | **10,540** |
| Polyclinic | - | 42 | 349 | 391 | 17 | 71 | 954 | 1,042 |
| Maternity/ Nursing | - | 2 | 89 | 91 | - | 2 | 101 | 103 |
| Nyinginezo* | 25 | 37 | 2,258 | 2,320 | 194 | 7 | 1,797 | 1,998 |
| **Jumla** | **7,627** | **1,096** | **4,123** | **12,846** | **8,223** | **1,092** | **4,368** | **13,683** |

**Chanzo**: Wizara ya Afya

* Inajumuisha kliniki, maabara na vituo vya uchangiaji wa damu

### Hali ya Utoaji Huduma

396. Mwaka 2025, wagonjwa waliohudumiwa katika vituo vya kutolea huduma za afya walikuwa 48,090,590 ikilinganishwa na wagonjwa 47,495,667 waliohudumiwa mwaka 2024. Ongezeko la wagonjwa lilitokana na kuendelea kuboreshwa kwa huduma za afya, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba na kusogezwa kwa vituo karibu na wananchi. Kati ya hao, wagonjwa wa nje walikuwa 46,174,546 na wagonjwa wa kulazwa walikuwa 1,916,044. Aidha, idadi ya vitanda vya wagonjwa iliongezeka kwa asilimia 8.0 na kufikia 156,932 mwaka 2025 ikilinganishwa na vitanda 145,374 mwaka 2024. Hii ilitokana na kuendelea kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya na kukamilika kwa majengo ya vyumba vya wagonjwa mahututi pamoja na vyumba vya huduma za dharura ambavyo viliongeza uhitaji wa vitanda.

**Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba**

397. Mwaka 2025, upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 87.0 ikilinganishwa na asilimia 86.0 mwaka 2024 (**Jedwali Na. 17.2**). Ongezeko hilo lilitokana na kuimarishwa kwa utoaji wa huduma za afya ikiwemo upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.

**Jedwali Na. 17.2: Upatikanaji wa Dawa katika Vituo vya Kutolea Huduma za Afya, Mwaka 2024 - 2025**

| Ngazi ya Kituo | Idadi ya aina za dawa zinazotakiwa | Upatikanaji wa Dawa (Asilimia) | |
|---|---|---|---|
| | | 2024 | 2025 |
| Zahanati | 101 | 75 | 78.0 |
| Vituo vya Afya | 181 | 78 | 81.0 |
| Hospitali za Wilaya | 207 | 79 | 82.0 |
| Hospitali za Rufaa za Mikoa | 212 | 97 | 97.0 |
| Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda | 238 | 99 | 98.0 |
| **Wastani** | | **86.0** | **87.0** |

**Chanzo**: Wizara ya Afya

**Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto**

398. Mwaka 2025, wajawazito 2,916,250 walihudhuria kliniki ikilinganishwa na wajawazito 2,712,948 waliohudhuria kliniki mwaka 2024. Kati ya hao, wajawazito 1,342,047 (asilimia 46.1) walifanya hudhurio la kwanza kabla ya majuma 12 ikilinganishwa na wajawazito 1,184,977 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kutolewa elimu ya afya kwa umma kupitia redio na televisheni kuhusu umuhimu wa kuhudhuria kliniki mapema.

399. Mwaka 2025, wajawazito 2,140,158 walihudhuria kliniki angalau mara nne (4) sawa na asilimia 73.4 ya wajawazito 2,916,250 waliohudhuria kliniki. Aidha, wajawazito waliohudhuria kliniki na kupima Virusi vya Ukimwi (VVU) walikuwa asilimia 96.1 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 98.3 mwaka 2024. Kati ya hao, asilimia 0.49 ya wajawazito waligundulika kuwa na VVU mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 0.58 mwaka 2024. Vilevile, asilimia 99.7 ya wajawazito waliogundulika kuwa na VVU walianzishiwa matibabu ya kufubaza virusi mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 97.7 mwaka 2024.

400. Mwaka 2025, wanawake 656,869 walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi ikilinganishwa na wanawake 733,927 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 10.5. Kati ya hao, wanawake 22,421 (asilimia 3.4) waligundulika kuwa na saratani ya mlango wa kizazi na wanawake 15,635 (asilimia 2.4) waligundulika kuwa na mabadiliko ya awali ya saratani.

401. Mwaka 2025, huduma za dharura za afya ya uzazi na mtoto mchanga ziliendelea kuboreshwa kwa kuongeza idadi ya vituo vya afya vinavyofanya upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni. Katika kipindi hicho, vituo hivyo vilifikia 762 ikilinganishwa na vituo 577 mwaka 2024. Aidha, wodi maalum za huduma kwa watoto wachanga wagonjwa zilifikia 415 mwaka 2025 kutoka wodi 362 mwaka 2024.

402. Mwaka 2025, watoto 2,449,812 walizaliwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ikilinganishwa na watoto 2,219,417 waliozaliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 10.4. Katika kipindi hicho, watoto 3,357,034 wenye umri chini ya mwaka mmoja walitarajiwa kupata chanjo mbalimbali ikilinganishwa na watoto 3,113,112 mwaka 2024. Kati ya hao, watoto waliopata chanjo ya PENTA - 3 walikuwa asilimia 96, Surua Rubella - 1 (asilimia 98), Surua Rubella - 2 (asilimia 94), OPV - 3 (asilimia 95), Rota - 3 (asilimia 89) na PCV - 3 (asilimia 95).

**Huduma za Matibabu ya Kibingwa**

403. Mwaka 2025, huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi ziliendelea kutolewa katika hospitali maalum nchini. Katika kipindi hicho, wagonjwa waliopandikizwa figo walifikia 165 ikilinganishwa na wagonjwa 149 mwaka 2024. Aidha, wagonjwa waliopata huduma ya upandikizaji wa uroto walifikia 25 mwaka 2025 ikilinganishwa na wagonjwa 20 mwaka 2024. Vilevile, wagonjwa waliowekewa puto ili kupunguza uzito walifikia 193 mwaka 2025 ikilinganishwa na wagonjwa 186 mwaka 2024. Katika kipindi hicho, wagonjwa waliofanyiwa upasuaji wa moyo kwa kutumia mtambo maalum walifikia 2,886 ikilinganishwa na wagonjwa 2,695 mwaka 2024. Halikadhalika, watoto waliopandikiziwa vifaa vya usikivu walifikia 96 mwaka 2025 ikilinganishwa na watoto 83 mwaka 2024.

404. Mwaka 2025, wagonjwa waliopata huduma ya upandikizaji wa nyonga bandia walifikia 243 kutoka wagonjwa 237 mwaka 2024. Katika kipindi hicho, wagonjwa waliofanyiwa upasuaji wa magoti kwa njia ya matundu walifikia 513 kutoka wagonjwa 471 waliofanyiwa upasuaji mwaka 2024. Aidha, wanawake waliopata huduma ya upandikizaji mimba walifikia 13 mwaka 2025 ikilinganishwa na wanawake nane (8) mwaka 2024. Ongezeko la wagonjwa waliopata huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi lilitokana na kuongezeka kwa teknolojia na upatikanaji wa vifaa tiba pamoja na jitihada za Serikali katika kusomesha na kuongeza idadi ya madaktari bingwa bobezi.

405. Mwaka 2025, huduma za ubingwa bobezi ziliendelea kuimarishwa kwa kununua na kusimika mashine ya *Positron Emission Tomography and Computerized Tomography - PET/CT scan* katika hospitali ya Saratani ya Ocean Road. Aidha, idadi ya wagonjwa wanaoweza kuchunguzwa kupitia mashine hiyo iliongezeka na kufikia wagonjwa 20 kwa siku mwaka 2025 ikilinganishwa na wagonjwa watano (5) mwaka 2024.

**Udhibiti wa Malaria**

406. Mwaka 2025, vipimo 28,206,100 vya haraka vya malaria na vichupa 1,926,133 vya dawa ya sindano ya kutibu malaria kali vilinunuliwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini ikilinganishwa na vipimo 9,644,925 na vichupa 3,739,685 vilivyonunuliwa na kusambazwa mwaka 2024. Ongezeko la vipimo vilivyonunuliwa lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya vipimo katika vituo vya afya. Katika kipindi hicho, visa vya maambukizi ya malaria vilipungua kwa asilimia 15.5 na kufikia wagonjwa 2,836,977 ikilinganishwa na wagonjwa 3,357,685 mwaka 2024. Kupungua kwa maambukizi kulitokana na uzingatiaji wa kanuni za kujikinga, ikiwemo matumizi sahihi ya vyandarua na jitihada zilizofanywa na Serikali kuangamiza viluilui vya mbu. Katika jitihada za kupunguza visa vya maambukizi mapya ya malaria, Serikali kupitia mfuko wa afya wa pamoja (Global fund) ilinunua na kusambaza vyandarua 8,179,233 vyenye dawa katika mikoa yenye maambukizi ya juu ya malaria mwaka 2025 ikilinganishwa na vyandarua 8,078,158 vilivyonuuliwa na kusambazwa mwaka 2024

407. Mwaka 2025, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu - NIMR kupitia vituo 34 ilifanya uchunguzi wa mbu 17,526 waenezao malaria ikilinganishwa na mbu 14,720 waliofanyiwa uchunguzi mwaka 2024. Matokeo ya uchunguzi huo yalionesha kuwa mbu 9,417, sawa na asilimia 53.7 walikuwa aina ya *Anopheles gambiae* s.s na mbu 5,474 walikuwa *Anopheles funestus* (asilimia 31.2). Aidha, mbu 2,635 sawa na asilimia 15.03 walikuwa aina ya *Clux qunqufaciatus* ambao hawaenezi malaria. Vilevile, uchambuzi huo ulionesha kuwa uwezo wa mbu kueneza vimelea vya malaria ulipungua na kufikia asilimia 0.04 mwaka 2025 kutoka asilimia 0.05 mwaka 2024. Upungufu huo ulitokana na utekelezaji wa afua mbalimbali za udhibiti wa mbu waenezao malaria, ikiwemo upuliziaji wa viuadudu vya kibaiolojia katika mazalia ya mbu na uhamasishaji wa jamii kuhusu usafi wa mazingira ili kuondoa vyanzo vya mazalia ya mbu.

**Udhibiti wa Kifua Kikuu**

408. Mwaka 2025, wagonjwa 80,639 wa kifua kikuu waligundulika na kuanzishiwa matibabu ikilinganishwa na wagonjwa 76,684 waliogundulika na kuanzishiwa matibabu mwaka 2024. Aidha, wagonjwa 255 wa kifua kikuu sugu kati ya wagonjwa 290 waliogundulika, sawa na asilimia 87.9 walianzishiwa matibabu. Vilevile, vituo vinavyotoa huduma ya matibabu ya kifua kikuu sugu vilifikia 373 mwaka 2025 kutoka vituo 305 vilivyotoa huduma mwaka 2024. Katika kipindi hicho, idadi ya wagonjwa waliogundulika kuwa na kifua kikuu kwa kutumia vipimo vya maabara ilifikia asilimia 65.0 ikilinganishwa na asilimia 61.0 mwaka 2024. Mashine za kupima kifua kikuu kwa njia ya vinasaba zilifikia 574 mwaka 2025 kutoka mashine 569 mwaka 2024.

**Lishe**

409. Mwaka 2025, Mpango Jumuishi wa Pili wa Taifa wa Lishe (2021/22 - 2025/26) uliendelea kutekelezwa ili kukabiliana na athari za lishe duni na kuimarisha ukuaji wa watoto. Katika kipindi hicho, watoto 2,303,566 walinyonyeshwa maziwa ya mama ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa, sawa na asilimia 94 ya lengo ikilinganishwa na watoto 1,145,739 (asilimia 93) mwaka 2024. Aidha, matone ya vitamini A kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano yaliendelea kutolewa kwa watoto 9,408,384 (asilimia 99.8) mwaka 2025 ikilinganishwa na watoto 9,456,378 mwaka 2024.

410. Mwaka 2025, watoto waliozaliwa na uzito pungufu walikuwa asilimia 5.1 ikilinganishwa na asilimia 5.2 mwaka 2024. Hii ilitokana na utekelezaji wa afua za lishe kwa wajawazito, ikiwemo utoaji wa vidonge vya madini chuma, elimu ya lishe, ulaji wa vyakula vilivyoongezwa virutubisho na mlo kamili pamoja na kuhudhuria kliniki kwa wakati.

**Mafunzo katika Kada za Afya**

411. Mwaka 2025, wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya afya katika ngazi ya stashahada walikuwa 25,586 (wanawake 13,955 na wanaume 11,631) ikilinganishwa na wanafunzi 24,823 waliodahiliwa mwaka 2024. Aidha, wanafunzi waliohitimu ngazi ya stashahada katika kozi za afya walikuwa 14,716 (wanawake 8,151 na wanaume 6,565) mwaka 2025 ikilinganishwa na wanafunzi 17,850 mwaka 2024 (**Jedwali Na. 17.3**).

**Jedwali Na. 17.3: Wanafunzi Waliodahiliwa na Kuhitimu katika Vyuo vya Mafunzo ya Afya Kada za Kati, Mwaka 2025**

| Kada | Waliodahiliwa | | | Waliohitimu | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanawake | Wanaume | Jumla | Wanawake | Wanaume | Jumla |
| Utabibu wa Kinywa na Meno | 518 | 681 | 1,199 | 86 | 120 | 206 |
| Utabibu | 2,860 | 3,433 | 6,293 | 2,277 | 2,663 | 4,940 |
| Tiba Lishe | 182 | 127 | 309 | 0 | 0 | 0 |
| Radiografia | 992 | 1,297 | 2,289 | 43 | 57 | 100 |
| Afya ya Mazingira | 63 | 103 | 166 | 35 | 75 | 110 |
| Sayansi ya Taarifa za Afya | 62 | 51 | 113 | 18 | 11 | 29 |
| Teknolojia ya Utunzaji Kumbukumbu na Taarifa za Afya | 119 | 121 | 240 | 33 | 26 | 59 |
| Sayansi ya Maabara Tiba | 1,036 | 1,190 | 2,226 | 342 | 381 | 723 |
| Uuguzi na Ukunga | 2,601 | 1,282 | 3,883 | 2,337 | 1,378 | 3,715 |
| Tiba Kazi | 17 | 12 | 29 | 0 | 0 | 0 |
| Optometria | 107 | 141 | 248 | 9 | 13 | 22 |
| Ufamasia | 5,084 | 2,824 | 7,908 | 2,888 | 1,770 | 4,658 |
| Fisiotherapia | 305 | 364 | 669 | 72 | 50 | 122 |
| Stashahada ya Juu ya Huduma ya Uuguzi wa Afya ya Akili | 9 | 5 | 14 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **13,955** | **11,631** | **25,586** | **8,151** | **6,565** | **14,716** |

**Chanzo**: Wizara ya Afya

## MAENDELEO YA JAMII

### Huduma ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto

412. Mwaka 2025, Serikali iliendelea kuratibu utoaji wa huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano (5) katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana. Hadi Desemba 2025, vituo vya kulelea watoto wadogo mchana vilivyosajiliwa vilifikia 4,723 kutoka vituo 4,391 kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, watoto 244,263 (wavulana 119,272 na wasichana 124,991) waliandikishwa katika vituo hivyo mwaka 2025 ikilinganishwa na watoto 203,926 walioandikishwa mwaka 2024.

413. Mwaka 2025, madawati 14 yalianzishwa kwenye stendi za mabasi na bandari ili kudhibiti usafirishaji haramu wa watoto nchini ikilinganishwa na madawati 11 yaliyoanzishwa mwaka 2024. Madawati hayo yalianzishwa katika mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Dar es Salaam, Kagera, Mbeya, Morogoro, Dodoma, Geita, Njombe, Tabora na Ruvuma. Madawati yaliyoanzishwa yanatoa huduma za ustawi wa jamii kwa makundi maalum, ikiwemo watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani. Hadi Desemba 2025, watoto 2,669 (wavulana 1,512 na wasichana 1,187) waliokolewa kupitia madawati hayo na kuunganishwa na huduma za ustawi wa jamii ikilinganishwa na watoto 1,869 kipindi kama hicho mwaka 2024.

414. Hadi Desemba 2025, makao binafsi ya watoto yalifikia 433 ikilinganishwa na makao binafsi 374 kipindi kama hicho mwaka 2024. Katika kipindi hicho, watoto 16,130 (wavulana 8,138 na wasichana 7,992) walihudumiwa katika makao hayo ikilinganishwa na watoto 13,381 waliohudumiwa mwaka 2024. Kwa upande mwingine, leseni za makao 39 ya watoto zilihuishwa mwaka 2025 ikilinganishwa na leseni 18 zilizohuishwa mwaka 2024.

### Huduma za Ustawi na Maendeleo ya Watoto

415. Mwaka 2025, watoto 6,182 (Wavulana 3,407 na Wasichana 2,775) walio katika mazingira hatarishi walitambuliwa ikilinganishwa na watoto 5,353 (wavulana 2,825 na wasichana 2,528) mwaka 2024. Kati ya hao, watoto 5,663 waliunganishwa na familia zao, watoto 448 walipelekwa katika makao ya watoto na watoto 71 waliwekwa chini ya walezi wa kuaminika ikilinganishwa na watoto 812 waliounganishwa na familia zao, watoto 256 waliopelekwa katika makao ya watoto, watoto 65 waliwekwa kwa walezi wa kuaminika na watoto 25 waliounganishwa na vyuo vya ufundi mwaka 2024.

416. Mwaka 2025, Serikali iliendelea kutoa huduma za msingi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi wanaoishi katika Makao ya watoto ya Taifa Kurasini (Dar es Salaam) na Kikombo (Dodoma). Katika kipindi hicho, watoto 382 (wavulana 226 na wasichana 156) walipatiwa huduma za msingi ikilinganishwa na watoto 252 waliopatiwa huduma hizo mwaka 2024. Aidha, watoto 16,130 (wavulana 8,138 na wasichana 7,992) walipatiwa huduma za msingi kupitia makao binafsi ya watoto ikilinganishwa na watoto 13,381

waliopatiwa huduma mwaka 2024. Kwa upande mwingine, watoto 293 walio katika mazingira hatarishi walikuwa na bima ya afya ya NHIF mwaka 2025 ikilinganishwa na watoto 101 waliokuwa na bima mwaka 2024.

417. Mwaka 2025, watoto 154 (wavulana 148 na wasichana 6) walio katika mkinzano na sheria walipatiwa huduma za msingi, ikiwemo chakula, malazi, mavazi, afya, shughuli za kujitegemea, msaada wa kisaikolojia na kijamii na kuunganishwa na familia zao ikilinganishwa na watoto 104 waliopata huduma hizo mwaka 2024. Aidha, wavulana 26 walihukumiwa na kupelekwa katika Shule ya Maadilisho ya Irambo mkoani Mbeya ikilinganishwa na msichana 1 na wavulana 11 waliohukumiwa mwaka 2024.

418. Hadi Desemba 2025, madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto yaliyoanzishwa kwenye shule za msingi na sekondari yalifikia 4,886 kutoka madawati 3,106 kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, walimu 3,979 walipata mafunzo ya namna ya kuanzisha madawati, kusimamia na kuratibu afua za ulinzi na usalama wa mtoto ndani na nje ya shule mwaka 2025 ikilinganishwa na walimu 3,570 waliopata mafunzo mwaka 2024. Kwa upande mwingine, mabaraza ya watoto katika ngazi za mikoa, halmashauri, kata na kijiji/mtaa yalifikia 1,515 Desemba 2025 kutoka mabaraza 1,395 kipindi kama hicho mwaka 2024. Mabaraza hayo ni jukwaa linalowezesha watoto kushiriki katika masuala yanayowahusu kulingana na umri wao.

**Ukatili wa Kijinsia**

419. Mwaka 2025, Serikali iliendelea na juhudi za kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Katika kipindi hicho, matukio 1,300 ya ukatili wa kijinsia, ikiwemo ubakaji, kujeruhi, shambulio la aibu, ukeketaji na lugha za matusi yalitolewa taarifa ikilinganishwa na matukio 19,717 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 93.4. Kwa upande mwingine, matukio 13,430 ya ukatili dhidi ya watoto yalitolewa taarifa mwaka 2025 ikilinganishwa na matukio 7,320 mwaka 2024. Kupungua kwa matukio ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto yaliyotolewa taarifa kulichagiwa na juhudi za Serikali na wadau mbalimbali za kutokomeza matukio ya ukatili, ikiwemo utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi Wanawake na Watoto (MTAKUWWA II).

420. Mwaka 2025, Serikali iliendelea kuratibu uanzishwaji wa madawati ya jinsia katika maeneo ya umma, hususan kwenye masoko. Katika kipindi hicho, madawati 551 yalianzishwa na kufikia jumla ya madawati 789 katika mikoa 16 ikilinganishwa na madawati mapya 238 yaliyoanzishwa mwaka 2024. Aidha, madawati ya jinsia yaliyoanzishwa katika taasisi za elimu ya juu na elimu ya kati yalifikia 362 mwaka 2025 kutoka madawati 332 mwaka 2024.

**Huduma za Ustawi kwa Wazee na Wasiojiweza**

421. Mwaka 2025, wazee 224 wasiojiweza (wanaume 139 na wanawake 85) walipewa huduma za msingi, ikiwemo chakula, malazi, mavazi na huduma za afya katika makazi 14 ya wazee yanayomilikiwa na Serikali ikilinganishwa na wazee 245 wasiojiweza waliopata huduma za msingi mwaka 2024. Aidha, wazee 274 wasiojiweza (wanaume 117 na wanawake 157) walihudumiwa katika makazi 16 ya wazee yanayomilikiwa na sekta binafsi ikilinganishwa na wazee 279 wasiojiweza waliohudumiwa mwaka 2024.

422. Mwaka 2025, Serikali ilitambua wazee na wasiojiweza 4,975,473 (wanaume 2,293,263 na wanawake 2,682,210) ikilinganishwa na wazee na wasiojiweza 2,353,758 waliotambuliwa mwaka 2024. Aidha, wazee na wasiojiweza 2,199,588 (wanaume 1,010,076 na wanawake 1,189,512) walipatiwa bima ya afya ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za afya ikilinganishwa na wazee na wasiojiweza 80,995 waliopatiwa bima ya afya mwaka 2024. Ongezeko hilo lilitokana na clinic zilizofanyika katika halmashauri ili kubaini na kuwatambua wazee na wasiojiweza na kuwapatia bima ya afya.

**Mafunzo ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii**

423. Mwaka 2025, wanafunzi 11,068 (wanaume 3,892 na wanawake 7,176) walidahiliwa katika taasisi na vyuo vya ustawi na maendeleo ya jamii ikiliganishwa na wanafunzi 13,912 waliodahiliwa mwaka 2024 (**Jedwali Na. 17.4**). Aidha, wanafunzi 9,712 walihitimu mwaka 2025 ikiliganishwa na wanafunzi 9,943 waliohitimu mwaka 2024.

**Jedwali Na. 17.4: Udahili wa Wanafunzi katika Taasisi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, Mwaka 2024 - 2025**

| Taasisi | Ngazi ya Elimu | 2024 | | | 2025 | | | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla | |
| Vyuo vya Maendeleo ya Jamii | Stashahada | 550 | 1,190 | 1,740 | 1,055 | 2,133 | 3,188 | 83.2 |
| | Astashahada | 1,197 | 2,229 | 3,426 | 586 | 1,232 | 1,818 | -46.9 |
| | **Jumla ndogo** | **1,747** | **3,419** | **5,166** | **1,641** | **3,365** | **5,006** | **-3.1** |
| Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru | Astashahada | 856 | 659 | 1,515 | 381 | 553 | 934 | -38.3 |
| | Stashahada | 359 | 163 | 522 | 554 | 760 | 1,314 | * |
| | Shahada | 646 | 389 | 1,035 | 338 | 714 | 1,052 | 1.6 |
| | Stashahada ya Juu | 2 | 5 | 7 | 65 | 53 | 118 | * |
| | Shahada ya Uzamili | 73 | 77 | 150 | 113 | 117 | 230 | 53.3 |
| | **Jumla ndogo** | **1,936** | **1,293** | **3,229** | **1,451** | **2,197** | **3,648** | **13.0** |
| Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama | Astashahada | 691 | 1,159 | 1,850 | 375 | 613 | 988 | -46.6 |
| | Stashahada | 276 | 461 | 737 | 63 | 103 | 166 | -77.5 |
| | Shahada | 830 | 1,940 | 2,770 | 337 | 824 | 1,161 | -58.1 |
| | Stashahada ya ya juu/Uzamili | 14 | 2 | 16 | 5 | 5 | 10 | -37.5 |
| | Shahada ya Uzamili | 56 | 88 | 144 | 20 | 69 | 89 | -38.2 |
| | **Jumla ndogo** | **1,867** | **3,650** | **5,517** | **800** | **1,614** | **2,414** | **-56.2** |
| **Jumla kuu** | | **5,550** | **8,362** | **13,912** | **3,892** | **7,176** | **11,068** | **-20.4** |

**Chanzo**: Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

*Badiliko linazidi asilimia 100

**Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

424. Mwaka 2025, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,609 yalisajiliwa ikilinganishwa na Mashirika 1,438 yaliyosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 12.9. Kati ya hayo, mashirika 61 yalikuwa ya kimataifa, mashirika 1,475 ya kitaifa, mashirika 41 ngazi ya mkoa na mashirika 32 ngazi ya wilaya. Mashirika yaliyosajiliwa yalijikita katika utekelezaji wa afua mbalimbali, ikiwemo elimu, afya, uwezeshaji wa jamii, nishati, maji, utawala bora, haki za binadamu, masuala ya jinsia na kilimo.

425. Mwaka 2025, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yalipokea shilingi trilioni 1.289 kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ikilinganishwa na shilingi bilioni 671.44 zilizopokelewa mwaka 2024. Hii ilitokana na ongezeko la usajili wa Mashirika mapya. Aidha, Serikali ilifanya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,035 katika mikoa 16 ikilinganishwa na Mashirika 507 yaliyofuatiliwa katika mikoa 15 mwaka 2024. Mashirika yaliyofuatiliwa mwaka 2025 yalikuwa katika mikoa ya Iringa, Morogoro, Tanga, Dar es Salaam, Singida, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Kigoma, Tabora, Simiyu, Njombe, Songwe, Mbeya na Rukwa. Katika ufuatiliaji huo, hakukuwa na Shirika lililobainika kukiuka sheria na taratibu.

**Jedwali Na. 67: IDADI YA WAGONJWA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA, MWAKA 2010 - 2025**

| Mwaka | Wagonjwa wa Nje | | | | Wagonjwa waliolazwa | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Hospitali | Zahanati | Vituo vya Afya | Jumla | | |
| 2010 | 2,341,114 | 35,990,843 | 5,742,693 | 44,074,650 | 3,784,957 | 47,859,607 |
| 2011 | 2,622,048 | 39,917,117 | 6,431,816 | 48,970,981 | 4,239,152 | 53,210,133 |
| 2012 | 2,815,529 | 41,333,522 | 6,657,817 | 50,806,868 | 4,388,108 | 55,194,976 |
| 2013 | 2,903,275 | 42,682,479 | 6,873,056 | 52,458,810 | 4,529,971 | 56,988,781 |
| 2014 | 5,910,725 | 14,008,692 | 475,295 | 20,394,712 | 1,665,935 | 22,060,647 |
| 2015 | 4,480,781 | 25,072,487 | 6,006,466 | 35,559,734 | 1,858,956 | 37,418,690 |
| 2016 | 4,984,645 | 20,859,281 | 6,515,219 | 32,359,145 | 1,775,835 | 34,134,980 |
| 2017 | 5,266,252 | 21,115,639 | 7,050,725 | 33,432,616 | 1,650,224 | 35,082,840 |
| 2018 | 4,675,045 | 27,473,506 | 8,903,461 | 41,052,012 | 1,359,264 | 42,411,276 |
| 2019 | 9,821,148 | 26,500,182 | 10,153,322 | 46,474,652 | 1,852,720 | 48,327,372 |
| 2020 | 10,150,504 | 22,154,653 | 9,741,820 | 42,046,977 | 1,852,720 | 43,899,697 |
| 2021 | 11,348,037 | 19,705,594 | 9,219,985 | 40,273,616 | 1,651,001 | 41,924,617 |
| 2022 | 27,290,723 | 1,486,649 | 12,567,881 | 41,345,253 | 1,626,308 | 42,971,561 |
| 2023 | 14,047,587 | 9,399,664 | 19,959,991 | 43,407,242 | 1,757,240 | 45,164,482 |
| 2024 | 14,109,193 | 20,907,765 | 10,612,603 | 45,629,561 | 1,866,106 | 47,495,667 |
| 2025 | 13,905,015 | 21,882,783 | 10,386,748 | 46,174,546 | 1,916,044 | 48,090,590 |

**Chanzo:** Wizara ya Afya

**Jedwali Na. 68: IDADI YA VITANDA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA NCHINI, MWAKA 2024 - 2025**

| Aina ya Vituo | 2024 | | | | 2025 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Shirika la kujitolea/ Dini | Binafsi | Jumla | Serikali | Shirika la kujitolea/ Dini | Binafsi | Jumla |
| Hospitali ya Taifa | 1,478 | 0 | 0 | 1,478 | 1,653 | - | - | 1,653 |
| Hospitali Maalum za Kibingwa | 633 | 0 | 0 | 633 | 1,969 | - | - | 1,969 |
| Hospitali za Rufaa za Kanda | 1,659 | 1515 | 170 | 3,344 | 3,816 | 1,675 | 1,386 | 6,877 |
| Hospitali za Mikoa | 12,667 | 2083 | 375 | 15,125 | 8,334 | 3,490 | 2,446 | 14,270 |
| Hospitali za Wilaya | 11,957 | 6123 | 1177 | 19,257 | 24,300 | 13,399 | 3,470 | 41,169 |
| Hospitali nyingine | 0 | 2,238 | 1,260 | 3,498 | 44 | 306 | 2,871 | 3,221 |
| Vituo vya Afya | 10,085 | 5,302 | 15,550 | 30,937 | 32,338 | 5,752 | 3,401 | 41,491 |
| Zahanati | 47,878 | 12,037 | 11,187 | 71,102 | 36,022 | 5,390 | 4,870 | 46,282 |
| **Jumla** | **86,357** | **29,298** | **29,719** | **145,374** | **108,476** | **30,012** | **18,444** | **156,932** |

**Chanzo:** Wizara ya Afya



Sehemu ya Tatu

# Maendeleo katika Sekta Nyingine

# SURA YA 18

## MASUALA MTAMBUKA NA MAENDELEO YA WATU

### MASUALA MTAMBUKA

**Mazingira**

426. Mwaka 2025, miradi 534 ilipata hati za Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) ikilinganishwa na miradi 1,764 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 69.7. Hii ilitokana na maboresho ya kisheria yaliyoongeza vigezo vya tathmini, ikiwemo uzingatiaji wa athari za mabadiliko ya tabianchi katika utekelezaji wa miradi.

427. Mwaka 2025, miradi 42 ilipata vyeti vya Ukaguzi wa Mazingira ikilinganishwa na miradi 126 iliyopata vyeti mwaka 2024. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya miradi kutokukidhi vigezo kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na hivyo kutoruhusiwa kuendelea kutekelezwa. Katika kipindi hicho, hati tano (5) za Tathmini ya Athari kwa Mazingira Kimkakati (TMK) zilitolewa ikilinganishwa na hati tatu (3) zilizotolewa mwaka 2024 (**Jedwali Na. 18.1**). Hii ilitokana na kuongezeka kwa uelewa na matumizi ya TMK katika upangaji na utekelezaji wa sera, mipango na programu mbalimbali. Kwa upande mwingine, vibali 123 vya taka hatarishi vikijumuisha vibali vya kuhifadhi, kukusanya, kusafirisha ndani ya nchi, kupitisha nchini na kusafirisha nje ya nchi vilitolewa mwaka 2025 ikilinganishwa na vibali 154 vilivyotolewa mwaka 2024.

**Jedwali Na. 18.1: Vyeti vya Tathmini na Ukaguzi wa Mazingira, Mwaka 2021-2025**

| Aina ya Vyeti | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Vyeti vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira Kimkakati (TMK) | 1 | 2 | 3 | 3 | 5 |
| Vyeti vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) | 950 | 1,079 | 1,260 | 1,764 | 534 |
| Vyeti vya Ukaguzi wa Mazingira | - | 199 | 281 | 126 | 42 |
| **Jumla** | **951** | **1,280** | **1,544** | **1,893** | **581** |

**Chanzo:** Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira

428. Mwaka 2025, miti 224,795,501 ilipandwa kupitia Kampeni ya upandaji na utunzaji miti ikilinganishwa na miti 286,657,203 iliyopandwa kupitia Kampeni hiyo mwaka 2024. Kati ya hiyo, miti 182,084,356 ilistawi, sawa na asilimia 81.0 ya miti iliyopandwa ikilinganishwa na miti 223,716,211 iliyostawi mwaka 2024.

429. Mwaka 2025, Serikali iliendelea kutekeleza Kanuni na Mwongozo wa Taifa wa Usimamizi wa Biashara ya Kaboni kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji katika biashara hiyo. Katika kipindi hicho, kampuni zilizowekeza katika biashara ya kaboni zilifikia 82 kutoka kampuni 66 zilizowekeza mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 24.2. Hii ilitokana na fursa za uwekezaji katika biashara ya kaboni, ikiwemo kampuni kutambulika kimataifa.

**Usalama wa Raia**

430. Mwaka 2025, makosa makubwa ya jinai 46,334 yalitolewa taarifa ikilinganishwa na makosa 50,574 yaliyotolewa taarifa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 6.0. Kwa upande mwingine, makosa madogo yaliyotolewa taarifa yalikuwa 549,215 mwaka 2025 ikilinganishwa na makosa 564,477 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 2.7 (**Jedwali Na. 18.2**). Kupungua kwa makosa yaliyotolewa taarifa kulitokana na kuimarika kwa hali ya ulinzi na usalama nchini, ikiwemo kuongezeka kwa doria za vyombo vya ulinzi na usalama, kuimarika kwa ulinzi shirikishi wa jamii, matumizi ya teknolojia katika kuzuia na kugundua uhalifu, pamoja na kuendelea kutolewa kwa elimu ya utii wa sheria kwa wananchi.

**Jedwali Na. 18.2: Mchanganuo wa Makosa Makubwa ya Jinai, Mwaka 2024 - 2025**

| **Aina ya Makosa** | **2024** | **2025** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---:|---:|---:|
| Makosa dhidi ya Binadamu | 13,076 | 11,826 | -9.6 |
| Makosa ya Kuwania Mali | 20,946 | 18,134 | -13.4 |
| Uhalifu wa Kifedha | 924 | 830 | -10.2 |
| Makosa dhidi ya Maadili ya Jamii | 15,628 | 15,544 | -0.5 |
| **Jumla** | **50,574** | **46,334** | **-8.4** |

**Chanzo:** Wizara ya Mambo ya Ndani

431. Mwaka 2025, matukio makubwa ya ajali yaliyotolewa taarifa yalikuwa 1,364 (barabarani 1,347, majini 16 na angani 1) ikilinganishwa na matukio 1,735 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 21.4. Aidha, matukio ya ajali 911 yalisababisha vifo vya watu 1,275 na majeruhi 2,295 ikilinganishwa na matukio ya ajali 1,170 yaliyosababisha vifo vya watu 1,715 na majeruhi 2,719 mwaka 2024, sawa na upungufu wa vifo na majeruhi wa asilimia 25.7 na asilimia 15.6 mtawalia. Hii ilitokana na usimamizi wa sheria za barabarani, doria, elimu na operesheni za mara kwa mara.

432. Mwaka 2025 idadi ya wafungwa na mahabusu katika magereza yote nchini ilikuwa 23,956 (wafungwa 19,613 na mahabusu 4,343) ikilinganishwa na wafungwa na mahabusu 26,755 mwaka 2024. Katika kipindi hicho, idadi ya wahalifu iliendelea kupungua na iliendana na uwezo wa magereza kisheria wa kuhifadhi wafungwa 29,902. Kupungua kwa idadi ya wahalifu kulitokana na ushirikiano baina ya vyombo vya haki jinai, ikiwemo Mahakama, Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na wadau wengine. Kwa upande mwingine, wafungwa 1,667 walitolewa magerezani kupitia taratibu za sheria mwaka 2025 ikilinganishwa na wafungwa 2,630 walionufaika na msamaha wa Rais ambapo wafungwa 51 waliachiliwa huru na wafungwa 2,579 walipunguziwa adhabu ya vifungo mwaka 2024. Kati ya wafungwa waliotolewa magerezani kupitia taratibu za sheria, wafungwa 654 walinufaika na adhabu ya vifungo vya nje, wafungwa 865

walinufaika kutumikia kifungo cha nje kupitia huduma kwa jamii, wafungwa 112 walinufaika na Parole, na wafungwa 36 walinufaika na Msamaha wa Rais.

433. Mwaka 2025, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilipokea miito 3,148 ya matukio ya moto ikilinganishwa na miito 2,634 iliyopokelewa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 19.5. Kuongezeka kwa matukio hayo kulichangiwa na matumizi yasiyo sahihi ya nishati, ikiwemo umeme na gesi. Aidha, miito ya maokozi 1,427 ilipokelewa mwaka 2025 ikilinganishwa na miito ya maokozi 1,182 iliyopokelewa mwaka 2024. Kwa upande mwingine, Jeshi lilitoa elimu kwa umma kuhusu kinga na tahadhari dhidi ya majanga ya moto kupitia vyombo vya habari, ikiwemo vipindi 1,179 vya redio na vipindi 58 vya luninga mwaka 2025 ikilinganishwa na vipindi 865 vya redio na vipindi 97 vya luninga 2024. Vilevile, Jeshi lilifanya kaguzi za kinga na tahadhari dhidi ya moto katika maeneo 67,215 mwaka 2025 ikilinganishwa na maeneo 63,763 yaliyokaguliwa mwaka 2024.

434. Mwaka 2025, hati 111,212 za kusafiria zilitolewa kwa watanzania ikilinganishwa na hati 164,252 zilizotolewa mwaka 2024. Hii ilitokana na kupungua kwa maombi ya hati za kusafiria nje ya nchi kwa ajili ya kutafuta fursa za biashara, masomo na ajira. Katika kipindi hicho, watanzania 555,148 walitoka nchini ikilinganishwa na watanzania 507,032 waliotoka nchini mwaka 2024. Aidha, watanzania 528,402 waliingia nchini mwaka 2025 ikilinganishwa na watanzania 486,874 waliongia nchini mwaka 2024. Kwa upande mwingine, vibali vya ukaazi 23,647 vilitolewa mwaka 2025 ikilinganishwa na vibali vya ukaazi 22,500 vilivyotolewa mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za uwekezaji na biashara nchini.

435. Mwaka 2025, wageni 2,330,715 waliingia nchini kwa vibali halali ikilinganishwa na wageni 2,009,183 walioingia nchini mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 16.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za utalii na uwekezaji nchini. Aidha, wageni 2,091,764 walitoka nchini kwa vibali halali ikilinganishwa na wageni 1,824,938 waliotoka nchini mwaka 2024.

436. Mwaka 2025, waomba hifadhi 3,986 walipokelewa nchini ikilinganishwa na waomba hifadhi 725 waliopokelewa nchini mwaka 2024. Katika kipindi hicho, wakimbizi 7,547 walitafutiwa suluhisho la kudumu ikilinganishwa na wakimbizi 20,309 waliotafutiwa suluhisho la kudumu mwaka 2024. Kati ya hao, wakimbizi 6,563 walirejea katika nchi zao kwa hiari mwaka 2025 ikilinganishwa na wakimbizi 13,856 waliorejea kwa hiari mwaka 2024. Vilevile, wakimbizi 954 walihamishiwa nchi ya tatu mwaka 2025 ikilinganishwa na wakimbizi 6,453 waliohamishiwa nchi ya tatu mwaka 2024.

**Utambuzi na Usajili wa Watu**

437. Hadi Desemba 2025, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa - NIDA ilitambua na kusajili wananchi 26,442,997 kutoka wananchi 25,484,820 waliotambuliwa na kusajiliwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Katika kipindi hicho, namba za utambulisho zilizozalishwa zilifikia 22,326,111 kutoka namba za utambulisho 21,354,858 Desemba 2024, sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Hadi Desemba 2025, NIDA ilizalisha vitambulisho 21,344,070 kutoka vitambulisho 21,115,671 vilivyozalishwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Katika kipindi hicho, NIDA ilikuwa imeunganisha taasisi 138 (taasisi za umma 75 na taasisi binafsi 63) katika mfumo wa Usajili na Utambuzi wa watu ikilinganishwa na taasisi 124 zilizokuwa zimeunganishwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko la taasisi zilizounganishwa lilitokana na kuongezeka kwa uelewa wa umuhimu wa matumizi ya mfumo wa kidijitali katika kuhakiki na kuthibitisha taarifa za wananchi katika utoaji wa huduma.

**Usajili wa Jumuiya**

438. Mwaka 2025, Ofisi ya Msajili wa Jumuiya ilisajili jumuiya 311 ikilinganishwa na jumuiya 528 zilizosajiliwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 41.1. Upungufu huo ulitokana na maombi machache yaliyowasilishwa kufuatia mabadiliko ya mazingira ya ufadhili kutoka kwa baadhi ya washirika wa maendeleo.

**Usajili, Ufilisi na Udhamini**

439. Mwaka 2025, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini - RITA ulisajili vizazi 1,624,013 ikilinganishwa na vizazi 1,682,214 vilivyosajiliwa mwaka 2024. Katika kipindi hicho, watoto 667,232 walisajiliwa kupitia Mpango wa Usajili kwa Watoto Walio Chini ya Umri wa Miaka Mitano ikilinganishwa na watoto 1,109,710 waliosajiliwa mwaka 2024. Aidha, vizazi 956,781 vilisajiliwa kupitia usajili wa kawaida mwaka 2025 ikilinganishwa na vizazi 572,504 vilivyosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 67.1. Hii ilichangiwa na matumizi ya mfumo wa e-RITA. Kwa upande mwingine, matukio 40,814 ya vifo yalisajiliwa ikilinganishwa na matukio 39,071 yaliyosajiliwa mwaka 2024. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya vyeti vya vifo katika kupata huduma mbalimbali ikiwemo bima, mikopo ya elimu ya juu na mirathi.

440. Mwaka 2025, RITA ilisajili na kutoa hati za viapo vya ndoa 52,341 ikilinganishwa na hati 50,592 zilizosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 3.5. Hii ilitokana na matumizi ya e-RITA katika kuwasilisha taarifa za hati za viapo vya ndoa kwa Msajili Mkuu. Kwa upande mwingine, RITA ilisajili hati za talaka 762 mwaka 2025 ikilinganishwa na hati za talaka 1,569 zilizosajiliwa mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 51.4. Aidha, RITA ilisajili hati 32 za watoto wa kuasili kufuatia amri za Mahakama ikilinganishwa na hati 39 zilizosajiliwa mwaka 2024.

441. Mwaka 2025, RITA ilitoa hati 77 za miunganisho ya wadhamini ikilinganishwa na hati 165 zilizotolewa mwaka 2024. Upungufu huo ulitokana na uelewa mdogo wa taasisi kuhusu wajibu wa kisheria wa kusajili bodi. Hadi Desemba 2025, bodi za wadhamini zilikuwa 5,243 kutoka bodi za wadhamini 4,954 kipindi kama hicho mwaka 2024. Idadi hiyo ilitokana na kusajiliwa kwa bodi za wadhamini 1,494, kufutwa kwa bodi za wadhamini 743 kwa kushindwa kuwasilisha mrejesho wa wadhamini katika Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu, na bodi za wadhamini 462 kuhamishiwa kundi la Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Aidha, wosia 229 ziliandikwa na kuhifadhiwa mwaka 2025 ikilinganishwa na wosia 181 zilizoandikwa na kuhifadhiwa mwaka 2024. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kwa utoaji wa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa wosia katika kupunguza migogoro ya mali za familia pindi mwenye mali anapofariki.

**Maendeleo ya Sheria na Mahakama**

442. Mwaka 2025, mikataba 3,226 ya kitaifa na kimataifa ilifanyiwa upekuzi ikilinganishwa na mikataba 1,806 iliyofanyiwa upekuzi mwaka 2024. Aidha, hati 675 za makubaliano zilifanyiwa upekuzi ikilinganishwa na hati 515 zilizofanyiwa upekuzi mwaka 2024. Mikataba hiyo ilihusisha ununuzi, ujenzi na ukarabati wa majengo na utoaji wa huduma za jamii.

443. Mwaka 2025, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) iliendesha mashauri 10,750 ikilinganishwa na mashauri 8,981 yaliyoendeshwa mwaka 2024. Kati ya hayo, mashauri 9,885 yalikuwa madai ya kitaifa, mashauri 36 madai ya kimataifa na mashauri 829 madai ya kikatiba na haki za binadamu. Katika kipindi hicho, OWMS ilimaliza mashauri 1,295 ikilinganishwa na mashauri 1,486 yaliyomalizika mwaka 2024. Kati ya hayo, mashauri 1,107 yalikuwa ya kitaifa, mashauri matatu (3) ya kimataifa na mashauri 185 ya kikatiba na haki za binadamu. Aidha, OWMS ilibakiwa na mashauri 9,455 yaliyoendelea kusikilizwa katika mahakama na mabaraza mbalimbali ndani na nje ya nchi.

444. Mwaka 2025, OWMS ilishughulikia mashauri 254 ya usuluhishi ikilinganishwa na mashauri 229 yaliyoshughulikiwa mwaka 2024. Kati ya hayo, mashauri 222 yalihusu usuluhishi wa kitaifa na mashauri 32 yalihusu usuluhishi wa kimataifa. Aidha, mashauri 29 (kitaifa 26 na kimataifa 3) yalimalizwa mahakamani na kwenye mabaraza kwa njia ya majadiliano. Vilevile, mashauri 225 ya usuluhishi wa kitaifa na kimataifa yaliendelea katika mahakama na mabaraza ndani na nje ya nchi.

445. Mwaka 2025, kliniki za ushauri wa kisheria zilifanyika katika Mikoa ya Manyara, Simiyu na Dar es Salaam. Kupitia kliniki hizo, wananchi 5,516 walipata elimu na kushughulikia migogoro 560 ya kisheria. Hii ilihusisha migogoro 275 ya ardhi, 37 ya ndoa, 48 jinai, 59 madai, 31 ajira, 24 ukatili wa kijinsia, 54 mirathi, 10 matunzo ya watoto na 22

masuala mtambuka. Baadhi ya migogoro ilihitimishwa na wananchi kupata haki zao na mingine ilikabidhiwa kwenye kamati za mkoa na wilaya kwa ufuatiliaji.

**Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu**

446. Mwaka 2025, Serikali kupitia Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu iliokoa waathirika 158 wa usafirishaji haramu wa binadamu na kuwapatia huduma muhimu ikilinganishwa na waathirika 127 waliookolewa na kusaidiwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 24.4. Hii ilichangiwa na kuimarika kwa mifumo ya utambuzi wa waathirika na kuongezeka kwa uelewa wa jamii kuhusu utoaji wa taarifa za vitendo vya usafirishaji haramu wa binadamu kufuatia kampeni za elimu na uhamasishaji. Katika kipindi hicho, wahalifu 19 waliojihusisha na usafirishaji haramu wa binadamu walikamatwa na kufikishwa mahakamani ikilinganishwa na wahalifu 15 waliokamatwa na kufikishwa mahakamani mwaka 2024. Hii ilitokana na uchunguzi na operesheni zilizofanyika kudhibiti mitandao iliyojihusisha na usafirishaji haramu wa binadamu pamoja na elimu iliyotolewa kwa umma kuhusu viashiria, madhara na njia za kutoa taarifa za vitendo vya uhalifu huo.

**Mapambano dhidi ya Rushwa**


447. Mwaka 2025, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilifanya mapitio 635 ya mifumo ya kazi na utoaji huduma kama ilivyokuwa mwaka 2024. Aidha, TAKUKURU ilifanya ukaguzi wa matumizi ya rasilimali za umma katika utekelezaji wa miradi 1,605 ya maendeleo mwaka 2025 ikilinganishwa na miradi 1,834 iliyokaguliwa mwaka 2024. Miradi hiyo ilihusisha sekta za utawala, nishati, ujenzi, maji, fedha, elimu, afya, kilimo, uchukuzi na viwanda. Kati ya miradi iliyokaguliwa, miradi miwili (2) ilibainika kuwa na kasoro katika utekelezaji ikilinganishwa na miradi 205 iliyobainika kuwa na kasoro mwaka 2024. Upungufu huo ulitokana na utoaji wa elimu na uzingatiaji wa mipango ya utekelezaji wa miradi.

448. Mwaka 2025, TAKUKURU ilifungua mashauri ya rushwa 500 katika mahakama mbalimbali nchini ikilinganishwa na mashauri 662 yaliyofunguliwa mwaka 2024. Aidha, mashauri 527 yalitolewa uamuzi mahakamani mwaka 2025 ikilinganishwa na mashauri 676 yaliyotolewa uamuzi mwaka 2024. Kutokana na uamuzi uliotolewa, Jamhuri ilishinda mashauri 413 ikilinganishwa na mashauri 436 iliyoshinda mwaka 2024.

449. Kwa mujibu wa taarifa ya Transparency International (TI) ya mwaka 2025, Tanzania ilipata alama 40 kati ya 100 katika Fahirisi ya Rushwa ikilinganishwa na alama 41 mwaka 2024 (**Kielelezo Na. 18.1**). Kwa matokeo hayo, Tanzania ilishika nafasi ya pili miongoni mwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na nafasi ya 14 barani Afrika kama ilivyokuwa mwaka 2024. Katika kupambana na rushwa katika sekta ya umma, Tanzania ilishuka hadi nafasi ya 84 kati ya nchi 182 mwaka 2025 kutoka nafasi ya 82 mwaka 2024.

Matokeo ya Fahirisi ya Rushwa yanaonesha kuwa hali ya udhibiti wa rushwa nchini imebaki kuwa shwari kwa ujumla, ingawa kuna kushuka kidogo kwa alama na nafasi ya kimataifa, hali inayoashiria haja ya kuimarisha zaidi juhudi za kuzuia na kupambana na rushwa.

**Kielelezo Na. 18.1: Mwenendo wa Fahirisi ya Rushwa katika Sekta ya Umma, Mwaka 2017 - 2025**




**Jitihada za Kupunguza Umaskini**

450. Mwaka 2025, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF. Hadi Desemba 2025, kaya zilizonufaika na Mpango wa TASAF zilikuwa 901,721 zenye wanakaya 3,829,710 (wanawake 2,144,217 na wanaume 1,685,493) kutoka kaya 1,371,916 zenye wanakaya 6,983,665 kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 34.3. Hii ilitokana na utekelezaji wa utaratibu wa kuhitimu kwa kaya (graduation) zilizoimarika kiuchumi.

451. Mwaka 2025, watoto wenye umri hadi miaka mitano (5) waliotakiwa kuhudhuria kliniki walionufaika na Mpango wa TASAF walikuwa 108,004, sawa na asilimia 2.8 ya wanufaika wote na wazee wenye umri zaidi ya miaka 60 walikuwa 507,929 (asilimia 13.3), kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 18.3**. Aidha, kaya zilizoimarika kiuchumi na kuweza kumudu kuendesha maisha bila kutegemea ruzuku ya TASAF zilifikia 470,195 mwaka 2025 kutoka kaya 394,505 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 19.2. Hii ilitokana na utoaji wa ruzuku ya uzalishaji mali na mafunzo kwa kaya hizo uliosaidia kuendeleza shughuli za kuongeza kipato.

**Jedwali Na. 18.3: Wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini, Mwaka 2024 - 2025**

| Jinsia | Idadi ya Wanufaika | | Idadi ya Wanufaika kwa Umri Mwaka 2025 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2024 | 2025 | 0 - 5 | 6 - 18 | 19 - 60 | 60+ |
| Wanaume | 3,489,958 | 1,685,493 | 37,523 | 690,885 | 777,624 | 179,461 |
| Wanawake | 3,493,707 | 2,144,217 | 70,481 | 744,509 | 1,000,759 | 328,468 |
| **Jumla** | **6,983,665** | **3,829,710** | **108,004** | **1,435,394** | **1,778,383** | **507,929** |
| **Asilimia ya wanufaika** | | | **2.8** | **37.5** | **46.4** | **13.3** |

**Chanzo**: Mfuko wa Maendeleo ya Jamii

452. Hadi Desemba 2025, shilingi bilioni 2,229.13 zilitolewa kupitia uhawilishaji wa fedha kwa wanufaika ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,035.58 zilizotolewa kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 9.5. Aidha, vikundi 74,967 vyenye wanachama 996,308 (wanawake 854,480 na wanaume 141,828) viliundwa kutoka katika kaya maskini mwaka 2025 ikilinganishwa na vikundi 68,346 vyenye wanachama 906,958 mwaka 2024, sawa na ongezeko la vikundi kwa asilimia 9.7. Hii ilitokana na wanufaika kuhamasika kuunda vikundi vya kuweka akiba na kukopeshana kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali. Vilevile, shilingi bilioni 8.9 zilikopeshwa kwa wanachama wa vikundi kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 7.6 zilizokopeshwa mwaka 2024.


453. Mwaka 2025, Serikali kwa kushirikiana na walengwa wa Mpango wa TASAF iliendelea kutekeleza miradi ya ajira za muda kwa lengo la kuongeza kipato cha kaya maskini na kuchochea maendeleo ya jamii. Katika kipindi hicho, miradi 32,783 iliyotekelezwa ilitoa ajira za muda na shilingi bilioni 248.9 zililipwa kwa walengwa walioshiriki katika utekelezaji wa miradi ikilinganishwa na miradi 27,863 mwaka 2024. Aidha, miradi hiyo ilinufaisha kaya 814,889 mwaka 2025 ikilinganishwa na kaya 662,374 zilizonufaika mwaka 2024. Miradi hiyo ililenga sekta za huduma za jamii ikiwemo afya, elimu na maji.

454. Mwaka 2025, Serikali ilikamilisha zoezi la Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi Tanzania - IHBS ambapo kwa mara ya kwanza utafiti huu umefanyika kwa pamoja kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na hivyo kutoa matokeo ya jumla ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kabla ya zoezi hilo la pamoja, Tanzania Bara ilishafanya tafiti saba (7) kuanzia mwaka 1969 na Tanzania Zanzibar tafiti nne (4) tangu mwaka 2004/05. Utafiti huu ni chanzo kikuu cha kutoa takwimu za viashiria vya upimaji na utekelezaji wa jitihada za Serikali za kupunguza umaskini na kukuza uchumi katika ngazi zote za utawala nchini.


455. Matokeo ya Utafiti yanaonesha kuwa jumla ya watu 16,980,274 Tanzania, sawa na asilimia 24.9 ya watu wote wanaishi katika hali ya umaskini wa mahitaji ya msingi mwaka

2025. Kati ya hao, Tanzania bara walikuwa watu 16,563,733 na Tanzania Zanzibar watu 416,541. Aidha, mwenendo wa kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi Tanzania Bara umeendelea kupungua kutoka asilimia 34.4 mwaka 2007 hadi asilimia 25.1 mwaka 2025. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, mwenendo wa kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi nao umeendelea kupungua kutoka asilimia 34.4 mwaka 2009/10 hadi asilimia 19.9 mwaka 2025. Kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi ni kikubwa zaidi kwa maeneo ya vijijini ikilinganishwa na mijini (**Kielelezo Na. 18.2a na Kielelezo Na. 18.2b**).

**Kielelezo Na. 18.2a: Kiwango cha Umaskini wa Mahitaji ya Msingi Tanzania Bara**




**Kielelezo Na. 18.2b: Kiwango cha Umaskini wa Mahitaji ya Msingi Tanzania Zanzibar**




456. Kulingana na matokeo hayo, kaya maskini zilizonufaika kupitia programu ya TASAF zimepungua na kufikia asilimia 6.7 ya watu Tanzania Bara mwaka 2025 kutoka asilimia 8.4 mwaka 2017/18. Hii ni kutokana na jitihada za Serikali katika kuinua hali za maisha ya wananchi kupitia utekelezaji wa programu mbalimbali za kuwezesha wananchi kiuchumi ikiwemo programu ya TASAF zilizowezesha wananchi kujikwamua kiuchumi. Hata hivyo, taarifa hizi zinaonesha kuwa bado jitihada zaidi zinahitajika kuendelea kupambana na adui umasikini.

457. Kwa upande wa viashiria visivyo vya umaskini, matokeo ya Utafiti wa IBHS yanaonesha kuwa kaya zenye makazi yaliyojengwa kwa vifaa vilivyoboreshwa (paa, sakafu na ukuta) zimeendelea kuongezeka. Kwa mujibu wa Utafiti zaidi ya asilimia 75 ya kaya Tanzania zinamiliki makazi wanayoishi na asilimia 55 ya kaya Tanzania zinaishi kwenye makazi bora (paa asilimia 89.7, kuta asilimia 66.8 na sakafu asilimia 60.1). Aidha, kwa mujibu wa matokeo ya Utafiti wa IHBS, idadi ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi wanaojua kusoma na kuandika imeongezeka na kufikia asilimia 88.0 kwa wanaume na asilimia 82.1 kwa wanawake mwaka 2025 ikilinganishwa na wanaume asilimia 86.8 na wanawake asilimia 79.5 kulingana na matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

## SURA YA 19

## UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI

**Usajili wa Miradi ya Uwekezaji**

458. Mwaka 2025, Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Tanzania - TISEZA ilisajili miradi 956 ikilinganishwa na miradi 901 iliyosajiliwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 6.1. Kati ya hiyo, miradi 297 ilikuwa ya wawekezaji wa ndani, miradi 473 ya wageni na miradi 185 ya ubia kati ya wawekezaji wa ndani na wageni. Aidha, miradi iliyosajiliwa ilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 11,429.80 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 9,312.69 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 22.7. Hii ilichangiwa na kuendelea kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara, utoaji wa huduma kwa njia ya kielektroniki pamoja na kupeleka huduma karibu na wawekezaji kupitia ofisi za kanda. Kati ya miradi iliyosajiliwa, miradi 66 ilikuwa ya upanuzi na ukarabati mwaka 2025 ikilinganishwa na miradi 51 ya upanuzi na ukarabati iliyosajiliwa mwaka 2024. Miradi iliyosajiliwa ilizalisha fursa za ajira 180,574 mwaka 2025 ikilinganishwa na fursa za ajira 212,293 zilizozalishwa mwaka 2024.

**Mgawanyo wa Miradi Iliyosajiliwa Kisekta**

459. Mwaka 2025, sekta ya uzalishaji viwandani iliongoza kwa kusajili miradi yenye thamani ya dola za Marekani milioni 4,713.68, ikifuatiwa na sekta ya majengo ya biashara dola za Marekani milioni 1,563.55 na sekta ya kilimo dola za Marekani milioni 1,264.52. Katika kipindi hicho, sekta ya uzalishaji viwandani iliongoza kwa usajili wa miradi 422, ikifuatiwa na usafirishaji mizigo miradi 135 na ujenzi wa majengo ya biashara miradi 108 (**Jedwali Na. 19.1**).

**Jedwali Na. 19.1: Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa Mwaka 2025**

| Na. | Miradi iliyosajiliwa | | | | | Fursa za Ajira | Thamani (Dola za Marekani Milioni) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Sekta | Watanzania | Wageni | Ubia | Jumla | | |
| 1. | Uzalishaji viwandani | 86 | 262 | 74 | 422 | 63,722 | 4,713.68 |
| 2. | Ujenzi majengo ya biashara | 26 | 66 | 16 | 108 | 33,391 | 1,563.55 |
| 3. | Usafirishaji mizigo | 84 | 28 | 23 | 135 | 20,036 | 1,029.48 |
| 4. | Kilimo | 33 | 48 | 21 | 102 | 33,986 | 1,264.52 |
| 5. | Utalii | 41 | 21 | 31 | 93 | 5,877 | 927.54 |
| 6. | Miundombinu ya kiuchumi | 9 | 13 | 3 | 25 | 17,862 | 731.42 |
| 7. | Nishati | 4 | 4 | 5 | 13 | 692 | 488.21 |
| 8. | Madini | 2 | 12 | 4 | 18 | 1,310 | 360.77 |
| 9. | Huduma | 6 | 12 | 7 | 25 | 2,393 | 141.32 |
| 10. | Mawasiliano | 0 | 2 | - | 2 | 197 | 126.01 |
| 11. | Rasilimali watu | 5 | 5 | - | 10 | 966 | 72.3 |
| 12. | TEHAMA | 1 | 0 | | 1 | 60 | 6.0 |
| 13. | Huduma za kifedha | 1 | 0 | 1 | 2 | 82 | 5.0 |
| | **Jumla** | **298** | **473** | **185** | **956** | **180,574** | **11,429.80** |

**Chanzo**: Kituo cha Uwekezaji Tanzania

### Mgawanyo wa Miradi Iliyosajiliwa Kimkoa

460. Mwaka 2025, Mkoa wa Dar es Salaam uliendelea kuongoza kwa usajili wa miradi 343, sawa na asilimia 35.9 ya miradi yote, ikifuatiwa na Mkoa wa Pwani miradi 217 (asilimia 22.7) na Arusha miradi 68 (asilimia 7.1), kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 19.2**.

**Jedwali Na. 19.2: Mgawanyo wa Miradi Iliyosajiliwa Kimkoa Mwaka 2025**

| Mkoa | Sekta | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kilimo | Ujenzi majengo ya biashara | Miundombinu ya kiuchumi | Nishati | Huduma za Fedha | Rasilimali watu | Uzalishaji viwandani | Huduma | Mawasiliano | Madini | TEHAMA | Utalii | Usafirishaji | Jumla ya Miradi | Mgawanyo (Asilimia) |
| Dar-es-salaam | 2 | 68 | 12 | 1 | 1 | 7 | 124 | 17 | 1 | 0 | 1 | 19 | 90 | 343 | 35.9 |
| Pwani | 18 | 19 | 8 | 2 | 0 | 0 | 148 | 0 | 1 | 0 | 0 | 4 | 17 | 217 | 22.7 |
| Arusha | 8 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 14 | 3 | 0 | 0 | 0 | 32 | 6 | 68 | 7.1 |
| Dodoma | 4 | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 | 20 | 1 | 0 | 2 | 0 | 5 | 4 | 42 | 4.4 |
| Mwanza | 5 | 3 | 1 | 2 | 0 | 2 | 16 | 2 | 0 | 1 | 0 | 2 | 4 | 38 | 4.0 |
| Geita | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 21 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 26 | 2.7 |
| Morogoro | 12 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 1 | 23 | 2.4 |
| Tanga | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 3 | 21 | 2.2 |
| Iringa | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 21 | 2.2 |
| Kilimanjaro | 4 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 8 | 0 | 0 | 1 | 0 | 4 | 0 | 20 | 2.1 |
| Mara | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 14 | 0 | 19 | 2.0 |
| Mbeya | 5 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 8 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 18 | 1.9 |
| Shinyanga | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 | | 2 | 0 | 0 | 2 | 14 | 1.5 |
| Njombe | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 13 | 1.4 |
| Mtwara | 5 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 12 | 1.3 |
| Songwe | 0 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 10 | 1.0 |
| Lindi | 4 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 10 | 1.0 |
| Manyara | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 7 | 0.7 |
| Kagera | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0.7 |
| Rukwa | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 6 | 0.6 |
| Singida | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 5 | 0.5 |
| Kigoma | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 5 | 0.5 |
| Katavi | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0.4 |
| Ruvuma | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0.3 |
| Tabora | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0.3 |
| Simiyu | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0.2 |
| **Jumla** | **102** | **108** | **25** | **13** | **1** | **10** | **422** | **25** | **2** | **18** | **2** | **93** | **135** | **956** | **100.0** |

**Chanzo**: Kituo cha Uwekezaji Tanzania

### Uwekezaji wa Sekta Binafsi Ndani ya Nchi

461. Kwa mujibu wa mwelekeo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, sekta binafsi inakusudiwa kuwa mhimili mkuu wa utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kuchangia

takribani asilimia 70 ya rasilimali zinazohitajika. Katika kufanikisha azma hiyo, Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji sambamba na kusimamia utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti kwa lengo la kuongeza uwezo wa sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na maendeleo. Hali hiyo imeanza kuonesha matokeo chanya kupitia ongezeko la mikopo inayotolewa kwa sekta binafsi. Mwaka 2025, mikopo iliyotolewa na benki za biashara kwa sekta binafsi iliongezeka kwa asilimia 23.6 na kufikia shilingi bilioni 44,603.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 36,097.4 mwaka 2024. Mwenendo huu unaashiria kuongezeka kwa mchango wa sekta binafsi katika kuchochea ukuaji wa uchumi na kusaidia utekelezaji wa malengo ya maendeleo ya muda mrefu.

**Uwekezaji wa Sekta Binafsi Kutoka Nje**

462. Kwa mujibu wa Taarifa ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2025, uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje (stock) uliongezeka kwa asilimia 12.1 na kufikia dola za Marekani milioni 24,754.1 mwaka 2024 kutoka dola za Marekani milioni 22,074.4 mwaka 2023. Kati ya kiasi hicho, uwekezaji wa moja kwa moja - FDI ulifikia dola za Marekani milioni 21,698.9, sawa na asilimia 87.7 ya uwekezaji wote, uwekezaji wa hisa ulifikia dola za Marekani 272.7 (asilimia 1.1) na uwekezaji mwingine ulifikia dola za Marekani 2,782.5 (asilimia 11.2). Katika kipindi hicho, mitaji iliyowekezwa na sekta binafsi kutoka nje ya nchi kwa bei za miaka husika (inflows) ilikuwa dola za Marekani milioni 1,984.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,694.8 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 17.1 (**Jedwali Na. 19.3**).

**Jedwali Na. 19.3: Uwekezaji wa Sekta Binafsi kutoka Nje ya Nchi (Dola za Marekani Milioni), Mwaka 2020 - 2024**

| Aina ya uwekezaji | Kiasi kilichowekezwa (Inflows) | | | | | Limbikizo lililowekezwa (Stock) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023r | 2024 |
| Uwekezaji wa moja kwa moja kutoka Nje | 943.8 | 1,190.5 | 1,437.6 | 1,648.9 | 1,656.0 | 15,612.6 | 15,741.1 | 18,095.8 | 19,455.3 | 21,698.9 |
| Uwekezaji wa Hisa | 1.8 | 4.9 | 0.2 | 1.4 | 6.5 | 124.8 | 126.8 | 195.8 | 216.7 | 272.7 |
| Uwekezaji mwingine | -85.5 | -8.6 | 308.1 | 44.5 | 322.1 | 2,724.5 | 3,056.5 | 3,890.8 | 2,402.4 | 2,782.5 |
| **Jumla** | **860.1** | **1,186.8** | **1,745.8** | **1,694.8** | **1,984.6** | **18,461.9** | **18,924.3** | **22,182.4** | **22,074.4** | **24,754.1** |


**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

**Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje**

463. Mwaka 2024, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI inflows) ulikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 1,656.0 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,648.9 mwaka 2023 (**Kielelezo Na. 19.1**). Katika kipindi hicho, mchango wa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nchi za EAC na SADC ulikuwa asilimia 4.4 na asilimia 20.6 mtawalia ikilinganishwa na asilimia 3.9 na asilimia 26.1 mwaka 2023. Aidha, nchi ya Kenya ilichangia zaidi katika uwekezaji kutoka nchi za EAC na Afrika Kusini kwa upande wa SADC. Kwa upande mwingine, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nchi za Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo - OECD ulikuwa asilimia 55.6 mwaka 2024

ikilinganishwa na asilimia 44.2 mwaka 2023 ambapo nchi ya Uingereza iliongoza kwa asilimia 54.3 (**Jedwali Na. 19.4**).

**Kielelezo Na. 19.1: Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje, Mwaka 2020 - 2024**




**Jedwali Na. 19.4: Uwekezaji wa Moja kwa Moja Kikanda na Makundi ya Kiuchumi (Dola za Marekani Milioni), Mwaka 2020 - 2024**


| Kanda/Nchi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Mchango (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **OECD** | **284.0** | **271.4** | **614.2** | **698.7** | **920.8** | **55.6** |
| Uingereza | 111.4 | 149.3 | 124.4 | 167.4 | 499.8 | 30.2 |
| Umoja wa Falme za Kiarabu | 7.3 | 3.8 | -0.1 | 27.5 | 167.5 | 10.1 |
| Uholanzi | 56.6 | 73.2 | 181.9 | 134.2 | 109.9 | 6.6 |
| Denmaki | 12.0 | 20.3 | 24.0 | 30.1 | 40.1 | 2.4 |
| Ujerumani | -6.7 | -3.3 | 19.1 | 4.8 | 38.2 | 2.3 |
| Australia | -109.8 | -186.5 | 82.8 | 217.0 | 26.3 | 1.6 |
| Ufaransa | 31.7 | 42.0 | 39.4 | 6.1 | 24.2 | 1.5 |
| Nchi nyingine za OECD | 181.6 | 172.6 | 142.8 | 111.8 | 14.7 | 0.9 |
| **SADC** | **44.2** | **126.5** | **208.6** | **430.9** | **341.3** | **20.6** |
| Botswana | -0.6 | -0.5 | 3.9 | 56.0 | -2.4 | -0.1 |
| Mauritius | 48.9 | 73.5 | 150.3 | 242.0 | 101.8 | 6.1 |
| Afrika ya Kusini | -6.2 | 51.4 | 54.4 | 121.8 | 247.4 | 14.9 |
| Eswatini | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Nchi nyingine za SADC | 2.2 | 2.1 | -0.1 | 11.1 | -5.6 | -0.3 |
| **EAC** | **24.7** | **30.0** | **49.9** | **64.8** | **73.1** | **4.4** |
| Burundi | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Kenya | 24.6 | 30.3 | 48.9 | 63.8 | 71.5 | 4.3 |
| Rwanda | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Sudani Kusini | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Uganda | 0.1 | -0.2 | 1.0 | 1.1 | 1.5 | 0.1 |
| DRC | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Somalia | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 0.0 |
| **Kanda nyingine** | **590.8** | **762.6** | **564.9** | **454.4** | **320.8** | **19.4** |
| **Jumla Kuu** | **943.8** | **1,190.5** | **1,437.6** | **1,648.9** | **1,656.0** | **100.0** |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania


**Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje kwa Shughuli za Kiuchumi**

464. Mwaka 2024, shughuli za uchimbaji madini na mawe zilikuwa na uwekezaji mkubwa zaidi wenye thamani ya dola za Marekani milioni 442.2, ikifuatiwa na fedha na bima dola za Marekani milioni 401.3, uzalishaji bidhaa viwandani dola za Marekani milioni 223.1 na habari na mawasiliano dola za Marekani milioni 152.1. Shughuli hizo zilichangia wastani wa asilimia 73.6 ya uwekezaji wote wa moja kwa moja kutoka nje. Aidha, shughuli za kilimo, ujenzi, na usafirishaji na uhifadhi mizigo zilivutia uwekezaji wa moja kwa moja wa asilimia 19.4 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 5.8 mwaka 2023 (**Kielelezo Na. 19.2** na **Jedwali Na. 19.5**).

**Kielelezo Na. 19.2a: Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje ya Nchi kwa Shughuli za Kiuchumi, Limbikizo Mwaka 2024 (Dola za Marekani Milioni)**




**Kielelezo Na. 19.2b: Mchanganuo wa Kiasi Kilichowekezwa kutoka Nje ya Nchi kwa Shughuli za Kiuchumi Mwaka 2024 (Asilimia)**



**Jedwali Na. 19.5: Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje kwa Shughuli za Kiuchumi (Dola za Marekani Milioni), Mwaka 2020 - 2024**

| Shughuli za kiuchumi | Kiasi kilichowekezwa | | | | | Limbikizo lililowekezwa | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
| Malazi na Huduma za Chakula | -7.5 | -0.3 | 36.3 | 15.2 | 23.6 | 372.2 | 356.9 | 545.7 | 419.7 | 279.8 |
| Huduma zinazohusiana na Utawala | -12.0 | 2.0 | -3.7 | 4.4 | 10.3 | 61.2 | 78.1 | 123.2 | 124.1 | 140.6 |
| Kilimo | 15.5 | 20.8 | 14.3 | 57.8 | 130.4 | 1,596.4 | 579.5 | 660.4 | 761.6 | 844.3 |
| Sanaa na Burudani | 0.0 | 0.1 | 0.7 | 0.1 | 0.0 | 0.6 | 2.1 | 1.4 | 0.0 | 0.0 |
| Ujenzi | -2.3 | -15.4 | 15.5 | 19.6 | 112.9 | 286.1 | 305.8 | 292.0 | 274.1 | 414.3 |
| Elimu | 0.8 | -2.2 | -0.1 | -0.5 | -0.3 | 10.5 | 9.7 | 7.9 | 7.0 | 7.1 |
| Umeme na Gesi | -22.8 | -2.3 | 1.5 | 8.0 | 9.5 | 36.7 | 13.9 | 48.6 | 46.5 | 59.6 |
| Fedha na Bima | 85.4 | 132.8 | 238.4 | 267.6 | 401.3 | 1,321.7 | 1,463.7 | 1,565.8 | 1,913.1 | 2,531.2 |
| Afya na Huduma za Jamii | -1.2 | 11.3 | -4.4 | 4.1 | -1.7 | 60.0 | 92.7 | 16.5 | 54.8 | 55.0 |
| Habari na Mawasiliano | 60.3 | 34.5 | 89.5 | 198.0 | 152.1 | 1,517.2 | 1,204.6 | 2,044.4 | 2,570.2 | 2,895.1 |
| Uzalishaji Viwandani | 176.2 | 352.0 | 180.1 | 361.0 | 223.1 | 2,375.1 | 2,412.1 | 3,132.1 | 2,976.5 | 3,344.9 |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 614.2 | 596.3 | 847.1 | 532.5 | 442.2 | 7,205.0 | 8,509.1 | 8,640.6 | 9,157.8 | 9,798.7 |
| Shughuli za kitaalamu na kisayansi | 1.0 | 0.6 | 0.0 | 0.4 | 0.2 | 20.1 | 0.2 | 20.1 | 17.5 | 18.7 |
| Upangishaji Majengo | -4.0 | -1.2 | -0.2 | 6.4 | 6.7 | 58.3 | 83.5 | 71.2 | 81.1 | 93.0 |
| Usafirishaji na Uhifadhi Mizigo | 26.6 | 18.1 | 12.1 | 18.0 | 77.4 | 213.6 | 129.5 | 278.4 | 301.9 | 422.1 |
| Biashara | 13.4 | 43.5 | 10.7 | 156.3 | 68.6 | 477.9 | 499.8 | 647.7 | 749.6 | 794.6 |
| **Jumla** | **943.8** | **1,190.5** | **1,437.6** | **1,648.9** | **1,656.0** | **15,612.6** | **15,741.1** | **18,095.8** | **19,455.3** | **21,698.9** |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

### Mazingira ya Biashara na Uwekezaji

465. Mwaka 2025, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI). Katika kipindi hicho, utekelezaji wa Mpango huo uliwezesha maboresho ya sheria na kanuni 28 ikijumuisha kufutwa au kupunguzwa kwa tozo na ada 245 ikilinganishwa na tozo na ada 37 zilizofutwa au kupunguzwa mwaka 2024. Aidha, Mfumo wa Pamoja wa Ubadilishanaji wa Taarifa Serikalini - GovESB uliendelea kuwezesha mifumo ya Serikali kuwasiliana kwa urahisi na kubadilishana taarifa. Hadi Desemba 2025, mifumo 252 ya taasisi 200 za umma ilikuwa imeunganishwa kupitia mfumo wa GovESB ikilinganishwa na mifumo 202 ya taasisi 179 za umma iliyounganishwa kipindi kama hicho mwaka 2024.

466. Mwaka 2025, Serikali iliendelea kuimarisha na kuboresha Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato Serikalini - GePG ili kurahisisha ulipaji ada na tozo mbalimbali Serikalini. Hadi Desemba 2025, watoa huduma na taasisi 1,236 waliunganishwa katika mfumo huo kutoka watoa huduma na taasisi 1007 zilizokuwa zimeunganishwa kipindi kama hicho mwaka 2024.

### Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

467. Mwaka 2025, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi - NEEC kupitia mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi lilitoa mikopo, dhamana na ruzuku zenye thamani ya shilingi bilioni 2,439 kwa wajasiriamali wananchi 8,659,360 (wanawake 4,243,086 na wanaume 4,416,274) ikilinganishwa na shilingi bilioni 759.7 zilizotolewa kwa wajasiriamali 6,183,835 mwaka 2024. Hii ilitokana na Serikali kuendelea kuimarisha uratibu na utendaji wa mifuko na programu za uwezeshaji pamoja na kuwepo kwa

mazingira wezeshi yaliyotoa fursa za biashara kwa wajasiriamali. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 1,197 zilitolewa kama mikopo ya moja kwa moja na dhamana kwa wanufaika 375,011, shilingi bilioni 1,135 ilikuwa ruzuku iliyotolewa kwa wanufaika 8,238,289 na shilingi bilioni 106.97 zilitolewa kwa wanufaika 46,060 kupitia programu za uwezeshaji zinazolenga kuongeza fursa za ajira kwa wananchi. Aidha, mifuko na programu ilizalisha ajira 10,026,124 (wanawake 5,691,198 na wanaume 4,334,926) mwaka 2025 ikilinganishwa na ajira 8,153,224 zilizozalishwa mwaka 2024. Kwa upande mwingine, shilingi bilioni 981.5 sawa na asilimia 82 ilirejeshwa mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 493.9 zilizorejeshwa mwaka 2024 kutokana na mikopo iliyoiva katika miaka husika (**Jedwali Na. 19.6**).

**Jedwali Na. 19.6: Mchanganuo wa Mikopo Iliyotolewa kwa Shughuli za Kiuchumi (Shilingi Milioni), Mwaka 2024 - 2025**

| Sekta | 2024 | | 2025 | | Mchango (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|
| | Kiasi | Marejesho | Kiasi | Marejesho | |
| Afya | 12,621 | 16,520 | 37,000 | 30,340 | 3.1 |
| Elimu | 49,987 | 64,220 | 146,400 | 120,048 | 12.2 |
| Madini | 32,986 | 39,126 | 96,600 | 79,212 | 8.1 |
| Kilimo | 190,118 | 198,645 | 556,800 | 456,576 | 46.5 |
| Utalii | 37,709 | 63,195 | 110,400 | 90,528 | 9.2 |
| Viwanda na Biashara | 57,416 | 74,673 | 168,400 | 138,088 | 14.1 |
| Nishati | 20,784 | 28,993 | 60,900 | 49,938 | 5.1 |
| Nyinginezo | 6,429 | 8,542 | 20,500 | 16,810 | 1.7 |
| **Jumla** | **408,049** | **493,915** | **1,197,000** | **981,540** | **100** |

**Chanzo:** Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

468. Mwaka 2025, NEEC iliratibu utoaji wa mafunzo kwa wajasiriamali 691,755 (wanawake 387,302 na wanaume 304,453) ikilinganishwa na wajasiriamali 628,514 waliopata mafunzo mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 10.1. Hii ilitokana na uhamasishaji na mwitikio wa wajasiriamali kushiriki katika mafunzo mbalimbali ya uwezeshaji wananchi kiuchumi.

469. Hadi Desemba 2025, vituo vya uwezeshaji wananchi kiuchumi vilikuwa 29 ikilinganishwa na vituo 27 kipindi kama hicho mwaka 2024. Vituo hivyo vilitoa huduma kwa wananchi 49,828 (wanawake 24,712 na wanaume 25,116) mwaka 2025 ikilinganishwa na wananchi 43,716 waliopata huduma mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 14.0. Hii ilitokana na kuongezwa kwa baadhi ya huduma muhimu katika vituo, ikiwemo urasimishaji wa biashara kwa njia za leseni, usajili wa vikundi, pamoja na huduma za ruzuku, dhamana za mikopo, masoko na ushauri wa kitaalamu. Katika kipindi hicho, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 15.19 ilitolewa kupitia vituo vya uwezeshaji kwa wajasiriamali 1,435 (wanawake 731, wanaume 704) ikilinganishwa na mikopo ya shilingi bilioni 7.09 iliyotolewa kwa wajasiriamali 341 mwaka 2024. Ongezeko la mikopo na wanufaika

kulichangiwa na kuanzishwa kwa huduma ya mikopo ya asilimia 10 kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kupitia vituo vya uwezeshaji. Aidha, marejesho ya mikopo yalikuwa shilingi bilioni 14.4 sawa na asilimia 95 ya mikopo iliyoiva mwaka 2025 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6.73 (asilimia 94.9) mwaka 2024. Urejeshaji wa mikopo unaoridhisha ulitokana na jitihada za viongozi wa vituo kutembelea miradi ya wanufaika wa mikopo na utunzaji wa kumbukumbu za fedha.

**Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati**

470. Mwaka 2025, miradi ya kimkakati na uwekezaji katika sekta mbalimbali ilizalisha ajira za moja kwa moja 286,219 ikilinganishwa na ajira 217,808 zilizozalishwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 31.4. Kati ya ajira zilizozalishwa, walikuwa ajira 273,790 zilikuwa za watanzania na ajira 12,429 za wageni mwaka 2025 ikilinganishwa na ajira 208,526 za watanzania na ajira 9,282 za wageni mwaka 2024. Ongezeko la ajira kwa watanzania lilitokana na uzingatiaji wa vipengele vya mikataba kuhusu ushiriki wa watanzania katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati. Kwa upande mwingine, miradi ya kimkakati 5,330 yenye thamani ya bilioni 12.09 ilitekelezwa mwaka 2025 ikilinganishwa na miradi 4,691 iliyotekelezwa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 13.6. Kati ya miradi hiyo, wakandarasi wa kitanzania walishiriki katika kutekeleza miradi 5,177, sawa na asilimia 97.1 na wakandarasi wa kigeni walitekeleza miradi 153. Kati ya thamani ya miradi yote iliyotekelezwa, shilingi bilioni 5.06 sawa na asilimia 42.14 zilienda kwa kampuni za ndani na shilingi bilioni 6.99 sawa na asilimia 57.86 zilienda kwa kampuni za kigeni.

**Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

471. Mwaka 2025, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi iliendelea kutekeleza miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi - PPP kama njia mbadala ya ugharamiaji wa miradi ya maendeleo. Hadi Desemba 2025, miradi nane (8) yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 3.94 ilitekelezwa kwa njia ya PPP ikilinganishwa na miradi minne (4) iliyotekelezwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Miradi hiyo ni pamoja na: ujenzi wa kituo cha biashara Kariakoo; uendeshaji na ukarabati wa bandari ya Dar es Salaam kupitia Kampuni DP World and ADAN Group; ukarabati, uendeshaji, na usimamizi wa reli ya Tanzania - Zambia (TAZARA); na uendeshaji wa mabasi yaendayo haraka Awamu ya I na II Dar es Salaam. Katika kipindi hicho, miradi mitatu (3) ilifikia hatua ya majadiliano ya mikataba ikijumuisha: mradi wa ujenzi wa hoteli ya nyota nne, mradi wa kituo cha biashara katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere; na mradi wa ukaguzi wa vyombo vya moto. Kwa upande mwingine, miradi mitatu (3) ilikuwa katika hatua za ununuzi wa mbia mwaka 2025 ikilinganishwa na miradi minne (4) iliyokuwa katika hatua za ununuzi mwaka 2024. Miradi hiyo ni ujenzi wa barabara ya haraka Kibaha - Chalinze Lot 1 (78 km), Chalinze - Morogoro Lot 2 (84.9 km) na ujenzi wa nyumba za wanafunzi katika chuo cha CBE.

**Jedwali Na. 69: KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA: MIRADI YA UWEKEZAJI ILIYOSAJILIWA, MWAKA 2024 - 2025**

| Sekta | 2024 | | | | | | | | 2025 | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | A | B | C | D | E | F | G | H | A | B | C | D | E | F | G | H |
| Kilimo | 79 | 73 | 6 | 28 | 38 | 13 | 125,760 | 687.2 | 102 | 92 | 10 | 33 | 48 | 21 | 33,986 | 1,264.5 |
| Mawasiliano | 5 | 4 | 1 | 1 | 2 | 2 | 836 | 809.7 | 2 | 1 | 1 | 0 | 2 | 0 | 197 | 126.0 |
| Utalii | 83 | 75 | 8 | 43 | 18 | 22 | 6,949 | 348.8 | 93 | 77 | 16 | 41 | 21 | 31 | 5,877 | 927.5 |
| Uzalishaji Viwandani | 415 | 400 | 15 | 98 | 237 | 80 | 45,883 | 4,079.0 | 422 | 396 | 26 | 86 | 262 | 74 | 63,722 | 4,713.7 |
| Majengo ya biashara | 105 | 103 | 2 | 32 | 57 | 16 | 7,475 | 1,135.1 | 108 | 105 | 3 | 26 | 66 | 16 | 33,391 | 1,563.6 |
| Usafirishaji Mizigo | 149 | 132 | 17 | 92 | 29 | 28 | 18,622 | 1,361.2 | 135 | 127 | 8 | 84 | 28 | 23 | 20,036 | 1,029.5 |
| Huduma | 25 | 25 | 0 | 9 | 9 | 7 | 2,937 | 285.3 | 24 | 24 | | 6 | 12 | 7 | 2,393 | 141.3 |
| Rasilimali Watu | 14 | 13 | 1 | 9 | 4 | 1 | 2,181 | 142.7 | 10 | 10 | 0 | 5 | 5 | 0 | 966 | 72.3 |
| Madini | 7 | 7 | 0 | 2 | 1 | 4 | 135 | 7.4 | 18 | 18 | 0 | 2 | 12 | 4 | 1,310 | 360.8 |
| Nishati | 11 | 10 | 1 | 3 | 6 | 2 | 204 | 112.5 | 13 | 13 | 0 | 4 | 4 | 5 | 692 | 488.2 |
| Miundombinu ya Kiuchumi | 7 | 7 | 0 | 4 | 3 | 0 | 1,283 | 298.8 | 25 | 23 | 2 | 9 | 13 | 3 | 17,862 | 731.4 |
| Huduma za kifedha | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 28 | 45 | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 82 | 5.0 |
| TEHAMA | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 60 | 6.0 |
| **Jumla** | **901** | **850** | **51** | **321** | **404** | **176** | **212,293** | **9,312.7** | **956** | **890** | **66** | **298** | **473** | **185** | **180,574** | **11,429.8** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania

A Jumla ya Miradi Iliyosajiliwa

B Miradi Mipya

C Miradi inayoendelea

D Miradi ya wazawa

E Miradi ya Wageni

F Miradi ya Ubia

G Ajira

H Thamani ya Uwekezaji (USD Milioni)



Sehemu ya Nne

# Suala Maalum Kimaendeleo

## SURA YA 20

## MABORESHO YA TAKWIMU ZA PATO LA TAIFA

**Utangulizi**

472. Serikali inatekeleza mipango na mikakati mbalimbali ili kuboresha ustawi wa wananchi kwa kupunguza tofauti za kipato na kutokomeza umaskini. Ili kufikia azma hiyo, ni muhimu kuhakikisha upatikanaji wa takwimu sahihi zinazokidhi mahitaji kwa wakati na hivyo kufikia maamuzi yenye tija yanayozingatia upatikanaji wa takwimu sahihi na kwa wakati kwa maendeleo ya Taifa. Aidha, kukosekana kwa takwimu hizo kunaweza kusababisha matumizi yasiyo sahihi ya rasilimali adimu na kupunguza kiwango cha ustawi wa wananchi na Taifa kwa ujumla. Kwa msingi huo, Serikali imekuwa ikifanya maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa kwa kutumia mwaka wa kizio unaoakisi uhalisia kwa lengo la kupata makadirio sahihi ya ukubwa na muundo wa uchumi kwa kuzingatia miongozo mbalimbali ya kimataifa.

473. Mwaka wa kizio ni mwaka wa rejea unaotumika kukokotoa takwimu linganifu za Pato la Taifa za miaka mbalimbali. Kubadilisha mwaka wa kizio kunatokana na sababu mbalimbali ikiwemo; mabadiliko katika mifumo ya uzalishaji wa bidhaa katika uchumi; mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma; mabadiliko ya bidhaa kutokana na kukua kwa teknolojia na ubunifu; na mabadiliko ya mahitaji, ikiwemo mwenendo wa matumizi na upatikanaji wa bidhaa za kukuza mitaji. Kadiri mwenendo wa matumizi na uzalishaji unavyobadilika, mfumo wa bei nao hubadilika, hivyo kuendelea kutumia mwaka wa kizio wa zamani hauakisi hali halisi ya mwenendo wa uchumi. Aidha, matumizi ya takwimu za Pato la Taifa ni pamoja na: kutathmini hali ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi na Pato halisi la Taifa katika kipindi husika; kupanga mipango ya maendeleo na kutoa maamuzi ya kisera; kupima mchango wa shughuli za kiuchumi katika Pato la Taifa katika kipindi husika; msingi wa utayarishaji wa bajeti ya Serikali; kulinganisha uchumi wa nchi na nchi nyingine; kutathmini mabadiliko yanayotokea katika uchumi; na kuwianisha viashiria mbalimbali vya kiuchumi na Pato halisi la Taifa, ikiwemo deni la Serikali na mapato ya kodi.

**Historia ya Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa**

474. Uandaaji wa takwimu za Pato la Taifa kwa Tanzania Bara ulianza mwaka 1954. Tangu wakati huo, kumekuwa na maboresho ya miongozo ya kimataifa inayotumika katika kukokotoa Pato la Taifa, ikijumuisha mabadiliko katika wigo wa shughuli zote za kiuchumi. Takwimu za Pato la Taifa za vipindi vilivyopita zilitayarishwa kwa kuzingatia dhana, tafsiri na mchanganuo wa shughuli za kiuchumi unaotokana na mifumo ya ukokotoaji wa takwimu za Pato la Taifa wa Umoja wa Mataifa (United Nations Systems of National Accounts) ya miaka ya 1953, 1968, 1993 na 2008. Tangu kuanza kwa uandaaji wa takwimu za Pato la

Taifa kwa Tanzania Bara, maboresho ya takwimu hizo yamefanyika kwa awamu saba kama ifuatavyo:

i. Maboresho ya kwanza yalitumia mwaka wa kizio 1966 na yalizingatia Mfumo wa Ukokotoaji wa Takwimu za Pato la Taifa wa Umoja wa Mataifa wa Mwaka 1953;
ii. Maboresho ya pili yalitumia mwaka wa kizio 1976 na yalizingatia Mfumo wa Mwaka 1968;
iii. Maboresho ya tatu yalitumia mwaka wa kizio 1992 na yalizingatia Mfumo wa Mwaka 1968 na sehemu ya Mfumo wa Mwaka 1993;
iv. Maboresho ya nne yalitumia mwaka wa kizio 2001 na yalizingatia Mfumo wa Mwaka 1993;
v. Maboresho ya tano yalitumia mwaka wa kizio 2007 na yalizingatia Mfumo wa Mwaka 1993 na sehemu ya Mfumo wa Mwaka 2008;
vi. Maboresho ya sita yalitumia mwaka wa kizio 2015 na yalizingatia Mfumo wa Mwaka 2008; na
vii. Maboresho ya saba yametumia mwaka wa kizio 2019 na yamezingatia Mfumo wa Mwaka 2008.

**Dhana na Umuhimu wa Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa**

475. Maboresho ya takwimu za Pato la Taifa ni mchakato unaohusisha kubadilisha mwaka wa kizio uliopitwa na wakati na kutumia mwaka wa kizio wenye taarifa za karibuni. Maboresho hayo hufanyika ili kuhakikisha kuwa ukokotoaji wa takwimu za Pato la Taifa unaendana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia. Maboresho ya takwimu za Pato la Taifa hufanyika kwa sababu zifuatazo:

i. Takwimu za mwaka wa kizio husika kupitwa na wakati na hivyo kushindwa kutoa taswira halisi ya mabadiliko ya muundo wa uchumi kwa wakati huo;
ii. Kujumuisha mabadiliko yaliyojitokeza katika uchumi kwenye mifumo ya uzalishaji bidhaa, matumizi na uwekezaji;
iii. Kuzingatia mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma yaliyotokea katika kipindi husika;
iv. Kuhuisha orodha ya bidhaa kutokana na maendeleo ya kijamii, kisayansi, kiteknolojia na ubunifu yanayosabisha bidhaa mpya kuingia sokoni huku bidhaa za zamani zikipungua na kupotea;
v. Kujumuisha taarifa mpya kutoka katika taarifa za kiutawala, sensa na tafiti zilizofanyika miaka ya karibuni; na
vi. Kuzingatia matakwa mapya ya Mfumo wa Kimataifa wa kutayarisha takwimu za Pato la Taifa na miongozo ya kuainisha shughuli za kiuchumi.

476. Kutokana na sababu zilizoainishwa, ni muhimu kubadilisha mwaka wa kizio ili kuboresha makadirio ya kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa na kuendana na mabadiliko ya uchumi kwa ujumla.

**Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa kwa Kutumia Mwaka wa Kizio 2019**

477. Maboresho ya takwimu za Pato la Taifa ya sasa ni ya saba kihistoria. Maboresho haya yametumia mwaka wa kizio 2019 na Mfumo wa Ukokotoaji wa Takwimu za Pato la Taifa wa Mwaka 2008 (Systems of National Accounts - SNA 2008). Lengo la maboresho haya ni kuzingatia miongozo ya kikanda na kimataifa ambayo inazitaka nchi wanachama kufanya maboresho katika takwimu za Pato la Taifa (rebasing) kila baada ya miaka mitano (5). Hatua hii inalenga kufikia ubora na usahihi wa takwimu za kiuchumi, kutoa taswira halisi ya mwenendo wa uchumi, na kuhakikisha usawa na ulinganifu wa takwimu za Pato la Taifa. Malengo mengine ni kuwezesha: uandaji wa mipango na ufanyaji wa maamuzi kwa Serikali; kuwa na takwimu za uhakika za kufanyia tafiti; na upatikanaji wa viashiria kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya kitaifa na kimataifa.

478. Kwa kuzingatia takwa la kufanya maboresho ya takwimu za Pato la Taifa kila baada ya miaka mitano, mwaka 2020 ulipaswa kuwa mwaka wa kizio. Hata hivyo, mwaka huo haukukidhi vigezo vya kuwa mwaka wa kizio kutokana na mdororo wa kiuchumi uliosababishwa na janga la UVIKO-19. Hivyo, mwaka 2019 ulichaguliwa kutokana na kukidhi vigezo muhimu, ikiwemo utulivu wa kiuchumi na upatikanaji wa takwimu za kuaminika kutoka kwenye tafiti, sensa na vyanzo vya kiutawala.

479. Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa kwa kutumia mwaka wa kizio 2019 yalizingatia miongozo, kanuni, mbinu na mifumo inayokubalika kimataifa, hususan Mfumo wa Ukokotoaji wa Takwimu za Pato la Taifa wa Mwaka 2008 na Mwongozo wa Kuainisha Shughuli Mbalimbali za Kiuchumi - ISIC Rev. 4. Aidha, maboresho hayo yalitumia mbinu ya Mizania ya Ugavi na Matumizi (Supply and Use Tables) ambayo iliwezesha upatikanaji wa takwimu za Pato la Taifa kwa njia za uzalishaji wa bidhaa na huduma, matumizi na mapato.

480. Taarifa zilizotumika katika kuandaa takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka wa kizio 2019 kwa Tanzania Bara zilijumuisha:

i. Tafiti na Sensa: Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022; Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Mwaka 2017/18; Utafiti wa Watu wenye Uwezo wa Kufanya Kazi (ILFS) wa Mwaka 2020/21; Sensa ya Kilimo ya Mwaka 2019/20; na Utafiti wa Mwaka wa Uzalishaji Viwandani 2018;

ii. Takwimu za Kiutawala: takwimu za uagizaji na uuzaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi, takwimu za mapato na matumizi ya Serikali pamoja na takwimu za mauzo kwenye mfumo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani; na

iii. Tafiti Maalumu: Utafiti wa Faida ya Biashara wa Mwaka 2019; Utafiti wa Asasi Zisizo za Kiserikali Zinazohudumia Kaya Binafsi wa Mwaka 2019; na Utafiti wa Sekta ya Huduma wa Mwaka 2019.

481. Vyanzo vya takwimu na taarifa zilizotumika katika zoezi hili ni pamoja na: Wizara ya Fedha; Benki Kuu ya Tanzania; Ofisi ya Taifa ya Takwimu; Mamlaka ya Mapato Tanzania; na Wizara za kisekta, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma.

**Muhtasari wa Matokeo ya Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa**

482. Maboresho ya mwaka wa kizio yameleta mabadiliko katika mwenendo wa Pato la Taifa na viashiria vingine vya kiuchumi katika maeneo mbalimbali, ikiwemo:

a) **Thamani ya Pato Ghafi la Taifa**

483. Mwaka 2019, thamani ya Pato ghafi la Taifa kwa bei za mwaka 2019 ambao ni mwaka mpya wa kizio ilikuwa shilingi bilioni 139,135.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 134,540.2 kwa mwaka wa kizio wa 2015, sawa na ongezeko la asilimia 3.4 (**Jedwali Na. 20.1)**. Ongezeko hilo lilitokana na maboresho ya vyanzo vya taarifa na takwimu kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi, ikiwemo uzalishaji umeme na usambazaji wa gesi pamoja na kuongezeka kwa mawanda katika sekta ya maji. Aidha, sababu nyingine ni utumiaji wa taarifa mpya za tafiti, maboresho katika mbinu za ukokotoaji kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi na mabadiliko katika muundo wa uzalishaji na matumizi ya bidhaa na huduma. Katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita (2016 - 2025), Pato ghafi la Taifa liliongezeka kwa wastani wa asilimia 9.6 kwa mwaka wa kizio wa 2019 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 9.3 kwa mwaka wa kizio wa 2015 (**Jedwali Na. 20.2)**. Ongezeko la Pato ghafi la Taifa linaashiria uwepo wa mabadiliko ya kimfumo katika uchumi, mwenendo wa uzalishaji, matumizi, uwekezaji, na wastani wa bei za bidhaa na huduma.

**Jedwali Na. 20.1: Mwenendo wa Mabadiliko ya Pato la Taifa, Baada ya Maboresho ya Mwaka wa Kizio**

| Mwaka wa Kizio | Pato la Taifa (Shilingi Milioni) | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|
| 1966 | 21,053.0 | |
| 1976 | 21,652.0 | 2.8 |
| 1992 | 1,275,915.6 | 82.8 |
| 2001 | 9,100,274.0 | 19.4 |
| 2007 | 26,770,431.8 | 27.8 |
| 2015 | 94,349,315.7 | 3.8 |
| **2019** | **139,135,212.3** | **3.4** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu


**Jedwali Na. 20.2: Mwenendo wa Pato Ghafi la Taifa kwa Bei za Miaka Husika (Shilingi Milioni)**

| Mwaka | Mwaka wa Kizio 2015 | Mwaka wa Kizio 2019 | Badiliko | Badiliko Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 2015 | 94,349,316 | 93,591,198 | -758,118 | -0.8 |
| 2016 | 108,362,324 | 105,696,548 | -2,665,777 | -2.5 |
| 2017 | 118,742,133 | 116,596,419 | -2,145,714 | -1.8 |
| 2018 | 123,997,772 | 129,186,992 | 5,189,219 | 4.2 |
| 2019 | 134,540,194 | 139,135,212 | 4,595,018 | 3.4 |
| 2020 | 145,384,353 | 149,620,933 | 4,236,580 | 2.9 |
| 2021 | 156,167,137 | 161,468,405 | 5,301,268 | 3.4 |
| 2022 | 170,820,032 | 178,515,913 | 7,695,880 | 4.5 |
| 2023 | 186,753,685 | 192,868,267 | 6,114,583 | 3.3 |
| 2024 | 205,846,493 | 211,779,525 | 5,933,032 | 2.9 |
| 2025 | 228,510,423 | 234,104,003 | 5,593,580 | 2.4 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

484. Matokeo ya maboresho ya mwaka wa kizio 2019 yanaonesha ongezeko la thamani katika shughuli za viwanda na ujenzi, huduma pamoja na kodi katika bidhaa na huduma ikilinganishwa na mwaka wa kizio 2015. Aidha, thamani ya shughuli za kilimo ilipungua kwa mwaka wa kizio 2019 ikilinganishwa na mwaka wa kizio 2015, kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 20.1.**

**Kielelezo Na. 20.1: Thamani ya Pato Ghafi la Taifa kwa Mwaka 2019**




**Thamani ya Pato katika Shughuli za Kiuchumi**

485. Mwaka 2019, thamani ya pato ghafi katika shughuli mbalimbali za kiuchumi imebadilika kutokana na maboresho ya mwaka wa kizio, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 20.3**. Pato ghafi liliongezeka katika baadhi ya shughuli za kiuchumi, ikiwemo: malazi na huduma ya chakula kwa asilimia 114.8; umeme na usambazaji gesi (asilimia 46.4); afya na huduma za jamii (asilimia 24.7); sanaa, michezo na burudani (asilimia 16.4); na pato ghafi la kazi za nyumbani kama mwajiri liliongezeka kwa asilimia 30.9. Ongezeko hilo lilitokana na matumizi ya matokeo ya tafiti kuhusu sekta ya huduma na mapato yatokananayo na shuguli za utalii, kujumuishwa kwa takwimu za usambazi wa gesi na maboresho ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi. Aidha, pato ghafi kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi lilikuwa na ukuaji hasi ikilinganishwa na mwaka wa kizio wa 2015, ikiwemo pato ghafi la kilimo cha mazao lililoshuka kwa asilimia 7.8, mifugo (asilimia 8.7), viwanda (asilimia 3.7) na shughuli za kitaalumu na ufundi (asilimia 23.5). Hii ilitokana na maboresho ya mauzo ghafi na utaratibu unaotumika katika ukokotoaji.

**Jedwali Na. 20.3: Thamani ya Pato Ghafi la Taifa kwa Mwaka 2019 (Shilingi Milioni) Kabla na Baada ya Maboresho ya Mwaka wa Kizio**

| **Shughuli za Kiuchumi** | **2015** | **2019** | **Badiliko** | **Badiliko(Asilimia)** |
|---|---|---|---|---|
| Kilimo | 36,447,871 | 34,531,749 | -1,916,122 | -5.3 |
| Kilimo cha Mazao | 20,066,646 | 18,498,565 | -1,568,081 | -7.8 |
| Mifugo | 10,357,287 | 9,457,254 | -900,033 | -8.7 |
| Misitu | 3,641,955 | 3,984,921 | 342,966 | 9.4 |
| Uvuvi | 2,381,982 | 2,591,008 | 209,026 | 8.8 |
| Viwanda na Ujenzi | 37,385,883 | 37,621,647 | 235,764 | 0.6 |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 7,164,222 | 7,382,971 | 218,750 | 3.1 |
| Viwanda | 10,512,034 | 10,123,642 | -388,392 | -3.7 |
| Umeme na usambazaji gesi | 369,917 | 541,731 | 171,814 | 46.4 |
| Maji safi na Maji taka | 590,324 | 680,656 | 90,332 | 15.3 |
| Ujenzi | 18,749,387 | 18,892,648 | 143,261 | 0.8 |
| Huduma | 50,952,480 | 56,214,390 | 5,261,910 | 10.3 |
| Biashara na Matengenezo | 12,286,407 | 12,261,827 | -24,579 | -0.2 |
| Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo | 9,622,792 | 10,569,576 | 946,784 | 9.8 |
| Malazi na Huduma ya Chakula | 1,680,222 | 3,608,481 | 1,928,259 | 114.8 |
| Habari na Mawasiliano | 2,052,242 | 2,166,463 | 114,222 | 5.6 |
| Fedha na Bima | 4,927,613 | 5,075,182 | 147,569 | 3 |
| Upangishaji Majengo | 3,869,528 | 3,962,175 | 92,647 | 2.4 |
| Shughuli za Kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 753,302 | 576,175 | -177,127 | -23.5 |
| Shughuli/Huduma Zinazohusiana na Utawal | 3,340,939 | 3,233,509 | -107,430 | -3.2 |
| Utawala na Ulinzi | 5,354,893 | 6,186,903 | 832,011 | 15.5 |
| Elimu | 3,322,028 | 3,599,275 | 277,247 | 8.3 |
| Afya na Huduma za Jamii | 1,932,964 | 2,409,985 | 477,022 | 24.7 |
| Sanaa, Michezo na Burudani | 427,887 | 498,036 | 70,150 | 16.4 |
| Huduma Nyingine | 1,140,417 | 1,751,021 | 610,604 | 53.5 |
| Shughuli za Kaya Katika Kuajiri | 241,246 | 315,780 | 74,534 | 30.9 |
| Jumla ya Ongezeko la Thamani | 124,786,234 | 128,367,786 | 3,581,552 | 2.9 |
| Ongeza Kodi katika Bidhaa | 9,753,960 | 10,767,426 | 1,013,466 | 10.4 |
| **Pato la Taifa kwa Bei za soko** | **134,540,194** | **139,135,212** | **4,595,018** | **3.4** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

486. Maboresho ya mwaka wa kizio 2019 yamesababisha mabadiliko ya mchango wa baadhi ya shughuli za kiuchumi katika Pato la Taifa kutokana na mabadiliko ya bei, bidhaa, teknolojia na tabia za walaji. Aidha, mchango wa shughuli za huduma katika Pato la Taifa umeongezeka wakati mchango wa shughuli za kilimo na viwanda na ujenzi umepungua ikilinganishwa na mwaka wa kizio 2015. Kupungua kwa mchango wa shughuli za kilimo katika uchumi inaashiria jitihada zinazochukuliwa na Serikali katika kuimarisha shughuli nyingine za kiuchumi kwa lengo la kupanua wigo wa uchumi na kupunguza utegemezi katika sekta ya kilimo. Mchango wa shughuli za uchumi katika Pato la Taifa ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 20.4**.

**Jedwali Na. 20.4: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi Katika Pato la Taifa Mwaka 2019 (Asilimia)**

| **Shughuli za Kiuchumi** | **2015** | **2019** |
|---|---|---|
| **Kilimo** | **27.1** | **24.8** |
| Kilimo cha Mazao | 14.9 | 13.3 |
| Mifugo | 7.7 | 6.8 |
| Misitu | 2.7 | 2.9 |
| Uvuvi | 1.8 | 1.9 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **27.8** | **27.0** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 5.3 | 5.3 |
| Viwanda | 7.8 | 7.3 |
| Umeme | 0.3 | 0.4 |
| Maji safi na Maji taka | 0.4 | 0.5 |
| Ujenzi | 13.9 | 13.6 |
| **Huduma** | **37.9** | **40.4** |
| Biashara na Matengenezo | 9.1 | 8.8 |
| Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo | 7.2 | 7.6 |
| Malazi na Huduma ya Chakula | 1.2 | 2.6 |
| Habari na Mawasiliano | 1.5 | 1.6 |
| Fedha na Bima | 3.7 | 3.6 |
| Upangishaji Majengo | 2.9 | 2.8 |
| Shughuli za Kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 0.6 | 0.4 |
| Shughuli/Huduma Zinazohusiana na Utawala | 2.5 | 2.3 |
| Utawala na Ulinzi | 4.0 | 4.4 |
| Elimu | 2.5 | 2.6 |
| Afya na Huduma za Jamii | 1.4 | 1.7 |
| Sanaa, Michezo na Burudani | 0.3 | 0.4 |
| Huduma Nyingine | 0.8 | 1.3 |
| Shughuli za Kaya Katika Kuajiri | 0.2 | 0.2 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **92.8** | **92.3** |
| Ongeza Kodi katika Bidhaa | 7.2 | 7.7 |
| **Pato la Taifa kwa Bei za soko** | **100.0** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Thamani ya Pato Halisi la Taifa

487. Thamani ya Pato halisi la Taifa kwa bei za mwaka wa kizio 2019 ilikuwa shilingi bilioni 139,135.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 123,139.2 kwa mwaka wa kizio 2015, sawa na ongezeko la asilimia 13.0 (**Jedwali Na. 20.5**). Ongezeko hilo lilitokana na mabadiliko ya bei ya bidhaa na huduma pamoja maboresho ya vyanzo vya taarifa na takwimu kwa baadhi ya sekta, ikiwemo uzalishaji umeme na usambazaji wa gesi pamoja na kuongezeka kwa mawanda katika sekta ya maji. Hii inaashiria uwepo wa mabadiliko ya uzalishaji wa bidhaa na huduma katika sekta mbalimbali za kiuchumi.

**Jedwali Na. 20.5: Thamani ya Pato Halisi la Taifa kwa Mwaka 2019, Kabla na Baada ya Maboresho ya Mwaka wa Kizio (Shilingi Milioni)**

| Shughuli za Kiuchumi | 2015 | 2019 | Badiliko | Badiliko Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **Kilimo** | **30,802,622** | **34,531,749** | **-1,916,122** | **12.1** |
| Kilimo cha Mazao | 16,372,351 | 18,498,565 | -1,568,081 | 13.0 |
| Mifugo | 8,687,238 | 9,457,254 | -900,033 | 8.9 |
| Misitu | 3,499,684 | 3,984,921 | 342,966 | 13.9 |
| Uvuvi | 2,243,349 | 2,591,008 | 209,026 | 15.5 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **34,912,847** | **37,621,647** | 235,764 | **7.8** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 5,485,112 | 7,382,971 | 218,750 | 34.6 |
| Viwanda | 10,184,558 | 10,123,642 | -388,392 | -0.6 |
| Umeme | 994,879 | 541,731 | 171,814 | -45.5 |
| Maji safi na Maji taka | 510,411 | 680,656 | 90,332 | 33.4 |
| Ujenzi | 17,737,886 | 18,892,648 | 143,261 | 6.5 |
| **Huduma** | **48,133,895** | **56,214,390** | **5,261,910** | **16.8** |
| Biashara na Matengenezo | 10,984,480 | 12,261,827 | -24,579 | 11.6 |
| Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo | 9,493,191 | 10,569,576 | 946,784 | 11.3 |
| Malazi na Huduma ya Chakula | 1,645,950 | 3,608,481 | 1,928,259 | 119.2 |
| Habari na Mawasiliano | 2,133,312 | 2,166,463 | 114,222 | 1.6 |
| Fedha na Bima | 4,281,167 | 5,075,182 | 147,569 | 18.5 |
| Upangishaji Majengo | 3,505,485 | 3,962,175 | 92,647 | 13.0 |
| Shughuli za Kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 821,635 | 576,175 | -177,127 | -82.6 |
| Shughuli zinazohusiana na Utawala | 3,311,753 | 3,233,509 | -107,430 | -38.3 |
| Utawala na Ulinzi | 5,238,491 | 6,186,903 | 832,011 | 18.1 |
| Elimu | 3,257,406 | 3,599,275 | 277,247 | 10.5 |
| Afya na Huduma za Jamii | 1,833,514 | 2,409,985 | 477,022 | 31.4 |
| Sanaa, Michezo na Burudani | 389,225 | 498,036 | 70,150 | 28.0 |
| Huduma Nyingine | 1,037,083 | 1,751,021 | 610,604 | 68.8 |
| Shughuli za Kaya Katika Kuajiri | 201,203 | 315,780 | 74,534 | 56.9 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **113,849,364** | **128,367,786** | **3,581,552** | **12.8** |
| Ongeza Kodi katika Bidhaa | 9,289,875 | 10,767,426 | 1,013,466 | 15.9 |
| **Pato la Taifa kwa Bei za soko** | **123,139,239** | **139,135,212** | **4,595,018** | **13.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

488. Maboresho ya mwaka wa kizio 2019 yamesababisha mabadiliko ya viwango vya ukuaji katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. Aidha, ukuaji kwa shughuli za kilimo na shughuli za viwanda na ujenzi ulikuwa asilimia 5.9 na asilimia 11.8 mtawalia mwaka wa kizio 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.4 na asilimia 11.4 mwaka wa kizio 2015. Kwa upande mwingine, ukuaji wa shughuli za huduma ulikuwa asilimia 4.0 mwaka wa kizio 2019 ikilinganishwa na asilimia 5.9 mwaka wa kizio 2015 (**Jedwali Na. 20.6**).

**Jedwali Na. 20.6: Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi Katika Pato la Taifa Mwaka 2019 (Asilimia), Kabla na Baada ya Maboresho ya Mwaka wa Kizio**

| **Shughuli za Kiuchumi** | **2015** | **2019** |
|---|---|---|
| **Kilimo** | **4.4** | **5.9** |
| Kilimo cha Mazao | 4.4 | 4.6 |
| Mifugo | 5 | 5.6 |
| Misitu | 4.8 | 6.9 |
| Uvuvi | 1.5 | 16 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **11.4** | **11.8** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 17.7 | 19.0 |
| Viwanda | 5.8 | 5.7 |
| Umeme | 7.2 | 9.8 |
| Maji safi na Maji taka | 6.9 | 6.9 |
| Ujenzi | 13.3 | 13.0 |
| **Huduma** | **5.9** | **4.0** |
| Biashara na Matengenezo | 4.8 | 5.4 |
| Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo | 8.7 | 4.9 |
| Malazi na Huduma ya Chakula | 2.6 | 4.7 |
| Habari na Mawasiliano | 7.2 | 4.2 |
| Fedha na Bima | 4.5 | 5.7 |
| Upangishaji Majengo | 4.5 | 2.0 |
| Shughuli za Kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 7.6 | 7.1 |
| Shughuli/Huduma Zinazohusiana na Utawala | 8.4 | 0.6 |
| Utawala na Ulinzi | 3.4 | -2.1 |
| Elimu | 6.9 | 4.7 |
| Afya na Huduma za Jamii | 5.0 | 8.8 |
| Sanaa, Michezo na Burudani | 11.2 | 3.0 |
| Huduma Nyingine | 6.7 | 7.3 |
| Shughuli za Kaya Katika Kuajiri | 3.1 | 3.1 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **7.1** | **6.7** |
| Ongeza Kodi katika Bidhaa | 4.7 | 3.1 |
| **Pato la Taifa kwa Bei za soko** | **6.9** | **6.4** |


**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Viwango vya Ukuaji wa Uchumi**

489. Uchumi wa Tanzania umeendelea kuwa imara licha ya wastani wa ukuaji kwa kipindi cha mwongo mmoja (2016 - 2025) kupungua katika mwaka wa kizio wa 2019 ikilinganishwa na ukuaji katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa kizio 2015. Katika kipindi hicho, Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 5.6 kwa mwaka wa kizio 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 5.8 kwa mwaka wa kizio 2015 (**Kielelezo Na. 20.2**). Katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2025, wastani wa ukuaji wa

shughuli za kilimo ulikuwa asilimia 5.1, madini na uchimbaji mawe asilimia 6.5, uzalishaji viwandani asilimia 5.8, ujenzi asilimia 6.5 na afya asilimia 6.5 kabla ya maboresho ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.6, asilimia 9.1, asilimia 6.1, asilimia 8.4, na asilimia 6.8 baada ya maboresho kwa mtiririko huo. Kwa upande mwingine, Pato halisi la Taifa lilikua kwa asilimia 6.4 mwaka 2019 kwa kutumia mwaka wa kizio 2019 ikilinganishwa na asilimia 6.9 kwa mwaka wa kizio 2015.

**Kielelezo Na. 20.2: Mwenendo wa Ukuaji Halisi wa Pato la Taifa, Mwaka 2015 - 2025**





**Matokeo katika Viashiria vya Uchumi**


490. Matokeo ya maboresho ya mwaka wa kizio 2019 yamesababisha uwiano wa viashiria vya uchumi vinavyokokotolewa kwa kutumia takwimu za Pato la Taifa kubadilika. Aidha, wastani wa Pato kwa mtu mwaka 2019 ulikuwa shilingi 2,563,988 kwa mwaka wa kizio 2019 ikilinganishwa na shilingi 2,479,311 kwa mwaka wa kizio 2015 (**Kielelezo Na. 20.3**). Hata hivyo, mwaka 2019/20 uwiano wa mapato ya ndani na mapato ya kodi kwa Pato la Taifa umepungua na kuwa asilimia 14.6 na asilimia 12.1 mtawalia kwa kutumia mwaka wa kizio 2019 ikilinganishwa na asilimia 15.0 na asilimia 12.5 kwa mwaka wa kizio 2015 **(Kielelezo Na. 20.4**). Kwa upande mwingine, uwiano wa deni la Serikali kwa Pato ghafi la Taifa mwaka 2019/20 ulikuwa asilimia 37.9 kwa mwaka wa kizio 2019 ikilinganishwa na uwiano wa asilimia 39.1 kwa mwaka wa kizio 2015 (**Kielelezo Na. 20.5**). Hata hivyo, ipo haja ya kutafsiri mabadiliko hayo kwa makini na usahihi hasa wakati wa kujenga hoja ya kufanya maamuzi. Mathalani kupungua kwa uwiano wa deni la Serikali kwa pato la Taifa kunaweza kusimaanishe kuongezeka kwa wigo wa kukopa kwani thamani ya deni na kiwango cha malipo ya deni hakijabadilika. Vilevile kupungua kwa nakisi ya bajeti kama

sehemu ya Pato la Taifa kusitumike kama kigezo cha kuongeza mikopo kwani kiwango cha thamani ya mikopo kilichopo kwa ajili ya kuziba nakisi ya bajeti bado ni kikubwa.


**Kielelezo Na. 20.3: Mwenendo wa Wastani wa Pato kwa Mtu, Mwaka 2015 - 2025**





**Kielelezo Na. 20.4: Mwenendo wa Uwiano wa Mapato ya Kodi kwa Pato la Taifa, Mwaka 2010/11 - 2024/25**




**Kielelezo Na. 20.5: Mwenendo wa Uwiano wa Deni la Serikali kwa Pato la Taifa, Mwaka 2015/16 - 2024/25**




**Kielelezo Na. 20.6: Mwenendo wa Uwiano wa Nakisi ya Bajeti Ikijumuisha Misaada kwa Pato la Taifa**



**Kielelezo Na. 20.7: Mwenendo wa Sekta ya Nje kwa Pato la Taifa**




**Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa katika Nchi Nyingine**

491. Nchi nyingine zimekuwa zikifanya maboresho ya takwimu za Pato la Taifa kwa lengo la kupata makadirio sahihi ya ukubwa, muundo na mabadiliko katika shughuli za kiuchumi kwa nchi husika. Mathalani, nchi ya Sierra Leone ilifanya maboresho ya takwimu za Pato la Taifa mwaka 2018 na Uganda mwaka 2019. **Jedwali Na. 20.7** linaonesha baadhi ya nchi zilizofanya maboresho ya takwimu za Pato la Taifakwa miaka ya hivi karibuni.

**Jedwali Na. 20.7: Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa katika Nchi Nyingine**

| Nchi | Mwaka wa Kizio wa Awali | Mwaka Mpya wa Kizio |
|---|---:|---:|
| Sierra Leone | 2006 | 2018 |
| Nigeria | 2010 | 2019 |
| Uganda | 2009/10 | 2016/17 |
| Kenya | 2009 | 2016 |
| Tanzania | 2015 | 2019 |


**Hitimisho**

492. Maboresho ya takwimu za Pato la Taifa hufanyika ili kuhakikisha ukokotoaji wa Pato la Taifa unaendana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia pamoja na uzingatiaji wa matakwa ya kimataifa. Maboresho ya mwaka wa kizio 2019 yamesababisha mabadiliko mbalimbali, ikiwemo kuongezeka kwa thamani ya Pato la Taifa ikilinganishwa na mwaka wa kizio wa 2015 na kubadilika kwa viwango vya ukuaji na mchango wa shughuli za kiuchumi katika Pato la Taifa. Aidha, uwiano wa baadhi ya viashiria vya uchumi vinavyopimwa kwa kutumia Pato la Taifa umebadilika. Hata hivyo,


mabadiliko hayo sio makubwa ikilinganishwa na uwiano unaokokotolewa kwa kutumia mwaka wa kizio wa 2015.

493. Maboresho ya takwimu za Pato la Taifa yanaongeza usahihi na ubora wa takwimu zitakazotumika katika maandalizi ya mipango ya maendeleo na maamuzi ya kisera yanayoendana na uhalisia. Maboresho hayo yatawezesha matumizi sahihi ya rasilimali adimu katika kuongeza ustawi wa wananchi na Taifa kwa ujumla, kupata makadirio sahihi ya ukubwa na muundo wa uchumi kwa kuzingatia miongozo na makubaliano ya kikanda na kimataifa, na kutumika kujilinganisha na mwenendo na ukuaji wa Pato la Taifa la nchi nyingine.

## Kiwango cha Umaskini wa Mahitaji ya Msingi Tanzania Bara (Asilimia ya Idadi ya Watu)




## Mwenendo wa Mapato ya Ndani kwa Pato Ghafi la Taifa




## Afya Jumuishi kwa Uchumi Imara



Wizara ya Fedha
Mji wa Serikali Mtumba
Mtaa wa Hazina
S.L.P 2802
Dodoma
https://www.mof.go.tz